

HIKI NDICHO CHUO CHA
SALA YA UMOJA

na
KUSONGEZA SAKRAMENTI

tena cha

KAWAIDA ZA MAMBO YA IBADA YA KANISA

kama ilivyo ada ya

KANISA LA UINGEREZA:

pamoja na

ZABURI ZI DAUDI

NA TARATIBU NA JINSI YA KUFANYA, NA KUAMURU,
NA KUWEKWA, WAWE

MABISHOPU, na MAKASISI, na MASHEMASI
na kadhalika

(*The Book of Common Prayer*
in the Swahili Language)

LONDON
SOCIETY FOR PROMOTING
CHRISTIAN KNOWLEDGE

1943

MAMBO YALIYOMO HUMU

	Ukarasa
1. Zaburi Zilizokhusika na siku kuu	v
2. Taratibu ya Sala ya Asubuhi	1
3. Taratibu ya Sala ya Joini	17
4. Wakati wa Sala ya Asubuhi	29
5. Litania	33
6. Sala na Shukrani	40
7. Shukrani	45
8. Sala na Shukrani kadhwakadha	48
9. Sala na Nyaraka na Injili vya Mwaka Mzima	63
10. Taratibu ya Kusongeza Karamu ya Bwana ; au, Ushirika Mtakatifu	219
11. Taratibu ya Kuwabatiza Watoto mbele ya Watu	247
12. Ubatizo wa Faragha Kuwasongezea Watoto Wachanga Nyumbani	256
13. Taratibu ya Kubatiza Watu Wazima	263
14. Majibizano (au Katekisimo)	272
15. Taratibu ya Kuthubutisha	279
16. Taratibu ya Ndoa	284
17. Taratibu ya Kuwaangalia Wagonjiwa	295
18. Walio hawawezi Kuwasongezea Ushirika	305
19. Taratibu ya Kuzika Maiti	307
20. Shukrani za Wanawake baada ya Kwisha Kuzaa	315
21. Maonyo ya Ghadhabu zake Mwenyezi Mungu	318
22. Zaburi za Daudi	327
23. Taratibu na Jinsi ya Kufanya, na Kuamuru, na Kuwekwa Wawe	477
24. Sharti Thelathini na Kenda za Dini	507
25. Taratibu ya Kuonyesha Uzazi	523
26. Taratibu Iwezayo Kutumiwa kwa Kuzika Mtoto	527
27. Taratibu ya Kuwatia Wasikizi Katiki Kundila Watafiti	531
28. Taratibu ya Kuwakubali Watafiti wawe Wasomaji	534
29. Taratibu ya Ndoa	539
30. Kuweka wakf Msikiti	546
31. Taratibu ya Kuweka Jiwe la Msingi wa Msikiti	554

ZABURI ZILIZOKHUSIKA NA SIKU KUU

	Asubuhi	Jioni
Siku ya Uzazi wa Bwana	Zaburi 19	Zaburi 89
" "	" 45	" 110
" "	" 85	" 132
Jumatano ya Ivu	Zaburi 6	Zaburi 102
" "	" 32	" 130
" "	" 38	" 143
Juma Njema	Zaburi 22	Zaburi 69
" "	" 40	" 88
" "	" 54	
Siku ya Kufufuka kwa Bwana	Zaburi 2	Zaburi 113
" "	" 57	" 114
" "	" 111	" 118
Siku ya Kupaa	Zaburi 8	Zaburi 24
" "	" 15	" 47
" "	" 21	" 108
Pentecost	Zaburi 48	Zaburi 104
" "	" 68	" 145

TARATIBU YA SALA YA ASUBUHI YA KILA SIKU MWAKA MZIMA

¶ *Mwanzo wa Sala ya Asubuhi yule Padre husoma kwa sauti kuu
aya moja au zaidi ya Maandiko Matakatifu katika hizo
zilizowekwa : kisha hunena yafuatanyo na aya hizo.*

MTU mbaya atakapotubu na kuuacha huo ubaya wake
Malioufanya, akayasanya yaliyo halali na haki, ataipo-
nya nafsi yake awe hai. *Ezekieli 18. 27*

Ninakiri mimi makosa yangu, na dhambi yangu i mbele
yangu daima. *Zaburi 51. 3*

Ufiche uso wako, usitazame dhambi zangu, uzifute
hatia zangu zote. *Zaburi 51. 9*

Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika : moyo
uliovunjika na kupondeka, ewe Mungu, hutaudharau.

Zaburi 51. 17
Rarueni mioyo yenu, msirarue mavao yenu, nanyi
rejeeni kwa Yehova Mungu wenu : kwa kuwa yeye ni
mwenye neema na huruma : si mwepesi wa hasira, ni
mwiningi wa rehema : naye hujutia lile shari.

Yoeli 2. 13
Ni ya Yehova Mungu wetu huruma na msamaha, kwani
tumemwasi, wala hatukusikiza sauti ya Yehova Mungu
wetu kwa kwenenda katika sheria yake aliyotuvekea mbele
yetu. *Danieli 9. 9-10*

Ewe Yehova, nirudi, ila kwa haki, si kwa hasira, usije
tukandidhili. *Yeremia 10. 24*

Tubuni, kwani usalme wa mbingu umekwisha kukaribia.
Mathayo 3. 2

Nitaondoka, niende kwa baba, nikamwambie, Baba,
nimekosa juu ya mbingu na mbele zako ; sistahili tena
kuitwa mwanayo. *Luka 15. 18-19*

Ewe Yehova, usimhukumu mtumishi wako ; kwani
mbele zako hakuna aliye hai atakaychesabiwa kuwa ni
mwenye haki. *Zaburi 143. 2*

Ikiwa twanena ya kwamba hatuna dhambi, twapoteza nafsi zetu, na hiyo kweli haimo ndani yetu. Ila ikiwa twaziungama dhambi zetu, yeze ni mwaminifu kisha yuna haki akatusamehe dhambi zetu na kutusafi na uovo wote.

I Yohana 1. 8-9

Ni roho Mwenyezi Mungu ; nao wenye kumbabu imewapasa kuabudu katika roho na kweli.

Yohana 4. 24

Mwabuduni Yehova kwa uzuri wa utakatifu ; tetemekeni mbele zake, nchi yote. Zaburi 96. 9

Usiku umekwendelea sana, mchana umekaribia : basi na tuzivilie mbali zile kazi za giza, na kujivisha silaha za mwanga. Warumi 13. 12

Uzazi wa Bwana wetu, au Christmas

Ninawahubirini habari nzuri za furaha nydingi zitakazokuwa ni za wenyeji wote ; kwani leo amezaliwa kwa ajili yenu katika mji wa Daudi, Mwokozi, naye ni Kristo Bwana. Luka 2. 10-11

Katika neno hili hayo mapenzi ya Mwenyezi Mungu yamefanywa wazi ndani yetu sisi, ya kwamba Mwenyezi Mungu amemtuma Mwanawewe mzaliwa pekee aingie duniani, ili kwamba tupate kuwa hai kwa yeze. I Yohana 4. 9

Mafumuo

Tokea kucha kwake jua hata kutua kwake lilo, jina langu ni kuu katika watu wa hao mataifa ; tena kila pahali uvumba wasongezwa katika jina langu, na dhabihu iliyosafii : kwa kuwa jina langu ni kuu katika watu wa hao mataifa, asema Yehova wa majeshi.

Malaki 1. 11

Yehova ameujulisha wokofu wake ; machoni pa mataifa amedhihirisha haki yake. Zaburi 98. 2

Mateso

Angalieni, mwone kwamba pana majonzi mengine yawayo yote yaliyo mfano wa majonzi niliyo nayo mimi, hayo niliyotendewa. Maomboleo 1. 12

Ijumaa Njema

Mwenyezi Mungu ayadhihirisha kwetu mapenzi yake mwenyejewa aliyotupenda, kwa maana, tulipokuwa takali wenye dhambi, Kristo akafa kwa ajili yetu.

Warumi 5. 8

Siku ilio kabla ya Ufufuo

Ukae kimya mbele za Yehova, ukamnjojee wala usikasirike ; naye atakupa haja za moyo wako.

Zaburi 37. 7, 4

Ufufuo

Na ashukuriwe Mwenyezi Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye katika rehema zake kuu, ametuzaa sisi mara ya pili kwa njia ya kufufuliwa kwake Yesu Kristo.

I Petero 1. 3

Siku ya Kupaa

Kwa kuwa tuna kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mwenyezi Mungu, na tukiendee hicho kiti-cha-neema kwa uthubutifu, ili kwamba tupate rehema na kuona neema ya kutusaidia wakati wa haja.

Wahibirania 4.14, 16

Pentecost

Mapenzi ya Mwenyezi Mungu yamekwisha kumi-minwa na kutiwa ndani ya mioyo yetu na Roho Mtakatifu ambaye tumepewa sisi. Warumi 5. 5

Utatu

Mwenyezi Mungu ni mapenzi ; na yeze akaaye katika mapenzi yuakaa ndani ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu yuakaa ndani yake yeze.

I Yohana 4. 16

Watakatifu Wote

Kwa kuwa tumezingirwa na wingu kubwa la mashahidi jinsi hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na hiyo dhambi iliyotuzunguka sisi kwa wepesi, na tupige mbio kwa uvumilivu kwa yale mashindano

SALA YA ASUBUHI

yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, mwenye kuanziliza na mwenye kutimiliza imani yetu.

Wahibirania 12. 1-2

Siku za Watakatifu

Mwenye haki atakumbukwa milele. Kuwakumbuka hao wenyе haki huwa na baraka.

Zaburi 112. 6 ; Mifano 10. 7

Mwaka Mya

Hao wamnganjeao Yehova watarejeza upya nguvu zao ; watakwea juu kwa mabawa mfano wa kipungu ; watapiga mbio, wasichoke ; watakwenda kwa miguu, nao hawatazima roho.

Isaya 40, 31

Mavuno

Nchi na vyote vijazavyo ni mali ya Yehova.

Zaburi 24. 1

Wakati wa Mashaka

Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu : msaada uonekanao wakati wa mateso.

Zaburi 46. 1

Mambo ya Usalme

Mataifa wafurahi na kuimba kwa furaha : kwani wewe utawahukumu watu kwa haki, utawaongoza watu walioko duniani.

Zaburi 67. 4

ENYI ndugu zangu mpendwao sana, twaonyeshwa katika Maandiko mwahali kadhwakadha, ya kukiri na kuyaungama madhambi yetu na viovu vyetu kila namna ; pasipo kuvificha wala kuvifinika mbele ya uso wa Mwenyezi Mungu Babaetu wa mbinguni : twaonyeshwa ya kuiungama kwa moyo wa unyonge na unyenyekevu, wenyе kutubia na kufuata ; ili kwamba kwa wema wake na rehema zake zisizo ukomo, tupate kusamehewa. Nasi ingawa kule kumwekea wazi Mwenyezi Mungu madhambi yetu kwa uynyenyekevu ni neno litupasalo sana kila wakati ; ni zaidi sana wakati tukutanapo wenyewe kwa wenyewe, kuja kumshukuru kwa rehema kuu tulizopokea mikononi mwake, na kumsifu kama ilivyopasa sana, na kusikiza Neno lake lililo takatifu, na kumtaka kadiri ya tulivyo na

SALA YA ASUBUHI

haja navyo, rohoni hata mwilini. Basi, kwa ajili ya hayo, mimi nawasihi ninyi nyote mliopo, mfuatane nami kwa miyo myeupe, na sauti nyenyekevu, tuje tukaribie katika kiti cha neema ya mbinguni, mseme nyuma yangu ;

¶ Hapa Padre aweza kusema maneno kama haya, akiona ni vizuri ;

TUKIWA tumepiga magoti, na tukae kimya kwa dakika chache, tukikumbuka ya kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi hapa.

¶ Haya ni maneno ya watu pia wote, ya kuungama makosa, nayo husemwa na watu wote nyuma yake yule Padre, hali wamepiga magoti pia wote.

EWE Baba, Mwenyezi, Mwingi wa rehema ; Sisi tume-kosa, Tumepotea njia zako, kama kondoo waliopotea Tumefuata mno mashauri na tamaa za miyo yetu wenyewe. Tumekosa sheria zako takatifu. Yaliyopasa kuyafanya hatukuyafanya, Tumefanya yasiyotupasa kuyafanya : Wala hatuna salama ndani yetu wenyewe. Ila wewe, Bwana, uturehemu, sisi wakosaji dhaifu : Ewe Mungu, uwasamehe wenyе kuyaungama makosa yao. Uwakubali waliotubia : Kama ahadi zako walizofunuliwa wanadamu katika Kristo Yesu, Bwana wetu. Kisha, Baba mwingi wa rehema, Utupe kwa ajili yake yeze ; Ya sisi kuishi tangu leo maisha ya uchaji-wa-Mungu na haki na mambo ya kiasi, Kwa kulitukuza jina lako lililo safi. Amina.

¶ Ghofira, au Ondoleo la madhambi : nalo hutankwa na Kasisi pekee, hali amesimama, watu wakali wamepiga magoti.

MWENYEZI Mungu, Babaye Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye hataki mauti ya mwenye dhambi, afadhalii ataka auache uovu wake awe hai : naye amewapa amri watumishi wake, amewaagiza, ya kuwaeleza na kuwambia watu wake waliotubia, ya wao kusamehewa na kuondolewa madhambi yao : yeze huwasamehe na kuwondolea madhambi wote waliotubu kweli, walioamini Injili yake takatifu pasipo kuitilia shaka. Kwa ajili ya

hayo na tumwombe atupe toba ya kweli, atupe na Roho wake Mtakatifu, ili tuyafanyayo hivi sasa yampendeze ; na maisha yetu ya tangu sasa yawe safi na utakatifu, ili mwisho tufikilie katika furaha zake za milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu.

¶ Hapa na kila pakomapo Sala watu huitika, Amina.

¶ Kisha Padre hupiga magoti na kuisoma Sala ya Bwana kwa sauti ya kusikilikan : na watu nao hali wamepiga magoti, husoma pomoja naye : kwa wakati huo, na kila itumiwapo katika Ibada ya Mwenyezi Mungu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalte wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamche, watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribwi ; Utuokoe maovuni : Kwa kuwa ufalme, na nguvu, na utukufu, ni vyako milele. *Amina.*

¶ Kisha husoma,

Ewe Bwana, ufunue midonio yetu.

Huitika. Na vinywa vyetu vitatangaza utukufu wako.

Padre. Ewe Mungu, utuokoe upesi.

Huitika. Ewe Bwana, utusaidie haraka.

¶ Wakati huo watu wakiisha kusimama wote, Padre husoma,

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Huitika. Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

Padre. Msifuni Bwana.

Huitika. Jina la Bwana lisifiwe.

¶ Hapa husomwa au kuimbwa Zaburi hii ifuatanayo : isipokuwa Idi ya Ufufuo, ndipo Wimbo mwingine uamriwapo : tena na kila siku ya mwezi kumi na kenda haisomvi hapa, ila husomwa katika taratibu ya Zaburi kama desturi.

VENITE EXULTEMUS DOMINO

Zaburi 95

HAYA ! na tumwimbie Yehova kwa furaha : na tumshangilie Mwamba wa Wokofu wetu.

Twendeni haraka, tukasimarme mbele ya uso wake na shukrani : tumshangilie kwa zaburi.

Kwani Yehova ni Mungu Mkuu : ni Mfalme mkuu, juu ya miungu yote.

Ambaye mabopo makuu ya dunia ya mkononi mwake : na vilele vya milima pia ni vyake.

Ambaye bahari ni yake, Mwenyewe aliifanya : mikono yake iliumba nchi kavu.

Njoni tukaabudu, tusujudu : tupige na magoti mbele za Yehova mwenye kutufanya.

Kwani ndiye Mungu wetu : nasi tu watu wa uchunga wake, tu kondoo za mkonon wake.

Leo, lau kwamba mwaistikia sauti yake, msifanye mizito miyo yenu : kama mlivyofanya huko Meriba, kama siku ya Masa, mle barani.

Babazenu waliponionja : walinihakikisha, waliniona nifanyavyo.

Miaka arobaini nilichukizwa na kizazi kile, nikasema : Wao ni taifa la watu watangao miyo yao, wala hawakuelwa na njia zangu.

Ndipo nilipoapa kwa hasira zangu : Hawaingii katika starehe yangu.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu :

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

¶ Ndipo hapo huandama Zaburi, kwa taratibu yake, kama ilivyo-agizwa. Hata baada ya mwisho wa kila Zaburi mwaka mzima, na mwisho wa Benedicite, na Benedictus, na Magnificat, na Nunc Dimittis, husomwa maneno haya,

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu :

Huitika. Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina*

¶ Ndipo husomwa wazi kwa sauti ya kusikilikanja Somo la Kwanza, katika Agano la Kale, kama ilivoagizwa katika Kalendari, isipokuwa ni siku ilivoagizwa Masomo ya kuhusika. Naye mwonye kusoma husimama akajilekeza kwa kuangalia watu wapate kumsikia sana, kadiri ya waliopo. Kisha baadaye na usomwe, au uimbiwe, utungo nitwao Te Deum Laudamus kila siku ya mwaka mzima.

¶ Tunza : Ya kwamba mwanzo wa kila Somo, yule mwonye kusoma husema, Mwanzo wa mlango kadhawakadha, wa Chuo kadhawakadha, au Mwanzo wa Kifungu kadhawakadha : Na mwisho wa kila Somo, husema, Somo la Kwanza, au la Pili, limekoma hapo.

TE DEUM LAUDAMUS

TWAKUSIFU Mungu : twakukiri wewe ndiwe Bwana.

Dunia nzima yakuabudu : Baba uliyeko milele.

Malaika wote wakupazia sauti : mbingu na nguvu zilizomo zote.

Makerubi na Maserafi daima : wakupazia sauti wewe.

Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu : Yehova Mungu wa majeshi.

Mbingu na nchi zimejaa : enzi ya utukufu wako tele.

Wakusifu wewe : jamaa tukufu ya Mitume.

Wakusifu wewe : kikao chenye sifa njema cha manabii.

Wakusifu wewe : jeshi safi la mashahidi.

Kanisa takatifu, duniani mote : lakukiri wewe.

Baba mwonye enzi : isiyo ukomo.

Mwanayo wa kuheshimiwa : aliye kweli, aliye pekee :

Tena Roho : Mtakatifu, Msadaa.

Wewe ndiwe Mfalme wa Utukufu : ewe Kristo.

Wewe ndiwe Mwana wa Milele : wa Baba.

Wewe, ulipositia katika kukomboa binadamu : hukuchukizwa na tumbo la Mwanamwali.

Wewe, uliposhinda uchungu wa mauti : uliwafunulia Ufalme wa mbingu wenye imani.

Wewe wakaa upande wa mkonono wa kuume wa Mungu : enzini mwake Baba.

Twasadiki ya kwamba utakuja : kuwa Mwamuzi wetu.

Basi twakutaka wewe, uwasaide watumwa wako : uliowakomboa kwa damu yako ya thamani.

Uwape kuhesabiwa katika utukufu wa milele : pamoja na watakatifu wako.

Uwaweke salama watu wako, Bwana : uubarikie urithi wako.

Nawe uwatawale : uwainue wao milele.

Siku hata siku : twakutukuza wewe ;

Na jina lako twalisifu : milele na milele.

Uwe radhi Bwana : hii siku ya leo utulinde na dhambi.

Uturehemu Bwana : uturehemu sisi.

Rehema zako, Bwana, zishuke juu yetu : kama vile tuliviyokutumaini wewe.

Nimekutumaini wewe, Bwana : sitafedheheka milele.

¶ Au utungo huu,

BENEDICITE, OMNIA OPERA

ENYI Kazi zote za Yehova, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Malaika za Yehova, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Mbingu, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Maji yaliyo juu ya Anga, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Nguvu zote za Yehova, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Jua na Mwezi, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Nyota za Mbinguni, mshukuruni Yehova ; msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Manyonyota na Umande, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Pepo za Mwenyezi Mungu, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Moto na Chaka, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Masika na Kaskazi, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Umande na Kipupwe, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Maji ya Kuganda na Baridi, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Barafu na Theluji, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Masiku na Michana, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Mwanga na Giza, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Umeme na Mawingu, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Na Nchi nayo imshukuru Yehova : na imsifu, imtukuze milele.

Enyi Milima na Vilima, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Majani Mabichi yaliyo juu ya Nchi nyote, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Vijito nya Maji, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Bahari, nanyi Mito ya Maji, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Nyangumi, nanyi mtukutao Majini, nyote, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Nyuni za Angani nyote, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi nyote Nyama za Mwitu na za Miji, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Wanadamu, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Israeli naye na amshukuru Yehova : amsifu, amtukuze milele.

Enyi Makuhani wa Yehova, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Watumishi wa Yehova, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Nafsi na Roho za Wenye-Haki, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Watu Watakatifu, Wanyenyeketu wa

Mioyo, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Enyi Anania, na Azaria, na Misaeli, mshukuruni Yehova : msifuni, mtukuzeni milele.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu :

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Hapo husomwa vivyo Somo la Pili, katika Agano Jipya. Na baadaye Wimbo huu unoaoandama, isipokuwa utukiaipo huu kuosomwa katika Mlango uliohusiska na siku yake au ukasomwa kuwa Injili siku ya Mbatizaji Yohana.

BENEDICTUS

Luka 1, 68-79

A SHUKURIWE Bwana, Mungu wa Isiraeli : kwa Akuwa amewaangalia watu wake, amewafanya na ukombozi ;

Tena ametuiniulia pembe ya wokofu : katika nyumba ya Daudi mtumishi wake ;

Kama alivyosema kwa vinywa vyaa manabii wake watakatifu : waliokuwako tangu milele ;

Maana, wokofu katika adui zetu : na katika mikono ya wote watuchukiao ;

Kuwaonea huruma baba zetu : na kukumbuka maagano yake matakatifu ;

Kiapo alichomwapia : babaetu Iburahimu ;

Ya kwamba atatupa : tuli hali tumeokoka na mikono ya adui zetu ;

Kumtumikia pasipo hofu kwa utakatifu na haki : mbele zake siku zetu zote.

Nawe, kijana wewe, utaitwa Nabii wa Aliye-juu-sana : kwani utamtangulia Bwana mbele ya uso wake, kumtengezeza njia zake.

Ili kuwapo watu wake kuujua wokofu : kwa kusamehewa dhambi zao,

Kwa huruma za ndani za Mungu wetu : kwa hizo itatangalia Alfajiri itokayo juu.

Iwang'arie waketio katika giza na kivuli cha mauti : ili katuongoza miguu yetu njia ya amani.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu :

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo.
Amina.

¶ Au Wimbo hui katika Zaburi,

JUBILATE DEO

Zaburi 100

MSHANGILIENI Yehova, dunia nzima : mtumikieni Yehova kwa furaha, njoni mbele zake kwa kutekerea.

Mjeni Yehova ndiye Mungu : ndiye aliyetufanya, nasi tu wake : tu watu wake, tu kondoo za malisha yake.

Ingieni malangoni mwake kwa shukrani, nyuani mwake kwa sifa : mshukuruni, mlitarikie jina lake.

Kwani Yehova ndiye mwema, ni za milele ihisani zake : uaminifu wake wafikilia vizazi vyote.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu :

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo.
Amina.

¶ Hapo huimbwa au husomwa Imani ya Mitume na yule Padre na wale watu, halii wote wamesimama : isipokuwa haisomwi Imani hii siku hizo ambazo imeagizwa kusomwa Imani ya Mtakatifu Athanasio.

NAAMINI kwa Mungu Baba, Mwenyezi, Muumbambingu na nchi :

Na kwa Yesu Kristo, Mwanawe pekee, Bwana wetu, ambaye alitungishwa mimba na Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Mwanamwali Mariamu, Akateswa katika enzi ya Pontio Pilato, Akasalibiwaa, akafa, akazikwa, Akashuka na kuingia kuzimu ; Hata siku ya tatu akasimama tena, ametoka kwa wafu, Akapaa na kuingia mbinguni, Naye ameketi upande wa mkonono wa kuume wa Mwenyezi Mungu, Baba ; Ndiko atakakotoka, kuja kuwaamua walio hai hata waliokufa.

Naamini kwa Roho Mtakatifu ; na Kanisa Takatifu liliilo ulimwenguni mote ; na Ushirika wa Watakatifu ; na Madhambi kusamehewa ; na Mwili kufufuka ; na Maisha ya milele. *Amina.*

¶ Kisha husaliwa Sala hizo zifuatazo hapa, watu halii wamepiga magoti kwa makini ; yule Padre hutangulia kutamka kwa sauti kuu,

Bwana na awe pamoja nanyi.
Huitika. Na awe pamoja na roho yako.
Padre. Na tuombe.

Bwana, uturehemu.
Kristo, uturehemu.
Bwana, uturehemu.

¶ Hapo yule Padre na waimbaji na wale watu husoma Sala ya Bwana kwa sauti kuu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na nje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kurutoshaa. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa ; Utuokoe maovuni. *Amina.*

¶ Hapo Padre husimama na kusema,
Ewe Bwana, utuonyeshe rehema yako juu yetu.

Huitika. Utupe na wokofu wako.
Padre. Ewe Bwana, uinweke salama Mfalme.

Huitika. Nawe usitikize kwa rehema, wakati tukulunganapao.

Padre. Uwavike haki watumishi wako.
Huitika. Uwaweke na furaha wateule wako

Padre. Ewe Bwana, uwaokoe watu wako.
Huitika. Ubarikie na urithi wako.

Padre. Ewe Bwana, utupe amani kwa hizi zaman zetu.
Huitika. Kwa maana, hakuna mwenye kututetea, asiyejewa wewe, Mwenyezi Mungu.

Padre. Ewe Mwenyezi Mungu, utufanye safi miyo yetu ndani.
Huitika. Wala usituondolee Roho wako Mtakatifu.

Hapo husuata Sala tatu : ya Kwanza ni ya Siku ile, maana, ni ile ile iliyoamriwa katika Ushirika : ya Pili ni ya kuombea Amani : ya Tatu ni ya kuombea Neema ya kuishi vyema. Na Sala mbili hizo za mwisho hazibadiliki, husomwa siku zote wakati wa Sala ya Asubuhi mwaka mzima, kama zifuatanganavyo hapa : na wale watu hali wamepiga magoti wote.

SALA YA PILI, YA KUOMBEA AMANI

EWE Mwenyezi Mungu, Mwenye kubuni amani na E kupenda mapatano, maisha yetu ya milele ya katika kukujuu wewe, kukutumikia wewe ndio uhuru uliokamili : utukingie sisi watumishi wako wanyenyekevu kila tukifuliwa na adui ; ili kwa kutumaini sana ulinzi wako, tusiche nguvu za adui zetu wawao wote, kwa uwezo wa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA YA TATU, YA KUOMBEA NEEMA

EWE Bwana, Babaetu wa mbinguni, Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, uliyetufikisha katika mwanzo wa siku hii salama ; utuhifadhi leo kwa nguvu zako zisizowezekana ; nawe ukubali ya kwamba siku hii tusiangukie katika dhambi, wala kuingia katika hatari kwa neno lolote ; bali iwe viitendo vyetu vyote kuamrishwa na uongozi wako, hata tukafanye daima yaliyolekea machoni mwako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

- K**atika maimbio na penye waimbaji, hapa huletwala Wimbo.
Kisha hapa husomwa Sala hizi tano zifuatato, isipokuwa wakati isomevapo Litania : na wakati huo, sala zisomwazo ni hizo mbili za mwisho, kama vile zilivoyekwa hapa.

SALA YA KUMWOMBEA MTUKUFU MFALME

EWE Bwana, Babaetu wa mbinguni, mtukufu, mweza, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana, Mtawala-maseyidi pekeo, nawe huko uliko kitini mwako unawaangalia watu wote pia wakao duniani ; sisi twakuomba sana umwangalie kwa neema yako Bwana wetu Sultani mwenye ihisan, Mfalme *GEORGE* ; umwongeze sana neema hiyo ipatikanayo kwa Roho wako Mtakatifu, hata awe siku zote kuyashika uyapendayo wewe, na kwenenda

umlekezako : umvike vipawa vyako vya mbinguni kwa wingi ; umkirimu kuiishi sana kwa afya na uwezo ; umtie nguvu apate kuwashinda na kuwapita adui zake wote ; na baada ya haya, kisha, afikilie furaha na baraka zisizokoma ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA YA KUWAOMBIA WATU WA JAMAA YA UFALME

EWE Mwenyezi Mungu, shina la wema wote, sisi twakuomba sana kwa unyenyekevu umbarikie mkewe mfalme wetu, Bibi *Elizabeth* mwenye fadhili, na Bibi *Mary* mamaake mfalme, na *Princess Elizabeth*, na jamaa wote wa Ufalme : uwavike Roho wako Mtakatifu ; uwaneemeshe neema yako ya mbinguni ; uwafanishe kwa raha yote ; uwafakishe na katika ufalme wako wa milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA YA KUWAOMBIA MAPADRE WA KANISANI NA WATU WAO

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, kila miujiza Ebora hakuna mwenye kuifanya isipokuwa wewe ; twa-waombia mabishopu wetu na watunza roho za watu, na vikao vyote vya watu walivyopewa hao kuvitunza, ya kwamba uwashushie Roho wako, ambaye ni Mpaji wa neema yako ; kisha, ili kwamba watu hao wakupendeze kweli, uwamiminie umande usiokoma wa baraka yako. Utupe haya, twakuomba, Bwana, kwa ajili ya heshima ya Msada wetu, Mwombezi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

SALA YA MTAKATIFU CHRYSOSTOM

EWE Mwenyezi Mungu, uliyetupa neema sisi kwa ni moja ; nawe ndiwe mwenye kutoa ahadi ya kwamba, watu wawili watatu watakoputanika pamoja kwa jina lako, utawapa wakutakayo : ututimizie sasa, Bwana, haja zetu na sala zetu watumishi wako, kwa jinsi yatakavyotufaa ; kwa kutupa kuijua kweli yako katika ulimwengu huu, na maisha ya milele katika ulimwengu ujao. *Amina.*

2 Wakorintho 13. 14

NEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, viwe pamoa nasi sote milele. *Amina.*

Taratibu ya Sala ya Asubuhi ya kila siku mwaka
mzima imekoma hapa

TARATIBU YA SALA YA JIONI YA KILA SIKU MWAKA MZIMA

¶ *Mwanizo wa Sala ya Jioni yule Padre husoma kwa sauti kuu aya moja au zaidi ya Maandiko Matakatifu katika hizo zilizowekwa : kisha hunena yafuatanyo na aya hizo.*

MTU mbaya atakapotubu na kuuacha huo ubaya wake Maliofanya, akayafanya yaliyo halali na haki, ataiponya nafsi yake awe hai. *Ezekieli 18. 27*

Ninakiri mimi makosa yangu, na dhambi yangu i mbele yangu daima. *Zaburi 51. 3*

Ufiche uso wako, usitazame dhambi zangu, uzifute hatia zangu zote. *Zaburi 51. 9*

Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika : moyo uliuvunjika na kupondeka, ewe Mungu, hutaudharau. *Zaburi 51. 17*

Rarueni mioyo yenu, msirarue mavao yenu, nanyi rejeeni kwa Yehova Mungu wenu : kwa kuwa yeye ni mwenye neema na huruma : si mwepesi wa hasira, ni mwiningi wa rehema : naye hujutia lile shari. *Yoeli 2. 13*

Ni ya Yehova Mungu wetu huruma na msamaha, kwani tumemwasi, wala hatukusikiza sauti ya Yehova Mungu wetu kwa kwenenda katika sheria yake aliyotukewa mbele yetu. *Danieli 9. 9-10*

Ewe Yehova, nirudi, ila kwa haki, si kwa hasira, usije ukaniidhili. *Yeremia 10. 24*

Tubuni, kwani ufalme wa mbingu umekwisha kukaribia. *Mathayo 3. 2*

Nitaondoka, niende kwa baba, nikamwambie, Baba, nimkosa juu ya mbingu na mbele zako ; sistahili tena kuitwa mwanayo. *Luka 15. 18-19*

Ewe Yehova, usimhukumu mtumishi wako ; kwani mbele zako hakuna aliye hai atakayehesabiwa kuwa ni mwenye haki. *Zaburi 143. 2*

Ikiwa twanena ya kwamba hatuna dhambi, twapoteza nafsi zetu, na hiyo kweli haimo ndani yetu. Ila ikiwa twaziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu kisha yuna haki akatusamehe dhambi zetu na kutusafi na uovo wote.

I Yohana 1. 8-9

Ni roho Mwenyezi Mungu; nao wenyewe kumwabudu imewapasa kuabudu katika roho na kweli.

Yohana 4. 24

Mwabuduni Yehova kwa uzuri wa utakatifi; tete-mekeni mbele zake, nchi yote. *Zaburi 96. 9*

Usiku umekwendelea sana, mchana umekaribia: basi na tuzivilie mbali zile kazi za giza, na kujivisha silaha za mwanga. *Warumi 13. 12*

Uzazi wa Bwana wetu, au Christmas

Ninawahubirini habari nzuri za furaha nyingi zitakazokuwa ni za wenyeji wote; kwani leo amezaliwa kwa ajili yenu katika mji wa Daudi, Mwokozi, naye ni Kristo Bwana. *Luka 2. 10-11*

Katika neno hili hayo mapenzi ya Mwenyezi Mungu yamefanywa wazi ndani yetu sisi, ya kwamba Mwenyezi Mungu amemtuma Mwanawewe mzaliwa pekee aingie duniani, ili kwamba tupate kuwa hai kwa ye. *I Yohana 4. 9*

Mafunuo

Tokea kucha kwake jua hata kutua kwake lilo, jina langu ni kuu katika watu wa hao mataifa; tena kila pahali uvumba wasongezwa katika jina langu, na dhabihu iliyo safi: kwa kuwa jina langu ni kuu katika watu wa hao mataifa, asema Yehova wa majeshi.

Malaki 1. 11

Yehova ameujulisha wokofu wake; machoni pa mataifa amedhihirisha haki yake. *Zaburi 98. 2*

Mateso

Angalieni, mwone kwamba pana majonzi mengine yawayo yote yaliyo mfano wa majonzi niliyo nayo mimi, hayo niliyotendewa. *Maomboleo 1. 12*

Ijumaa Njema

Mwenyezi Mungu ayadhihirisha kwetu mapenzi yake mwenyejewa aliilotupenda, kwa maana, tulipokuwa tukali wenyewe dhambi, Kristo akafa kwa ajili yetu.

Warumi 5. 8

Siku iliyo kabla ya Ufufuo

Ukae kimya mbele za Yehova, ukamngojee wala usikasirike; naye atakupa haja za moyo wako.

Zaburi 37. 7, 4

Ufufuo

Na ashukuriwe Mwenyezi Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye katika rehema zake kuu, ametuzaa sisi mara ya pili kwa njia ya kufufuliwa kwake Yesu Kristo. *I Petero 1. 3*

Siku ya Kupaa

Kwa kuwa tuna kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mwenyezi Mungu, na tukiendee hicho kiti-cha-neema kwa uthubutifu, ili kwamba tupate rehema na kuona neema ya kutusaidia wakati wa haja. *Wahibirania 4. 14, 16*

Pentecost

Mapenzi ya Mwenyezi Mungu yamekwisha kumi-minwa na kutiwa ndani ya mioyo yetu na Roho Mtakatifu ambaye tumepewa sisi. *Warumi 5. 5*

Utatu

Mwenyezi Mungu ni mapenzi; na ye ye akaaye katika mapenzi yuakaa ndani ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu yuakaa ndani yake ye. *I Yohana 4. 16*

Watakatifu Wote

Kwa kuwa tumezingirwa na wingu kubwa la mashahidi jansi hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na

hiyo dhambi iliyotuzunguka sisi kwa wepesi, na tupige mbio kwa uvumilivu kwa yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtzama Yesu, mwenye kuanziliza na mwenye kutimiliza imani yetu.

Wahibirania 12. 1-2

Siku za Watakatifu

Mwenye haki atakumbukwa milele. Kuwakumbuka hao wenye haki huwa na baraka.

Zaburi 112. 6 ; Mifano 10. 7

Mwaka Mpya

Hao warngojeao Yehova watarejeza upya nguvu zao ; watakwea juu kwa mabawa mfano wa kipungu ; watapiga mbio, wasichoke ; watakwenda kwa miguu, nao hawatazima roho.

Isaya 40. 31

Mavuno

Nchi na vyote vijazavyo ni mali ya Yehova.

Zaburi 24. 1

Wakati wa Mashaka

Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu : msaada uonekanao wakati wa mateso.

Zaburi 46. 1

Mambo ya Ufalme

Mataifa wafurahi na kuimba kwa furaha : kwani wewe utawahukumu watu kwa haki, utawaongoza watu walioko duniani.

Zaburi 67. 4

ENYI ndugu zangu mpendwao sana, twaonyeshwa katika Maandiko mwahali kadhwakadha, ya kukiri na kuyaungama madhambi yetu na viovu vyetu kila namna ; pasipo kuvificha wala kuvifinika mbele ya uso wa Mwenyezi Mungu Babaetu wa mbinguni : twaonyeshwa ya kuiungama kwa moyo wa unyotige na unyenyekevu, wenye kutubia na kufuata ; ili kwamba kwa wema wake na rehema zake zisizo ukomo, tupate kusamehewa. Nasi ingawa kule kumwekea wazi Mwenyezi Mungu madhambi yetu kwa unyenyekevu ni neno litupasalo sana kila wakati ;

ni zaidi sana wakati tukutanapo wenye kwa wenye kwa kumshukuru kwa rehema kuu tulizopokea mikononi mwake, na kumsifu kama ilivyopasa sana, na kusikiza Neno lake lililo takatifu, na kumtaka kadiri ya tulivyo na haja navyo, rohoni hata mwilini. Basi, kwa ajili ya hayo, mimi nawasibi ninyi nyote mliopo, mfuatane nami kwa miyo myeupe, na sauti nyenyekevu, tuje tukaribie katika kiti cha neema ya mbinguni, mseme nyuma yangu ;

¶ Hapa Padre aweza kusema maneno kama haya, akiona ni vizuri :

TUKIWA tumepiga magoti, na tukae kimya kwa dakikachache, tukikumbuka ya kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi hapa.

¶ Haya ni maneno ya watu pia wote, ya kuungama makosa, nayo husemwa na watu wote nyuma yake yule Padre, hali wamepiga magoti pia wote.

EWE Baba, Mwenyezi, Mwingi wa rehema ; Sisi tumekosa, Tumepotea njia zako, kama kondoo waliopotea. Tumefuata mno mashauri na tamaa za miyo yetu wenye kwa kuiungama makosa yao. Uwakubali waliotubia : Kama ahadi zako walizofunuliwa wanadamu katika Kristo Yesu, Bwana wetu. Kisha, Baba mwingi wa rehema, Utupe kwa ajili yake yeye ; Ya sisi kuishi tangi leo maisha ya uchaji-wa-Mungu na haki na mambo ya kiasi, Kwa kulitukuza jina lako lililo safi. *Amina.*

¶ Ghofira, au Ondoleo la madhambi : nalo hutamkwa na Kasisi pekee, hali amesimama, watu wakali wamepiga magoti.

MWENYEZI Mungu, Babaye Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye hataki mauti ya mwenye dhambi, afadhalii ataka auache uoyu wake awe hai : naye amewapa

amri watumishi wake, amewaagiza, ya kuwaeleza na kuwaambia watu wake waliotubia, ya wao kusamehewa na kuondolewa madhambi yao : ye ye huwasamehe na kuwondolea madhambi wote waliotubu kweli, walioamini Injili yake takatifu pasipo kuitilia shaka. Kwa ajili ya hayo na tumwombe atupe toba ya kweli, atupe na Roho wake Mtakatifu, ili tuyafanyayo hivi sasa yampendeze ; na maisha yetu ya tangu sasa yawe safi na utakatifu, ili mwisho tufikilie katika furaha zake za milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu.

¶ Hapa na kila pakomapo Sala watu huitika, Amina.

¶ Kisha Padre hupiga magoti na kuisoma Sala ya Bwana kwa sauti ya kusikilikanu : na watu nao hali wamepiga magoti, husoma pamoja naye : kwa wakati huo, na kila itumiwapo katika Ibada ya Mwanyezu Mungu.

BABAETU uliyembinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa ; Utuokoe maovuni : Kwa kuwa ufalme, na nguvu, na urukufu, ni vyako milele. *Amina.*

¶ Kisha husoma,

Ewe Bwana, ufunue midomo yetu.

Huitika. Na vinywa vyetu vitatangaza utukufu wako.

Padre. Ewe Mungu, utuokoe upesi.

Huitika. Ewe Bwana, utusaidie haraka.

¶ Wakati huo watu wakiisha kusinama wote, Padre husoma,

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Huitika. Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

Padre. Msifuni Bwana.

Huitika. Jina la Bwana lisifiwe.

¶ Hapa husomwa au kuimbwa Zaburi, kwa taratibu yake kama ilivyoagizwa. Kisha husomwa Somo la Agano la Kale kama ilivyoagizwa. Na baada ya hayo, huwa Magnificat (au Wimbo wa Mwanamwali Mariamu Mbarikiwa), kama ilivyoletwa hapa.

MAGNIFICAT

Luka 1. 46-55

MOYO wangu wamtukuza Bwana : na roho yangu mimemfurahia Mungu Mwokozi wangu.

Kwa kuwa ameuangalia : unyonge wa kijakazi chake.

Kwani tazama, mwanzo wa sasa : watanitaja kwa wema vizazi vyote.

Kwa kuwa Mwenye-nguvu amenifanyia mambo makuu : na Jina lake ni takatifu.

Tena rehema zake hufikilia vizazi na vizazi : kwa hao wenye kumcha.

Amefanya ubora kwa mfono wake : amewatawanya wenye unyeti katika mawazo ya mioyo yao.

Wenye kutawala amewashusha katika viti vyao vy enzi : tena amewatukuza wanyonge.

Wenye njaa amewajazia tele viti vyema : na matajiri amewaondo utupu.

Amemsaidia Isiraeli mtumishi wake, apate kuwakumbukia rehema : kama alivyosema na baba zetu, Iburahimu na uzao wake, milele.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

¶ Au, badala yake ni Zaburi hii : isipokuwa Mwezi Kumi na Kenda, husomwa hii katika Zaburi, kama zifuananavyo daima.

CANTATE DOMINO

Zaburi 98

MWIMBIENI Yehova wimbo mpya : kwani amefanya mambo ya ajabu.

Mkono wa kuume wake ye ye : mfono wake mtakatifu umemtendea wokofu.

Yehova ametamburisha wokofu wake : machoni mwa hao mataifa ameifanya wazi haki yake.

Amekumbuka ihisani yake na uaminifu wake : kwa nyumba ya Isiraeli.

Ncha zote za nchi zimeuona : wokofu wa Mungu wetu.

Mshangilieni Yehova, nchi nzima yote : inueni sauti, imbeni kwa furaha, imbeni zaburi.

Mwimbieni Yehova za kinanda : kwa kinanda na sauti ya zaburi.

Kwa tarumbeta na baragumu : shangilieni mbele za Mfalme Yehova.

Bahari na ititime na vilivyoja humo : ulimwengu na wauketio.

Mito na ipige kofi : vilima na viimbe kwa furaha pamoja,

Mbele za Yehova : kwa kuwa yuaja ili kuihukumu nchi.

Ulimwengu atauhukumu haki : na hao mataifa kwa ulikevu.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ Kisha husomwa Somo katika Agano Jipya, kama ilivyoamriwa. Na baadaye, Nunc Dimitis (au Wimbo wa Simeon), kama ulivyoletwa hapa.

NUNC DIMITTIS

Luka 2. 29-32

SASA wamruhusu mtumwa wako, Bwana : mfano wa Sneno lako, kwa amani.

Kwa kuwa macho yangu : yameuona wokofu wako, Uliouweka tayari : mbele ya watu wote ;

Mwanga wa kuwafunulia mambo mataifa : tena utukufu wa watu wako Isiraeli.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ Au, badala yake huwa Wimbo huu katika Zaburi, isipokuwa kwa siku ya Mwezi Kumi na Mbili.

DEUS MISEREATUR

Zaburi 67

MUNGU na atufanyie fadhili, atubarikie : na atufikizie nuru za uso wake kwetu :

Ili njia yako itamburikane juu ya nchi : wokofu wako ujulikane katika mataifa wote.

Watu na wakushukuru wewe, Mungu : watu wote pia na wakushukuru wewe.

Mataifa na wafurahi, waimbe kwa furaha : kwa kuwa wewe utawahukumu watu haki, utawaongoza mataifa walio duniani.

Watu na wakushukuru wewe, Mungu : watu wote pia na wakushukuru wewe.

Nchi na itoe mazao yake : Mungu, Mungu wetu, na atubarikie.

Mungu atatubarikia : ncha zote za dunia na zimche yeye.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ Hapo huimbwa au husomwa Imani ya Mitume na yule Padre : a wale watu, hali swamesimama.

NAAMINI kwa Mungu Baba, Mwenyezi, Muumba-mbingi na nchi :

Na kwa Yesu Kristo, Mwanawе pekee, Bwana wetu, ambaye alitungishwa mimba na Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Mwanamwali Mariamu, Akateswa katika enzi ya Pontio Pilato, Akasalibiwa, akafa, akazikwa, Akashuka na kuingia kuzimu ; Hata siku ya tatu akasimama tena, ametoka kwa wafu, Akapaa na kuingia mbinguni, Naye ameketi upande wa mkono wa kuume wa Mwenyezi Mungu, Baba ; Ndiko atakakotoka, kuja kuwaamua walio hai hata waliokufa.

Naamini kwa Roho Mtakatifu ; na Kanisa Takatifu

lililo ulimwenguni mote ; na Ushirika wa Watakatifu ; na Madhambi kusamehewa ; na Mwili kufufuka ; na Maisha ya milele. Amina.

¶ Kisha husaliwa Sala hizo zifuatazo hapa, watu hali wamepiga magoti kwa makini ; yule Padre hutangulia kutamka kwa sauti kuu,

Bwana na awe pamoja nanyi.

Huitika. Na awe pamoja na roho yako.

Padre. Na tuombe.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

¶ Hapo yule Padre na waimbaji na wale watu husoma Sala ya Bwana kua sauti kuu.

BABAETU ulije mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa ; Utuokoe maovuni. Amina.

¶ Hapo Padre husimama akasema,

Ewe Bwana, utuonyeshe rehema yako juu yetu ;

Huitika. Utupe na wokofu wako.

Padre. Ewe Bwana, umweke salama Mfalme.

Huitika. Nawe utusikize kwa rehema, wakati tukulunganapo.

Padre. Uwavike haki watumishi wako.

Huitika. Uwaweke na furaha wateule wako.

Padre. Ewe Bwana, uwaokoe watu wako.

Huitika. Ubarikie na urithi wako.

Padre. Ewe Bwana, utupe amani kwa hizi zamani zetu ;

Huitika. Kwa maana, hakuna mwenye kututetea, asiyekuwa wewe, Mwenyezi Mungu.

Padre. Ewe Mwenyezi Mungu, utufanye safi mioyo yetu ndani.

Huitika. Wala usituondolee Roho wako Mtakatifu.

¶ Hapo hifuata Sala tatu ; ya Kwanza ni ya Siku ile ; ya Pili ni ya kuombea Amani ; ya Tatu ni ya kuombea Msaada wa kukingia hatari zote, kama ijetawayo humu baadaye ; na Sala hizi mbili za mwisho husoma siku zote wakati wa Sala ya Jioni mwaka mzima, hazibadiliki.

SALA YA PILI KATIKA SALA YA JIONI

EWE Mwenyezi Mungu, ambaye kwako wewe huanza tamaa takatifu zote, na mashauri mema yote, na kazi za haki zote ; utupe watumishi wako hiyo amani ambayo ulimwengu hauwezi kutupa ; ili mioyo yetu ikazane katika kuyashika maagizo yako, kisha na kwa vile tunavyolindwa na wewe na hofu ya adui zetu, iwe sisi kwendesha siku zetu kwa starehe na utulivu ; kwa ajili ya kustahili kwake Yesu Kristo, Mwokozi wetu. *Amina.*

SALA YA TATU, YA KUOMBEA MSAADA KILA WAKATI WA HATARI

UTUTILIE nuru katika giza yetu, twakuomba Bwana ; nawe kwa rehema zako kubwa utuhifadhi na hatari zote na zani zote za usiku huu ; kwa ajili ya mapenzi ya Mwanayo pekee, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

¶ Katika mambio na penye waimbaji, hapa huleta Wimbo.

SALA YA KUMWOMBEA MTUKUFU MFALME

EWE Bwana, Babaetu wa mbinguni, mtukufu, mweza, Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana, Mtawala-maseyidi pekeo, nawe huko uliko kitini mwako unawa-angalia watu wote pia qaa duniani ; sisi twakuomba sana umwangalie kwa neema yako Bwana wetu Sultanii mwenye ihisani, Mfalme *GEORGE* ; umwongeze sana neema hiyo ipatikanayo kwa Roho wako Mtakatifu, hata awe siku zote kuyashika uyapendayo wewe, na kwenenda umlekezako : umvike vipawa vyako vya mbinguni kwa wingi ; umkirimu kuishi sana kwa afya na uwemo ; umtie nguvu apate kuwashinda na kuwapita adui zake wote ; na baada ya haya, kisha, afikilie furaha na baraka zisizokoma ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

**SALA YA KUWAOMBEA WATU WA JAMAA YA
UFALME**

EWE Mwenyezi Mungu, shina la wema wote, sisi twakuomba sana kwa unyenyekevu umbarikie mkewe mfalme wetu, Bibi *Elizabeth* mwenye fadhili, na Bibi *Mary* mamaake mfalme, na *Princess Elizabeth*, na jamaa wote wa Ufalme: uwavike Roho wako Mtakatifu; uwaneemeshe neema yako ya mbinguni; uwafanishe kwa raha yote; uwafikishe na katika usalme wako wa milele; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

**SALA YA KUWAOMBEA MAPADRE WA KANISANI NA
WATU WAO**

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, kila miujiza bora hakuna mwenye kuifanya isipokuwa wewe; twawaombea mabishopu wetu na watanzao roho za watu, na vikao vyote vya watu walivyopewa hao kuvitunza, ya kwamba uwashushie Roho wako, ambaye ni Mpaji wa neema yako; kisha, ili kwamba watu hao wakupendeze kweli, uwamiminie urmande usiokoma wa baraka yako. Utupe haya, twakuomba, Bwana, kwa ajili ya heshima ya Msada wetu, Mwombezi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

SALA YA MTAKATIFU CHRYSOSTOM

EWE Mwenyezi Mungu, uliyetupa neema sisi kwa wakati huu kukuletea wewe maombi yetu sote pia kwa nia moja; nave ndiwe mwenye kutoa ahadi ya kwamba, watu wawili watatu watakapokutanika pamoja kwa jina lako, utawapa wakutakayo: ututimizie sasa, Bwana, haja zetu na sala zetu watumishi wako, kwa jinsi yatakavyotufaa; kwa kutupa kuijua kweli yako katika ulimwengu huu, na maisha ya milele katika ulimwengu ujao. *Amina.*

2 *Wakorintho 13. 14*

NEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, viwe pamoja nasi sote milele. *Amina.*

Taratibu ya Salaya Jioni ya kila siku mwaka mzima imekoma hapa

WAKATI WA SALA YA ASUBUHI

¶ *Katika Idi hizi*; Idi ya Uzazi wa Kristo (*au, Christmas*), na ya Mafunuo, na ya Mtakatifu Mathia, na ya Ufufuo, na ya Kupaa juu, na ya Pentecost, na ya Mtakatifu Yohana Mbatizaji, na ya Mtakatifu Yakobo, na ya Mtakatifu Baritolamayo, na ya Mtakatifu Mathayo, na ya Mtakatifu Simoni pamoja na Mtakatifu Yuda, na ya Mtakatifu Andarea, na ya Jumapili ya Utatu, katika wakati wa *Sala ya Asubuhi*, badala ya *Imani ya Mitume*, huimbwa au hisomwa huku kukiri kwa *Imani* yetu ya Ukristo, ambako huiwa *Imani* ya Mtakatifu Athanasio, na huyo Padre na wale watu, hali wamesimama.

QUICUNQUE VULT

APENDAYE aokoke, awaye yote, linalomlazimu Akwanza: ni kuishika *Imani* iliyo ya Kanisa la Kristo lililo ulimwenguni mote.

Nayo *Imani* hiyo mtu asipoishika kwa utimilifu wake na kuisafi: hana shaka atapotea milele.

Nayo hii ndiyo *Imani* iliyo ya Kanisa la Kristo lililo ulimwenguni mote: ya sisi kumwabudu Mungu mmoja katika Utatu, na ule Utatu katika Umoja.

Pasipo kuzichanganya kwa fujo Nafsi zake: wala kui-gawanya ile tabia yake ya asili.

Kwani mna Nafsi moja ya Baba, na Nafsi ya pili ya Mwana: na Nafsi moja tena ya Roho Mtakatifu.

Lakini ule Uungu, katika Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, ni Uungu Mmoja tu: ule Utukufu wake ni sawa, ile enzi yake ni ya milele katika Umoja.

Kama alivyo Baba, na Mwana yu vivyo: yu vivyo na Roho Mtakatifu.

Baba asiyembwa, na Mwana asiyembwa: na Roho Mtakatifu asiyembwa.

Baba asiyefahamika, na Mwana asiyefahamika: na Roho Mtakatifu asiyefahamika.

Baba yuko milele, na Mwana yuko milele : na Roho Mtakatifu yuko milele.

Pamoja na haya, hakuna watatu wa milele : wa milele ni mmoja.

Kisha ni vivyo hivyo hakuna watatu wasiofahamika, wala hakuna watatu wasioumbwa : bali aliye kono ni mmoja asiyembwa, ni mmoja asiyefahamika.

Ni kama vile, Baba ni Mwenyezi, na Mwana ni Mwenyezi : na Roho Mtakatifu ni Mwenyezi.

Kisha, hakuna watatu walio Wenyesi : aliye Mwenyezi ni Mmoja.

Ni vivyo, Baba ni Mungu, na Mwana ni Mungu : na Roho Mtakatifu ni Mungu.

Kisha hakuna Waungu watatu : lakini aliye kono ni Mungu Mmoja.

Ni vivyo Baba ni Bwana, na Mwana ni Bwana : na Roho Mtakatifu ni Bwana.

Kisha hakuna Mabwana watatu : lakini aliye kono ni Bwana Mmoja.

Kwani kama ilivyotulazimisha Kweli ya Ukristo kumkiri kila Nafsi moja kuwa Mungu : naye kuwa Bwana :

Ndivyo tulivyokatazwa na Dini iliyo ya Kanisa la Ukristo lililo ulimwenguni mote kusema kwamba kuna Waungu watatu : au kwamba kuna Mabwana watatu.

Baba alivyo hakufanywa na awaye yote : hakuumbwaa, hakuzawa.

Mwana alivyo ni katika Baba pekee : hakufanywa, hakuumbwaa, ila amezawaa.

Roho Mtakatifu alivyo ni katika Baba na katika Mwana : hakufanywa, hakuumbwaa, ila yuatoka.

Ni hivyo, aliye kono ni Baba mmoja, hakuna Mababa watatu, ni Mwana mmoja, hakuna Wana watatu : ni Roho Mtakatifu mmoja, hakuna Maroho Watakatifu watatu.

Na katika Utatu huo, hakuna aliye mbele, wala aliye nyuma : hakuna mkuubwa kuliko mwensiwe, hakuna mdogo kuliko mwensiwe.

Ila Nafsi zote tatu ziko milele katika umoja : kisha ni sawa katika umoja.

Hata liliopasa katika mambo yote, kama ilivyotangulia kutajwa : ni la kuabudiwa ule Umoja katika Utatu, na ule Utatu katika Umoja.

Basi na apendaye aokoke : inampasa kuuona hivyo ule Utatu.

Na zaidi ya hayo, yamlazimu kwa wokofu wa milele : kuamini sawasawa na katika habari ya Bwana wetu Yesu Kristo kufanywa mwili.

Kwani imani iliyonyoka ni hiyo, ya sisi kuamini mio-yoni na kukiri : kwamba Bwana wetu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ni Mungu, naye ni Binadamu ;

Ni Mungu, kwa Yeye kutokana na Tabia ya Asili ya Baba, amezawa kabla ya dahari : ni Binadamu, kutokana na Tabia ya Asili ya Mamaye, amezaliwa katika ulimwengu huu ;

Ni Mungu mtimilifu, ni Binadamu mtimilifu : mwenye kuwa na nafsi yenyewe akili na mwili wa Binadamu.

Yu sawa na Baba kwa hesabu ya Uungu : apitwa na Baba kwa hesabu ya u-Binadamu.

Kisha na angawa ni Mungu pamoja na kuwa Binadamu : lakini yeze si wawili, ila Kristo ni mmoja.

Na alivyo mmoja, si kwa ule Uungu kugeuka kuwa mwili : ila ni kwa ule u-Binadamu kutwawa kuwa katika Mungu ;

Ni mmoja halisi : si kwa ile Tabia ya Asili kuchanganya kwa fujo : ni kwa umoja wa Nafsi.

Kwani kama ambavyo moyo wenye akili na mwili wa ki-Binadamu ni Binadamu mmoja : ndivyo ilivyokuwa Mungu na Binadamu kuwa ni Kristo mmoja ;

Aliyeteseka kwa ajili ya wokofu wetu : akashuka chini kuzimu, akasimama tena kwa siku ya tatu, hali ametoka kwa wafu.

Akapaa akaingia mbinguni, naye ameketi upande wa mkonko wa kuume wa Baba, Mungu Mwenyezi : nako ndiko atakakotoka, kuja kuwashukumu walio hai hata walio kufu.

Naye wakati wa kurudi kwake inapasa watu wote kufufuka kusimama na miili yao : na kutoa hesabu ya vitendo vyao, kila mmoja.

Kisha waliofanya mema wataingia katika maisha ya milele : waliofanya maovu wataingia katika moto wa milele.

Hiyo ndiyo Imanī ya Kanisa la Kristo lililo ulimwenguni mote : nayo mtu asipoīamini sawa kwa uaminifu, hapati kuokoka.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

LITANIA

¶ Hapa yalerwa LITANIA, au Matangamano ya Sala, hutumiwa katika mwisho wa Sala ya Asubuhi, kwa siku za Jumapili na Jumatano na Ijuna, na nyakati nyingine atakazooza vyema yule Mwencie amri ; nayo huimbwa au husomwa.

E WE Mungu Baba, wa mbinguni : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Ewe Mungu Baba, wa mbinguni : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Ewe Mungu Mwana, Mkombozi wa ulimwengu : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Ewe Mungu Roho Mtakatifu, utokaye kwa Baba na kwa Mwana : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Ewe Mungu Roho Mtakatifu, utokaye kwa Baba na kwa Mwana : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Ewe Utatu, Mtakatifu, Mwenye-baraka, Mtukufu, Nafsi tatu, Mungu mmoja : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Ewe Utatu, Mtakatifu, Mwenye-baraka, Mtukufu, Nafsi tatu, Mungu mmoja : uturehemu maskini wenyewe dhambi.

Usikumbuke makosa yetu, Bwana, wala makcsa ya baba zetu ; wala usitwae kisasi cha dhambi zetu ; utusamehe, Bwana mwema, utusamehe watu wako, uliowakomboa kwa damu yako ya thamani, wala usitukasirikie milele.

Utusamehe, Bwana mwema.

Uovu wote na madhara yote ; dhambi, na hila, na majoribu ya Shetani ; hasira zako, na kuhukumiwa adhabu ya milele,

Bwana mwema, utuokoe nayo.

Upofu wa moyo kila aina : kunyeta, na kujiona, na unafiki ; uhaside, na uchukivu, na mfundo wa moyo, na upungufu wa mapenzi kila aina,

Bwana mwema, utuokoe nayo.

Uzinifu, na dhambi za mauti nytingine kila aina ; na hila zote za dunia, na mwili, na Shetani,

Bwana mwema, utuokoe nayo.

Radi na tufani ; baa, na tauni, na njaa ; vita na uuaji, na mauti ya ghafula,

Bwana mwema, utuokoe nayo.

Fitina, na shauri la uasi, na uhalifu kila aina ; elimu ya uwongo, na uzuzi, na matengano kila aina ; uzito wa moyo, na kudharau Neno lako na Maagizo yako,

Bwana mwema, utuokoe nayo.

Nawe kwa siri ya Ulivyotwaa mwili ; na kwa Kuzaliwa kwako kutakatifu na Kutahiriwa kwako ; kwa huo Ubatizo wako, na hivyo Ulivyofunga, Ukajaribiwa,

Bwana mwema, utuokoe.

Kwa hiyo Dhiki iliyokupata na hizo Hari zako za damu ; kwa Msalaba wako na Mateso yako ; kwa Mauti yako ya thamani na Kuzikwa kwako ; kwa Kufufuka kwako kutukufu na Kupaa kwako ; na kwa Roho Mtakatifu kutujia,

Bwana mwema, utuokoe.

Kila tusumbuliwapo, na kila tufanikiwapo ; saa ya kufa, na siku ya hukumu,

Bwana mwema, utuokoe.

Sisi wenyewe dhambi twakuomba sana utusikize, Ewe Bwana Mungu wetu ; kisha uone vyema kulkamuru na kilitawala kanisa lako takatifu lililo ulimwenguni mote liishike njia iliyolcke ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi kumweka na kumtia imara katika ibada yako ilioy kweli, na katika maisha yaliyolekea na kutakata, Mtumishi wako *GEORGE*, Mfalme wetu mwenye fadhilli nyangi, Mtawala wetu ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi kumtawala moyo wake kwa imani yako, na kicho chako, na mapenzi yako, naye siku zote aendelee kukutumaini wewe, atafute na heshima yako na utukufu wako kwa mambo yote ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi wewe kuwa Mteteaji wake, na ulinzi wake, kwa kumpa kushinda adui zake wote ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi kuwabarikia na kuwahifadhi mkewe Mfalme wetu, Bibi *Elizabeth* mwenye fadhili, na Bibi *Mary* mamaake Mfalme, na *Princess Elizabeth*, na jamaa wote wa Ufalme ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, kuwafikiliza neema yako Wakubwa wa nchi hii, na walio na amri wote, ili waupate usfalme wako wa mbinguni ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, hao mabishopu wote, na makasisi wote, na mashemasi wote ; kuwapa mwanga wa kweli ulio na maarifa na fahamu ya Neno lako, walifunue na kuliweka wazi, huku kwa kuhubiri na huku kwa kuishi ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

(Uwe radhi kuwabarikia watumishi wako watakaokubaliwa sasa kuwa mashemasi na makasisi, uwamiminie neema yako, ili watimizie kazi yao kwa kujenga kanisa lako, na kwa kutukuzza jina lako takatifu ;

Kutumiwa katika majuma ya Nyakati nne za mwaka ; na siku ya watu kupewa daraja la kanisa kwa kuwekewa mikono.

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, hao wazee wa Baraza ya Mfalme na jamii ya Makabaila, kuwavika fadhili, na hekima, na fahamu ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, hao Wenye-amri kuwabarikia na kuwalinda, kwa kuwapa neema ya kupisha hukumu kwa haki na kuitetea ile kweli ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, watu wako wote, kuwabarikia na kuwalinda ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi mataifa yote, kuwapa umoja, na amani, na masikizano ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, kutupa sisi miyo ya kukupenda na kukucha, na kufanya bidii kuyanyosha maisha yetu kama maagizo yako ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, watu wako pia wote, kuwapa ma^ong^eo ya

LITANIA

neema, ili wawe wenye kulisikiza Neno lako kwa unyenyekevu, na kulipokea kwa mapenzi yaliyo safi, na kuzaa matunda ya Roho ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, kadiri ya waliokosa, wenye kudanganyika, kuwatia katika njia ya kweli ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, hao waliosimama kuwapa nguvu ; na wenye miyo dhaifu kuwatia imara na kuwasaidia ; na waliangoanga kuwainiu ; hata mwishowe kumpomosha Shetani chini ya miguu yetu ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, walio katika hatari, na uhitaji, na masumbuko, kuwatunza na kuwasaidia na kuwatuza miyo, pia wote ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, watu wote wasafirio bara na bahari, na wanawake wenye uchungu, na watu waugua, na watoto wakuao, kuwalinda wote ; na wafungwa wote na mateka wote kuwafikiliza huruma zako ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, watoto mayatima na wanawake waliofiliwa na waume, na wote walio hali ya ukiwa na kuonewa, watu hao kuwahifadhi na kuwaruzuku ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi kuwarehemu watu wote ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, adui zetu, na watesi wetu, na watu watuambao kwa uovu, kuwasamehe, na kuwalekeza miyo yao katika njia ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, kutupa matunda ya nchi kwa aina zake na kutuhifadhia, tuplicate kuyatumia na kuyafurahia kwa zamani zake ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

Uwe radhi, kutupa sisi toba ya kweli ; nawe usitamehe madhambi yetu yote, na ulegevu wetu wote, na ujinga wetu wote ; nawe utuvike neema ya Roho wako Mtakatifu, tuyafanyize maisha yetu kama Neno lako takatifu ;

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

LITANIA

Mwana wa Mungu ; twakuomba utusikize.

Mwana wa Mungu ; twakuomba utusikize.

Ewe Mwana-wa-kondoo wa Mwenyezi Mungu, mwenye kuziondoa dhambi za ulimwengu ;

Utupe amani yako.

Ewe Mwana-wa-kondoo wa Mwenyezi Mungu, mwenye kuziondoa dhambi za ulimwengu ;

Uturehemu.

Ewe Kristo, utusikize.

Ewe Kristo, utusikize.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

¶ Ndipo hapo yule Padre, na wale watu pamoja naye, huisoma Sala ya Bwana.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo inkate wetu wa kututosha. Nawe usitamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupileke katika kujaribiwa ; Utuokoe maovuni. Amina.

Padre. Ewe Bwana, usitutwae kama makosa yetu.

Huitika. Wala usitupatilize kwa viovu vyetu.

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, Baba mwingi wa rehema, huyadharau maugazi ya moyo uliovunjika, wala kutamani kwao walio na majonzi ; uzikubali kwa rehema sala zetu tukuleteazo mbele zako kwa mashaka yetu yote na ukiwa wetu wote, kila yatulemeapo ; utusikize kwa neema, ili hivyo viovu, tutengezewavyo na hila na werevu wa Shetani au binadamu, vitanguke, viondolewe ; navyo kwa uangalizi wa wema wako vitawanyike ; ili kwamba sisi watumishi wako tusidhuriike kwa masumbuko yawayo yote,

LITANIA

twendelee katika kukushukuru wewe daima katika kanisa lako takatifu, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu.

Ewe Bwana, inuka, utusaidie, utuponye kwa ajili ya jina lako.

Ewe Mwenyezi Mungu, sisi tumesikia kwa masikio yetu, baba zetu warnetuwekea wazi mambo makuu uliyofanya kwa siku zao, na zamani za kale mbele yao.

Ewe Bwana, inuka, utusaidie, utuponye kwa ajili ya heshima yako.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Huitika. Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Utukinge na adui zetu, Ewe Kristo.

Uyaangalie kwa fadhili yako mateso yetu.

Uyatazame majonzi ya mioyo yetu kwa huruma.

Uyasamehe makosa ya watu wako kwa rehema.

Uzisikize sala zetu, uzikubali pamoja na kuturehemu.

Ewe Mwana wa Daudi, uturehemu.

Hivi sasa na zamani zote ukubali kutusikiza, Ewe Kristo.

Utesikize kwa fadhili yako, Ewe Kristo ; utesikize kwa fadhili yako, Ewe Bwana Kristo.

Padre. Ewe Bwana, rehema zako na zionekane kwetu ; Huitika. Kwa vile tunavyokutumaini wewe.

Na tuombe.

EWE Baba, tu miguuni pako, twakuomba sana uurehemu udhaifu wetu ; nawe kwa ajili ya utukufu wa jina lako, utupishie mbali maovu hayo yote tuliyostahili kwa haki mno ; tena utukirimu ya kwamba, kila tukipatikana na mashaka tulitie tumaini letu lote na mategemeo yetu yote katika rehema zako, na kwendelea daima katika kukutumikia kwa maisha safi na utakatifu, kwa kukuletea heshima na utukufu : kwa Mwombzei wetu, Msaada wetu, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

LITANIA

SALA YA MTAKATIFU CHRYSOSTOM

EWE Mwenyezi Mungu, uliyetupa neema sisi kwa wakati huu kukuletea wewe maombi yetu sote pia kwa nia moja ; nawe ndiwe mwenye kutoa ahadi ya kwamba, waru wawili watatu watakapokutanika pamoja kwa jina lako, utawapa wakutakayo : ututimizie sasa, Bwana, haja zetu na sala zetu watumishi wako, kwa jinsi yatakavyotufaa ; kwa kutupa kuijua kweli yako katika ulimwengu huu, na maisha ya milele katika ulimwengu ujao. *Amina.*

2 Wakorintho 13. 14

NEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, viwe pamoja nasi sote milele. *Amina.*

LITANIA imekoma hapa

SALA NA SHUKRANI

za nyakati za haja mbalimbali

Hutumiwa kabla ya Sala mbili za mwisho katika Litania, au katika Sala za Asubuhi na Jioni.

Sala

YA KUOMBEA MVUA

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, wewe kwa Mwanayo Yesu Kristo umewapa ahadi watu wote ambao wautafuta ufalme wako, na haki yake, ya wewe kuwapa hao vitu vyote vipasavyo kuwa riziki za miiili yao ; twakuomba sana, utuletee hivi sasa katika wakati wa uhitaji wetu, mvua na manyonyota mema, kadiri ya kutupa kuyapokea mazao ya nchi, kwa utozo wetu na heshima yako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

YA KUOMBEA KIANGA

EWE Mwenyezi Mungu, wewe hapo kale kwa ajili ya makosa ya binadamu uliigharikisha dunia nzima, isipokuwa watu wanane, kisha baadaye kwa rehema zako kubwa ukatoa ahadi ya kutoiangamiza tena dunia kama vile ; sisi tu miguuni pako, na tungawa tulistahili kupigwa na wewe kwa hiyo mvua iliyopita kiasi na hayo maji yaliyo mengi mno, lakini twakuomba sana utuonapo tumetubia kweli, utujalie kupokea mazao ya nchi kwa wakati wake : tujifunze huku kuyafanyiza upya maisha yetu kwa ajili ya adhabu yako hii, na huku *kukupa sifa na utukufu kwa ajili ya upole wako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

ZAMANI ZA SHIDA NA NJAA

EWE Mwenyezi Mungu, Baba wa mbinguni, ni katika vipawa vyako, la kunya mvua na nchi kubarikiwa, la nyama kuzaa na samaki kuwa wengi ; twakuomba uyangalie mteso ya watu wako ; nawe ukubali ya kwamba hii shida na hii njaa, ituadhibuyo hivi sasa kwa haki sana

kwa ajili ya viovu vyetu, igeuzwe kwa wema wako na rehema zako iwe neema na urahisi ; kwa ajili ya mapenzi ya Yesu Kristo, Bwana wetu, naye ni wa kusifiwa pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, kwa heshima yote na utukufu wote, sasa na milele. *Amina.*

Au hii,

EWE Mungu, Baba wa rehema, wewe uliyeigeuza Shida na njaa iliyokuwako Samaria zamani za nabii Elisha, ikageuka mara moja ikawa neema na urahisi ; uturehemu sisi tunaopiga sasa kwa mashaka kama hayo kwa ajili ya dhambi zetu, tusaidiwe kama vile ; uyazidishe mazao ya nchi kwa baraka yako ya mbinguni ; ukubali ya kwamba sisi tutakaoupokea ukarimu wako mwingi, tuutumie huo kwa kuuzidisha utukufu wako, na kuwasaidia wenye dhiki, na kwa manufaa ya nafsi zetu ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

ZAMANI ZA VITA NA MISHINDO

EWE Mwenyezi Mungu, Sultani wa masultani wote, Mtawala mambo pia, nguvu zako hakuna kiumbe kimoja awezaye kuzipinga, ni haki yako wewe kuwaadhibu wenyе dhambi, na kuwarehemu wanaotubia kwa kweli ; utuokoe sisi, twakuomba kwa unyenyekevu, na kutepusha na mikono ya adui zetu ; uvipunguze viburi vyao, uuondoe na uovu wao, uwabatilie hila zao ; ili tuwekwe salama milele na kila hatari kwa kucaa silaha za ulinzi wako, tupate kukutukuza wewe uliye pekeo Mpaji wa kushinda kote ; kwa ajili ya wema wake Mwanayo pekee, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

ZAMANI ZA TAUNI AU MARADHI, YALIYOWAPATA WATU WOTE

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa hasira zako uliwashushia watu wako tauni wakati walipomwasi Musa na Haruni kwa ule ushupavu wao, mle barani ; nawe katika zamani za mfalme Daudi ukaua watu elfu sabuini kwa tauni, lakini ulipokumbuka rehema zako ukawaokoa waliosalia ; utuhurumie sisi tulio dhaifu

wenye madhambi, ambao sasa twapatikana na ugonjwa mwingi na kufa kwingi ; nawe kama vilé uliviyokubali kufanyiwa sadaka wakati ule, ukamwamuru Malaika wako mwangamizi aache, asiadhibu ; na sasa uridhike vivyo katuondolea hii tauni, na haya maradhi mazito ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Katika MAJUMA ya NYAKATI NNE za MWAKA, zasomwa kila siku, kwa ajili ya watu watakaopewa DARAJA TAKATIFU :*

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, Euliyepata kanisa nchi zote kwa kulinunua kwa damu ya thamani ya Mpenzi wako Mwanayo ; uliangalie kwa rehema hilo kanisa lako, nawe wakati huu wa sasa, uziongoze sana na kuzitawala sana nia za watumishi wako mabishopu, wachungaji wa kundi lako, ili wasije wakawa kumwekea mtu mikono ghafula, awaye yote ; lakini na wachague kwa uaminifu na akili watu wanaofaa kutumika katika utumishi mtakatifu wa kanisa lako. Na hao watakaopewa daraja ya utumishi uwao wote, wewe uwape neema yako na radhi yako ya mbinguni ; ili kwamba huku kwa maisha yao na huku kwa kufunza kwao wauoneshe utukufu wako, wauendeleze na wokofu wa watu wote ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

EWE Mwenyezi Mungu, Mpaji wa vipawa vyema vyote, ambaye kwa uangalizi wako wa Uungu ume-weka madaraja mbali-mbali ya watumishi ndani ya Kanisa lako ; sisi miguuni pako twawaombea watu wote watakaoitwa humo kya utumishi uwao wote na uwakili uwao wote ; ya kwamba uwape neema yako, na kuwao-ngeza sana watu hao kweli ya elimu yako, na kuwapa usafi wa maisha, hata iwe wao kutumika mbele zako kwa uaminifu, kwa kuvutia utukufu jina lako kuu, na kulifaa kanisa lako takatifu ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ni Sala ifaayo kusomwa baada ya zilizotangulia mojawapo.*

EWE Mungu, ndiyo tabia yako kuwarehemu watu Emilele, na kuwasamehe, upokee hizi haja zetu nyekevu ; nasi tujapofungwa na kuzuiwa kwa mikufu ya madhambi yetu, lakini hizo huruma za wingi wa rehema zako na zitufungue ; kwa heshima yake Yesu Kristo, Mwombezi wetu, Msaada wetu. *Amina.*

¶ *Sala ya kuombea MKUTANO-wa-SHAURI uitwao PARLIAMENT, nayo husomwa muda unapokutana.*

EWE Mungu, mwingi wa neema, sisi twakunyenyekea miguuni pako, kisha kama vile tuucombeavyo Ufalme huu pia wote, tuombeacho sana ni' Mkutano-wa-shauri wa Parliament, hali umekutanika wakati huu wa sasa chini ya Mfalme wetu mcha-Mungu sana, mwenye fadhili sana ; nawe uone vyema kuyaongoza mashauri yao yote, kwa kuuongeza utukufu wako, na kwa kulifaa kanisa lako, na kwa kuleta salama na heshima na manufaa ya yeye Mkuu wetu, na ufalme wake ; ili kwamba, mambo yote jinsi yatakavyotengenezwa na kuamrishwa kwa bidii zao katika misingi bora ya salama, hata amani na raha, na kweli na haki, na dini na uchaji-wa-Mungu, yawe imara mambo hayo na kwendelezwa mbele kwetu hata vizazi vyote. Sisi, haja hizi na nyininge zote, twawaombea miguuni pako watu hao, na nafsi zetu na kanisa lako zima, kwa jina lake na Uombezi wake Yesu Kristo, Bwana wetu, Mwokozi wetu, abarikishaye kwa wingi. *Amina.*

¶ *Sala ya kuwaombea watu wa kila daraja, nayo hutumiwa kama wakati usioagizwa Litania.*

EWE Mungu, ndiwe Muumba watu wote, na ulinzi wao ; sisi tu miguuni pako, twawaombea wanadamu wote, kila aina na kila daraja ; uone vyema kuwaonyesha njia zako, salama yako iokoayo uwajuvishes mataifa yote. Na tuombealo sana, ni la kanisa lako lililo ulimwenguni mote hali yake kuwa njema ; liongozwe na kutawaliwa sana na Roho wako Mwema, hata wote wapendaao kuitwa

SALA

jina la Kristo, waongozwe katika njia ya kweli, na kuishika imani kwa umoja wa roho, na kifungo cha amani, na maisha yaliyolekeea. Baada ya haya, twa-kusongezea haja zao na kuzitia kwa wema wako wa ubaba, watu wawao wote wasumbukao na kuteseka kwa neno liwalo lote, la moyo, au la mwili, au la hali ; * (hasa hao watakiwao sala zetu,) uwe mwenye kuwatuliza na kuwasaidia, kila mtu kwa kadiri ya haja yake, huku ukiwapa kuvumilia katika mateso yao, na kupona masumbuko yao kwa salama. Na haya twakuomba kwa ajili ya Yesu Kristo. *Amina.*

* Haya ni ya kusonwa wakati zitakwapo sala za Mkuano.

SHUKRANI

SHUKRANI YA WATU WOTE

EWE Mwenyezi Mungu, Baba mwenye kila rehema, sisi watumishi wako tusiofaa, twakushukuru kwa unyenyekevu sana, kwa miyo yetu, ya wema wako wote na ihisani yako pia, uliyo nayo kwetu sisi na watu wote ; * (hasa hao watakao sasa kukupazia sifa na shukrani kwa neema zako ulizowapa hivi karibu.) Twakushukuru sisi ya tulivyoombwa, na kuhifadhiwa, na baraka zote za maisha haya ; ila zaidi sana, twakushukuru kwa mapenzi yako yasiyopimika kwa vile ulivyoukomboa ulimwengu kwa Bwana wetu Yesu Kristo ; tena kwa njia za neema, na tumaini la utukufu. Nasi twaomba sana kwako, kuwa na fahamu njema ya rchema zako zote, hata miyo yetu nayo iwe kukupelekea shukrani isiyo shaka, tupate kuonyesha sifa zako, huku kwa midomo yetu, na kuku kwa maisha yetu ; kwa vile tutakavyojivika katika utumishi wako, na kwenenda kwa utakatifu na haki siku zetu zote mbele zako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, ambaye ni wa kuheshimiwa na kutukuzwa pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, milele na milele. *Amina.*

* Maneno haya ni ya kusonwa wakati walioombwa warapo kutaka kumrejeza Mwenyezi Mungu sifa.

KWA AJILI YA MVUA

EWE Mungu Babaetu wa mbinguni, wewe kwa uangalizi wako wa neema huinyesha juu ya nchi mvua ya Mwaka na ya Vuli, ili itoe mazao yawe ni matumizi ya wanadamu ; sisi tu miguuni pako, twakushukuru kwa vile ulivyoona vyema kutupa msaada wakati wa hiyo shida yetu kuu, ukatuletea mwishowe mvua ya furaha, ukauburudisha urithi wako ulipokuwa mkavu, kwa kututuza mno miyo yetu sisi watumishi wako tusiofaa, na kulitkuza jina lako takatifu ; kwa rehema zako zilizo katika Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AJILI YA KIANGA

EWE Bwana Mungu, wewe una haki hivyo ulivyotupiga E kwa mvua isiyo kiasi, na maji mengi, nawe kwa rehema zako umetutuza roho zetu, umetufurahisha, kwa majira yalivyobadilika hivi kwa kufaa na kubariki ; sisi twalisifu na kulitkuza jina lako takatifu, kwa ajili ya rehema zako hizo, nasi hututaacha kutangaza wema wako kizazi hata kizazi, milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AJILI YA WINGI WA VYAKULA

EWE Baba mwinci wa rehema, wewe kwa wema wako Na fadhili zako umeyasikia maombi kanisa lako lili-yokuomba kwa uchaji-wa-Mungu, nawe huo uhitaji wetu na upungufu wetu umeugeuza umekuwa urahisi na wingi ; sisi twakushukuru miguuni pako kwa ajili ya huo upaji wako mkuu ; nasi twakuomba sana uudumishe kwetu, ili nchi yetu ituzalie mazao yake ya kuongea kwake, kwa utukufu wako na utuzo wetu ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AJILI YA AMANI NA KUEPUSHWA NA ADUI ZETU

EWE Mwenyezi Mungu, wewe ndiwe Mnara wa imara E wenye ulinzi wa watumishi wako nyusoni mwa adui zao ; sisi twakushukuru na kukupa asante kwa ulivytuepusha na hizo hatari kubwa zilizotuzunguka ; tume-kubali ya kuwa ni wema wako wewe, sisi kutoitiwa mikononi mwao kuwa mateka yao ; nasi twakuomba sana utudumishie rehema zako namna hii, ili ulimwengu wote ukujue wewe kuwa u Mwokozi wetu, Mponyi wetu mwenye nguvu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AJILI YA AMANI KURUDISHWA KATIKA WENYEJI

EWE Mungu, huna mwanzo huna mwisho, nawe Ndiwe Babaetu wa mbinguni ; ni wewe pekeo unayewafanya jamaa kuwa na nia moja katika nyumba yao, na

kunyamazisha jeuri za watu wakaidi na uasi ; sisi twalisifu jina lako takatifu, ya kwamba umependa kuituliza mishindo yenye fitina iliyokuwako hivi karibu ; nasi twakuomba sana miguuni pako, utupe neema sote pia, ili mwanzo wa sasa tuende katika maagizo yako matakatisu kwa kutii, na kwa tutakavyoishi maisha matulivu na amani katika kicho cha Mungu na haki kwa wenzetu, tukupe daima sadaka yetu ya sifa na shukrani kwa ajili ya hizo rehema ulizoturehemu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AJILI YA KUEPUKANA NA MARADHI YA TAUNI, AU MARADHI MENGINE YOYOTE

EWE Bwana Mungu, wewe umetupiga kwa ajili ya madhambi yetu, umetuangamiza kwa ajili ya makosa yetu, kwa mapatilizo mazito ya' utisho uliyotupatiliza hivi karibu ; nawe sasa, ulivyokumbuka rehema humo katika hukumu yako, umeziokoa roho zetu katika kinywa cha mauti ; twausongezea wema wako wa ubaba nafsi zetu, maana, roho zetu na miili yetu, ulivyoviponya wewe hivi sasa, viwe hivyo ni sadaka ilioyai kwako wewe, kwa tutakavyozisifu na kuzifahamu daima hizo rehema zako ndani ya Kanisa lako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

SISI tu miguuni pako, tumekubali mbele zako, ewe Baba mwinci wa rehema, ya kwamba adhabu zote wakamiwazo maasi katika sheria yako yangelitupata sisi kwa haki, kwa ajili ya hayo makosa yetu, na huo uzito wa mioyo yetu : lakini kwa kuwa umependa kwa rehema zako zenye huruma, kwa maana ya huko kujinyenyeka kwetu sisi wanyonge tusiofaa, kuyakomesha hayo maradhi yenye wito tuliyoadhibiwa kwa uzito hivi karibu, na kwa ulivyorudisha sauti ya furaha na afya nyumbani mwetu ; twakusongeza, ewe Mungu mtukufu, hizi dhabihu zetu za sifa na shukrani, kwa kulitkuza na kulisifu jina lako la ubora, kwa hivyo ulivyotuponya na kutuangalia ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA NA SHUKRANI KADHAWAKADHA

Sala na Shukrani hizi zifuatazo hapa hutumiwa kama Padre aonavyo vyema, zaidi baada ya Sala ya Tatu, au mwisho wa Litania, au katika Taratibu ya Ushirika Mtakatifu, baada ya Sala-ya Siku hiyo, au ya Sala ya kuombea Kanisa lililo katika vita hapa dumiani, au mbele ya Baraka.

SALA

(Sala hizi zaweza kusemwa pasipo vifungu vyake. Kisha yawezekana watu kutakwa kuomba kimya.)

KUMWOMBEA MFALME NA WOTE WALIO NA AMRI CHINI YAKE

Na tumwombee Mfalme na wote waliopewa amri chini yake.

Padre. Mfalme atazifurahia nguvu zako, ewe Yehova.

Huitika. Na wokofu wako ataufanya shangwe nyingi sana.

EWE Mwenyezi Mungu, shina la wema wote, sisi Tu miguuni pako, twakuomba umbariki Bwana wetu Mfalme *GEORGE*, na mikutano yote ya mashauri ilioy katika ufalme wake wote, na wote waliopewa amri chini yake : zaidi mtumishi wako . . . Governor wetu, na wote walio pamoja naye katika Serkali ya nchi hii ; ili wayatengeneze mambo yote kwa hekima na haki na amani, kwa kuliletea jina lako takatifu heshima, na kwa kufaa kanisa lako na watu wako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KUOMBEA UFALME WETU

Na tuuombee Ufalme wetu

Padre. Mungu huyu ni Mungu wetu milele na milele :

Huitika. Yeye ndiye atakayetuongoza hata mauti.

EWE Mwenyezi Mungu, ndiwe utawalaye katika Ufalme wa wanadamu, umemweka Bwana wetu Mfalme *GEORGE* juu ya ufalme mkubwa katika pande zote za ulimwengu : twakuomba uwavute watu wakao mumo, ambao kwa taifa na lugha na desturi zao wa mbali-mbali, wawe na ushirika wa kweli, ili kwa kuchukuliana mizigo yao, na kufanya kazi pamoja katika mapatano ya ndugu, wapate kutimiza uytakayo wewe kwa uangalizi wako, na kusongeza mbele ufalme wako wa milele. Twakuomba utusamehe dhambi zetu na upungufu wetu ; ututenge mbali na kujipenda wenye, na kiburi, kisha utupe neema kuvitumia vipawa vyako vyema nya utaratibu na ungwana, kwa kukuletea utukufu, na kwa kuwafaa wanadamu, kwa Yesu Kristo Mwanayo, Bwana wetu, naye apewe utukufu na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, milele na milele. *Amina..*

KUONGEZEKA UTUMISHI MTAKATIFU

Na tuombe Utumishi Mtakatifu uongezeke

Padre. Mwombeni Bwana wa mavuno : Huitika. Awapeleke watenda-kazi katika mavuno yake.

EWE Mwenyezi Mungu, uuangalie kwa rehema Ulimwengu huu ulioukomboa kwa damu ya Mwanayo mpenzi wako, uilekeze mioyo ya watu wengi wajitoe kwa ajili ya utumishi mtakatifu wa kanisa lako ; ili kwa kazi zao mwanga wako ung'ae gizani, na kwa wateule wako kukamilishwa, kuja kwake ufalme wako kuhimizwe ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA KAZI YA KUENEZA INJILI

(Yafaa sana kwamba kila fumapili Sala moja katika hizi tatu isomive.)

Na tuombe kwamba Ufalme wa Kristo uenee ulimwenguni.

Padre. Wahubirini mataifa habari za utukufu wake :

Huitika. Na watu wote habari za maajabu yake.

EWE Mungu wa mataifa yote ya dunia, ukumbuke jamii ya watu wa mataifa, ambao, wajapoumbwa katika sura zako, hawajui mapenzi yako ; kisha kwa ajili ya upatanisho wa Mwanayo Yesu Kristo, ujalie kwamba kwa maombi ya kanisa lako takatifu na kazi zake, waokolewe katika dini za uwongo na kutoamini, wavutwe kukuabudu wewe : kwa ye ye uliyemleta awe wokofu wetu, na ufufuo na uzima wa wote waaminio, Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

Padre. Jinsi ilivyo mizuri miguu ya wale wahubirio habari njema ya amani :

Huitika. Watangazao habari za wokofu.

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, Uliyeonesha mapenzi yako kwa kuntuma Mwanayo mzalihi pekee aje ulimwenguni, ili wote wapate uzima kwa ye ye : ulimiminie kanisa lako Roho wako, ili litimize amri zake kuhubiri Injili kwa kila kiumbe ; twakuomba uwapeleke watenda-kazi katika mavuno yako ; uwakinge katika hatari zote na majoribu yote ; utele upesi wakati ambao kujaa kwao mataifa kutatimia, na Isiraeli wote wataokoka ; kwa Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

Padre. Uniombe nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako :

Huitika. Na miisho ya dunia kuwa milki yako.

EWE Mwenyezi Mungu, uliyefanya mataifa yote ya wanadamu kuwa wa damu moja wakae juu ya nchi, ukamtuma Mwanayo, Mwenye-baraka Yesu

Kristo, ahubiri amani kwao walio mbali, na walio karibu : uwajalie watu wote wa ulimwengu wakutafute na kukuona, ukatimize haraka ahadi yako, ewe Bwana, ya kwamba utawamiminia watu wote Roho wako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KUOMBEEA UMOJA

Na tuombe Wakristo wote wakae na umoja wa moyo.

Padre. Jinsi lilivyo jambo jema, tena la kupeendeza.

Huitika. Ndugu wakikaa pamoja, kwa umoja halisi.

EWE Bwana Yesu Kristo, uliwaambia mitume wako, Nawaachia amani ; amani yangu nawapa ; usiziangalie dhambi zetu, uiangalie imani ya kanisa lako, na kulijalia amani na umoja kama vile utakavyo wewe : uishiye na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele na milele. *Amina.*

Au hii,

EWE Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Mwokozi wetu wa pekee, Mkuu wa amani ; utujalie kufikiri sana miyoni mwetu jinsi ziliyyo kuu hatari tulizo nazo' kwa mashaka ya kutengana wenywewe kwa wenywewe. Utuondolee machukio yote na kuhukumiana, na kila neno lituzuialo tusiwe na umoja na mapatano katika kukucha wewe : na kwa kuwa Mwili ni mmoja tu, Roho ni mmoja, Tumaini la mwito wetu ni moja, Bwana ni mmoja, Imani ni moja, Ubatizo ni mmoja, Mungu ni mmoja, naye ni Babaetu sisi sote, tangu sasa tuwe vivyo na moyo mmoja, roho moja, tuungamanishwe katika kifungo kimoja kitakatifu cha kweli na amani, cha imani na mapenzi, nasi kwa nia moja na kwa kinywa kimoja tukutukuze wewe ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA

**WAKATI WA UBISHOPU AU UCHUNGA
KUTOKUWA NA MWENYEWE.**

Na tuombe kwamba Padre mwaminifu aletwe katika Ubishopu huu
(au, Uchunga huu)

Padre. Uwavike haki watumishi wako :
Huitika. Uwaweke na furaha wateule wako.

E WE Mwenyezi Mungu, Mpaji wa kila kipawa
chemba, twakuomba kwa neema yako uliangalie kanisa lako, ukaziongoze kwa hekima yako ya mbinguni nia za wale amba ni juu yao kumchagua Bishopu wa Ubishopu huu, (au, Padre wa Uchunga huu), ili tupewe mchunga mwaminifu, atakayelisha kundi lako sawasawa na mapenzi yako, na kukufanyia tayari watu wa kukupendeza ; kwa Yesu Kristo, Mwanayo wa pekee, Bwana wetu. *Amina.*

KWA KUITUNZA SABATO

Na tuombe kwamba Siku ya Bwana itakaswe.

Padre. Siku hii ndiyo aliyoifanya Yehova :
Huitika. Tutashangilia na kuifurahia.

E WE Mwenyezi Mungu, umewapa watu siku ya
kupumzika, nawe kwa Roho wako aliye kanisani umetakasa siku ya kwanza ya juma, iwe ukumbusho hata milele wa kufufuka kwa Mwanayo : utujalie kwamba kwa jinsi tutakavyotumia kipawa chako hiki tupate raha na nguvu rohoni hata mwilini, ili tukutumikie kwa uaminifu siku zote za maisha yetu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA WALE WATAKAOTHUBUTISHWA

Na tuwaombee wale wanaowekwa tayari
kuthubutishwa

Padre. Roho wako ni mwema :
Huitika. Uwaongoze katika nchi ya haki.

SALA

E WE Mungu, wewe kwa mafundisho ya Mwanayo
Yesu Kristo uliwaweka wanafunzi tayari kuijina na Msaada : twakuomba uwaweke tayari katika mioyo na akili watumishi wako watakao wakati huu kupewa zaidi Roho Mtakatifu kwa kutiwa mikono, ili wakiya na mioyo iliyotubu na kuamini, wajazwe nguvu kwa jinsi yeye atakavyokaa ndani yao ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA MKUTANO MKUU WA UBISHOPU, ISOMWE
KATIKA JUMAPILI KABLA YA MKUTANO MKUU
WA UBISHOPU, AU MKUTANO WA KANISA

Na tuombe baraka ya Mungu iwe juu ya Mkutano Mkuu wa Ubishopu huu (au Mkutano huu wa Kanisa).

Padre. Akili na uwezo viko pamoja na Mungu :
Huitika. Yeye ana mashauri na fahamu.

T WAKUOMBA, ewe Mwenyezi Mungu, uwangoze
kwa mwanga wa Roho wako Mtakatifu, mabishopu na mapadre na watu wengine katika Mkutano Mkuu wa Ubishopu, (au Mkutano wa Kanisa), ili washauriane kwa hekima kwa ajili ya kulifaa kanisa lako na kulitokuza jina lako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA SKULI

Na tuziombee skuli zetu

Padre. Kumcha Yehova ndio mwanzo wa hekima :
Huitika. Wote wafanyaaya haya wana akili njema.

E WE Babaetu wa mbinguni, Mwanayo Mwenye-
baraka alisema, Waacheni watoto wanijilie : twakuomba uwafanikishe waalimu wote na wanafunzi wao kwa baraka yako ; kisha kama akili za watoto wako zitiwavyo mwanga kwa kupewa elimu, na mioyo yao nayo ivutwe daima na Roho wako Mtakatifu,

hata wakupende wewe na Mwanayo, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

KWA SKULI ZA JUMAPILI

Na tuziombee Skuli za Jumapili

Padre. Maneno haya nikuagizayo leo yatakuwa katika moyo wako :

Huitika. Nayo wafunze watoto wako kwa bidii.

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, Euliyawatia watoto wako katika ulinzi wa kanisa lako takatifu, walindwe na kulewa : uwatие nuru ya hekima yako waalimu na wanafunzi ; ili wakifurahi katika kujua kweli yako, wakuabudu na kukutumikia siku zote za maisha yao ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA MAKOLEJI NA MADARASA MENGINE YA ELIMU

Na tuombee makoleji na madarasa mengine ya elimu

Padre. Kumcha Yehova ndio akili :

Huitika. Na kuepkana na uovu ndio fahamu.

UWE radhi, ewe Bwana, kuzifanikisha kwa baraka yako kazi za makoleji yote, na skuli, ili wao wakutumikiao mumo, waalimu na wanafunzi pia, wandalame siku zote mapenzi yako matakatifu, na kuongozwa wajue kweli yako : hata baraka ije juu ya kanisa na nchi kwa sababu ya kusoma kwao, na wao wenyewe wafanyewe kustahili kuwa washiriki wa uzima wa milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AMANI ULIMWENGUNI

Na tuwaombee ulimwengu uwe na amani

Padre. Yehova ameketi ali Mfalme milele :

Huitika. Yehova atawabariki watu wake kwa amani.

EWE Mwenyezi Mungu, kwako wewe hutoka emawazo yote ya kweli na ya amani : twakuomba, uwajalie watu wote kupenda amani kwa kweli ; ukawaongoze wao wafanyao mashauri ya mataifa ya ulimwengu, kwa kuwapa hekima yako takatifu iletayo amani, ili usalme wako uendelee mbele katika utulivu wote, hata dunia iayajue kabisa mapenzi yako, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA USHIRIKA-WA-MASHAURI WA MATAIFA (LEAGUE OF NATIONS)

Na tuuombee Ushirika-wa-Mashauri wa Mataifa

Padre. Akomesha vita hata mwisho wa dunia :

Huitika. Auvunja uta, aukata mkuki, ayateketeza magari motoni.

T'WAKUOMBA, ewe Bwana, uwajalie watu wa Ushirika-wa-Mashauri wa Mataifa maongozi yako yaliyo na nguvu zote za kuamrisha. Uwape wote walio mumo mwanga na fahamu ili wayajue mapenzi yako, na uthabiti na nguvu kuyatimiza. Na viwe mashauri yao na hukumu zao kutiwa miyoni mwao na kutengenezwa na wewe, ili adili na amani vithubutishwe katika mataifa ya ulimwengu, na usalme wako uendelee katika haki na mapendano ya ndugu, kwa utukufu wako na kwa hali njema ya wanadamu, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA WASAFIRI WA BAHARI

Na tuwaombee wote wasafirio baharini

Padre. Hao wameziona kazi za Yehova :

Huitika. Na maajabu yake vilindini.

EWE Bwanga Mungu wa milele, ni wewe pekeo Utandazaye mbingu, na kutawala kiburi cha bahari : uwe radhi kuwalinda wote washukao baharini katika merikebu, wafanyao kazi katika maji mengi.

SALA

Uwahifadhi mwilini na rohoni : uzifanikishe kazi zao ; wakati wa hatari uwe mlinzi wao, ukawalete hata bandari wanayoitamani ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA AMANI KWA WATENDAO KAZI KATIKA
NCHI YETU

Na tuombe kwamba watenda-kazi wawe na
amani wao kwa wao

Padre. Msiwiwe na mtu kitu kiwacho chote, ila
nenó hili kupendana ninyi kwa ninyi :

Huitika. Kwani huyo ampendaye mwenziwe
amekwisha kuitimiza sheria.

EWE Mungu, Baba wa wanadamu wote, twakuuo-
mba utuvuvie mapenzi, na kweli, na haki, hata
katika shughuli zetu zote tulizo nazo wenyewe kwa
wenyewe, utuonyeshe tulivyo ndugu ndani yako wewe,
kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

Na tuombe kwamba Mungu alete hekima na haki,
ili mashaka yaliyoko sasa kwa watendao kazi
yaishe

Padre. Pisheni hukumu mkatende ya haki :

Huitika. Kwani wokofu wangu kuja kwake ni
karibu, na haki yangu kufunuliwa.

EWE Mwenyezi Mungu, Baba wa wanadamu wote,
ewewe umeamuru kwamba watu wote waishi na
kutenda kazi zao pamoja kama ndugu ; sisi tu miguuni
pako, twakuomba kwamba wao wasiosikizana sasa
uwaondolee mashindano yote na ugomi, ili watafute
yaliyo ya haki na sawasawa tu, waendelee siku zote
katika mapatano na masikizano ya ndugu, ili wajipatie
wema wenyewe na kufanikisha ufalme wetu ; kwa
Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA

SIKU ZA KUOMBEA MAVUNO

Na tuombe Mungu ayabariki mazao ya nchi na
kazi za wanadamu

Padre. Macho ya wote yakulekea wewe, ewe
Yehova :

Huitika. Nawe huwapa chakula chao kwa wakati
wake.

EWE Mwenyezi Mungu, uliyebariki nchi iwe na
ematunda mengi, na kuzaa kila kitu cha kuhitajiwa
na wanadamu kwa maisha yao : twakuomba uzifa-
nikishe kazi za wakulima, ukatujalie mvua ya kutosha
ili tuvune mazao ya nchi, na kufurahiwa siku zote
katika wema wako, kwa utukufu wa jina lako takatifu ;
kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

EWE Mwenyezi Mungu, uliyefanya bahari na
vyote vипитаво mumо, uyabariki mavuno ya
bahari, yawe mengi kwa wakati wake, uwabariki
wavuvi wetu nao, na mabaharia, wawe salama katika
hatari zote za majini ; hata sisi sote kwa mioyo ya
shukrani tukukiri wewe uliyе Bwana wa bahari na wa
nchi kavu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Au hii,

EWE Baba Mwenyezi, kwa Mwanayo Yesu Kristo
umetakasa kazi iwe kwa hali njema ya wanadamu ;
twakuomba uwafanikishe wote walio na amali katika
nchi hii, na kazi zao ; walindwe katika majoribu yao
yote na hatari zote ziwapatazo, nao huku wakipata
ijara ipasayo kazi zao, wakusifu kwa kuwa na mwendo
ulio sawasawa na mapenzi yako ; kwa Yesu Kristo,
Bwana wetu. *Amina.*

KWA KILIMO KIZURI

Na tuombe tuletewe kilimo kizuri

Padre. Atawafanyia wamchao yale watakayo :
Huitika. Naye atasikia kilio chao na kuwaokoa.

SALA

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu, kwa maneno ya Mwanayo, Yesu Kristo, uliahidi kwamba wao watafutao kwanza ufalme wako na haki yako watapewa vyote vipasavyo kuiokoa miili yao : twakuomba utuletee kilimo kizuri, ili tupate mavuno ya nchi kwa kutufaa sisi, na kwa heshima ya jina lako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

WAKATI WA NJAA

Na tuombe tuletewe msaada wakati huu wa njaa

Padre. Umtweke Yehova mzigo wako :
Huitika. Naye atakutegemeza.

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, Euliyetufundisha kwa maneno ya Mwanayo Mwenye-baraka kukuomba wewe riziki zetu : twakuomba uyaangalie mashaka ya watu wako, utuletee msaada wa kututosha katika uhitaji wetu huu tulio nao. Uongeze mavuno ya nchi kwa baraka yako ya mbinguni, ukatujalie sisi tuvipokee kwa shukrani vipawa yya neema yako, tukavitunie kwa utukufu wako, na kwa kuwasaidia wao walio na uhitaji, na kwa kutufaa sisi wenyeewe : kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

WAKATI WA TAUNI AU UGONJWA

Na tuombe tuletewe msaada wakati huu wa ugonjwa

Padre. Anayekusamehe maovu yako yote :
Huitika. Anayekuponya magonjwa yako yote.

TWAKUOMBA, ewe Bwana wa rehema, utusaidie na kutuochoa sisi tunaopatikana na ugonjwa mwingi na kufa. Utugeuzie mashaka haya yetu makuu, yatuletee baraka, ukawabarikie siku zote wale wafanyao kazi ya kujaribu kukinga wanadamu katika magonjwa na maumivu ; kwa yeye aliyeponza na kutakasa maumivu, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

SALA

WAKATI WA VITA

Na tumwombe Mungu atusaidie na kuntuongoza wakati huu wa vita

Padre. Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu :
Huitika. Msaada uonekanao wakati wa mateso.

EWE Bwana Mwenyezi, ndiwe ngome ya imara kwa wote wakuaminio ; utulinde sasa na siku zote ; ikiwa mapenzi yako utupe kushinda ; uwaa-ngalie kwa rehema waliojeruhiwa na wafungwa, uwatieve moyo wanaofadhaika ; uwafariji waliofiwa ; uwasaidie walio katika kufariki ; uwarehemu wote ; uhimize wakati wa vita kukoma katika ulimwengu wote ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA WAGONJWA

Na tuwaombee wagonjwa

Padre. Huwaponya waliopondeka moyo :
Huitika. Na kuyafunga majeraha yao.

EWE Baba Mwenyezi, Mpaji wa maisha na afya, Twakuomba uwaangalie kwa rehema wagonjwa wote, hasa wao wanaotakiwa maombi yetu, ili kwa baraka yako juu yao, na juu ya wao wawatumikiao, ikiwa mapenzi yako warudishiwe afya yao ya mwili na ya roho, nao wakutolee shukrani katika kanisa lako takatifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA HOSPITALI

Na tuombe baraka ya Mungu iwe juu ya Hospitali zote

Padre. Mwenyeewe aliupokea udhaifu wetu :
Huitika. Akayachukua na magonjwa yetu.

EWE Mwenyezi Mungu, Mwanayo Mwenye-baraka alikuwa akizunguka akitenda kazi njema, akapoza kila namna ya ugonjwa na udhaifu katika

SALA

watu ; twakuomba kwamba kazi yake hii ya neema iendelee kwetu, zaidi katika hospitali za nchi yetu ; uwatue moyo wagonjwa, uwapoze na kuwatakasa ; uwape madaktari na hao wawasaidiao na wauguzi wote akili na ustadi, na huruma na uvumilivu ; uwabarikie wote wanaojitahidi kuzuia maumivu na kuhimiza mashauri yako ya mapenzi ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KUWAKUMBUKA WAAMINIFU MAREHEMU
Na tukumbuke mbele za Mungu waaminifu
marehemu

*Padre. Wenyehaki huishi milele :
Huitika. Na thawabu yao iko kwa Yehova.*

EWE Mungu wa roho za wote wenyehaki mwili, twalisifu na kulitkuza jina lako takatifu kwa ajili ya watumishi wako wote walioitimiza mwendo wao katika imani yako na kicho chako. Twakuomba kwamba tulivyotiwa moyo kwa vielelezo vyao vizuri, na kupewa nguvu kwa kuwa na ushirika nao, tuone-kane nasi pamoja nao kuwa tunastahili kupokea schemeu ya urithi wa watakatifu walio katika nuru ; kwa kustahili kwake Mwanayo, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Watukutaka kuomba kwa ajili ya haja nyngine, itatosha kusema, Na tuombee (jinsi kadhwakachha), kisha watu wawe kinyanya kitambo kidogo. Ndipo husema,*

*Padre. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu :
Huitika. Kilio chetu kikufikilie.*

**SALA ZIWEZAZO KUTUMIWA BAADA YA HIZO
ZA MBELE**

EWE Mwenyezi Mungu, ni hali yako wewe siku zote kuwa mwenye rehema na msamaha, utusikize sili tulio miguuni pako tukuombayyo ; nasi tujapo-

SALA

fungwa na kuzuiwa kwa minyororo ya dhambi zetu, huruma zako nyangi na zitufungue ; kwa heshima ya Yesu Kristo, Mwombezi wetu, Msaada wetu. *Amina.*

UI KUMBUKE, ewe Bwana, kazi uliyotenda ndani yetu, usikumbuke tunavyostahili kupewa ; kisha uliyotuita kukutumikia, utujalie tuwe wa kustahili mwito wetu, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Bwana, utuchukuze mchana wote wa maisha haya ya taabu, hata kutwa, zitakapotulia kelele za ulimwengu huu, ra fadhaa ya maisha itakoma, na kazi yetu itakwisha. Ndipo, ewe Bwana, kwa rehema zako, utupe makao ya salama, na raha takatifu, na amani mwisho wake. *Amina.*

SHUKRANI

KWA KILIMO KIZURI

EWE Bwana Mwenyezi Mungu, uliyetusaidia na kututuliza sisi watumishi wako, kwa kutupa kilimo kizuri ; twakushukuru sana kwa mioyo yetu kwa wema wako huu kwetu ; twakuomba utupe neema tuvitumie vipawa vyako vyote kwa heshima na utukufu wa jina lako takatifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

KWA BARAKA ZA MAVUNO

EWE Bwana Mwenyezi Mungu, Muumba, Baba wa wote, twakushukuru sana kwa mioyo yetu, kwa vile uliyowaagizia wanadamu nyakati za kupanda na kuvuna, na kwa kutupa sasa mazao ya nchi kwa wakati wake. Jina lako tukufu twalisifu na kulitkuza kwa rehema zako hizi na nyngine zote nazo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

**KWA KUOKOKA WAKATI WA TAUNI AU WA
UGONJWA**

EWE Bwana Mungu, moyo wako haupendi kuwatesa wanadamu : twakushukuru sana kwa vile uliviyotuokoa kwa rehema zako katika ugonjwa na mashaka, nasi kwa miyo ya shukrani twataka kuktotea, ewe Baba mwema, nafsi zetu, roho na miili, tuwe kwako sadaka iliyo hai, siku zote tukusifu na kutukuza huruma zako katika Kanisa lako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Watu wakinata kutoa shukrani kwa rehema nyingine, itatosha kusema, Na turnshukuru Mwenyezi Mungu (kwa jinsi kadhwakadha), kisha watu wawe kimya kitambo kidogo. Ndipo husema,*

Padre. Mshukuruni Yehova kwa kuwa yu mwema :

Huitika. Kwa maana fadhili zake ni za milele.

¶ *Zikiisha Sala na Shukrani kisomwe kimoja katika vikomo hivi, naayo vyawezza kutumiwa baada ya Sala ya Tatu katika Sala ya Jioni.*

KWA Mungu Baba aliyetupenda na kutukirimu katika huyo Mpenzi :

Kwa Mungu Mwana, aliyetupenda na kutufungua katika dhambi zetu kwa damu yake :

Kwa Mungu Roho Mtakatifu, amiminaye mapenzi ya Mungu katika miyo yetu :

Mungu wa pekee wa kweli na apewe mapenzi yote na utukufu wote sasa na hata milele. *Amina.*

Au hiki,

MUNGU aliye Mwenyezi, Mwenye rehema, Matubarikie na kutulinda usiku huu na hata milele. *Amina.*

¶ *Tunza kwamba isipokuwa Bishopu kuagiza vingine, baada ya mwisho wa Sala ya Asubuti, au Sala ya Jioni, au ya Taratibu nyininge ya Ibada, Padre awenza, akiona mvizuri, kusali kwa maneno yake mwenyewe.*

**SALA NA NYARAKA NA INJILI VYA
MWAKA MZIMA**

¶ *Tunza. Sala iliyoagizwa kutumiwa kila Jumapili au kila Idi iliyo na Kesha yake au Matengezo yake, husomwa katika Sala ya Jioni ya siku ya kuamka siku hiyo.*

JUMAPILI YA KWANZA KATIKA WAKATI WA KUJA

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, utupe neema tuzitupe kazi za Egiza, tuvikwe silaha za nuru, hivi tuliyio katika zamani za maisha haya yapatikanayo na mauti, nayo ndiyo aliyoayaingia Mwanayo Yesu Kristo, wakati alipokuja kutuangalia, hali amejifanya mnyenyekuvu sana ; ili kwamba, katika siku ya mwisho, wakati wa kuja kwake tena kwa enzi yake kubwa, kuwahukumu walio hai na waliokufa pia, tuwe sisi ni watu wa kufufuka kwa maisha yasiyopatikana na mauti, kwa ajili yake yeye, anayeishi pamoa na wewe na Roho Mtakatifu, sasa na milele. *Amina.*

¶ *Sala hii husomwa kila siku pamoja na sala nyingine za Kiwa, hata yatakapokuja Matengezo ya Uzazi wa Kristo.*

Waraka. Warumi 13. 8-14

MSIWIWE na mtu kitu kiwacho chote, ila *neno hili* kupendana ninyi kwa ninyi : kwani huyo ampendaye mwensiwe amekwisha kuitimiza sheria. Kwani *neno hili*, Usizini, Usiue, Usiibe, Usimshuhudie mwenzio kwa uwongo, Usikitamani *kitu cha mwenzio*, tena likiwako agizo jingine, limejumlishwa katika *neno hili*, nalo ni hili, Utampenda mwenzio kama upendavyo nafsi yako. Yale mapenzi hayatendi kilicho kibaya kwa mwensiwe : basi utimilifu wa ile sheria ni yale mapenzi. Tena *neno hili*, tu hali ya kuujua ule wakati, ya kwamba sasa ni saa yenu ya kuamka katika usingizi : kwani sasa wokofu wetu u

karibu nasi kuliko tulipoamini *kwanza*. Usiku umekwendelea sana, mchana umekaribia : basi na *tazivulie* mbali zile kazi za giza, na kujivisha silaha za mwanga. Twe-nende kwa makini kama mchana : si katika kucheza ngoma na kulewa, si katika uzinzu na ulanifu, si katika mashindano na wivu. Lakini kajivisheni Bwana Yesu Kristo, tena msifanye kujitengeza kwa mwili, mpate *kuzitimiza* shauku *zake*.

Injili. Mathayo 21. 1-13

HATA walipouputa karibu mji wa Yerusalemu, wakifika hata Bethifage, katika kilima cha Mizeituni, hapo ndipo Yesu alipotuma wawili katika wanafunzi wake, aka-waambia, Ingieni kijiji kilicholekea imbele yenu, mara mtamwona punda amefungwa, na mwana wa punda pamoja naye : wafungueni mnilettee. Na mtu akiwaambia neno, mwambieni, Bwana ana haja nao : mara ile atawaleta. Hayo yalitendeka ili yatimie yaliyonenwa na nabii, hapo anaposema, Mwambieni binti Zayuni, Huyu ndiye, Mfalme wako akujia ; ni mnyenyeketu hali yake, amepanda juu ya punda, na punda mtoto, mwana wa punda. Wakaenda wale wanafunzi wakafanya kama walivoagizwa na Yesu, wakamleta punda na mwanawewe, wakawatandika nguo zao, naye akapanda. Na ule nkutano wingi wao walitandika nguo zao katika njia : wengine wakikata matawi ya miti, wakitandika njiani. Makutano waliomtangulia na waliomfuata wakapiga ukelele, wakisema, Hosana ni ya Mwana wa Daudi : amebarikiwa anayekuja kwa Jina la Bwana ; Hosana kwa juu sana. Hata alipoingia Yerusalemu, ukatibuka mji mzima, watu wakinena, Ni nani huyo ? Wale makutano wakinena, Huyu ndiye nabii, *jina lake aitwa* Yesu, *ni mtu* wa Nazarethi iliyo Galilaya. Kisha akaingia Yesu katika hekalu la Mwenyezi Mungu, akawatoa nje wote waliokuwa wakiua na kununua mle hekaluni, akazipindua na meza za wenye kubadili pesa, na viti vyaa wenye kuuza njiwa : naye akiwaambia, Imeandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala, nanyi mwaifanya ni pango ya wevi.

JUMAPILI YA PILI KATIKA WAKATI WA KUJA
Sala

EWE Bwana Mwenye-baraka, uliyeamuru yaandikwe Maandiko Matakatifu yote kuwa mafunzo yetu ; utupe ya kwamba tuyasikie, na kuyasoma, na kuyashika, na kujifunza hayo, na kuyafikiri miyoni mwetutu kwa jinsi hiyo ya kwamba tupate, kwa uvumilivu na imara ya Neno lako takatifu, kulishika na kulitunza milele tumaini hilo lenye baraka ya maisha yasiyokoma, tuliyopewa na wewe katika Mwokozi wetu Yesu Kristo. *Amina.*

Waraka. Warumi 15. 4-13

KWANI mambo yaliyo yoyote yaliyotangulia kuanidikwa, yaliandikwa kwa mafunzo yetu, ili kwamba kwa uvumilivu na kwa msaada wa hayo maandiko tuwe na matumaini. Basi Mwenyezi Mungu mwenye uvumilivu na msaada na awape ninyi muwe na nia moja ninyi kwa mmoja na kinywa kimoja kumtukuza Mwenyezi Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Kwa sababu hii kubalianeni ninyi kwa ninyi, vivile kama Kristo naye ali-yowakubali ninyi, kwa utukufu wa Mungu. Kwani nanena ya kwamba Kristo alifanywa mtumishi wa tohara kwa ajili ya kweli ya Mungu, apate kuzitia nguvu zile aladi *walizopewa* wale mababa, tena watu wa hao mataifa wapate kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa ajili ya rehema yake ; kama ilivyoandikwa, Kwa ajili ya neno hili nitakusifu wewe mbele ya hao mataifa, tena nitaliimbia jina lako. Yuanena tena, Kafurahini, enyi watu wa hao mataifa, pamoja na watu wake. Tena, Msifuni Bwana, mataifa, mlioko nyote ; mpazieni sauti, mbegu zote za watu. Tena, Isaya anena, Litakuwako shina la Yesii, naye yeze anayeinuka kutawala juu ya hao mataifa : watu wa hao mataifa watatumaini kwake yeze. Basi Mungu wa matumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate ninyi kujawa tele na matumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Injili. Luka 21. 25-33

TENA kutakuwa na ishara katika jua na mwezi na nyota ; na juu ya nchi dhiki ya mataifa yanayoshangaa kwa kivumi cha bahari na msuko-suko wake ; watu waki-vunjiaka mioyo kwa kicho na kungojea mambo utakayoingia ulimwengu : kwa kuwa nguvu za mbinguni zitacheza-cheza. Na zamani zile ndipo watakapomwona Mwana wa binadamu yuaja ndani ya wingu pamoja na uwezo na enzi kuu. Nayo yanapoanza kutokea mambo hayo, tangamkeni ninyi, mwinue na vichwa vyenu, kwa kuwa huo ukombozi wenu wakaribia. Aliwaambia mithali : Utazameni mtini na miti wenziwe yote : wakati iishapo kuchepuza mwaona na kutambua nafsini mwenu kuwa majira ya matunda yako karibu. Nanyi ni vivyo, mna-poona mambo haya yaanza kutokea, jueni kwamba umekuwa karibu ufalme wa Mungu. Ni kweli nawaambia kwamba, hakitapita kamwe kizazi hiki hata yaishe kutimia yote. Mbingu na nchi zitaondoka, lakini maneno yangu hayaondoki kamwe.

JUMAPILI YA TATU KATIKA WAKATI WA KUJA

Sala

WE Bwana Yesu Kristo, ambaye ulipokuja pale kwanza ulimtoa njumbe wako, ukamtanguliza mbele zako apate kukutengezea njia ; utupe ya kwamba hao walio watumishi wako na mawakili wa siri zako, watengeze na kuiandaa njia yako kama vile yeye, kwa kuigeuza mioyo ya maasi kuilekeza katika hekima ya wenye haki, ili kwamba utakapokuja mara ya pili kwa kuuhukumu ulimwengu, tuonekane kuwa ni watu wa kukubaliwa machoni pako, uishiye na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu siku zote, Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Waraka. 1 Wakorintho 4. 1-5

BINADAMU na atuhesabu sisi kuwa tu watumishi wa Kristo na mawakili wa siri za Mungu. Hapo napo, hutakwa kwa mawakili kwamba mtu aonekane kuwa mwa-

minifu. Ila kwangu mimi ni neno lililo dogo sana, kwamba nihukumiwe na ninyi, au na siku ya binadamu ; naam, wala siihukumu nafsi yangu. Kwani sijui neno juu ya nafsi yangu : lakini kwa sababu hiyo sikuhesabiwa kuwa na haki : ila anitafitiye mimi ni Bwana. Kwa ajili ya hayo msihukumu neno mbele ya wakati wake, hata Bwana aje, naye ndiye atakayeyaweka wazi mambo yaliyofichwa ya gizani, tena atayafanya wazi mashauri ya mioyo, ndipo na kila mtu atakuwa na sifa yake itokanayo na Mwenyezi Mungu.

Injili. Mathayo 11. 2-10

NAYE Yohana aliposikia mle kifungoni vitendo vyake Kristo, akaruma wawili katika wanafunzi wake kumuuliza, Wewe ndiwe ajaye au tumngojee mwingine ? Yesu akawajibu akaawaambia, Endeni mkamrudishie habari Yohana ya mnayoyasikia na mnayoyaona : watovu wa macho waona, na viwete waenenda, wenye ukoma wasafiwa, na viziwi wasikia, na maiti wafufuliwa, na maskini wahubiriwa habari njema. Na heri ni ya asiye-kunguwaa kwangu mimi. Na hao walipoondoka akaanza Yesu kuwaliza wale makutano katika Yohana : Ni lipi millokwenda nje huko barani kulitazama ? je, ni mwanzini unaosukwa-sukwa na upepo ? Walakin ni lipi millokwenda nje kuliona ? ni mwenye kuvaav mavaao maororo ? Angalia, wavaao maororo wamo katika nyumba za wafalme. Lakini milikwendea nini huko nje ? Ni kutaka kuona nabii ? Naam, nawaambia ninyi, ni lililo kuu kuliko nabii. Kwani huyu ndiye aliyeandikiwa maneno haya : Angalia, mimi nimemtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakayetengeza njia yako mbele zako.

JUMAPILI YA NNE KATIKA WAKATI WA KUJA

Sala

ZITANGAMSHE nguvu zako twakuomba, ewe Bwana, nawe uje kwetu sisi, utuletee msaada kwa uwezo mwingi li kwamba, tungawa twazuiwa mino na

madhambi yetu na uovu wetu, na kuvutiwa nyuma mno katika mashindano ya mbio tunayoagizwa, pamoja na hayo yote usikawie huo wema wa neema yako na rehema zako kutusaidia na kutuponya ; kwa alivyokuridhi Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu, naye ndiye wa kuheshimiwa na kutukuzwa pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, milele. *Amina.*

Waraka. Wafilipi 4. 4-7

FURAHINI katika Bwana siku zote : tena nitasema, Furahini. Na upole wenu ujulikane kwa watu wote. Bwana yu karibu. Msifadhaike kwa neno lolote ; lakini haja zenu katika kila neno zifulishwe kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya kusali na kuomba pamoja na shukrani. Na amani ya Mwenyezi Mungu, inayopita fahamu zilizo zote, itailinda mioyo yenu na fikira zenu pia, katika Kristo Yesu.

Injili. Yohana 1. 19-28

NA huu ndio ushuhuda wake Yohana, wakati Maya-hudi walipotuma kwake makuhani na Walawi kutoka Yerusalem, kwenda kumuuliza, Ndiwe nani ? Naye akakubali, wala hakukana ; akakubali, akasema, Mimi siye Kristo. Wakamuuliza, Ni nini basi ? Ndiwe Elija wewe ? Akasema, Siye mimi. Wewe ndiye nabii ? Akajibu, Si mimi. Basi wakamwambia, Ndiwe nani ? tupate kuwapa jawabu waliotuleta. Wasemaje kwa nafsi yako ? Akasema, Ndimi sauti ya anayepiga ukelele barani, Inyosheni njia ya Bwana, kama alivyosema nabii Isaya. Nao walitumwa kutoka kwa Mafarisayo. Wakamuuliza, wakamwambia, Kwani wewe kubatiza, kwamba wewe hu Kristo, wala hu Elija, wala hu yule nabii ? Yohana akawajibu, asema, Mimi nabatiza kwa maji ; kati yenu amesimama huyo msiyemjua ninyi, ndiye mwenye kuja nyuma yangu, ambaye si kiasi changu kumfungulia kigwe cha kiatu chake. Haya yalikuwa Bethania ng'ambu ya Yorodani, pahali alipokuwa Yohana akibatiza.

IDI YA UZAZI WA BWANA WETU, AU SIKU ALIYOZALIWA KRISTO, ITWAYO,

CHRISTMAS

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe umetupa sisi Mwanyayo mzaliwa pekee, apate kutwaa tabia yetu kuwa nayo yeye, na kuzaliwa na mwanamwali safi, kama wakati huu wa sasa ; utupe sisi ya kwamba, kwa hivyo tunavyozaliwa mara ya pili na kufanywa kuwa wanayo kwa kuchaguliwa na neema, turejezwe upya kila siku na Roho wako Mtakatifu ; kwa ajili ya yeye huyo Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye yuaishi na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja daima, hata milele. *Amina.*

Waraka. Wahibirania 1. 1-12

MWENYEZI Mungu akisha kunena na hao mababa kwa njia ya maneno ya manabii katika zamani za kale kwa mafungu aina nyininge-nyininge na kwa njia aina nyininge-nyininge, mwisho wa siku hizo amenena nasi katika Mwanawe, ambaye amemweka awe mrithi wa vitu vyote, tena alivumba viumbi vyote kwa *mkono wake* yeye ; ambaye kwa kuwa yeye ni umemetufu wa utukufu wake, na mfano hasa wa *sura za nafsi* yake, tena kwa kuwa aviweka vitu vyote kwa neno la uwezo wake, akisha kuleta uitakoso wa madhambi, akaketi upande wa *mkono* wa kuume wa Ukuu katika pahali palipo juu ; akisha kuwa kwa kadiri hiyo mtukufu kuliko hao malaika, kama vile alivyorithi jina lilitotengenka, kuwapita wao. Kwani alimwambia malaika yupi, majira yoyote, Mwanganu ni wewe, mimi leo nimekuzaa ; na tena, Mimi nitakuwa kwake Baba, naye atakuwa kwangu mwana ? Tena hapo anapomita mzaliwa-wa-kwanza katika ulimwengu asema, Malaika wote wa Mungu na wamsujudie yeye. Na katika habari za malaika asema, Anayewafanya malaika zake wawe upепо, na watumishi wake kuwa mwali

wa moto : ila habari za Mwana, *azinena hivi*, Ewe Mwenyezi Mungu, kiti chako cha enzi huwe tangu milele hata milele ; fimbo-ya-enzi iliyo ya ulekevu, ni fimbo-ya-enzi ya ufalme wako, wewe umependa haki ukiuchukira ule ubaya ; ndipo na Mwenyezi Mungu, naye ni Mwenyezi Mungu wako, alikupaka mafuta, mafuta ya furaha, kuwipita washirika wako. Na, *neno hili tena*, Wewe Bwana, hapo kale, hii nchi uliipiga msingi ; na kazi za mikono yako ni hizo mbingu : hizo zitaangamia ; ila wewe wadumu : nazozote zitachakaa kama vile nguo ; tena mfano wa nguo-ya-juu utazikunja, kama vile nguo, nazozitabadijika : lakini wewe ndiwe ye ye yule, na miaka yako haitakoma.

Injili. Yohana I. 1-14

HAPO kwanza liko lile Neno, nalo Neno lilikuwa kwa Mwenyezi Mungu, nalo Neno lilikuwa ni Mwenyezi Mungu. Hilo lilikuwako mwanzo kwa Mwenyezi Mungu. Vitu vyote vilifanywa kwake yeye, wala pasipokuwa na yeye hakifanaywa hata kitu kimoya ambacho kimefanywa. Ndani yake mlikuwa na uzima, nao uzima ulikuwa ni mwanga wao wanadamu. Nao mwanga hung'ara katika giza, wala giza haikuupata. Alitokea mitu mmoja ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana. Huyo alikuja kwa ushuhuda, apate kuushuhudia ule mwanga, watu wote wapate kuamini kwa ajili yake. Hakuwa mwanga yeye, alikuja apate kuushuhudia mwanga. Ulikuwako mwanga ulio kweli, unaomtia mwanga kila mtu, ukiingia katika ulimwengu. Alikuwamo ulimwenguni, nao ulimwengu ulifanywa kwake huyo, wala ulimwengu haukumjua. Alikujia vyake, wale wake wasimpokee yeye. Na kadiri ya waliomtwaa akawapa amri, kufanyika wao wana wa Mwenyezi Mungu, hao wanaoamini kwa jina lake : waliozaliwa, si kwa damu, wala kwa kupenda kwa mwili, wala kwa kupenda kwa mtumume, isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu. Nalo Neno likafanywa mwili, likatua kati yetu, nasi tukauona utukufu wake utukufu kama wa mzaliwa pekee, aliyetoka kwa Baba, limejawa na neema na kweli.

IDI YA MTAKATIFU STEFANO

Sala

UKUBALI, ewe Bwana, ya kwamba sisi kadiri ya tutakavyopatikana na mashaka hapa duniani, kwa ajili ya kule kuishuhudia kweli yako, tuzidi kuangaza macho mbinguni tu, ili tuuone kwa imani ule utukufu utakaofunuliwa baadaye ; kisha, kwa kule kujawa na Roho Mtakatifu, tujifunze kuwapenda na kuwaomeba baraka watesaji wetu wawao wote, kwa kukifuata kielelezoo chake yule shahidi wako wa kwanza, mtakatifu Stefano, aliyeomegaomeba wauaji wake kwako wewe, ewe Yesu Mwenye-baraka, unayesimama upande wa mkonon wa kuume wa Mwenyezi Mungu, kwa kuwalettea msaada watu wote wanaoudhiwa kwa ajili yako wewe, Mwombezi wetu pekee, Msaada wetu. *Amina.*

¶ *Hapo husuata Sala ya Uzazi wa Bwana, nayo isiachwe kusomwa kila siku hata yaje Matengezo ya Idi ya Tohara.*

Badala ya Waraka. Vitendo 7. 55-60

STEFANO, ali hali ya kujawa na Roho Mtakatifu, sakataliza macho yake akiangalia mbinguni, akauna utukufu wa Mwenyezi Mungu, *akanwona* na Yesu amesimama upande wa mkonon wa kuume wa Mungu, akasema, Angalieni ! naona mbingu zimefunuka wazi, na yule Mwana wa binadamu amesimama upande wa mkonon wa kuume wa Mungu. Wakapiga ukelele kwa sauti kubwa, wakaziba masikio yao, na kumrukia kwa nia moja juu yake ; wakamtupa nje ya mji, na kumuua kwa kumpiga kwa mawe : wale mashahidi wakayaweka mavao yao miguuni pa mtu mmoja hirimu, jina lake aliyeitwa Saulo. Basi wakampiga Stefano kwa mawe, naye ali hali ya kulingana *Bwana*, akisema, Ewe Bwana Yesu, pokea roho yangu. Akapiga magoti, akalia kwa sauti kubwa na *kunena*, Ewe Bwana, usiwaandikie dhambi hii. Ali-pokwisha kusema hayo, akalala.

Injili. Mathayo 23. 34-39

KWA ajili ya neno hilo, sasa mimi natuma kwenu manabii na watu wa hekima na wana-wa-vyuoni : katika wao hawa mtawaua, na hawa mtawasalibu, na

katika wao hawa mtawapiga mjeledi misikitini mwenu, na kuwafukuza mji na mji : ili ipate kuja juu yenu ninyi kila damu iliyotakata inayomwagika juu ya nchi, tangu damu ya Habilii yule mwenye haki, hata damu ya Zakaria mwana wa Barakia, mliyemuua katikati ya hekalu la ndani na madhabahu. Ni kweli nawaambia, kizazi hiki kitajiliwa juu yake na haya yote. Ewe Yerusalem, Yerusalem, *ewe mji* unaowaua manabii na kuwapiga kwa mawe waliotumwa kwako, ni mara nyungapi nilizokuwa mimi nikitaka kuwakusanya wanayo wewe hali kuku avikusanyavyo visfaranga vyake chini ya mbawaba yake, msikubali. Hiyo ndiyo, hiyo nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. Kwani nawaambia, hamnioni tena kamwe, hata mseme, Amebarikiwa anayekuja kwa Jina la Bwana.

IDI YA MTAKATIFU YOHANA MHUBIRI-WA-HABARI-NJEMA

Sala

TWAKUOMBA sana, ewe Bwana mwenye ihisani, uliletii hili kanisa lako nuru za mwanga wako, ili kwamba kwa kung'ariziwa na elimu ya mbarikiwa mtume wako, mhubiri wako, mtakatifu Yohana, kwa jinsi litakavyokwenda katika mwanga wa kweli yako, lifikilie mwisho katika mwanga wa maisha ya milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Johana 1. 1-10

HAYO yaliyokuwako tangu mwanzo, **hayo tuliyosikia**, hayo tuliyoyaona kwa macho yetu, hayo tuliyoyaangalia, na mikono yetu iliyapapasa-papasa, katika habari za Neno la uhai (na huo uhai ulifunuliwa, nasi tumeuona, kisha twashuhudia, na kuwahubiri ninyi ule uhai, *maana*, ule uhai wa milele, huo uliokuwa pamoja na Baba, na kufunuliwa kwetu) ; hayo tuliyoyaona na kuyasikia twawahubiri na ninyi nanyi, mpate kuwa na ushirika pamoja nasi : naam, na ushirika wetu ni pamoja na yeeye Baba, na pamoja na Mwanawe Yesu Kristo :

nasi twayaandika mambo haya ili kwamba furaha yetu itimie. Tena ujumbe tuliosikia kwake ni huu, nasi twawahubiri ninyi, ya kwamba, *Mwenyezi Mungu* ni nuru, na ndani yake hapana giza kabisa. Ikiwa twasema ya kwamba tuna ushirika pamoja naye, kisha twaenenda katika giza, twanena uwongo, wala hatufanyi lilio la kweli : ila ikiwa twaenenda katika hizo nuru kama yeeye alivyo katika nuru, tuna ushirika sisi kwa sisi, na damu ya Yesu Kristo Mwanawe hutusafi na dhambi yote. Ikiwa twanena ya kwamba hatuna dhambi, twapoteza nafsi zetu, na hiyo kweli haimo ndani yetu. Ila ikiwa twazitungama dhambi zetu, yeeye ni mwaminifu kisha yuna haki hata akatusamehe dhambi zetu na kurusafi na uovu wote. Ikiwa twasema ya kwamba hatukukosa, twamfanya yeeye kuwa mwongo, na neno lake halimo ndani yetu.

Injili. Yohana 21. 19-25

YESU akamwambia *Petero*, Nifuate. Petero akiisha kuzunguka, akamwona yule mwanafunzi Yesu aliyekuwa akimpenda awafuata : naye ndiye aliyebenukia kifuani mwake Yesu wakati wa karamu, huku amwambia, Bwana, ni nani huyo anayekusaliti ? Basi Petero ali-mwona huyo, akamwambia Yesu, Bwana, na huyu, je ? Yesu akamwambia, Nikipenda akae hata nije, kwako yadburuni ? Wewe nifuate. Basi neno hili likatangaa kwa wale ndugu, ya kwamba mwanafunzi yule hafi ; wala siyo aliyonenea Yesu kwamba hafi ; ila, Nikipenda akae hata nije, kwako yadburuni ? Huyu ndiye mwanafunzi anayeyashuhudia mambo haya, naye ndiye aliye-yaandika maneno haya, nasi ushuhuda wake tumeujua kuwa ni kweli. Yako na mengi tena aliyyoyatenda Yesu, ambayo kwamba, yatakapoandikwa moja moja, nadhani hata ulimwengu mzima hauvikunjukii vyuo vitakavyoadikwa.

IDI YA WASIO-MAKOSA

Sala

EWE *Mwenyezi Mungu*, ni wewe uliyetimiza uwezo kwa vinywa vya watoto wadogo, na wenye kuamwa ; ukawapa wana wadogo kukutukuza wewe kwa mauti yao ;

uvive na kuondoa viovu vyote ndani yetu sisi, huku ukutitia nguvu sana kwa neema yako, ili kwamba kwa maisha yetu kutokuwa na aibu na imani yetu kuwa imara hata mauti, iwe sisi kulitukuza daima jina lako takatifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Ufunuo 14. 1-5

KISHA niliona, na huyo ndiye, huyo Mwana-wa-kondoo amesimama juu ya mlima wa Zayuni, na *watu* laki moja na elfu arobaini na nne pamoja naye, wenyenye jina lake na jina la Babaye yameandikwa katika vipaji nya nyuso zao. Nami nilisikia sauti yatoka mbinguni kama vile sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi kuu : na hiyo sauti nilioisikia ilikuwa kama wenyenye kupiga vinanda-vya-kinubi wakivipiga vinanda vyao : nao waimba kama vile wimbo mpya mbele ya kile kitichenzi, na mbele ya hao nyama-wenyenye-uhai wanane, na hao wazee : na hapana mtu aliyeweza kujifunza wimbo huo isipokuwa ni hao *watu* laki moja na elfu arobaini na nne *ndio walioweza*, hao walionunuliwa katika nchi. Hawa ndio wasiotiwa najisi pamoja na wanawake ; kwani wa tohara. Hawa ndio wamwandamao huyo Mwana-wa-kondoo, kila aendapo. Hawa walinunuliwa katika wandalamu, wawe malimbuko kwa Mwenyezi Mungu na kwa huyo Mwana-wa-kondoo. Na katika kinywa chao haukuonekana uwongo : hawana aibu mbele ya kiti-cha-enzi cha Mwenyezi Mungu.

Injili. Mathayo 2. 13-18

HUYO ndiye, malaika wa Bwana akamtokea Yusufu katika ndoto, akamwambia, Ondoka hapo ulipo umtwa yule mtoto na mamaye, ukimbilie Misiri, ukae kuko hata nitakapokuambia : kwani Herode aja kumtafuta yule mtoto ili kumwangamiza. Naye akasimama aka-mtwaa yule mtoto na mamaye, akaondoka na usiku, akaenda zake Misiri ; akakaa kuko hata Herode alipokwisha *kufa*, lipate kutimia hilo lililonenwa na Bwana kwa kinywa cha nabii, Kumtoa Misiri nilimwita Mwanangu.

Ndipo hapo Herode akajiona amechekwa na wale mama-jusi, akakasirika mno, akatumwa watu akawaangamiza watoto wote waurne wanaokaa Bethilehemu na kando-kando yake kila pahali, waliopata miaka miwili na upungufu wa miaka miwili, kama majira aliyyoyahakikisha na wale mama-jusi. Wakati huo likatimia lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yeremia, aliponena, Rama kumeskilikana sauti, kulia na kupiga kite ; Raheli yuwalilia wanawe ; hakubali kunyamazishwa, maana hawako.

JUMAPILI IANDAMAYO BAADA YA UZAZI WA BWANA
Sala

EW WE Mwenyezi Mungu, wewe umetupa sisi Mwanayo Emzaliwa pekee, apate kutwaa tabia yetu kuwa nayo yeye, na kuzaliwa na mwanamwali safi, kama wakati huu wa sasa ; utupe sisi ya kwamba, kwa hiyyo tulivyozaaliwa mara ya pili na kufanywa kuwa wanayo kwa kuchaguliwa na neema, turejezwe upya kila siku na Roho wako Mtakatifu : kwa ajili ya yeye huyo Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye yuaishi na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja daima, hata milele. *Amina.*

Waraka. Wagalatia 4. 1-7

ILA nanena kwamba, muda wote mriithi awapo mtoto Thana tofauti yeye na mtumwa, ajapokuwa yu bwana wa wote : lakini yupo chini ya mawasii na mawakili hata wakati ulioamriwa na babaye. Na sisi tu vivyo hiyyo, hapo tulipokuwa watoto, tulitumikishwa chini ya mafunzo-ya-kwanza ya dunia : ila hapo utimilifu wa wakati ulipokuja, Mwenyezi Mungu akamtuma Mwanawe, alizaliwa na mwanamke, alizaliwa chini ya sheria, ili kwamba apate kuwakomboa hao waliokuwa chini ya sheria, ili tupate kupata-kuwa-wana. Na kwa kuwa mu wana, Mwenyezi Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe aingie miyoni mwetu na kupiga ukelele, Ewe Baba, Babaetu. Hata umekuwa hu mtumwa tena lakini umekuwa mwana : na ukiwa mwana umekuwa mriithi wa Mungu kwa njia ya Kristo.

Injili. Mathayo 1. 18-25

NA Yesu Kristo kuzawa kwake kuliktuwa hivi : wakati Mariamu mamaye alipoposwa na Yusufu, kabla hawajasongoleana, akaonekana yuna mimba kwa Roho Mtakatifu. Na yule mumewe, yule Yusufu, kwa vile alivyo mtu wa haki hataki kumwaibisha, akataka kumwacha kwa siri. Alipokuwa akiyawaza hayo, wakati huo malaika wa Bwana akamtorea katika ndoto, aka-mwambia, Ewe Yusufu mwana wa Daudi, usiche kumtwaa Mariamu mkeo, kwani hicho kilichotungwa mimba ndani yake chatokana na Roho Mtakatifu : naye atamzaa Mwana, utamwita na jina lake YESU, kwani ndiye atakayewaokoa watu wake na madhambi yao. Nayo yote haya yamekuwa ili lipate kutimia lilitollenwa na Bwana kwa kinywa cha nabii, aliposema, Angalieni, mwanamwali atakuwa na mimba, tena atamzaa mwana mwanamumume, naye jina lake watamwita Imanweli ; maana yake likigeuzwa, ni Mwenyezi Mungu pamoja nasi. Na Yusufu alipoondoka usingizini mwake, akafanya kama alivyoagizwa na malaika wa Bwana, akamtwaanikewe, wala hakunjua hata alipokwisha kumzaa mwana mwanamumume kifungua mimba : akamwita jina lake YESU.

IDI YA KUPASHWA TOHARA KRISTO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, huyo Mwanayo Mwenye-baraka uliamuru atahiriwe apate kuifua sheria kwa ajili ya wanadamu : utupe nasi tohara ya kweli ya Roho, ili kwamba kwa kutahiriwa katika miyo yetu na via vyetu yote, na kufiliiwa na tamaa zote za ulimwengu na za mwili; tuyafuate kwa kila jambo mapenzi yako yaliyobarikiwa ; kwa yeze Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 4. 8-14

HERI ni yake mtu huyo ambaye Bwana hamhesabii Dhambini. Basi, je, barake hiyo i juu ya wale wa tohara tu, au i juu ya wale wasio tohara pia ? kwani

twasema, Kwa Iburahimu imani yake ilihesabiwa kuwa ni haki. Ilihesabiwa ? alipokuwa tohara au alipokuwa hajatahiriwa ? Sipo alipokuwa tohara, ila alipokuwa hajatahiriwa : naye alipokea alama ya tohara, ni muhuri wa ile imani aliyokuwa nayo, alipokuwa hajatahiriwa ; ili kwamba awe baba wa wale wote wanaoamini, wajapokuwa katika kutotahiriwa, ili kwamba wao pia wahesabiwe kuwa na haki ; tena awe baba wa tohara kwa wale amba si wa tohara tu, lakini zaidi waenda kwa kufuata nyayo za ile imani ya babaetu Iburahimu *aliyokuwa nayo* naye alikuwa hajatahiriwa. Kwani ile ahadi walipewa Iburahimu na uzazi wake, ya kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu, *haikunfikilia kwa njia ya ile sheria* lakini *alipewa kwa njia ya haki ya imani*. Kwani kwamba wale walio wa sheria .ni kufanywa warithi, imani imekuwa haina faida, na ile ahadi imefanywa kuwa si ahadi tena.

Injili. Luka 2. 15-21

IKAWA walipoondoka kwao wale malaika, walipowaacha Iwakienda mbinguni, wakasemezana wale wachunga wao kwa wao : Twendeni basi, tufulize hata Bethilehemu, tukaone neno hilo lilitokuwa, alilotujuvisha Bwana. Wakaenda upesi wakamkuta Mariamu na Yusufu, na mtoto mchanga naye amelala katika hero. Hata walipokwisha kumwona wakawaambia habari ya maneno walioambiwa katika yule mtoto. Wote waliosikia wakastaajabu kwa yale walioambiwa na wachunga. Lakini Mariamu alikuwa kuyaweka maneno yale yote, akiyawaza moyoni mwake. Wakarudi wale wachunga, huku wakimtukuza Mungu na kumsifu kwa yote waliosikia na kuona, vivile kama walivyoambiwa. Hata zilipotimia siku nane za kumpasha tohara mtoto, alitwa jina lake YESU, kama alivyoitwa na malaika asijachukuliwa mimba.

¶ Sala hii na Waraka huu na Injili hii husomwa kila siku hata ifike Idi ya Mafunuo.

IDI YA MAFUNUO,
au, ya Kristo kufunuliwa mbele ya hao mataifa

Sala

EWE Mungu, wewe uliwafunulia mataifa Mwanayo Emzaliwa pekee kwa uongozi wa nyota ; nawe ukubali kwa rehema zako ya kwamba, sisi tunaokujua sasa kwa kuamini, mwishowe, baada ya kwisha maisha haya ya sasa, tuufurahie Uungu wako mtukufu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 3. 1-12

KWA sababu hii mimi Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi watu 'wa hao mataifa, kwamba mmesikia habari ya uwakili wa ile neema ya Mwenyezi Mungu, niliopewa mimi kwa ajili yenu : ya kwamba nilijuvishwa ile siri kwa ufunuo, vivile kama niliyotangulia kuandika kwa maneno machache, na kwa hayo mtakayosoma mtapata kuelewa na sahamu yangu katika siri ya Kristo : ambayo hawakujuvishwa wanadamu katika vizazi vingine, kama ilivyofunuliwa sasa katika Roho kwa mitume wake watakatifu na manabii *wake* : *maana*, watu wa hao mataifa wamekuwa washirika wa urithi, na via vya mwili mmoja, na washirika, kwa njia ya ile habari njema, wa ile ahadi iliyo katika Kristo Yesu ; *habari njema* ambayo nilikuwa mtumishi wake sawasawa na kipawa cha neema ile ya Mwenyezi Mungu niliyopewa mimi sawasawa na kitendo cha uwezo wake. Mimi, niliye mdogo wa watakatifu walio wadogo sana, nilipewa neema hii, *maana*, niwhabiriru watu wa hao mataifa utajiri wa Kristo usiotafutika : na kuwatia mwanga *wapate kujua* wote jinsi ulivyo ile uwakili wa siri ambayo imefichwa tangu zamani zote katika Mwenyezi Mungu aliyeumba vitu vyote kwa njia ya Yesu Kristo : ili kwamba hekima ya Mwenyezi Mungu iliyo na namna nyingi ijuvishwe sasa kwa zile enzi, na zile amri zilizo mbinguni, kwa njia ya kanisa, sawasawa na makusudi ya

milele aliyokusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu : ambaye katika yeye tuna uthubutifu na kuingia ndani kwa kutumaini kwa njia ya imani *yetu* kwake.

Injili. Mathayo 2. 1-12

NA alipokwisha kuzaliwa Yesu huko Bethilehemu ya Yudea katika siku za mfalme Herode, wakati huo watu mamajusi, watoka pande za mashariki, wakafikilia Yerusalem, wanena, Yuko wapi yule aliyezaliwa mfalme wa Mayahudi ? kwani nyota yake huyo tumeionna pande za mashariki, tumekuja ili kumwabudu. Aliposikia yale mfalme Herode akaingiwa na hofu, yeye na Yerusalemu yote pamoja naye. Akiisha kuwakutanisha makuhanu wakuu na wana-wa-vyuoni pia wote, akawauliza, Ni wapi Kristo atakapoza liwa ? Wao wakamwambia, Katika Bethilehemu ya Yudea, kwani ndivyo ilivyoandikwa kwa mnkonu wa nabii, ya kwamba, Nawe Bethilehemu, nchi ya Yuda, kamwe hu mdogo mionganu mwa wakubwa wa Yuda : kwani kutoka kwako wewe atatoka mwenye kutawala, mtu atakayewachunga watu wangu Israeli. Ndipo Herode akawaita siri wale mamajusi akawataka hakika ya majira yake ile nyota kuonekana. Akawapeleka hata Bethilehemu, akawaambia, Enendeni mkaapeleze hakika-hakika katika habari ya yule mwana, mtakapo-mwona rudini tena mkaniletu habari, nipate nami kwenda kumwabudu. Wale walipokwisha kusikia maneno ya mfalme wakaenda, nayo nyota waliyoiona pande za mashariki, ile, yawatangulia hata ikaenda ikasimama juu ya pahali alipo yule mwana mchanga. Wakaiona ile nyota, wakafurahi furaha kubwa mno. Walipofikilia ndani ya nyumba, wakamwona mwana na Mariamu mamaye, wakaanguka na nchi, wakamwabudu, wakafungua akiba zao, wakamsongezea *yule mwana* vipawa, dhahabu na ubani na manemane. Kisha baadaye walipoonywa na Mwenyezi Mungu kwa kuotesha ya kutorejea kwa Herode, wakashika njia nyininge wakaenda zao kwao.

JUMAPILI YA KWANZA BAADA YA MAFUNUO

Sala

TWAKUOMBA sana, ewe Bwana, kwa rehema zako uwakubalie watu wako wanyenyeketu wakuombay, ukawape kuyatambua na kuyajua yawapasayo kuyafanya, tena uwape na neema yako na msaada wako, ili wayatimiz yote kwa uaminifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 12. 1-5

BASI nataka sana kwenu ninyi ndugu zangu, kwa buruma za Mwenyezi Mungu, msongeze mili yenu iwe sadaka ilioy hai, *iliyo takatifu*, ipendekezayo kwa Mwenyezi Mungu, ndiyo ibada yenu ifaayo. Nanyi msifanuishwe nafsi zenu na *mambo ya zamani* hizi : lakini mbadilishwe kwa kufanya upya akili zenu, mpare kuyajua sana yale mapenzi ya Mwenyezi Mungu yale yaliyo mema, yaliyokubalika, yaliyo matimilifi. Kwani nanena katika ile neema niliyopewa, *namwambia* kila mtu aliye mionganii mwenu, asifikirie nafsi yake zaidi ya yale yampasayo kufikiri : lakini ajifikirie kwa kiasi, vivile kama Mwenyezi Mungu alivyomgawanyia kila mtu kiasi *chake* cha imani. Kwani ni vivile kama katika mwili mmoja tulivyo na via vingi, na via hivi vyote havina kazi moja : sisi ni vivyo, tulio wengi, tu mwili mmoja katika Kristo, tena tu via kila mmoja kwa mwensiwe.

Injili. Luka 2. 41-52

NAO wazee wake walikuwa wakienda Yerusalem mwaka hata mwaka katika idi ya Pasaka. Hata alipopata umri wake miaka kumi na miwili, nao wakakwea kwenda Yerusalem kama desturi ya idi : walipokwisha kutimiza zile siku wakarudi kwao, ilikuwa kusalia nyuma yule kijana Yesu huko Yerusalem, wazazi wake hawana habari. Wamdhania kwamba yu *mumo* katika safari ; wakaenda mwendo wa kuchwa, ikawa kumtafuta kwa jamaa zao na wenziwao. Hata walipomwona hako,

wakarudi kuko Yerusalem, wakimtafuta. Hata kwa siku ya tatu wakamwona katika hekalu, ameketi katikati ya wana-wa-vyuoni, akiwasikiza, akiwaliza na masiala. Wakastaajabu wote, kadiri ya waliomsikia, kwa fahamu zake na jawabu zake. Nao walipomwona wakashangaa, nmaye akamwambia, Mwanangu, ni nini kutufanya hivi ? Angalia, mimi na babaako tulikuwa tukikutafuta huku tukisikitika. Akawaambia, Kwani kunitafuta ? Hamnijui kwamba imenipasa kuwa katika mambo ya Babaangu ? Yasiwaelee maana yake lile neno alilowambia. Akashuka, akaenda pamoja nao hata Nazarethi, alikuwa akiwatii ; na nmaye akiyaweka haya yote moyoni mwake. Naye Yesu alikuwa akiendelea katika hekima na kimo, na katika fadhilli kwa Mungu na kwa watu.

*JUMAPILI YA PILI BAADA YA MAFUNUO**Sala*

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, uamrishaye mambo yote ya mbinguni na ya duniani ; utege masikio yako ya rehema kwa maombi yetu watu wako, utupe amani yako, tuwe nayo siku zote tutakazokuwa hai duniani ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 12. 6-16

TENA tuna vipawa mbali-mbali, sawasawa na ile neema tuliyopewa sisi, kwamba ni ujumbe, *na tuthubiri* sawasawa na kiasi cha imani yetu : au utumishi, *na tutumike* katika utumishi wetu : au ye ye afunzaye *na atumike* katika kufunza kwake : ye ye aonyaye, *na atumike* katika kuonya kwake : awapaye *watu*, *na awape* kwa ukarimu : ye ye aamrishaye, *na aamrishe* kwa bidii : ye ye amhurumiaye *mwensiwe*, *na amhurumie* kwa furaha. Mapenzi na yasiwe na unafiki. Iweni wenye kukataa kiovu : kilicho chema shikamaneni nacho. Kapendaneni kwa wema kila mtu na mwensiwe katika mapenzi yapasayo ndugu : wenye kutangulizana wenywewe kwa wenywewe

katika heshima : si walegevu katika bidii yenu : wenyewe kuwaka moto katika roho zenu : wenyewe kumtumikia Bwana : wenyewe kufurahi katika matumaini : wenyewe kuvumilia *mkiwa* na mateso : wenyewe kudumu sana katika kuomba Mungu : wenyewe kufanya changizo kwa uhitaji wao watakatifu : wenyewe kujibidiisha na kuwakaribisha wageni. Wabarikieni hao wawaudhio ninyi : kabarikieni wala msiapize. Furahini pamoja na hao wanaofurahi : kalieni na hao wanaolia. Nuieni nia moja ninyi kwa ninyi. Msiveke nia zenu katika yale yaliyotukuka, lakini mridhike na hao walio wanyenyekuju.

Injili. Yohana 2. 1-11

HATA siku ya tatu kulikuwa na arusi Kana ya Galilaya, na mamaye Yesu alikuwa papo. Na Yesu na wanafunzi wake walikuwa wameitwa arusini. Hata ilipowaishia divai, mamaye Yesu akamwambia, Hawana divai. Yesu akamwambia, Nina nini mimi na wewe, mwanimakie? Hajaja saa yangu. Mamaye akawaambia watumishi, Awaambialo lote, fanyeni. Napo palikuwa na kasiki sita za mawe zimesimama kama kutawadha kwoo Mayahudi, kila moja yakunjukia kiasi cha nzio mbili tatu. Yesu akawaambia, Jazeni maji kasiki. Wakazijaza tele. Akawaambia, Tekeni sasa, mkampelekee mkuu wa kikao. Wakampelekea. Hata mkuu wa kikao alipoyaonja maji, yamekuwa divai, wala hajui inapotoka ; wanaojua ni wale watumishi walioyateka maji : mkuu wa kikao akamwita bwana-arusi ; kisha akamwambia, Kila mtu kwanza huleta divai njema, hata watu wakiisha kunywa sana, akaleta isiyokuwa nzuri : nawe divai nzuri umeiziuia hata sasa. Mwanzo huu wa ishara zake alifanya Yesu Kana ya Galilaya akaufanya wazi utukufu wake ; wanafunzi wake wakaamini kwake.

JUMAPILI YA TATU BAADA YA MAFUNUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, twakuomba Uuangalie kwa rehemaa huu udhaifu wetu, na kila tukisongwa na hatari na shida uunyoshe kwetu mkono wako

wa kuume, uwe msadaa wetu na ulinzi wetu, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 12. 16-21

MSIWE wenyewe akili kwa nafsi zenu wenye. Msimili pe mtu awaye yote uovu kwa uovu. Muwe wenyewe kutangulia kutengeza mambo mema mbele ya watu wote. Ikiwezekana, kwa upande wenu, muwe na amani pamoja na wanadamu wote. Msitafute kisasi, wapenzi wangu, lakini afadhali iachieni hasira *ya Mungu* nafasi : kwani imeandikwa, Kisasi ni changu mimii, mimi nitalipa, anena Bwana. Lakini adui wako akiwa na njaa, mpe chakula : akiwa na kiu, mpe *maji* ya kunywa : kwani katika kufanya hivyo utamtweka na kuongeza makaa ya moto juu ya kichwa chake. Isiwe ninyi kushindwa na uovu, lakini kaushindeni ule uovu kwa wema.

Injili Mathayo 8. 1-13

ALIPOSHUKA Yesu mlimani akaandamwa na maku-tano mengi. Naye huyo ndiye, akaendewa na mwenye ukoma akamsujudia, akamwambia, Bwana, utakapo, waweza kunitakasa. Yesu akaunyosha mkono akamgusa : akamwambia, Nataka : utakate. Papo hapo akatakata ukoma wake. Yesu akamwambia, Angalia usimwambie mtu neno ; enenda ukamwonyeshe kuhani nafsi yako, utoe na kipawa kilichoagizwa na Musa, uwe ushuhuda kwoo. Na kuingia kwake Kaperinaumu, akaendewa na akida mmoja, yuamsihi-sihi na kumwambia, Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani mwili wake umeimpooza, naye yuateswa sana. Yesu akamwambia, Mimi nitakuja nikampoz. Yule akida akamjibu akanena, Bwana, mimi si mtu wa kujiliwa na wewe ukaingia chini ya paa langu : lakini wewe nena tamko moja tu, atapoa mtumishi wangu. Kwani nami ni mtu chini ya amri, nina askari chini yangu ; nami humwambia huyu, Enda, akaenda : nikamwambia huyu, Njoo, akaja : nikamwambia na mtumishi wangu, Fanya hili, akafanya. Aliposikia Yesu yale akastaajabu, akawaambia waliomwandama,

Ni kweli nawaambia, hata katika Israeli sijaona imani ipatayo kama hii. Ila nawaambia ya kwamba watakuja wengi kutoka maawioni na machweoni waje waketi chakulani pamoja na Iburahimu na Isaka na Yakobo, katika ufalme wa mbingu ; wale wana wa ufalme watutupa katika giza iliyo nje : kutakuwa na kulia huko na kukaza-kaza meno. Yesu akamwambia akida, Enenda, na iwe kwako kama ulivyoamini. Akapozwa yule mtumishi wake katika saa ile.

JUMAPILI YA NNE BAADA YA MAFUNUO

Sala

EWE Mungu, watujua hali yetu, ya kwamba kwa E tulivyokaa katika mambo ya hatari nyingi yaliyotuzunguka kote-kote, tumekuwa hatuwezi kusimama sawasawa, kwa sababu ya unyonge wa tabia yetu tuliyo nayo : twakuomba utilinde kwa hifadhi yako na uwezo wako, viwe hivyo vyenye kutuwcka salama na kila zani, na kutuponya kila tujaribiwapo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 13. 1-7

KILA mwenye uhai na awe chini ya *wenye kutawala* walio juu yake : kwani hapana *mwenye kutawala* asiyetokana na Mungu : na yule *mwenye kutawala* aliyeo amewekwa na Mungu. Kwa ajili ya hayo, yule atakayeshindana na *yule mwenye kutawala* huyapinga yale maagizo ya Mwenyezi Mungu : nao wapingao watajipatia hukumu wenye. Kwani wale mahakimu si utisho kwa ile kazi njema, lakini kwa ile mbaya. Nawe wataka usiche *yule mwenye kutawala*? fanya lililo jema, nawe utapata sifa kwa huyo *mwenye kutawala*. Kwani ni mtumishi wa Mungu kwako wewe kwa ajili ya wema. Ila ikiwa wewe kufanya lililo baya, uche : kwani hauchukui ule upanga pasipokuwa na sababu : kwani ni mtumishi wa Mungu, *mwenye kulipa* kisasi kwa hasira, kwake yule atendaye

lililo baya. Ndipo ipasapo, muwe chini ya amri, si kwa sababu ya ile hasira tu, lakini na kwa ajili ya nia pia. Kwani ni kwa sababu hii mwatoa na kodi : kwani ni watumishi wa Mungu, wenye kudumu siku zote katika neno lilo hilo. Kwa ajili ya hayo lipeni kwa wote kile kipasacho : kodi kwa yule impasaye kodi : ushuru kwa yule umpasaye ushuru : hofu kwa yule impasaye hofu : heshima kwa yule impasaye heshima.

Injili. Mathayo 8. 23-34

HATA alipopanda chomboni, akaandamwa na *wanafunzi* wake. Nayo, hiyo ndiyo, ikaingia dharuba kuu mle baharini, hata kikawa chombo kufinikwa na mawimbi ; na mwenyewe alikuwa amelala. Wakamwendea *wanafunzi wake* wakamwamsha, wamwambia, Bwana, utuokoe ; tu katika kupotea ! Akawaambia, Kwani kuwa na hofu ninyi ! mu wachache wa imani ! Ndipo hapo akasimama akaukemea upepo na bahari, ikawa shwari kuu. Wakastaajabu wale watu, wanena, Yu jinsi gani mtu huyu hata atiwe na upepo na bahari ? Hata kufika kwake ng'ambu katika nchi ya Wagadari, akatokewa na watu wawili, watu waliopagawa na pepo, nao watoka makaburini ; ni wakali sana watu hao, hata asiweze mtu kupita njia ile. Nao hao ndio, wakapiga ukelele, wanena, Sisi tuna nini na wewe, Yesu, Mwana wa Mungu ? Je, umekuja hapa kabla ya wakati wetu kuja kututesa ? Palikuwa na kundi la nguruwe wengi hapo, li mbali na wao, lalisha. Ikawa wale pepo kumsihisihi, wanena, Kwamba watutoa, tupeleke tukaingie katika kundi la nguruwe. Akawaambia, Endeni. Wakawatoka wale *watu wawili*, wakaenda wakaingia lile kundi la nguruwe ; nalo, hilo kundi lote likateremka gengeni likashukia baharini, wakafa katika maji. Na walisha wakakimbia, wakaenda majini kwao, wakaenda wakatoa habari ya yaliyowapata yote, na ya wale waliopagawa. Nao wakati huo walitoka wale watu mji mzima kwenda kumlaki Yesu ; walipomwona wakamsihii apate kuondoka mipankani mwa *kwenda kwingine*.

JUMAPILI YA TANO BAADA YA MAFUNUO

Sala

TWAKUOMBA sana, ewe Bwana, hili kanisa lako, nyumba yako, ulilinde daima katika dini yako ya kweli; ili kwamba hao walitegeremeo tumaini la neema yako ya mbinguni, hilo tu, walindwe milele na uwezo wako mkuu; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wakolosai 3. 12-17

BASI, kama wateule wa Mwenyezi Mungu, walio watakatifu na waliopendwa, kajivikeni huruma za ndani, na vitendo vyema, na unyenyekevu, na upole, na uvumilivu; kuchukuana ninyi kwa ninyi, na kusameheana kila mtu na mwensiwe, mtu awaye yote akiwa na neno na mwensiwe; vivile kama Bwana alivyowasamehe ninyi, nanyi fanyeni vivyo: na zaidi ya mambo hayo yote iweni na mapenzi, ambayo ni kifungo cha utimilifu. Amani ya Kristo na itawale ndani ya mioyo yenu, nanyi mliitwa katika mwili mmoja mpate hiyo *amani*: tena iweni na shukrani. Neno la Kristo na liketi ndani yenu kwa utajiri katika hekima yote: mkifunzana na kuonyana ninyi kwa ninyi kwa zaburi na nyimbo na tenzi za rohoni, huku mkimwimbia Mwenyezi Mungu kwa neema mioyoni mwenu. Tena kila jambo mfanyalo, katika neno na katika kazi, *tendeni* yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mwenyezi Mungu Baba kwa njia yake yeye.

Injili. Mathayo 13. 24-30

UTFALME wa mbingu umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika shamba lake: lakini muda watu walipolala, alikwenda adui yake akapanda na zawani katikati ya nganu, akaenda zake. Ilipotepuza miche ikaza mashuke, ndipo zilipotokeza zawani nazo. Basi wakenda watumishi wa mwenye nyumba, wakamwambia; Bwana, hukupanda mbegu njema katika shamba lako? Limepatikanaje na zawani? Akawaambia, Ni mtu adui aliyefanya hivyo. Watumishi wakamwambia, Je, wataka

tuende tukazikusanye? Akasema, La; msije katika kuzikusanya kwenu zawani mkaing'oa na nganu. Via-cheni vikamee vyote viwili hata mavunoni: na majira ya mavuno nitawaambia wavunao, Kusanyeni kwanza zawani mzifunge mizigo mpate kuziteketeza: na nganu ikusanyieni ghalani mwangu.

*JUMAPILI YA SITA BAADA YA MAFUNUO**Sala*

EWE Mungu, Mwanayo Mwenye-baraka alifunuliwa Eili apate kuziangamiza kazi za Shetani, na kutufanya sisi kuwa wana wa Mungu, warithi wa uzima wa milele; twakuomba, utupe ya kwamba kwa kuwa na tumaini hilo sisi, tujisafi wenywewe karma yeye alivyo safi; hata wakati atakapotokea mara ya pili na uwezo mkuu na utukufu mwingi, iwe sisi nasi kufananishwa naye, na kuwamo katika usalme wa enzi yake ya milele; humo aishimo na kutawala pamoja na wewe Baba na wewe Roho Mtakatifu, Mungu Mmoja, milele. *Amina.*

Waraka. 1 Yohana 3. 1-8

ANGALIENI, ni mapenzi namna gani yeye Baba aliyotupa sisi, kwamba tuitwe wana wa Mungu: nasi ndio. Kwa ajili ya hayo, hiyo dunia haitujui sisi, kwa sababu haikumjua yeye. Wapenzi wangu, tu watoto wa Mungu sasa, nalo halijafunuliwa bado hilo tutakalokuwa. Twajua ya kwamba, akifunuliwa, tutakuwa mfano mmoja na yeye; kwa kuwa tutamwona yeye vivile kama alivyo. Na kila mtu aliye na matumaini haya kwake yeye, husafi nafsi yake vivile kama yeye alivyo safi. Kila mtu afanyaye dhambi, afanya naye maasia: na dhambi ndiyo kuasi. Nanyi mwajua ya kwamba alifunuliwa yeye ili kwamba aziondoe dhambi; wala hamna dhambi ndani yake yeye. Kila mtu akaaye ndani yake hafanyi dhambi; kila mtu afanyaye dhambi hakumwona yeye, wala hakumjua. Watoto wangu wadogo, mtu awaye yote na asiwapoteze ninyi: yeye afanyaye haki ndiye mwenye haki: vivile kama yeye alivyo mwenye haki: yeye afanyaye dhambi

ametokana na Shetani ; kwa kuwa huyo Shetani hufanya dhambi tangu mwanzo. Yeye mwana wa Mwenyezi Mungu alifunuliwa kwa ajili ya neno hilo, ili kwamba aziharibu hizo kazi za Shetani.

Injili. Mathayo 24. 23-31

WAKATI huo mtu akiwaambia, Huyu ndiye, Kristo huyu hapa ! au, Huyo ndiye huko ! msisadiki. Kwani watatoka Wakristo wa uwongo, na manabii wa uwongo, watoe ishara kubwa kubwa na vioja, kwa kuwepoteza, kwamba yawezekana, hata wale wateule. Nanyi, hayo ndiyo, nimetangulia kuwaambia ! Basi watakapowaambia, Huyo ndiye, yuko barani ; msitoke nje : Huyo ndiye, yumo vyumba vya siri ; msisadiki. Kwani kama vile umeme utokavyo maawioni uking'aria machweoni, ndivyo iwavyo kuja kwake Mwana wa binadamu. Kwani pahali patakapokuwa na mfu na tai hukusanyaika papo. Lakini mara, baada ya matoes ya siku zile, juu litageuka giza, na mwezi hautatoa nuru zake, na nyota zitaanguka mbinguni, na hizi nguvu za mbinguni zita-cheza-cheza. Kisha wakati huo ndipo itakapoonekana mbinguni ishara yake Mwana wa binadamu, na wakati huo watakaa msiba makabila yote ya nchi : kisha watamwona Mwana wa binadamu yuaja juu ya mawingu ya mbingu, kwa nguvu na utukufu mwangi. Kisha awatsuma malaika zake kwa sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake pamoja kuwatoa pande za pepo nne, kutoka ncha hii ya mbingu hata ncha hii.

JUMAPILI YA TATU MBELE YA SAUMU
(iitwayo Septuagesima)

Sala

TWAKUOMBA, ewe Bwana, uzisikize kwa ihisani yako sala za watu wako ; ili kwamba sisi, tulioadhibiwa kwa haki, kwa ajili ya makosa yetu, tuokolewe na kurehemewa na wewe kwa upole wako, kwa utukufu wa jina lako ; kwa Yesu Kristo, Mponyi wetu, anayeishi na kutawala siku zote pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja milele. *Amina.*

Waraka. i Wakorintho 9. 24-27

HAMJUI ya kwamba hao wapigao mbio katika mashi-ndano, hupiga mbio wote, ila ni mmoja apataye tuzo ? Na vivyo hivyo pigezi mbio ili impate. Na kila mtu aliye na bidii katika michezo huzuia nafsi katika mambo yote. Basi hao ni kufanya, ili kwamba wapate taji iharibikayo, ila sisi ni *kupata taji* isiyoharibika. Basi sasa mimi jinsi nipigavyo mbio, si kama asiyekuwa na hakika ; jinsi nipigavyo makonde, si kama anayepiga anga tu : lakini naupondaponda mwili wangu na kuutumikisha, isiwe kwa njia yoyote baada ya kuwahubiri wengine nikawa mwenyewe kutupwa kando.

Injili. Mathayo 20. 1-16

KWANI ufalme wa mbingu ni mfano wa mtu mwenye nyumba, aliyetoka asubuhi na mapema kwenda kuajiri wakulima, *wapate* kumlimia shamba lake la mizabibu. Akiisha kuagana na wakulima siku kwa thumuni akawapeleka katika shamba lake la mizabibu. Akatoka yapata saa tatu, akaona wengine wamesimama sokoni hawana kazi ; akawaambia nao, Endeni nanyi katika shamba la mizabibu, kisha nitawapa kilicho haki yenu. Wakaenda. Akatoka tena yapata saa ya sita na saa ya tisa, akifanya kama vile. Hata kama wakati wa saa ya kumi na moja akatoka akaona wengine wamesimama, hawana kazi, akawaambia na wao, Mbona mmesimama hapa kuchwa hamna kazi ? Wakamwambia, Kwa sababu hakutuajiri mtu. Akawaambia, Endeni nanyi katika shamba, nanyi mtapata haki yenu. Basi ilipoingia jioni, yule bwana wa shamba akamwambia nokoa wake, Kawaite wakulima, uwape ujira wao, uanze tangu wa mwisho hata wa kwanza. Wakaenda walioajiriwa katika saa ya kumi na moja wakapokea kila mtu thumuni. Hata walipokwenda wa kwanza, walidhani kwamba watapata zaidi, wakapatna nao vivyo thumuni thumuni. Walipokwisha kupokea ikawa kumnung'unikia yule mwenye nyumba, wakinena, Hao wa mwisho wamefanya kazi ya saa moja tu, nawe umewalinganisha na sisi, watu tuliochukua mzigzo na hari

ya mchana kuchwa. Naye akamjibu mmoja wao, aka-mwambia, Rafiki, sikudhili mu. Hukuagana nami kwa thumuni? Shika haki yako ujiendee zako; nataka kumpa huyu wa mwisho sawasawa na wewe. Hainipasi kufanya kama nitakalo katika mali yangu mwenyewe? Au jicho lako limekuwa ovu kwa hivi nilivyo mwema? Ni hivyo itakuwa walio nyuma kuwa mbele, na walio mbele kuwa nyuma, kwani wenyenye kuitwa ni wengi, wenyenye kuchaguliwa ndio wachache.

JUMAPILI YA PILI MBELE YA SAUMU
(iiitwayo Sexagesima)

Sala

EWE Bwana Mungu, wewe watuona ya kwamba hatutumaini kazi yetu tufanyayo wenyewe iwayo yote; ukubali kwa rehema ya kwamba kwa nguvu zako wewe tukingwe kwa kila uovu: kwa Yesu Kristo, Bwana wetu Amina.

Waraka. 2 Wakorintho 11. 19-31

MWAVUMILIA na wapumbavu kwa furaha, nanyi mu wenyenye akili. Kwani mwavumilia na mtu, akiwafanya watumwa, akiwala, akiwateka nyara, akijikuza, akiwapiga usoni. Nanena kwa jinsi ya kujivunja heshima kana kwamba tulikuwa wanyonge sisi. Ila kwa neno lolote atakalosubutu mwininge (nanena kwa upumbavu) na mimi nasubutu. Je, ni Wahibirania wao? na mimi pia. Ni Waisiraeli wao? na mimi pia. Ni kizazi cha Iburahimu wao? na mimi pia. Ni watumishi wa Kristo wao? (nanena kama mwenye wazimu) mimi ni zaidi; katika taabu za kazi zaidi sana, katika magereza mara nyingi zaidi, katika mapigo yaliyozidi sana, katika mauti mara nyingi. Nilipokea mikononi mwa Mayahudi mara tano *kupigwa mijeledi* arobaini kupungua moja. Nilipigwa kwa bakora mara tatu, nilipigwa kwa mawe mara moja, nilivunjikiwa na merikebu *nili safarini* mara tatu, nilikuwa katika bahari usiku mmoja na mchana mmoja: *katika safari* mara nyingi, *katika hatari za mito*, *katika hatari za*

wevi, *katika hatari kwa watu wa kabila langu*, *katika hatari kwa watu wa hao mataifa*, *katika hatari za mijini*, *katika hatari za barani*, *katika hatari zi baharini*, *katika hatari kwa ndugu za uwongo*; *katika taabu za kazi na uchungu*, *katika kukesha mara nyingi*, *katika njaa na kiu*, *katika kufungu mara nyingi*, *katika baridi na utupu*. Bila hayo nisiyoyataja, kuna kazi hiyo inilemeayo kila siku, nayo ni maangalizi ya makanisa yote. Ni nani aliye mnyonge nami si ninyonge? ni nani akunguwazwaye nami sioni kuchukwa? Ikinipasa kujisifu nitajisifu kwa mambo hayo ya unyonge wangu. Mwenyezi Mungu, naye ni Babaye Bwana Yesu, aliyebarikiwa milele, ajua ya kwamba sineni uwongo.

Injili. Luka 8. 4-15

WALIPOKUTANIKA watu wengi, na wale watokao miji miji wakimwendea, akasema nao kwa mithali: Mpanzi wa mbegu, huyo ndiye, alitoka kwenda kupanda mbegu yake: alipokuwa akipanda, tembe nyingine zikaanguka kando ya njia, zikakanyagwa-kanyagwa, zikaliwa na nyuni wa angani: nyingine zikaanguka penye mwamba; zilipocheputa zikakauka mara kwa kule kukosa kwake rutuba. Nyingine zikaanguka kati ya miiba, ile miiba ikacheputa pamoa nazo, ikazisonga zikafa. Nyingine zikaanguka katika nchi ya udongo mwema, zikacheputa, zikazaa moja kwa mia. Akiisha kusema haya ikawa kupiga ukelele: Mwenye masikio ya kusikia na asikie! Wanafunzi wake wakamuuliza, Maana yake ni nini mithali hiyo? Akasema, Ninyi mmepewaa kujua siri za ufalme wa Mungu: na wengine wote kwa mithali mithali, ili kwamba wangaona wasione, wangasikia wasifahamu. Nayo ndiyo maana yake mithali: Mbegu ni neno la Mungu. Wa kando ya njia ni hao waliosikia, kisha akaenda Shetani akaliondoa lile neno miyoni mwao, wasije wakaamini wakaokoka. Wa juu ya mwamba ni hao ambaa wakiisha kusikia hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana shina hao, ni watu waaminio kitambo kidogo, hata wakati wa kujaribiwa ni kukengeuka. Walioanguka miibani ni hao waliosikia, hata wakaenda vile wakasongo-

lewa na fadhaa na mali na anasa vya maisha haya, wasiivishe chochote. Na wa katika udongo mwema, ni watu waliosikia neno, wakalishika katika miyo myema iliyleka, wakaza mazao kwa kuvumilia.

JUMAPILI ILIY MBELE YA SAUMU

(iitwayo Quinquagesima)

Sala

EWE Bwana, wewe umetufunza ya kwamba, kazi zetu zote hazifai tukikosa kule kupendana ; umtume kwetu Roho wako Mtakatifu, aje atumwagie ndani ya miyo yetu hicho kipawa chako kilicho kizuri sana cha kupendana, nacho ndicho kifungo chenyewe cha amani na kila aina ya wema, ambacho mtu akikosa hicho anakuuwa ni maiti machoni pako, ajapokuwa yu hai : utupe haya kwa ajili ya Yesu Kristo, Mwanayo pekee. *Amina.*

Waraka. 1 Wakorintho 13. 1-13

NIJPONENA kwa lugha za wanadamu na za malaika, nami sina mapenzi, nimkuwa shaba ivumayo au tuwasi la kugonga. Nijapokuwa na unabii, na kuzijua siri zote na ujuzi wote : nijapokuwa na imani yote hata kutamisha vilima, nisipokuwa na mapenzi, mimi si kitu. Nami nijapotoa vitu vyang'vyote kuwalisha *maskini*, nijapotoa mwili wangu upigwe moto, nisipokuwa na mapenzi, sifai lolote. Mapenzi huvumilia, hutenda mema : mapenzi hayana wiyu ; wala hayanyeti ; wala hayajivuni ; wala hayakosi adabu ; wala hayatafuti ambalo ni la nafsi yake ; wala hayakasirishwi upesi ; wala hayahesabii ule uovu ; wala hayafurahii madhambi ; ila hufurahi pamoja na ile kweli ; mapenzi husesitiri yote, huamini yote, hutumaini yote, huvumilia yote. Mapenzi hayakomi milele : ila *ukiwapo* unabii, utafanywa kuwa si kitu : *zikiwapo* lugha, zitakoma ; *ukiwapo* ujuzi, utafanywa kuwa si kitu. Kwani twajua kwa upungufu, twafanya na unabii kwa upungufu ; hapo kitakapokuja hicho kilicho kitimilifu, hapo hicho kilicho kipungufu kitaondolewa. Nilipokuwa mtoto, nilinena kama mtoto, nilifahamu kama mtoto, nilifikiri kama mtoto ; sasa nilipo

mtu mzima, nimeviondoa vile vya utoto. Kwani hivi sasa twaona katika kioo, kama kitendawili ; ila hapo *mkuona* uso kwa uso : hivi sasa najua kwa upungufu ; ila hapo nitajua sana, vivile kama nilivyojulikana nami sana. Ilia hivi sasa yakaa imani, na matumaini, na mapenzi, haya matatu ; ila katika hayo matatu kubwa lao mno ni mapenzi.

Injili. Luka 18. 31-43

AKAWATWAA wale watu kumi na wawili, akawambia, Haya ndiyo, tu katika kukwea kwenda Yerusalem, na alioandikiwa Mwana wa binadamu na manabii yatakuja kutimia yote. Kwani atatiwa mikonorii mwa hao mataifa, tena atafanyiwa dhihaka, ataonewa na kutemewa mate : wampige na mjeledi, kisha watamuua ; hata kwa siku ya tatu atafufuka. Wala wao hayakuwaelea maneno yale hata mojawapo, jambo lile likawafichamania, wasitambue maana yake aliyoyanena. Ikawa alipopata karibu ya Yeriko, mtu mmoja kipofu alikuwa ameketi kando ya njia, akiomba sadaka : aliposikia watu wapita kundi zima, akauliza ni neno gani hilo. Wakamweleza kwamba, Apitaye ni Yesu Mnazari. Akapiga ukelele, aikananga, Ewe Yesu Mwana wa Daudi, nirehemu ! Wale waliotangulia wakamkanya, wakamwambia anyamaze : akazidi sana kuinua sauti yake : Ewe Mwana wa Daudi, nirehemu ! Yesu akasimama, akaamuru aletwe kwake. Alipokwisha kumsongelea akamuuliza, akisema, Wataka nikufanyie nini ? Akamwambia, Bwana, nirejee kuona kwangu. Yesu akamwambia, Rejea kuona kwake mara : akamwandama, huku akimsifu Mungu. Na wenyeji wote walipoona neno lile walikuwa kumtukuzza Mwenyezi Mungu.

SIKU YA KWANZA YA SAUMU, IITWAYO JUMATANO YA IVU*Sala*

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, wewe huvichukii ulivyovifanya hata kimoja, ndiwe mwenye kumsamehe makosa yake kila mtu anayetubia ; utuumbie

ndani yetu miyo mipya iliysagika, ili kwa kuyalilia makosa yetu kama ilivyopasa na kuukiri huuudhaifu wetu, tupate kwako wewe, Mungu mwenye rehema zote, msamaha na maondoleo yaliyotimia ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Sala hii husomwa kila siku muda wote wa Saumu, baada ya Sala iliyohusika na siku hiyo.

Badala ya Waraka. Yoeli 2. 12-17

GEUKENI mnilekee mimi, asema Yehova, kwa miyo Gyenu yote, na kwa kufunga, na kwa kulia, na kwa kuombolea : nanyi rarueni miyo yenu, msirarue mavao yenu, nanyi rejeeni kwa Yehova Mungu wenu : kwa kuwa yeze ni mwenye neema na huruma : si mwepesi kwa hasira, ni mwinci wa rehema : naye hujutia lile shari. Ni nani ajuaye kwamba hatageuka na kujuta, na kutuachia baraka nyuma yake, hata sadaka ya unga na sadaka ya kinywiwa kwa Yehova Mungu wenu ? Pigeni tarumbeta katika Zayuni, itakaseni saumu, pigeni mbiu ya mkutano wa makini : wakusanyeni hao watu pamoja, utakaseni huo mkutano, wakusanyeni pamoja hao wazee, wakutanisheni hao watoto, na hao wenye kuamwa matiti : huyo bwana-arusi na atoke katika chumba chake, na huyo biki-arusi naye na atoke katika chumba chake cha ndani. Hao makuhani, hao watumishi wa Yehova, na walie kati ya hiyo baraza na hayo madhabahu, nao na waserme, Uwasamehe watu wako, ewe Yehova, nawe usitoe urithi wako uwe kutukanwa, hata hao mataifa watawale juu yao : kwa maana gani watasema wao kati ya hayo makabila ya watu, Je, Mungu wao yu wapi ?

Injili. Mathayo 6. 16-21

NA mtakapofunga, msikaushe nyuso zenu kama wale wanafiki : kwani wao hupotoa nyuso zao wapate kuonekana na watu kuwa wao wafunga. Ni kweli nawaa-mbia, wansha kupokea ujira wao. Ila wewe ukifunga, ujipake mafuta kichwani mwako, unawe na uso wako : usije ukaonekana na watu kuwa wafunga, uonekane kwa Babaako aliye sirini ; na Babaako aonaye sirini atakulipa

dhahiri. Msiweke hazina zenu za akiba juu ya nchi, napo ndipo nondo na kutu viharibupo, na wevi hutoboa na kuiba ; ila hazina zenu za akiba ziwekeni mbinguni, pasi-poharibika kitu kwa nondo wala kutu, na wevi hawatoboi wala hawaibi. Kwani palipo na akiba yako na moyo wako huwa papo.

JUMAPILI YA KWANZA KATIKA SAUMU

Sala

EWE Bwana, wewe kwa ajili yetu ulifunga michana E arrobaini na masiku yake ; utupe sisi neema ya rohoni, ili kwamba kadiri tutakayo kujinyima mambo yetu wenye miili yetu itawaliwe na Roho wako, tukufuate wewe daima, kwa hivi ututiavyo bidii ya uchaji-wa-Mungu katika haki na utakatifu wa kweli, ili tuwe wenye kukuhestimu na kukutukuza wewe, unayeishi na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja milele. *Amina.*

Waraka. 2 Wakorintho 6. 1-10

NASI kwa kufanya kazi *pamoja naye twawasihi* ninyi nanyi msiipokee neema ya Mwenyezi Mungu bure (kwani anena, Nilikusikiza wakati uliokubaliwa, na katika siku ya wokofu nilikusaidia ; huu ndio, wakati uliokubaliwa ni sasa : hii ndio, siku ya wokofu ni sasa) : isiye kuleta sababu yoyote ya kukunguwaza katika neno lolote, ili kwamba utumishi wetu usilaumiwe ; lakini kwa kujipatia wenye ukubali katika mambo yote kama watumishi wa Mungu, katika subira nyingi, katika mateso, katika shida, katika taabu, katika mapigo, katika kufungwa gerezani, katika mishindo-shindo, katika taabu za kazi, katika kukesha, katika kufunga ; katika kutakaswa, katika ujuzi, katika uvumilivu, katika kutendea mema, katika Roho Mtakatifu, katika mapenzi yasiyo na unafiki, katika neno la kweli, katika uwezo wa Mungu ; kwa silaha za haki upande wa mkonono wa kulia na upande wa mkonono wa kushoto, kwa utukufu na kwa kukosa heshima, kwa kusingiziwa na kwa kusifiwa ; kama wenye kupoteza, nasi tu

wasema-kweli ; kama tusiojulikana, nasi twafahamiwa sana ; kama tufao, kumbe tu hai ; kama turudiwao, nasi hatuuawi ; kama tu wenye majonzi, ila ni kufurahi daima ; kama tu maskini, ila ni kuwatahirisha wengi ; kama tusiokuwa na kitu, ila tu wenye vitu vyote.

Injili. Mathayo 4. 1-11

NDIPO hapo Yesu akachukuliwa barani na Roho Mtakatifu, kwenda kujaribiwa na Ibilisi. Alipo-kwisha kufunga michana arobaini na masiku yake, mwisho wake akaumwa na njaa. Akaenda mjaribu akamwambia, Kwamba ndiwe Mwana wa Mwenyezi Mungu, yaambie mawe haya yawe mikate. Naye akamjibu akamwambia, Imeandikwa, Mwana wa Adamu hataishi kwa mkate tu, *ataishi* kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mwenyezi Mungu. Ndipo hapo akamchukua yule Ibilisi akaenda naye hata Mji Mtakatifu, akamweka juu ya kilele cha hekalu *kilicho kikuu*. Akamwambia, Kwamba ndiwe Mwana wa Mwenyezi Mungu, jitupe chini, kwani imeandikwa, Yeye atawaagiza malaika zake kwa ajili yako, kisha watakuinua kwa mikono yao, usije popote ukakunguwaza mguu wako katika jiwe. Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako. Yule Ibilisi akamchukua tena, akaenda naye katika kilima kirefu sana ; akamwonyesha ufalme pia wote wa ulimwengu na utukufu wake huo, akamwambia, Mambo yale yote nitakupa utakaponisujudia na kuniabudu. Ndipo hapo Yesu akamwambia, Enda zako Shetani ; kwani imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umtumikie yeye pekee. Ndipo Ibilisi alipomwacha : nao, hao ndio, malaika wakaenda pale wakamtumikia.

JUMAPILI YA PILI KATIKA SAUMU

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe watuona ya kwamba kwa nafsi zetu hatuna nguvu za kujipa msaada wenye ; utulinde, nije katika miili yetu, na ndani katika roho zetu ; tupate kulindwa na mashaka yote yenye

kuukuta mwili, na mawazo maovu yote yenye kupigana na roho na kuidhuru ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Wathesalonike 4. 1-8

MWISHO basi, ndugu zetu, twawaomba na kuwataka ninyi katika Bwana Yesu, ili kwamba kama mlivypo-pokea kwetu jinsi iwapasavyo kwenenda na kumpendeza Mungu, vivile kama mwendavyo, mpate kuzidi sana. Kwani mwajua ni maagizo gani tuliyowapa kwa njia ya Bwana Yesu. Kwani atakalo Mwenyezi Mungu ni huo utakatifu wenu, mijepushe na uasherati ninyi ; kila mtu kwenu na ajue kumiiki nafsi yake mwenyeewe katika utakatifu na heshima, si katika shauku na tamaa, kama vile hao *watu wa* hao mataifa wasiomjua Mwenyezi Mungu : mtu asimdhilimu wala kumdaganya nduguye katika jambo hilo ; kwa sababu Bwana ni mpatalizi katika mambo haya yote ; vivile kama tuliyotangulia kuwaonya na kushuhudia. Kwani Mwenyezi Mungu hakutuita kwa uchafu, lakini ni katika utakatifu. Basi hivi yeye akataaye hamkatai binadamu, lakini *humkataa* Mwenyezi Mungu, yeye awapaye ninyi Roho wake Mtakatifu.

Injili. Mathayo 15. 21-28

YESU akatoka humo, akaenda kando katika pande za Turo na Sidoni. Naye, huyo ndiye, mwanamke wa Kikanani, naye ni mtu wa katika mipaka ile, akatokea akampigia kelele, yuanena, Nirehemu Bwana, Mwana wa Daudi ; binti yangu yuateswa sana na pepo. Asimjibu neno. Wakamwendea wanafunzi wake wakamsih, wanena, Mpe ruhusa mwanamke, kwa kuwa atufuata huku akitupigia kelele. Akajibu akanena, Sikutumwa ila kwa kondoo wapotevu wa nyumba ya Isiraeli. Naye *mwanamke* akamwendea, ikawa kumsujudia, yuanena, Bwana, nisaidie. Akajibu akamwambia, Si vyema kuutwaa mkate wao wana kuwatupia mbwa. Akanena, Ndiyo Bwana, kwani hata mbwa hula katika makombo yaangukayo

mezani pa bwana zao. Ndipo hapo Yesu akamjibu akamwambia, Ewe mwanamke, imani yako ni kubwa : na yawe kwako kama utakavyo. Akapoaa binti yake kwa saa ile ile.

JUMAPILI YA TATU KATIKA SAUMU

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, twakuomba uyakubali haya maombi yetu watu wako tukuombayo kwa moyo, nawe utunyoshee mkonzo wa kuurme wako wa enzi, ututete na kutukinga na adui zetu wawao wote ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 5. 1-14

BASI iweni wafuasi wa Mwenyezi Mungu, kama watoto wapendwao : tena mwenende katika mapenzi, vivile kama Kristo naye alivyowapenda ninyi, na kutoa nafsi yake kwa ajili yetu, kipawa na sadaka ya Mungu iwe harufu ya manukato. Ila uzinifu na uchafu wote na kutamani-tamani na visitajwe kati yenu kabisa, vivile kama viwasavyo watakatifu : wala ulanifu, wala mazungumzo ya upuzi, wala ubishi, mambo ambayo hayapasi : lakini afadhali shukrani. Kwani mwajua neno hili hakikahakika, ya kwamba mwasherati, wala mtu mchafu, wala mwenye kutamani-tamani, ndiye mwenye kuabudu sanamu, hana urithi ulio wote katika ufalme wa Kristo na wa Mungu. Na mtu asiwadanganye kwa maneno ya ubatili : kwani kwa sababu ya mambo hayo hasira ya Mwenyezi Mungu huwafikilia wana wa maasia. Basi isiwe ninyi kuwa washirika pamoja nao : kwani hapo kwanza mlikuwa mu giza, ila sasa mu mwanga katika Bwana : enendeni kama watoto wa mwanga (kwani tunda la mwanga ni katika wema wote na haki na kweli), huku mkihakikisha kile kipendezacho sana kwa Bwana : tena msiwe na ushirika na zile kazi za giza zisizo na matunda *mema*, ila afadhali ni kuzinenea : kwani ni aibu hata kuyanena mambo hayo yafanywayo na wao kwa siri. Ila mambo yote hapo yatakopari piwa yadhihirishwa na

mwanga : kwani kila kitu kilichofunuliwa ni mwanga. Kwa sababu hii asema, Amka ewe uliyelala, kafufuke, ukatoke kwa wafu, na Kristo atakuletea mwanga.

Injili. Luka 11. 14-28

YESU alikuwa akimtoa pepo, *naye ni pepo* bubu, ikawa akiisha kutoka yule pepo akasema yule aliyekuwa bubu, wale makutano *ya watu* wakastajabu. Wengine wakasema, Ni kwa Beelizebuli, mkubwa wa pepo, mtu huyo awatoavyo watu pepo. Wengine wakamjaribu-jaribu wakamtaka ishara itoke mbinguni. Naye akajua mawazo yao akawaambia, Kila ufalme uliogawanyikana juu ya nafsi yake huvunjwa, na kila nyumba iliyogawanyikana huanguka. Basi na Shetani naye kwamba amegawanyikana juu ya nafsi yake, utapata wapi kusimama ule ufalme wake ? kwa kuwa ninyi mwasema kwamba ni kwa Beelizebuli niwatoavyo watu pepo. Basi kwamba mimi nawatoa pepo kwa Beelizebuli, je, wana wenu wawatoa kwa nani ? Kwa ajili ya hayo hao watakuwa waamuzi wenu. Lakini niwatoavyo pepo mimi, kwamba ni kwa chanda chake Mwenyezi Mungu, ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia ! Mtu mwenye nguvu aliyejifunga silaha zake akikaa hali ya kulinda nyumba yake, vile vitu vyake vi salama ; lakini atakopokwendewa na mwenziwe aliye na nguvu zaidi ya yeye, na kumshinda, humnyang'anya zile silaha zake alizokuwa akitumaini, akagawanya na vyombo vyake. Asiyekuwa hali moja nami, yu kinyume changu, na asiyekusanya pamoja nami hutawanya. Wakati atokwapo mtu na roho mchafu hupita mwahali msimo maji, yuatafuta pa kupumzika ; akiona pahali hakuna, husema, Nitairejea ile nyumba yangu niliyotoka. Hata akifika, akaiona imefagiwa imepambwa : ndipo akaenda akawatwaa wenziwe maroho saba waovu kuliko yeye, wakaingia wakakaa humo, ikawa mtu yule hali yake ya mwisho ni mbaya kuliko ya kwanza. Ikawa katika kusema kwake maneno haya, mwanamke mmoja wa katika mukutano akainua sauti yake, akamwambia, Yana heri matumbo yaliyokuzaa wewe, na matiti uliyoamwa.

Naye akasema, Afadhalii, wana heri wasikiao neno lake
Mwenyezi Mungu na kulishika.

JUMAPILI YA NNE KATIKA SAUMU
Sala

EWE Mwenyezi Mungu, ukubali, twakuomba, ya kwamba tungawa twafaa mno sisi kuadhibiwa kwa maovu yetu, lakini kwa kutulizwa mioyo yetu kwa neema yako, tupate kuponywa kwa rehema zako ; kwa Bwana wetu Mwokozi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

Waraka. Wagalatia 4. 21-31

NIAMBIENI, ninyi mtakao kuwa chini ya sheria, je, hamwisikizi ile sheria ? Kwani imeandikwa ya kuwa Iburahimu alikuwa na wana wawili wanawaume, mmoja alizaliwa na suria, na wa pili alizaliwa na mwanamke wa kiungwana. Pamoja na hayo, huyo aliyezaliwa na huyo suria alizaliwa kwa jinsi ya mwili, na huyo aliyezaliwa na huyo mwanamke wa kiungwana alizaliwa kwa njia ya ahadi. Mambo hayo ni kitendawili : kwani *wanawake* hao *wameonyeshwa* kuwa maagano mawili : moja litokalo mlima wa Sinai, lizaalo wana kwa utumwa, ambalo ni Hagari. Na huyo Hagari ni mlima Sinai katika Bara-Arabu, uliolingamana na Yerusalemu wa sasa : kwani uko utumwani pamoja na wanawe. Ila Yerusalemu ulio juu ni huru, nao ndio mamaetu. Kwani imeandikwa, Ufurahi, ewe uliye tasa usiyezaa wana ; uteo sauti ukapige ukelele wewe usiyeona uchungu wa uzazi : kwa kuwa wana wa huyo aliye pekee huwa wengi zaidi ya huyo aliye na mumewe. Basi, ndugu zangu, sisi tu wana wa ahadi sawasawa na Isaka. Lakini kama wakati ule huyo aliyezaliwa kwa jinsi ya mwili alivyomuudhi huyo *aliyezaliwa* kwa jinsi ya Roho, hata sasa ni vivyo. Lakini maandiko yasema nini ? Mfukuze huyo suria na mwanawe pia : kwani mwana wa suria hatarithi pamoja na mwana wa mwanamke wa kiungwana. Ndipo, ndugu zangu, sisi hatu wana wa suria, lakini tu wana wa mwanamke wa kiungwana.

Injili. Yohana 6. 1-14

BAADA ya haya akaondoka Yesu akaenda ng'ambu ya bahari ya Galilaya, nayo ndiyo bahari ya Tiberia. Akaandamwa na watu makundi-makundi, kwa kuwa walikuwa waziona ishara awafanyiato wenyewe magonjwa. Akakwea kilimani Yesu, akaketi huko pamoja na wana-funzi wake. Na Pasaka ihikuwa karibu, nayo ndiyo idi yao Mayahudi. Basi Yesu akainua macho yake, hata alipowaona ni wengi sana watu wamjiao, akamwambia Filipu, Tukanunue wapi mikate, hawa wapate kula ? Nalo alilineni kwa kumjaribu, kwani aliyajua mwenyewe atakayokuja kuyafanya. Filipu akamjibu, mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi kila mmoja wao atwae kidogo. Mimoja katika wanafunzi wake, Andarea, nduguye Simoni Petero, akamwambia, Hapa pana kijana mmoja, yuna mikate mitano ya shairi, na samaki wadogo wawili ; lakini ni kitu gani hicho, cha kuwatoshwa watu wengi hivi ? Yesu akasema, Watengezeni watu waketi *nchi*. Napo palikuwa na majani mengi mabichi pahali hapo. Basi wakaketi, watu waume hesabu yao wapata elfu tano. Basi Yesu akaitwaa mikate, hata aliposhukuru akawapa wanafunzi wake nao *wakawagawanya* walioketi, na katika wale samaki vilevile, kadiri ya waliviyotaka. Hata wali-pokwisha kushiba, akawaambia wanafunzi wake, Kusanyeni makombo yaliyosalia, kisipotee kitu. Basi wakayusanya ; wakajaza vikapu kumi na vivili, makombo yatokayo katika mikate mitano ya shairi, yamewasalia waliokula. Basi wale watu walipoona ishara aliyoifanya, wakasema, Huyu ndiye kweli nabii ajaye ulimwenguni.

JUMAPILI YA TANO YA SAUMU

Sala

TWAKUOMBA, ewe Mwenyezi Mungu, uwaangalie kwa rehema hawa watu wako ; ili kwamba wapate kutawaliwa na wewe kwa wema wako mwingi, na kuwekwa salama daima, miili yao na roho zao ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wahibirania 9. 11-15

ILA Kristo akiisha kuja, kuhani mkuu wa hayo mambo imema yatakayokuja, kwa njia ya lile hema lililo bora zaidi na ukamilifu zaidi, lisilofanywa kwa mikono, maana, si la uumbaji huu, wala kwa njia ya damu ya mbuzi na wana wa ng'ombe, ila kwa njia ya damu yake mwenyewe, alingia mara moja tu katika pahali patakatifu, akiisha kupata makombozi ya milele. Kwani ikiwa damu ya mbuzi na ng'ombe, na ivu la mtamba kunyonyizwa juu ya hao walioitwa najisi, kutakasa hata kwa kuusafi mwili : ni zaidi kiasi gani hiyo damu ya Kristo, ambaye, kwa njia ya Roho wa milele, alitoa nafsi yake pasipo laamu na kumpa Mwenyezi Mungu, itatakasa nia zenu kuziacha kazi zilizo maiti, hata kumtumikia Mungu aliye hai ? Kwa ajili ya hayo, ye ye ni mwene kuleta agano jipya, yakiisha kuwako yale mauti kwa ukombozi wa makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza, hao walioitwa waipate ahadi ya huo urithi wa milele.

Injili. Yohana 8. 46-59

YESU alisema, Ni nani kwenu anishuhudiaye kwa dhambi ? Kwamba nainena kweli, ni nini kutoniamini ninyi ? Aliye katika Mwenyezi Mungu huyasikia maneno yake Mwenyezi Mungu. Ninyi kwa ajili ya neno hili hamyasikii, kwa kuwa hamu katika Mwenyezi Mungu. Mayahudi wakamjibu, wakamwambia, Hatukusema vyema sisi, U Msamaria, nawe una pepo ? Yesu akawajibu, Mimi sina pepo ; mimi namheshimu Babaangu, nanyi mwaniyunja heshima. Nami utukufu wangu siutafuti. Yuko autafutaye, na kuhukumu. Ni kweli, ni kweli nawaambia, Mtu atakaposhika neno langu, haoni mauti milele. Mayahudi wakamwambia : Sasa tumekutambua kuwa una pepo. Iburahimu amekufa, na manabii *wamekufa*, nawe wanena, Mtu atakaposhika neno langu haonji mauti milele. Wewe u mkubwa kuliko babaetu Iburahimu ? naye alikuwa, na manabii walikuwa. Wajifanya u nani ? Yesu akawajibu, Mimi nikwa najitukuzu mwenyewe, utukufu wangu si kitu. Yuko Babaangu,

ambaye mwasema kwamba ni Mungu wenu. Nanyi hamkumtambua ; ila mimi nimemjua. Nami nitakaposema simjui, nitakuwa mwongo, mfano wenu ninyi. Ila mimi nimemjua, na neno lake nalishika. Babaenu Iburahimu alifurahi kwa vile atakavyoiona siku yangu ; akaiona akafurahi. Basi Mayahudi wakamwambia, Hujawa mwana wa miaka hamsini, nawe umemwona Iburahimu ? Yesu akawaambia, Ni kweli, ni kweli nawaambia, Kwanza Iburahimu hajakuwako, mimi niko. Basi wakaokota mawe kutaka kumpiga, Yesu akajificha, akatoka hekaluni, naye akapita katikati yao akaenda zake.

JUMAPILI ITANGULIAYO MBELE YA IDI YA UFUFUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, wewe jinsi Euliviyowapenda wanadamu kwa mapenzi ya ndani sana, ulimtuma Yesu Kristo Mwanayo Mwokozi wetu, kuja kuutwaa mwili wetu, hata akapatikana na mauti msalabani ; ili kwamba wote walio katika mbegu ya kibinadamu wafuate kielelezo chake alichotupa cha unyenyekevu mkuu : ukubali kwa rehema ya kwamba sisi tupate kufuata kielelezo chake cha kuvumilia na kuwa washirika naye katika kufufuka kwake ; kwa ye ye Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wafilipi 2. 5-11

IWENI na nia ii hii ndani yenu iliyokuwa ndani ya Kristo Yesu nayo : ambaye ye ye alipokuwa katika sura za *mfano wa* Mungu, hakukuhesabu kufanywa sawa na Mungu kuwa ni jambo lenye kutamaniwa, lakini akifanya nafsi yake utupu, huku akiutwaa mfano wa mtumwa, akawa sawasawa na binadamu : kisha akionekana kuwa na umbo kama wa binadamu akainyenyekeza nafsi yake, akawa mwene kutee hata mauti, naam, hata mauti ya msalaba. Kwa ajili ya hayo Mwenyezi Mungu naye alimtukuzu sana, akampa jina hilo ambalo li juu kuliko kila jina : ili kwamba tipate kupigwa katika jina la Yesu kila

goti, la walioko mbinguni, na la walio nchi, na la walio chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Injili. Mathayo 27. 1-54

LIPOKUWA asubuhi, makuhani wakuu wote na walio Iwazee katika wale wenyeji wakafanya shauri katika Yesu, ili kumuua. Wakamfunga, wakaenda naye wakamtia kwa liwali Pilato. Ndipo hapo Yudas, yule mwenye kumsaliti, kumwona kwake kwamba amekwisha kuhukumiwa, akajuta, akavitwaa vile vipande thelathini vya fedha akavirudisha kwa makuhani wakuu na wazee : akanena, Nimekosa nilivyoisaliti damu isyo aili. Wao wakanena, Yatupasani sisii ? yaangalie wewe ! Naye akiisha kuvitupa vipande vya fedha katika hekalu akaondoka ; kisha akaenda akajisongoa. Makuhani wakuu wakavitwaa vipande vya fedha, wakanena, Si halali kuvitia katika kanzi ya Mungu, kwa vilivyokuwa ni kima cha damu. Waka-fanya shauri wakaenda wakalinunua shamba la mfinanzi kwa hivyo vipande, liwe pahali pa kuzika wageni. Ndipo shamba hilo jina lake likaitwa Shamba la Damu, hata hii siku ya leo. Ndipo hapo likatimia lile lilionenwa na nabii Yeremia, maneno haya, Kisha wakavitwaa vile vipande thelathini vya fedha, kima chake yule aliyetiwa kima, wana wa Israeli waliyemtia kima, wakavitoa kwa kunununa-shamba la mfinanzi, kama alivyonigiza Bwana. Naye Yesu alisimama mbele ya liwali. Liwali akamuulla, yuanena, Wewe ndiye mfalme wa Mayahudi ? Yesu akamwambia, Wewe wasema. Na kushtakiwa kwake na makuhani wakuu na wazee hakujibu lolote. Ndipo hapo Pilato akamwambia, Husiki ni mangapi wakushuhudiayo wewe ? Naye hakumjibu, hata kwa neno moja, hata ikawa kustaajabu mno yule liwali. Na zamani za idi hiyo liwali ilikuwa ni ada kwake kuwafungulia kundi la watu mfungwa mmoja wamtakaye. Na zamani hiyo walikuwa na infungwa mmoja ajulikanaye, aitwa Baraba. Basi walipokwisha kukutana Pilato akawauliza, Mwataka niwaachilie yupi mmoja : Baraba au Yesu aitwaye Kristo ? Kwani

alijua kwamba wamemtia kwake kwa husuda. Alipoketi yule Pilato katika ulili wa hukumu, mkewe akampelekea ujumbe, akasema, Huyo mtu wa haki usiwe na neno wewe naye, kwani leo nimcematikana na mambo mengi katika ndoto kwa ajili yake. Na wale makuhani wakuu na wazee wakawageuze nia wale makutano wapate kumtaka Baraba kwake, na Yesu wamwangamize. Liwali akawajibu akawaambia, Watu wawili hawa ni yupi mnayemtaka niwafungulie ? Wakamwambia, Baraba. Pilato na kuwaambia, Nimfanyeje basi Yesu aitwaye Kristo ? Wakamwambia, pia wote, Na asalibiwe ! Liwali akanena, Kwani, amefanya uovu gani ? Wao na kuzidi kupiga ukelele, wanena, Na asalibiwe ! Pilato alipojiona hafai lolote, ghasia yazidi kwendelea tu, akatwaa maji akanawa mikono yake mbele ya makutano, akasema, Mimi simo katika damu yake huyu mtu wa haki. Angalieni ninyi jambo hili. Wakamjibu wale wenyeji pia wote, wakanena, Damu yake na iwe juu yetu na wana wetu ! Ndipo hapo akawafungulia Baraba, akampiga Yesu mjledi, akawaachia apate kusalibiwa. Ndipo hapo askari zake liwali wakampokea Yesu wakamtia katika ukumbi wa nyumba ya liwali, wakamkusanyikia kikozi kizima ; wakamvua mavao yake wakamvika kitambi chekundi. Wakasuka taji ya miiba wakamvika kichwani, wakamtilia na mwanzi katika mkono wake wa kuume : ikawa kumpigia magoti huku wamchezea, na kunena, Salamu, Mfalme wa Mayahudi ! Kisha wakamtemea mate wakaushika ule mwanzi wakimpiga-piga kichwani ; hata wakiisha kumchezea, wakamvua kile kitambi wakamvika mavao yake, wakaenda naye wakamwongoza kwenda kumsalibu. Wa katika kutoka nje ya mji wakamwona mtu mmoja Mkurene, jina ake aitwa Simoni ; mtu huyu wakamtenza nguvu apate kumchukulia msalaba wake. Hata walipofika pahali pamoja jina lake paitwa Golgotha, maana yake jina hilo ni Pahali pa Bongo, wakampa divai imechanganywa na nyongo, apate kunywa ; alipoinonoja asikubali kunywa. Walipomsalibu wakagawanya nguo zake kwa kupiga kura : ili lipate kutimia lile lilionenwa na nabii, Wamegawanya mavao yangu, na nguo yangu wameipigia kura. Wakaketi

kumlinda pale pale. Wakatia na mashtaka yake juu ya kichwa chake, yameandikwa, HUYU NDIYE YESU, MFALME WA MAYAHUDI. Ndipo hapo ilikuwa kusalibiwa pamoja naye wevi wawili, mmoja upande wa mkono wake wa kulia, na mmoja upande wa mkono wake wa kushoto. Ikawa kumtukana watu wapitao njiani huku watukusa-tukusa vichwa vyao wakinena, Ewe ulivunjaye hekalu na kulibuni kwa siku tatu, jikoe mwenyewe. Kwamba ndiye *wewe* Mwanawe Mwenyezi Mungu, shuka huko uliko msalabani. Na wale makuhani wakuu *wakafanya kama tile*, *wakimfanya* dhihaka wao pamoja na wana-wa-vyuoni na wazee, wakinena, Aliokoa watu, mwenyewe hawezi kujiokoa. Mfalme wa Isiraeli mi yeye : na ashuke hivi sasa msalabani mwake, nasi tutaa-mini kwake. Aliamini kwa Mwenyezi Mungu : na amponye hivi sasa kwamba yu radhi naye ; kwani alisema, Mimi ni Mwanawe Mungu. Ikawa kumfyolea kama yale wale wevi nao, wale waliosalibiwa pamoja naye. Basi ilipofika saa ya sita kukafunga giza nchi nzima, ikaendelea hata saa ya tisa. Ilipopata saa ya tisa, Yesu akapiga ukelele kwa sauti kuu, anena, Elii, Elii, lama sabakithani ? maana yake, Mungu wangu, Mungu wangu, kwani wewe kuniacha ? Waliposikia wengine katika waliosimama pale, ilikuwa kunena, Amwita Elija. Mara akapiga mbio mmojawapo katika wao akaenda sifunji akaijaza siki na kuitia mwanzini, akawa kumnywesha. Wensiwe wakanena, Acha, na tutazame kwamba Elija yuaja kumwo-ko. Yesu akapiga ukelele tena kwa sauti kuu, kisha akitoa roho yake. Mara pazia ya hekalu ikapasuka pande mbili tokea juu hata chini, nchi ikatetema, miamba ikapasuka, makaburi yakafunuka yakawa wazi, na miili mingi ya watu watakatifu waliolala ikainuka ; wakatoka makaburini mwao baada ya kuinuka kwake *Bwana*, wakaingia ndani ya Mji Mtakatifu, wakawatokea wengi waziwazi. Akida wa askari mia, na waliokawapo naye, watu wamlindao Yesu, walipokiona kitetemo cha nchi na mambo yale yaliyokuwa, wakacha mno wakinena, Ni kweli huyu alikuwa ni Mwana wa Mwenyezi Mungu.

JUMATATU MBELE YA UFUFUO

Badala ya Waraka. Isaya 63. 1-19

Ni nani huyu ajaye kutoka Edomu, huyu mwenye mavao yenyе rangi nyekundu sana, atokaye Bozira ? huyu aliye na nguo zake za shani, huku akienda mbele katika wingi wa nguvu zake ? Ni mimi ninenaye katika haki, niliye na uwezo wa kuokoa. Je, nguo zako zimekuwa nyekundu kwa sababu gani, na kwani mavao yako kuwa kama mavao ya mtu akanyagaye kinu cha divai ? Mimi nimekanyaga kinu cha divai peke yangu, katika hao wenyeji hapakuwa na mtu pamoja nami ; naam, niliwakanyaga kwa hasira zangu, na kuwakanyagakanyaga sana kwa ghadhabu zangu za moto-moto ; na hiyo damu-ya-maisha yao imenirukia katika mavao yangu, nami nimeziharibu nguo zangu zote. Kwa kuwa nilikuwa na hiyo siku ya kisasi moyoni mwangu, tena mwaka wa hao wakombolewa wangu umefika. Nami nikaangalia, napo hapakuwa na mtu mwenye kusaidia ; nikashangaa kwa kuwa hakuna mwenye kuhimili : kwa sababu hii mkono wangu mwenyewe uknipatia wokofu ; na ghadhabu zangu za moto-moto ndizo zilizonihiimili. Nami nikawakanyaga hao wenyeji kwa hasira zangu, na kuwalevya kwa ghadhabu zangu za moto-moto, nami nikaimwaga damu-ya-maisha yao juu ya nchi. Nitayataja mambo ya ihisani ya Yehova, na sifa za Yehova, mfano wa hayo yote aliyotutendea ; na huo wingi wa wema kwa nyumba ya Isiraeli, aliowatendea mfano wa rehemza zake, na mfano wa wingi wa mambo yake ya ihisani. Kwa kuwa alisema, Hakika yao hao ni watu wangu, ni wana wasiotenda uwongo : basi akawa mwokozi wao. Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na huyo malaika wa uso wake akawaokoa : katika mapenzi yake na huruma zake akawakomboa ; naye akawainua na kuwachukua siku zote za kale. Ila wao wakaasi na kuisumbua roho yake takatifu : basi alibadilika kuwa adui yao, naye mwenyewe akawapiga vita. Hapo ndipo alipozikumbuka siku za kale, huyo Musa, na hao watu wake, *akinena*, Yu wapi huyo aliywakweza kuwatoa katika bahari pamoja na

mchunga wa kundi lake? Yu wapi ye ye aliyeitia roho yake takatifu katikati yao? Yeye aliyeuendesha mkonono wake wenye utukufu kuumeni kwa Musa? yeye aliye-yapasua hayo maji mbele yao, apate kufanyia nafsi yake jina la milele? yeye aliyeawendesha vinani, mfano wa farasi barani, wasikunguwa? Kama ng'ombe watere-mkao kwenda bondeni, roho wa Yehova akawapumzisha: ni vivyo uliviyowaongoza watu wako upate kufanyia nafsi yako jina lenye utukufu. Angalia chini tokea mbinguni uliko ukaone katika makazi ya utakatifu wako na utukufu wako: u wapi vivu wako na vitendo vyako vya ubora vi wapi? shauku za moyo wako na rehema zako zazuiliwa zisinifilikie mimi. Kwa kuwa wewe u babaetu, ajapokuwa huyo Iburahimu hatujui, na Israeli hatukubali; wewe, ewe Yehova, u babaetu: mkombozi wetu tangu milele, ni jina lako. Ewe Yehova, watukosesha katika njia zako kwa sababu gani, na kufanya miyo yetu kuwa mizito katika kicho chako? Rejea kwa ajili ya watumishi wako, hayo makabila ya urithi wako. Watu wako watakatifu waliumilki muda mchache tu; adui zako wame-pakanyaga-kanya pahali patakatifu pako. Tumekuwa mfano wa hao ambao hukutawala juu yao popote; mfano wa hao ambao hawakuitwa kwa jina lako.

Injili. Mariko 14. 1-72

HATA baada ya siku mbili ilikuwa idi ya Pasaka, na *Mikate* isiyo chachu; makuhani wakuu na wana-wavyoni wakitafuta njia ya kumshika kwa hila, wapate kumuua: kwani walisema, Tusimshike kwa siku ya idi, kisije kikatukia kishindo cha wenyeji. Alipokuwa Bethania katika nyumba ya Simoni mkomona, naye ameketi chakulani, akaja mwanamke yuna chupa njema, mna manukato yenye thamani: akaivunja chupa akamwinikia kichwani mwake. Palikuwa na wengine waliochukiwa nafsi mwao: wanena, Kwani kuyapoteza manukato haya? Kwa kuwa manukato haya humkini kuuzwa kwa zaidi ya robo mia tatu, wakapewa maskini. Ikawa kumka-sirikia yule mwanamke. Yesu akasema, Mwacheni huyu:

ni nini kumuudhi? Amenifanyia mimi kazi njema. Kwani maskini mnao siku zote pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwafanyia vyema; ila mimi hamnamini siku zote. Amefanya aliyo nayo; ameshika mbele kuutia mwili wangu manukato, kwa kuutengezea maziko. Ni kweli nawaambia, Kila patakohubiriwa Injili, katika ulimwengu wote, litasemwa na hili alilotenda huyu, uwe ukumbusho' wake. Yule Yudas Mwiskariota, naye ni mmoja katika wale kumi na wawili, akaondoka akaenda kwa makuhani wakuu, apate kumtia mikononi mwao. Waliposikia wakafurahi, wakaagana naye kumpa fedha, akatafuta muda utakaomwafiki kumtia mikononi mwao. Hata kwa siku ya kwanza ya mikate isiyo chachu, wakati wa kumchinja kwao Pasaka, wanafunzi wake wakamuuliza, Wataka tuende tukatengeze pahali gani, ukamlie Pasaka? Akatuma wawili katika wanafunzi wake, akawaambia, Endeni mjini, mtatokewa na mtu mbele yenu, yuna mtungi wa maji ameuchukua, mwandameni huyo; hata atakapoingia pahali, mwambieni mwenye nyumba, Bwana anena, Ki wapi chumba changu cha kulia, nikamlie Pasaka pamoja na wanafunzi wangu? Naye mwenyewe atawaonyesha ghorofa kubwa, imetandikwa tayari; basi tutengezeen humo. Wakatoka wale wanafunzi, wakaenda wakaingia mjini, wakaona vivile kama alivyowaambia, wakamtengeza Pasaka. Hata ilipoingia jioni akaenda pamoja na wale kumi na wawili. Kisha walipokaa chakulani wakila chakula, Yesu akanena, Ni kweli nawaambia, ya kwamba mmoja wenu ninyi atanisaliti, mtu alaye nami. Wakaanza kuingiwa na machungu, na kumuuliza mmoja mmoja, Je, ni mimi? Naye akajibu, akawaambia, Ni mmoja katika hawa kumi na wawili, nitu mwenye kuchovya pamoja nami sahanini. Kwa kuwa huyu Mwana wa binadamu naye yuaenenda, vivile kama alivyoandikiwa; ila ole wake mtu yule, Mwana wa binadamu atakayesalitiwa kwake; ingekuwa vyema kwake, kwamba hakuzaliwa mtu yule. Na walipokuwa wakila, akautwaa mikate akaubarikia akawapa; akanena, Twaei, mle, huu ndio mwili wangu. Akatwaa na kikombe, aliposhukuru akawapa, wakaki-

nywea pia wote. Akawaambia, Hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagwayo kwa ajili ya wengi. Ni kweli nawaambia, sinywi tena kamwe katika uzao wa mzabibu hata siku nitakayounywa uli mpya katika ufalme wa Mungu. Na wakiisha kuimba zaburi wakatoka wakaenda kilima cha Mizeituni. Akawaambia Yesu ya kwamba, Nyote mtakunguwazwa kwangu mimi usiku wa leo, kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungu, kondoo watatawanyikana. Lakini baada ya kuinuka kwangu nitawatangulia kwenda Galilaya. Yule Petero akamwambia, Na wote wajapokunguwazwa, lakini mimi sikunguwazwi. Yesu akamwambia, Ni kweli nakuambia ya kwamba wewe, huu usiku wa leo, mbele ya jimbi kuwika mara mbili, utanikana mara tatu. Naye akazidi sana kusema, Nijapolazimishwa kufa pamoja nawe, lakini sikukani kamwe. Na wale wakanena vivyo, pia wote. Wakafika pahali pakiitwa jina lake Gethiseman: akawaambia wanafunzi wake, Ketini hapa, hata nisali. Akamtwaa Petero na Yakobo na Yohana, akaenda nao, akaanza kufadhaika sana na kusumbuka mno. Akawaambia, Nina huzuni mno moyo wangu, kukaribia mauti; kaeni hapa muwe macho. Akaenda mbele punde, ikawa kuanguka nchi, naye akiomba kwamba saa hii imwondokce, ikiwezekana, yuanena, Aba, Baba, mambo yote yawezekana kwako; kiondoe kwangu kikombe hiki; lakini yasiye nipayendayo mimi, na yawe upendayo wewe. Kisha akaja akawaona wamelala usingizi; akamuuliza Petero, Je, Simoni, umelala? hukuweza kuwa macho saa moja? Iwени macho mwombe, ili kwamba msingie kujaribiwani; hii roho hakika yake i tayari, lakini mwili ni mnyonge. Akaondoka pale tena akaenda akaomba kwa kunena maneno yale yale. Akaja tena akawaona wamelala, kwani macho yao yalikuwa mazito, hawajui la kumjibu. Akaja mara ya tatu, akawaambia, Sasa laleni, mpumzike: yatosha; hiyo saa insha kufika. Huyu Mwana wa binadamu yuatiwa mikononi mwa wenye dhambi. Ondokeni, tuende. Huyu ndiye, amekaribia anisalitiye. Mara hiyo, mwenyewe akali akinena, akatokea Yudas, naye ni mmoja katika wale kumi na wawili, yuna mkutano

mkubwa pamoja naye, wenye panga na fimbo, watoka kwa makuhani wakuu na wana-wa-vyuoni na wazee. Naye yule amsalitiye alikuwa amewapa dalili, akawaambia, Nitakayembusu, huyo ndiye. Mshikeni mwende naye salama. Akiisha kufika mara akamwendea, yuanena, Ewe Mwalimu! akambusu. Wakampelekea mikono yao wakamshika. Na mmoja katika wale waliosimama karibu akaufuta upanga wake akamtema mtunwawe kuhani mkuu, akamkata sikio. Yesu akawajibu, akawaambia, Je, mmetokea kama mmatafutao mwivi, na mapanga na magongo, kunishika mimi? Michana yote nilikuwa kwenu katika hekalu nikifunza, msinishike. Ila haya yamekuwa yapate kutimizwa maandiko. Wakamwacha wote, wakakimbia. Ikawa hirimu mmoja, kumfuata, amejitanda nguo ya katani, *mwili wake u tupu*; wakamshika. Naye akiacha kitambaa cha katani, akawakimbia tuputupu. Wakaenda naye Yesu kwa kuhani mkuu: wakamkutanikia makuhani wakuu na wazee na wana-wa-vyuoni pia wote. Na Petero alimfuata kwa mbali hata mle ndani, katika ua wa kuhani mkuu, naye alikuwa amekaa pamoja na wangojezi, yuaota moto mwangani. Na makuhani wakuu, na baraza nzima, walikuwa kumtafutia ushuhuda juu yake Yesu, kutaka kumuua; wasipate. Kwani ilikuwa wengi kushuhudia uwongo kwake, wala usipatane ushuhuda wao. Kisha wakasimama wengine wakishuhudia uwongo kwake, wakinena, Sisi tumensikia yuanena, ya kwamba, Mimi nitalitangua hekalu hili lililofanywa kwa mikono, nami kwa siku tatu nitajenga la pili lisilofanywa kwa mikono. Wala kwa haya haukupatana ule ushuhuda wao. Yule kuhani mkuu akasimama katikati, akamuuliza Yesu, yuanena, Je, hutujibu lolote? ni makosa gani wakushuhudiayo watu hawa? Naye alikuwa ananyamaza, asijibu kwa lolote. Ikawa yule kuhani mkuu kumuuliza mara ya pili; akamuuliza, Wewe ndiye Kristo, mwanaawe Mwenye-baraka? Na Yesu akanena, Mimi ndiye: nanyi mtamwona Mwana wa binadamu ameketi upande wa mikono wa kuume wa enzi, yuaja pamoja na mawingu ya mbinguni. Na yule kuhani mkuu akararua mayao

yake, akanena, Tuna haja gani tena ya mashahidi ? Mmeyasikia matukano yake. Je, mwaonaje ? • Na waliopo wote wakamhukumu kupasa kuuawa. Wakaanza wengine kumtemea mate, na kumfumba uso wake, na kumpiga makofi na kumwambia, Tabiri ; na wale wangojezi nao wakampokea kwa kumpiga makofi. Hata alipokuwa unani Petero pale chini, akaja mmoja katika vijakazi vya kuhanii mkuu ; alipomwona yule Petero yuaota moto akamtulizia macho, akamwambia, Nawe ulikuwa pamoja na Mnazari yule, *maana*, Yesu. Akaana, akanena, Siyajui mwenyewe wala siyatambui uyanenayo wewe. Akatoka nje langoni. Jimbi likawika. Yule kijakazi akamwona, akaanza mara ya pili kuwaambia waliosimama karibu, ya kwamba, Huyu ni katika wao. Naye ikawa kukana mara ya pili. Hata baadaye punde ikawa kumwambia tena yule Petero wale waliosimama karibu, Ni kweli wewe u katika wao ; kwani nawe u mtu wa Kigalilaya, na lugha yako yaonyesha hivyo. Naye akaanza kuapiza na kuapa, Mimi simjui mtu huyu mnayemtaja. Mara hiyo likawika jimbi la pili.

JUMANNE MBELE YA UFUFUO

Badala ya Waraka, Isaya 50. 5-11

YEYE Yehova Mwenyezi Mungu amenifunua sikio langu, nami sikuwa mwasi, wala sikurudi nyuma. Niliwapa maungo yangu hao wenye kupiga, na machavu yangu *niliwasongezea* hao waliozing'oa ndevu zangu : sikuficha uso wangu katika kuaibishwa na kutemewa mate. Kwa kuwa ye ye Yehova Mwenyezi Mungu atanisaidia ; kwa sababu hii sikutahayari : basi nimeweka uso wangu kama jiwe gumu, nami najua ya kwamba sitapatikana na aibu. Yeye anipaye haki yu karibu ; ni nani atakayeteta nami ? na tuisimame pamoja : ni nani aliye mwenyewe hukumu yangu ? na anikaribie. Angalia, Yehova Mwenyezi Mungu atanisaidia ; ni nani atakayenihukumu kuwa ni mkosa ? angalia, hao wote watachakaa kama vile uvao ; na nondo atawala. Ni nani kati yenu amchaye Yehova, mwenyewe kuitii sauti ya mtumishi wake ? ajapokuwa yuaenenda gizani, naye hana mwanga, na alitumaini jina

la Yehova, na kumtegemea Mwenyezi Mungu wake. Angalieni, enyi nyote mwashao moto, ninyi wenye kuji-zongo-zonga vyenge vya moto mliviyowasha : haya, enendeni katika mwali wa moto wenu, na kati ya vile vyenge vya moto mliviyowasha. Haya mtayapata mkononi mwangu, nanyi mtalala nchi kwa huzuni.

Injili. Mariko 15. 1-39

PAPO hapo alfajiri wakafanya mashauri wale makuhani wakuu, pamoja na wazee na wana-wa-vyuoni na baraza nzima, wakamfunga Yesu, wakamchukua wakaenda naye wakamtia mikononi mwa Pilato. Pilato akamuuliza, Je, wewe ndiye mfalme wa Mayahudi ? Naye akamjibu akamwambia, Wewe wanena. Ikawa makuhani wakuu kumshtaki mambo mengi : asijibu neno lolote. Naye Pilato akamuuliza mara ya pili, yuanena, Hujibu lolote ? Angalia yalivyo mengi wakushtakiyo ! Wala hakujibu tena Yesu kwa lolote, hata Pilato akastaajabu. Na zamani za idi ilikuwa ye ye kuwafungulia mfungwa mmoja, wamtakaye. Basi alikuwako mtu mmoja jina lake aitwa Baraba, amefungwa pamoja na wale waliofanya fitina, nao ni watu ambao kwamba katika ile fitina wameua watu. Wakakwea juu lile kundi la watu, wakaanza kupiga ukelele na kutaka awafanyie kama awafanyiavyo daima. Yule Pilato akawajibu, anena, Mwataka niwafungulie Mfalmie wa Mayahudi ? Kwani amejua ya kuwa ni kwa husuda makuhani wakuu walivyomtia mikononi mwake. Na wale makuhani wakuu wakautukusa-tukusa mkutano, *wakiwaambia*, Ni afadhalii awafungulie Baraba. Yule Pilato akawajibu mara ya pili, akawaambia, Nimfanyeje basi huyu mnayemwita Mfalmie wa Mayahudi ? Waka-piga ukelele tena, Msalibu. Ikawa Pilato kuwaaliza, Kwani amefanya uovu gani ? Wao na kuzidi mno kupiga ukelele, Msalibu. Na Pilato akipenda kuufanyia mkutano liwafurahishalo, akawafungulia Baraba ; aka-mwacha Yesu apate kusalibiwa, alipokwisha kumpiga mjeledi. Na wale askari wakamchukua Yesu, wakaenda naye ndani ya ukumbi wa nyumba ya liwali, wakakutanisha kikozi kizima, wakamvika nguo ya rangi ya zamba-

rau, walipokwisha kusuka taji ya miiba wakamvika. Wakaanza kumpa salamu, wakamwambia, Salamu, Mfalme wa Mayahudi ! Ikawa kumpiga kichwani kwa mwanzi, wakimtemea na mate ; wakapiga na magoti, na kumsujudia. Hata wakiisha kumchezea-chezea, wakamvua nguo ya rangi ya zambarau wakanvika mavao yake, kisha wakatoka naye nje wapate kumsalibu. Wakamtenza nguvu mtu mmoja mpita-njia jina lake aitwa Simoni Mkurene, yuatoka shamba, mtu huyu ni babayao Alekisandaro na Rufo, apate kumchukulia msalaba wake. Wakamchukua Yesu wakaenda naye pahali paitwa Golgotha, maana yake ikitafsiriwa ni pahali pa Fuvu la Kichwa. Ikawa kumpa mvinyo iliyochanganywa na manemane ; asiitwae. Wakamsalibu. Wakagawanya mavao yake, kwa kufanya kura katika hayo, kwamba kila mwenye chake atwae. Nayo ilikuwa saa ya tatu, wakamsalibu. Na anwani ya hukumu yake ilikuwa imeandikwa juu, MFALME WA MAYAHUDI. Wakasalibu pamoja naye wevi wawili, huyu upande wa mkono wake wa kuume, na huyu mkono wake wa kushoto. Maandiko yakatimia yasemayo, Naye alihesabiwa katika hesabu ya hao wakosao. Ikawa wale wapitao kumtukana, huku watukusa-tukusa vichwa vyao, wakinena, Uoo ! ultanguaye hekalu, na kulijenga kwa siku tatu, jioke mwenyewe, ushuke msalabani. Wale makuhani wakuu nao wakimfanya dhihaka kama vile, wenyewe kwa wenyewe, wao na wana-wa-vyuoni, ikawa kusemezana, Aliwaokoa wensiwe, mwenyewe hawezи kuijokoa. Kristo Mfalme wa Isiraeli na ashuke sasa msalabani, tuone, tupate kuamini ! Na wale waliosalibiwa pamoja naye wakintukana. Hata ikifika saa ya sita kulifunga giza nchi nzima hata saa ya tisa. Hata saa ya tisa Yesu akapiga ukelele kwa sauti kuu, akisema, Eloi, Eloi, lama sabakithani ? maana yake, Mungu wangu, Mungu wangu, umeniachaka kwa ajili ya nini ? Wengine katika waliosimama pale waliposikia wakanena, Huyu ndiye, yuamlingana Elija ! Na mtu mmoja akaenda mbio, akajaza sifunji siki, akitaita katika mwanzi, ikawa kumnywesha, huku yuanena, Acheni ! na tumwangalie kwamba aja Elija kuja kumshu-

sha. Yesu akapiga ukelele kwa sauti kuu, akatokwa na roho. Pazia ya hekalu ikapasuka ikawa *pande* mbili, tokea juu hata chini. Na yule mkubwa wa askari mia aliyesimama hapo amemkibili, alipoona ya kwamba amepiga ukelele na kutokwa na roho kwa jinsi hiyo, akasema, Ni kweli mtu huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu.

JUMATANO MBELE YA UFUFUO

Waraka. Wahibiranja 9. 16-28

KWANI yakiwapo mausio-ya-urithi, ni sharti kuwe na mauti yake yeye aliyeausia. Kwani mausio-ya-urithi yana nguvu hapo palipokuwa na mauti, auje, yana nguvu popote akiwapo yu hai huyo aliyeausia ? Ndipo hata *agano* lile la kwanza halikuanzilizwa pasipokuwa na damu. Kwani hapo kila amri ikiisha kunenwa na Musa na wale watu wote, sawasawa na sheria, akatwa damu ya hao wana-wa-*ng'ombe* na hao mbuzi, pamoja na maji na sufi nyekundu na husopo, naye akanyunyiza juu ya chuo chenyewe, na juu ya hao watu wote, akisema, Ni damu ya agano hii, Mwenyezi Mungu alilowaagizia ninyi. Tena lile hema na vyombo vyote vya hizo kazi akavinyunyizidam uivyo hivyo. Tena, katika ile sheria, karibu na vitu vyote hutakata kwa damu, tena pasipo kumwagika damu haupatikani msamaha. Basi ilikuwa ni sharti kwamba ile mifano ya vile vya mbinguni vitakaswe kwa *dhabihu* hizo ; ila vite vitu vya mbinguni vyenyewe ni *kutakaswa* kwa *dhabihu* zilizo bora kukiko hizo. Kwani Kristo hakuingia pahali patakatifu *palipo* pa kweli ; lakini *aliingia* katika zile mbingu hasa, aonekane sasa mbele za Mwenyezi Mungu kwa ajili yetu : wala si kwamba atoe nafsi yake mwenyewe mara nyangi ; mfano wa kuhanimkuu aingiavyo katika pahali patakatifu mwaka baada ya mwaka na damu isiyokuwa yake ; au hivyo ingempasa yeye kuteswa mara nyangi tangu kupigwa msingi ulimwengu : ila sasa mara moja kwa utimilifu wa hizo zamani amefunuliwa apate kuziondoa dhambi kwa njia ya *dhabihu* ya nafsi yake mwenyewe. Tena kama wanadamu

walivyowekewa kufa mara moja, na baadaye hukumu ; ni vivyo na Kristo naye, akiisha kutolewa mara moja apate kuzichukua dhambi za watu wengi, yeye, *yuu* mbali na dhambi, atatoka mara ya pili kwa hao wamngjeao hata wapate wokofu.

Injili. Luka 22. 1-71

IKAKARIBIA idi ya mikate isiyotiwa chachu, nayo Indyo iitwayo Idi ya Pasaka. Tena makuhani wakuu na waandishi walikuwa kutafuta njia ya kumuua, kwani walikuwa wakiwacha wenyejii. Shetani akamwingia Yudasi, yule aitwaye Mwisikariota, naye ni katika hesabu ya wale kumi na wawili : akaondoka, akaenda akasema na makuhani wakuu na wakubwa wa askari, jinsi atakavyom-saliti nao. Wakafurahi wakafanya agano naye la kumpa fedha. Akaafikana *nao*, ikawa kutafuta majira ya kumsaliti faragha isiyokuwa na watu. Ikaja siku ya Isiyo Chachu, ile iliyopasa kuchinjwa *kondoo wa* Pasaka. Akawatuma Petero na Yohana, akawaambia, Endeni mkatuandalie Pasaka tupate kumla. Wakamwambia, Wataka tkuandalie wapi ? Akawaambia, Mtakapoingia ndani ya mji mtakutwa na mtu amechukua mtungi wa maji : mtu huyo mfuateni hata mfikilie nyumba ataka-yoingia ; mwambieni mwenye nyumba, Mwalimu akua-mbia, Ki wapi chumba cha kulia nikalie Pasaka mimi na wanafunzi wangu ? Naye atawaonyesha chumba kikubwa ghorofani kinsha kutandikwa vyombo : andalieni humo. Wakaenda wakaona vivile kama alivyowaambia, waka-mwandaa Pasaka. Hata ulipofika wakati wake akaketi chakulani yeye na wale mitume kumi na wawili pamoja naye. Akawaambia, Pasaka huyu nimetamani sana kumla pamoja nanyi kabla sijapatikana na mashaka. Kwani nawaambia kwamba simli tena kamwe hata yaishe kukamilika mambo yake katika ufalme wa Mungu. Akapokea kikombe, alipokwisha kushukuru akasema, Twaeni hiki mkagawanye nanyi kwa nanyi : kwani nawaambia kwamba, tokea sasa sinywi mimi katika uzao wa mzabibu, hata uje ufalme wa Mungu. Akatwaa na mkate, alipokwisha kushukuru akauvunja akawapa, aki-

nena, Huu ndio mwili wangu utolewao kwa ajili yenu : fanyeni *neno* hili kwa kunikumbuka. Na kikombe nacho vivyo hivyo baada ya kwisha kula ; yuanena, Kikombe hiki ndilo agano jipyä katika damu yangu, imwagwayo kwa ajili yenu. Na haya yote, huu ndio, inkono wake anisalitiye upo nami hapa mezani ! Kwa kuwa Mwana wa binadamu hakika yake yuaenda kama ilivyozimwi kwake : pamoja na haya, ole wake mtu huyo atakayemsaliti ! Wakaanza kuulizana wao kwa wao, ni nani kwa atakayetenda jambo hilo. Yakaondoka na mashindano kwao : kana kwamba ni nani adhaniwaye kuwa mkubwa. Akawaambia, Wale mataifa-taifa, wafalme wao wawata wala-tawala, na walio na hukumu juu yao huitwa wafanyakaji-wa-wema. Ninyi hamwi karma vile : lakini aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye kijana, na mwenye kutawala kama atumikaye. Kwani aliye mkubwa ni yupi, yule aliyeketi chakulani au yule atumikaye ? Siye yule aliyeketi ? Lakini mimi katikati yenu nimekuwa kama atumikaye. Nanyi ndinyi mlidumu nami katika kujari-biwa kwangu. Nami ni katika kuwaagizia ufalme, kama vile nilivyoagiziwa mimi na Babaangu ; mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu : nanyi mtaketi juu ya viti nya enzi, huku mkiwahukumu mababila kumi na mawili ya Israeli. Bwana akasema, Ewe Simoni, Simoni ! huyo ndiye, Shetani amewataka kuwapetepetepeta kama nganu ipепetwavyo. Lakini mimi nimeomba kwa ajili yako, ili kwamba imani yako isitindike ; basi nawe ukiisha kurejea wathubutishe nduguzo, Akamwambia, Bwana, mimi niwapo pamoja nawe ni tayari kwenda kifungoni au hata kifoni. Akanena, Nakwambia, Petero, leo halitawika jimbi, ila utakwisha kunikana mara tatu kutoa nijua. Akawauliza, Je, pale nilipowatumwa hamna kifuko wala mkoba wala viatu, mlipungukiwa na chochote ? Wakasema, 'A'a ! Akawaambia, Lakini sasa aliye na kifuko na akichukue na mkoba vivyo ; na asiyekuwa na upanga auze nguo yake anunue. Kwani nawaambia kwamba maandiko haya hayana budi yatatimia kwangu mimi, ya kwamba : Naye alihesabiwa mionganii mwa wakosaji. Kwani yanipasayo

yana na matimio yake. Wakasema, Bwana, hizi ndizo, panga mbili ! Akawaambia, Yatosha. Naye akatoka akaenda kilima cha Mizeituni kama desturi yake. Akaandamwa na wale wanafunzi nao. Alipokwisha kufika pahali pale akawaambia, Ombeni kwa Mungu kwamba msingie kujaribiwani. Mwenyewe akajitenga nao kiasi cha kutupa jiwe, akapiga magoti ikawa kuomba ; akanena, Ewe Baba, kwamba wapenda, niondolee kikombe hiki. Pamoja na haya, yasiwe nipedavyo mimi, yawe upendavyo wewe. Akatoureka na malaika mmoja atoka mbinguni, yuamtia nguvu. Naye ali katika dhiki, akazidi sana kuomba Mungu, zikawa hari zake kama magande-gande ya damu yakishuka nchi. Hata alipoondoka katika kule kuomba kwake, akaenda kwa wanafunzi wake, akawaona wamelala usingizi kwa majonzi ; akawaambia, Ni nini kulala usingizi ? Ondokeni mwombe kwa Mungu, msije mkaingia katika kujaribiwa. Basi yu katika kunena hayo, nao hao ndio, mukutano wa watu ; na yule aitwaye Yudasi, ni mmoja katika wale kumi na wawili, amewatangulia mbele yao. Akamsongelea Yesu ili kumbusu. Yesu akamwambia, Je, Yudasi, wamsaliti Mwana wa binadamu kwa buso ? Na wale walio kando-kando yake walipo-yaona mambo yale yatakavyokwenda, wakamwambia, Bwana, je, tuwapige kwa upanga ? Mtu mmoja katika wao akampiga mtumwa wake kuhani mkuu, akamkata sikio la upande wa mkono wa kuume. Yesu akajibu akasema, Ridhieni kwa haya tu ! akamgusa sikio lake akampoza. Yesu akawaambia wale waliomjia juu yake, makuhani wakuu na maakida wa hekaluni na wazee, Je, mmetokea kama mnaomtafuta mwivji, na mapanga na magongo ? Msininyoshee mikono juu yangu nami nili pamoja nanyi kila siku katika hekalu : isipokuwa hii ndiyo saa yenu, nayo ndiyo amri yake hiyo giza. Wakamshika wakamwongoza, wakaenda naye nyumbani kwa kuhani mkuu. Na Petero alimfuata kwa mbali. Nao walipo-kwisha kuwashaa moto katikati ya ua, wakiketi pamoja, ilikuwa Petero kuketi katikati yao. Kijakazi kimoja akamwona ameketi penye mwanga, akamkulizia macho, akanena, Na huyu alikuwa pamoja naye. Akamkana,

akasema, Ewe mwanamke, simjui. Baadaye punde mtu mwingine akimwona akamwambia, Nawe u katika wao. Petero akanena, Ewe mtu we, si mimi ! Kisha baadaye kama kitambo cha saa moja, mtu mwingine akakaza sana, akasema, Hakika yake huyu alikuwapo pamoja naye, kwani naye ni Mgaililaya. Petero akasema, Mtu wewe, siyajui maana yake uneneayo ! Yu katika kunena hivi, mara likawika jimbi. Bwana akazuunguka, akamwangalia Petero. Petero akakumbuka maneno ya Bwana, alivyomwambia, kana kwamba : Leo kwanza lisijawaka jimbi utanikana mara tatu. Akatoka nje, akalia kwa uchungu. Kisha wale wanawaume waliomzuua Yesu walikuwa kumfanya dhihaka, wakimpiga-piga. Hata walipokwisha kumfumba macho wakimpiga uso na kumuuliza-uliza wakinena, Tabiri, ni nani aliyekupiga ? Ikawa kumtolea na maneno mengine mengi kwa kutukana. Hata kulipokucha, mara ukakutanika mukutano wao walio wazee katika wenyeji, makuhani wakuu na waandishi. Wakamwongoza wakaenda naye katika baraza yao, huku wakinena, Wewe kwamba ndiwe Kristo, tuambie. Akawaambia, Nijapowaambia hamtasadiki kamwe : tena nijapowauliza neno hamtanijibu wala kunifufungua. Ila tangi sasa Mwana wa binadamu atakuwa kuketi upande wa inkono wa kuume wa nguvu zake Mwenyezi Mungu. Wakasema pia wote, Basi wewe u Mwana wa Mungu ? Akawaambia, Ninyi mwasema kwamba mimi ndiye. Wakasema, Tuna haja gani tena ya ushuhuda ? kwani wenyewe tumemsikia kwa kinywa chake.

ALHAMISI MBELE YA UFUFUO

Waraka. 1 Wakorintho 11. 17-34

KATIKA kuwapa maagizo haya siwasifu, kwa kuwa mwakutana, si kwa ajili ya yaliyo mema zaidi, lakini kwa yaliyo mabaya zaidi. Kwani kwanza, mtakapokutana ninyi ndani ya kanisa, nasikia ya kwamba kuna matanguano kati yenu : nami nusu yake nasadiki. Kwani hapana budi utakuwa uzusi kati yenu, ili kwamba hao waliohakikishwa wawe dhahiri kati yenu. Basi hapo

ninyi mtakapokutana pamoja, haimkini kwenu kula chakula cha Bwana : kwani katika kula kwenu huyu hutwaa chakula chake mwenyewe kabla ya huyu, na huyu ana njaa, na huyu ameleta. Ni nini? hamna nyumba zenu kula na kunywa? auje, mwalidharau kanisa la Mwenyezi Mungu, na kuwatahayarisha hao wasio na kitu? Je, niwaambieni? Niwasifu kwa ajili ya hayo? La, siwasifu. Kwani mimi nilipokea kwa Bwana hicho ambacho niliwapa ninyi nami, ya kwamba, Bwana Yesu usiku ule aliosalitiwa alitwa mkate: kisha alipokwisha kushukuru akauvunja, akanena, Twaeni, mle: ni mwili wangu huu, ambaou umevunjika kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi. Ni kama vile, *akakitwaa* na kikombe baada ya chakula, akanena, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu: fanyeni hivi kila mnapotunya, kwa kunikumbuka mimi. Kwani kila mlapo mkate huu na kunywa kikombe hiki, mwaonyesha mauti ya Bwana hata aje. Kwa ajili ya hayo kila mtu atakayekula mkate huo au kunywa kikombe hicho cha Bwana naye hastahili, ana hukumu ya ule mwili na ile damu ya Bwana. Ila binadamu na ajijaribu nafsi yake, na *huku kujijaribu* ale katika ule mkate na kunywa katika kile kikombe. Kwani huyo alaye na kunywa naye hastahili, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, ikiwa haupambanui ule mwili wa Bwana. Kwa sababu hiyo wengi kwenu ni wanyonge, na wengine ni wagonjwa, na walioala si haba. Ila kwamba sisi tulizipambanua nafsi zetu wenye, tusingehukumiwa. Ila tukihukumiwa twarudiwa na Bwana, ili kwamba tusihukumiwe adhabu pamoja na dunia. Kwa ajili ya hayo, ndugu zangu, mtakapokutana pamoja kula chakula, ngojeaneni ninyi kwa ninyi. Kwamba mtu ana njaa, na ale nyumbani kwake: ili kwamba kukutana kwenu kusiwe kwa hukumu. Na yale yasaliayo nitakapokuja nitayatengeza.

Injili. Luka 23. 1-49

UKASIMAMA mukutano wote, wakaenda naye kwa Pilato. Wakaanza kumshtaki, wanena, Huyu tumemwona akipotoa-potoa taifa letu na kuzulia kupewa kodi

Kaisari, akisema kwamba mwenyewe ni Kristo, ni mfalme. Pilato akamuuliza, akanena, Wewe ndiye mfalme wa Mayahudi? Akamjibu akanena, Wewe wasema. Pilato akasema nao wale makuhani wakuu na makutano ya watu, akawaambia, Mtu huyu sioni kwake neno ovu. Nao wakakaza sana, wasema kwamba, Yuawafitini wenyiji, akifunza watu nchi nzima ya Uyahudi koteckote, tokea Galilaya mpaka hapa. Aliposikia Pilato *kutajwa Galilaya* aauliza kwamba mtu huyu ni Mgalilaya. Kisha alipoipata hakika yake kuwa yu chini ya hukumu ya Herode, akampeleka kwa Herode, kwa kuwa wakati huo alikuwako Yerusalem. Na Herode alipomwona Yesu, akafurahi sana, kwani alikuwa akitamani kumwona tangu hapo, kwa vile alivyoikia habari nyangi juu yake, akitumaini kuona miujiza atakayoitenda ye: naye akamuuliza-uliza maneno mengi, wala asimjibu neno. Wakasimama wale makuhani wakuu na waandishi, wakamshtaki kwa kukaza sana. Na Herode akamfanya duni, na askari zake nao, akamfanya na dhihaka, huku yuamvika uvao mzuri; akamrudisha kwa Pilato. Basi siku ile ile Pilato na Herode wakafanya urafiki; kwani hapo kwanza walikuwa na utesi wenyewe kwa wenyewe. Pilato akawakutanisha makuhani wakuu na watu wakubwa na wenyiji, akawaambia, Mtu huyu mmeniletea kama apotoaye watu; nami, huyu ndiye, nilipoamua mambo yake mbele yenu, sikuona kwake kosa lolote katika mnayomshtaki: wala hata Herode, kwani amemrudisha kwetu; naye, huyu ndiye, halikutendeka kwake neno lipasalo mauti. Basi nitamrudi, kisha nimfungue. (Kwani ni sharti awafungulie mmoja wakati wa idi.) Wakampigia ukelele jamii ya walioopo, wasema, Mwondoe huyu, utufungulie Baraba. Naye ni mtu mmoja aliyetupwa gerezani kwa ajili ya fitina na uuaji uliotokea katika mji. Akasema nao tena yule Pilato, yuataka kumfungua Yesu. Wao wakipiga ukelele tu, wanena, Msalibu! msalibu! Yeye akawaambia mara ya tatu, Kwani, amefanya uovu gani huyu? Sikuona kwake neno lipasalo mauti. Basi nitamrudi, kisha nimfungue. Wakakaza sana kuinua sauti kumtaka kwamba asalibiwe, sauti zao pamoja na sauti za makuhani

wakuu zikashinda. Pilato akaamua kwamba yawe kama watakayo ; naye akawafungulia yule aliyetupwa gerezani kwa sababu ya fitina na uuaji, yule walijemtaka kwake ; akamta Yesu katika kutaka hukuo. Hata walipokuwa katika kumwondo, wakamshika mtu mmoja atokaye shamba, jina lake akiitwa Simoni Mkurene, wakamtweka ule msalaba, apate kuuchukua, kwenda nao nyuma yake Yesu. Ikawa yeje kuandamwa na wenyeji mkutano mkuu, na wanawake, nao wampigao vifua na kuombolea kwake. Akazunguka Yesu akawalekeea, akasema, Enyi wanawake, wana wa Yerusalem, msinililie mimi : lilieni nafsi zenu na wana wenu. Kwani, hizo ndizo, siku zaja watakapo sema, Raha ni ya walio tasa ! na ya matumbo yasiyozaa na matiti yasiyoamwisha ! Ndipo watakapoanza kuiambia milima, Tuangukieni juu yetu : na vilima, Tufinikeni. Kwani mambo haya kwamba wayatenda katika mtu mbichi, je, katika ule mkavu huwaje ? Wakaja nao na watu wawili tena, wakosaji, kwenda kuuawa pamoja naye. Hata walipofika pahali paitwapo Fuvu la Kichwa, hapo ndipo walipomsalibu pamoja na wale wakosaji, mmoja upande wa mkono wa kuume, mmoja upande wa mkono wa kushoto. Yesu akasema, Ewe Baba, wasamehe, kwani hawajui wfanyakalo. Walipogawanya mavao yake, wakafanya kura. Walikuwa wanasis mama wale wenyeji wakitazama. Na wale wakubwa nao wakimtolea ufyozi, wanena, Aliokoa wenziwe ; na ajiokoe mwenyeewe, kwamba ndiye Kristo wake Mungu huyu, mteule wake ! Ikawa kumfanya dhihaka wale askari nao, wakimwendendea na kumsongezea siki, huku wakinena, Wewe kwamba ndiye msalme wa Mayahudi iokoe nafsi yako. Basi hapo juu yake palikuwa na anwani, iliyandikwa kwa Kiyunani, na Kilatini, na Kihibirania : HUYU NDIYE MFALME WA MAYAHUDI. Na wale wakosaji wale waliotungi-kwa, mmojawapo alikuwa kumtukana, yuasema, Wewe hu Kristo ? okoa nafsi yako na sisi. Akajibu yule mwensiwe, kwa kumkaripia, akamwambia, Wewe humchi Mungu nawe, kwa kuwa u katika laumu ii hii ? Nasi tuna haki, kwani hivi twarudishiwa mfano wa vitendo vyetu : lakini huyu hakutenda kamiwe lisilokuwa. Kisha aka-

mwambia Yesu, Ewe Bwana, nikumbuke hapo utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia, Ni kweli nakuambia, hivi leo utakuwa nami peponi. Na wakati huo ulikuwa kama wa kuingia saa ya sita, kuka-funga giza nchi yote mpaka saa ya tisa, huku juu likipungua nuru zake : pazia ya hekalu ikapasuka kati. Naye Yesu akapiga ukelele kwa sauti kuu, akanena, Ewe Babaangu, roho yangu naitia mikononi mwako. Kusema kwake haya akatokwa na roho. Na yule mkubwa wa askari mia alipoona yaliyokuwa, alimtukuzza Mwenyezi Mungu, akinena, Hapana shaka, mtu huyu alikuwa mwenye haki ! Na yale makundi ya watu waliokutanikia kuona mambo yale, walipoona yaliyotendeke, wakarudi pia wote huku wajipiga-piga vifua vyao. Na watu wote waliojuana naye, na wanawake nao waliokuwa wakifuatana naye tokea huko Galilaya, wali-kuwa wamesimama kwa mbali, watazama mambo haya.

IJUMAA NJEMA

(au, Siku ya Kuteseka kwake Bwana wetu)

Sala

TWAKUOMBA sana, ewe Mwenyezi Mungu, uiangalie kwa rehema hii nyumba yako, ambayo kwa ajili yake Bwana wetu Yesu Kristo alikuwa radhi kusalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu waovu, hata akapatikana na mauti msalabani ; naye sasa amekuwa yuaishi na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, ambaye kwa Roho wako kanisa lote limetawaliwa na kutakaswa ; twakuomba uyasikize hayo maombi yetu na hizi sala zetu tukuleteazo wewe sasa, kwa kuwaombea watu wa kila daraja katika kanisa lako takatifu, kila mtu katika kazi yake akutumikie kwa kweli na haki, kwa Bwana wetu, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

EWE Mungu mwenye huruma, Muumba wa watu wote, Echuchukii ulivyovifanya hata kimoja, wala hutaki mauti ya mwenye dhambi, waona ni vyema afadhali ageuke na kuishi : uwarehemu wote Mayahudi, na Waislamu, na Makafiri, na waipingao dini ya kweli, uwaondolee ujinga uwao wote, na uzito wote walio nao wa moyo, uwatoc na dharau ya neno lako, nawe uwaongoze, ewe Bwana wa rehema, uwaletee kwao, maana, ndani ya kundi lako, na iwe wao kuupata wokofu pamoja na wote wateule Waisiraeli wa kweli, liwe zizi moja, Mchunga mmoja, naye ni Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Waraka. Wahibirania 10. 1-25

KWANI hiyo sheria, kwa kuwa ilikuwa na uvuli wa vitu vyema vijavyo, si sura hasa za vitu hivyo, kwa dhabihu zile zitolewazo daima kila mwaka haiwezi milele kuwakamilisha hao wakaribiao. Je, hapo hazingekoma kutolewa, kwa sababu hao waabuduo wakiisha kutakaswa mara moja hawangekuwa na nia za kutambua dhambi tena ? Lakini katika dhabihu hizo kuna ukumbusho wa dhambi kila mwaka. Kwani haviwezekani kwamba damu ya ng'ombe na mbuzi kuondoa dhambi. Kwa ajili ya hayo, hapo aingiapo katika ulimwengu asema, Dhabihu na vipawa hukuzitaka, ila ulinitengeza mwili ; vipawa vizima vya kuteketezwa na sadaka kwa ajili ya dhambi hukupendezewa nazo : ndipo nikasema, Labeka, nsha kuja ! (katika kurasa za chuo nimeandikiwa) kuyafanya uyatakayo wewe, Mwenyezi Mungu. Alivyosema hapo nyuma, ya kwamba, Dhabihu na vipawa, na vipawa vizima vya kuteketezwa na *sadaka* kwa ajili ya dhambi, hukuzitaka wala hukupendezewa nazo (hizo zitolewazo katika sheria), hapo ndipo aliponena, Labeka, nsha kuja, kuyafanya uyatakayo wewe, ewe Mungu. Aliondoa hilo la kwanza, ili kwamba alithubutishe hilo la pili. Kwa ajili ya hayo aliyyotaka yeye sisi tumetakaswa, kwa njia ya kutolewa kwake huo mwili wa Yesu Kristo mara moja tu. Tena na kila kuhani yuasimama kila siku akifanya utu-

mishi na kuzitoa dhabihu zizo hizo mara nyingi, ambazo popote haziwezi kuondoa madhambi : ila mtu huyo akiisha kuitoa dhabihu moja kwa ajili ya madhambi hata milele, akaketi upande wa mkonono wa kuume wa Mwenyezi Mungu ; tangu hapo akingoja hata adui zake wawekwe wawe ncha-za-nyayo *chini* ya miguu yake. Kwani kwa sadaka moja amewakamilisha hata milele hao waliotakaswa. Roho Mtakatifu naye atushuhudia : kwani baada ya kunena *neno hili*, Hili ndilo agano nitakalofanya nao baada ya siku hizo, anena Bwana ; nitawapa sheria zangu katika miyo yao, tena nitaziandika katika nia zao ; *ndipo asemapo na neno hili*, Dhambi zao na maasia yao sitaya-kumbuka tena baadaye. Basi hapo ukiwapo msamaha wa hizi, hapana tena sadaka kwa ajili ya dhambi. Basi, ndugu zangu, kwa kuwa tuna uthubutifu wa kuingia ndani ya pahali patakatifu katika damu ya Yesu, kwa njia ile aliyo tuanzilizia, njia ilio mpya yenye uhai, kwa njia ya pazia, maana, mwili wake ; tena *kwa kuwa tuna* kuhani aliye mkuu juu ya nyumba ya Mwenyezi Mungu ; na tukaribie na moyo wa kweli katika utimilifu wa imani, wenye miyo iliyonyunyizwa tuache nia mbaya, na miili yetu kuoshwa kwa maji yaliyotakata : na tuyashike sana maungamo ya matumaini yetu yasitukute ; kwa kuwa yeye aliyahidi ni mwaminifu : na tujulianeni sisi kwa sisi na kuhimizana kwa mapenzi na kazi zilizo njema ; na tusiache kukutana pamoja sisi kwa sisi, *tusiwe* kama desturi ya watu wengine ilivyo, lakini iwe kuonyana ; kisha na kufanya zaidi sana kwa kadiri mwonavyo siku hiyo kukaribia.

Injili. Yohana 19. 1-37

NDIPO hapo Pilato akamtwa Yesu, akampiga mjeledi. Wale askari wakasuka taji ya miiba. Wakamvika kichwani mwake. Wakamvika na nguo ya rangi ya zambarau. Ikawa kumwendea na kusema, Salamu, Mfalme wa Mayahudi, na kumtia misubukuo. Akatoka nje Pilato, mara ya pili : akawaambia, Huyu ndiye, nawaleta nje, mpare kumjua kwamba sioni batili kwake. Basi akatoka nje Yesu, amevaa ile taji ya miiba

na ile nguo ya rangi ya zambarau. Akawaambia, Huyu ndiye, mtu huyu. Basi wale makuhani wakutu na wangojezi, walipomwona, wakapiga ukelele, wasema, Kamsalibu ! kamsalibu ! Pilato akawaambia, Mtwaeni ninyi mkamsalibu ; kwani mimi sioni batili kwake. Mayahudi wakamjibu, Sisi tuna sheria yetu ; hata kwa sheria hiyo astahili mauti : kwa kuwa amejifanya Mwana wa Mungu. Basi aliposikia Pilato neno hili akazidi kufanya hofu ; akaingia tena katika nyumba ya uliwali, akamuuliza Yesu, Watokea wapi ? wala Yesu asimjibu. Basi Pilato akamuuliza, Je, husemi nami ? Wewe hunijui ya kuwa mimi nina amri ya kukuacha, nina na amri ya kukusalibu ? Yesu akamjibu, Hungekuwa na amri kwangu mimi kwa lolote, kwamba hukupewa kutoka juu. Kwa ajili ya hayo, aliye na dhambi sana ni yule aliyenitia mikononi mwako. Kwa sababu hiyo ikawa Pilato kutafuta njia ya kurnwacha. Ila Mayahudi walikuwa wakipiga ukelele, wasema, Ukimwacha mtu huyu, hu rafikiye Kaisari. Kila ajifanyaye mfalme humtusha Kaisari. Basi Pilato aliposikia maneno yale akamtoa nje Yesu ; akaketi juu ya baraza ya hukumu, pahali paitwa Sakafu ya Mawe, Kihibirania chake ni Gabatha. Nayo ilikuwa ni siku ya kuandalia idi ya Pasaka, kama wakati wa saa ya sita. Akawaambia Mayahudi, Huyu ndiye, mfalme wenu, huyu. Basi wakapiga ukelele, Kamwondoe ! kamwondoe ! kamsalibu ! Pilato akawaambia, Je, mfalme wenu, nimsalibu ? Wakajibu makuhani wakuu, Hatuna sisi mfalme ila Kaisari. Ndipo hapo basi akamsongeza kwao apate kusalibwa. Basi wakamshika Yesu wakaenda naye : naye ameuchukua msalaba wake yeye, akaenda nje *ya mji*, akaenda pahali paitwa Fuvu la Kichwa, na pahali hapo Kihibirania paitwa Golgotha ; wakamsalibu papo, na watu wawili tena pamoja naye, huku mmoja na huku mmoja, yeye Yesu yu katikati. Pilato akaandika na anwani, akaibandika juu ya msalaba, nayo imeandikwa : YESU MNAZARI, MFALME WA MAYAHUDI. Basi na hiyo anwani wakaisoma watu wengi katika Mayahudi, kwa kuwa pahali hapo ni karibu na mji, hapo aliposalibwa Yesu : nayo iliandikwa Kihibirania na Kilatini

na Kiyutanani. Basi ikawa kumwambia Pilato makuhani wakuu wa Mayahudi, Usiandike, ni Mfalme wa Mayahudi ; andika kwamba, Alisema yule, Mimi ndiye Mfalme wa Mayahudi. Akajibu Pilato, Niliyoyaandika nimekwisha kuyaandika. Basi wale askari walipokwisha kumsalibu Yesu, ndipo walipotwaa nguo zake wakafanya mafungu manne, kila askari mmoja fungu moja : *wakatwaa* na kanzu yake. Nayo ilikuwa haina mshono kanzu, imefumwa nzima tokea juu hata chini. Basi wakasemezana wao kwa wao, Na tusiipasue : tuifanyie kura itakuwa ya nani. Yapate kutimia yale maandiko yanenayo : Waligawanya nguo zangu wao kwa wao, wakafanya na kura ya uvao wangu. Haya basi, ndiyo waliyoyafanya wale askari. Na hapo katika msalaba wa Yesu walikuwa wamesimama mamaye, na nduguye mamaye Mariamu mkewe Kileopa, na Mariamu Mmagidala. Basi Yesu kuwaona kwake mamaye na yule mwanafunzi wamesimama kando, mwenyewe aliyempenda, akamwambia mamaye, Mwanamke, huyu ndiye, mwanayo, huyu ! Kisha akamwambia yule mwanafunzi, Huyu ndiye, mamaako ! Basi tangu saa ile yule mwanafunzi akamtwaakamta nyumbani mwake. Baada ya hayo Yesu, ali hali amejuu kuwa mambo yote sasa yamekwisha, yapate kutimia yale maandiko, akasema, Nina kiu. Palikuwa pamewekwa chombo hapo kimejaa siki ; basi wakatwaa sifunji iliyojaa siki wakaitia katika ufito wa mzobi, wakamsongeza kinywani. Basi Yesu alipoipokea siki aka-sema, Imekwisha ; akainamisha kichwa akasalimu roho. Basi wale Mayahudi, kwa vile ilivyokuwa siku ya kute-ngeza, wasipate kuchelewa wale maiti juu ya misalaba hata siku ya sabatu, kwani ilikuwa siku kuu siku ya sabatu ile, wakamtaka Pilato kwamba ivunjwe miguu yao, waondolewe. Basi wakaenda wale askari wakamvunja miguu yule wa kwanza na mwenziwe yule aliyangikwa pamoja naye : hata walipomwendea Yesu, wakamwona amekwisha kufa, wasimvunje miguu ; isipokuwa mmojawapo katika wale askari akamchoma fumo la ubavu, mara akatowka na damu na maji. Naye aliyeaona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni wa kweli, naye huyo amejuu kuwa ni

mwenye^c kusema kweli yeye, nanyi mpate kuamini. Kwani yalikuwa haya ili yapate kutimia yale **maandiko** : Mfupa wake hautavunjika. Kisha yasema tena maa-ndiko mengine, Watamwinulia macho huyo wali-entumbua.

MATENGEZO YA IDI YA UFUFUO

Sala

UKUBALI, ewe Bwana, ya kwamba, kama vile tubatizwavyo sisi ndani ya mauti ya Mwanayo Mwenye-baraka Mwokozi wetu Yesu Kristo, tupate na kuzikwa pamoja naye vilevile, kwa kuyatia mautini daima mambo yetu mabovu ya tamaa, ili kwamba kwa kupita ndani ya kaburi, ndani ya mlango wa mauti, tufikilie katika kufufuliwani kwetu kwenye furaha ; kwa ajili ya kustahili kwake yeye, ambaye alikuifa, akazikwa, akafufuka, kwa ajili yetu, Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Petero 3. 17-22

KWANI ni vyema zaidi, kuteswa kwa sababu ya mliviyotenda mema kuliko kwa sababu ya mliviyotenda maovu, ikiwa ndivyo yatakavyo mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, *maana*, mwenye haki kwa ajili ya hao wasio na haki, ili kwamba atulete kwa Mwenyezi Mungu ; akiuawa katika mwili, na kufanywa hai katika roho ; ambayo katika hiyo akaenda na kuzihubiri zile roho zilizokuwa gerezani, ambazo, hapo kale zilikuwa hazikutii, hapo uvumilivu wa Mwenyezi Mungu ulipongoja katika siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikite-ngezwa, ambamo ndani yake wachache, maana, ni nafsi nane, waliokolewa kwa njia ya maji : ambayo yawaokoa na ninyi sasa, kwa mfano ule ule, *maana*, ni ubatizo, si kuzie-pua taka za mwili, bali ni kule kutaka jawabu ya moyo ulio mwema kwa upande wa Mungu, kwa njia ya kufufuliwa kwake Yesu Kristo ; ambaye yuko upande wa mkonono wa kuume wa Mwenyezi Mungu, maana, amekwendia mbinguni ; vikiisha kutiishwa kwake malaika na amri na nguvu.

Injili. Mathayo 27. 57-66

ILIPOINGIA jioni akaenda mtu mmoja tajiri, *mtu* wa Arimathea, akiitwa Yusufu, naye mwenyewe ni mwana-funzi wa Yesu : akaenda huyo kwa Pilato akautaka mwili wa Yesu. Ndipo hapo Pilato akaamuru apewe. Yusufu akautwaa ule mwili akauzonga-zonga kitambaa cha katani kilicho safi, akauweka katika kaburi lake yeye jipy, alilolikomba mwambani : kisha akabingirisha jiwe kubwa mbele ya mlango wa kaburi, akaenda zake. Na paali papo walikuwapo Mariamu Mmagidala na yule Mariamu wa pili, wameketi mbele ya kaburi. Siku ya pili yake, nayo ndiyo iliyoandama baada ya Matengezo ya idi, makuhani wakuu na Mafarisayo wakamkutanikia Pilato, wakanena, Bwana, twakumbuka kwamba yule mdanganayifu alisema, naye akali hai, Mimi baada ya siku tatu nitainuka. Basi amuru litunzwe sana kaburi hata siku ya tatu ; wasije usiku wanafunzi wake wakaenda wakamwiba, wakawaambia wale wenyeji, Ameinuka kutoka kwa wafu : yakawa madanganyo ya mwisho kuwa mabaya kupita ya kwanza. Pilato akawaambia, Ulinzi mnao : endeni mkalitunze sana kaburi kadiri ya mijuuavyo. Wakaenda wakalitunza sana kaburi, kwa kulipiga jiwe muhuri, pamoja na ule ulinzi.

IDI YA UFUFUO

¶ Katika Sala ya Asubuhi, badala ya Zaburi ya, Haya, na tumwimbie, w.k., husomwa au huimbwa Nyinbo hizi.

PASAKA wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka kwa ajili yetu, naye ni Kristo : basi na tuifanye karamu ;

Si kwa chachu ya kale, wala kwa chachu ya uadui na uovu : ila kwa mkate usio chachu wa weupe wa moyo na kweli.

¶ Wakorintho 5. 7-8.

Kristo kwa kuwa amekwisha kufufuliwa kutoka kwa wafu, hafi tena : mauti hayatawali juu yake tena.

Kwani vile alivyokufa, alizifilia dhambi mara moja, basi : na vile aishivyo, yuaishi kwa Mwenyezi Mungu.

Nanyi ni vivyo jihesabuni wenyewe kuwa mu wafu kweli-kweli kwa zile dhambi : kisha mu hai kwa Mwenyezi Mungu, katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Warumi 6. 9-11.

Ila sasa Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu : naye amekuwa ni malimbuko ya hao walilola.

Kwani kwa kuwa mauti *yakaja* kwa njia ya binadamu : kufufuka kwa wafu vivyo *huja* kwa njia ya binadamu.

Kwani vivile kama wote wafavyo katika Adamu : vivyo katika Kristo wote watafanya kuwa hai.

I Wakorintho 15. 20-22.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa Mwanayo mzaliwa Epekee Yesu Kristo umeyashinda mauti, umetufungulia na lango la maisha ya milele ; sisi tu miguuni pako, twa-kutaka ya kwamba, kama neema yako ituongozavyo, wewe hututilia miyoni mwetu tamaa zilizo njema, tuwe sisi nasi kwa msaada wako wa daima kuzitimiliza sawasawa hizo tamaa ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Waraka. Wakolosai 3. 1-7

BASI kwamba mme fufuliwa pamoja na Kristo, takeni mambo hayo yaliyo juu, hapo alipo Kristo, ameketi upande wa m^kono wa kuume wa Mwenyezi Mungu. Fikirini sana hayo yaliyo juu si hayo yaliyo katika nchi. Kwani mliku fa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mwenyezi Mungu. Hapo Kristo atakapofunuliwa, *ambaye ndiye* uhai wetu, ndipo nanyi mtafunuliwa katika utukufu pamoja naye. Basi viueni via vyenu vilivyo juu ya nchi ; *navyo ni uzinifu*, na uchafu, na tamaa mbaya, na shauku mbovu, na kutamani-tamani,

nako ni kuabudu sanamu ; kwa ajili ya mambo hayo hasira ya Mwenyezi Mungu huja juu ya wana wa maasia : na ninyi nanyi mliku wenda katika mambo yayo hayo kwanza, hapo mlipoishi katika mambo hayo.

Injili. Yohana 20. 1-10

HATA siku ya kwanza ya juma yule Mariamu Mmagidala akaenda na mapema, kukali giza-giza, hata kaburini ; akaliona jiwe limeondolewa katika kaburi. Basi akaenda mbio, akamwendea Simoni Petero, aka-mwendea na yule mwanafunzi mwenzive, yule aliye kuwa Yesu akimpenda, akawaambia, Wememtoa Bwana kaburini wamekwenda naye : hatumjui walipomweka. Aka-toka Petero na yule mwanafunzi mwenzive, ikawa kwenenda hata kaburini. Nao waenda mbio wote, yule mwanafunzi mwenzive akamshinda Petero kwa mbio, akapata kaburini mbele. Kisha akainama na kuchungulia, akaiona sanda imewekwa nchi, wala asiingie. Basi Simoni Petero naye akaja, amfua yule, akaingia ndani ya kaburi ; akaiona sanda imewekwa ; na mandili ili-yokuwa kichwani mwake, haikuwekwa pamoja na sanda, imekunjwa-kunjwa imewekwa pahali peke yake. Basi, ndipo hapo akaingia na yule mwanafunzi mwenzive, yule aliye fika kwanza kaburini, akaona, akaamini. Kwani walikuwa hawajalijua lilivyoandikwa, kwamba imempasa kuinuka kutoka kwa wafu. Basi wakaondoka wale wanafunzi mara ya pili kwenda kwoo.

JUMATATU BAADA YA IDI YA UFUFUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa Mwanayo mzaliwa Epekee Yesu Kristo umeyashinda mauti, umetufungulia na lango la maisha ya milele ; sisi tu miguuni pako, twa-kutaka ya kwamba, kama neema yako ituongozavyo, wewe hututilia miyoni mwetu tamaa zilizo njema, tuwe sisi nasi kwa msaada wako wa daima kuzitimiliza sawasawa hizo tamaa ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 10. 34-43

PETERO akafunua kinywa, akasema, Ni kweli nata-mbu ya kwamba Mwenyezi Mungu hana mape-ndeleo : lakini katika kila taifa, amchaye, na kutenda yenye haki, hukubaliwa na yeye. Lile neno alilowape-lekeea wana wa Isiraeli, akihubiri habari njema ya-amani kwa Yesu Kristo (yeye ndiye Bwana wa wote), neno hilo ninyi wenye mwaliujia, lililotangazwa katika nchi nzima ya Yudea likianza kutoka Galilaya, baada ya ubatizo ule uliohubiriwa na Yohana ; ni Yesu Mnazari, jinsi Mungu alivyomtia mafuta *nayo ni* Roho Mtakatifu na uwezo ; aliyekuwa akizunguka-zunguka akitenda vyema, na kuwapoza wote walioonewa na Shetani ; kwa kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja naye. Sisi tu mashahidi wa mambo hayo yote aliyoafanya yeye katika nchi ya Mayahudi na ndani ya Yerusalem pia ; naye ni yeye waliyemuua, wakimtungika juu ya mti. Mtu huyo Mwenyezi Mungu akamfusua siku ya tatu, na kumtoa adhihirishwe, si kwa wenyeji wote, lakini kwa wale mashahidi ambao Mwenyezi Mungu alitangulia kuwachagua, ni sisi, tulikula na kunywa pamoja naye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu. Naye alituagiza kuwahubiri wenyeji, na kushuhudia ya kwamba ni huyo aliyewekwa na Mungu awe Mwamuzi wa walio hai hata na waliokufa. Manabii wote wamshuhudia yeye, ya kwamba kwa jina lake yeye kila mtu aaminie kwake atapata kusamehewa dhambi.

Injili. Luka 24. 13-35

NA siku ile ile watu wawili wa mionganoni mwao walii-kuwa wakienenda kijiji kimoja kilichokuwa mbali na Yerusalem mwendo wa saa mbili, jina lake kijiji hicho kikiitwa Emao. Ikawa kusimulia wao kwa wao katika mambo yale yote yaliyotukia. Nao wa katika kusimulia hivi na kuhujiana, Yesu nafsi yake akakaribia, ikawa kuandamana nao. Lakini yakazuliwa macho yao, wasimtambue. Akawaambia, Ni maneno ya namna gani hayo mzungumzayo hivi mkienenda ? Wakasimama na kuku-

nja nyuso *kwa msiba*. Akamjibu mmojawapo jina lake akiitwa Kileopa, akamwambia, Wewe siku hizi waketi Yerusalem pekeyo hata usiyasikie yaliyotukia siku hizi ? Akawauliza, Ni kama yapi ? Wakamwambia, Ni mambo yaliyompata Yesu Mnazari, aliyekuwa mtu nabii mwénye uwezo wa kunena na kutenda mbele za Mwenyezi Mungu na ya wenyeji wote : tena jinsi makuhani waküu na wakubwa wetu waliviyomtia katika hukumu ya mauti wakamsalibu. Na sisi tulikuwa tukimtumaini kuwa mtu huyo ndiye atakayewakomboa Isiraeli. Pamoja na haya yote, tangu kutendeka mambo hayo leo ni tatu : isipokuwa wanawake kadhwakadha watu wa kikaoni mwetu sisi wametushangaza, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema ; wasiuone mwili wake, wamekuja wametuambia kwamba wameona na malaika kuwatokea, na kuwaambia kwamba yu hai. Na wengine wa mionganoni mwetu wamekwenda kuko kaburini wameona vivyo hivyo, kama walivyo sema wanawake ; ila yeye hawakumwona. Akawaambia, Enyi msiokuwa na fahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote yaliyosemwa na manabii ! Ehe, haikumpasa Kristo kupatikana na mambo haya, na kuingia katika utukufu wake ? Akaanza tokea kwa Musa na manabii wote, akawaeleza-eleza katika maandiko yote, kuliko mambo yapasayo nafsi yake. Kisha wakakaribia kijiji waendacho : akajifanya kama aendaye pahali mbali. Wakamnasihi, wanena, Keti pamoja nasi, kwa kuwa kumekuwa karibu na kuchwa ; na juu limekwhisha kupunga tena. Akaingia ndani ili kuketi nao. Wakati alipoketi nao katika chakula, akatwaa mkate akaubarikia, na kuuvunja, kisha akawapa. Yakafumbuka macho yao wakamtambua, kisha akawafichamania. Wakasemezana wao kwa wao : Je, hata mioyo yetu haikutuwaka ndani yetu, muda alipokuwa akitusimulia njiani huku akitufunilia maadiko ? Wakaondoka saa ile ile, wakarejea Yerusalem, wakawaona wale kumi na mmoja wamekutanika, wao na walio pamoja nao, wasema kwamba, Bwana amefufuka 'kweli-kweli, naye amemtokea Simoni. Ikawa wao kuwapa habari ya mambo ya njiani, na jinsi alivyojlikana na wao katika kuuvunja mkate.

JUMANNE BAADA YA UFUFUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa Mwanayo mzaliwa pekee Yesu Kristo umeyashinda mauti, umetufungulia na lango la maisha ya milele ; sisi tu miguuni pako, twakutaka ya kwamba, kama neema yako ituongozavyo, wewe hututilia miyoni mwetu tamaa zilizo njema, tuwe sisi nasi kwa msaada wako wa daima kuzitimiliza sawasawa hizo tamaa ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 13. 26-41

NANYI ndugu zangu, watoto wa kizazi cha Iburahimu, nanyi kwenu mnaomcha Mwenyezi Mungu, habari ya wokofu huu imeletwa kwetu sisi. Kwani wale waketio Yerusalem, pamoja na wakubwa wao, kwa kuwa hawakumjua, wala *hawakufahamu* sauti za manabii zisomwazo kila sabatu, walizitimiza kwa kumhukumu. Nao ijpokuwa hawakuona kwake sababu ya kumuua, wakamwomba Pilato kwamba auawe. Basi walipokwisha kutimiza mambo yote aliyandikiwa, wakamshusha kumwondoza katika ule mti, wakamtia kaburini. Ila Mwenyezi Mungu akamfufua kumtoa kwa wafu : naye alionekana siku nyangi na wale waliopanda kwenda Yerusalem pamoja naye kutoka Galilaya, ambao ndio mashahidi wake mbele ya wenyeji sasa. Na sisi twawaleta ninyi habari njema ya ile ahadi waliopewa mababa, jinsi Mwenyezi Mungu alivyoitimiza ile ile kwetu sisi tulio watoto wao kwa kumfufua Yesu ; kama ilivyoadikwa katika zaburi ya pili, Wewe u mwanangu, mimi leo nimekuzaa. Na katika *habari ile* ya kumfufua kumtoa kwa wafu, asiurudie uharibifu tena, anena hivi, Nitawapa ninyi *baraka* za Daudi zilizo takatifu na uaminifu. Kwa kuwa yuaoema tena katika *zaburi* nyingine, Hutamtoa Mtakatifu waks awe kuharibika. Kwani Daudi baada ya yeze kulitumikia shauri la Mwenyezi Mungu katika kizazi

chake, yeze alilala, akawekwa pamoja na babaze, naye akawa kuharibika. Ila yeze aliyefufufuliwa na Mwenyezi Mungu hakuona uharibifu. Basi jambo hili na lijulkane kwenu ninyi ndugu zetu, ya kwamba, kwa mtu huyo mmehubiriwa msamaha wa dhambi : tena kwa yeze kila aaminiye amepewa haki katika mambo yale yote ambayo katika hayo sheria ya Musa haikuweza kumpa haki. Basi tunzeni, yasiwafikilie yale yaliyonenwa katika *vyno vya manabii* : Angalieni, enyi wenye kudharau, kastaajabuni, mwangamie, kwa kuwa mimi natenda kazi katika siku zenu, kazi ambayo ninyi hamtaiamini popote, ijapokuwa mtu mmoja kuwafunulia.

Injili. Luka 24. 36-48

BASI wa katika kusimulia maneno haya, mwenyewe bakasimama katikati yao, akawaambia, Amani na iwe kwenu. Wakafadhaika wakaingwa na hofu, ikawa kudhani kwamba yule warmwonaye ni roho. Akawaambia, Ni nini kufadhaika, tena ni nini kuondokewa na mawazo miyoni mwenu ? Niangalieni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi nafsi yangu. Nishikenishikeni mniangalie, kwani roho haina mwili na mifupa, kama mnionavyo nayo mimi. Akiisha kusema haya akawaonyesha mikono yake na miguu yake. Basi wali-pokuwa hawajasadiki kwa furaha waliyoona, wakali kustaajabu, akawaambia, Mna chakula hapa kilicho chote ? Wakampa kipande cha samaki wa kuoka na cha kitata cha asali, akavitwaa akala mbele yao. Basi akawaambia, Haya ndiyo maneno yangu niliyokuwa nikiwasimulia nikali pamoja nanyi ; ya kwamba imepasa kutimia mambo yote niliyoandikiwa mimi katika torati ya Musa na manabii na zaburi. Ndipo akawafunulia akili zao ili wapate kuelewa na maandiko. Akawaambia, Ndivyo ilivyoadikwa, na ndivyo ilivyompasa Kristo kupatikana na mambo haya, na kufufuka katika wafu kwa siku ya tatu ; na kuhubiriwa mataifa yote ya kutubu na kusamehewa madhambi kwa jina lake, mwanzo tangu Yerusalem. Ninyi ndinyi mashahidi katika mambo haya.

Sala

EWE Baba Mwenyezi, Mwanayo mzaliwa pekee ulitupa Eafe kwa makosa yetu, akasimame tena kwa kutupa haki ; ukubali ya kwamba tuitupe chachu ya uadui na uovu, hata iwe sisi kukutumikia daima kwa maisha safi katika kweli, kwa kustahili kwake yeye huyo Mwanayo, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Yohana 5. 4-12

KILA kilichoza liwa kuto kana na Mwenyezi Mungu chashinda hiyo dunia : na huku ndiko kushinda kulikoishinda dunia, nayo ni imani yetu. Naye ni nani aishindaye hiyo dunia, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mwenyezi Mungu ? Huyu ndiye aliye kuja kwa njia ya maji na damu, Yesu Kristo ; si katika hayo maji tu, lakini katika hayo maji na hiyo damu. Kisha ni yeye Roho ashuhudiaye, kwa sababu huyo Roho ndiye ile kweli. Kwa kuwa wako watatu washuhudiao mbinguni, ni yeye Baba, na hilo Neno, na huyo Roho Mtakatifu : na hao watatu ni kitu kimoja. Wako na watatu washuhudiao duniani, ni huyo Roho, na hayo maji, na hiyo damu : na hao watatu ni katika moja. Tukipokea ushuhuda wa wanadamu, ushuhuda wa Mwenyezi Mungu ni mkuu zaidi : maana, ushuhuda wa Mwenyezi Mungu ni huu, ya kwamba, amekwisha kushuhudia katika habari za Mwanawe. Yeye aaminiye kwake Mwana wa Mwenyezi Mungu anao huo ushuhuda ndani ya nafsi yake : yeye asiyewamini Mwenyezi Mungu amekwisha kumfanya kuwa mwongo ; kwa sababu hakua mini ule ushuhuda ambao Mwenyezi Mungu ameushuhudia katika habari za Mwanawe. Na ushuhuda ni huu, ya kwamba, Mwenyezi Mungu ametupa sisi uhai wa milele, na uhai huo ni katika Mwanawe. Yeye aliye naye huyo Mwana anao na huo uhai ; yeye asiyeh naye huyo Mwana wa Mwenyezi Mungu hana huo uhai.

Injili. Yohana 20. 19-23

BASI siku ile ile, nayo ni ya sabatu-mosi, kulipoku-chwa, ile milango imekwisha kufungwa pale wali-pokupo wanafunzi, maana kwa hofu waliyo nayo ya Mayahudi, akaenda Yesu akasimama katikati ; akawaambia, Amani iwe kwenu ! Aliposema hayo, akawao-nyesha mikono yake na ubavu wake. Ndipo wakafurahi wanafunzi kwa kumwona Bwana. Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu ! Kanja vile alivyonitura Baba, nami nawapeleka vivyo. Akisema haya akawavuvia, akawaambia, Twaeni Roho Mtakatifu. Kadiri ya watu mwasameheo madhambi, yamesamehewa kwao : kadiri ya watu mwazuilia madhambi, yamezui liwa kwao.

JUMAPILI YA PILI BAADA YA IDI YA UFUFUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, ulitupa Mwanayo mzaliwa pekee awe kwetu dhabihu kwa ajili ya dhambi, na kielelezo cha maisha ya uchaji-wa-Mungu ; utupe neema tupate kwendelea katika kuyapokea manufaa yake yasiyothaminika kwa asante nyingi sana, kisha na iwe sisi siku zote kujitia bidii ya kuzifua hatua zilizobarikiwa za maisha yake matakatifu sana ; kwa mwenyewe Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Petero 2. 19-25

JAMBO hili ni jema sana, ikiwa mtu kwa nia ilekeayo kwa Mungu kupata majonzi, kwa kupatikana na mateso yasiyo haki. Kwani, ikiwa mfanyakapo dhambi mwapi gwa makofii nanyi mwavumilia, mtapata sifa gani ? lakini mfanyakapo mema, ikiwa kupatikana na mateso, nanyi mwavumilia, jambo hili ni jema sana kwa Mungu. Kwani mliitiwa jambo lilo hilo : kwa kuwa Kristo naye alipatikana na mateso kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili kwamba mzifuate nyayo zake : ambaye hakufanya dhambi, wala haikupatikana hila kinywani mwake : ambaye, alipotukanwa yeye hakujibu matukano ; alipo-

patikana na mateso hakutoa makamio ; ila akajitegemeza kwake yeze aamuaye kwa haki : ambaye yeze nafsi yake akazichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya Mt, ili kwamba sisi hali tumesha kufa kwa hizo dhambi, tuwe hai kwa haki ; ambaye, kwa mapigo yake mlipozwa. Kwani mlikuwa mwapotea kama kondoo ; lakini sasa mmerejea kwa huyo Mchunga wa nafsi zenu, *naye ndiye Mwangalizi wa nafsi zenu*.

Injili. Yohana 10. 11-16

MIMI ndimi mchunga mwema. Mchunga mwema muhuweka nchi uhai wake kwa ajili ya kondoo. Ila mtu mwajiriwa ambaye si mchunga, mtu yasiyokuwa mali yake wale kondoo, humwona mbwa-mwitu yuaja, akawacha kondoo akakimbia, yule mbwa-mwitu akawakamata na kuwatawanya-tawanya ; mwajiriwa hukimbia kwa kuwa ni mwajiriwa yeze, wala hayafikiri ya kondoo. Mimi ndimi mchunga mwema ; nami hao wangu nawajua, nao wanijua walio wangu, kama Babaangu anijuavyo, nami nimjuavyo Baba ; tena uhai wangu nauweka nchi kwa ajili ya kondoo. Nami nina kondoo wengine, wasiokuwa wa zizi hili ; nao hao imenipasa kuwaongoza, na sauti yangu wataisikia : kisha, watakuwa ni kundi moja, mchunga mmoja.

JUMAPILI YA TATU BAADA YA IDI YA UFUFUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, uwaonyeshaye mwanga wa kweli yako hao wakosao, ili wapate kurejea katika njia ya haki ; uwape wote walokubaliwa katika ushirika wa Dini ya Kikristo, wapate kukataa mambo yote yapingamanayo na ufuasi huo waifuatao, uwape na kuyaendelea yote ambayo kwamba yalingana nao ; kwa ajili ya Mwo-kozi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

Waraka. 1 Petero 2. 11-27

WAPENZI wangu, nataka kwenu mlibyo wageni na wasafiri, kajiepusheni na shauku za mwili, ambazo zapingana na nafsi ; mkawe na mwendo mzuri mbele ya

watu wa hao mataifa ; ili kwamba katika neno hilo ambalo wawasingizia ninyi kama mu watendaji-wa-uovu, iwe wao, kwa sababu ya vitendo vyenu vizuri wavionavyo, kumtukuzza Mwenyezi Mungu katika siku ya kuangaliwa. Jiwekeni kwa ajili ya Bwana chini ya kila amri iliyowekwa na binadamu : kwamba ni chini ya mfalme, kama ndiye *mbo* ; au kwamba ni chini ya maliwali, kama ndio walitumwa na yeze kwa mapatilizo ya watendaji-wa-uovu, na kwa sifa ya watendaji-wa-wema. Kwa kuwa ndivyo yalivyo mapenzi ya Mwenyezi Mungu, kwamba kwa kutenda wema mpate kuunyamazisha huo ujinga wa wana-damu wasio na akili : kama mu huru, ila si wenye kutumia uhuru wenu kama kifiniko cha uovu, lakini ni kama watumwa wa Mungu. Waheshimuni watu wote. Upendeni huo udugu. Mcheni Mungu. Mheshimuni mfalme.

Injili. Yohana 16. 16-22

YESU akaawaambia *wanafunzi wake*, Kuna kitambo kidogo hamnioni tena, kuna na kitambo kidogo cha pili nanyi mtaniona, kwa kuwa naenda zangu kwa Baba. Basi wakasema *wanafunzi wake* wengine wao kwa wao, Ni neno gani hilo atuambialo : Kuna kitambo kidogo wala hamnioni, kuna na kitambo kidogo tena, nanyi mtaniona ; na hilo, Kwa kuwa naenda zangu kwa Baba ? Basi wali-sema, Ni nini hilo anenalo : Kitambo kidogo ? Hatuyaji aneneayo. Aliuja Yesu kwamba wapenda kumuuliza, akaawaambia, Je, muulizanayo hivi ninyi kwa ninyi ndiyo haya : ya mimi kuwaambia, Kuna kitambo kidogo nanyi hamnioni ; kuna na kitambo kidogo cha pili nanyi mtaniona ? Ni kweli, ni kweli nawambia : ninyi mtaliza mwombolee, ulimwengu utafurahi : ninyi mtakuwa na majonzi, lakini yale majonzi yenu yatageuzwa furaha. Mwanamke azaapo huwa na majonzi, kwa kuwa imefika saa yake ; lakini akiisha kumzaa yule mwana, haukumbuki tena ule uchungu kwa ajili ya furaha afurahiazo mtu kuza-liwa ulimwenguni. Nanyi hivi sasa mna majonzi ; lakini nitawaona tena ; na miyo yenu itafurahi, na ile furaha yenu mtu hawaondolei kamwe.

JUMAPILI YA NNE BAADA YA IDI YA UFUFUO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, ni wewe pekeo uwezaye kuitawala mioyo ya ukaidi na mapenzi ya utukutu ya wanadamu wenyе dhambi; uwape watu wako kuyapenda uliyowaagiza, na kuvitamani ulivywapa ahadi, ili hivyo, hata humu katika mageule yote mbali-imbali ya ulimwengu, tuwe sisi kuituliza sana mioyo yetu huko kwenye furaha za kweli; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Yakobo 1. 17-21

KILA kipawa chema na kila karama ilio kamilifu hutoka juu, hushuka chini kutoka kwake yeze Baba wa nuru, ambaye kwake hapana mageule wala uvuli uletwao kwa kugeuka. Kwa kupenda kwake mwenyewe ametuzaa kwa neno la kweli, tupate kuwa sisi kama malimbuko ya viumbe vyake. Ndugu zangu niwapendao sana, mwajua *neno hili*. Kila binadamu na awe mwepesi wa kusikia, mpole wa kunena, mvumilivu wa hasira: kwani hasira ya mtu haitendi haki ya Mwenyezi Mungu. Kwa ajili ya hayo, kwa kuweka kando uchafu wote na wingi wa maovu, kapokeeni kwa upole lile neno lilolotuliwa, ambalo laweza kuziokoa nafsi zenu.

Injili. Yohana 16. 5-15

YESU akawaambia *wanafunzi wake*, Sasa naondoka naenda kwake aliyenileta; wala hapana mmoja wenu anjulizaye. Waenda wapi? Ila kwa hivyo niliywaaambia *maneno* haya, mmejawaa na huzuni mioyo yenu. Pamoja na haya, niwaambiayo ni kweli: yawafaa niondoke; kwani nisipoondoka, yule Msaada hatawajia: nami nikienda, nitampeleka kwenu. Naye huyo atakapokuja, atashuhudia uovu ulimwengu, kwa dhambi na kwa haki na kwa hukumu: kwa dhambi, kwa huwa hawaamini kwangu mimi; kwa haki, kwa kuwa naondoka, naenda kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa hukumu, kwa kuwa

mkubwa wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa. Bado nikali na maneno mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyachukua hivi sasa. Ila yeze atakapokuja, yule Roho wa kweli, atawaongoza awatie katika kweli yote; kwani hatanena kwa nafsi yake, ila kadiri ya atakayosikia atanena, na mambo yajayo atawajuvisha. Yule ndiye atakayenitokuza mimi: kwa kuwa atawaa katika yangu awajuvishe ninyi. Mambo yote aliyo nayo Baba ni yangu. Ndipo nikasema kwamba yule hutwaa katika yangu na kuwajuvisha ninyi.

*JUMAPILI YA TANO BAADA YA IDI YA UFUFUO**Sala*

EWE Bwana, ni wewe asili ya mema yote: basi utukirimu sisi waja wako tulio miguuni pako, tuvuviwe na wewe uliye Mtakatifu, ili tupewe kuyawaza mambo mema; utukirimu na kuongozwa na rehema yako, ili tupate kuyatenda: kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

Waraka. Yakobo 1. 22-27

ILA muwe watendaji wa neno, si wasikizi tu, na kuzidanganya nafsi zenu wenyewe. Kwa kuwa mtu awaye yote akiwa ni msikizi wa neno wala si mtendaji, huyo ni mfano wa mtu auangaliaye uso wake, aliovyaliwa nao, katika kioo: kwani aiangalia nafsi yake mwenyewe, kisha akaenda zake, mara husahau jinsi alivyojiona. Ila yeze achunguliyate katika sheria kamilifu, hiyo ya uhuru, na kudumu *vivyo*, naye si msikizi msahaulivu, lakini mtendaji wa ile kazi, huyo atakuwa na baraka katika kufanya kazi kwake. Mtu akijidhania kuwa ni mchaji-wa-Mungu, naye hafungi ulimi wake kwa lijamu, lakini adanganya moyo wake, mtu huyo uchaji-wa-Mungu wake ni bure. Uchaji-wa-Mungu safi usio najisi mbele za Mwenyezi Mungu Baba ni huu, kuwaendea hao wasio na baba na hao wajane waliosiliwa katika mateso yao, na kuilinda nafsi yake na dunia isiwe na taka.

Injili. Yohana 16. 23-33

NI kweli, ni kweli nawaambia, mtakapomtaka neno Baba atawapa kwa jina langu. Hivi hamijataka neno kwa jina langu : takeni, mtapewa ; furaha yenu ipate kutimizwa. Maneno haya nimesema nanyi kwa mifano ; ila saa yaja ambayo sitasema nanyi kwa mifano tena, ila habari ya Baba nitawaeleza waziwazi. Siku ile mtaomba kwa jina langu. Wala siwaambii kwamba nitanitaka Baba mimi kwa ajili yenu ; kwani mwenyewe Baba awapenda kwa vile mlivyonipenda mimi na kuniamini, ya kuwa mimi nilitoka kwa Baba. Nilitoka kwa Baba nikaingia ulimwenguni ; tena hivi nauacha ulimwengu, naenda zangu kwa Baba. Wakasema wanafunzi wake, Kumbe sasa wanena waziwazi, wala husemi mfano uwao wote. Sasa tumekujua kuwa mambo yote umeyajua ; wala huna haja ya kuulizwa na mtu. Kwa neno hili twaamini ya kuwa ilitoka kwa Mungu. Yesu akawaijibu, Hivi sasa mwaamini ? Hiyo ndiyo, yaja saa, tena imekwisha kufika, ya ninyi kwenda kutawanyikana, kila mtu kwao kwao, mniache mimi peke yangu : nami si peke yangu, kwa kuwa Baba yu pamoja nami. *Maneno* haya nimewaambia ninyi, ili ndani yangu muwe na amani. Ndani ya ulimwengu ninyi mna machungu : lakini tangamkeni ; mimi nimeushinda ulimwengu.

IDI YA KUPAA BWANA WETU

Sala

TWAKUOMBA, ewe Mwenyezi Mungu, utupe ya kwamba, kama hivyo sisi tulivoamini ya kuwa Mwanayo mzaliwa pekee Bwana wetu, Yesu Kristo, amepaa juu ameingia na mbinguni, iwe sisi nasi wenyewe kupaa vivyo kwa mioyo yetu na nia zetu, na kukaa huko pamoja naye daima ; ambaye yuaishi na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 1. 1-II

EWE Theofilo, nilitunga chuo cha kwanza cha yote Ealiyoanza Yesu kuyafanya na kufunza, hata siku aliypokewa juu, alipokuwa amekwisha kuwaachia maagizo, kwa Roho Mtakatifu, wale mitume ambaao aliwachagua ; wale ambaao aliaonyesha nafsi yake, kwa dalili nydingi za hakika, ali hai, baada ya kuteseka kwake, akionekana nao muda wa siku arobaini, akinena mambo ya ufalme wa Mungu : naye ali hali ya kukutana nao, akawausia kwamba wasitoke Yerusalem, ila waingojee ahadi ya Baba, ambayo, *alisema*, mmeisikia kwangu. Kwani Yohana alibatiza kwa maji kweli, kisha ninyi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu, baada ya siku chache tu. Basi walipokuwa wamekutana pamoa, wakamuuliza, wakasema, Je, Bwana, utawarejeza Israeli ufalme wao kwa siku hizi tulizo nazo ? Akawaambia, Haya si yenu ninyi kuyajua majira au nyakati ambazo ye ye Baba ameziweka katika amri yake mwenyewe. Lakini mtapata uwezo, Roho Mtakatifu atakapowajilia juu yenu, mtakuwa mashahidi wangu, katika Yerusalem, na Yudea yote, na Samaria, hata mwisho wa dunia. Alipokwisha kusema nao maneno hayo, ilikuwa kuangalia, akainuliwa juu, wingu likamchukua *likamwondo* machoni mwao. Na katika kung'aza kwao macho yao kuangalia mbinguni, alipokuwa akienda zake, mara hawa ndio, watu wawili waliovaa nguo nyeupe wakasimama nao ; wakiwaambia, Enyi watu wa Galilaya, kwani kusimama mkatazama mbinguni ? Yesu, ye ye huyo ambaye amepokewa juu mbinguni, kutoka kwenu, atarejea mfano ule ule, kama mliviyomwona akienda zake mbinguni.

Injili. Mariko 16. 14-20

BAADA yake akawatokea wale kumi na mmoja, Bwameketi chakulani ; akawasimangiza ya kule kutoamini kwao, na walivyo na ugumu mioyo yao ; kwa kuwa hawakuwaamini wale waliomwona ameinuka *kutoka kwa wafu*. Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mote, mka-vihubiri injili viumbi vyote. Mwenye kuamini na

kubatizwa atao koka : na mwenye kutoamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitawaandama walioamini : kwa jina langu watatoa pepo ; watasema kwa ndimi mpya-mpya. Wataokota nyoka, na watakapokunywa kiuacho chochote hakitawadhusu kabisa : watawaweka mikono yao wagognwa, nao watapoa. Basi ni hivi ; Bwana Yesu baada ya kusema nao akapokewa juu mbinguni, akaketi upande wa mikono wa kuume wa Mwenyezi Mungu. Na wale wakatoka, wakahubiri mwahali mote, yeze Bwana akitenda kazi pamoja nao, akilitia nguvu lile neno kwa ishara ziliandamiazo. Amina.

JUMAPILI ILIYOANDAMA BAADA YA IDI YA KUPAA

Sala

EWE Mungu, Mfalme wa Utukufu, wewe umemkuza Yesu Kristo Mwanayo mzaliwa pekee, umempaza hata ufalme wako wa mbinguni kwa furaha kuu ya kushinda ; twakuomba usituache pasipo na msaada, bali utuleteet Roho wako Mtakatifu, aje atutulize, apate kutuinua na kututia utukufuni mle mle, alimotangulia kupaa yeze Mwokozi wetu Kristo ; naye ndiye aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Waraka. 1 Petero 4. 7-II

ILA mwisho wa vitu vyote umekaribia : basi iweni na lakili kamili, mkeshe katika kuomba Mungu : zaidi ya mambo yote iweni na mapenzi ya kuzidi ninyi kwa ninyi ; kwa kuwa mapenzi yafinika wingi wa dhambi : huku mnikaribishana ninyi kwa ninyi pasipo kunung'unika : vivile kama kila mtu alivyopata kipawa ; mnikitumia kati yenu kama mawakili wema wa neema za Mungu zilizo za aina nydingi ; kwamba mtu anena, *na anene* kama vile mausio ya Mungu ; kwamba mtu atumika, *na atumike* kama katika nguvu alizopewa na Mwenyezi Mungu : ili kwamba Mwenyezi Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa njia ya Yesu Kristo, ambaye ni wake ule utukufu na uwezo hata milele na nilele. *Amina.*

Injili. Yohana 15. 26-16. 4

LAKINI atakapokuja yule Msada nitakayewaletea mimi kutoka kwa Baba, naye ndiye Roho wa kweli mwenye kutoka kwa Baba, huyo ndiye atakayenishuhudia. Ninyi nanyi mtashuhudia, kwa kuwa mu pamoja nami tangu mwanzo. *Maneno* haya nimewaambia msije mkakunguwazwa. Watawapigia marufuku ya misikiti ; kisha saa yaja ambayo kila mwenye kuwaa atajidhania kuwa amsongezea Mwenyezi Mungu ibada. Nayo haya watawafanyia, kwa kuwa hawakumjua Baba wala mimi. Ila *maneno* haya nimewaambia, ili kwamba itakapokuja saa yake mpate kuyakumbuka, ya kuwa haya ndiyo niliyo-waambia.

IDI YA PENTECOST

Sala

EWE Mungu, wewe kwa majira kama haya uliwafunza miyo yao watu wako waaminifu kwa kuwaletea mwanga wa Roho wako Mtakatifu ; utupe nasi kwa yeze Roho, tuwe na fahamu njema kwa mambo yote, na siku zote tuufurahie utulizi wake mtakatifu ; kwa kustahili kwake Yesu Kristo, Mwokozi wetu, ambaye yuaishi na kutawala pamoja nawe katika umoja wa yeze Roho, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 2. I-II

ILIPOTIMIA siku ya Pentecost, walikuwa pahali pamoja wote. Mara kukatoka kivumi ghafula mbinguni, kama kishindo cha upopo mkuu, kikajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Wakatokewa na ndimi kama *miali* ya moto zilizogawanywa, zikawakalia juu ya kila mmoja. Wakajawa na Roho Mtakatifu wote, wakaanza kunena kwa ndimi mbali-mbali, kama yeze Roho alivyowapa matamko. Palikuwa na Mayahudi watawa wakiketi Yerusalem, wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti hiyo iliposikiwa, mikutano ukakutana na kufadhaika, kwa kuwa kila mtu aliwasikia wakinena lugha yake mweywewe. Wakastaajabu wote na kupigwa na mshangao,

wakisemezana wao kwa wao, Tazameni, hawa wote wanenao si watu wa Galilaya? Imekuaje sisi kila mtu kusikia lugha yake mwenyewe, *ile ile tuliyovyaliva nayo?* Waparithi na Wamedi, na Waelamiti, na watu waketio Mesopotamia, na Yudea, na Kapadokia, na Ponto, na Asia, na Ferugia, na Pamfulia, na Misiri, na pande za Libia karibu ya Kurene, na wageni watokao Rumi, waliokuwa ni Mayahudi na waongofu, tena Wakiriti na Waarabu, twawasikia *watu* hawa wakisema kwa lugha zetu mambo matukufu ya Mwenyezi Mungu.

Injili. Yohana 14. 15-31

YESU akawaambia *wanafunzi wake*, Mkinipenda mtayashika maagizo yangu. Nami nitamtaka Baba, naye atawapa Msaada mwingine, apate kuwa pamoja nanyi milele, naye ni Roho wa kweli, ulimwengu usiowenza kumtwa, kwa kuwa haumwoni wala haumjui : ila ninyi mwamjua, kwa kuwa aketi kwenu, naye atakuwa ndani yenu. Sitawaacha mayatima : naja kwenu. Bado kitambo kidogo ulimwengu haunioni tena, ila ninyi mwaniiona; kwa hivyo niishivyo mimi nanyi mtaishi. Kwa siku ile intajua ninyi kwamba mimi ni ndani ya Babaangu, nanyi mu ndani yangu, nami ni ndani yenu. Mwenye kuwa nayo maagizo yangu na kuyashika, huyo ndiye anipendaye : naye mwenye kunipenda, atapendwa yeye na Babaangu, nami nitampenda, kisha nitamfunulia nafsi yangu. Yudasi akamwambia, *naye siye Mwisikariota*, Ewe Bwana, imekuaje wewe kutaka kujifunua kwetu sisi, wala si kwa ulimwengu? Yesu akamjibu akamwambia, Mtu akini-penda, atashika neno langu, na Babaangu atampenda; nasi tutakuja kwake, tufanye makao kwaké. Asiyenipenda hashiki maneno yangu : nalo neno mlinisikialo, si langu mimi, ni la Baba aliyenileta. *Maneno* haya nime-waambia nili kwenu. Lakini yule Msaada, yule Roho Mtakatifu atakayeletwa na Baba kwa jina langu, yeye atawafunza mambo yote, naye atawakumbusha niliyo-waambia yote. Nawaachia amani. Amani yangu na-wapa. Si kama upavyo ulimwengu hivyo niwapavyo mimi. Miyo yenu isifadhaike, wala isifanye hofu. Mlinisikia

nilivyowaambia, Naenenda, kisha nawajia. Kwamba mwanipenda, mngefurahi kwa vile nilivyosema, Naenda kwake Baba ; kwa kuwa yeye Baba ni mkubwa kuliko mimi. Nami nimewaambia sasa kabla yasijawa, ili, yatakapokwisha kuwa, mpate kuamini. Sina mengi tena nitakayowaambia, kwani yuaja nkubwa wa ulimwengu huu ; wala hana alilo nalo ndani yangu. Lakini ulimwengu upate kunijua kwamba nampenda Baba ; kisha kama vile alivyoniagiza Baba, ndivyo nitendavyo.

JUMATATU BAADA YA PENTECOST

Sala

EWE Mungu, wewe kwa majira kama haya uliwafunza miyo yao watu wako waaminifu kwa kuwaletea mwanga wa Roho wako Mtakatifu ; utupe nasi kwa yeye Roho tuwe na fahamu njema kwa mambo yote, na siku zote tuufurahie utilizi wake mtakatifu ; kwa kustahili kwake Yesu Kristo, Mwokozi wetu, ambaye yuaishi na kutawala pamoja nawe katika umoja wa yeye Roho, uli Mungu mimoja, milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo yya Mitume 10. 34-48

PETERO akafunua kinywa, akasema, Ni kweli nata-mbu ya kwamba Mwenyezi Mungu hana mapendeleo : lakini katika kila taifa, amchaye, na kutenda yenye haki, hukubaliwa na yeye. Lile neno alilowapelekia wana wa Israeli, akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo (yeye ndiye Bwana wa wote), neno hilo ninyi wenyewe mwaijua, lilitotangazwa katika nchi nzima ya Yudea likianza kutoka Galilaya, baada ya ubatizo ule uliohubiriwa na Yohana ; ni Yesu Mnazari, jinsi Mungu alivyomtia mafuta *nayo ni* Roho Mtakatifu na uwezo ; aliyekuwa akizunguka-zunguka akitenda vyema, na kuwapoza wote walioonewa na Shetani ; kwa kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja naye. Sisi tu mashahidi wa mambo hayo yote aliyoyafanya yeye katika nchi ya Mayahudi na ndani ya Yerusalem pia ; naye ni yeye waliyemuua, wakimtungika juu ya mti. Mtu huyo

Mwenyezi Mungu akamfufua siku ya tatu, na kumtoa adhihirishwe, si kwa wenyeji wote, lakiqi kwa wale mashahidi ambao Mwenyezi Mungu alitangulia kuwachagua, ni sisi, tuliokulua na kunywa pamoja naye baada ya' kufufuka kwake kutoka kwa wafu. Naye alituagiza kuwahubiri wenyeji, na kushuhudia ya kwamba ni huyo aliywewkwa na Mungu awe Mwamuzi wa walio hai hata na waliokufa. Manabii wote wamshuhudia yeyc, ya kwamba kwa jina lake yeze kila mta aaminie kwake atapata kusamehewa dhambi. Petero alipokuwa akinena maneno hayo, Roho Mtakatifu akawashukia wote waliokuwa wakilisikiza lile neno. Wale wa tohara walioamini, kadiri ya wale waliokuja pamoja na Petero, wakashangaa, kwa kuwa kipawa cha Roho Mtakatifu walimwagiwa watu wa hao mataifa nao. Kwani waliwasikia wakinena kwa lugha *mbali-imbali*, na kumtukaza Mwenyezi Mungu. Ndipo Petero akajibu, Ni nani awezaye kukataza maji, wasibatizwe watu hawa ambao wamempokea Roho Mtakatifu sawasawa na sisi? Basi akaamuru wabatizwe kwa jina la Yesu Kristo. Ndipo wakamtaka aketi nao *ingawa* siku chache.

Injili. Yohana 3. 16-21

MWENYEZI Mungu jinsi alivyopenda ulimwengu, amewapa *watu* Mwanawe mzaliwa pekee, kila mwenye kuamini kwake asipotee, awe na uzima wa milele. Kwani Mwenyezi Mungu hakumtuma Mwanawe kuja ulimwenguni kwamba akauhukumu ulimwengu, alimtuma ulimwengu upate kuokoka kwake. Mwenye kuamini kwake hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa kuwa hakuamini kwa jina la Mwanazaliwa pekee wa Mungu. Nayo ndiyo hukumu, hiyo, ya kuwa mwanga umeingia ulimwenguni, watu wakapenda giza zaidi ya mwanga, kwani zile kazi zao zilikuwa mbovu. Kwani kila mwenye kutenda ya aibu auchukia mwanga, naye hauendei mwanga, zisije zikakashifiwa zile kazi zake. Na mwenye kufanya kweli huuendea mwanga, ili kazi zake zipate kufanya wazi, ya kuwa zimetendwa katika Mungu.

JUMANNE BAADA YA PENTECOST

Sala

EWE Mungu, wewe kwa majira kama haya uliwafunza miyo yao watu wako waaminifu kwa kuwalettea mwanga wa Roho wako Mtakatifu, utupe nasi kwa yeze Roho tuwe na fahamu njema kwa mambo yote, na siku zote tuufurahie utilizi wake mtakatifu: kwa kustahili kwake Yesu Kristo, Mwokozi wetu, ambaye yuaishi na kutawala pamoja nawe katika umoja wa yeze Roho, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 8. 14-17

BASISI wale mitume waliokuwa ndani ya Jerusalemu Bwaliposikia ya kwamba Samaria imelipokea neno la Mwenyezi Mungu, wakawapelekea Petero na Yohana: ambao walipokwisha kuteremka kwao, wakawaombea, ili kwamba wapewe Roho Mtakatifu: kwani hajamshukia mta wao hata mmoja: isipokuwa wamebatizwa katika jina la Bwana Yesu. Ndipo wakawekeea mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

Injili. Yohana 10. 1-10

NI kweli, ni kweli nawaambia, asiyeingia kwa mlangoni katika zizi la kondoo, akweaye kwa pengine, ni mwivi huyo, tena ni mpokonyi. Na aingiaye kwa mlangoni ndiye mchunga wao kondoo. Yeye ndiye afunguliwaye mlango na mnganjezi, nao kondoo huisikia sauti yake, akawaita kondoo zake kila mmoja kwa jina lake, akawaongoza nje. Akiisha kuwatoa nje wale kondoo wake wote, huwatangulia mbele yao; nao kondoo humfuata, kwa kuwa waijua sauti yake. Na mta mgeni hawamfuati, wamkimbia, kwa kuwa hawazijui sauti za wageni. Simo hii aliwaambia Yesu, wala wasiyatambue ni maneno gani aliyonena nao. Basi akaawambia mara ya pili Yesu, Ni kweli, ni kweli nawaambia, mimi ndimi mlango wao kondoo. Waliokuja mbele yangu wote ni wevi, tena ni wapokonyi; na kondoo hawakuwasikia. Mimi ndio

mlango ; mtu atakapoingia kwangu mimi ataokoka, naye ataingia ndani akitoka nje, na malisha atayaona. Mwivi haji ila kwa kuiba na kuchinja na kuangamiza : mimi nilikuja wapate kuwa na uzima, kisha wawe nao kwa wingi zaidi.

JUMAPILI YA UTATU

Sala

E WE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, wewe huna mwanzo huna mwisho ; nawe umetupa neema sisi watu wako, ya kuukubali utukufu wa Utatu wako usio mwanzo wala mwisho, kwa tulivyoikiri imani ya kweli ; umetupa na kuuabudu ule Umoja kwa tulivyovikwa uwezo wa Uungu mtukufu ; twakuomba sana, utudumishe mumu katika imara ya imani hii, utukinge daima na kila uovu ; nawe ndiwe uihiye na kutawala, uli Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Badala ya Waraka. Ufunuo 4. 1-11

B AADA ya mambo hayo niliona, na huo ndio, mlanga bukafunguka katika hizo mbingu, na sauti ya kwanza niliyoisikia, sauti kama vile ya baragumu, ikinena nami, mmoja asemaye, Kwea huku, nami nitakuonyesha mambo hayo ambayo hayana budi yatakuwako baadaye. Mara nilikuwa katika Roho : na hicho ndicho, kiti-cha-enzi kikawekwa mbinguni, na mmoja ameketi juu ya kile kiti ; na yeze aliyeketi alikuwa kuangaliwa mfano wa jiwe la jasipi na akiki : na kisiki-cha-mvua kilizunguka hicho kiti-cha-enzi, kuangaliwa mfano wa zumaradi. Tena viti ishirini na vinne vilikuwa vyazunguka hicho kiti-cha-enzi : na kati viti vile *niliwaona* wazee ishirini na wanne waketi, walikuwa wamevikwa mavao meupe ; na juu ya vichwa vyao *walikuwa na taji za dhahabu*. Na kile kiti-cha-enzi kilitoka umeme na sauti na radi. Tena taa saba za moto zilikuwa zawaka mbele ya kile kiti-cha-enzi, ambazo ndizo hizo Roho saba za Mwenyezi Mungu ; tena mbele ya kiti-cha-enzi *kilikuwako kitu* kama bahari yenye kuonya, mfano wa bilauri ; na katikati ya kiti-cha-

enzi na kando-kando ya kiti-cha-enzi, *walikuwako* nyama-wenye-uhai wanne waliokuwa wamejawa na macho mbele na nyuma. Na huyo nyama wa kwanza alikuwa mfano wa simba, na huyo nyama wa pili *alikuwa* mfano wa mwana-wa-*ng'ombe*, na huyo nyama wa tatu alikuwa na uso kama vile wa binadamu, na huyo nyama wa nne *alikuwa* mfano wa tai mwénye kuruka. Na hao nyama-wenye-uhai wanne kila mmoja wao alikuwa na mabawa sita, nao wamejawa na macho kotekote na ndani : nao hawapumziki mchana wala usiku, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mwenyezi Mungu, Mweza-wa-yote, aliyekuwapo, naye yupo, naye ndiye mwénye kuja. Kisha hapo, hao nyama-wenye-uhai watakapompa yeze aketiye katika kiti-cha-enzi utukufu na heshima na shukrani, yeze aliye hai hata milele na milele, ndipo hao wazee ishirini na wanne watakapopomoka mbele zake yeze mwénye kuketi katika kile kiti-cha-enzi, nao watamsujidua yeze aliye hai hata milele na milele, nao watazibwaga hizo taji zao mbele ya kiti-cha-enzi, wakisema, Wastahili wewe, Bwana wetu, nawe u Mwenyezi Mungu wetu, kuupokea huu utukufu na hii heshima na huu uwezo : kwa kuwa ni wewe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapendeleo yako vilikuwapo, kisha viakaumbwa.

Injili. Yohana 3. 1-15

D ALIKUWA na mtu mmoja katika Mafarisayo jina lake akiita Nikodemo, naye ni mkubwa katika Mayahudi. Huyo akamwenda *Yesu* usiku, akamwambia, Ewe Rabii, twakujua u mwalimu, umekuja kutoka kwa Mungu, kwani hapana aezaye kuzifanya ishara hizo ufanyazo wewe isipokuwa Mwenyezi Mungu yu pamoja naye. Yesu akamjibu akamwambia, Ni kweli, ni kweli, nakuambia, asipozaliwa mtu uzazi utokao juu, *asipozaliwa upya mtu*, hawezi kuuona ufalme wa Mwenyezi Mungu. Nikodemo akamwambia, Huwaje mtu kuzaliwa ali mzee ? Aweza kuingia mära ya pili tumboni mwa mamaye akazaliwa ? Yesu akamjibu, Ni kweli, ni kweli, nakuambia, asipozaliwa mtu kwa maji na Roho, hawezi kuuingia

ufalme wa Mwenyezi Mungu. Kilichozaaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaaliwa kwa Roho ni roho. Sione ajabu ya kuwa nimekuambia, Imewapasa kuzaliwa uzazi utokao juu, *kuzaliwa upya*. Upopo huvumia upendako, na sauti yake waisikia, ila huuoni utokeako, wala uendeako. Ndivyo awavyo kila aliyezaliwa kwake Roho. Nikodemoo akamjibu, akamwambia, Mambo haya huwaje, hata yakawa hiyo? Yesu akamjibu akamwambia, Wewe u mwalimu wa Isiraeli, na haya hayakuelei? Ni kweli, ni kweli, nakuambia, Sisi twanena tuyauyayo; twashuhudia tuliyoyaona, wala ushuhuda wetu hamuukubali. Kwamba nimewaambia ya duniani msiamini, mtaaminije nikawaambia ya mbinguni? Tena hakuna aliyepaa akaenda mbinguni ila huyo aliyeshuka mbinguni, naye huyo ni Mwana wa binadamu mwenye kuwako mbinguni. Tena kama Musa alivyomwinua nyoka katika bara, imempasa Mwana wa binadamu kuinuliwa vivyo: ili kwamba kila mwenye kuamini kwake awe na uzima wa milele.

JUMAPILI YA KWANZA BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mungu, wewe ndiwe nguvu za wakutumainio; Uzukubali sala setu kwa rehema: nawe kwa vile huu udhaifu wa binadamu usiviyoweza kutenda neno jema liwalo lote pasipokuwa na wewe, utupe msaada wa neema yako, ili kwamba sisi kwa kuyatimiza maagizo yako, tukupendeze huku kwa maombi yetu na huku kwa vitendo yetu; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Yohana 4. 7-21

WAPENZI wangu, na tupendane sisi kwa sisi: kwa sababu mapenzi yametokana na Mwenyezi Mungu; na kila apendaye amezaliwa kwa kutokana na Mwenyezi Mungu, kisha amjua Mwenyezi Mungu. Yeye asiyependa hamjui Mwenyezi Mungu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni mapenzi. Katika neno hili hayo mapenzi ya Mwenyezi Mungu yamefanywa wazi ndani yetu sisi, ya kwamba Mwenyezi Mungu amemtuma Mwanawee mza-

liwa pekee aingie duniani, ili kwamba tupate kuwa hai kwa yeye. Katika jambo hili ndiyo mapenzi, si kwamba sisi tulimpenda Mwenyezi Mungu, lakini kwamba yeye alitupenda sisi, kisha akamtuma Mwanawee *awe dhabihi* kwa ajili ya dhambi setu. Wapenzi wangu, kwamba Mwenyezi Mungu alitupenda sisi jinsi hiyo, imetupasa kupendana sisi kwa sisi. Hapana aliywemwona Mungu kabisa: ikiwa twapendana sisi kwa sisi, Mwenyezi Mungu yuakaa ndani yetu, na mapenzi yake yamekamilika ndani yetu: katika neno hili twajua ya kwamba twakaa ndani yake, na yeye ndani yetu, kwa sababu ametupa katika Roho wake. Nasi tumeona na kushuhudia ya kwamba yeye Baba amemtuma Mwana, awe Mwokozi wa dunia. Awaye yote atakayekiri ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu yuakaa ndani yake, na yeye ndani ya Mwenyezi Mungu. Nasi twajua kisha tumekwisha kuyaamini hayo mapenzi Mwenyezi Mungu aliyo nayo ndani yetu. Mwenyezi Mungu ni mapenzi; na yeye akaaye katika mapenzi yuakaa ndani ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu yuakaa ndani yake yeye. Katika neno hili mapenzi yamekamilika kwetu sisi, ili kwamba tuwe na nafasi katika hiyo siku ya hukumu; kwa sababu vivile kama yeye alivyo, nasi tu vivyo katika dunia hii. Hapana hofu katika mapenzi: lakini mapenzi yaliyokamilika yatupa hofu iwe nje, kwa sababu hofu ina adhabu; na yeye aliye na hofu hakukamilika katika mapenzi. Sisi twampenda, kwa sababu yeye alitupenda sisi kwanza. Akiwa mtu kusema, Nampenda Mwenyezi Mungu, naye amchukia nduguye, ni mwongo; kwani yeye asiyempenda nduguye ambaye amemwona, hawezikumpenda Mwenyezi Mungu ambaye hakumwona. Nasi tuna mausio haya yatokayo kwake, ya kwamba yeye ampendaye Mwenyezi Mungu, na ampende na nduguye.

Injili. Luka 16. 19-31

PALIKUWA na mtu mmoja mwenye mali, akivaa nguo za rangi ya zambarau na katani njema, akitafuna raha na kufuata anasa daima: tena palikuwa na maskini, jina

lake akiitwa Lazaro, aliyebwagwa mlangoni pake, yuna vidonda vingi, huku akitarmani kushiba viangukavyo mezani pa tajiri : hata wakaenda mbwa wakarambamra vidonda vyake. Baadaye yule maskini akafa, akachukuliwa na malaika, wakaenda naye wakamtia katika kifua cha Iburahimu. Na yule tajiri naye akafa, akazikwa. Akavua macho kule kuzimu, naye ali matesoni, akamwona Iburahimu kwa mbali, na Lazaro ali kifuani mwake. Akainua sauti, akasema, Ewe baba Iburahimu, nihurumie, umpeleke Lazaro ili achovye maji ncha ya kidole chake, aje aniburudishe huu ulimi wangu ; kwani nateswa katika mwali huu wa moto. Iburahimu akamwambia, Ewe mwanangu, kumbuka kwamba mambo yako mema uliyapokea hapo ulipokuwa hai duniani, na Lazaro naye vivyo alipatikana na mabaya : naye sasa yuatuzwa hapa, na wewe waumizwa. Na juu ya haya yote, kwetu na kwenu pametiwa shimo kuu katikati, ili kwamba watakao kutoka huku kupertia kwenu wasiweze, na huko kwenu watu wasivukie huku. Akamwambia, Basi, nakuomba, baba, umpeleke nyumbani kwa babaangu, kwani nina ndugu zangu watu watano, aende akawashuhudie, wasije wao wakaingia pahali hapa pa mateso. Iburahimu akamwambia, Musa wanaye, na manabii wanao ; na wawasikize wao. Akamwambia, La, baba Iburahimu, lakini watakapokwendewa na mtu atokaye kuzimu watatubu. Akamwambia, Wasipomsikiza Musa na manabii, hawatashika maneno ya mtu hata atokaye kuzimu.

JUMAPILI YA PILI BAADA YA UTATU

Sala

EWE Bwana, wewe huachi daima kuwasaidia na kuwaongoza hao uwakubalio kuwalea katika imara ya hofu yako na mapenzi yako : utulinde sisi, twakuomba, katika hifadhi ya uangalizi wako wema, utuweke hali ya kulihofu na kulipenda daima jina lako takatifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Yohana 3. 13-24

MSISTAAJABU, ndugu zangu, dunia ikiwachukia ninyi. Sisi twajua ya kwamba tumekwisha kupita kutoka mautini na kuingia katika uhai, kwa sababu twwapenda hao ndugu. Yeye asiyependa yuakaa katika mauti. Kila mtu amchukiaye nduguye ni muuaji : nanyi mwajua ya kwamba hápana muuaji aliye na uhai wa milele wenye kukaa ndani yake. Kwa neno hili twajua mapenzi, kwa kuwa yeye aliweka nafsi yake nchi kwa ajili yetu sisi : nasi imetupasa kuweka nafsi zetu nchi kwa ajili ya hao ndugu. Ila yeye aliye na vitu-vipasavyo-maisha ya dunia hii, kisha akamwona nduguye ni mwenye kuhitaji, naye akazifunga huruma zake zisimfikilie, hayo mapenzi ya Mwenyezi Mungu yakaaje ndani yake huyo ? Watoto wangu wadogo, tusipende kwa neno wala kwa ulimi, lakini katika kazi na kweli. Kwa neno hili tutajua ya kwamba twatokaha na ile kweli, na kuihakikia mioyo yetu mbele zake, katika neno hilo ambalo hiyo mioyo yetu yatuonea makosa ; kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu, naye ayajua mambo yote. Wapenzi wangu, ikiwa hiyo mioyo yetu haituonei makosa, tume-kuwa na nafasi upande wa Mwenyezi Mungu ; na kila tutakalomba twapokea kwake, kwa sababu twayashika mausio yake, kisha twafanya mambo hayo yapendezayo mbele zake. Na mausio yake ni haya, kwamba tuamini kwa jina la Mwanawе Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi, vivile kama alivyotuusia yeye. Naye ayashikaye mausio yake yuakaa ndani yake, naye ndani yake yeye. Na kwa neno hili twajua ya kwamba anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.

Injili. Luka 14. 16-24

AKAMWAMBIA, Mtu mmoja alikuwa amefanya karamu kuu, akaalika watu wengi. Hata wakati wa kula chakula akamtuma mtumwa wake kwenda kuwaita wale walioalkwa, Njoni, kwa kuwa vyakula viko tayari. Wakaanza kutoa udhuru wote kwa nia moja. Wa kwanza akamwambia, Nimenunua shamba, nami sharti

niende nikaliangalie : tafadhalii unisamehe. Akasema mwingine, Nimenunu ng'ombe jozi tano, nami naenda kuzijaribu : tafadhalii unisamehe. Mwingine akasema, Nimeoa mke, ndipo nami nisipate kuja. Akaenda yule mtumwa, akampa habari bwana wake ya mambo haya. Ndipo akakasirika yule mwenye-nyumba, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi, uende njia kuu na mitaa ya mji, ukawatwae maskini na vigutu na vipofu na viguu, uje nao uwatiae ndani. Akasema yule mtumwa, Bwana, hayo uliyoagiza yansha kutendeka ; hata sasa ikaliko nafasi. Yule bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende njia za mashamba na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kuja tele. Kwani nawaambia kwamba katika waume hao walioalikwa, hapana mmoja atakayeona chakula changu kamwe !

JUMAPILI YA TATU BAADA YA UTATU

Sala

EWE Bwana, twakuomba sana utsikize kwa rehema, Enawe uliotutia tamaa isiyo shaka ya kukuomba, utupe sisi kulindwa na kutulizwa kwa msaada wako wa nguvu katika hatari zote na mashaka yote : kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Petero 5. 5-II

NINYI nyote kajivisheni unyenyekevu, mpate kutumikiana ninyi kwa ninyi : kwa kuwa Mwenyezi Mungu awapinga wenyenye, ila wanyenyekevu huwapa neema. Jinyenyekezeni basi chini ya mkono ulio na ukuu wa Mwenyezi Mungu, ili kwamba awakuze ninyi wakati upasao ; huku mkimtupia juu yake ye ye fadhaa zenu zote, kwa kuwa ye ye afikiri kwa ajili yenu. Iweni na akili, mkakeshe ; huyo adui wenu Shetani, kama simba angurumaye, huenda huku na huku akimtafuta atakayemmiza ; naye mpingeni, mthubutike katika imani yenu, mkijua ya kwamba mateso yayo hayo yatimizwa katika ndugu zenu walio duniani. Naye Mwenyezi Mungu wa neema yote, ye ye aliyeaita ninyi ili mpate utukufu wake wa milele

katika Kristo Yesu, mkiisha kuteswa muda mchache, mwenyewe atawarejeza upya, na kuwathubutisha, na kuwatia nguvu, na kuwatia imara. Ni wake utukufu na uwezo hata milele na milele. *Amina.*

Injili. Luka 15. 1-10

BASI watozi wa ushuru na wenyenye dhambi walikuwa kumsongelea ili wamsikize pia wote. Ikawa kunung'unika Mafarisayo na waandishi, wakisema, Huyu yuawakubali wenyenye dhambi, tena yuala nao. Akawaambia mithali hii, akisema, Kwenu kuna mtu gani mwenyekondoo mia, naye akiwa amempotaa mmojawapo hawaachi wale tisa wa tisini mle barani, akaenda akamtafuta-tafuta yule aliyeptoea hata amwone ? Naye akiisha kumwona, hujitweka mabegani mwake kwa kufurahi. Kisha afikapo nyumbani kwake, huwaita rafikize na jirani, akawaambia, Furahiwени nami, kwa kuwa nimekwisha kumwona yule kondoo wangu aliyeptoea ! Nawaambia kwamba kutakuwa na furaha mbinguni vivyo hivyo kwa ajili ya mtu mmoja mwenyene dhambi atubuye, zaidi ya itakavyokuwa kwa watu tisa wa tisini wenye haki wasio haja ya kutubu. Au kuna mwanamke gani mwenyene rupia kumi, naye apotewapo na rupia moja, hawashi taa akafagia katika nyumba, akatafuta kwa bidii hata aione ? Hata akiisha kuiona, akawakusanya rafikize wake na wanawake jirani zake, akawaambia, Furahiwени nami, kwa kuwa nimeionaa rupia ile iliyonipotea ! Nawaambia hata kwa malaika zake Mwenyezi Mungu kuna furaha vivyo hivyo kwa ajili ya mtu mmoja mwenyene dhambi atubuye.

JUMAPILI YA NNE BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mungu, uwali daye wote wakutumainio, pasipokuwa na wewe hakuna' kilicho na nguvu, hakuna kitakatifu ; utuongezee rehema zako uzifanye nyangi kwetu, ili kwamba, kwa kuwa wewe ndiwe mtawala wetu na kiongozi chetu tupite katika mambo ya dunia kisha tusipotewe na mambo ya milele. Uyakubali haya, ewe

Baba wa mbinguni, kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu.
Amina.

Waraka. Warumi 8. 18-23

KWANI nahesabu ya kwamba mateso ya wakati huu wa sasa hayastahili kufananishwa na ule utukufu uta-kaofunuliwa kwetu sisi. Kwani maangalizi yake uumbaji hungojea ufunuo wa wana wa Mwenyezi Mungu. Kwani ule uumbaji uliwekwa chini ya udanganyifu, si kwa kutaka wenyewe, lakini ni kwa ajili ya yeye aliyeuweka *hivyo*, katika tumaini ya kwamba ule uumbaji wenyewe nao utafanya kuwa huru kutoka katika ule utumwa wa uharibifu, uufikilie uhuru wa utukufu wa wana wa Mwenyezi Mungu. Kwani twajua ya kwamba uumbaji mzima huuuga pamoja na kuona uchungu pamoja hata hivi sasa. Wala si hayo tu, lakini na sisi wenyewe pia tulio na malimbuko ya Roho, hata sisi wenyewe twaagua ndani ya nafsi zetu, tukikungojea kukubaliwu-kuwa-wana *kzetu*, maana, ni ukombozi wa mili yetu.

Injili. Luka 6. 36-42

BASI iweni na huruma, kama Babaenu naye alivyo na huruma. Msihukumuni, nanyi hamtahukumiwa : msilaumuni nanyi hamtaalaumiwa : waachieni watu, nanyi mtaachiwa. Toeni vitu, nanyi mtapewa ; kipimo chema, kimeshindiliwa na kusukwa-sukwa hata kime-mwagika tena, ndicho watakachowapa vifuani mwenu. Kwani kipimo mpimiacho ndicho mtakachokuja kupi-miwa. Akawaambia na mithali, Je, mtu aliye kipofu aweza kumwongoza kipofu mwensiwe? Ehe, hawa-taangukia shimonii wote wawili? Mwanafunzi hawi juu ya mwalimu wake, lakini kila aliye hitimu huwa kama mwalimu wake. Nawe hicho kitakataka kilicho ndani ya jicho la nduguyo wakiangaliliani, na boriti iliyo ndani ya jicho lako huna habari nayo! Au utapatataje kumwambia nduguyo, Ndugu yangu, niacha nikakutoe hicho kitakataka kilicho ndani ya jicho lako, nawe hiyo boriti iliyo ndani ya jicho lako, mbona huiangalii! Mnafiki wewe, jitoe kwanza boriti ya jichoni mwako, ndipo utakapoona

vyema kukitoa kitakataka kilicho ndani ya jicho la nduguyo.

JUMAPILI YA TANO BAADA YA UTATU

Sala

UKUBALI, ewe Bwana, twakuomba sana, ya kwamba mwendo wa ulimwengu ulekezwe na uongozi wako katika utulivu, hata hili kanisa lako likutumikie kwa furaha, katika hali ya uchaji-wa-Mungu na utulivu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Petero 3. 8-15

IWENI na nia mfano mmoja nyote, wenyewe kuhuru-imiana kwa upole, na wenyewe kupendana kama ndugu, na wenyewe huruma za ndani, na wenyewe miyo ya unyenye-kevu : si wenyewe kulipana uovu kwa uovu, au matukano kwa matukano ; lakini ni kinyume cha hayo mbarikiane ; kwa kuwa ndilo mliloitiwa, ili kwamba mrithi baraka. Kwani, yeye atakayeupenda uhai, na kuona siku zilizo njema, na auzuie ulimi wake na uovu, na midomo yake nayo na kule kusema kwa hila : na ajiepue na uovu, afanye ambalo ni jema ; na atafute amani, na kuiandama mbio. Kwa kuwa, macho ya Bwana ya juu yao watendao haki, na masikio yake yalekea maombi yao : ila uso wa Bwana ni juu ya hao watendao uovu. Naye ni nani atakayewafanyia viovu, mkiwa wenyewe bidii kwa yaliyo mema? Lakini ikiwa mwateswa nanyi kwa ajili ya haki, mu wenyewe heri : ila msiche kutisha kwao, wala msifa-dhaike ; ila mtakaseni yeye Kristo miyoni mwenu, kama ndiye Bwana.

Injili. Luka 5. 1-11

IKAWA ulipomsonga ule mikutano ili kusikiza maneno Iya Mungu, alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesarethi, akaona madau mawili yamekaa kando ya ziwa, wameshuka wavuvi, waosha nyavu zao. Akapanda katika madau hayo mojawapo, nalo ni la Simoni, aka-

mtaka alipeleke mbali kidogo na ufuo. Akaketi, ikawa kuwafunza makutano mumo dauni. Hata alipokwisha kunena maneno yake, akamwambia Simoni, Lipeleke hata kinani dau, mkatie nyavu zenu mvue numbi. Simoni akamjibu akamwambia, Bwana mkubwa, hivi tumeefanya kazi kucha hatukupata kitu : lakini kwa neno lako nitazitia nyavu. Hata wakiisha kufanya mambo yale wakapata samaki tumbi-tumbi, nyavu zao zikawa kuraruka : wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa dau la pili, wapate' kujua kuwasaidia ; wakaja, wakayajaza yale madaur yao tele, yote mawili, hata yakataka kuzama Akiisha kuona yale Simoni Petero, akaanguka magotini pake Yesu, akamwambia, Ondoka kwangu, kwa kuwa ni mtu mwenye dhambi, ewe Bwana. Kwani alistaajabu yeje na wote waliokuwa naye, kwa numbi ya samaki walivovua ; na Yakobo na Yohana wana wa Zebedi, vivyo, nao watu hao ni washirika wake Simoni. Yesu akamwambia Simoni, Usiche, mwanzo wa sasa utakuwa kuvua watu. Hata walipokwisha kuegesha madau yao pwani, wakaacha vyote, wakamfuata.

JUMAPILI YA SITA BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mungu, umewatengezea hao wakupendao mambo ambayo kwamba wema wake umeピta fahamu za binadamu, utumiminie ndani ya mioyo yetu mapenzi, namna ambayo kwa kukupenda wewe zaidi ya vyote tupate kuzifkililia ahadi zako, nazo zapita yote tuwezayo kuyatamani ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 6. 3-11

HAMJUI ya kwamba sisi, kadiri yetu tulibatizwa na kutiwa katika Yesu Kristo, tulibatizwa hata kuyafkililia mauti yake ? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ule ubatizo kufikilia mauti : ili kwamba, kama Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, na

sisi ni vivyo twendelee katika upya wa uhai. Kwani kwamba sisi tumekuwa wenye kuungwa naye katika mfano wa mauti yake, ni vivyo *tutaungwa naye kwa mfano wa kufufuka kwake* : maana, twalijua neno hili, ya kwamba, nafsi yetu ya kale ilisalibiwa pamoja naye, ili kwamba mwili wa dhambi uharibiwe, ili baadaye tusiitumikie tena dhambi ; kwani yeje aliyekufa ameepukana na dhambi. Basi, kwamba tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kwamba tutaishi pamoja naye : maana, twajua ya kwamba Kristo kwa kuwa amekwisha kufufuliwa kutoka kwa wafu, hafi tena : mauti hayatawali juu yake tena. Kwani vile alivyokufa, alizifilia dhambi mara moja basi : na vile aishivyo, yuaishi kwa Mwenyezi Mungu. Nanyi ni vivyo jihesabuni wenywewe kuwa mu wafu kweli-kweli kwa zile dhambi, kisha mu hai kwa Mwenyezi Mungu, katika Kristo Yesu, Bwana wetu.

Injili. Mathayo 5. 20-26

YESU akawaambia *wanafunzi wake ya kwamba*, Hiyo haki yenu isipozidi ya wana-wa-vyuoni na Mafarisayo, hamtauingia kamwe ufalme wa mbingu. Mmesikia kwamba waliambiwa watu wa kale, Usiue, na atakayeuwa atakuwa mtu wa kuhukumiwa ya mauti : ila mimi nawaambia ya kwamba kila mmoja atakayemkasirikia nduguye pasina sababu, huyu ndiye atakayekiwa mtu wa kuhukumiwa ; na atakayemwambia nduguye ya kumfylea atakuwa ni mtu wa baraza ; na atakayemwita mpuimbavu, utampasa moto wa jahanamu. Basi uwapo kakisongeza kile kipawa chako katika patolewapo sadaka, ukakumbuka hapo ya nduguyo kuwa na jambo kwako, kiache papo kipawa chako, mbele ya patolewapo sadaka, uende ; kwanza kapatane na nduguyo, ndipo uje wewe utoe kipawa chako. Uwe mwenye kusikizana na akudaiye upesi, ukali naye njiani, asije akakupeleka yule akudaiye kwa kadhi, naye akakupeleka kwa jumadari, ukatiwa na kifungoni. Ni kweli nakuambia, hutoki kamwe humo hata ulipe senti ya mwisho.

JUMAPILI YA SABA BAADA YA UTATU
Sala

EWE Bwana, uliye na uwezo wote na nguvu zote, mwenye kuanziliza na kukirimu vitu vyema vyote : uiyatie mapenzi ya jina lako ndani ya miyo yetu ; uikuze ndani yetu dini ya kweli, na kutulea katika hali ya wema uliotimia, nawe utuweke vivyo hivyo, kwa rehema zako kuu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 6. 19-23

NANENA kwa ki-binadamu, kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu : kwani kama mlivytanguliza via vyenu viwe watumwa wa uchafu, na wa maasia hata *kwendelea na* maasia ; ni vivyo sasa vitangulizeni via vyenu viwe watumwa wa haki hata *kuufikilia* utakatifu. Kwani mlipokuwa watumwa wa dhambi mlikuwa mahuru kwa *upande wa* haki. Wakati huo basi mlikuwa na matunda gani *katika mambo hayo* ambayo sasa mwayaonea haya ? kwani mwisho wa mambo hayo ni mauti. Ila hivi sasa mkiisha kufanywa mahuru na kutoptana na dhambi, na kuwa watumwa wa Mwenyezi Mungu, mnayo matunda yenu kuufikilia utakatifu, na mwisho *ni uzima* wa milele. Kwani mshahara wa dhambi ni mauti ; lakini kipawa chake Mwenyezi Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Injili. Mariko 8. 1-9

KATIKA siku zile, ulikuapo mukutano mkuu mara ya pili, nao wakakosa chakula, akawaita wanafunzi wake akawaambia, Nauonea huruma mukutano, kwa kuwa leo ni tatu wadumu pamoja nami hawana chakula : nami nitakapowapa ruhusa, kuwapeleka majumbani mwao na njaa, watazima miyo njiani ; na wengine wao watoka mbali. Wanafunzi wake wakamjibu, *Kama* hapa atapata wapi mtu kuwashibisha watu hawa mikate, hapa barani ? Akawauliza, mna mikate mingapi ? Wakasema, Saba. Akuamuru ule mukutano kuketi nchi ; akaitwa ile mikate saba, alipokwisha kushukuru akaivunja, ikawa kuwapa

wanafunzi wake kuwaandikia ; wakauandikia mukutano. Wana na samaki wadogo wachache ; akiisha kuwabarikia, akawaambia kuwaandikia na hawa. Wakala, wakashiba, wakaondoa na masaza ya vipande vilivyovunjika, kapu saba. Na waliokula walikuwa wapata watu elfu nne ; kisha akawapa ruhusa.

JUMAPILI YA NANE BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mungu, uangalizi wako usiopungua ndio upangao Emambo yote, ya mbinguni na ya duniani ; sisi tulio miguuni pako twakuomba utuepushie mambo yote yata-kayotudhuru ; utupe na vitu vyote vitakavyotufaa ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 8. 12-17

BASI kwa ajili ya hayo, ndugu zangu, tu wadeni, si kwa mwili, kuishi kwa *mambo ya* mwili : kwani ikiwa mwaishi kwa *mambo ya* mwili mwendelea kufa : ila mkivua vitendo vya mwili kwa roho mtakuwa hai. Kwani wote kadiri ya wale walioongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Kwani hamkuipokea roho ya utumwa tena *ifikiliayo* hofu : lakini mmeipokea roho ya kukubaliwa-kuwa-wana, ambayo kwa hiyo twapiga ukelele, *twasema*, Ewe Baba, Babaetu. Roho mwenyewe *naye* ashuhudia pamoja na roho zetu ya kwamba tu wana wa Mungu : ikiwa tu wana, basi tu warithi ; warithi wa Mungu, warithi pamoja na Kristo : ikiwa twateswa pamoja *naye*, ili kwamba tutukuzwe nasi pamoja *naye*.

Injili. Mathayo 7. 15-21

ILA jilinden na manabii wa uwongo, ambao wao waja kwenu wamevaa mavao ya kondoo, nao kwa ndani ni mbwa-mwitu wa kunyakua-nyakua. Kwa matunda yao mtawatambua. Je, ni kutunda zabibu mibani ? au tini ni kutunda katika imbaruti-mwitu ? Ni hivyo kila mti ulio

na tabia njema huzaa na matunda mema, na mti mwovu huzaa matunda maovu. Hauwezi mti wa tabia njema kuzaa matunda mabaya, wala mti mwovu kuzaa matunda mema. Kila mti usiozaa matunda mema hukatwa ukatupwa motoni. Basi ni hivyo, ni kwa matunda yao mtakavyowatambua wale. Si kila mmoja aniambiye, Bwana, Bwana, atakayeingia ndani ya ufalme wa mbinguni : lakini ni afanyaye mapenzi ya Babaangu aliye mbinguni.

JUMAPILI YA TISA BAADA YA UTATU

Sala

TWAKUOMBA sana Bwana, utupe moyo wa kuya-waza yafaayo yote na kuyatenda daima ; ili kwamba tungawa sisi hatuwezi kufanya neno lolote la haki pasipokuwa na wewe, lakini kwa kuwezeshwa na wewe tuishi kama upendavyo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Wakorintho 10. 1-13

KWANI sitaki ninyi, ndugu zangu, kutojua ya kwamba khao mababa yetu wote walikuwa chini ya lile wingu; kisha wote wakapita ndani ya bahari : nao wakabatizwa wote wawe wa Musa, ndani ya wingu tena ndani ya bahari : nao wote wakala chakula kile kimoja cha rohoni : tena wakanywa wote kinyewwa kile kimoja cha rohoni : kwani wakanywa katika mwamba wa rohoni ulioandamana nao : na mwamba huo ulikuwa ni Kristo. Lakini Mwenyezi Mungu hakupendezewa na wengi sana mionganoni mwao : kwani walitoweshwa jangwani. Basi mambo hayo yalikuwa ni vielelezo vyetu, ili kwamba tusiyatamani maovu kama wale walivyoyatamani nao. Wala msibudu sanamu, kama wengine mionganoni mwao walivyofanya : vivile kama ilivyoandikwa, Watu waliketi kula na kunywa, kisha wakainuka wacheze. Wala tusizini kama wengine mionganoni mwao walivyozini, wakaanguka siku moja watu elfu ishirini na tatu. Wala tusimjaribu Bwana, kama wengine nao mionganoni mwao

walivyomjaribu, nao wakauawa na wale nyoka. Wala msinung'unike, kama wengine nao mionganoni mwao walivyonung'unika, wakauawa na yule muuaji. Basi mambo hayo yote yaliwapata wao yawe ni vielelezo : nayo yalia-ndikwa kwa ajili ya kutuhofisha sisi, ambao tumefikiliwa na miisho ya zamani. Kwa ajili ya hayo ajidhaniye kwamba asimama na ajitunze asianguke. Hayakuwapata ninyi maonjo yasiyokuwa hayo ambayo binadamu ayawenza kuyahimili : ila Mwenyezi Mungu ni mwaminifu, naye hatawaacha ninyi kuonjwa zaidi ya hayo mwenzayo : lakini pamoja na hayo maonjo atafanya na njia ya kuokoka, mpare nguvu za kuhimili.

Injili. Luka 16. 1-9

YESU akawaambia wanafunzi wake : Palikuwa na mtu mmoja mwenye mali alikuwa na msimamizi wake, akashtakiwa kwake kuwa yuapoteza mali yake. Akamwita, akamwambia, Ni mambo gani hayo nisikiayo kwako ? Toa hesabu ya usimamizi wako, kwani huwezi tena kusimamia mali yangu. Yule msimamizi akasema moyoni mwake, Nifanyeje, na bwana wangu yuaninya ng'anya usimamizi ? Kulima, sina nguvu : kuomba watu, naona haya. Nimejua nitakalofanya, ili kwamba wakati niondolewapo katika usimamizi waje wanikaribishe majumbani mwao. Akawaita wale wadeni wa bwana wake waje kwake kila mmoja. Akamwambia yule wa kwanza, Wawiwa nini na bwana wangu ? Akamwambia, Kasiki mia za mafuta. Akamwambia, Twaa hiyo hati yako, uketi upesi uandike hamsini. Kisha akamwambia wa pili wake, Nawe wawiwa nini ? Akamwambia, Jizila mia za nganu. Akamwambia, Twaa hiyo hati yako uandike themanini. Yule bwana akamsifu msimamizi mwenye udhalimu, kwa vile alivyofanya akili ; kwa kuwa wana wa ulimwengu huu katika kizazi chao huwa na akili zaidi ya wana wa mwanga. Nami nawaambia, Fanyeni urafiki mumo katika mali ya udhalimu, ili kwamba yatakapokosekana hayo, waje wawakaribishe katika vivuli vya milele.

JUMAPILI YA KUMI BAADA YA UTATU

Sala

MASIKIO ya rehema zako, ewe Bwana, na yategeke kwa sala za watumishi wako walio miguuni pako ; kisha, ili kwamba wayapate wakuombayo, uwafanye wawe watu wa kukuomba kama yakupendezayo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Wakorintho 12. 1-11

BASI sasa ndugu zangu, sitaki ninyi kutojua habari za *vipawa vya rohoni*. Mwajua ya kwamba mlipokuwa mu watu wa hao mataifa, mlipotewa na kufuata wale sanamu wasio na sauti, vivile kama mlivyoongozwa. Kwa sababu hii nawajuvisha ninyi ya kwamba, hapana mtu anenaye katika Roho wa Mungu, mwenye kunena, Yesu ni anathema : tena hapana aezaye kunena, Yesu ni Bwana, isipokuwa katika Roho Mtakatifu. Basi ziko tofauti za *vipawa*, ila Roho ni *huyo mmoja*. Tena ziko tofauti za *mangojezi*, na Bwana ni *yeye mmoja*. Tena ziko tofauti za *jinsi za kazi*, ila Mungu ni *yeye mmoja* atendaye kazi zote katika wote. Na kila mmoja hupewa ufunuo wa Reho apate faida. Kwani mmoja hupewa neno la hekima kwa njia ya Roho : *mwingine hupewa* neno la maarifa katika *yeye Roho mmoja* : *mwingine hupewa imani* katika *yeye Roho mmoja* : *mwingine hupewa vipawa vya kupoza magonjwa* katika *yeye Roho mmoja* : *mwingine hupewa kutenda vitendo vya nguvu* : *mwingine hupewa unabii* : *mwingine kupambanua roho* : *mwingine namna za lugha* : *mwingine kufasiri lugha* : ila mambo haya yote ayatenda *yeye Roho mmoja*, na kumgawanya kila mtu mbali-*mbali* vivile kama apendavyo.

Injili. Luka 19. 41-48

HATA kupata kwake karibu alipouona mji, akau-lilia, akinena, Iau kwamba wayajua nawe, kwa hii siku ya leo, yapasayo amani yako ! lakini sasa yamekusichamania macho yako ! Kwani zitakukuta siku

watakazokuzungusha boma adui zako, wakuzingire na kukuzuia kote-kote ; tena watakupomosha na nchi wewe na wanayo ndani yako, wasisaze ndani yako jiwe lililo juu ya jiwe mwensiwe, kwa ajili ya hivyo usivyojuza zamani za kuangaliwa kwako. Akaingia hekaluni, akaanza kuwatoa wale wfafanyao biashara humo, akawaambia, Imeandikwa kwamba, Na nyumba yangu itakuwa nyumba ya kusali ; lakini ninyi mmeifanya ni pango ya wevi. Tena alikuwa akihubiri daima mle hekaluni. Ikawa makuhani wakuu na waandishi kutafuta *njia ya kumwangamiza*, wao na walio wakuu katika wenyeji : wasione la kutenda, kwani jamii ya wenyeji walikuwa wakimtegemea kwa kumsikiza.

JUMAPILI YA KUMI NA MOJA BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mungu, wewe huonyesha hizo nguvu zako zisizo-wezekana katika rehema zako na huruma zako ; utupe kwa rehema kiasi hicho cha neema yako, ambacho kwamba kitatupa sisi kwenenda mbio katika *njia ya maagizo yako*, hata tuzifikilie ahadi za neema yako, na kufanywa tuwe na fungu katika mali zako za *mbinguni*, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Wakorintho 15. 1-11

SASA basi, ndugu zangu, nawajuvisha ninyi ile habari *Snjema niliyowahubiri*, ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mwasimama, nayo ni kwa hiyo mwaokolewa ; *nawajuvisha, nasema*, ni kwa maneno gani niliyowahubiri ninyi, mkiishika sana, isipokuwa mliamini bure. Kwani niliwapa ninyi kwanza ile ile niliyopokea nami, ya kwamba Kristo alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu, sawasawa na maandiko : tena kwamba alizikwa ; tena kwamba amefufuliwa siku ya tatu, sawasawa na maandiko ; tena kwamba alimtokea Kefa : kisha *akawatokea* hao kumi na wawili : kisha akawatokea ndugu wapata zaidi ya watu mia tano kwa mara moja, ambao wingi wao wako hata sasa, ila wengine *mionganii mwao* wamelala : kisha akamtokea Yakobo ; kisha *akawatokea* hao mitume wote ; mwisho

wa wote, kama ni mmoja asiyezaliwa wakati upasao, aknitokea mimi. Kwani mimi ni duni yao mitume, nisi yestahili kuitwa mitume, kwa maana, nililiudhi hilo kanisa la Mwenyezi Mungu. Ila kwa neema ya Mungu ni kama nilivyo ; na neema yake niliyopewa haikuwa ya bure ; lakini nilitaabikia kazi zaidi ya wale wote ; ila si mimi, lakini ni neema ya Mwenyezi Mungu iliyokuwa pamoja nami. Basi kwamba ni mimi, kwamba ni wao, ndivyo tuhubirivyo, tena ndivyo mlivyoamini.

Injili. Luka 18. 9-14

AKAWAAMBIA mithali na watu fulani waliojikinai Akana kwamba ni wenye haki wao, wakiwadharau wenginewe ; akawaambia mithali hii : Walikwea watu wawili kwenda kusali hekaluni : mmoja ni Farisayo, wa pili ni mtozaji-wa-ushuru. Yule Farisayo akasiñama akionba moyoni mwake kama haya : Mwenyezi Mungu, nakuambia asante, kwa kuwa mimi si mfano wa watu wenzangu : wanyang'anyi, wasio haki, waasherati, wala kama huyu mtozaji-wa-ushuru naye. Mimi hufunga juma siku mbili, tena hutoa zaka ushuru wa nipatavyo vyote. Na yule mtozaji alisimama kwa mbali, hasubutu hata kuinua macho yake mbinguni, akiijipiga makonde kifuanu, huku yuanena, Mwenyezi Mungu, niwelee radhi mimi mwenye dhambi. Nawaambia, huyu aliposhuka kwenda nyumbani kwake, alikuwa amepewa haki zaidi ya yule : kwa kuwa kila ajitukuzaye hutwezwa, ajitwezaye hutukuzwa.

JUMAPILI YA KUMI NA MBILI BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho, ewewe siku zote u mwepesi zaidi wa kusikia kuliko sisi wa kukuomba, umezoeca kutupa zaidi ya tutakavyo na yatufaavyo kupewa ; utumwagie juu yetu wingi wa rehemu yako, utusamehe hayo tuyachayo kwa kujijua kuwa na makosa, utupe na hivyo vitu vyema ambavyo sisi hatufai kuviomba, ila kwa afaavyo na atuombeavyo Mwanayo, Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

Warakka. 2 Wakorintho 3. 4-9

NASI tumetumaimi hivi kwa Mwenyezi Mungu kwa njia ya Kristo ; si kwamba twatosha sisi nafsi zetu kufikiri neno lolote kama ni lenye kutokana na nafsi zetu, lakini uteshelezo wetu umetokana na Mwenyezi Mungu : naye ndiye aliyetufanya sisi kutosha tuwe watumishi wa agano jipyä ; si wa andiko, lakini ni wa roho : kwani lile andiko huua, ila ile roho huleta uhai. Ila kwamba ule utumishi wa mauti, ulioandikwa na kuchorwa katika mawe, ulikuwa na utukufu, hata hao wana wa Isiraeli wasiweze kuutazama uso wa Musa sana kwa ajili ya utukufu wa uso wake ; *utukufu* uliokuwa watoweka : je, huo utumishi wa roho hautakuwa na utukufu afadhali ? Kwani kwamba utumishi wa hukumu-ya-adhabu ni utukufu, basi afadhali zaidi sana utumishi wa haki utazidi kuwa katika utukufu sana.

Injili. Mariko 7. 31-37

AKATOKA tena pande za Turo akapita ndani ya Sidoni akaenda hata bahari ya Galilaya kati-kati ya pande za Dekapoli. Wakamletea *mtu mmoja* kiziwi naye yuna kigugumizi, wakamtaka sana amweke mkono. Akamtwaa akamwepua na mkutano akaenda naye faragha, akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate aka-mgusa ulimi wake ; akiisha kuangalia juu mbinguni akaugua, akamwambia, Efatha, maana yake, Funguka. Mara yakafunguka masikio yake, kikalegea kifungo cha ulimi wake, ikawa kusema sawasawa. Akawausia kuto-mwambia mtu, lakini kadiri ya alivyowausia, wakazidi tu kuitangaza habari. Ikawa wao kushangaa mno mno, huku wanena, Pia ametenda vyema : viziwi yuawafanya kusikia, na mabubu kusema.

JUMAPILI YA KUMI NA TATTU BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, mwenye huruma, kwa kuwa ni kwa ihisani yako tu, wapatavyo watu wako waa-minifu kukutumikia kwa kufaa na kusifiwa ; utupe sisi,

twakuomba sana, ya kukutumikia kwa uaminifu sana hapa duniani, hata mwisho tusikose kuzifilikilia ahadi zako za mbinguni ; kwa kustahili kwake Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wagalatia 3. 16-22

BASI hizo ahadi zilinenwa kwa Iburahimu na kizazi chake. Hasemi, Vizazi, kama ni vingi : lakin kama ni kimoja, Na kizazi chako, ambacho ni Kristo. Basi nanena neno hili : Agano lilitangulia kuthubutishwa na Mwenyezi Mungu katika Kristo, ile sheria, iliyokuja miaka mia nne wa thelathini baadaye, hailibatili hata kuitangua ile ahadi. Kwani huo urithi ukiwa kwa njia ya sheria si wa ahadi tena : ila Mwenyezi Mungu alimpia Iburahimu kwa njia ya ahadi. Basi hiyo sheria ni nini ? Iliongeza na hiyo kwa ajili ya kutupa mpaka, hata ule uzao uliopewa ile ahadi utakapokuja, iliagizwa kwa njia ya malaika katika mkono wa mpatanishi. Basi mpatanishi hawi wa mmoja tu : ila Mwenyezi Mungu ni mmoja tu. Je, hiyo sheria imezishikia kinyume hizo ahadi za Mwenyezi Mungu ? La, hasha : kwani kwamba sheria ilitolewa iwezayo kuleta uhai, hapana shaka haki ingekuwa kwa njia ya sheria. Lakini maandiko yamevifunga yitu vyote viwe chini ya dhambi, ili kwamba hao waaminio wapewe ile ahadi itokayo kwa imani ilio kwa Yesu Kristo.

Injili. Luka 10. 23-37

RAHA ndao ambao macho yao yaona myaonayo ninyi ! Kwani hayo myaonayo ninyi nawaambia kwamba, na manabii na wafalme wengi wametamani kuyaona, wasiyone : nao wametamani kuyasikia myasikiayo ninyi, wala hawakuyasikia. Wakati huo akainuka mwali mu mmoja wa torati, yuamwonja : akamuuliza, Mwalimu, nifanye neno gani hata niurithi uzima wa milele ? Akamwambia, Imeandikwaje katika torati ? wasomaje ? Akamjibu akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na roho yako yote, na nguvu zako zote, na nia yako yote : na mwenzio mpende kama nafsi

yako. Akamwambia, Umejibu haki : fanya haya nawe uitaishi. Naye akitaka kujipa haki, akamuuliza Yesu, Basi mwenzangu ni nani ? Yesu akajibu akasema, Mtu mmoja alishuka Yerusalem kwendwa Yeriko, akaangukia kati ya wevi, wakamvua nguo, wakamtia na jeraha, hata walipoondoka wakamwacha karibu ya kufa. Ikatukia mara hiyo kuhani mmoja kushuka kwa njia ile, alipo-mwona akapitia kando. Akatoka na Mlawi vivyo, alipopata pahali hapo akimwona akapitia kando. Lakini Msamaria mmoja katika kusafiri kwake akamwendea pale alipo, alimwona akaingiwa na huruma ; akasongea karibu, akamgangga jeraha zake, akamtia mafuta na divai ; akampandisha juu ya nyama wake, akaenda naye akampeleka katika nyumba ya wageni, akamtunza. Hata kwa siku ya pili alipoondoka akatoka dinari mbili akampa yule mwenye nyumba ya wageni, akamwambia, Mtunze vyema, na ufanyapo gharama zaidi, nitakaporejea nitakuja kukulipa. Ehe, katika hao watu watatu, ni yupi umwanye kuwa ni mwensiwe yule aliyeangukia kati ya wevi ? Akamwambia, Ni yule aliywonea huruma. Yesu akamwambia, Enenda ; nawe fanya vivyo.

JUMAPILI YA KUMI NA NNE BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho ; Utupe sisi kuongea imani, na matumaini, na kupenda-na ; tena kwamba tuvipate ulivyoviahidi, utupe kuyapenda uliyoyausia ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wagalatia 5. 16-24

ILA nasema, enendeni kwa *nguvu za Roho*, nanyi hamta-zitimiza shauku za mwili. Kwani huu mwili hutamani kwa *kushindana* na Roho, na Roho *kushindana* na mwili : kwani hizi zimepingamana wenyewe kwa wenyewe : ili msipate kuyafanya hayo mtakayo. Ila mkiongozwa na Roho, hamu chini ya sheria. Basi kazi za mwili zi wazi, nazo ni uzinifu, na uasherati, na uchafu, na ulanifu, na kuabudu sanamu, na uchawi, na uadui, na utesi, na vivu,

na hasira, na matata, na kufarikana, na uzuzi, na husuda, na uuaji, na ulevi, na mambo ya ngoma, na mengineyeo kama hayo : kuliko mambo hayo natangulia kuwaambia, vivile kama nilivyo sema wazi, ya kwamba hao watendao mambo kama hayo hawataurithi ufalme wa Mungu. Ila tunda la Roho nalo ni mapenzi, na furaha, na amani, na uvumilivu, na matengezo-ya-mambo, na utu-wema, na uaminifu, na upole, na kudhibiti-nafsi : hapana sheria juu ya mambo mfano wa haya : na hao walio wa Kristo Yesu wansha kuusalibu huo mwili pamoja na tamaa zake mbovu na shauku zake.

Injili. Luka 17. 11-19

KISHA ikawa katika kwenda kwake Yerusalem ali-kuwa kupita kati-kati ya Samaria na Galilaya : hata alipoingia katika kijiji kimoja, akaonana na wakoma watu kumi, wanawaume, wakasimama kwa mbali : wakainua sauti wakasema, Ewe Yesu, ewe bwana mkubwa, uture-hemu ! Alipowaona akawaambia, Enendeni mkajionyeshe kwa makuhani. Ikawa katika kuondoka kwao pale wakasafiwa. Mmoja katika wao alipojiona amepoa, akarudi, huku amsifu Mwenyezi Mungu kwa sauti kuu ; akaenda akapomoka kiuso-uso miguuni pake, huku aki-mwambia asante ; naye alikuwa Msamaria. Yesu aka-jibu akanena, Hawakutakaswa wote kumi ? Hao kenda wa wapi ? Je, hapana aliyeonekana kurudi kuja kumpa utukufu Mwenyezi Mungu isipokuwa huyu mgeni ? Kisha akamwambia, Inuka uende : imani yako imekuokoa.

JUMAPILI YA KUMI NA TANO BAADA YA UTATU

Sala

ULILINDE kanisa lako, twakuomba sana, ewe Bwana, kwa rehema zako za daima, na kwa kuwa unyonge wa binadamu pasipokuwa na wewe hauna budi kuanguka, utuweke salama daima kwa msaada wako, tupate kulindwa na kila uovu, utuongozes tuvifikilie vyote vitakavyotufaa kwa wokofu wetu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wagalatia 6. 11-18

ANGALIENI, jinsi zilivyo kubwa hizi harufu niwa-andikiazo kwa mkono wangu mwenyeewe. Kadiri ya hao watakao kuonekana vyema katika mambo ya mwili, hao wawashurutisha ninyi kupashwa tohara : ili kwamba wasiudhiwe kwa ajili ya msalaba wa Kristo, *sababu ni hiyo tu*. Kwani hata hao watahiriwao hawaishiki sheria we-nyewe : lakini wataka ninyi kutahiriwa ili kwamba wapate kujisifu katika mambo ya miili yenu. Ila iwe mbali nami kujisifu isipokuwa katika msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo dunia imesalibiwa kwangu mimi, na mimi kwa dunia. Kwani katika Kristo kutahiriwa si kitu wala kutotahiriwa, lakini ni kiumbe kipywa. Na kadiri ya hao watengenza miendo yao kwa cheo hiki, amani na iwe juu yao, na rehema, na juu ya Israeli wa Mwenyezi Mungu. Mwanzo wa sasa na mtu asimioneet taabu : kwani mimi nazichukua chomo za Bwana Yesu *zilizochomwa* katika mwili wangu. Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu, ndugu zangu. Amina.

Injili. Mathayo 6. 24-34

HAPANA mmoja awezaye kuwatumikia mabwana wawili, kwani ama atamchukia huyu ampende huyu, au atashikamana na huyu amdhara huyu. Hamwezi kuwatumikia Mungu na mali. Kwa ajili ya hayo nawaa-mibia ninyi : Msiaze-aze mno ya uhai wenu, mtakula nini, wala mtakunuya nini ; wala ya miili yenu, mtavaa nini. Je, ule uhai si bora zaidi ya chakula, na ule mwili si bora kuliko mavao ? Waangalieni nyuni wa angani, ya kuwa wao hawapandi, hawavuni, hawakusanyi maghalani, nao Babaenu wa mbinguni ndiye awalishaye. Je, ninyi hamu afadhalii zaidi ya wao ? Ila ni nani kwenu, naye kwa kule kuaza kwake aweza kukiiongeza kimo chake kiasi cha mkono mmoja ? Na yale mavao nayo, kwani kuyaaza-aza mno ? Yatunzeni maua ya kondeni, jinsi yameavyo : hayafanyi shughuli wala hayasuki : nami nawaambia ya kwamba Suleimani na utukufu wake wote, hakuva mavao

kama livaavyo ua mojawapo hayo. Na yale maua ya kondeni, ambayo yapatikana leo na kesho hutupwa mabivini *yakateketea*, kwamba Mwenyezi Mungu yuayavisha hivyo, hatazidi sana kuwavisha nanyi, enyi wachache wa imani? Basi msifanye kuaza-aza mno, mkisema, Tutakula nini? au, Tutakunywa nini? au, Tutavaa nini? Kwani yote haya hutafutwa na wale wa hao mataifa-taifa; kwani Babaenu wa mbinguni awajua ya kuwa ninyi mna haja nayo haya yote. Ila kwanza taftuteni ufalme wake Mwenyezi Mungu na wema wake, na haya yote mtaongezewa ninyi. Basi msiazee-zae ya kesho: kwani kesho itakuja iaze-aze ya nafsi yake. Kwani hutoshwa ile siku na maovu yake.

JUMAPILI YA KUMI NA SITA BAADA YA UTATU

Sala

TWAKUOMBA sana, ewe Bwana, huruma zako za daima na zilisafi kanisa lako na kuliweka salama; kisha kwa vile lisivyoweza kulindwa pasipokuwa na msaada wako, uzidi wewe kulilinda kwa kulipenda na kulitetea daima; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 3. 13-21

KWA ajili ya hayo nataka kwamba msife mioyo kwa sababu ya mateso yangu nilioy nayo kwa ajili yenu, nayo ndiyo utukufu wenu. Kwa sababu hii napiga magoti yangu mbele za Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa yeye imeitwa jina kila jamaa katika mbingu na juu ya nchi, ili kwamba awape ninyi, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, mwongezwe nguvu kwa njia ya Roho wake katika mtu wenu wa ndani: kwamba Kristo aketi mioyoni mwenu kwa njia ya imani *yenu*: ili kwamba ninyi, mkiisha kuwa na shina na msingi katika mapenzi, hata mweze kufikilia, pamoja na watakatifu wote, jinsi ulivyo upana na urefu, na yafikavyo juu na yaendavyo chini, na kuyafahamu mapenzi ya Kristo yapitayo fahamu, ili impate kujawa hata *kufikilia* kila kujaa kwa Mwenyezi Mungu. Sasa kwake yeye awezaye kutufanya mno mno kuliko yote tutakayo na tuwazayo, sawasawa na ule uweco

utendoa ndani yetu, kwake yeye na uwe utukufu katika kanisa na katika Kristo Yesu vizazi vyote milele na milele. *Amina.*

Injili. Luka 7. 11-17

HATA baada ya haya punde, akaenda mji mmoja jina lake ukiitia Naini, naye ameandamwa na wengi katika wanafunzi wake na mukutano mkuu wa watu wengine. Hata alipouputa karibu ule mji, langoni pake, huyu ndiyé, maiti yuachukuliwa nje, ni mwana wa pekee wa mamaye, naye ni mjane, na watu wa mji wengi wali pamoja naye. Bwana alipomwona akamwonea huruma akamwambia, Usilie. Akasongea, akaigusa jeneza: wakasimama wale walioichukua. Akamwambia, Ewe kijana, nakuambia, Inu. Yule maiti akainuka, akaketi, akaanza kusema. Akampa mamaye. Wakaingiwa na hofu pia wote, ikawa kumtukuzwa Mwenyezi Mungu, huku wakisema, Kwetu ametokea nabii mkuu: tena, Mwenyezi Mungu amewangalia watu wake. Ikatoka ile habari yake, ikaenea Yudea yote na nchi zote za kando-kando.

JUMAPILI YA KUMI NA SABA BAADA YA UTATU

Sala

TWAKUOMBA, ewe Bwana, neema yako na idumu katika kututangulia na kutuandama, kisha na itutie bidii tuwe wenye kufanya kazi njema zote daima; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 4. 1-6

BASI mimi mfungwa katika Bwana, nawataka ninyi mwenende kama vipasavyo mwito wenu mliontiwa, kwa unyenyekevu wote wa moyo, na upole, na uvumilivu, mkiichukuana ninyi kwa ninyi katika mapenzi: huku mkitahidi kuuhiadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili ni mmoja, na Roho ni mmoja, vivile kama mlivyoitwa katika tumaini moja la mwito wenu: Bwana mmoja, na imani moja, na ubatizo mmoja, Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, ambaye yu juu ya wote, na kuenea wote, na ndani ya wote.

Injili. Luka 14. 1-11

KISHA ikawa alipoingia ndani ya nyumba ya mmojawapo katika wakuu wa Mafarisayo kwa siku ya sabatu ili kula chakula, nao walikuwa kumwangalia hivi ; naye huyo ndiye, mtu mmoja mwenye ugonjwa wa safura yu papo, amemkabili mbele yake. Yesu akajibu, akasema nao wale walimu wa torati na Mafarisayo, akawauliza, Je ni halali kupoza kwa siku ya sabatu, au la ? Wao wakanynamaza. Akamshika, akampoza, akampa ruhusa ya kuondoka. Kisha akajibu akawaambia, Ni nani katika ninyi aangukiwaye na ng'ombe wake au punda wake katika kisima, wala mara ile asimwopoe kwa siku ya sabatu ? Nao wasiweze kuyajibu maneno hayo. Basi akawaambia mithali wale walioitwa, akitunza wachaguayyo makao ya mbele ; akasema : Utakapoalikwa na mtu ukaenda arusini, usiketti makazi ya mbele ; isije ikawa amealikwa mtu mwenye kuheshimiwa zaidi ya wewe, kisha akaja yule aliyewaalika nyote, akakuambia, Mpishe huyu ! ukawa kushika pahali pa nyuma sana kwa kutahayari. Lakini wewe utakapoalikwa, enda ukakae pale nyuma, ili ajapo yule aliyekualika akuambie, Rafiki, songea mbele punde ; ndipo nawe utakapokuwa na heshima mbele ya watu wote walioketi nawe. Kwa kuwa kila mwenye kutukuza nafsi yake atatwezwa, na mwenye kutweza nafsi yake atatukuzwa.

JUMAPILI YA KUMI NA NANE BAADA YA UTATU

Sala

TWAKUOMBA, ewe Bwana, uwape watu wako neema ya kuyashinda majaribu ya ulimwengu na mwili na Ibilisi, na kukufuata wewe tu, Mungu pekeo wa kweli, kwa miyo iliyotakata na nia zilizosafika : kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Wakorintho 1. 4-8

NAMSHUKURU Mwenyezi Mungu wangu siku zote kwa ajili yenu, kwa sababu ya ile neema ya Mwenyezi Mungu mliyopewa ninyi katika Kristo Yesu : kwa kuwa

katika ye ye mmetajirishwa katika kila neno, katika kutamka kote na ujuzi wote ; vivile kama ushahidi wa Kristo ulivyo fanywa kuwa na nguvu ndani yenu ; hata ninyi hampungukiri na kipawa kilicho chote ; nanyi mu hali ya kungojea ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo ; naye ndiye atakayewafanya kuwa na nguvu hata mwisho, msiwe na uaili katika siku ya Bwana wetu Yesu Kristo.

Injili. Mathayo 22. 34-46

NA Mafarisayo waliposikia ya alivyowafumba kinywa wale Masadukai, wakakutanikia pamoja. Mmoja katika wao, *amali yake ni* mwali mu wa torati, akamuuliza kwa kumjaribu, akanena, Ewe Mwalimu, ni lipi katika maagizo lililo kubwa ndani ya torati ? Yesu akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako wote na nafsi yako yote na nia yako yote. Hilo ndilo agizo lililo kuu, tena ni la kwanza. Na la pili ni mfano wake, nalo ni hili : Mpende mwenzio kama *upendavyo* nafsi yako. Katika maagizo mawili hayo vimetundamana torati yote na manabii wote. Walipokwisha kukutanika Mafarisayo, Yesu akawauliza, yuanena, Mwaonaje ninyi katika Kristo ? ni Mwana wa nani ? Wakamwambia, Ni Mwana wa Daudi. Akawauliza, Ilikuaje basi Daudi katika Roho kumwita Bwana ye ye ? akinena, Bwana alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkonon wangu wa kuume, hata nikawaweke adui zako chini ya nyayo zako. Basi kwamba yule Daudi yuamwita Bwana, amekuwaje ni mwanawе naye ? Wala hapana mmoja aliyeweza kumjibu neno ; wala toka siku ile hapakuwa na mtu aliyesubutu kumuuliza neno tena.

JUMAPILI YA KUMI NA KENDA BAADA YA UTATU

Sala

WE Mungu, kwa kuwa pasipokuwa na wewe hatuwezi Eukupendeza, utupe kwa rehema ya kwamba Roho wako Mtakatifu atuongozwa na kututawala miyo yetu katika mambo yote, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 4. 17-32

BASI nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana, Bninyi msiende tena kama waendavyo watu wengine wa hao mataifa katika ubatili wa akili zao, wansha kutiwa giza fahamu zao, wakitengwa mbali na uhai wa Mwenyezi Mungu, kwa njia ya ujinga ulio ndani yao kwa sababu miyo yao imefanya ugumu: ambao wakiisha kufa ganzi walitoa nafsi zao na kujitua kwa uasherati wapate kuchuma katika uchafu wote na kutamani-tamani. Ila ninyi sivyo mlivyojfunza Kristo: ikiwa mmesikia na kufunzwa katika yehe, vivile kama kweli ilivyo katika Yesu: kwamba, kwa jinsi ya mambo ya maisha yenu ya kale, mvue na kuweka kando huyo binadamu aliye mkuukuu, aharibikaye kwa kufuata shauku za udanganyifu: mkafanywe watu wapya katika roho ya akili zenu, mkavikwe binadamu mpya, ambaye kwa jinsi ya Mungu ameumbwa katika haki na utakatifu wa ile kweli. Ndipo, mnikataa uwongo, kila mtu na anene yaliyo kweli na mwensiwe: kwa kuwa tu via wenye kwa wenye. Mkasirike, ila msifanye dhambi: msiliache jua kutua nanyi mna hasira: wala msimpe Shetani nafasi. Huyo aliyeiba na asiibe tena: ila afadhali afanye amali kwa mikono yake kutenda kilicho chema, ili kwamba awe na kitu cha kumpa huyo aliye mhitaji. Neno bovu na lisitoke vinywani, mwenu, lakini hilo lilio jema kwa majengo kama uhitaji ulivyo, ili kwamba lipate kuwapa neema wasikiao. Tena msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mwenyezi Mungu, ambaye ndani yake miltiwa muhuri hata ile siku ya ukombozi. Uchungu wote na hasira na ghadhabu na kelele na matukano, na viondolewe kwenu pamoja na maovu yote: ila muwe na ihisani ninyi kwa ninyi, na kuoneana huruma, na kusameheana ninyi kwa ninyi, vivile kama Mwenyezi Mungu naye alivyowasamehe ninyi katika Kristo.

Injili. Mathayo 9. 1-8

AKAPANDA chomboni akavuka, akaenda mjini kwake ayeye. Nawe angalia, wakamchukua mtu yuna ugo-njwa wa kupooza, amelala kitandani, wakaenda naye

kwake. Yesu alipoona imani yao akamwambia mwene ugonjwa wa kupooza, Moyo wako na uwe mkuu, mwanangu; dhambi zako zimesamehewa. Nao mara wengine katika wana-wa-vyuoni wakanena nafsini mwao, Huyu atukana Mungu. Akajua Yesu mawazo yao akawaambia, Ni ya nini ninyi kuaza mawazo mabaya miyoni mwenu? Kwani jepesi ni lipi, kusema, Zimesamehewa kwako dhambi zako, au kusema, Ondoka uenende? Lakini mpate kujua, ya kuwa yuna amri Mwana wa binadamu juu ya nchi ya kusamehe madhambi (ndipo hapo akamwambia yule mwene ugonjwa wa kupooza), Ondoka, uchukue na matandiko yako uende zako nyumbani kwako. Akasimama akaenda zake nyumbani kwake. Makutano waliopoona yale wakastaajabu, wakamtukuza Mwenyezi Mungu, awapaye binadamu amri jinsi hiyo.

JUMAPILI YA ISHIRINI BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe u mwingi wa rehema; kwa ihisani yako nyingi utulinde, twakuomba sana, na mambo yote yenye kutudhuru, hata sisi tukiwa tayari katika mili yetu na miyo yetu, tutimize yote kwa furaha uyatakayo wewe kwetu; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 5. 15-21

BASI angalieni kwa kujifunza sana mwendavyo, si kama wasio na akili, lakini kama wenye akili: na kuutumia ule wakati kwa akili, kwa kuwa siku hizi ni *siku* mbovu. Kwa sababu hii msiwe wapumbavu, lakini kafahamuni mapenzi ya Bwana jinsi yalivyo. Nanyi msilewe kwa divai, ambamo mna uasherati, lakini mkajawe na Roho: mkasemezane ninyi kwa ninyi na zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni, mkaimbwe na kufanya sauti nzuri miyoni mwenu kwa Bwana: huku mkipa shukrani Mwenyezi Mungu, naye ndiye Baba, daima, kwa ajili ya vitu vyote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo: huku mkinenyekanea ninyi kwa ninyi katika kicho cha Kristo.

Injili. Mathayo 22. 1-14

YESU akanena, Ufalme wa mbingu umefanana na mtu mmoja mfalme, aliyemfanya mwanawе arusi, aka-watuma watumwa wake wakawaite watakwao arusini : wakakataa kuja. Kisha akatuma watumwa wengine tena, akawaambia, Kawaambieni watakwao, Hiki ndicho, chakula changu nimekitengeza : ng'ombe zangu na vinono vyangu vimekwisha kuchinjwa, na vyote vimekuwa tayari : njoni arusini. Lakini waliyafanya mepesi maneno yake, wakaenda zao, mmoja kiungani kwake, wa pili katika bia-shara yake : na waliosalia wakawatwa watumwa wake wakawatenda maovu, wakawaua. Yule mfalme aliposikia hayo akakasirika, akatoa majeshi yake, akawaangamiza wale wauaji, na mji wao akauteketeza moto. Ndipo hapо akawaambia watumwa wake, Arusi i tayari, lakini walioitwa hawakustahili. Endeni basi katika maachano ya njia na kadiri ya mtakaona waineni arusini. Hata wakiisha kutoka wale watumwa, wakipata katika njia za nje, wakawakusanya wote kadiri ya waliowaona, kwamba ni wabaya, kwamba ni wema, arusi ikatengea kwa wageni. Lakini alipoingia mfalme kuwaangalia wageni, alimwona mtu mmoja mle hakuvaao vao la arusi. Akamwambia, Rafiki, ulingiaje humu nave huna vao la arusi? Akanyamaza kimya. Ndipo hapо mfalme akawaambia waandazi wa karamu, Mfungeni mikono na miguu mkamchukue mka-mtupe katika giza ya nje sana : kutakuwa na kilio huko na kukaza meno. Kwani wenye kuitwa ni wengi, wateule ndio wachache.

JUMAPILI YA ISHIRINI NA MOJA BAADA YA UTATU

Sala

TWAKUOMBA, ewe Bwana, uliye mwingu wa rehema, utupe watu wako waaminifu msamaha na amani, ili kwa kusafiwa na makosa yetu yote, tupate kukutumikia kwa utulivu wa moyo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 6. 10-20

MWANZO wa sasa, ndugu zangu, iweni na uwezo katika Bwana, na katika ubora wa nguvu zake. Vaeni silaha kamilifu ya Mwenyezi Mungu, kwamba mweze kusimama na kuupinga uzuzi wa Shetani. Kwa kuwa kupigana-pambaja kwetu si kupigana na nyama na damu, lakini na zile enzi, na hizo amri, na hao watawalao katika giza ya ulimwengu huu, na majeshi ya roho za uovu katika zile mbingu. Kwa ajili ya hayo twaeni silaha kamilifu ya Mwenyezi Mungu, ili kwamba mweze kushinda katika siku hiyo mbovu, tena mkiisha kutenda hayo yote, kusimama. Simameni basi, mkiisha kufungwa vyuno vyenu na ile kweli, mkiisha kuvalaa kigao-chakifuanı ambacho ni haki, miguu yenu ikivikwa maandalio ya habari njema ya amani : pamoja na yote hayo mkaainue na *kuichukua* ngao ya imani, kwa hiyo mtawewe kuizima mishare yote yenye moto ya huyo mwovu. Tena kajitwalieni chepeu-cha-chuma cha wokofu, na huo upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu : mkiomba Mungu kila wakati katika Roho, kwa njia ya maombi yote na kusali, na kukesha katika jambo hili, kwa kudumu kote na kunyenyekea kwa ajili ya watakatifu wote, na kwa ajili yangu mimi, ili kwamba nipewe matamko katika kufunua kinywa changu, nijuvishe ile siri ya habari njema kwa uthubutifu, ambayo kwa ajili yake hiyo ni mjumbe katika minyororo : ili kwambı ninene katika hiyo kwa kuthubutisha, kama inipasavyo kunena.

Injili. Yohana 4. 46-54

KULIKUWA na mtu mmoja wa ufalme, mwanawе Khawezi Kaperinaumu. Huyo aliposikia kwamba Yesu amekuja Galilaya kutoka Yudea, akaondoka akamwendea, akamtaka ashuke, aje akampoze mwanawе, kwani yuataka kufa. Basi Yesu akamwambia, Msipoona ishara na mambo ya ajabu, hamtaamini kamwe. Mtu wa ufalme akamwambia, Ewe Bwana, shuka asijafa mtoto wangu. Yesu akamwambia, Enenda, mwanayo yu hai. Akaliamini yule mtu lile neno aliloambiwa na Yesu,

akaenda. Naye yu katika kushuka, akatokewa na watumwa wake, wamwambia ya mtoto wake kuwa hai. Basi aka-wauliza habari ya saa alioanza kuona vyema. Ndipo wakamwambia, Jana wakati wa saa saba homa ilimwacha. Basi akajua babaye kwamba ndiyo saa ile alioyambwa na Yesu, Mwanayo yu hai; akaaminini, yeze na nyumba yake nzima. Hii ndiyo ishara ya pili tena aliofanya Yesu, alipokwisha kwenda Galilaya kutoka Yudea.

JUMAPILI YA ISHIRINI NA MBILI BAADA YA UTATU

Sala

HILO kanisa lako, nalo ndilo watu wa nyumba yako, twakuomba, ewe Bwana, ulilinde katika hali ya kukucha daima; lipate kulindwa na wewe na mashaka yawayo yote, kisha na liwe na bidii nyangi ya uchajii-wa-Mungu katika kukutumikia wewe kwa kazi njema, ili kulitokuza jina lako; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wafilipi I. 3-II

NAMSHUKURU Mwenyezi Mungu wangu kila niwakumbukapo, siku zote katika kuomba kwangu kote, ni kutamka kuomba kwangu kwa furaha kwa ajili yenu ninyi nyote, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuitangaza ile habari njema tangu siku ile ya kwanza hata hivi sasa; nikiamini neno hili sana, ya kwamba, yeze aliyeianza kazi njema ndani yenu, ataitimiliza hata siku ya Yesu Kristo: vivile kama ilivyo haki kwangu mimi kudhani hivi kwa ajili yenu ninyi nyote, kwa sababu ninanyi moyoni mwangu, kwa kuwa, ninyi nyote mmekuwa washirika wa neema pamoa nami katika kufungwa kwangu na katika kuitetea hiyo habari njema na kuitia nguvu. Mwenyezi Mungu ndiye shahidi wangu, jinsi niwatamaniyvo sana ninyi nyote katika huruma za ndani za Kristo Yesu. Nami naomba neno hili, ili kwamba mapenzi yenu yajae kwa wingi zaidi na zaidi katika ujuzi na katika fahamu yote; impate kuyapambanua hayo yaliyo na tofauti; ili muwe wa miyo safi pasina makunguwazo hata siku ya Kristo; mkijawa na matunda ya haki,

ambayo ni kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

Injili. Mathayo 18. 21-35

NDIPO hapo akamwendea Petero akamwambia, Ewe Bwana, ndugu yangu anikose mara nyingapi nami nikamsamehe? hata mara saba? Yesu akamwambia, Sikuambii ya kumsamehe mara saba; msamehe hata saba mara sabuni. Kwa ajili ya hayo ufalme wa mbingu umefanana na mtu mmoja mfalme aliyetaka hesabu kwa watumwaze. Alipoanza kufanya hesabu nao, akaletewa mtumwa mmoja awiwa talanto elfu kumi. Alipokosa cha kumlipa, bwana wake akaamuru auzwe, yeze na mkewe na wanawe na alivyo navyo vyote, na kulipwa awiwacho. Akaanguka nchi yule mtumwa, ikawa kumsujudia, yuanena, Bwana, nitwaa pole mimi, nitakuja nikulipe vyote. Akaingiwa na huruma bwana wa mtumwa yule, akamfungua, akamsamehe deni yake. Lakini alipotoka mtumwa huyo akamwona mmoja katika wajoli zake amwia dinari hamsini, akamshika shingo akanena, Nilipa nikuwiacho. Yule mjoliwe akaanguka nchi miguuni pake akamsihii akamsihii, yuanena, Nitwaa pole nami nitakuja nikulipe vyote. Asikubali, akaenda akamtupa kifungoni hata alipe awiwacho. Wajolize walipoona yaliyokuwa wakasikitika sana wakaenda wakamweleza bwana wao yote, kadiri ya yaliyokuwa. Ndipo hapo bwana wake akamwita, akamwambia, Ewe mtumwa mwovu wewe, nilikusamehe deni ile yote kwa ulivyonisiji: ehe, haikukupasa nawe kumhurumia mjoliyo, kama vile mimi nilivyokuhurumia? Akakasirika bwana wake, akamtia kwa watesaji, hata alipe kila awiwacho. Ndivyo na Babaangu wa mbinguni atakayowatenda ninyi, misiposameheana kila mtu na nduguye, katika ndani ya miyo yenu.

JUMAPILI YA ISHIRINI NA TATU BAADA YA UTATU

Sala

EWE Mungu, makimbilio yetu ni wewe, nguvu zetu ni wewe, nawe ndiwe asili ya wema wote; twakuomba sana uwe radhi kuyasikia kwa wepesi hayo likuombayo

kanisa lako kwa kutii, utupe ya kwamba tuyatakayo kwa uaminifu tuyapate kwa ukamilifu : kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Wafilipi 3. 17-21

NDUGU zangu, iweni wafuasi wa mimi pamoja, tena watunzeni sana hao waendao hivyo vivile kama sisi tulivyokuwa vielelezo kwenu. Kwani wengi waenda, ambao nimewaambia habari zao mara nydingi, na sasa nawaambia hata kwa kumwaga machozi, wamekuwa adui za msalaba wa Kristo : ambao mwisho wao ni kuangamia, ambao mungu wao ni matumbo yao ; na utukufu wao ni katika aibu yao, nao wavitumia vitu vya nchi. Kwani sisi, uwenyeji wetu ni katika mbingu ; ambazo kutoka hizo twamngeoja Mwokozi, *naye ni* Bwana Yesu Kristo : atakayeugeuza mwili huu wa unyonge wetu uwe mfanomojo na mwili wa utukufu wake, kadiri ya kutenda kwake awezavyo yeche hata kuvitweza vitu vyote viwe chini yake.

Injili. Mathayo 22. 15-22

NDIPO hapo wakaenda Mafarisayo wakafanya shauri la watakavyomtega kwa maneno. Wakawatumwa kwake wanafunzi wao, wao na mila ya Herode, kwenda kusema, Mwalimu, tumekujua u msema-kweli, na njia yake Mwenyezi Mungu waifunza kweli, wala humchi mtu awaye yote : kwani huoni nyuso za wanadamu. Basi tuambie, waonaje wewe ? Kumpa kodi Kaisari ni halali, si halali ? Akafahamu Yesu ule uovu wao, akanena, Kwani kunijaribu ninyi, wanafiki ? Nionyesheni fedha ya kodi. Wakamletea dinari. Akawauliza, Ni ya nani sura hii na anwani hii ? Wakamwambia, Ni ya Kaisari. Ndipo hapo akawaambia, Basi vya Kaisari mlipeni Kaisari, na vya Mwenyezi Mungu mlipeni Mwenyezi Mungu. Hata wakiisha kusikia neno lile wakastaaajabu, wakamwacha, wakaenda zao.

JUMAPILI YA ISHIRINI NA NNE BAADA YA UTATU
Sala

T'WAKUOMBA sana, ewe Bwana, utuondolee hatia zetu watu wako, ili sisi sote kwa wingi wa ihisani yako tufunguliwe vifungo vya makosa yetu yote tuliyokukosa kwa huu unyonge wetu. Utujalie haya, ewe Baba wa mbinguni, kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu, Mwo-kozi wetu Mwenye-baraka. *Amina.*

Waraka. Wakolosai I. 3-12

TWAMSHUKURU Mwenyezi Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, na kuwaombea ninyi siku zote, tukiisha kusikia *habari* ya imani yenu katika Kristo Yesu, na *habari* ya mapenzi yenu mliyo nayo kwa watakatifu wote, kwa ajili ya matumaini hayo mliyowekewa katika zile mbingu, ambayo mmejkwisha kusikia habari zake katika neno la kweli la ila habari njema, iliyowafikilia ninyi, vivile kama iliyyo katika dunia nzima, kwa kuzaa matunda na kuongea, vivile kama iliyvokuwa ndani yenu ninyi pia, tangu siku ile mliyoisikia ile neema ya Mungu na kuijua kwa hakika ; vivile kama mliyoyifunza kwa Epafara mjoli wetu mpendwa, naye ni mtumishi mwaminiyu wa Kristo kwa ajili yetu, naye ndiye aliyetufunulia mapenzi yenu mliyo nayo katika Roho. Kwa ajili ya hayo sisi nasi, tangu siku ile tuliposikia, hatuachi kuomba na kutaka kwa ajili yenu, ili kwamba mjawe na ujuzi wa mapenzi yake katika hekima yote na akili za rohoni, mwenende kama ipasavyo kwa Bwana kwa kupendeza sana kwa kuzaa matunda katika kila kazi njema, na kwa kuongea katika kumjua Mwenyezi Mungu ; mkiwezeshwa kwa kila nguvu sawasawa na ubora wa utukufu wake, hata *kufikilia* saburi yote na uvumilivu wote pamoja na furaha ; mkipshukuru yeche Baba, ambaye ametufanya sisi kustahili kupata fungu la urithi wa watakatifu katika zile nuru.

Injili. Mathayo 9. 18-26

YU katika kusema nao yale, naye, mara akaenda mtu mmoja mkubwa akamsujudia akinena, Binti wangu sasa hivi amefariki : lakini njoo wewe ukamweke mkonono,

atakuwa hai. Yesu akainuka akamwandama yule mtu, yeze na wanafunzi wake nao. Wakati huo mwanamke mmoja, atokwa na damu tokea muda wa miaka kumi na miwili, akamwendea kwa nyuma, akaugusa upindo wa nguo yake; kwani alinena nafsini mwake, Nikigusa na ingawa nguo yake, nitapoa niwe mzima. Lakini Yesu akageuka, na alipomwona akamwambia, Uwe na moyo mkuu, binti: imani yako imekupoza. Akaoa yule mwanamke akawa mzima tokea saa ile. Akaenda Yesu nyumbani kwa yule mtu mkubwa, akiwaona wapigao filimbi na watu walioutanika wafanya ghasia, ikawa kunena, Rudini nyuma, kwani hakufa msichana, amelala tu. Wakamdhihaki. Wakiisha kutolewa nje wale walio-kutanika, akaingia ndani akamshika mkono; akainuka yule msichana. Ikatoka habari yake ikaenea nchi ile yote.

JUMAPILI YA ISHIRINI NA TANO BAADA YA UTATU Sala

EWE Bwana, twakuomba sana, uwaamshe hao watu Ewako waaminifu, ili kwamba, kwa vile watakavyozaa kwa wingi matunda ya kazi njema, iwe wao kupata kufurahishwa na wewe vivyo kwa wingi; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Yeremia 23. 5-8

ANGALIENI, siku zaja, asema Yehova, ambazo *katika siku hizo nitamwinulia Daudi Chipukizi lenye haki, naye atatawala mfalme, naye atatenda kwa akili, naye atafanya hukumu na ulekevu katika nchi.* Siku zake Yuda ataokoka, na Isiraeli ataketi salama salimini: na jina lake atakaloitwa ni hili, Yehova ndiye hakl yetu. Kwa sababu hiyo, angalieni, siku zaja, anena Yehova, ambazo *katika siku hizo hawatasema tena maneno haya,* Kama Yehova alivyo hai, aliywakweza wana wa Isiraeli kutoka nchi ya Misiri; lakini *watasema,* Kama Yehova alivyo hai, yeze aliywakweza na kuwaongoza wa mbegu ya nyumba ya Isiraeli kutoka nchi ile ya kaskazini, na kutoka nchi zile zote nilizowachungia; nao wataketi nchi yao wenyewe.

Injili. Yohana 6. 5-14

BASI Yesu akainua macho yake, hata alipowaona ni wengu sana watu wamjiao, akamwambia Filipu, Tukanunue wapi mikate, hawa wapate kula? Nalo alilinenya kwa kumjaribu, kwani aliyajua mwenyewe atakayokuja kuyafanya. Filipu akamjibu, Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi kila mmoja wao akatwae kidogo. Mmoja katika wanafunzi wake, Andarea, nduguye Simoni Petero, akamwambia, Hapa pana kijana mmoja, yuna mikate mitano ya shairi, na samaki wawii iwadogo; lakini ni kitu gani hicho, cha kuwatoshya watu wengi hivi? Yesu akasema, Watengezeni watu waketi *nchi.* Napo palikuwa na majani mengi mabichi pahali hapo. Basi wakaketi, watu waime hesabu yao wapata elfu tano. Basi Yesu akaitwa mikate, hata aliposhukuru akawapa wanafunzi wake, nao *wakawagawanya walioketi,* na katika wale samaki vilevile, kadiri ya walivyotaka. Hata walipokwisha kushiba, akawaambia wanafunzi wake, Kusanyeni makombo yaliyosalia, kisipotee kitu. Basi wakayakusanya; wakajaza vikapu kumi na viwili, makombo yatokayo katika mikate mitano ya shairi, yamewasalia waliokula. Basi wale watu walipoona ishara aliyoifanya, wakasema, Huyu ndiye kweli nabii ajaye ulimwenguni.

IKadiri ya siku za Jumapili zilizobaki, kabla isijafika Jumapili ya Wakati wa Kuja, hutwaliwa Maweko ya Ibada ya Jumapili zile zilizorukizwa baada ya Idi ya Majfunuo, kwa hesabu ya zilizopungua *hapa.* Na Jumapili zikipungua, hayo yaliyozidi humu hurukizwa. Lakini Sala hii na Waraka huu na Injili hii hutumiwa daima katika siku ya Jumapili itangulilayo mbele ya Wakati wa Kuja.

IDI YA MTAKATIFU ANDAREA

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe ndiwe uliyempa neema yule mtrume wako mtakatifu, Andarea, nayo ikampa kuitika mwito wa Mwanayo Yesu Kristo kwa upesi, akamfua pasipo kukawia; utujalie sisi sote, ya kwamba

kwa hivyo tulivyoitwa na Neno lako takatifu, mwanzo wa sasa tujitoe nafsi zetu tuyatimize maagizo yako matakifu : kwa yeze huyo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Warumi 10. 9-21

UKIWA utamkiri Yesu kwa kinywa chako kuwa ndiye Bwana, tena kuamini katika moyo wako ya kwamba Mwenyezi Mungu amemwinua kumtoa kwa wafu, utaokoka : kwani kwa moyo mtu huamini aifkilie haki, na kwa kinywa hukiri aufkilie wokofu. Kwani maandiko yanena, Awaye yote atakayeamin kwake hataaibishwa. Kwani hapana tofauti katika Yahudi na Yunani : kwani *Bwana* yeze huyo mmoja ni Bwana wa wote, ni tajiri kwa wote watakoamlingana : kwani, Awaye yote atakayelingana jina la Bwana ataokoka. Je, watamlinganaje yeze ambaye hawaajaamini kwake ? nao wataaminije kwake yeze ambaye hawaajasikia ? nao watasikiae pasipo mhubiri ? Je, watahubirije wasipotumwa ? vivile kama ilivyoandikwa, A ! jinsi ilivyo mizuri miguu ya wale wahubirio habari njema ya amani, waletao habari njema ya mambo mema ! Lakini si wote walioitii ile habari njema. Kwani Isaya anena, Bwana, ni nani aliyeiamini habari yetu ? Basi hivi imani *huja* kwa njia ya kusikia, na kusikia *huja* kwa njia ya neno lake Kristo. Basi, nauliza, Je, hawakusikia ? Ehe, kweli, Sauti yao ilitoka na kuenea nchi yote ; na maneno yao *yalifika* hata ncha za ulimwengu. Lakini nauliza, Je, hawakuju Israeli ? Musa kwanza yuanena, Mimi nitawatia ninyi wivu kwa lisilo-kuwa taifa, nitawakasiri kwa taifa lisilo na akili. Kisha Isaya naye ni mthubutifu sana, na kunena, Nilipatikana na watu wasionitafuta : nikawa dhahiri kwa wale wasioniuliza. Ila juu ya Israeli anena, Mchana kuchwa nilinyosha mikono yangu kwa watu wasiotii, wenye kinyume.

Injili. Mathayo 4. 18-22

NAYE Yesu yuzunguka hivi kando-kando ya pwani ya bahari ya Galilaya akaona watu wawili, mtu na nduguye, Simoni aitwaye Petero na Andarea nduguye,

watupa kimia baharini, kwani ni wavuvi. Akawambia, Njoni mniandame nyuma yangu, nami nitawafanya muwe wavuvi wa watu. Nao wakaacha nyavu zao mara, wakamfuata. Kisha akaenenda mbele kutoka pale, akaona na wawili tena, mtu na nduguye, Yakobo mwana na Zebedi, na Yohana nduguye, wa ndani ya dau pamoja na Zebedi baba yao, watengeza nyavu zao ; akawaita. Nao wakaliacha mara lile dau, wakamwacha na baba yao, wakamfuata.

IDI YA MTAKATIFU THOMA MTUME

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho, Eni kwa ajili ya kuithubutisha zaidi hii imani wewe ulivyomwacha yule Thoma, mtume wako mtakatifu, aingiwe, na shaka juu ya kufufuka kwake Mwanayo ; utupe ya kwamba, jinsi tutakavyomwamini Mwanayo Yesu Kristo kwa ukamilifu sana, tusifanye tashwishi kwa neno liwalo lote : ili kwamba imani yetu isilaumiwe majira yoyote mbele zako. Nawe Bwana, utusikize kwa haya kwa ajili yake yeze huyo Yesu Kristo, ambaye huheshi-miwa na kutukuzwa pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, sasa na milele. *Amina.*

Waraka. Waefeso 2. 19-22

BASI hivi hamu wageni wapitaji tena, lakini muwenyeji pamoja na watakatifu, na wa nyumba ya Mwenyezi Mungu, kwa maana mmejengwa juu ya nisingi ambaa ni mitume na manabii, Kristo Yesu mwenyeve ni pembe kuu ; ambaye ndani yake yeze kila jengo, likiungamanishwa vyema, hukua liwe hekalu takatifu katika Bwana : ambaye katika yeze na ninyi pia mmejengwa muwe maskani ya Mwenyezi Mungu katika Roho.

Injili. Yohana 20. 24-31

ILA Thoma, naye ni mmoja katika wale kumi na wawili, Imaana ya jina lake ni Pata, hakuwapo pamoja nao wakati alipokuja Yesu. Basi wale wanafunzi wenziwe

walikuwa kumwambia, Tumemwona Bwana. Naye aka-wambia, Mimi nisipoona alama za misumāri mikononi mwake, nikapachika na kidole changu katika alama za misumari, nikapachika na mkono wangu katika ubavu wake, sitaamini kamwe. Hata baada ya siku nane wanafunzi wake walikuwamo tena mle, na Thoma yu pamoja nao : Yesu akaenda, milango imekwisha kufungwa, akasimama katikati akasema, Amani iwe kwenu ! Kisha akamwambia Thoma, Lete hapa hicho kidole chako uka-angularie mikono yangu ; lete na mkono wako, uupachike ubavuni mwangu ; nawe usiwe mtu asiye imani, uwe na imani. Thoma akamjibu akamwambia, Bwana wangu, tena Mwenyezi Mungu wangu ! Yesu akamwambia, Thoma, ni kwa kuwa umeniona ndipo umeamini ? Wamebarikiya hao wasioona nao wakaamini. Haya basi, kuna na ishara nyangi tena alizozitenda Yesu mbele ya wale wanafunzi, zisizoandikwa katika chuo hiki ; ila zimeandikwa hizi mpate kumwamini Yesu kuwa ndiye Kristo, Mwana wa Mungu ; kisha kwamba katika kua-minni kwenu muwe na uzima katika jina lake.

IDI YA KUONGOKA KWAKE MTAKATIFU PAULO

Sala

EWE Mungu, dunia nzima umeieneza mwanga wa Injili kwa kuhubiri kwake yule Paulo mtume wako mbarikiwa ; utujalie sisi, twakuomba sana, ya kwamba kwa vile tutakavyoikumbuka daima ile ajabu ya kuongoka kwake, tuwe wenye kukushukuru kwa jambo hilo kwa kuyafuata mafunzo yale ya utakatifu aliyokuwa akiyafunza yeye ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 9. 1-22

ILA yule Saulo, akali akiwakamia wanafunzi wa Bwanaa kwa makamio na uuaji, akamwendea kuhani mkuu, akataka kwake nyaraka aende nazo Dameski hata misikitii, ili kwamba akiwaona watu walio wa Njia ile, wkaii, waume, wakiwa wake, apate kuwaleta hata Yerusalemu

halil wamefungwa. Naye alipokuwa akienda, ikawa kukaribia mji wa Dameski : mara nuru zilitoka mbinguni zikamemetuka kwa pande zake zote : akaanguka nchi, akasikia sauti ikitsema naye, *ikitsema*, Saulo, Saulo, ni nini kuniudhi ? Naye aauliza, U nani wewe Bwana ? Naye Bwana akamjibu, Ni mimi Yesu ambaye *waniudhi* wewe : ni uzito kwako kuzipiga konzo mateke. Naye akateteme ka na kushangaa akasema, Bwana, wataka nifanyi nini ? Bwana akamwambia, Inuka, kaingie ndani ya mji, nawe utaambiwa ni jambo gani likupasalo kulifanya. Wale watu waliokuwa wamesafiri naye wakasimama kimya, wakisikia sauti wala hawamwoni mtu awaye yote. Saulo akainuka nchi ; alipofunua macho yake asione kitu chochote : wakamwongoza kwa kumshika mkono, na kumpeleka Dameski. Naye alikuwa haoni muda wa siku tatu, asile wala asinywe chochote. Basi Dameski alikuwako mwanafunzi mmoja jina lake akiitwa Anania ; Bwana akasema naye katika maono, *akimwita*, Anania. Naye akaaitika, Labeka, ni mimi Bwana. Bwana akamwambia, Inuka, uende njia ile iitwayo Kunyoka, kaulize mtu mmoja jina lake aitwa Saulo wa Tariso, katika nyumba ya Yudas : kwani, huyo ndiye, yuaomba Mungu ; naye amenywona katika maono mtu jina lake aitwaye Anania, akiingia na kumwekeea mikono yake juu yake, ili kwamba apate kuona. Anania akajibu, Bwana, nimesikia habari za mtu huyo kwa watu wengi, ni mambo mangapi mabaya aliywafanya watakatifu wako Yerusalemu : kisha hapa ana amri itokayo kwa makuhani wakuu awafunge wote walinganao jina lako. Bwana akamwambia, Nenda zako : kwa kuwa yeye ni chombo kilichochaguliwa kwangu mimi, kuchukua jina langu mbele ya hao mataifa, na wafalme, na wana wa Isiraeli : kwani mimi nitamwonyesha ni mambo mangapi yampasyo kupatikana nayo kwa ajili ya jina langu. Anania akaenda zake, akaingia nyumbani ; akamwekeea mikono yake juu yake akamwambia, Saulo, ndugu yangu, Bwana amenituma, yeye Yesu aliyekutokea katika njia uliyokujia, upate kuona, na kujawa na Roho Mtakatifu. Mara vikaanguka vitu kutoka machoni mwake kama magamba,

naye akaona; akaondoka, akabatizwa; kisha akala chakula na kupata nguvu. Naye Saulo alikuwa partoja na wanafunzi ndani ya Dameski siku kadhawakadha. Mara ndani ya misikiti akahubiri *habari za Yesu*, ya kwamba ni Mwana wa Mungu. Wote waliomsikiza wakapigwa na mshangao, wakasema, Huyu si yule aliye-kuwa akiwaudhi wale waliokingana jina hilo ndani ya Yerusalem? naye alikuwa amekuja hapa kwa ajili hiyo ili kwamba awapeleke, hali ya kufungwa, mbele ya makuhani wakuu. Saulo akazidi kupata nguvu, na kuwafadhaisha Mayahudi walioketi Dameski, akihakikisha ya kwamba huyo ni Kristo halisi.

Injili. Mathayo 19. 27-30

NDIPO hapo Petero akamjibu akamwambia, Angalia, nisi tumeacha vyote tumckufuata wewe: tutapata nini basi nisi? Yesu akawaambia, Ni kweli nawaambia, ya kwamba ninyi mlioniandama, katika zamani za kuzaliwa upya, wakati atakapoketi Mwana wa binadamu katika kit cha utukufu wake, wakati huo nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, huku mkiwhukumu makabila kumi na mawili ya Israeli. Na kila mmoja aliyeacha majumba, au nduguze wa kiume au wa kike, au babaye, au mamaye, au mkewe, au wana, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atazidishiwa mara mia, na maisha ya milele atayarithi. Lakini itakuwa watu wengi walio mbele kuwa wa nyuma, na walio nyuma kuwa mbele.

IDI YA KUHUDHURISHWA KWAKE KRISTO HEKALUNI,
nayo huitwa*

KUTAKATA KWAKE MTAKATIFU MARIAMU MWANAMWALI
baada ya kuzaa
Sala

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho, Etwajinyenyekeza tukikuomba uliye Mfalme wetu ya kwamba, kama vile Mwanayo pekee alivyoletwa ndani ya hekalu kama wakati wa hii siku ya leo, naye alikuwa na

mwili mfano wetu, iwe vivyo nasi kuletwa kwako tuli na miyo iliyosafiwa na kutakawa: kwa yeye huyo Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Malaki 3. 1-5

ANGALIENI, namtuma mjumbe wangu, naye ataite-angeza njia mbele yangu: Yehova naye, yeye mnayemtaka, atalijilia hekalu lake ghafula: na huyo mjumbe wa agano, ambaye mwapendezewa kwake, huyo ndiye, yuaja, anena Yehova wa majeshi. Lakini ni nani atakayehimili ile siku ya kuja kwake? tena ni nani atakayesimama atakapokuja yeye? kwa kuwa yeye ni mfano wa moto wa mwenye kuhakikisha fedha, tena yu mfano wa sabuni ya huyo afuaye nguo: naye ataketi mfano wa mwenye kuhakikisha na kuisafi fedha, naye atawasafi hao wana wa Lawi, na kuwachuja kama vile dhahabu na fedha vichujwayo: nao watamsongeza Yehova sadaka katika haki. Hapo ndipo sadaka ya Yuda na ya Yerusalem itakapopendeza kwa Yehova, kama vile katika siku za kale, na kama miaka ya zamani. Nami nitawasongelea ninyi karibu katika hukumu; nami nitakuwa ushuhuda wa upesi juu ya wachawi, na juu ya wazinifu, na juu yao waapao kwa uzuzi, na juu ya hao wamwoneao mwenye kuajiriwa kwa ajili ya mshahara wake, na hao wamwoneao mijane aliyeifiwa na mumewe, na mayatima, na hao wamdhilimu mgeni *asipate haki yake*, nao hawanichi mimi, asema Yehova wa majeshi.

Injili. Luka 2. 22-40

HATA zilipotimia siku za kujitakasa kwao kama sheria ya Musa, wakakwea wakaenda naye Yerusalem, kwenda kumweka kwa Bwana (kama ilivyoandikwa katika sheria ya Bwana, ya kwamba: Kila mume afunguaye tumbo na aitwe mtakatifu kwa Bwana), wapate na kutoa sadaka, kama ilivyonenwa katika sheria ya Bwana, Jozи ya njiwa, au makinda mawili ya njiwamanga. Naye huyo ndiye, palikuwa na mtu Yerusalem jina lake akitwa Simeoni, naye ni mtu mwenye haki huyo na uchaji-wa-

Mungu, yuangojea faraja ya Isiraeli ; na Roho Mtakatifu alikuwa juu yake. Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu kuwa hataona kufa ila amwone kwanza Kristo wa Bwana. Akaenda ali ndani ya Roho, akingia hekaluni : nao wa katika kumpeleka ndani mtoto Yesu wale wazee wake wawili, kwenda kumfanyia kama ilivyokuwa desturi ya sheria, naye akampokea mikononi mwake, akambarikia Mungu : akasema, Sasa waruruhusu mtumwa wako, Bwana, mfano wa neno lako, kwa amani ; kwa kuwa macho yangu yameuona wokofu wako, uliouweka tayari nyusoni mwa wenyeji, nchi zote, mwanga wa kuwasunulia mambo mataifa, tena utukufu wa wenycji wako Isiraeli. Na Yusufu na mamaye yule mtoto walikuwa wakistaajabu kwa yale yaliyosemwa juu yake. Simeoni akawabarikia, akamwambia Mariamu yule mamayemu, Huyu ndiye, huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka wengi walio Isiraeli, na kwa dalili itakayonenewa kinyume. Nawe utakupita upanga kati ya moyo wako, yapate kufunuliwa mawazo ndani ya miyo mingi. Palikuwa na nabii mke, akiitwa Anna, binti Fanueli, katika kabilia la Asheri ; naye umri wake umekwendelea siku nyingi : aliketi na mume miaka saba baada ya uanawali wake. Naye ni mjane wa miaka themanini na minne ; wala haondoki katika hekalu, akiabudu usiku na mchana kwa kufunga kwingi na kunyenyeka. Naye saa ile akatokea alikuwa kumshukuru Bwana, akisema habari zake na wote waliokuwa wakinangojea wokofu Yerusalem. Hata walipokwisha kutimiza mambo yote yaliyopaswa na sheria ya Bwana, wakarudi Galilaya ; wakaenda mjini kwao Nazarethi. Yule mtoto akawa kukua, na kuongea nguvu roho yake, amejawa na hekima, na fadhili ya Mungu ilikuwa juu yake.

IDI YA MTAKATIFU MATHIA

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, hapo kale badala ya yule salata yule Yudas, wewe ulimchagua mtumwa wako mwaminifu Mathia, akawa ni mmoja katika hesabu ya

mitume kumi na wawili ; utupe ya kwamba hili kanisa lako liwe hali ya kulindwa siku zote lisangiwe na mitume ya uwongo, bali litunzwe na kuongozwa na walisha wa kweli waaminifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, *Amina*.

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume i. 15-26

KATIKA siku hizo Petero alisimama katikati ya ndugu hao (walikuwa watu wengi waliokutanika pamoja, ambao jumla yao wapata kama mia na ishirini), akasema, Ndugu zangu, ilipasa maandiko yatimizwe, ambayo yali-tangulia kunenwa na Roho Mtakatifu kwa kinywa cha Daudi, habari ya Yudas, aliyekuwa kiongozi cha wale waliomshika Yesu. Kwa maana, alikuwa akihesabiwa ni mmoja katika sisi, na kupata sehemu yake katika utumishi huu. (Basi mtu huyo alinunua kiwanda kwa ijara ya uovu wake ; akaanguka kifuni-funi akapasuka, matumbo yake yote yakamwagika. Jambo hilo likajulikana na *watu* wote walioketi Yerusalem, hata kiwanda hicho kikaitwa Akelidama, kwa lugha yao, maana, ni kiwanda cha damu.) Kwani imeandikwa ndani ya chuo cha Zaburi, Makao yake na yawe matupu, yasiketiwe na mtu awaye yote : na, Uangalizi wake utwalive na mwingine. Basi inapasa kwamba mtu mimoja, katika hao waliofuatana nasi siku zote alipokuwa ye ye Bwana Yesu akiingia na kutoka kati yetu, kuanza kwa ubatizo wa Yohana, hata siku hiyo aliyopokewa juu kutoka kwetu, awe shahidi pamoja nasi wa kufufuliwa kwake. Wakaweka watu wawili, Yusufu alieitwa Barasaba, naye alikuwa na jina jingine, nalo ni Yusto, na Mathia. Nao wakaomba Mungu wakasema, Ewe Bwana ujuaye miyo ya watu wote, tuonye uliye-mchagua wewe katika hawa wawili, ashike pahali, katika utumishi na utume huu, alioukosha Yudas, aende pahali pake mwenyeze. Wakafanya kura katika hao ; kura ikamwanguia Mathia ; naye akahesabiwa pamoja na wale mitume kumi na mmoja.

Injili. Mathayo II. 25-30

NDIPO akajibu Yesu akanena, Nakushukuru wewe Baba, Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya umewaficha walio na hekima na akili, umewafunilia wana wachanga. Ndiyo yaliyo, Baba, kwa kuwa iliku-pendeza mbele zako yawe hivyo. Mambo yote nimepewa mimi na Babaangu ; wala hakuna amjuaye Mwana ila ye ye Baba ; wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana, na awaye yote yule Mwana atakayempenda kumfunulia. Njoni kwangu ninyi nyote mtaabikao kwa kazi nzito, mliolemelewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitwenkeni kongwa langu, mijifunze kwangu, kwa kuwa ni mpole miini, ni mnyenyeketu wa moyo, nanyi mtaona kustarehe katika nafsi zenu. Kwani kongwa langu ni jepesi, na mzigo wangu ni hafifu.

**IDI YA KUPEWA HABARI KWAKE MBARIKIWA
MARIAMU MWANAMWALI**

Sala

EWE Bwana, twakuomba sana, utumimini neema yako Emiyoni mwetu ; ili kwa vile sisi tulivyopata habari ya kufanywa mwili Mwanayo Yesu Kristo kwa ujumbe uliokuja na malaika, sasa kwa kusalibiwa na kuteseka kwake tuwe wenyewe kuperlekwa mbele vivyo hivyo hata utukufu wa kufufuka kwake ; kwa ye ye huyo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Isaya 7. 10-15

NA Yehova akanena na Ahazi tena ; akisema, Jitakie ishara ya Yehova Mungu wako ; itake katika hayo yaliyo chini sana, au katika hayo yaliyo juu sana. Na Ahazi akasema, Sitataka *ishara* mimi, wala sitamjaribu Yehova. Naye akasema, Sikizeni sasa, enyi wa nyumba ya Daudi ; Je, ni neno dogo kwenu kuwachokesha watu, hata iwe ninyi kumchokesha na Mwenyezi Mungu wangu pia ? Kwa ajili ya hayo Yehova mwenyewe atawapa ninyi ishara ; Huyo ndiye, mwaniamwali attachukua mimba, naye atazaa mwana mwaniamume, naye atamwita

jina lake Imanweli. Siagi na asali atakula, hapo ajuapo kuyakataa yale maovu, na kuyachagua yale mema.

Injili. Luka I. 26-38

HATA mwezi wa sita, malaika Gabirieli akatumwa jina lake Nazarethi, kwa mwaniamwali mmoja aliye poswa na mtu mume jina lake akiitwa Yusufu, mtu wa nyumba ya Daudi ; na yule mwaniamwali jina lake akiitwa Mariamu. Akaingia kwake akamwendea akasema, Salamu *m yako*, uliyefadhiiliwa ; Bwana yu pamoja nawe : umebarikiwa kati ya wanawake. Alipomwona, akafanya hofu kwa maneno yake, akawaza, Salamu hiyo i jinsi gani ? Malaika akamwambia, Usiche, Mariamu, kwani umepata fadhili kwa Mwenyezi Mungu. Angalia, utachukua mimba uzae mwana mwaniamume : naye jina lake utamwita YESU. *Mwana* huyo atakuwa mkubwa, tena ataitwa Mwana wa Aliye-Juu-Sana, na Bwana Mungu atampa kiti cha babaye Daudi : naye atatawala juu ya nyumba ya Yakobo hata milele, wala hautakuwa na mwisho ufalme wake. Mariamu akamuuliza malaika, Litakuwaje nenó hili, nami simjui mume ? Malaika akamjibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, tena nguvu za Aliye-Juu-Sana zitakufinika kivuli : ndipo na Kitakatifu hicho kitakachozawa kwako kitiwe *Mwana* wa Mungu. Naye huyo ndiye, jamaa yako Elizabethi naye amechukua mimba ya mtoto mwaniamume katika uzee wake ; na huu ni mwezi wa sita kwake aliyeitwa tasa. Kwani kwa Mwenyezi Mungu hakutakuwa na neno lolote lisilomkinika. Mariamu akasema, Mimi hapa ni kijakazi cha Bwana ; na iwe kwangu kama maneno yako. Kisha akaondoka malaika akamwacha.

IDI YA MTAKATIFU MARIKO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, umetufundisha sisi watu wa Ekanisa lako takatifu kwa elimu ya mbinguni, hiyo aliyoukuwa nayo yule mhubiri wako, yule mtakatifu

Mariko ; utupe neema hiyo, ya kwamba tusiwe mfano wa watoto, tukachukuliwa na kila upepo wa elimu ya upuzi ; bali daima tuwe na uwezo katika kweli ya Injili yako takatifu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Waefeso 4. 7-16

ILA tulipewa kila mmoja wetu ile neema, kwa kadiri ya kipimo cha kipawa cha Kristo. Kwa ajili ya hayo, asema, Alipopaa juu, aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa. (Basi neno hili, Alipopaa, ni nini, isipokuwa ya kwamba alishuka pia na kuingia mwahali mwa chini mwa nchi ? Yeye aliyeshuka ndiye yeye huyo aliyepaa juu sana kuliko zile mbingu zote, ili kwamba avijaya vitu vyote.) Naye akawapa watu wengine *wave* mitume : na wengine *wave* manabii : na wengine *wave* wahubiri wa ile habari njema : na wengine *wave* wachunga na waalimu : kwa kukamilika kwao watakatifu, kufikilia kazi ya utumishi, kwa majengo ya mwili wa Kristo : hata tuufikilie ule umoja wa imani pia sote, na *unoja* wa kule kumjua Mwana wa Mwenyezi Mungu, hata *kuwa* mtu mtimilifi, hata kipimo cha umri wa kujaa kwake Kristo : ili kwamba tusiwe watoto wachanga mwanzo wa sasa, kurushwa huku na huku, na kuchukuliwa na kuzungushwa na kila upepo wa elimu, kwa udanganyifu wa wanadamu, kwa hila, kwa kufuata uzusi wa upotevu : ila kwa kunena kweli katika mapenzi tukue tumfikilie yeye katika mambo yote ; ambaye ndiye kichwa, yeye Kristo, kuanza kwake yeye, mwili mzima ukiungamanishwa vycma na kushikamana pamoja kwa njia ya kila kiungo kiletacho manufaa, sawasawa na kutenda kwa kila fungu pekee kipimo chake, hivi hukua ule mwili kwa majengo yake wenywewe katika mapenzi.

Injili. Yohana 15. 1-11

MIMI ndio mzabibu wa kweli, na mkulima wake ni Babaangu. Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda ye ye huliondoa, na kila tawi lizaalo matunda, ye ye hulisafi, lizidi kuzaa matunda. Ninyi mmekuwa safi tangi hapo, kwa ajili ya neno nililowaambia. Kaeni

ndani yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile lisivyoweza tawi kuzaa matunda kwa nafsi yake, lisipokaa ndani ya mzabibu, wala ninyi hamwezi, msipokaa ndani yangu. Mimi ndio mzabibu, matawi ni ninyi. Mtu ambaye akaa ndani yangu, nami nikiwa ndani yake, huzaa matunda mengi huyo, kwa kuwa pasipo mimi hamwezi kufanya neno liwalo lote. Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi *litupwavyo*, akakauka ; nayo watu huyakusanya na kuyatupa motoni, yakateketea. Mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, takeni impendalo lote, nanyi mtafanyiwa. Kwa hilo hutukuzwa Babaangu : ya kwamba mzae matunda mengi ; nanyi mtakuwa wanafunzi kwangu. Kama alivyonipenda Baba, nami nimewapenda ninyi vivyo. Kaeni katika mapenzi yangu. Mtakapoyashika maagizo yangu, mtakaa katika mapenzi yangu, vivile kama niliviyoyashika mimi maagizo ya Babaangu, na kukaa katika mapenzi yake. *Maneno* haya nimewaambia, kwamba furaha yangu mimi ipate kuwamo ndani yenu, na furaha yenu ipate kutimia.

IDI YA WATAKATIFU FILIPU NA YAKOBO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, kukujua kweli wewe ndiko kuishi milele ; utupe sisi kurnjua kwa utimilifi Mwanayo Yesu Kristo, kuwa ndiye Njia, ndiye Kweli, naye ndiye Uzima ; ili kwamba kwa kuzifuata nyayo zao wale mitume wako watakatifu, mtakatifu Filipu na mtakatifu Yakobo, tuwe sisi watu wa kwenenda kwa kujikaza katika njia ifikishayo maisha ya milele ; kwa yeye Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Yakobo 1. 1-12

YAKOBO, mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo, waraka wang'u huu uyafikilie makabila hayo kumi na mawili yaliyo ya Matawanyikano, Salamu. Ihesabuni kuwa ni furaha tupu, ndugu zangu, hapo mwangukapo katika majaribu aina nyingine-nyingine ; huku

mkjua ya kwamba hayo maonjo ya imani yenu huleta uvumilivu. Huo uvumilivu na uwe na kazi yake timilifu, ili kwamba muwe mliotimia sana, tena wazima kabisa, msiozungukiwa na lolote. Ila watu wa kwenu mmajawapo akiwa amepungukiwa na hekima, na amwombe Mungu awapaye watu wote kwa ukarimu naye hasimangizi ; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani, asifanye tashwishi ya lolote : kwani ye ye afanyaye tashwishi ni mfano wa wimbi la bahari likirushwa-rushwa na upopo na kutupwa-tupwa. Kwani binadamu huyo na asidhani ya kwamba atapata chochote kwa Bwana ; mtu mwene mashauri mawili, asiyetua katika njia zake zote. Ila ndugu aliye mnyonge, na ajisifu katika kukuzawa kwake ; na huyo tajiri, katika kutwezwa kwake : kwa kuwa kama vile ua la nyasi ndivyo atakavyoondoka. Kwani hilo jua lapaa pamoja na upopo uteketeteao, na kuzikausha hizo nyasi ; na ua lake huanguka, na uzuri wa umbo lake hupotea ; na tajiri atasinya vivyo hivyo katika miendo yake. Ana heri mtu huyo avumiliaye kujari-biwa : kwa kuwa akiisha kuhakikishwa atapata taji ya uhai, ambayo Bwana aliwaahidia hao wampendao.

Injili. Yohana 14. 1-14

YESU akawaambia wanafunzi wake, Msifadhaike miyo yenu ; mwaamini kwa Mwenyezi Mungu, na kwangu mimi aminini. Katika nyumba ya Babaangu mna makao mengi ; na kwamba haikuwa hivyo ningeli-waambia, kwa kuwa naenda kuwatengezea pahali. Nami nitakapokwenda na kuwatengezea pahali nitakuja tena, kisha nitawakaribisha kwa nafsi yangu, ili mimi nilipo nanyi muwe papo. Na huko niendeako mimi mwakujua, mwajua na njia. Thoma akamwambia, Ewe Bwana, uendeako hatukujui, tutaijuaje njia ? Yesu akamwambia, Mimi ndiyo njia, mimi ndiyo kweli, mimi ndio uzima ; mtu haji kwa Baba ila anipite mimi. Kwamba mlinijua, na Babaangu mngelejua. Toka sasa mwamjua, kisha mmemwona. Filipu akamwambia, Ewe Bwana, tuonyeshe ye ye Baba, yatutosha. Yesu akamwambia, Nime-

kuwa pamoja nanyi muda huu wote nawe usinjue, Filipu ? Aliyeniona mimi amemwona ye ye Baba. Mbona unanena, Tuonyeshe Baba ? Je, huamini kuwa mimi ni ndani ya Baba, naye Baba yu ndani yangu ? Maneno niwaambiayo siyasemi kwa nafsi yangu ; lakini ye ye Baba akaavyo ndani yangu hutenda kazi zake. Ni amini kuwa mimi ni ndani ya Baba, naye Baba yu ndani yangu. Au la, ni amini kwa ajili ya zile kazi, tu ! Ni kweli, ni kweli, nawaambia, mwene yuamini kwangu mimi kazi nitendazo mimi naye atazitenda, atatenda na kubwa kuliko hizi ; kwa kuwa mimi naenda kwa Babaangu. Na mtakalotaka kwa jina langu nitalifanya, liwalo lote : apate kutukuzwa ye ye Baba kwake Mwana. Mtakaponitaka neno kwa jina langu nitalifanya.

IDI YA MTAKATIFU BARANABA

Sala

EWE Bwana Mwenyezi Mungu, yule mtume wako Ematakati, Baranaba, ulimvika vipawa vikubwa nya Roho Mtakati ; twakuomba sana usituache sisi tukavikosa vipawa vyako namna namna, wala tusikose neema yako, tupate kuvitumia daima vipawa hivyo kwa kuheshimu na kukutukuza ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

Badala ya Waraka. Vitendo nya Mitume II. 22-30

NA habari yao ikafika hata kwa masikio ya kanisa lililokuwa ndani ya Yerusalem : nao wakamtuma Baranaba aende Antiochia : naye alipofika na kuiona neema ya Mungu, akafurahi ; akawahimiza wote, kwamba washikamane na Bwana kwa makusudi ya moyo : kwa kuwa alikuwa mtu mwema na kujawa na Roho Mtakati na imani : watu wengi wakaongezeka upande wa Bwana. Kisha Baranaba akatoka kwenda Tariso kumtafuta Saulo : alipokwisha kumwona, akamleta Antiochia. Ikawa kukanika muda wa mwaka mziima pamoja na kanisa, wakawafunza watu wengi ; wale wanafunzi walianza kuitwa Wakristo hapo ndani ya mji wa Antiochia. Siku hizo

manabii waliteremka kutoka Yerusalemu kwenda Antiochia. Mtu mmoja mionganii mwao jina lake akiitwa Agabo aka-simama, na kuonyesha kwa *nguvu za* Roho kwamba njaa kuu itakuja juu ya dunia nzima ; nayo ikawa katika siku za Kaisari Kilaudio. Na wale wanafunzi, kila mtu kama alivyofanikiwa, wakakusudia kuwapelekea msaada ndugu zao walioketi katika Yudea : nao wakafanya vivyo, waki-wapelekea wazee kwa mikono ya Baranaba na Saulo.

Injili. Yohana 15. 12-16

HAJA ndiyo maagizo yangu mimi : mpendane ninyi kwa ninyi, kama niliviyowapenda. Mtu hana mape-nzi kuzidi haya, ya ye ye kuweka nchi uhai wake kwa ajili ya rafiki zake. Ninyi mmekuwa rafiki zangu, mfanyapo hayo niwaagizayo. Tangu sasa siwaiti watumwa, kwa kuwa mtumwa hajui afanyalo bwana wake ; nimewaita rafiki ninyi, kwa kuwa kila nilosikia na Babaangu nime-wajuvisha. Hamkunichagua mimi, nimewachagua ninyi, kisha nimewaweka, ili mwenende mkizaa matunda, na matunda yenu yapate kukaa ; ili kwamba kila mmakalo Baba kwa jina langu awape lilo.

IDI YA MTAKATIFU YOHANA MBATIZAJI

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, uanganlii wako ndilo lililompa mtumwayo mtakatifu Yohana kuzaliwa kwa ajabu, likamtuma kumtengenza njia Mwanayo Mwokozi wetu, kwa kuhubiri watu ya kutubia ; utupe sisi kufuata mafunzo yake na maisha yake matakatifu sana, hata tuwe sisi watu wa kutubu kweli kama vile alivyokuwa akifunza ye ; kisha na kama vile alivyotupa kielelezo, tuwe siku zote wenye kusema ambayo ni kweli, tuukemee na uovo pasina kucha watu, nasi tuvumilie katika mateso kwa ajili ya ile kweli ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Isaya 40. 1-11

WATUZENI mioyo, watuzeni mioyo watu wangu, asema Mwenyezi Mungu wenu. Ufurahisheni mioyo Yerusalemu, kaulinganeni mkaaseme ya kwamba

mateso yake yametimia, kwamba upotofu wake umeli-piwa ; kwariba amepokea mkononi mwa Yehova mara mbili kwa sababu ya dhambi zake zote. Ni sauti ya mtu mmoja apigaye ukelele, *asema*, Itengezeni barani njia ya Yehova, inyosheni katika wangwa njia kuu ya Mungu wetu. Kila bonde litakuzwa, na kila mlima na kilima kitatwezwaa chini : na hapo palipo kombo patanyoshwa, napo paparuzapo patafanywa sawa : na utukufu wa Yehova utafunuliwa, na wenye mwili wote pamoja wata-uona : kwa kuwa kinywa cha Yehova kimeyatamka hayo. Ni sauti ya mtu mmoja asemaye, Piga ukelele ! Tena mwininge akauliza, Nipige ukelele wa nini ? *Akaitika, Nena*, Wenye mwili wote ni nyasi, na wema wake wote ni kama ua la shambani : hizo nyasi hunyauka, hilo ua lasinyaa ; kwa sababu pumzi za Yehova huvuvia juu yake : hakika yao hao watu ni nyasi. Hizo nyasi hunyauka, hilo ua lasinyaa : lakini neno la Mwenyezi Mungu wetu husimama milele. Ewe wewe uuhubiriye Zayuni habari njema, kwea juu katika mlima mrefu ; ewe wewe uuhubiriye Yerusalemu habari njema, inua sauti yako kwa nguvu ; iinue usiche ; iambie hiyo miji ya Yuda, Huyo ndiye, Mwenyezi Mungu wenu ! Angalia, Bwana Mungu atakuja msiano wa shujaa, na mkonono wake utatalawa kwa ajili yake : angalia, thawabu yake anayo pamoja naye, na ijara yake i mbele yake. Atalilisha kundi lake kama mchunga *alishavyo*, wana-wa-kondoo atawaambata mikononi mwake, naye atawachukua kifupi mwake, na hao *kondoo* waamwishao atawachunga polepole.

Injili. Luka 1. 57-80

ZIKAMTIMILIA Elizabethi zamani zake za kuzaa, Zakazaa mwana mwanamume. Wakasikia jirani zake na jamaa zake, ya kwamba Bwana amemfanyia nyingi reherma zake, wakafurahi pamoja naye. Kisha ikawa kwa siku ya nane kulikuja watu kuja kumpasha tohara yule mtoto ; ikawa kumwita Zakaria kwa kufuata jina la babaye. Mamaye akasema, La, sivyo ; lakini na aitwe Yohana. Wakasema naye, wakamwambia, Katika jamaa zako hakuna mtu mwenye kuitwa jina hilo. Wakamle-

kezea babaye kujua atakavyomwita. Akataka kibao cha kuanidikia, akaandika, akawaambia, Jina lake ni Yohana. Wakastaajabu wote. Papo hapo kikafunuka kinywa chake, ulimi wake ukafunguka, akanena kwa kumsifu Mungu. Waketio kando-kando yao wakaingiwa na hofu pia wote ; ikatangazwa maneno haya yote nchi nzima ya milimani mwa Yudea. Wote walioyaskia wakayaweka miyoni mwao, wakasema, Mtoto huyu atakuwa namna gani ? Kwani mkono wa Bwana ulikuwa pamoja naye. Na Zakaria babaye *yule mtoto* akajawa na Roho Mtakatifu, akatabiri, akasema, Na ashukuriwe Bwana Mungu wa Israeli, kwa kuwa amewaangalia watu wake, amewafanya na ukombozi ; tene ametuiniulia pembe ya wokofu katika nyumba ya Daudi mtumishi wake ; (kama alivosema kwa vinywa vya manabii wake watakatifu waliokuwa tangu mwanzo), kutupa wokofu mbele ya adui zetu na katika mikono ya wote watuchukiao ; kuzifanya rehema zake juu ya baba zetu, na kukumbuka agano lake takatifu ; kiapo alichomwapia babaetu Iburahimu, ya kwamba atatupa, tuli hali tumeokoka na mikono ya adui zetu, kumtumikia pasipo hofu kwa utakatifu na haki mbele zake siku zetu zote. Nawe, mtoto wewe, utaitwa nabii wa Aliye-Juu-Sana, kwani utamtangulia Bwana mbele ya uso wake kumtengezea njia zake, ili kuwapa watu wake kuujua wokofu kwa kusamehewa dhambi zao ; kwa ajili ya huruma za ndani za Mungu wetu, kwa hizo nuru itokayo juu imetufikia, iwang'arie waketio katika giza na kivuli cha mauti ; ili katuongoza miguu yetu njia ya amani. Yule mtoto akawa kukua, na kuongea nguvu rohoni mwake, akakaa katika mabara hata siku aliyoonekana kwa Israeli

IDI YA MTAKATIFU PTERO

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa Mwanayo Yesu Kristo ndiwe uliyempa yule mtume wako mtakatifu Petero vipawa vingi vizuri, ukamuusia sana kulilisha kundi lako ; twakuomba sana uwawezeshe mabishopu

wote, na wachungaji wote, wawe wenye kulihubiri kwa bidii Neno lako takatifu ; na wale watu nao wawe wenye kulifuata kwa kutii lile Neno ; ili kwamba apate kupewa kila mimoja taji ya utukufu usio mwisho ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 12. 1-II

BASI mfalme Herode alinyosha mikono yake kama wakati huo, apate kuwatenda uovu watu wengine wa kanisa. Akamuua Yakobo ndugu yake Yohana kwa upanga. Alipoona ya kwamba yanapendekeza kwa Mayahudi, akaongeza, akamshika na Petero. Siku hizo zilikuwa ni siku za mkaate usiotiwa chachu. Alipokwisha kumshika, akamweka gerezani, akamtia mikononi mwa askari wanne wanne mara nne warlinde : akipendelea kumtoa na kumweka mbele ya wenyeji baada ya *Idi ya Pasaka*. Basi Petero alitunzwala gerezani : ilia kanisa likaombia Mungu kwa bidii kwa ajili yake. Hapo Herode alipotaka kumtoa nje, usiku ule ule, Petero alikuwa amelala katikati ya askari wawili, amefungwa na minyororo miwili : na mlangoni pana walini walinda gereza. Mara huyu ndiye, malaika wa Bwana amesimama karibu naye, nuru zikang'ara chumbani : akampiga Petero ubavuni, akamwambia, Ondoka upesi. Minyororo ile ikaanguka kuntoka mikononi. Malaika akamwambia, Jifunge, uvae na viatu vyako. Naye akafanya. Tena akamwambia, Jitande nguo yako, uniandame. Akatoka nje akamwandama : lakini asifahamu kuwa ni kweli yale yaliyofanywa na malaika, ilia alidhani kwamba ameona maono. Basi walipokuwa wamekwisha kupita kilinzi cha kwanza na cha pili, wakalifikilia lile langa la chuma la kuingilia mijini ; likawafungukia lenyewe : wakatoka nje, wakapita kwendelea mbele katika njia moja ; mara malaika akaondoka akamwacha. Petero alipotia fahamu, akasema, Sasa najua hakika kwamba Bwana ametuma malaika wake kuja kuniokoa na mkono wa Herode, na kungojea kwao kote wenyeji wa Mayahudi.

Injili. Mathayo 16. 13-19

YESU akaenda pande za Kaisarea-kwa-Filipu, aka-wauliza wanafunzi wake, huku yuanena, Je, watu wasema mimi, Mwana wa binadamu, ni nani? Wakanena, Wengine wanena, U Mbatizaji Yohana, na wengine Elija, na wengine Yeremia au mmoja katika manabii. Akawauliza, Nanyi mwasema ni nani mimi? Simoni Petero akamjibu akamwambia, Wewe u Kristo Mwana wa Mwenyezi Mungu aliye Hai. Yesu akamjibu akamwambia, Heri ni yako, Simoni bari-Yona, kwa kuwa hili hukufunuliwa na mwili na damu; aliye kufunulia ni Babaangu aliye mbinguni. Nami nakuambia ya kwamba wewe ndiwe Petero, nami juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; na malango ya kuzimu hayatalishinda nguvu. Mimi nitakupa funguo za ufalme wa mbingu; na utakavyofunga huku nchi, vitakuwa vimefungikambingu-ni, na utakavyofunga huku nchi, vitafunguka mbingu-ni.

IDI YA MTAKATIFU YAKOBO MTUME

Sala

UTUPE, ewe Mungu mwinci wa rehema, ya kwamba kama vile yule mtakatifu Yakobo mtume wako, alivyomwacha mzee wake na alivyokuwa navyo vyote, akautii mwito wake Mwanayo Yesu Kristo pasipo kukawia, akamuata; iwe sisi nasi kuziacha tamaa za ulimwengu na mwili zote pia, tupate kukaa tayari daima kuyafluata maagizo yako matakatifu; kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 11. 27-12. 3

SIKU hizo manabii waliteremka kutoka Yerusalemkuwenda Antiokia. Mtu mmoja mionganini mwao jina lake akitiwa Agabo akasimama, na kuonyesha kwa *nguvu za Roho* kwamba njaa kuu itakuja juu ya dunia nzima; nayo ikawa katika siku za Kaisari Kilaudio. Na wale wanafunzi, kila mtu kama alivyofanikiwa, wakakusudia kuwapelekeea msaada ndugu zao walioketi katika Yudea: nao wakafanya vivyo, wakiwapelekeea wazee kwa mikono ya

Baranaba na Saulo. Basi mfalme Herode alinyosha mikono yake kama wakati huo, apate kuwatenda uovu watu wengine wa kanisa. Akamuua Yakobo ndugu yake Yohana kwa upanga. Alipoona ya kwamba yanapendekeza kwa Wayahudi, akaongeza, akamshika na Petero.

Injili. Mathayo 20. 20-28

NDIPO hapo akaendewa na mama yao wana wa Zebedi, pamoja na wanawe, huku yuamsujidua na kutaka haja kwake. Akamuuliza, Wataka nini? Akamwambia, Nena kwamba waketi wanangu wawili hawa, mmoja upande wa mikono wako wa kuume na mmoja upande wa mikono wako wa kushoto, katika ufalme wako. Yesu akawajibu akawaambia, Hamjui militakalo. Je, mwaweza kunywa ya kikombe niendacho kukinywa mimi, na kubatizwa kwa ubatizo huu ambao ninabatizwa nao? Wakamwambia, Twaweza. Akawaambia, Ya kikombe changu hakika yake mtakunywa, nanyi mtabatizwa kwa ubatizo huo ambao ninabatizwa nao, lakin kule kuketi upande wa mikono wangu wa kuume na upande wa mikono wangu wa kushoto, si langu mimi kule kuwapa, ila hupewa walioandaliwa na Babaangu. Waliposikia wale kumi wakawakasirikia yule mtu na nduguye. Ila Yesu aka-waita wamjie, kisha akanena, Mwawajua waliowatawala wale mataifa wajifanyakyo wenyewe kuwa mabwana juu yao; na wakubwa wao hujifanya kuwa maseyidi kwao. Hayatakuwa hayo kwenu ninyi, ila mtu awaye yote atakaye mwenyewe awe mkubwa kwenu, atakuwa ni mtumishi wenu; na atakaye kuwa wa kwanza wenu, atakuwa ni mtumwa wenu: kama ambavyo Mwana wa binadamu naye hakuja kwa kutumikiwa ila kwa kutumika yeye, na kutoa nafsi yake kuwa makombozi badala ya wengi.

IDI YA MTAKATIFU BARITOLOMAYO MTUME

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho, wewe ulimpa neema yule mitume wako Baritolomayo, kuliamini kweli hilo Neno lako na kulihubiri; twakuomba

sana ulipe kanisa lako kulipenda Neno hilo aliloamini yeye, na kulihibiri na kulikubali ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Vitendo vya Mitume 5. 12-16

TENA ishara nyingi na ajabu vikafanya katika wenyeji kwa mikono ya mitume, nao wote walikuwa ndani ya matao ya Suleimani, wenyewe moyo mmoja. Ila katika wale wenginewe hakusubutu mtu kushikamana nao, isipokuwa wenyeji wakawakuza ; na wenye kuamini wakaongezeka sana upande wa Bwana, makundi *ya watu* waume kwa wake ; hata ikawa ni kuchukua wagonjwa wao na kuwaweka nje katika njia kuu za mji, kuwalaza katika vitanda na wengine katika magodoro, ili kwamba Petero apitapo ngawa kivuli chake kimwangukie mmojawapo. Tena likakutanika kundi la *watu* lilitotoka miji iliyokuwa kando-kando ya Yerusalem, wakileta wagonjwa, na wale walio-pagawa na maroho wachafu : nao wakapozwa wote.

Injili. Luka 22. 24-30

YAKAONDOKA na mashindano kwo : kana kwa-mba ni nani adhaniwaye kuwa mkubwa. Akawaambia, Wale mataifa-taifa, wafalme wao wawatawala-tawala, na walio na hukumu juu yao huitwa wafanyaji-wa-wema. Ninyi hamwi kama vile : lakini aliye mkubwa kwenu na awc kama aliye kijana, na mwenye kutawala kama atumikaye. Kwani aliye mkubwa ni yupi, yule aliyeketi chakulani au yule atumikaye ? Siye yule aliyeketi ? Lakini mimi katikati yenu nimekuwa kama atumikaye. Nanyi ndinyi mliodumu nami katika kujaribiwa kwangu. Nami ni katika kuwaagizia ufalme, kama vile nilivyoagiziwa mimi na Babaangu ; mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu : nanyi mitaketi juu ya viti vya enzi, huku mkiwahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli.

IDI YA MTAKATIFU MATHAYO MITUME

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa kinywa cha Mwanayo Mwenye-baraka ulimwita yule Mathayo, ili aache kutoza ushuru awe mtume na mhubiri ; utunce-

meshe nasi ya kuacha mambo ya kutamani-tamani, na kule kupenda mno mali ya dunia, kwamba nasi tupate kumfuata yeye huyo Mwanayo, Yesu Kristo ; aishie na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja milele. *Amina.*

Waraka. 2 Wakorintho 4. 1-6

KWA ajili ya hayo, kwa kuwa tuna utumishi huu, kama tulivyorehemewa, hatuzimi roho : lakini tumeyakataa mambo yale yaliyofichwa ya aibu, tusiende katika hilaa, wala tusilitumie neno la Mwenyezi Mungu kwa udanganyifu ; lakini, kwa kuifanya wazi ile kweli, twadhihirisha nafsi zetu katika nia ya kila binadamu, mbele za Mwenyezi Mungu. Ila kwamba habari njema yetu imefinkwa utaji, imefinkwa katika hao waangamiao : ambaa ndani yao yule mungu wa dunia hii amewapofusha fikira zao hao wasioamini, kwamba nuru za ile habari njema ya utukufu wa Kristo, ambaye ndiye sura za Mwenyezi Mungu, zisiwamulikie. Kwani hatutangazi nafsi zetu, lakini *twamkubiri* Kristo Yesu kuwa ndiye Bwana, na sisi wenyeve kwamba tu watumwa wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa ni Mwenyezi Mungu aliyesema, Mwanga utang'ara kutoka katika giza, ambaye aling'ara katika mioyo yetu, kwa kumulika kwake ule ujuzi wa utukufu wa Mwenyezi Mungu katika uso wa Yesu Kristo.

Injili. Mathayo 9. 9-13

HATA alipopita Yesu kutoka pale akamwona *mtu* mmoja ameketi pahali patolewapo ushuru, jina lake aitwa Mathayo, akamwambia, Niandame. Akainuka, akamwandama. Ikawa wakati alipoketi nyumbani akila chakula, mara wakaja wengi watoa-ushuru na wenye-dhambi wakiketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake. Hata wale Mafarisayo walipowaona, ilikuwa kuwaliza wanafunzi wake, Kwani Mwalimu wenu kula pamoja na watoa-ushuru na wenye-dhambi ? Aliposikia akawaambia, Walio hawajambo hawana haja ya tabibu, lakini walio hawawezi *ndio watakao tabibu*. Endeni mkalitambue maana yake neno hili : Mimi nataka rehema wala si

dhabihu : kwani sikuja kuwaita walio na haki, lakini ni wenye dhambi wapate kutubu.

IDI YA MTAKATIFU MIKAELI NA MALAIKA PIA WOTE

Sala

EWE Mungu, Mkazi wa milele, huo utumishi wa malaika na binadamu umeuanziliza, umeupanga kwa taratibu ya ajabu ; utujalie sisi kwa rehemu zako, ya kwamba, kama hivyo wakutumikiavyo daima malaika zako watakatifu huko mbinguni, nasi watusaidie na kutulinda hapa duniani kwa utakavyowaagiza, kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Ufunuo 12. 7-12

KISHA palikuwa na vita mbinguni : Mikaeli na malaika zake kwenda kulipiga vita hilo joka ; na hilo joka nalo na malaika zake ye ye wakapigana vile vita ; nao hawakushinda nguvu, wala pahali pao hapakuonekana tena mbinguni. Na hilo joka kubwa libbwagwa chini, ni nyoka wa kale, ye ye aitwaye Ibilisi, tena aitwa Shetani, huyo mwenye kuwapoteza walimwengu wote ; alibwagwa nchi na malaika zake walibwagwa chini nao pamoja naye. Kisha nilisikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Hivi sasa umekuwa wokofu, na uwezo, na ufalme wa Mwenyezi Mungu wetu, na amri ya Kristo wake : kwa kuwa huyo mwenye kuwashtaki ndugu zetu amekwisha kubwagwa chini, ye ye awashtakiye mbele za Mwenyezi Mungu wetu mchana na usiku. Nao wakamshinda kwa njia ya hiyo damu ya Mwana-wa-kondoo, na kwa njia ya tamko la ushuhuda wao ; nao hawakuupenda uhai wao hata mauti. Kwa ajili ya hayo, furahini enyi mbingu, na ninyi mketio ndani yake. Ole wao waketio duniani na baharini : kwa kuwa huyo Ibilisi amewashukia ninyi, mwenye hasira kubwa, maana, ajua ya kwamba ana muda mchache tu.

Injili. Mathayo 18. 1-10

KATIKA saa ile wakaenda wale wanafunzi kwa Yesu wakanena, Basi ni nani aliye mkubwa katika ufalme wa mbingu ? Akaita mtoto mmoja, akamweka akasimama

katikati yao, akanena, Ni kweli nawaambia, msipogeu ka nkawa kama watoto wadogo, hamtauingia ufalme wa mbingu kamwe. Basi atakayejitweza mwenyewe akawa hali yake kama mtoto huyu, huyu ndiye aliye mkubwa katika ufalme wa mbingu. Naye awaye yote atakayemkubali mtoto mmoja mfano wa huyu, kwa maana ya jina langu, hunikubali mimi : na atakayemkunguwaza mmojawapo hawa wadogo waaminio kwangu mimi, huyu afaa atungikwe shingoni mwake jiwe asagialo punda akatoswe katika kina cha bahari. Ole ni wa ulimwengu kwa sababu ya makunguwazo ! kwani makunguwazo hayana budi na kuja ; walakin ole ni wa mtu yule ambaye kwa ye ye huja kunguwazo ! Na kikukunguwazacho, kwamba ni mikono wako, kwamba ni mguu wako, kikate ukitupe mbali nawe : ni vizuri kwako uingie uzimani uli hali u kigitu au kiwete, kuliko kutupwa uli na mikono miwili au miguu miwili katika moto wa milele. Na kwamba wakunguwazwa na jicho lako, ling'oe, ulitupe mbali nawe : ni vizuri kwako uingie uzimani uli na chongo, usitupwe uli na macho mawili katika jahanamu ya moto. Angalieni msiwadharau wadogo hawa mmojawapo, kwani nawaambia ninyi, ya kwamba malaika zao mbinguni hawaachi kuuona uso wa Babaangu aliye mbinguni.

IDI YA MTAKATIFU LUKA MHUBIRI

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, yule tabibu Luka, ambaye sifa yake i katika Injili, ulimwita wewe apate kuwa mhubiri wa Injili, na kupoza roho zao wanadamu : twakuomba ya kwamba tupozwe sisi maradhi yote ya roho zetu kwa dawa za afya za inafunzo aliyofunza ye ye ; kwa kustahili kwake Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 2 Timotheo 4. 5-15

ILA wewe kesha katika kila jambo, stahimili maovu, Ifanya kazi ya mhubiri wa habari njema, timiliza huo utumishi wako wa dini. Kwani mimi hivi sasa namwagwa, na wakati wa kuondoka kwangu umefika. Nimekwisha kupiga vile vita vilivyo vizuri, nimekwisha kutimiza

mwendo wa maisha yangu, nimekwisha kuilinda ile imani : baadaye nimewekewa taji ya haki, ambayo yeze Bwana, mwamuzi mwenye haki, atanipa katika siku hiyo : wala si mimi tu, ila na hao wote walioyapenda hayo mafunu yake. Jitahidi kuja kwangu kwa upesi : kwani Dema ameniacha, maana, alipenda dunia hii ya sasa, naye alikwanda Thesalonike : Keresiki *amekwenda Galatia, Tito amekwenda Dalamatia*. Luka peke yake ndiye niliye naye. Mtwa Mariko uje naye hapa : kwani yuanifa kwa utumishi. Ila Tukiko nilimtuma aende Efeso. Hiyo nguo ya kujitanda niliyoicha Teroa *mkononi mwa Karipo*, ilite utakapokuja, na vile vyuo pia, hasa vile vya ngovi. Alekisandaro huyo mhunzi-wa-sifuri alinitenda mabaya mengi : Bwana atamlipa sawasawa na kazi zake : nave uwe na hadhari naye sana, kwani maneno yetu anayapinga sana.

Injili. Luka 10. 1-7

KISHA baada ya haya Bwana akaweka na wengine watu Kasabuini, akawatuma wawili wawili kumtangulia mbele ya uso wake, waende kila mji na kila pahali alipoazimia kwenda mwenyewe. Akawaambia, Mavuno ni makubwa, lakini wale wafanyaji wa kazi ndio wachache : basi takeni kwa Bwana wa mavuno awapeleke wafanyaji wa kazi wende katika mavuno yake. Endeni ! mimi hapa nawatuma hali ya wana wa kondoo kati ya mbwa-mwitu. Msichukue mfuko wala mkoba, wala viatu, wala msimwankue mtu njiani. Na kila nyumba mtakayofikilia, iambieni kwanza, Na iwe amani juu ya nyumba hii : naye akiwa yumo mwana wa amani, amani yenu itamkalia juu yake, na kwamba hamo, itawarejea juu yenu. Basi kaeni nyumba ile ile, mkila mkinyya walivyo navyo wenyewe kwani mfanyaji wa kazi amestahili na ujira wake.

IDI YA WATAKATIFU SIMONI NA YUDA MITUME

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, hili kanisa lako umelijenga juu ya misingi ya mitume na manabii, nalo jiwe lake kuu la pembeni ni yeye Jesu Kristo : utupe kuungaman-

shwa sana katika umaja wa roho, kwa yale mafunzo yao, hata tufanywe sisi hekalu takatifu lenye kukubaliwa na wewe ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. Yuda 1-8

YUDA, mtumwa wa Yesu Kristo, nduguye Yakobo, waraka wangu huu uwafikilie hao walioitwa, wapeendwao katika Mungu Baba, walindwao kwa ajili ya Yesu Kristo : rehema na amani na mapenzi na yaongee kwenu. Wapenzi wangu, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia ninyi habari za wokofu ambaeo twasharikana pamoja, nilishurutishwa kuwaandikia ninyi niwahimize kwamba mjithadi sana kwa ajili ya hiyo imani waliopewa hao watakati, hiyo mara moja tu. Kwani wako wandalamu waliojitia kwa siri, hao ambaeo hapo kale walitangulia kuandikwa kwa hukumu hii, watu wasiomcha Mungu, wakiigeuza neema ya Mwenyezi Mungu wetu iwe ulanifu, na kumkanusha Mola wetu aliye pweke, naye ni Bwana wetu Yesu Kristo. Basi nataka niwakumbushe ninyi, ijapokuwa mwayajua mambo yote, hii mara moja tu, ya kwamba yeze Bwana akiisha kuwaokoa watu watoke nchi ya Misiri, baadaye akawaangamiza wale waliokuwa hawakuamini. Na malaika nao wasioilinda enzi yao wenye, lakini walilyaacha maskani yao yaliyowapasa, amewalinda katika pingu za milele chini ya giza hata hukumu ya siku ile kuu. Kama vile Sodoma na Gomora na miji ile iliyokuwa karibu nayo, wakiisha kujitia kwa uzinifu, mfanano mmoja vilevile na hao, na kufuata miili mingine, imewekwa wazi iwe kielelezo, katika adhabu ya moto wa milele. Na haya yote, hao nao, mfanano mmoja na wale, katika kuota kwao, wautia mwili najisi, na kuyaasi mamlaka, na kuyataja matukufu kwa uovu.

Injili. Yohana 15. 17-27

MAMBO haya nawaagiza, mpate kupendana ninyi kwa ninyi. Kwamba ulimwengu wawachukia ninyi, jueni kwamba ulinichukia mimi kwanza usijawachukia ninyi. Kwamba mu watu wa ulimwenguni, ulimwengu

ungependa ambacho ni chake ; lakini kwa hivyo ninyi msiviyokuwa watu wa ulimwenguni, na kwa vile mimi nilivyowachagua katika ulimwengu, ndipo ikawa ulimwengu wawachukia. Kumbukeni lile neno nililo-waambia : Mtumwa hawi mkubwa kuliko bwana wake. Kwamba waliniudhi mimi, na ninyi watawaudhi ; kwamba walishika neno langu, na lenu watalishika. Lakini hayo yote watawatenda kwa ajili ya jina langu : kwa kuwa hawamjui aliyenileta. Kwamba sikuja nikarena nao, wasingekuwa na dhambi : lakini sasa hawana udhuru wa hizi dhambi zao. Mwenye kunichukia mimi amchukia na Babaangu. Kwamba sikutenda kati yao kazi hizo ambazo hajazitenda mtu mwininge yoyote, wasingekuwa na dhambi : nao sasa wamekwisha kuniona na kunichukia, mimi na Babaangu pia. Ila haya yamekuwa, lipate kutimizwa lile neno lililoandikwa katika torati yao : la kwamba, Walinichukia bure. Lakini atakapokuja yule Msaaada nitakayewaletea mimi kutoka kwa Baba, naye ndiye Roho wa kweli mwenye kutoka kwa Baba, huyo ndiye atakayenishuhudia. Ninyi nanyi mta-shuhudia, kwa kuwa mu pamoja nami tangu mwanzo.

IDI YA WATAKATIFU PIA WOTE

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, wewe umewaungamanisha wateule wako wote kwa maungamano ya umoja na shirika iliyo katika mwili wake wa siri yeze Mwanayo Kristo Bwana wetu ; utupe nasi neema kuwafuata watakatifu wako wote waliobarikiwa kwa wema wa kila namna na mwendo wa haki, hata tuzifikilie na sisi furaha zisizosemeka, nazo ndizo ulizowatengezea hao wakupendao kweli ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Badala ya Waraka. Ufunuo 7. 2-12

NAMI nilimwona malaika mwininge akwea juu kutoka maawioni mwa jua, alikuwa na muhuri wa Mungu aliye hai : naye akawapigia ukelele wale malaika

wanne kwa sauti kuu, wale waliopewa kuidhuru nchi na bahari, akisema, Msiihdhuru nchi wala bahari wala miti, hata tukiisha kuwatia muhuri watumwa wa Mwenyezi Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao. Nami nilisikia hesabu ya hao walioitiwa muhuri, *ilikuwa ni* laki moja na elfu arobaini na nne, wenye kutiwa muhuri waliotoka kila kabilal a wana wa Isiraeli.

Wa kabilal la Yuda elfu kumi na mbili wenye kutiwa muhuri :

Wa kabilal la Reubini elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Gadi elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Asheri elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Naftali elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Manase elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Simeoni elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Lawi elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Isakari elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Zabuloni elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Yusufu elfu kumi na mbili :

Wa kabilal la Benjamini elfu kumi na mbili wenye kutiwa muhuri.

Baada ya haya niliona, nao huo ndio, mkutano mkubwa mno, ambao hapakuwa na mtu aliyeweza kuuhesabu, watoka kila taifa, nao ni wa kila kabilal, na jamaa, na lugha, walikuwa wamesimama mbele ya hicho kiticha-enzi na mbele ya huyo Mwana-wa-kondoo, walikuwa wamevikwa nguo ndefu nyeupe, nao walikuwa na makuti ya mtende mikononi mwao : nao wapiga ukelele kwa sauti kubwa mno, wakisema, Wokofu ni wa Mwenyezi Mungu wetu aktiye katika kiticha-enzi, tena ni wa Mwana-wa-kondoo. Na hao malaika wote walikuwa wamesimama kando-kando ya kiticha-enzi, na *kando-kando* ya wale wazee na wale nyama-wenye-uhai wanne ; nao wakapomoka mbele ya kiticha-enzi kwa nyuso zao, na kumsujidia Mwenyezi Mungu, wakisema, Amina : baraka, na utukufu, na hekima, na shukrani, na heshima, na uwemo, na nguvu zina Mwenyezi Mungu wetu hata milele na milele. *Amina.*

Injili. Mathayo 5. 1-12

NA alipowaona wale makutano akakwea mlimani, naklisha kuketi nchi akaendewa na wanafunzi wake ; akafunua kinywa chake, akawafunza : akisema, Wana heri wenyewe roho za kimaskini, kwa kuwa ufalme wa mbingu una wao. Wana heri wasikitikao, kwa kuwa ndio wata-kaotuzwa. Wana heri walio na upole, kwa kuwa wao ndio watakaoirithi nchi. Wana heri walio na njaa na kiu kwa *kutaka* na haki, kwa kuwa wao watashibishwa. Wana heri walio na rehemea, kwa kuwa wao watarehemewa. Wana heri walio safi moyo, kwa kuwa wao watamwona Mwenyezi Mungu. Wana heri wafanyao amani, kwa kuwa wao wataitwa wana wa Mwenyezi Mungu. Wana heri walioudhiwa kwa ajili ya mema, kwa kuwa ufalme wa mbingu una wao. Mna heri ninyi, wakati watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwasizingizia kila jinsi, kwa kunena uwongo, *ikiwa ni* kwa sababu yangu mimi. Furahiveni na kufunuka nyuso zenu, kwa kuwa ujira wenu ni mkubwa huko mbinguni. Kwani ni kama vile walivyo-waudhi manabii waliokuwako kabla yenu.

IDI YA MTAKATIFU MARIAMU MMAGIDALA

(July 22)

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, Mwanayo Mwenye-baraka alimwita na kumtakasa Mariamu Mmagidala awe shahidi wa kufufuka kwake : uturehemu na kutujalia kwa neema yako tupozwe katika unyonge wetu wote, na kukutumikia siku zote katika uwezo wa maisha ya milele ya Mwokozi wetu, ambaye pamoja na wewe na Roho Mtakatifu huishi na kutawala, Mungu mmoja milele. *Amina.*

Waraka. 2 Wakorintho 5. 14-17

KWANI mapenzi ya Kristo yatusonga ; maana, kwaamua hivi, ya kwamba mmoja akafa kwa ajili ya wote, basi wakafa wote ; naye akafa kwa ajili ya

wote, ili kwamba hao walio hai wasiwe hai kwa nafsi zao wenyeewe tena, lakini *ni kuwa hai* kwake ye ye aliye kufufuka kwa ajili yao na kufufuka tena. Hata imekuwa sisi mwanzo wa sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili ; na ingawa tulikuwa tukimfahamu Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumfahamu tena hivyo. Hata imekuwa mtu awaye yote akiwa ndani ya Kristo ni kiumbe kipyta ; vitu vile vyakale vimepita ; hivi ndivyo, vimikuwa vipyta.

Injili. Yohana 20. 11-18

NA Mariamu alikuwa amesimama kaburini kwa ndje, yuala ; basi yu hali ya kulia akachungulia ndani ya kaburi ; akaona malaika wawili wenye nguo nyeupe wameketi, mmoja upande wa kichwani, mmoja upande wa miguuni, hapo ulipolazwa mwili wa Yesu. Wakamwambia, Mwanamke, walilianiani ? Akawaambia, Ni kwa kuwa wamemwondoa Bwana wangu ; wala simjui walipomweka. Yuasema *maneno* haya akazunguka nyuma, akamwona Yesu amesimama, wala hamjui kuwa ndiye Yesu. Yesu akamwambia, Mwanamke, walilianiani ? Wamtafuta nani ? Yule amdhania ni mlinzi wa bustani, akamwambia, Ewe Bwana, kwamba umemchukua wewe niambie ulipomweka, niende mimi nikamwondoe. Yesu akamwambia, Mariamu ! Yule akazunguka, kisha akamwambia Kihibiranja, Raboni ! maana yake, Ewe Mwalimu. Yesu akamwambia, Usiniguse, kwani sijapaa kwenda kwa Babaang. Ila enda kwa ndugu zangu ukawaambie, Mimi napaa naenda kwa Babaangu, naye ndiye Babaenu ; naenda kwa Mungu wangu, naye ndiye Mungu wenu. Akaenda Mariamu Mmagidala akiwaeleza wanafunzi, ya kwamba, Nime-mwona Bwana ; akawaeleza na alivyambiwa naye *maneno* hayo.

KUGEUKA SURA

IDI YA KUGEUKA SURA

(August 6)

Sala

EWE Mungu, mbele ya kuteswa kwake Mwanayo mzaliwa pekee, ulifunua utukufu wake juu ya mlima mtakatifu ; utujalie sisi watumishi wako kumba tukiangalia kwa imani mwanga wa uso wake, tutiwe nguvu kuchukua msalaba, na kubadilishwa tuwe msfano mmoja na yeye, kutoka utukufu kufikilia utukufu ; kwa yeye Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Waraka. 1 Yohana 3. 1-3

ANGALIENI, ni mapenzi namna gani yeye Baba Aliyotupa sisi, kwamba tuitwe wana wa Mungu : nasi ndio. Kwa ajili ya hayo, hiyo dunia haitujui sisi, kwa sababu haikumjua yeye. Wapenzi wangu, tu watoto wa Mungu sasa, nalo halijafunuliwa bado hilo tutakalokuwa. Twajua ya kwamba, akifunuliwa, tutakuwa msfano mmoja na yeye ; kwa kuwa tutamwona yeye vivile kama alivyo. Na kila mtu aliye na matumaini haya kwake yeye, husafi nafsi yake vivile kama yeye alivyo safi.

Injili. Mariko 9. 2-7

KISHA baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petero na Yakobo na Yohana, akawakweza juu ya kilima kirefu peke yao faragha : akageuzwa sura zake mbele yao. Mavao yake yakawa ya kumemetuka, meupe mno, jinsi hiyo hakuna dobi mmoja duniani awezaye kuyatia weupe kama huo. Wakatokewa na Elija pamoja na Musa, nao wakisemezana na Yesu. Aka-jibu Petero akamwambia Yesu, Bwana mkubwa, ni vyema sisi kuwa hapa : na tufanye mahema matatu, moja lako wewe, na moja la Musa, na moja la Elija. Kwani hajui la kujibu ; kwa kuwa walikuwa wakichasana. Kilikuwa kiwingu kikawatia uvuli ; sauti ikatoka katika kiwingu, Huyu ndiye Mwanangu mpenzi wangu ; msikizeni yeye !

TARATIBU YA KUSONGEZA KARAMU YA BWANA ; AU, USHIRIKA MTAKATIFU

¶ *Kadiri ya walio na azima ya kushirikiana Ushirika Mtakatifu na wanepo majina yule Padre kabla ya jambo hilo, uchache ni usiku wa kuamkia siku ya kushirikiana.*

¶ *Na watu hao akionekana kwao mtu mwenye makosa yaliyo wazi, au aliyedhilimi mwenzive kwa maneno au kwa vitendo, ikawa ni sababu ya kulichukiza Kanisa ; yule Padre akiisha kupata hakika ya neno lile, humwiita yule miu akamvonya asisubutu kabisa kukaribia Meza ya Bwana, hata aishe kutoa dalili zilizo dhahiri za kutubia kwake kweli, na za ule mvendovo wake mbaya kugeuka ukarava mwema ; ili kwamba wapate kuridhika tena wale ambao mbele walichukiza katika Kanisa, kisha na wale aliowadhilimi nao awape haki zao ; au uchache ni kutoa ahadi ya kuwapa haki zao, atakapokwisha kupata nafasi.*

¶ *Ni vivyo hivyo, na watu atakaowona wa hali ya kukaliana kwa mfundo wa moyo na kuchukizana wenywewe kwa wenywewe, yule Padre huwatwaa kwa jinsi iyo hiyo ; asiwakubalie Ushirika wa Meza ya Bwana, hata awaone wansha kupatana. Na wale walifanya rofauti akitukubali yule mmoja kumsamehe mwenzive kwa moyo ulio safi kadiri ya aliyomkosa, na kusanya malipo, kwa kuwa naye alimchukiza mwenzive ; akawa yule wa pili hataki kuridhia umoja wa uchaa-wa-Mungu, yudumu hali ile ile ya upotofu na uchukizi ; hapo imempasa Padre kumpa ruhusa yule mwenye kutubia ya kuungia Ushirika Mtakatifu, akamkataza yule mishupavu. Isipokuwa kila awapo Padre kumsukumiza mtu kama ilivyoelvezwa katika maagizo haya katika upambanuzi huu, au huo uliotangulia, yamazimu kumwarifii habari yake yule Mwenye Amri kabla ya siku kumi na mne wala asizidi siku kumi na mne. Na yule Mwenye Amri humtenda yule aliye na makosa kama yaliyoagizwa katika Kanuni.*

¶ *Ile Meza ili hali imetandikwa nguo njema nyeupe ya katani, kwa kila zamani ya kushirikiana Ushirika, hukaa katikati ya Msikiti au katika Mwimbwamo, pale palipoagizwa kusaliva Sala za Asubuhi na Jioni. Na yule Kasisi ali hali amesimama pale penye Meza ya Bwana upande wa Kaskazini wa Meza, husema Sala ya Bwana, pamoja na Sala hiyo ifuatanyayo baadaye, wale watu wakiisha kupiga magoti.*

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo

mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. Amina.

Sala.

EWE Mwenyezi Mungu, kwako wewe miyo ya watu wote i wazi, na kila haja imejulikana, wala hakuna neno lililofichamana kwako ; uyasafi mawazo ya miyo yetu kwa kutuvuvilia Roho wako Mtakatifu, ili tukupende wewe kwa ukamilifu, tulitukuze na jina lako takatifu kama ipasavyo ; kwa Kristo Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Kasisi huwalekea wale watu, na kuwatajia Amri kumi zote kwa sauti ya kusikilikana ; na mwisho wa kila Amri wale watu, wali hali ile ile ya kupiga magoti, huitaka Mwenyezi Mungu msamaha wa hizo walizovicunja katika zamani zilizopita, wakaomba na neema wapate kuzishika mbeleni, wasije wakazivunja tena kama vile ; waseme namna hii :*

Kasisi.

MWENYEZI Mungu alinena maneno haya, huku Makisema, Mimi ni Yehova Mwenyezi Mungu wako. Usiwe na miungu mingine mbele zangu yoyote.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usifanye sanamu wa kuchonga, umbo lolote lililo juu mbinguni, au lililo chini duniani, au lililo chini ya dunia katika maji : usivisujidie, wala kuvitumikia : kwa kuwa mimi Yehova Mungu wako ni Mungu mwenye wivu, niwapatilizaye wana kwa uovu wa baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao ; na kuwapa rehema watu elfu elfu wanipendao, wayashikao maagizo yangu.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usitaje jina la Yehova Mungu wako kwa upuzi, kwani Yehova hatamfanya kuwa hana makosa mtu atajaye jina lake kwa upuzi.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Ikumbuke siku ya sabatu kuitakasa. Siku sita tumika, ufanye kazi zako zote ; ila siku ya saba ndiyo sabatu ya Yehova Mungu wako ; siku hiyo usifanye kazi, wewe, wala mwanayo mume na mke ; wala mtumwayo mume na mke ; wala nyama zako za mji ; wala mgeni wako aliye ndani ya malango yako ; maana, kwa siku sita Yehova alifanya mbingu na nchi, na bahari, na vyote vilivyo humo, akapumzika kwa siku ya saba ; ndipo akaibarikia Yehova ile siku ya sabatu, akaitakasa.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Mheshimu babaako na mamaako, siku zako zifanyike ndefu juu ya nchi upewayo na Yehova Mungu wako.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usiue.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usizini.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usiibe.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usimshuhudie mwenzio kwa uwongo.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze miyo yetu iishike amri hii.

Kasisi. Usitamani nyumba ya mwenzio, usimtamani mke wa mwenzio ; wala mtumwawe mume au mke ; wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala kiwacho chote alicho nacho mwenzio.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe uziandike miyoni mwetu amri zako hizi pia zote, sisi twakuomba sana.

| ¶ *Iko ruhusa kutosoma 'Amri kumi, isipokuua zisomwe (kwa uchache) mara moja kila mwezi siku ya Jumapili ; kisha wakati wa kutozisoma, mafupizo ya sheria yaliyotolewa na Bwana wetu yasomwe badala yake :*

Kasisi. Bwana wetu Yesu Kristo alisema : Sikiza,

Isiraeli ; Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja ; nawe mpende Bwana Mungu wako katika moyo wako wote, na nafsi yako yote, na nia yako yote, na nguvu zako zote. Hilo ni agizo la kwanza. La pili ni mfano wake, nalo ni hili : Mpende mwenzio kama nafsi yako. Hakuna jingine tena katika maagizo lililo kubwa zaidi ya haya. Katika maagizo mawili hayo imetundamana torati yote na manabii wote.

Watu. Bwana, uturehemu, nawe utulekeze mioyo yetu iishike amri hii.

¶ *Hapa hufuata moja ya Sala mbili hizi za kumwombea Mfalme, yule Kasisti ali amesimama kama vile, husema :*

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, ufalme wako hauna mwisho, Euwezo wako hauna upungufu ; ulirehemu kanisa lako pia lote ; nawe uutawale sana sana moyo wa mtumishi wako mteule wako **GEORGE**, Mfalme wetu, Mtawala wetu, hata yeye (kwa kumjua ni nani huyo amtumikiaye), mbele ya yote atafute kwanza mambo ya heshima yako wewe na utukufu wako wewe : na sisi na raia zake wote (kwa kule kufikiri kwetu ni nani aliyempa amri hiyo aliyonayo), tuwe wenye kumtumikia kwa uaminifu, na kumheshimu na kumtii kwa unyenyekeyu, katika wewe na kwa ajili yako, sawasawa na Neno lako na Maagizo yako mema ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala daima pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele. *Amina.*

Au hii,

EWE Mwenyezi Mungu, Mkazi wa milele, sisi huji-funza katika Neno lako takatifu ya kuwa mioyo ya wafalme i mkononi mwako, nawe huigeuza na kuiongoza kama uonavyo vyema kwa hekima yako ya Uungu ; sisi hapa tulipo miguuni pako, twakuomba kwa ajili ya Mfalme wetu, Mtawala wetu, **GEORGE**, mtumishi wako, ya kwamba wewe uugeuze na kuuongoza moyo wake sana, katika mawazo yake, na maneno yake, na vitendo vyake pia vyote, hata awe katika kuitafuta daima heshima yako

wewe na utukufu wako ; afanye bidii kuwatunza hao watu wako uliowatia mkononi mwake, apate kuwaweka hali ya nafuu na amani na uchaji-wa-Mungu : na haya twakumba, ewe Baba mwenye huruma, kwa ajili ya Mwanayo, Mpenzi wako, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo husomwa Sala ya siku hiyo. Nayo ikiisha kusomwa hiyo Sala, yule Padre husoma Waraka, akisema, Waraka (au, Fungu la Maandikoni lililoagizwa badala ya Waraka) umeandikwa katika Mlango kadhawakadha wa Waraka kadha, mwanzo Kifungo kadha. Nao ukiisha kusomwa ile Waraka, husema, Waraka umekoma hapa. Ndipo hapo husomwa Injili (watu huinika na kusimama wote) akisema, Injili takatifu imeandikwa katika Mlango kadhawakadha wa Injili kadha, mwanzo Kifungo kadha. Nayo ikiisha kusomwa ile Injili huimbwa au husomwa Imani hii ifuatanyo, watu wakali wamesimama kama vile.*

NAAMINI kwa Mwenyezi Mungu mmoja, Baba Mweza wa yote, Muumba mbingu na nchi, Na vitu vyote, vionekanavyo na visivyoonekana :

Tena kwa Bwana mmoja Yesu Kristo, Mwana wa Mungu Mzaliwa pekee, Mwenye kuzaliwa na Babaye kabla ya zamani zote, Mungu katika Mungu, Nuru katika Nuru, Mungu kweli katika Mungu kweli, Mwenye kuzaliwa wala si mwenye kuumbwa, Tabia yake ya asili na hiyo ya Baba ni mamoja, Tena kwa yeye vitu vyote viliumbwa : Naye kwa ajili yetu wanadamu na wokofu wetu alishuka kutoka mbinguni, Akafanyizwa mwili na Roho Mtakatifu kwa Mwanamwali Mariamu, Akafanywa binadamu, Naye akasalibiwa kwa ajili yetu katika enzi ya Pontio Pilato. Akateswa, akazikwa, Hata siku ya tatu akasimama tena, kama alivyoandikiwa katika Maandiko, Kisha akapaa akaingia mbinguni, Naye ameketi upande wa kuumeni wa Baba. Kisha atarudi na utukufu awaamue walio hai hata waliokufa : Na ufalme wake hauna mwisho.

Tena naamini kwa Roho Mtakatifu, Bwana, Mpaji wa uzima, Atokaye mwa Baba na Mwana, Naye pamoja na Baba na Mwana ni mwenye kuabudiwa na kutukuzwa kama vile, Naye ndiye aliyesema kwa vinywa vya manabii. Tena naamini kanisa moja lililo ulimwenguni mote, kama

lilivyowekwa na mitume. Ninakiri ubatizo mmoja wa kusamechewa madhambi, Nami nangojea waſu kufufuka, na maisha ya ulimwengu ujao. Amina.

I Kisha yule Padre huwaeleza wale watu mna Siku kuu gani au Siku za kufunga gani katika juma hilo lijal, ambazo zataka kushikwa. Kisha pawapo na sababu huwapa habari ya siku ya Ushiriko ; tena husomwa hati za maana, na notisi, na za kuzuiliwa waliokosa. Wala lisitangazwe neno wala kuhubiriwa humu misikitini katika muda wa Ibada ya Mungu, isipokuwa kwa kinywa cha yule Padre : wala yeye naye asitangaze wala kuhubiri neno ilia ambalo limeamriwa katika Kanuni za Chuo hiki, au lilioagizwa na Mfalme, au na Mwenye Amri ya Ibada aliye na pahali hapo.

I Haya hufuata Hotuba, au Maudha yoyote katika hayo, yaliyokwisha kuandaliwa, au yatakayoandaliiwa huko mbele, kwa amri ya wakubwa.

I Kisha yule Kasisi hurudi pale penye Meza ya Bwana, na kuyaanziliza Matoleo ya Sadaka, kwa kutamka Aya hizi, moja au zaidi, zifuatanazo hapo, kama aonavyo kufaa sana moyoni mwake.

NA mwanga wenu ung'are vivyo mbele ya watu, hata wazione kazi zenu nzuri, warmtukuze na Babaenu aliye mbinguni. *Mathayo 5. 16.*

Msiweke hazina zenu za akiba juu ya nchi, napo ndipo nondo na kutu viharibupo, na wevi hutoboa na kuiba ; ilia hazina zenu za akiba ziwekeni mbinguni, pasipoharibika kitu kwa nondo wala kutu, na wevi hawatoboi wala hawaibi. *Mathayo 6. 19-20.*

Basi na mambo yote kadiri myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni kadhalika. Kwani hiyo ndiyo torati na manabii. *Mathayo 7. 12.*

Si kila mmoja aniambiyaye, Bwana, Bwana, atakayeingia ndani ya ufalme wa mbingu : lakin ni afanyaye mapenzi ya Babaangu aliye mbinguni. *Mathayo 7. 21.*

Akasimama Zakayo akamwambia Bwana, Hivi ndivyo, Bwana, nusu ya vitu vyangu nawapa maskini, nami kwamba nimemnyang'anya mtu kwa njia ya hila katika neno lolote, namrudishia mara nne. *Luka 19. 8.*

Ni askari yupi atumikaye majira yoyote kwa gharama zake mwenyewe ? ni nani atuliate kiunga cha mizabibu,

naye asile matunda yake ? au ni nani alishaye kundi la nyama, naye asinywe maziwa ya kundi ?

I Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je, ni neno kubwa kwamba tutavuna vitu vyenu vya mwili ni ?

I Je, hamjui ya kwamba hao watumikao katika mambo ya hekalu, hula vitu vya hekaluni, na hao watumikao madhabahu wana sehemu yao pamoja na hayo madhabahu ? Ni vivyo hivyo, Bwana aliagiza kwamba hao waitangazao ile habari njema watapata kuishi katika hiyo habari njema.

I *Wakorintho 9. 13-14.*

Apandaye kwa choyo naye huvuna vya choyo. Apandaye kwa ukarimu, naye huvuna vya ukarimu. Kila mtu na afanye kama alivyoazimia moyoni mwake, si kwa kinyongo wala kwa lazima, kwani Mwenyezi Mungu yuampenda mtu apaye kwa kufurahi.

I *Wakorintho 9. 6-7.*

Ila yeye afunzwaye lile neno, na afanye ushirika na huyo afunzaye katika vitu vyema vyote. Msidanganyike, Mungu hafanyiwi dhihaka : kwani binadamu hicho apandacho, atakuja kuvuna hicho. *Wagalatia 6. 6-7.*

Basi hivi, kama tutakavyokuwa na nafasi, na tuwfanyie vyema watu wote, hasa hao jamaa wenye kuamini.

I *Wagalatia 6. 10.*

Ila uchaji-wa-Mungu pamoja na moyo uliokinai ni pato kuu : kwani hatukuingia na kitu ndani ya ulimwengu, kwa kuwa hata kutoka na kitu hatuvezi.

I *Timotheo 6. 6-7.*

Uwaagize hao walio matajiri katika zamani hizi za sasa, kwamba watende mema, wawe matajiri kwa kazi nzuri, wawe wapaji-wa-vitu, na wenye kufanya ushirika na wengine kwa moyo ; huku wakiziwekea akiba nafsi zao msingi mzuri hata wakati ujao, ili kwamba waushike uhai huo ambaao ndio *uhai* halisi.

I *Timotheo 6. 17-19.*

Kwani Mwenyezi Mungu hana batili hata akaisahau kazi yenu, na mapenzi yenu mliyoyaonya ya jina lake, kwa kuwatumikia kwenu watakatifu, nanyi mwawatumikia.

I *Wahibirania 6. 10.*

Ila msisahau kutenda mema na kushirikiana, kwani dhabihu namna hizi Mwenyezi Mungu huzifurahia.

Wahibirania 13. 16.

Ila yeye aliye na vitu-vipasavyo-maisha ya dunia hii, kisha akamwona nduguye ni mwenye kuhitaji, naye akazifunga huruma zake zisimfikilie, hayo mapenzi ya Mwenyezi Mungu yakaaje ndani yake huyo ?

1 Yohana 3. 17.

Wewe toa katika ulivyo navyo, usimgeuzie uso wako maskini awaye yote. Kwani ufanyapo hiyo utauona uso wa Bwana haugeuzwi kwako wewe. *Tobiti 4. 7.*

Uwe mwenye huruma kwa jinsi upatavyo. Utakapokuwa na kingi, toa kwa wingi ; utakapokuwa na kidogo, katika hicho kidogo wewe fanya bidii kumpasha mwenzio kwa ukarimu. Kwani kwa haya utaweka akiba njema ; utakuwa nayo kwa siku ya uhitaji. *Tobiti 4. 8.*

Mwenye kumhurumia maskini yuamkopesha Yehova, naye atamlipa hicho kitendo chake chema tena.

Mifano ya Maneno 19. 17.

Yu heri amkumbukaye maskini ; Yehova atamwokoa siku ya taabu. *Zaburi 41. 1.*

¶ *Muda zisomwapo aya hizi, wale mashemasi, au wale walinzi wa msikitii, au mitu mwininge afaaye mwenye kureka kwa ajili ya hayo, huzipokea katika kile kitasa kiwekwacho kwa haja hiyo na waabuduo mle msikitii sadaka za kuperwa maskini, na vingine vitakavoyotewa na wale watu kwa ajili ya Ibada : wakisha kumpelekea yule Kasisi kwa namna ya ibada, naye hukisongeza kile kitasa kwa unyenyekevu na kukiweka juu ya Meza takatifu.*

¶ *Na pawapo na Ushirika, yule Kasisi hutweka juu ya Meza Mkate na Divai kadiri ya aonavyo kutosha kwa haja ile. Hata yakiisha kufanywa hayo, yule Kasisi humena,*

Na tuiombee hali yake Kanisa la Kristo lililo katika vita hapa duniani.

EWE Mwenyezi Mungu uishiye milele, wewe umetu-funza kwa mtume wako mtakatifu kuwfanyia sala na maombi na shukrani watu wote ; sisi tu miguuni pako

twataka kwako kwa ajili ya rehema zako nytingi (*uzipokee sadaka zetu na matoleo yetu, nave hizi) sala zetu tunazotoa kwako, ewe Mungu Mfalme wetu, uzikubali ; huku tukikuomba wewe kulivuvia daima kanisa lako lililo ulimwenguni mote roho ya kweli

* Na pasipotozwa sadaka wala matoleo ndipo maneno haya (uzipokee sadaka zetu na matoleo yetu) yatarukizwa.

na umoja na kupatana : nave utupe ya kwamba wote walikubalio jina lako takatifu wapatane katika kweli ya Neno lako takatifu, na kuishi kwa umoja na mapendano ya uchaji-wa-Mungu. Tena, twataka kwako uwaokoe na kuwalinda wafalme wa Kikristo na maseyidi na wenyenzi pia wote ; na sana twamwombea mtumishi wako **GEORGE** Mfalme wetu ; tupate kutawaliwa chini yake kwa haki na utulivu ; nave uwape washauri wake wote, na waliopewa amri chini yake, kila mmoja, ya wao kuamua kwa kweli pasipo kufanya upendeleo, huku kwa kuadhibu uovu na shari, na huku kwa kuitunza dini yako ya kweli na mambo yaliyo mema. Uwape neema, ewe Baba wa mbinguni, mabishopu wote na watanzao roho za wenziwao, ili kwamba wao, kwa maisha yao na mafunzo yao wali-funue wazi Neno lako la kweli, na uhai, na Sakramenti zako takatifu wazisongeze kama taratibu yake kwa haki. Na watu wako wote uwape neema yako ya mbinguni ; na sana mukutano huu uliopo hapa ; ili kwamba, kwa miyo ya kunyenyeka na ibada ilio sawa, walisikize Neno lako takatifu, na kulipokea wakikutumikia wewe kwa utakatifu na haki siku zote waishizo duniani. Na sana twataka kwako, kwa kunyenyeka sana, kwa ajili ya wema wako, ewe Bwana, uwatalize na kuwasaidia wote ambao kwamba katika maisha haya yasiyodumu wamepatikana na mashaka, huzuni, uhitaji, ugonjwa, au baa nyininge iwayo yote. Kisha na jina lako takatifu twalishukuru kwa asante, kwa ajili ya watumishi wako wote waliofariki dunia katika imani yako na kicho chako : huku tukitaka kwako utupe nasi neema, tupate kufuata sana viclelezvo vyao vizuri, hata iwe sisi pamoja na wao kuurithi ufalme wako wa mbinguni : utupe haya, ewe Baba, kwa ajili ya Yesu Kristo, aliyekaa pweke Mwombezi wetu kati yetu sisi na wewe. *Amina.*

¶ Wakati aitangazapo habari yule Padre, ni siku gani utakaosongezwa Ushirika Mtakatifu (naye hufanya hivi siku zote kwa siku ya Jumapili au siku mojawapo katika Siku kuu za ibada ilio mbele ya siku hiyo, kwa karibu), baada ya kwisha kuhubiri, husoma Masisitizo haya yafuatanyo hapa.

E NYI wapenzi, kwa siku ya . . . ijayo mimi nakusudia E kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, kuwasongeza hao wote watakoakuwa na nia ya uchaji-wa-Mungu na ibada, Sakramenti hiyo yenye kutuliza itiayo nguvu sana ya Mwili na Damu ya Kristo ; ipate kupokewa na wao kwa kuukumbuka Msalaba wake na Mateso yake yaliyo na mafaa mengi ; ambayo kwa hayo peke yake sisi twapata msamaha wa madhambi yetu, na kufanywa ɿuwa washirika wa Ufalme wa mbingu. Basi kwa ajili ya hayo imetupasa kumpa Mwenyezi Mungu Babaetu wa mbinguni shukrani zilizo nyenyekevu sana, za ndani sana, kwa aliyotupa Mwanawe Mwokozi wetu Yesu Kristo, naye si kwamba apate kufa tu kwa ajili yetu, ila na apate kuwa ni chakula cha roho zetu cha kututia nguvu kwa hiyo Sakramenti takatifu. Nalo neno hilo la Mwenyezi Mungu likiwa lawatia nguvu na utulivu hao walipokeao kama ifaavyo kulipokea, lina na hatari mno kwa wasubutuo kulipokea ili hali hawafai kulipokea ; mimi lililonipasa sana ni kuwaonya ninyi na mapema, muwe katika kufikiri siri hii takatifu jinsi ilivyotukuka, na ilivyo na hatari itakapopokewa na watu ambao hawafai ; na jinsi mtakavyo-ypeleza na kuyapima yaliyo katika mioyo yenu (si juu-juu kama wanafiki kwa Mungu) ; mpate kujilia karamu ya ki-mbinguni namna hiyo kwa hali takatifu na usafi, mli hali mmeyavaa mavao ya arusi hayo ambayo yalilazimishwa na Mwenyezi Mungu katika Maandiko matakatifu, ili mpate kukaribishwa kama wenye kufaa kushirikiana katika Meza hiyo takatifu.

Njia yake basi, jinsi yake, itupayo kuyapata mambo hayo, ni hivi : Kwanza, mpelcleze katika maisha yenu na mazungumzo yenu kwa kuyalinganisha na Maagizo ya Mwenyezi Mungu ; na katika hayo mijionayo wenyeve mmeekosa mimo, kwa kupenda, au kunena, au kutenda, mlilie mambo yenu yalivyo na dhambi, na kuungama kwa Mwenyezi Mungu, kama wenye kukusudia sana kuyare-

jeza maisha yenu hali mpya. Nanyi mtakapoyaona makosa yenu kuwa hamkumkosa Mwenyezi Mungu tu, mmewakosa na wenzenu, ndipo hapo mtajipatanisha nao ; mridhie kurejeza na kulipa, kwa hali na mali, kadiri ya mtakavyoweza, katika kila milomtenda mwenzenu awaye yote la madhara au batili ; mridhie na kuwasamehe wenzenu nao waliowakosa ninyi, kama vile wenyeve mpendavyo impate kwa Mwenyezi Mungu naye msamaha wa makosa yenu ; kwani msipokaa hali hiyo, kule kushirikiana Ushirika Mtakatifu hakutawafa neno, mtazidi kuwa hali ya kupasa mapigo. Basi pakiwa pana mtu kwenu atukanaye Mungu, au aliye mzuizi au mwenye kupinga Neno lake ; ni mzinifu, au yuna mfundo, au husuda, au aliyetenda neno jingine la hatari lolote, ninyi mlivo hivi tubieni kwa madhambi yenu, au msiikaribie Meza ile takatifu ; msije mkaingiwa na Ibilisi ndani yenu baada ya kwisha kuitwaa ile Sakramenti takatifu, kama alivyointiwa Yudasi, akawajaza ninyi Ibilisi maovu kila jinsi, akawatia katika uangamivu wa roho pamoja na wa mwili.

Na kwa kuwa haifai mtu kuingia katika Ushirika Mtakatifu ila awapo anazitumaini kabisa rehema za Mwenyezi Mungu, yuna na moyo uliotulia ; ni hivyo, akipatikana mtu kwenu, moyo wake hakupata kuutuliza kwa jinsi hiyo, ajijua ni mhitaji wa kupewa faraja, au yuataka shauri, mtu huyo na aje kwangu au kwa mwingine mtumishi wa Neno lake Mwenyezi Mungu aliye na busara na elimu ya utakatifu, akayaseme yaliyomtia majonzi ; ili kwamba kwa kusongezewa Neno takatifu la Mwenyezi Mungu ayapokee mtu huyo manufaa ya ondoleo la dhambi, apewe na mashauri ya ki-rohoni, aambilie na maneno ya kumwonya njia, atulie moyo wake, na kuondoa kila shida na tashwishi.

¶ Au, awaonapo kwamba hawana bidii ya kuja kwa Ushirika Mtakatifu, badala ya yale hutumia masisitizo haya :

NDUGU zangu niwapendao mno, kwa siku ya . . . ijayo mimi kwa fadhili za Mwenyezi Mungu nakusudia kuifanya Karamu ya Bwana : basi ninyi nyote

mliopo hapa nawaalika mje katika karamu hiyo ; kisha kwa ajili ya Bwana Yesu Kristo nawaomba mwito huu msiukatae, nanyi awaalikaye na kuwaita ni Mwenyezi Mungu mwenyewe, kwa kule kuwapenda kwake sana. Au wenyewe hamwoni jinsi liliyo neno ovu na ubaya, aandaapo binadamu karamu ya vyakula vyema kwa gharama nydingi, akaandika na meza ya vinono, asisaze lolote ila la kuwakaribisha awaitao, nao wakakataa pasipokuwa na sababu, wasimtolee hata asante ! Hata ninyi mkitokewa na neno kama hili, asiyekasirika ni nani ? Ni nani asiyefikiri, Mimi nimeonewa, mimi nimedhilimiwa ? Basi ninyi nanyi, wapenzi sana sana katika Kristo, jilindeni wenyewe msije mkamtaia hasira Mwenyezi Mungu juu yenu mtakapo kujitenga na hii karamu yake iliyo takatifu sana. Ni upesi kusema mtu, Neno hili la Ushirika mimi siingii, maana nimeshikwa na udhuru mimi, nimezuiwa na mambo ya ulimwengu. Lakini je ! kwa Mwenyezi Mungu udhuru kama huo nao utakubaliwa kuwa ni neno la maana ? Au mtu akisema, Mimi nina dhambi sana, jinsi nilivyo mwenye dhambi mimi, basi nacha : ndipo nami nisije. Ninyi mbona hamtaki kutubia ? Wala hamzingatii ? Hivyo mlivyoalikwa na Mungu, je, hamwoni haya kusema, Hatuji ? Hivyo ilivyowapasa kurejea kwa Mwenyezi Mungu, mtatoa udhuru wa nafsi zenu mseme, Hatu tayari ? Fikirini basi wenyewe kwa wenyewe, jinsi usivyoaa udhuru wa uwongo kama huo mbele za Mwenyezi Mungu ! Wale waliokataa ile karamu ya Injili, wakasema, Tumenunua mashamba ; au, Twataka kwenda kuangalia jozi zetu za ng'ombe ; au, Tumeoa wake ; hawakuachiliwa kuwa wana udhuru hivyo, walihesabiwa hawafai kamwe kuila karamu ile ya ki-mbinguni. Basi mimi langu sitawacha ; Mwenyezi Mungu akipenda, nitakuwapo tayari ; nami kwa hayo niliyowekewa juu yangu ya utumishi huu nilio nao, nawaalika ninyi hivi sasa kwa jina lake Mwenyezi Mungu, nawaita kwa ajili ya Kristo, nawaonya kwa hivyo wenyewe mpendavyo kuokoka, mje nkashirikiane Ushirika Mtakatifu huu niwaalikao. Basi, kama vile Mwana wa Mungu alivyokubali kuutoa uhai wake kuutia katika kufa, alipoangikwa juu ya

msalaba kwa kuutuma wokofu wenu, nanyi ni vivyo inawapasa kuupokea Ushirika huu nao kwa kuikumbuka sadaka ya mauti yake yule, huku mkiyafuata mwepywewe aliyowausia. Msipofanya hivi, fikirini wenywewe, jinsi mtakavyomtenda Mwenyezi Mungu ya jeuri, fikirini na adhabu yake ilivyo kali, itakayokuja ilewe-lewe juu ya vichwa vyenu, mkiijiepuu kusudi na hii Meza ya Bwana, na kujitenga na hawa ndugu zenu wajao kula Karamu hiyo ya Chakula, ambacho ni cha mbinguni halisi. Mambo haya mkiyawaza miyioni kwa bidii, kwa neema ya Mwenyezi Mungu mtatibu na kurejea akili njema, nalo ni neno ambalo kwamba hatutawacha kuwaombea kwa kumnyeukea Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye Babaetu wa mbinguni, mlipate.

¶ Wakati wa kusongezwa ule Ushirika, wale watu watakaoshirikiana wakiisha kukaa kama watakavyopata kusongezewa taratibu Sakramenti takatifu, yule Kasisi husoma maonyo haya :

ENYI wapenzi sana katika Bwana, ninyi mlionna nia ya Ekuja kuingia Ushirika Mtakatifu wa Mwili na Damu vyake Mwokozi wetu Kristo, inawapasa kufikiri jinsi mtakatifu Paulo awasisitzavyo watu wote kufanya bidii ya kuijaribu miyo yao na kuipima, kwanza wasijasubutu kula katika Mkate ule na kunywa katika Kikombe kile. Kwani kama vile yalivyo mengi sana yale manufaa yake, iwapo tuna kweli ya moyo uliotubu, na imani iliyo hai, katika kuipokea Sakramenti hiyo takatifu, (kwani hapo ndipo tuulapo kwa jinsi ya rohoni ule Mwili wake Kristo, na kuinwyala ile Damu yake ; tukawa kukaa katika Kristo, Kristo akakaa ndani yetu ; tukawa kitu kimoja na Kristo, na Kristo nasi :) basi na ile hatari nayo huwa nydingi vivyo, iwapo twaipokea siri hiyo kwa jinsi isivyoaa. Kwani hivyo itakuwa sisi kuwa wakosa katika Mwili na Damu vyake Kristo Mwokozi wetu : twaila na kuinwyala hesabu ya hukumu yetu, kwa kule kutouona Mwili wake Bwana ; twamkasirisha Mwenyezi Mungu ; twamsongeza katika kutupiga kwa maradhi mengine mengine, na mauti namna namna. Basi, ndugu zangu, jihukumuni wenyewe msije mkahukumiwa na ye ye Bwana ; tubieni

sana wenyewe kwa madhambi yenu yaliyokwisha kupita ; iweni na imani iliyo hai kwa Kristo Mwokozi wetu, isiyoweza kurukusika ; tenegezeni maisha yenu, muwe wenyewe kupendana na watu wote ; ni hivyo mtakuwa watu mfaao kuwamo katika siri hizi zilizo takatifu. Na zaidi ya yote, juu ya yote, ninyi mmekuwa watu wa kumshukuru kwa kunyenyeka mno Mwenyezi Mungu, kwa miyo yenu yote, Mungu Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, kwa vile alivyoukombo ulimwengu kwa kufa kwake na kuteswa kwake yeze Mwokozi wetu Kristo, ambaye mwenyewe ni Mungu kisha ni Binadamu, aliyejifanya mdogo, hata ikawa yeze kuyakubali mauti ya Msalabani, kwa ajili yetu wenyewe dhambi wanyonge, tuliokuwa tumelala gizani katika uvuli wa mauti ; ili kwamba' apate kutufanya kuwa wana wa Mwenyezi Mungu, na kututukuza hata maisha yasiyokuwa na ukomo. Naye kwa vile alivyonaka tuyakumbuke daima yale mapenzi makuu ya Bwana wetu, Mwokozi wetu pekee, Yesu Kristo, alipokufa kwa ajili yetu, tusije tukayasahau popote manufaa yasiyohesabika aliyatupa kwa kutoa damu yake ya thamani ; ameweka na kuanziza siri ambazo ni takatifu, ili ziwe dalili za mapenzi yake, na ukumbusho wa daima wa kufa kwake, kwa kutuvutia faraja na utuliu mkuu visivyokoma. Basi na tumpe yeze, pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, kama iliviotupasa sana, shukrani ya daima, kwa kuijiweka wenyewe kabisa chini ya radhi yake na mapenzi yake matakatifu, tufanye na bidii kumtumikia kwa utakatifu na haki ya kweli siku zote za maisha yetu.

Ndipo hapo Kasisi huwaambia hao wausongeo Ushirika Matakifu maneno haya :

NINYI mtubiao kwa dhambi zenu kwa kweli, mlio na toba ya miyoni, mu katika kupendana na kusameheana na wenzeni, mna na nia ya kuyafanya upya maisha yenu, kwa kuyafuata maagizo ya Mwenyezi Mungu, kutaka kwenenda rokeaa sasa katika njia zake takatifu : songeeni hapa kwa imani mje mkaitwae Sakramenti takatifu hii, mpate kuituliza miyo yenu ; tena ungameni kwa Mwenyezi Mungu kwa kumnyenyeka, mpige magoti kwa upole.

Hapo wakaungamishwa na mmoja katika wale mapadre waliopo maungamo haya ya waliopo wote, kwa jina lao wote walio na nia ya kushirikiana katika Ushirika Mtakatifu ; yule Padre husoma akipiga magoti, na waliopo wote nao hupiga magoti kwa kujitweza, waseme :

EWE Mwenyezi Mungu uwezaye mambo yote, Wewe Endiwe Babaye Bwana wetu Yesu Kristo, nawe ndiwe Mtenzi mambo yote, Kisha ndiwe Mwamuzi wa watu wote : Sisi madhambi yetu na maovu yetu namna namna, Tu katika kuyaungama na kuyalilia, Tuliyokuwa tukiyatenda mara kwa mara, kwa njia ya mawazo, na maneno, na vitendo, kwa kukuchukiza mno mno, kwako wewe Mwenye Enzi ya Uungu, Huku tukikutia kasirani, na machungu ya haki. Sisi twatabia sana, Tumeona vibaya kwa kweli, Kwa ajili ya ukenguefu wetu huu ; Mambo haya tuyakumbuko yatuchukiza wenyewe ; Mzigo wake hauchukuliki kamwe. Uturehemu, uturehemu, ewe Baba mwenye rehema nydingi ; Kwa ajili ya Mwanayo Bwana wetu Yesu Kristo, utusamehe yote hayo yaliyopita ; Utupe ya kwamba mwanzo wa sasa tuendelee siku zote, Katika kukutumikia na kukupendeza, Kwa upya wa maisha, Kwa kulihestimu na kulitokuza jina lako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

Ndipo hapo asimamapo yule Kasisi, au husimama yule Bishopu akiwa yupo, hata akiisha kuwalekea wale watu akanena Ondoleo hili la madhambi.

MWENYEZI Mungu, Babaetu wa mbinguni, ambaye kwa wingi wa huruma zake amewapa ahadi ya msamaha wa madhambi wote hao wageukao kulekea kwake yeze kwa toba ya moyoni na imani ya kweli : awarehemu ninyi ; awasamehe na madhambi yenu yote na kuwaokoa nayo ; awakaze na kuwatia imara hata muutimize wema wote : awatieve katika uzima wa milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

Hapo yule Kasisi husema,

SIKIZENI maneno yalivyo mazuri ya kumtuza mtu moyo Mwokozi wetu Kristo awaambiayo wote hao warejeao kweli kumlekea yeze.

Njoni kwangu ninyi nyote mtaabikao kwa kazi nzito, mliolemelewa na mizigo, nami nitawapumzisha.

Mathayo 11. 28.

Mwenyezi Mungu jinsi alivyoupenda ulimwengu, amewapa *watu* Mwanawe mzaliwa pekee, kila mwenye kuamini kwake asipatee, awe na uzima wa milele.

Yohana 3. 16.

Sikizeni na aliyojanena mtakatifu Paulo.

Ni la kuaminipa lilo neno, tena lapasa kila kukubaliwa, ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi.

1 Timotheo 1. 15.

Sikizeni tena yaliyonenwa na mtakatifu Yohana.

Na atakafanya dhambi mmojawapo, tuna mwenye kutuombea kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki : naye ndiye dhabihu wa dhambi zetu.

1 Yohana 2. 1-2.

¶ *Hata baadaye yule Kasisi huendelea kunena,*

Ikuzeni miyo yenu.

Huitika. Twaikuza hata kwa Yehova.

Kasisi. Na tumshukuru Bwana wetu, Mwenyezi Mungu.

Huitika. Ndio wajibu wetu ; ndiyo yanayopasa kama haya.

¶ *Ndipo hapo yule Kasisi huilekeea Meza ya Bwana, na kunena,*

NDIO wajibu wetu wa haki, ndiyo yanayotupasa sana, na kutulazimu ; ya sisi kila wakati na kila pahali kusema asante kwako wewe Bwana, *Maneno yale* (Baba Baba Mtakatifu, Mwenye nguvu Mtakatifu) *hurukizwa* zote, Mwenyezi Mungu, usiye mwa-*kwoa Jumapili ya Utatu.*

¶ *Hapo hufuata dibaji zilizohusika kwa zamani zake ; ila siku nyininge zote huendelea na kusema,*

KWA ajili ya hayo sisi nasi pamoja na malaika na malaika wakuu, na jeshi lote la mbinguni, tu katika kulisifu na kulikuza jina lako tukufu, huko tukikutukuza milele, twanena, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Yehova Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu

wako : utukufu uwe kwako, ewe Mwenyezi Mungu uliyee juu. *Amina.*

DIBAJI ZILIZOHUSIKA

Kwa Siku ya Christmas, na siku saba ziandamazo baadaye

KWA vile uliviyotupa Mwanayo Mzaliwa pekee Yesu Kristo akazaliwe kwa ajili yetu kama majira haya ya sasa ; ambaye kwa ule utendaji wake Roho wako Mtakatifu, alifanyika binadamu halisi katika mwili wake yule mwanamwali Mariamu mamaye ; asipatikane na kipaku cha dhambi kiwacho chote, ili atusafi na dhambi zote : Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *wa kadhalika.*

Kwa Siku ya Ufufuo, na siku saba ziandamazo baadaye

ILA litupalo kkusifupu sana, ni ile habari tukufu ya kufufuka kwake Mwanayo Bwana wetu Yesu Kristo ; kwani ndiye Mwana-wa-kondoo wa Pasaka halisi, aliye-tolewa kwa ajili yetu, akaaondo makosa ya ulimwengu ; ambaye kwa kufa kwake aliyangamiza mauti, na kwa kufufuka kwake kurejea uhai aliturejezea uzima wa milele ; Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Siku ya Kupaa, na siku saba ziandamazo baadaye

KWA ajili ya Mwanayo umpendaye sana, naye ndiye Bwana wetu Yesu Kristo ; ambaye baada ya ile habari tukufu ya kufufuka kwake, aliwatokaewa waziwazi mitume yake wote, akaonekana kwao ali hali yuapaa juu kwenda mbinguni, akaenda kutufanyia pahali pa kukaa ili kwamba huko akaako yeye na sisi tupae kwenda kuko, tuwe watu wa kukaa na kutawala pamoja naye katika utukufu ; Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Siku ya Pentecost, na siku sita ziandamazo baadaye

KWA ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu ; ambaye kilikuwa ni kwa ahadi yake ya kweli sana Roho Mtakatifu aliviyotushukia kama wakati huu kutoka mbi-

nguni, pamoja na kivumi kikuu kilichokuja ghafula, kama cha dharuba kuu ya upepo, yuna na mfano wa ndimi za miali ya moto, zilizotenga juu ya vichwa vyao wale wanafunzi, kwa kuwafunza na kuwaongoza katika kweli yote : akawapa vipawa vya lugha mbali-mbali, na vya ushujaa na bidii, ili wapate kwendelea kuwafunza mataifa wote, wafulize wasichoke ; ikawa ndiyo sababu ya kurutoa sisi nasi katika giza, kututia mwangani ; kututoa katika upotevu, kututia katika kuijua njia ; maana, aliye mwanga wako na njia yako ni yeye Mwanayo Yesu Kristo : Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Idi ya Utatu ; hiyo tu

AMBAYE u Mungu mmoja, Bwana mmoja ; si Akwamba u Nafsi moja iliyo pweke, ila u nafsi tatu nawe uli katika Tabia ya Asili moja. Kwani hayo tuliyoshika kuyaainini katika habari ya Utukufu wake Baba, ndiyo tuyaaミニyo katika Mwana naye, na katika Roho Mtakatifu, hatuyatilii tofauti wala upungufu : Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

¶ *Dibaji hizi nyingine zisuatanazo hutumika kwa siku kadharakadha qionia vyema yule Kasisi.*

Kwa Idi ya Mafunuo, na siku saba ziandamazo baadaye

KWA Yesu Kristo, Bwana wetu : aliyefunua Utukufu wake katika hali ya mwili wetu upatwao na mauti : apate kuwatoa watu wote katika giza na kuwaleta katika nuru yake ya ajabu. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Alhamisi iliyo kabla ya Ufufuo

KWA Yesu Kristo, Bwana wetu, aliywapenda kwa walio wake ulimwenguni, aliwapenda hata mwisho : naye usiku wa kuamkia kuteswa kwake, alipoketi kula chakula pamoja na wanafunzi wake, aliweka siri hizi takatifu : ili sisi tuliokombolewa kwa kufa kwake na kuhuishwa kwa kufufuka kwake, tuwe

washirika wa tabia ya Uungu iliyo yake. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Siku za Kutakata kwake na Kupewa habari kwake mtakatifu Mariamu mwanamwali

KWA kuwa ulitupa Yesu Kristo Mwanayo wa pekee azaliwe kwa ajili ya wokofu wetu : naye alifanya binadamu kweli katika mwili wa mwana-mwali Mariamu mamaye, pasipo mawa ya dhambi, atusafishe katika dhambi zote. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Siku ya Kugeuka Sura

KWA kuwa utukufu wako uliokuwa katika Neno lililofanyizwa mwili ulimulika katika mlima mtakatifu mbele ya mashahidi wa ukuu wake : na sauti yako mwenyewe kutoka mbinguni ilimtaja Mwanayo mpendwa. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Kwa Siku ya Watakatifu wote, na Siku za mitume, na Siku za wahubiri wa Injili, na Siku ya Kuza-liwa kwake mtakatifu Yohana mbatizaji, isipo-kuwa imeagizwa dibaji ya Siku nyingine

ULIYETUPA katika haki ya watakatifu wako mfano wa maisha mema, na katika hali yao ili-yobarikiwa umetupa ahadi yenye utukufu ya tumaini la mwito wetu : ili sisi kwa kuwa tumezingirwa na wingu kubwa la mashahidi jinsi hii, tupige mbio kwa uvumilivu kwa yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu ; nasi pamoja nao tupokee taji ya utukufu, isiyonyauka. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, *w.k.*

Dibaji iwezayo kutumiwa katika siku ya kurweka wakf msikitii

NAWE, ijapokuwa mbingu za mbingu hazi-kutoshi, na utukufu wako u katika ulimwengu wote : wakubali kumtakasa mwahali muwe mwa

ibada yako, namo wawamiminia waaminifu wako vipawa vya neema. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, w.k.

Dibaji iwezayo kutumiwa Jumapili yoyote katika mwaka isiyo na dibaji yake

KWA Yesu Kristo, Bwana wetu; kwa kuwa yeye Kndiye Kuhani mkuu wa kweli, aliyetuosa dhambi zetu kwa damu yake, na kutufanya kuwa ufalme na makuhani kwako wewe, Mungu wetu, Babaetu. Kwa ajili ya hayo, sisi nasi, w.k.

¶ Na ikiisha dibaji hiyo, mara huimbwa au husomwa maneno yale,

KWA ajili ya hayo, sisi nasi pamoja na malaika na K malaika wakuu, na jeshi lote la mbinguni, tu katika kulisifu na kulikuza jina lako tukufu; huku tukikutukuza milele, twanena, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Yehova Mungu wa majeshi, mbingu na nchi zimejaa utukufu wako; utukufu uwe kwako, ewe Mwenyezi Mungu uliyee juu. Amina.

¶ Ndipo hapo yule Kasisi hupiga magoti penye Meza ya Bwana, na husema kwa jina la wote hao watakaoshirikiana Ushirika Mtakatifu maneno ya sala hii :

HATUSUBUTU kuijilia Meza yako, ewe Bwana Mwenye rehema, kwa kutumai haki yetu wenye, ila kwa kutumai rehema zako zilizozidi sana kwa wingi na ukuu. Hatustahili hata kuyazoa makombo yaliyo chini ya Meza yako. Lakini wewe ndiwe yeyle Bwana, nayo ndiyo sifa yako kuwa na rehema daima: basi utupe, ewe Bwana mwenye neema, jinsi tutakavyokula nyama ya Mwili wake Mwanayo Mpenzi wako Yesu Kristo, na kuinywa Damu yake, hata miili yetu iliyo na dhambi ipate kusafisha kwa Mwili wake, na roho zetu kuoshwa kwa Damu yake iliyo ya thamani sana, tupate kukaa hivi sasa na mbeleni ndani yake yeye, naye akae ndani yetu. Amina.

¶ Hata yule Kasisi akiisha kuvitengeza Mkate na Divai, halilimesimama mbele ya Meza takatifu, kwa jinsi atakavyozidi kuwa na wepesi na makini katika kuuvunja Mkate mbele ya wale watu, na kukitwaa Kikombe kukiishika mikononi mwake, huisoma Sala hii, ya kuviweka kwa Mungu :

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, ni kwa huruma za wema wako wewe ulivyonotupa Mwanayo wa pekee Yesu Kristo hata akafa juu ya Msalaba kuwa ni ukombozi wetu; ndipo hapo naye kwa kuyatoa matoleo mamoja nayo ni nafsi yake iliyotolewa mara moja tu, akafanya dhabihu na matoleo na kafara, vilivyokamiliika na kutimia na kutosha, kwa ajili ya makosa ya ulimwengu wote: naye akaweka, akatuusia sisi katika Injili yake takatifu kudumisha ukumbusho wa hayo mauti yake ya thamani, hata aje tena. Utusikize sisi tulio miguuni pako, ewe Baba mwenye huruma; nawe utukirimu ya kwamba, tuingapo kuvipokea hivi ulivyoviumba, navyo ni Mkate huu na Divai hii, kama vile alivyoviweka Mwanayo Mwokozi wetu Yesu Kristo, kwa kukumbuka kuteswa kwake na kufa kwake; tuwe wenye kushirikiana Mwili wake na Damu yake vilivyo barikiwa sana; ambaye kwa usiku huo wa kusalitiwa kwake, *alitwaa Mkate; hata alipokwisha kushukuru ḥakauunja, akawapa wanafunzi wake, akawaambia, Twaeni mle, ḥni Mwili wangu huu utolewao kwa ajili yenu: fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi. Ni kama vile na baada ya chakula ḥakakitwaa Kikombe; hata alipokwisha kushukuru, akawapa yuanna, Katika hiki nyweni nyote: ||kwani ni Damu yangu hii ya

* Hapo yule Kasisi hutwaa sahani na kukiishika mikononi mwake.

† Hapo huuvunja Mkate.

‡ Hapo huweka mkono Mkate huo wote.

§ Hapo hutwaa na kile kikombe na kukiishika mikononi mwake.

|| Hapo hukiweka mkono kila chombo (ama kikombe ama dunu), kilicho na Divai yoyote itakayorwekwa kwa mambo ya ibada.

Agano Jipy, imwagwayo kwa ajili yenu ninyi na kwa watu wengi, kwa msamaha wa madhambi; fanyeni hivi, kila mnywapo, kwa kunikumbuka mimi. Amina.

Ndipo hapo yule Kasisi kwanza huutwaa Ushirika yeye mwe-nyewe namna zote mbili, akiisha huendelea kuwapa mabishopu nao, na makasisi, na mashemasi, kwa namna iyo hiyo, kila wakiwapo watu hao, na baadaye huwapa hao watu kwa taratibu ambayo ni njema, akiwatilia mikononi mwao hali wamepiga magoti kwa unyenyekevu. Na kila akimpa mtu ule Mkate, Padre husema,

MWILI wa Bwana wetu Yesu Kristo, uliotolewa kwa Majili yako, na ukuweke salama mwili wako na roho yako hata uzima wa milele. Huu twaa uule, kwa kukumbuka alivyokufa Kristo kwa ajili yako ; nawe lisha moyo wako kwake, uamini ukishukuru.

Na Padre awapaye watu kile Kikombe husema,

DAMU ya Bwana wetu Yesu Kristo, iliyomwagwa kwa Ajili yako, na ikuweke salama mwili wako na roho yako hata uzima wa milele. Nywaa hii kwa kukumbuka Damu yake Kristo iliyomwagwa kwa ajili yako, uwe na shukrani.

Na utakapokwisha Mkate au Divai katika vilivywewka kwa Mungu kabla wale waliopo hawajashirikiana wote, yule Kasisi huweka kwa Mungu Mkate zaidi na Divai zaidi kwa kufuata kawaada iliyoadikwa juu katika hayo : tukiwa uliokwisha ni ule Mkate huanza katika : Mwokozi wetu Kristo kwa usiku huu wa kusalitiwa kwake, w.k. : ama ikiwa ni Divai huanza kwa : Ni kama vile na baada ya chakula w.k. : kwa kuvibarikisha vitu hivyo.

Wakiisha kushirikiana pia wote, hurudi yule Kasisi hata pale penye Meza ya Bwana, na kuviveka juu yake kwa unyenyekevu vile vilivyosalia katika zile asili za vitu zilizowekwa kwa Mungu, na kuvifinika kwa kitambaa chema cha katani.

Kisha ndipo hapo yule Kasisi huisoqa Sala ya Bwana, wale watu nao wakinena nyuma yake.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalte wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha, Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao, Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. Kwa kuwa ufalme, na nguvu, na utukufu, ni vyako milele. Amina.

Kisha baadaye husoma haya :

EWE Bwana, nawe ndiwe Babaetu wa mbinguni, sisi watumishi wako wanyenyekemu twatamani sana kwa wema wako wa Ubaba, uturehemu, nawe uipokee hii sadaka yetu ya sifa na shukrani ; twakuomba hivi tulivyo miguuni pako utukirimu kwa ajili ya kustahili kwake na mauti yake Mwanayo Yesu Kristo, na kwa tulivyo na imani kwa Damu yake, sisi na kanisa lako lote tupate msamaha wa madhambi yetu, na manufaa mengine yote ya Kuteswa kwake. Nasi hapa twatoa nafsi zetu, twajisongeza wenyewe mbele zako, ewe Bwana, miili yetu pamoja na roho zetu, tupate kuwa sadaka iliyo na maana na utakatifu na uhai kwako wewe ; nasi twakunyenyekea sana huku tukitaka kwako ya kwamba sisi sote tulioshirikiana Ushirika Mtakatifu huu tujawe na neema yako na baraka yako ya mbinguni. Basi na tungawa hatufai, kwa ajili ya madhambi yetu namna namna, kukutolea sadaka iwayo yote, lakini hii sadaka yetu ya sasa twakuomba uipokee ; maana, ndilo lililqtupasa neno hilo, ndio utumishi wetu tulioagizwa ; nawe usihesabu kustahili kwetu, ila utusamehe kila ukengefu wetu, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu ; ambaye wewe, pamoja naye, katika umoja wa Roho Mtakatifu, u katika kuheshimiwa na kutukuzwa milele kwake yeye, kwa utukufu wote na heshima yote, ewe Baba Mweza-wa-yote. Amina.

Au hii.

EWE Mwenyezi Mungu uishiye milele, twakushukuru kwa miyo yetu yote, kwa hivyo ulivytuneemesha sisi tuliojua kupokea siri hizi takatifu kama ipasavyo, hata ukatalisha chakula cha roho cha Mwili na Damu yake Mwanayo Mwokozi wetu Yesu Kristo vilivyo na thamani mno ; ukatuthubutishia sisi kwa ajili ya hayo neema yako na wema wako ; na kuwa tu viungo vya mwili wake halisi yeye Mwanayo, maana Mwili wake wa sirini, nacho ndicho kikao kilichobarikiwa cha wenye imani wote ; tena ya kuwa tu warithi sisi wa ufalme wako wa milele, kwa njia ya kurumaini, kwa kustahili kwa kuteswa kwake na

mauti yenyé thamani ya Mwanayo Mpenzi wako. Basi twakuomba sana, ewe Baba wa mbinguni, hapa miguuni pako tulipo, utusaidie kwa neema yako, tupate kwendelea katika umoja huo mtakatifu, tutimizie na kazi njema zote, kadiri ya ulizotutengeza tangu hapo, za kwendelea mbele ndani yake ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu, ambaye milele, pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, yuna heshima na utukufu uliotimia. *Amina.*

Hapo husomwa au huimbwa,

UTUKUFU una Mwenyezi Mungu aliye juu, duniani nako ni salama, na kwa binadamu ni ihisanî.

Twakusifû wewe, Twakuhimidi wewe, Twakuabudu wewe, Twakutukuza wewe, Twakushukuru wewe kwa ajili ya huo utukufu wako, Ewe Bwana Mwenyezi Mungu, Mfalme wa mbinguni, Mungu Baba Mweza-wa-yote.

Ewe Bwana, Yesu Kristo Mwana mzaliwa pekeo ; Bwana Mwenyezi Mungu, Mwana-wa-kondoo wa Mungu, Mwana wa Baba, Wewe uondoaye makosa ya ulimwengu, Utirehemu sisi. Wewe uondoaye makosa ya ulimwengu, Utirehemu sisi. Wewe uondoaye makosa ya ulimwengu, Upokee hii sala yetu. Wewe uliyekaa upande wa mkonon wa kuume wa Mwenyezi Mungu Baba, Utirehemu sisi.

Kwani ni wewe pekeo uliye mtakatifu ; Ni wewe pekeo uliye Bwana ; Ni wewe pekeo Kristo, pamoja na Roho Mtakatifu, uliyetukuka sana katika utukufu wa Mungu Baba. *Amina.*

¶ *Hapo yule Kasisi, ama yule Bishopu akiwa yupo, huwafumua wale watu kwa Baraka hii.*

AMANI ya Mungu, ipitayo fahamu zilizo zote, na Aiwalinde mioyo yenu na nia zenu katika kumjua na kumpenda Mungu, na Bwana wetu, Yesu Kristo Mwanawе. Na baraka ya Mungu Mweza-wa-yote, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, iwe mwenu ikae kwenu daimia. *Amina.*

¶ *Sala hizi zifuatazo husomwa baada ya kule kukusanya sadaka, kwa kila siku isiyokuwa na Ushirika huo, hutumiwa moja tu au zaidi ; nazo hizo husomwa baada ya Sala za Sala ya Asubuhi au ya Jioni, kila pakiwa na haja, au baada ya Sala za Ushirika Mtakatifu au za Litania, kila atakapoona yasaya yule Kasisi.*

EWE Bwana, uturehemu, utusaidie humu katika E kunyenyeka kwetu na kusali kwetu, nawe uilekeze njia yetu sisi watumishi wako, tupate kufikilia katika wokofu wa milele ; ili kwamba na ungawa huu ulimwengu tuliomo ndani yake wazungukia wenyeve na kuwapiga mnno, lakini iwe sisi watu wako kulindwa humo daima, kwa msaada wa neema yako ufikiliao kwa upesi ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Bwana Mweza, Mungu usiye mwanzo wala mwisho, twakuomba utunemeshe mioyo yetu pamoja na miili yetu, vipate kuongozwa hivyo na kutakaswa na kutawaliwa na wewe katika njia za sheria zako na vitendo vya mausio yako, ili kwa vile wewe utakavyotulinda duniani na milele, tuhifadhike miili yetu na roho zetu : kwa Bwana wetu, Mwokozi Yesu Kristo. *Amina.*

UTUTAKABALIE, twakuomba, ewe Mungu Mweza-wa-yote, ya kwamba maneno haya tuliyoyasikia leo kwa masikio yetu ya nje, yashikamanishwe sana kwa neema yako katika mioyo yetu ndani, hata yaza ndani yetu matunda ya maisha safi, kwa kuliletea jina lako heshima na utukufu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

UTUONGOZE, ewe Bwana, Katika vitendo vyetu vyote kwa fadhili ya neema yako, utupeleke mbele mumo kwa msaada wako daima ; ili kwa kazi zetu kuanzilizwa na kufulizwa na kutimilizwa ndani yako wewe, tulitukuze jina lako takatifu, na mwishowe tuyapate kwa rehema yako maisha ya milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, Mwanzo wa hekima zote ni wewe, huu uhitaji wetu wewe waufahamu mbele hatuaingia kukuomba, na ujinga wa kukuomba kwetu pia waujua ; twakuomba uurehemu udhaifu wetu, nawe hayo tusiyosubutu kuyaomba kwako kwa kuwa hatustahili pamoja na tusiyyajua kuyaomba kwa ajili ya utofu wetu

wa macho, pia uwe radhi kutupa ; kwa kustahili kwake Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Mungu Mweza-wa-yote, wewe umetupa ahadi ya Ekusikiza haja zao wote wakuombao kwa jina la Mwanayo ; twakuomba uyatege kwetu masikio yako, uturehemu sisi tuliojua kukusongezea hivi sasa sala zetu na haja zetu ; utupe ya kwamba tuyapate pasipo shaka hayo tuliyoyataka kwako kwa uaminifu kama mapenzi yako, ili hali ya uhitaji wetu isaidiwe, na utukufu wako utangae ; kwa ajili ya Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ Kwa kila siku ya Jumapili au ya Idi iwayo yote, usiposongezwa ule Ushirika, husomwa yote hayo yaliyoagizwa kusomwa kwa zamani za Ushirika, hata iishe Sala ya Kuwaombea Waru Wote (Na tuijombee hali yake Kanisa la Kristo lililo katika vita hapa duniani), pamoja na Sala hizi za sasa zinazotangulizwa moja tu au zaidi : na mwisho atie ile Baraka.

¶ Wala haisongezwi Karamu ya Bwana ila hapo wapatikanapo watu ambaa watosha hesabu yao kushirikiana katika Ushirika pamoja na yule Kasisi, kama mwenyewe aonavyo.

¶ Na watu wanganya hawakuzidi ishirini hesabu yao katika mipaka ya msikiti, ambaa wafaa kushirikiana Ushirika, na haya yote usifanyike Ushirika, ila wapatikanapo wanne, au uchache ni watatu wasipungue, watakaoshirikiana Ushirika huo pamoja na yule Kasisi.

¶ Na katika misikiti mikuu iliyo na viti vya Ubishopu, na misikiti ya jamaa : namo ni mtawahali mwenye makasisi wengi na mashe-masi wengi : hupokea Ushirika pia wote kila Jumapili wasipungue, pamoja na yule Kasisi, ila washikwapo na udhuru wa kuwaachisha.

¶ Na kwa kuepua kila huja iwezayo kuleta mashindano au ibada isiyopasa, kwa mtu awaye yote, katika habari ya ule Mkate au ya ile Divai, hutoshya kwa huja yake ukiwa Mkate namma yake ni kama huo uliwa siku zote : lakini na uwe katika wema wa mikate ya nganu, utakaopatikana kwa wepesi.

¶ Na kikisalia chochote katika Mkate na Divai, nacho hakiku-wekwa kwa Mungu, yule Padre hukichukua na kukitumia yeze : lakini kitakaposalia chochote katika hicho kilichowekwa kwa Mungu, na kisichukudiwe hata nye ya msikiti, ila mara baada ya kusema Baraka, yule Kasisi na wengine katika wale walioshirikiana Ushirika, ambaa kwamba atawaita waje

kwake, watakuwa wao kula na kunywa kwa ustahivu vile vilivyoasilia.

¶ Mkate na Divai vya Ushirika hulazimishwa Padre na Walinzi wa msikiti, kwa gharama za watu wa mipaka ya msikiti.

¶ Kisha tunza ! kila mtu wa humo mipakan, huangia Ushirika Mtakatifu mwaka kwa mara tatu asipungue na katika Ushirika huo mara tatu hizo, ya Idi ya Ufufuo asikosekane. Na mwaka hata mwaka katika zamani za Idi ya Ufufuo, kila mmoja wale waketrio humfanyia hesabu Padre, au mtu mmoja (au zaidi) awaye yote, aliye badala yake yule (au badala yao wale) : amlipe yule (au awalipe wale) maada yote ya kanisanii, ambayo hulipwa majira hayo na zamani hizo.

¶ Baada ya kwisha Ibada ya Mwenyezi Mungu, ile fedha iliyo-tolewa kupewa Mwenyezi Mungu hapo katika kukusanya sadaka, huitumia yule Padre na wale Walinzi kwa gharama za haja za uchajii-wa-Mungu na kuwefaa maskini, kama wata-kavyoona vyema wao wenyeewe : ila wakiwa hawapatanii wao kwa wao, katika jambo hili, na itumiwe kama atakavyoagiza Mwenye Amri kuu.

KWA ajili ya vile ilivyoamriwa katika kawaida hii ya kuisongeza Ibada ya Karamu ya Bwana, ya kila mwenye kuwamo katika Ushirika huo kuupokea kwa kupiga magoti yake (nayo ni amri iliyo na maana mazuri, kwa kuwa yaonyesha jinsi tulivyoayakiri sisi, kwa unyenyekevu na asante nyingi, yale manufaa yake Kristo wapewayo humo wote washirikianao kama ilivyopasa, na kwa ajili ya kujitenga na mambo ya maasia na fujo katika kushirikiana kwetu Ushirika, ambayo yamkini kuingia kwamba si amri kama hii); lakini pamoja na haya, asije mtu akavidhania mengine, akavitusha hivyo tupigavyo magoti sisi, ama ni mtu aliye mjinga au mnyonge, ama ni fitina au pingamizi ; basi, na ijulikane ya kuwa katika neno hili la kupiga magoti, hamna ibada, wala haifai kuwamo ibada, iwayo yote, ya Mkate wake ile Sakramenti au Divai yake, vipokewavyo humo kwa kitu chake hivyo : wala ibada ya Mwili na Damu vyake Kristo vya asili, vitaka-vyodhaniwa na mtu kupatikana humo kwa jinsi ya mwili. Kwani ule Mkate na ile Divai vya Sakramenti hiyo, vikali vinakaa mumo kila kimoja kina tabia yake ya asili, hiyo tu : basi hivyo imekuwa ibada yake haijuzu (kwani ingekuwa ni kuabudu sanamu, nayo ni machukizo kwa

Wakristo wote walio waaminifu) : nasi twavijua Mwili wake na Damu yake Mwokozi wetu Kristo zi mbinguni, havipo tena hapa chini : kwani imepingamana na kweli ya hali yake Mwili wake Kristo wa asili, utakapoambiwa ni wa kupatikana, wakati huo mmoja, katika mwahali mwangi.

TARATIBU YA KUWABATIZA WATOTO MBELE YA WATU, ambayo hutumiwa msikitini.

¶ Watu na waonywe kwamba, ni la kufaa zaidi Ubatizo kutousengeza isipokuwa kwa siku za Jumapili au Idi nyingine, maana, waabuduo huzidi kukutanika kuwa tele kwa siku hizo ; nalo neno hili liliqizwa, huku ili kwamba mkuiano upate kuewashuhudia wabatizwa hapo wapokewapo katika jumla ya Kanisa la Kristo ; huku kwamba katika kubatizwa kwao wale watoto jamii ya watu wazima walioapo wapata kukumbushua walivyoahidi wenye kwa Mwenyezi Mungu kila mmoja katika kubatizwa kwake. Kwa ajili ya hayo yafaa Ubatizo kusongeza kwa kutumia lugha hiyo itumikayo sana katika nchi. Pamoja na haya (kwa wakati wa kufaa), hubatizwa watoto kwa siku nyiningine iwayo yote.

¶ Nawe angalia, kila mtoto atakayebatizwa, wa kiume huwa na madhamini watatu, wavili wame, mmoja mke ; na mitoto wa kike, huwa na madhamini watatu, wavili wake, mmoja mume.

¶ Na wakipatikana watoto watakao kubatizwa, wazazi wao humpa habari yule Padre kabla ya usiku wa kuamka siku yake, au asubuhi yake, mbele ya Sala ya Asubuhi. Ndipo hapo wale madhamini na wenye nao watoto huenda na kukaa karibu ya fonti, ili kuwapo tayari ; kwamba ni Sala ya Asubuhi, baada ya kusoma Somo la pili ; kwamba ni Sala ya Jioni, baada ya kusoma Somo la pili ; kama atakavyoona vyema yule Padre kuyaamrisha. Na yule Padre huenda perye fonti (nayo hujazwa maji safi wakati huo), akiisha kusimama husema :

J E, watoto hawa wamebatizwa tangu hapo, hawa-jabatizwa ?

¶ Wakisema, La, hawajabatizwa, ndipo hapo yule Padre hue-ndelea kunena :

E NYI mpendwao sana, kwa ajili ya vile watu wote walivyochukuliwa mimba na kuzaliwa katika dhambi, na kwa kuwa Mwokozi wetu Kristo alinena, Hakuna mtu awezaye kuingia katika ufalme wa Mungu ila aliyezaliwa mara ya pili, aliyezaliwa uzazi mpya kwa maji na Roho Mtakatifu : mimi nawataka sana ninyi mmilingane Mungu

Baba kwa Bwana wetu Yesu Kristo, apate kuwapa watoto *hawa* kwa rehema zake zisizo mpaka neno moja ambalo kwa asili *yao hawawezi* kuwa nalo : nalo ni la *wao* kubatizwa kwa maji na Roho Mtakatifu, na kukaribishwa katika Kanisa lake Kristo lililo takatifu, na kufanya kuwa *viliyo* hai rya mumo Kanisani.

¶ *Ndipo hapo Padre hunena,*

Na tuombe.

EWE Mungu Mweza-wa-yote huna mwanzo huna mwisho : wewe kwa rehema zako kuu ulimwokoa Nuhu uliwaokoa na wa nyumbani mwake kwa ile safina, ukawaponya wao na kule kuangamia majini ; nawe uliwaongoza salama watu wako wana wa Isiraeli katikati ya Bahari Nyekundu, kwa kuonya humo mfano wa ubatizo wako mtakatifu : kisha kwa kubatizwa kwake Mwanayo Mpenzi wako sana Yesu Kristo, katika mto wa Yorodani, uliyatakasa maji kwa kuosha dhambi kwa maana ya ndani : sisi tuliope twakuomba kwa ajili ya rehema zako zisizo mpaka, uwaangalie watoto *hawa* kwa rehema, uwaoshe na kuwatakasa kwa Roho Mtakatifu : ili kwamba pamoja na kuokoka *kwao* na ghadhabu zako wakaribishwe na safinani mwa Kanisa lake Kristo ; kisha, kwa vile watakavyokaa katika imani, na kuwa hali ya furaha kwa kutumaini, na kukazwa shina *lao* katika kupendana, huku kuyavuka *kwao* mawimbi ya ulimwengu huu wa dhiki na taabu, wafikilie mwisho katika nchi ya maisha yaendeleayo milele, wapate kutawala pamoja na wewe katika nchi hiyo milele na milele : kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, mambo yote wayaweza wewe, wala hushindwi na kifo ; Msaada wao wote walio na uhitaji, Auni yao jamii ya wakukimbilia, Maisha yao waaminio, Kufufuliwani *kwao* waliokufa, pia hayo ni wewe : sisi twakulingana, twawaombea watoto *hawa*, ili hivi *wajavyo* katika ubatizo *wako* mtakatifu, walipate ondoleo la madhambi *yao* kwa uzazi mpya wa rohoni. Uwapokee, ewe Bwana, kama ulivyoahidi kwa Mwanayo Mpenzi wako sana, pale aliponena, Ombeni mtapewa :

tafuteni mtaona : bisheni mtafunguliwa. Na sasa na iwe vivyo : utupe tukuombao : tutafutao na tuone : utufungulie mlango sisi tubishao : ili kwamba watoto *hawa* wafurahie baraka iendeleayo milele ya joshio lako la mbinguni, na kupata kuufikilia ufalme wa milele uliotuahidi kwa Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo husimama wale watu, Padre hunena,*

Yasikizeni maneno ya Injili iliyoandikwa na mtakatifu Mariko, Mlango wa kumi, Kifungu cha kumi na tatu.

IKAWA watu kumpelekea watoto apate kuwagusa ; wale wanafunzi wakiwakemea waliowaleta. Yesu akiona yale yakamchukiza, akawaambia, Waacheni watoto wanjilie, msiwikanyeni : kwani ufalme wa Mwenyezi Mungu ni wa kama hawa. Ni kweli nawaambia, asiyepokea ufalme wa Mwenyezi Mungu kama vile mtoto, haingii ndani yake kamwe, awaye yote. Kisha akawachukua mikononi mwake, ikawa kuwabarikia, huku akiwawekea mikono.

¶ *Baada ya kwisha kusomwa Injili hii, yule Padre huonya maonyo hayo kwa kufupiza, katika maneno ya hiyo Injili.*

ENYI wapenzi, katika Injili hii mmeyasikia maneno ya Mwokozi wetu Kristo ; alivyoamuru kuletewa kwake watoto, na alivyowalaumu wale walioataka kuwatenga naye ; na awatakavyo watu wote wafuate mambo yao yasiyokuwa na uovu. Mmeona jinsi aliyoweka wazi kwa ishara zake na vitendo vyake vya nje kuwa yu radhi moyo wake na watoto wale, kwani aliwachukua mikononi mwake, aka-wawekea mikono na kuwabarikia. Basi, msitie shaka, aminini tu ndani ya miyo yenu, ya kuwa atawawelea radhi watoto *hawa* nao kuwakaribisha kwake ; tena atawachukua kwa mikono ya rehema zake ; atawapa na baraka ya maisha ya milele, na kuwafanya *wawe washirika* wa ufalmé wake usio mwisho. Kwa ajili ya hayo, sisi ambaeo tu watu tuliopewa hakika hivi ya kuwapenda kwake watoto *hawa* Babaetu wa mbinguni kama ilivyowekwa wazi na Yesu Kristo Mwanawe, nasi hatuna shaka ya

kuikubali kwake hii kazi yetu ya mapenzi, katika kuwaleta watoto *hawa* hata katika ubatizo wake mtakatifu ; na tumshukuru kwa imani na ibada ya kweli, tuseme,

EWE Mungu Mweza-wa-yote, huna mwanzo huna mwisho ; nave ndiwe Babaetu wa mbinguni ; sisi tu miguuni pako, twakuambia asante kwa ulivyonukirimu ya kutuita hata tukapata kuijua neema yako, na kuamini kwako : utuongeze ujuzi huo, uikaze miyoni mwetu imani hiyo milele. *Watoto hawa uwape Roho wako Mtakatifu*, wapate kuzawa uzazi ulio mpya, na kufanywa kuwa *watu* wa kuurithi wokofu usio mwisho : kwa ajili yake yeyle Bwana wetu, Yesu Kristo, aishiye na kutawala pamoja nave na Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre husema na wale madhamini maneno haya :*

ENYI niwapendao sana, *watoto hawa* mmewaleta hapa, *ewapate* kubatizwa, mmeomba ya kwamba Bwana wetu Yesu Kristo awe radhi *kuwapokea awaondolee dhambi zao*, awatakase kwa Roho Mtakatifu, awape na usalme wa mbingu, na uzima wa milele. Nanyi mmesikia jinsi alivyoahidi Bwana wetu Yesu Kristo, humo katika Injili yake, kwamba atatupa mambo hayo yote mliyoomba : naye ahadi hiyo hakosi yeye kwa upande wake, ataishika na kuitimiza. Basi kwa ajili ya hayo, baada ya ahadi aliyoahidi Kristo, inawapasa *watoto hawa nao* kwa upande *wao*, kuahidi kwa ndimi zenu madhamini, ya kwamba, *wakiisha kufikilia umri* wa kujitweka zenyewe ahadi hii, *watoto hawa* *watamkata* Shetani na kazi zake zote, na kuli amini daima Neno lake Mwenyezi Mungu lililo takatifu, na kuyashika maagizo yake kwa kutii.

Basi kwa ajili ya hayo nakuuliza :

JE, wewe kwa jina lake mtoto huyu, wamkataa Shetani na kazi zake zote, na furaha na utukufu visivyofaa vya ulimwengu huu, na kule kuyatamani-tamani mambo hayo

yote kwa shauku ; pamoja na tamaa za mwilini, hata uwe wewe kukataa kuvifua na kuchukuliwa navyo ?

Hujibu. Navikataa vyote.

Padre

JE, wewe waamini kwa Mungu Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi ?

Na kwa Yesu Kristo, Mwanawe mzaliwa pekee, Bwana wetu ? Na ya kuwa alitungishwa mimba na Roho Mtakatifu, akazaliwa na Mwanamwali Mariamu ; tena kuwa aliteswa katika enzi ya Pontio Pilato ; akasalibiwa, akafa, akazikwa ; akashuka na kuingia kuzimu, hata siku ya tatu akasimama tena, ametoka kwa wafu ; kisha akapaa na kuingia mbinguni ; tena ameketi upande wa mkonono wa kuume wa Mwenyezi Mungu Baba ; ndiko atakakotoka kuja tena, katika mwisho wa ulimwengu, kuwaamua walio hai hata waliokufa ?

Nawe waamini kwa Roho Mtakatifu ; Kanisa takatifu lililo ulimwenguni mote ; Ushirika wa watakatifu ; Madhabbi kusamehewa ; Mwili kufufuka ; na Maisha ya milele baada ya mauti ?

Hujibu. Haya yote ninayakubali sana kuyaamini.

Padre

JE, wataka ubatizwe katika imani hii ?
Hujibu. Nataka.

Padre

BASI, wataka kuyafuata mapenzi matakatifu ya Mwenyezi Mungu kwa kuyati, na kuyashika maagizo yake ; uyaandame hayo tu siku zote utakazokuwa hai ?
Hujibu. Nataka.

¶ *Ndipo hapo Padre hunena,*

EWE Mwenyezi Mungu mwenye rehema, *watoto hawa* *uwajalie* ya kwamba kwa vile atakavyozikwa Adamu wa kale aliye ndani *yao*, *wapewe* mtu mpya kufufuka ndani *yao*. *Amina.*

Uwajalie shauku zote za mwili zife ndani *yao* ; na

mambo yote yatakwayo na Roho yaye hai, yaongezeke daima ndani yao. *Amina.*

Uwajalie kuwa na uwezo na nguvu, wapate kushinda kwa furaha Shetani na ulimwengu na mwili. Amina.

Umjalie kila mmoja atakayewekwa nafsi yake kwako wewe pahali hapa kwa utumishi wetu sisi na usongezi wetu sisi, kuvikwa neema za mbinguni na kupewa thawabu ya milele, kwa rehemza zako, ewe Bwana Mungu utukuzwaye, uishiye hali umetawala mambo yote, milele. *Amina.*

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, wewe uli hai milele ; Ehuyo Mwanayo Mpenzi wako sana sana Yesu Kristo, kwa kutusamehe madhambi yetu, alitokwa na damu na maji sambamba katika ubavu wake ulio wa thamani sana, akawapa na amri wanafunzi wake, ya kwenda kuwafanya wanafunzi mataifa wote, na kuwabatiza, kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu ; twakuomba utege masikio yako kwetu mukutano wako ; nawe uyatakase maji haya yaye njia ya kuosha dhambi kwa maana ya ndani ; uwajalie watoto *hawa waendao* kubatizwa humo hivi sasa, wawe wenye kupokea neema yako iliyotimia, na kukaa daima mionganini mwa wanayo waaminifu wateule wako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre huwachukua wale watoto mmoja mmoja mikononi mwake, akiwaambia wale madhamini,*

Penzi jina mtoto huyu

¶ *Naye Padre humtaja jina lake kwa kufuata lile wamwambialo, kisha (wakiwa wanampa hakika ya kuwa atayaveza bila shaka), humtia mle ndani ya maji kwa humwangalia asije akapatikana na madhara, akinena,*

FULANI, mimi nakubatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. *Amina.*

¶ *Lakini watakapompa hakika ya kuwa hana nguvu sawasawa yule mtoto, hutoshia kumwagia yale maji, huku yuanena kama yaliyotangulia,*

FULANI, mimi nakubatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo hunena yule Padre,*

SISI twampokea mtoto huyu katika mukutano wa kundi Slake Kristo,* nasi twamtia alama ya msalaba ya kuno-nyesha kwamba baadaye hataona * *Ndipo hapo yule* haya kuikiri imani ya Kristo *Padre humpiga alama* msalibiwa, na kupigana kiime na *ya msalaba yule mtoto* dhambi na ulimwengu na Shetani, *katika japa la uso.* chini ya beramu yake ; na kwendelea kuwa askari mwa-minifu na utumishi wa Kristo, hata maisha yake ya duniani yaishe. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo Padre hunena,*

HIVI, enyi ndugu zangu mpendwao sana, tuwaonavyo watoto *hawa* kuwa *wamezaliwa uzazi* mpya, na kutuliwa katika mwili wa Kanisa la Kristo, na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo hayo mema : nasi tumwombe kwa umoja wa hali, *watoto hawa wayapishe* maisha yao yanayosalia duniani kwa mfano wa mwanzo huu.

¶ *Ndipo hapo hupiga magoti pia wote na kusema,*

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwaa, Utuokoe maovuni. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo hunena yule Padre,*

TWAKUSHUKURU sana, ewe Baba mwingi wa rehemza, kwa kuwa watoto *hawa* umeridhia kuwapa uzazi mpya kwa Roho wako Mtakatifu, na kuwakubali kuwa *wanao* wewe kwa ulezii wako ukawatia katika Kanisa lako lililo takatifu. Nasi hivi tulivyo miguuni pako twaomba kwako kwa unyenyekevu, kwamba watoto *hawa*, wali hali ya kufa na kutohana na dhambi, na kuwa hai kwa kuilekea haki, na kuwa ni *watu waliozikwa* pamoja na Kristo katika mauti yake : *uwape kumsalibu yule mtu wa*

kale, na kukomesha kabisa mwili wote wa dhambi pia : na ya kwamba, hivyo walivyopewa kuwa *washirika* wa kufa kwake *Mwanayo*, na *wave vivyo washirika* wa kufufuka kwake ; hata iwe mwishowe, baada ya haya, pamoja na waliobaki katika *Kanisa lako takatifu*, *wao nao wapate* kuwa *watu* wa *kuurithi* ufalme wako usiokuwa na mwisho : kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

¶ *Hapo ndipo husimama wote ; Padre huwaambia wale madhamini maonyo haya :*

KWA maana ya vile *walivyoahidi watoto hawa* kwa **N**dimi zenu ninyi madhamini *wao*, ya kumkataa Shetani na kazi zake zote, na kuamini kwa *Mwenyezi Mungu* na kumtumikia, inawapasa ninyi kukumbuka kwamba fungu lenu lililowapasa kila mmoja, ni kuangalia kwamba *watoto hawa wafunzwe* hapo *watakapokwisha* kuwa ni *watu* wa *kuelewa* nayo, jinsi zilivyo kubwa hizo nadhiri na ahadi na amana *walizozikiri* hapa kwa ndimi zenu. *Nao kwamba wapate*, kujajua zaidi mambo haya, sharti ni kuwataka *wasikize hotuba* ; na sana ni kuwatengezea ya *wao kujifunza Imani ya Mitume*, na *Sala ya Bwana*, na zile Amri Kumi, kwa lugha ya nchi *waketiyo*, na *kujifunza* mambo yote yaliyobaki ambayo yampasa mtu wa *Kikristo* kujajua na *kuyaamini*, *wapate* kuwa hali njema roho *zao* ; tena ni *kuwalea* hali ya *heshima* *wapate* *kuishi* *maisha yao* katika *kicho cha Mungu* na *dini ya Ukristo* ; huku mkikumbuka kuwa *huu ubatizo* *watuonya mfano* wa hali yetu *tuikiriyo* ; nayo ni ya kumwandama *Mwokozi* wetu *Kristo* kwa *kielelezo chake* *alichotuonya*, na *kufananishwa* hali zetu na hali *yake* ; ili kwamba, kama ye ye aliwyokufa na kufufuka kwa ajili yetu, sisi nasi tulio-batizwa tuwe *watu* wa *kufa* na *kutokana* na *dhambi*, na *kufufukia* *haki* ; huku tukiendelea katika *kuzifisha* *tamaa* zetu *mbovu* na *uharibifu* wetu, na *kuongea* kila siku katika kila lipasalo *heshima* na *uchaji-wa-Mungu* wa *maisha*.

¶ *Hapo ndipo atakapoongeza kusema haya,*

NINYI sharti ni kutunza kwamba *watoto hawa* wapelekwe kwa Bishopu *wapate* *kuwekewa* mikono na ye ye, *hapo watakapokwisha* *kujua kuisema Imani*, na

Sala ya Bwana, na zile Amri Kumi, kwa lugha ya nchi *waketiyo* ; na *kuongezewa* *mafunzo* *yaliyo* katika *Kate-kisimo* ya *kanisa* *yaliyotengezwa* *tangu* *hapo* kwa ajili ya *hayo*.

¶ *Nao Ubatizo ukiletwa wakati uso wa Sala ya Asubuhi au ya Jioni, Padre awafumue wale watu waliokutanika kwa kunena,*

BWANA na awabarikie na *kuwalinda*, Bwana na *Bawaangazie* uso wake, awape neema, Bwana na awainulie *nuru* ya uso wake, na *kuwapa* amani, sasa na hata milele. *Amina.*

¶ *Ni yakini sana, kwa Neno la Mungu, ya kuwa watoto walio-batizwa, wakifa hawajatenda dhambi za matendom, wameokoka watoto hawa havana shaka.*

¶ *Ili kuondoa kila shida na tashwishi katika itumiwavyo alama ya misalaba katika kubatiza : maftinuo ya hakika ya maana yake, na sababu zilizoiacha ikahifadhiwa mumo alama hiyo hupatikanu katika Kanuni ya Thelathini, iliyoanza kutangazwa mvaka elfu mia sita na mne.*

UBATIZO WA FARAGHA KUWASONGEZEA WATOTO WACHANGA NYUMBANI

¶ Mapadre wa kila msikitii na wawaonye wenyiji mara kwa mara ya kwamba wasikawishe ubatizo wa watoto wao baada ya Jumapili ya kwanza au ya pili iandamayo siku ya kuzalivwa kwake, au baada ya Idi nyiningine iandamayo katikati, isipoonekana sababu ambayo ni kubwa na maana, kama atakavyoionna ina haja yule Padre.

¶ Nao wawaonye ya kwamba, watakapokuwa hawana sababu kubwa au haja kubwa kama hiyo wasiwatake watoto wao kubatizwa nyumbani mwao. Lakinii .watakapopatikana na udhuru, hapo husongezwa ubatizo kwa kufuata namna hii :

¶ Kwanza, ye ye Padre wa msikitii (au asipopatikana huyu, ni Padre mwingine aliye na amri sheriani apatikanaye awaye yote) na waliopo wote na wamlingane Mwenyezi Mungu, wasome Sala ya Bwana, na katika sile sala zilizoanriwa kusomwa hapo mbele katika Kawaida ya Kuwabatiza Watoto mbele ya Watu, kadiri ya watakazopata kuzisoma, kama watakazowahi kwa majira waliyo nayo na haja iliyopo. Kisha baadaye yule mtoto hupewa jina na mmojavapo wale waliopo, Padre akamwagia maji, kwa kunena maneno haya :

FULANI, mimi nakubatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

¶ Ndipo hapo hupiga magoti jamii ya waliopo, yule Padre humshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunena :

TWAKUSHUKURU sana, ewe Baba mwinci wa rehema, kwa kuwa mtoto huyu umeridhia kumpa uzazi mpya kwa Roho wako Mtakatifu, na kumkubali kuwa mwanayo kwa ulezii wako, na kumtia katika mwili wa Kanisa lako lililo takatifu. Nasi hivi tulivyo miguniuni pako, twaomba kwako kwa unyenyekevu ya kwamba hivi aliyopewa kuwa mshirika wa kuwa kwake Mwanayo, na awe vivyo mshirika wa kufufuka kwake : hata iwe mwisho showe baada ya haya, pamoja na waliobaki katika watakatifu wako wateule, apate kuurithi ufalme wako usio mwisho ; kwa ye ye huyo Mwanayo Bwana wetu, Yesu Kristo. Amina.

¶ Nao wasitie shaka ya mtoto aliyebatizwa hivyo kuwa amebatizwa kama ifaavyo sheriani na itoshayyo katika haki, hata amekuewa hafai kubatizwa mara ya pili aliyebatizwa hivyo. Ila pamoja na haya, atakapojaliwa kuishi na kukua, mtoto aliyebatizwa kwa kufuata kawaada hii, afaa kuchukuliwa msikitini ili kwamba, akiwa ni Padre wa msikitii aliyebatiza mtoto yule, upewa hakika dhahiri uli mukutano wa kanisan yu kweli ya kawaada ya ubatizo ili yotangulia kutumiwa faragha : na mambo yawapo ni hayo husema hivi :

MIMI nawapa hakika ya mtoto huyu kuwa nilimbataiza, kama ilivyopasa na kuagizwa na kawaada ya Kanisa, majira kadhawakadha, pahali kadhawakadha, mbele ya mashahidi kadhawakadha.

¶ Lakini ikiwa mtoto yule alibatizwa na Padre mwingine afaayi sheriani awaye yote, ndipo hapo yule Padre wa msikitii wa pahali alipozaliwa na kubatizwa mtoto yule huuliza na kujaribu, apate kutambua kuwa alibatizwa kwa njia ya sheria, au hakubatizwa. Na hapo, hao wamletao mtoto awaye yote msikitini, watakapojibu kwamba mtoto amekwisha kubatizwa, basi wakati huo yule Padre na azidi kuwaauliza, anene,

MTOTO huyu alibatizwa na nani ?
Waliokuwapo ni nani na nani, wakati aliobatizwa mtoto huyu ?

Kwa ilivyowezekana mambo mengine yapasayo Sakramenti hii kukosekana, kwa sababu ya fadhaa au haraka watu waliyo nayo zamani za dhiki kama hizo, mimi kwa ajili ya hayo nawaauliza tena :

Mtoto huyu alibatizwa kwa kutumia kitu gani ?
Mtoto huyu alibatizwa kwa kutumia maneno gani ?

¶ Hata ikiwa, kwa vile wamjiburyo masiala haya wale waliomleta mtoto yule, ameyaona mambo yale yote kuwa yalitendeka kama ipasavyo, ndipo hapo ye ye hambarizi mtoto yule mara ya pili, ila humkaribisha kama aliye katika kundi la Wakristo wa kweli, kwa kunena maneno haya,

MIMI nawapa hakika ya jambo hili kuwa lilitendeka vyema loti kwa kufuata taratibu yake kama ambavyo yaafa katika kubatizwa kwake huyu mtoto : naye angawa alizaliwa hali yuna dhambi ya asili, hali yu chini ya ghadhabu zake Mwenyezi Mungu : lakinii sasa kwa joshio la kuzawa uzazi mpya katika ubatizo amekaribishwa mtoto

huyu katika mionganini mwa wana wa Mungu walio na urithi wa maisha ya milele : kwani Bwana wetu Yesu Kristo hawakatai watoto namna hii kuwarehemu na kuwaneemesha, ila kuwaita waje kwake kwa mwito wa mapenzi yake yaliyozidi sana, kama Injili takatifu ilivyoshuhudia kwa kutuza miyo yetu, kwa kutumia maneno kama haya :

Mariko 10. 13-16

IKAWA watu kumpelekea watoto apate kuwagusa ; Iwale wanafunzi wakiwakemea waliowaleta. Yesu akiona yale yakamchukiza, akawaambia, Waacheni watoto wanijilie, msiwakanyeni : kwani usfalme wa Mwenyezi Mungu ni wa kama hawa. Ni kweli nawaambia asiyepokea usfalme wa Mwenyezi Mungu kama vile mtoto, hainingi ndani yake kamwe, awaye yote. Kisha akawachukua mikononi mwake, ikawa kujabari, huku akiwawekea mikono.

¶ Baada ya kuishi kusomwa Injili, yule Padre huonya maonyo haya, kwa kufupiza, katika maneno ya hiyo Injili. :

ENYI wapenzi, katika Injili hii mmeyasikia maneno ya Mwokozi wetu Kristo ; alivyoamuru kuletewa kwake watoto na alivyowalaumu wale waliotaka kuwatenga naye ; na awatakavyo watu wote kufuata mambo yao yasiyokuwa na uovu. Mmeona jinsi alivyoweka wazi kwa ishara zake na vitendo vyake nya nje kuwa yu radhi moyo wake na watoto wale : kwani aliwachukua mikononi mwake, akawawekea mikono, na kuwabari. Basi, misitie shaka, aminini tu ndani ya miyo yenu, ya kuwa amemwelea radhi mtoto huyu naye kumkaribisha kwake : amempiga na pambaja kwa mikono ya rehema zake ; (kama alivyoahidi katika Neno lake takatifu), atampa baraka ya maisha ya milele na kumfanya kuwa mshirika wa usfalme wake usio mwisho. Kwa ajili ya hayo, sisi ambaeo tu watu tuliopewa hakika hivi, ya kumpenda kwake mtoto huyu Babaetu wa mbinguni kama ilivyowekwa wazi na Yesu Kristo Mwanawewe : na tumshukuru kwa imani na ibada ya kweli, tuiseme sala aliyotufunza Bwana wetu nafsi yake :

Babaetu uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme

wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututoshia. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. Amina.

EWE Mungu Mweza-wa-yote, huna mwanzo huna mwisho ; nawe ndiwe Babaetu wa mbinguni ; sisi tu miguni pako, twakuambia asante kwa ulivytukirimu ya kurtuita hata tukapata kujua neema yako, na kuamini kwako : utuongeze ujuzi huo, uikaze miyoni mwetu imani hiyo milele. Mtoto huyu umpe Roho wako Mtakatifu, apate kuzawa uzazi ulio mpya, na kufanywa kuwa mtu wa kuurithi wokofu usio mwisho : kwa ajili yake yeyle Bwana wetu, Yesu Kristo, aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. Amina.

¶ Ndipo hapo yule Padre huuliza jina lake mtoto yule, hata wakiisha kilitamka palepale wale madhamini jina lake, yule Padre hunena,

JE, wewe, kwa jina la mtoto huyu, wamkataa Shetani na kazi zake zote, na furaha na utukufu visivyo faa vya ulimwengu huu, na kule kuyatamani-tamani mambo hayo yote kwa shauku : pamoja na tamaa za mwilini, hata uwe wewe kukataa kuvifua na kuchukuliwa navyo ?

Hujibu. Navikataa vyote.

Padre

JE, wewe waamini kwa Mungu Baba, Mwenyezi, Muumba mbingui na nchi ?

Na kwa Yesu Kristo, Mwanawewe mzaliwa pekee, Bwana wetu ? Na ya kuwa alitungishwa mimba na Roho Mtakatifu, akazaliwa na Mwanamwali Mariamu : tena kuwa aliteswa katika enzi ya Pontio Pilato : akasalibiwa, akafa, akazikwa ; akashuka na kuingia kuzimu ; hata siku ya tatu akasimama tena ametoka kwa wafu ; kisha akapaa na kuingia mbinguni ; tena ameketi upande wa mkonono wa kuume wa Mwenyezi Mungu Baba ; ndiko atakakotoka

kuja tena, katika mwisho wa ulimwengu, kuwaamua walio hai hata waliokufa?

Nawe waarnini kwa Roho Mtakatifu : Kanisa takatifu lililo ulimwenguni mote : Ushirika wa watakatifu : Madhambi kusamehewa : Mwili kufufuka : na Maisha ya milele baada ya mauti?

Hujibu. Haya yote ninayakubali sana kuyaamini.

Padre

BASI, wataka kuyafuata mapenzi matakatifu ya Mwenyezi Mungu kwa kuyati, na kuyashika maagizo yake ; uyaandame hayo tu siku zote utakazokuwa hai?

Hujibu. Nataka.

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

SISI twampokea mtoto huyu katika mkutano wa kundi la Kristo, nasi twamtia alama ya msalaba* ya kuonyesha ya kwamba baadaye hataona haya * *Ndipo hapo yule kuikiri imani ya Kristo msalibiwa, Padre humpiga alama ya msalaba yule mtoto katika japa la uso.* beramu yake, na kwendelea kuwa askari mwaminifu na utumishi wa Kristo, hata maisha yake ya duniani yaishe. Amina.

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

HIWI, enyi ndugu zangu mpendwao sana, tumwo-navyo mtoto huyu kuwa amezaliwa uzazi mpya, na kutuliwa katika mwili wa Kanisa la Kristo, na tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mambo hayo mema, nasi tumwombe kwa umoja wa hali, mtoto huyu ayapishe maisha yake yanayosalia duniani kwa mfano wa mwanzo huu.

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

T'WAKUSHUKURU sana, ewe Baba mwingu wa rehema, kwa kuwa mtoto huyu umeridhia kumpa uzazi mpya kwa Roho wako Mtakatifu, na kumkubali kuwa mwanayo wewe kwa ulezi wako, ukarntia katika mwili wa Kanisa lako lililo takatifu. Nasi hivi tulivyo

miguuni pako, twomba kwako kwa unyenyekevu, kumba mtoto huyu, ali hali ya kufa na kutokana na dhambi, na kuwa hai kwa kuilekea haki, na kuwa ni mtu aliyezikwa pamoja na Kristo katika mauti yake : umpe kumsalibu yule mtu wa kale, na kuukomesha kabisa mwili wote wa dhambi : na ya kwamba, hivyo aliyopewa kuwa mshirika wa kufufuka kwake ; hata iwe mwishowe, baada ya haya, pamoja na waliobaki katika Kanisa lako takatifu, yeze naye apate kuwa mtu wa kuurithi ufalme wako usiokuwa na mwisho : kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

¶ *Hapo ndipo husimama wote ; Padre huwaambia wale madhamini maonyo haya :*

KWA maana ya vile aliyoaahidi mtoto huyu kwa ndimi zenu ninyi madhamini wake, ya kumkataa Shetani na kazi zake zote, na kuamini kwa Mwenyezi Mungu na kumtumikia, inawapasa ninyi kukumbuka kwamba fungu lenu lilowapasa kila mmoja, ni kuangalia kwamba mtoto huyu afunzwe, hapo atakapokwisha kuwa ni mtu wa kuelewa nayo, jinsi zilivyo kubwa hizo nadhiri na ahadi na amana alizozikiri hapa kwa ndimi zenu. Naye kwamba apate kuyajua zaidi mambo hayo, sharti ni kumtaka asikize hotuba ; na sana ni kumtenezeza ya yeze kujifunza Imani ya Mitume, na Sala ya Bwana, na zile Amri Kumi, kwa lugha ya nchi aketiyo, na kujifunza mambo yote yaliyobaki ambayo yampsaa mtu wa Kikristo kuyajua na kuyaamini apate kuwa hali njema roho yake ; tena ni kumlea hali ya heshima apate kuishi maisha yake katika kicho cha Mungu na dini ya Ukristo ; huku mkikumbuka kuwa huu ubatizo watuonya msano wa hali yetu tuikiryo : nayo ni ya kumwandama Mwokozi wetu Kristo kwa kielelezo chake alichotuonya, na kufananishwa hali zetu na hali yake : ili kwamba, kama yeze aliyokufa na kufufuka kwa ajili yetu, sisi nasi tuliobatizwa tuwe wa kufa na kutokana na dhambi, na kufufukia haki ; huku tukiendelea katika kuzifisha tamaa zetu mbovu na uharibifu wetu, na kuongea kila siku katika kila lipasalo heshima na uchaji-wa-Mungu wa maisha.

¶ Isipokuwa wale waliomleta kanisani mtoto yule watakapomjibu masiala yake yule Padre kwa kutohakikisha sawasawa, kuwa alibatizwa yule mtoto kwa maji, kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, (nayo ni mafungu yaliyo lazima katika ubatizo;) ndipo hapo yule Padre humbatiza kwa kui-fuata kawaida itanguilayo kabla ya hii, iliyoamriwa ya Kuwabatiza Watoto mbele ya Watu, isipokuwa zamani za kumtia yule mtoto katika fonti, hutumia maneno haya,

UKIWA hujabatizwa bado, Fulani, mimi nakubatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

TARATIBU YA KUBATIZA WATU WAZIMA,

maana, ambao kwamba waweza kujibu wenyewe.

¶ Watakapopatikana watu ambao kwamba wataka kubatizwa, nao ni watu wazima, ndipo hapo hupewa habari Bishopu, au mtu atakayewekwa kwa kuangalia mambo hayo, kabla ya siku yake muda wa juma moja zima usipungue; na watakaompa habari ni wale wazazi wao, au watu wengine ambao kwamba ni watu wenye akiili; ili kwamba iwe kama ipasayio, wapate kujulikana kuewa wamefunzwa ya kutosha katika asili za dini ya Kikristo, tena watu hao wahimizwe kujitewa tayari kwa kuomba na kufunga, wapate kupokea Sakramenti hii iliyo takatifu.

¶ Nao watakaponekana kuwa wafaa, ndipo hapo wale madhamini hukapo tayari (watu wakiisha kutamka kwa siku ya Junapili walioagana yote), wapate kuwaleta karibu ya fonti baada ya kwisha kusomva Somo la pili, kwaniba ni la Sala ya Asubuhi, kwamba ni la Sala ya Jioni, kama atakavyoona yule Padre.

¶ Padre akiusha kusimama palepale, huuliza, kwamba hapa pana mtu aliyebatizwa tangu hapo au hapana: watakapomwambia, Hapana, ndipo hapo yule Padre husema hivi,

ENYI niwapendao sana, kwa hivyo ambavyo watu wote wametungwa mimba na kuzaliwa katika dhambi (nacho kilichozaliwa kwa mwili huwa mwili), na walio katika mwili hawawezi kumpendeza Mwenyezi Mungu, ila wao waishi katika hali ya dhambi, huku wakifanya madhambi mengi ya vitendo; na kwa vile Bwana wetu Kristo asemavyo kwamba, Hawezi mtu kuingia usalme wake Mwenyezi Mungu asipokuwa ni mtu aliyezaliwa mara ya pili aliyezaliwa uzazi mpya kwa maji na Roho Mtakatifu: mimi hivi nawataka sana mmilingane Mwenyezi Mungu Baba kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ili kwamba kwa wema wake wa ukarimu awajalie watu hara kupata neno moja ambalo kwa tabia *yao ya asili hawawezi* kulipata: nalo ni la *wao* kubatizwa kwa maji na Roho Mtakatifu, na kukaribishwa katika Kanisa lake Kristo, na kufanywa kuwa via *vivilzyo* hai mumo Kanisani.

¶ Ndipo hapo Padre hunena,

Na tuombe

(¶ Ndipo hapo jamii ya waliokutana hupiga magoti.)

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, huna mwanzo huna mwisho, wewe kwa rehema zako kuu ulimwokoa Nuhu, uliwaokoa na wa nyumbani mwake, kwa ile safina, ukawaponya wao na kule kuangamia majini : tena uliwaongoza salama watu wako wana wa Isiraeli katikati ya Bahari Nyekundu, kwa kuonya humo mfano wa ubatizo wako mtakatifu : kisha kwa kubatizwa kwake Mwanayo Mpenzi wako sana Yesu Kristo katika mto wa Yorodani, uliyatakasa maji kwa kuosha dhambi kwa maana ya ndani : sisi tuliope twakuomba sana kwa ajili ya rehema zako zisizo mpaka, uwaangalie *watu hawa* kwa rehema, uwaoshe na kuwatakasa kwa Roho Mtakatifu : ili kwamba pamoja na kuokoka *kwo* na ghadhabu zako, *wakaribishwe* na safinani mwa Kanisa lake Kristo : kisha, kwa vile *watakavyokaa* katika imani, na kuwa hali ya furaha kwa kutumaini, na kukazwa mashina *yao* katika kupeendana, huku kuyavuka *kwo* mawimbi ya ulimwengu huu wa dhiki na taabu, *wafikilie* mwisho katika nchi ya maisha yaendeleayo milele, *wapate* kutawala pamoja na wewe katika nchi hiyo milele na milele : kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, mambo yote wayaweza wewe, wala hushindwi na kifo : Msada wao wote walio na uhitaji, Auni yao jamii ya wakukimbilia, Maisha yao waaminio, Kufufuliwa kwao waliokufa, pia hayo ni wewe : sisi twakulingana, twawaombea *watu hawa*, ili hivi *wajavyo* katika ubatizo wako mtakatifu *walipate* ondoleo la madhambi *yao* kwa uzazi mpya wa rohoni. *Uwapokee*, ewe Bwana kama ulivyoahidi kwa Mwanayo Mpenzi wako sana, pale aliponena, Ombeni mtaewa : *tafuteni mtaona* : bisheni mtafunguliwa. Na sasa iwe vivyo : utupe sisi tukuombao : tutafutao na tuone : utufungulie mlango sisi tubishao : ili kwamba *watu hawa* *wafurahie*

baraka iendeleayo milele ya joshio lako la mbinguni, na kupata kuufikilia usfalme wa milele uliotuahidi kwa Kristo Bwana wetu. *Amina.*

¶ Ndipo hapo husimama wale watu, Padre hunena,

Yasikizeni maneno ya Injili ilioandikwa na mtakatifu Yohana, Mlango wa tatu, mwanzo Kifungo cha kwanza.

PALIKUWA na mtu mmoja katika Mafarisayo jina lake akiitwa Nikodemo, naye ni mkubwa katika Mayahudi. Huyo akamwendea Yesu usiku, akamwambia, Ewe Rabii, twakujua u mwalimu, umekuja kutoka kwa Mungu, kwani hapana awezaye kuzifanya ishara hizo ufanyazo wewe isipokuwa Mwenyezi Mungu yu pamoja naye. Yesu akamjibu akamwambia, Ni kweli, ni kweli, nakuambia, asipozaliwa mtu uzazi utokao juu, *asipozaliwa upya mtu*, hawezi kuuona usfalme wa Mwenyezi Mungu. Nikodem akamwambia, Huwaje mtu kuzaliwa ali mzee ? Aweza kuingia mara ya pili tumboni mwa mamaye akazaliwa ? Yesu akamjibu, Ni kweli, ni kweli, nakuambia, asipozaliwa mtu kwa maji na Roho, hawezi kuingia usfalme wa Mwenyezi Mungu. Kilichozaaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaaliwa kwa Roho ni roho. Sione ajabu ya kuwa nimekuambia, Imewapasa kuzaliwa uzazi utokao juu, *kuzaliwa upya*. Upepo huvumia upendako, na sauti yake waisikia, ila huuoni utokeako, wala uendeako. Ndivyo awavyo kila aliyezaliwa kwake Roho.

¶ Kisha baadaye husema maneno ya maonyo haya yafuatanyo :

ENYI wapenzi, katika Injili hii mmeyasikia maneno yake halisi Mwokozi wetu Kristo, ya kwamba, asipozaliwa binadamu kwa maji na Roho, hawezi kuingia usfalme wa Mungu. Nanyi kwa neno hilo mwaweweza kutambua Sakramenti hii kuwa haina budi, iwapo yapatikana. Ni kama vile, na wakati wa kupaa kwake mbinguni (kama tusomavyo katika Mlango wa mwisho wa Injili yake mtakatifu Mariko) aliaagiza wanafunzi wake, akawaambia, Enendeni ulimwenguni mote, mkavihubiri Injili viumbe vyote. Mwenye kuamini na kubatizwa

ataokoka : na mwenye kutoamini atahuhukumiwa. Tena neno hilo latuonya wazi manufaa yake yalivyo makuu tuyapatayo mumo kwa ajili ya hayo. Ndiyo maana yake alivyojibu mtakatifu mtume Petero, wakati alipoanziza kuihubiri kwake Injili wengi walichomwaa miyoni mwao, wakamuuliza ye ye na mitume wenziwe, Enyi waume ndugu zetu, tufanyeje? akawaambia, Tubieni mkabatizwe kila mtu katika jina la Yesu Kristo, *mpate* msamaha wa dhambi zenu ; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwani ahadi hiyo ni kwa ajili yenu na kwa ajili ya watoto wenu, na kwa ajili ya wote walio mbali sana, kadiri ya watakaoitwa na Bwana Mungu wetu waje kwake. Tena akawaonya kwa maneno mengine mengi, na kuwasihii, akisema, Jiokoeni wenyewe na kizazi hiki kilicho kombo. Kwani (kama ashuhudiavyo mtume yeyle pahali pengine), ubatizo huo hutuokoa sisi sasa, maana, si kuziepua tako za mwili, bali ni kule kutaka jawabu ya moyo ulio mwema kwa upande wa Mungu, kwa njia ya kufufuliwa kwake Yesu Kristo. Basi msiyatilie shaka kwa lolote, amin'i tu ndani ya mioyo yenu, ya kuwa atawakaribisha na kuwawelea radhi *watu hawa nao*, waliopo hapa *wenye* kutubu kwa kweli na kumwenda kwa imani ; atawajalia kusamehewa madhambi *yao* na kupewa Roho Mtakatifu ; naye atawapa baraka ya uzima wa milele, atawafanya *wave washirika* wa ufalme wake wa milele.

Kwa ajili ya hayo, sisi ambaou tu watu tulipewa hakika hivi, ya Babaetu aliye mbinguni alivyowawelea radhi *watu hawa*, kama ilivyowekwa wazi na Yesu Kristo Mwanawe, na tumshukuru kwa imani na ibada ya kweli, tunene,

EWE Mungu Mweza-wa-yote, huna mwanzo huna *mwisho* : nave ndiwe Babaetu wa mbinguni ; sisi tu miguuni pako, twakuambia asante kwa ulivyonukirimu ya kutuita hata tukapata kujua neema yako na kuamini kwako ; utuongeze ujuzi huo, uikaze miyoni mwetu imani hiyo milele. *Watu hawa uwape* Roho wako Mtakatifu, *wapate* kuzawa uzazi ulio mpya, na kufanywa kuwa *watu* wa kuurithi wokofu usio *mwisho* : kwa Bwana

wetu Yesu Kristo, aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre husema na wale watakao kubatizwa maneno haya :*

ENYI mpendwao sana, mlikuja hapa kutaka kuupata Eubatizo mtakatifu, mmekwisha kusikia mlivyoombewa na waliokutana hapa, ya kwamba Bwana wetu Yesu Kristo akubali kuwakaribisha na kuwabarikia, na kuwondolea madhambi *yenu*, na kuwapa ufalme wa mbingu na uzima wa milele. *Nanyi mmesikia* kwamba Bwana wetu Yesu Kristo ameahidi katika Neno lake lililo takatifu, kuwa atatupa mambo yale yote tuliyomwomba ; naye ahadi hiyo hakosi ye ye upande wake, ataishika na kuitimiza. Basi kwa ajili ya hayo, baada ya ahadi hiyo akiyoahidi Kristo, imewapasa *ninyi* kwa upande *wenu* kuahidi mbele ya mashahidi *yenu* na jamii ya waliokutana hapa, ya kwamba *mtamkataa* Shetani na kazi zake zote, na kuliamini daima Neno lake Mwenyezi Mungu lililo takatifu, na kuyashika maagizo yake kwa kutii.

¶ *Ndipo hapo yule Padre huwaliza watu watakaobatizwa kila mmoja masidala haya :*

Huuliza

JE, wewe wamkataa Shetani na kazi zake zote, na furaha na utukufu visivyoofaa vyta ulimwengu huu, na kule kutamani-tamani mambo hayo yote kwa shauku ; pamoja na tamaa za mwilini, hata uwe wewe kukataa kuvifuata wala kuchukuliwa navyo ?

Hujibu. Navikataa vyote.

Huuliza

JE, wewe waamini kwa Mwenyezi Mungu Baba, Muumba mbingu na nchi ?

Na kwa Yesu Kristo, Mwanawe mzaliwa pekee, Bwana wetu ? Na ya kuwa alitungishwa mimba na Roho Mtakatifu, akazaliwa na mwanamwali Mariamu ; tena kuwa aliteswa katika enzi ya Pontio Pilato ; akasalibiwa, akafa,

akazikwa ; akashuka akaingia kuzimu, hata siku ya tatu akasimama tena : kisha akapaa na kuingja mbinguni ; tena ameketi upande wa mkono wa kuume wa Mwenyezi Mungu Baba, ndiko atakakotoka kuja tena, katika mwisho wa ulimwengu, kuwaamua walio hai hata waliokufa ?

Nawe waamini kwa Roho Mtakatifu ; Kanisa takatifu liliro ulimwenguni mote ; Ushirika wa watakatifu ; Madhambi kusamehewa ; Mwili kufufuka ; na Maisha ya milele baada ya maati ?

Hujibu. Haya yote nayaamini sana.

Huuiliza

JE, wataka ubatizwe katika imani hii ?
Hujibu. Nataka.

Huuiliza

BASI, wataka kuyafuata mapenzi matakatifu ya Mwenyezi Mungu kwa kuyatii, na kuyashika maagizo yake ; uyaandame hayo tu siku zote utakazokuwa hai ?

Hujibu. Nitafanya bidii kuyafanya, Mwenyezi Mungu akinisaidia.

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

EWE Mwenyezi Mungu mwenye rehema, *watu hawa* Uwajalie ya kwamba kwa vile atakavyozikwa Adamu wa kale aliye ndani *yao*, wapewe mtu mpya kufufuka ndani *yao*. *Amina.*

Uwajalie shauku zote za mwili zife ndani *yao* ; na mambo yote yatakwayo na Roho yaye hai, yaongezeka daima ndani *yao*. *Amina.*

Uwajalie kuwa na uwezo na nguvu, wapate kushinda kwa furaha Shetani na ulimwengu na mwili. *Amina.*

Umjalie kila imoja atakayewekwa nafsi yake kwako wewe pahali hapa kwa utumishi wetu sisi na usongezi wetu sisi, kuvikwa neema za mbinguni na kupewa thawabu ya milele, kwa rehema zako, ewe Bwana Mungu utukuzwaye, uishiye hali umetawala mambo yote, milele. *Amina.*

EWE Mungu Mweza-wa-yote, wewe uli hai milele ; Ehuyo Mwanayo Mpenzi wako sana sana Yesu Kristo, kwa kutusamehe madhambi yetu, alitokwa na maji na damu sambamba katika ubavu wake ulio wa thamani sana, akawapa na amri wanafunzi wake, ya kwenda kuwafanya wanafunzi mataifa wote, na kuwabatiza, kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu ; twakuomba utege masikio yako kwetu mkutano wako ; nawe uyatakase maji haya yaye njia ya kuosha dhambi kwa maana ya ndani ; uwajalie *watu hawa* waendao kubatizwa humo hivi sasa, wawe wenyewe kupokea neema yako iliyotimia, na kukaa daima miiongoni mwa wanayo waaminifu wateule wako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre humshika mkono wake wa kuume kila mu atakaye kubatizwa, hata akiisha kumveka kando ya fonti, pahali pafaaipo, kama aonavyo ni vyema, huwataka jina wale madhamini, kisha humvika majini au hummimini, kwa kunena,*

FULANI, mimi nakubatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

SISI twampokea mtu huyu katika mkutano wa kundi lake Kristo, nasi* twamtia alama ya msalaba, ya kuonyesha kwamba baadaye hataona haya kuikiri imani ya Kristo msalibiwa, na kupigana * *Ndipo hapo yule* kiume na dhambi na ulimwengu *Padre hunipiga alama na Shetani, chini ya beramu yake ; ya msalaba yule mtu na kwendelea kuwa askari mwa-katika japa la uso.* minifu na utumishi wa Kristo, hata maisha yake ya duniani yaishe. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

HIVI, enyi ndugu zangu mpendwao sana, tuwaonavyo *watu hawa* kuwa warmezaliwa uzazi mpya, na kutuliwa katika mwili wa Kanisa la Kristo, na tumshukuru. Mwenyezi Mungu kwa mambo haya mema : nasi tumwombe kwa umoja wa hali, *watu hawa* wapishe maisha *yao* yanayosalia duniani kwa mfano wa mwanzo huu.

¶ *Ndipo hapo hupiga magoti pia wote na kusema,*

BABAETU ulije mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalte wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usirupeleka katika kujaribiwaa, Utuokoe maovuni. Amina.

SISI tu miguuni pako twakushukuru wewe, Babaetu Swa mbinguni, kwa vile uliviyotujalia ya kuitwa kuja kuijua neema yako na kuamini kwako wewe ; utuongoze kuijua huku, ututhubutishe katika kuamini huku daima. Watu hawa uwape Roho wako Mtakatifu, ili kwamba, kwa walivyozawa upya na kufanywa kuwa warithi wa wokofu wa milele kwa Bwana wetu Yesu Kristo, waendelee kuwa watumishi kwako, wazifilie na ahadi zako, kwa yeyle Yesu Kristo Mwanayo, aishiye na kutawala pamoja nawe katika umoja wa yeyle Roho Mtakatifu, milele. Amina.

¶ *Wakiisha kusimama wote, yule Padre huwaambia wale madhamini,*

KWA vile walivyoahidi watu hawa mbele yenu ninyi madhamini wao, ya kumkataa Shetani na kazi zake zote, na kuamini kwa Mwenyezi Mungu na kumtumikia ; inawalazimu ninyi kukumbuka kwamba fungu lenu lililowapasa kila mmoja ni kuwakumbusha jinsi zilivyo kuu nadhiri na ahadi na amana walizozikiri hivi sasa mbele yenu ninyi mashahidi wao mlioteuliwa na wao ; nanyi imewapasa kuwataka wajitahidi kujitia katika mafunzo sawasawa na Neno lake Mwenyezi Mungu liliilo takatifu ; ili kwamba kwa kufanya hivyo wakue na kuongea katika neema na ujuzi wa Bwana wetu Yesu Kristo, na katika ulimwengu huu wa sasa kuishi hali ya kumcha Mungu, na haki, na makini.

¶ *Ndipo hapo huendelea kusema na wale waliobatizwa hapo, akinena,*

NANYI miliomvaa Kristo hivi kwa ubatizo, fungu lenu liwapasalo sana (kwa mlivyo fanywa ninyi kuwa wana wa Mungu na wa ule mwanga, kwa imani mliyo nayo

katika Yesu Kristo) ni la kwenenda kama kutakavyelingamana na mwito *wenu* wa Kikristo, na kama ilivyopaswa wana wa mwanga ; huku *mkikumbuka* daima ya kuwa huo ubatizo watuonya namna ya dini yetu tuliyokiri ; nayo ni kufuata kielelezoo cha Mwokozi wetu Kristo na kulinganishwa naye ; hata imekuwa, kama vile ye ye aliyyokufa akafufuka kwa ajili yetu, imetupasa sisi nasi tulibatizwa tufe kutokuwa na dhambi, na kufufukia haki, kwa kuyaua daima mambo yetu yote ya tamaa mbovu yaliooza, na kwendelea daima katika mambo ya heshima yote na hali ya kuishi katika kicho cha Mungu kabiisa kabisa.

¶ *Kila mtu aliyebatizwa kwa jinsi hii ni vyema athubutishwe na Bishopu baada ya kubatizwa kwake aktisha kuwa tayari ; ili kwamba apate kukaribishwa Ushirika Mtakatifu.*

¶ *Na pakiwa na watu ambao kwamba hawakubatizwa katika utoto wao waletwa ili kubatizwa, hawajafika miaka ya kuwa na akili na kuitwa daraka ya nafsi zao, yatosha itumiwapo kawaida ya Kuwabatiza Watoto mbele ya Watu, au (pachellewapo hatari) hutumia kawaida ya Ubatizo wa Faragha Kuwasongezee Watoto Wachanga Nyumbani, isipokuwa hugeuze neno la mtoto palipoandikwa hilo, na kulibadili kuwa mtu kila palipo na haja.*

MAJIBIZANO

(au Ḵatekisimo)

Nayo ni mafunzo ya kujifunza kila mtu kwanza
asijaletwa kwa Bishopu ili kuthubutishwa.

A. humuuliza B.

Jina lako nani ?

*B. humjibu A.*Jina langu mimi ni (*jina la Kikristo*).*A. Jina hilo ulipewa na kina nani ?*

*B. Jina hilo walionipa ni madhamini wangu, hapo
katika ubatizo wangu ; nami katika jambo hilo nilifanywa
kuwa kia cha Kristo, na kuwa mtoto wake Mwenyezi
Mungu, na kuwa mtu wa kuurithi usalme wa mbingu.*

*A. Ni neno gani walilokufanya madhamini wako
wakati huo ?*

*B. Walifanya mambo matatu kuyaahidi na kuyaweka
nadhire kwa jina langu mimi. La kwanza, ni la mimi
kumkataa Shetani na kazi zake zote, na furaha ya uli-
mwengu huu na upuzi wake, na shauku zote za mwili
zilizo na dhambi. Pili, kuwa nitaziamini Sharti zote za
Imahi ya Ukristo. Tatu, kuwa nitayashika mambo
matakatifu ya mapenzi yake Mwenyezi Mungu na maagizo
yake, na kuyaandama mambo hayo siku zote nitakazokuwa
hai duniani.*

*A. Je, huoni moyoni mwako kuwa umelazimiwa na
kuyaamini hayo waliyoyaahidi kwa jina lako, na kuya-
tenda ?*

*B. Hakika yangu ndiyo nionayo : nami kwa msaada
wake Mwenyezi Mungu nitatenda vivyo. Nami ndani
ya moyo wangu namshukuru Babaetu wa mbinguni kwa
vile alivyonii na kuniweka hali hii ya wokofu kwa*

Mwokozi wetu Yesu Kristo. Nami namwomba Mwe-
nyezi Mungu anipe neema yake, nipate kudumu mumu
humu hata mwisho wa maisha yangu.

A. Sema Sharti za Imani yako.

*B. Naamini kwa Mungu Baba Mwenyezi, Muumba
mbingu na nchi ; na kwa Yesu Kristo, Mwanawe pekee,
Bwana wetu ; ambaye alitungishwa mimba na Roho
Mtakatifu : akazaliwa na Mwanamwali Mariamu ; aka-
teswa katika enzi ya Pontio Pilato ; akasalibiwa, akafa,
akazikwa ; akashuka na kuingia kuzimu : hata siku ya
tatu akasimama tena, ametoka kwa wafu. Akapaa na
kuingia mbinguni ; naye ameketi upande wa kuume wa
Mwenyezi Mungu, Baba. Ndiko atakakotoka kuja
kuwaamua walio hai hata waliokufa.*

Naamini kwa Roho Mtakatifu ; na Kanisa takatifu
lililo ulimwenguni mote ; na Ushirika wa watakatifu ; na
Madhambi kusamehewa ; na Mwili kufufuka ; na
Maisha ya milele. Amina.

*A. Katika hizi Sharti za Imani yako ni mambo gani
ujifunzayo sana ?*

*B. Mimi kwanza hujifunza niamini kwa Mwenyezi
Mungu Baba, aliyeniumba mimi na ulimwengu wote pia.*

*Pili, niamini kwa Mungu Mwana, aliyenikomboa mimi
na wanadamu wote.*

Tatu, niamini kwa Mungu Roho Mtakatifu, anitakasaye
mimi na wateule wake Mwenyezi Mungu pia wote.

*A. Ulisema kwamba madhamini wako waliahidi kwa
ajili yako, ya kuwa utayashika maagizo yake Mwenyezi
Mungu ; maagizo hayo niambie ni mangapi hesabu yake ?*

*B. Ni kumi.**A. Ni kama yapi ?*

*B. Ni kama aliyyoyasema Mwenyezi Mungu katika
Chuo cha Exodus, Mlango wa Ishirini, aliponena, Mimi
ni Yehova Mwenyezi Mungu wako, niliyekutoa nchi ya
Misri, kutoka hiyo nyumba ya utumwa.*

*I. Usiwe na miungu mingine mbele zangu wawao
wote.*

*II. Usifanye sanamu ya kuchonga, umbo lolote lililo
juu mbinguni, au lililo chini duniani, au lililo chini ya*

dunia katika maji : usivisujudie, wala kuvitumikia : kwa kuwa mimi Yehova Mungu wako ni Mungu mwénye wivu, niwapatilizaye wana kwa uovu wa baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao ; na kuwapa rehemu watu elfu elfu wanipendao, wayashikao maagizo yangu.

III. Usitaje jina la Yehova Mungu wako kwa upuzi, kwani Yehova hatamfanya kuwa hana makosa mtu atajaye jina lake kwa upuzi.

IV. Ikumbuke siku ya sabatu kuitakasa. Siku sita tumika, ufanye kazi zako zote ; ila siku ya saba ndiyo sabatu ya Yehova Mungu wako ; siku hiyo usifanye kazi, wewe, wala mwanayo mume na mke ; wala mtumwayo mume na mke ; wala nyama zako za mji ; wala mgeni wako aliye ndani ya malango yako : maana, kwa siku sita Yehova alifanya mbingu na nchi, na bahari, na vyote viliyyo humo, akapumzika kwa siku ya saba : ndipo akaibarikia Yehova ile siku ya sabatu, akaitakasa.

V. Mheshimu babaako na mamaako, siku zako zifanyike ndefu juu ya nchi upewayo na Yehova Mungu wako.

VI. Usiue.

VII. Usizini.

VIII. Usibe.

IX. Usimshuhudie mwenzio kwa uwongo.

X. Usitamani nyumba ya mwenzio, usimtamani mke wa mwenzio ; wala mtumwawe, mume au mke ; wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala kiwachcho chote alicho nacho mwenzio.

A. Ujifunzayo sana katika maagizo haya ni mambo gani ?

B. Mimi nijifunzayo sana ni mambo mawili : yaliyonipasa kwa Mwenyezi Mungu, na yaliyonipasa kwa mwenzangu.

A. Je, yaliyokupasa kwa Mwenyezi Mungu ni yapi ?

B. Mimi yaliyonipasa kwa Mwenyezi Mungu ni kumwamini na kumcha na kumpenda, kwa moyo wangu wote, na akili zangu zote, na roho yangu yoje, na nguvu zangu zote ; na kumwabudu, na kumshukuru, na kute-

gemea kwake kabisa ; na kumlingana, na kumheshimu jina lake takatifu na Neno lake, na kumtumikia kweli siku zote niishizo.

A. Yaliyokupasa kwa mwenzio ni yapi ?

B. Yaliyonipasa kwa mwenzangu ni kumpenda kama nafsi yangu, na watu wote kuwatendea vyema kama ambavyo mwenyependa ningependa nitendewe na wao : ni kuwapenda babaangu na mamaangu, na kuwastahi na kuwasaidia : na kumstahi na kumtii Mfalme, na wote waliowekwa na amri chini yake : na kujinyenyekeza chini ya walio na amri juu yangu, na waalimu wangu, na wani-chungao roho, na bwana zangu, jamii ya walioko : na wanipitao kwa madaraja yao kuwakalia kwa unyenyekevu na ustahivu : nisimdhuru mtu awaye yote, katika kutenda wala katika kunena ; bali niwe mtu wa kweli na haki katika niyatendayo yote : tena niwe mtu nisiyemwekeea mwenzangu mfundo moyoni, wala kumchukia mtu awaye yote : tena niwe mtu mwénye kuizua mikono yangu na kuiba kitu chochote, na kujilinda ulimi wangu nisiseme maneno mabaya na uwongo, wala nisimsingizie mtu awaye yote : na kujilinda mwili wangu ili nikae hali ya kudhibiti nafsi yangu, na kujilinda na makuu na mambo mabaya ya ulevi na kuzini : tena ni kuwa mtu nisiyetamani mali ya mtu wala kuyalilia choyo ; bali niwe mwénye kujifunza na kujibidiisha kufanya kazi yangu nipaye riziki zangu, nipaye na kutenda yaliyonipasa katika daraja la maisha Mwenyezi Mungu atakayopenda kuniweka, iwayo yote.

Yule Mwalimu huendelea kuuliza,

A. Mwanangu mwema, neno hili moja fahamu sana, ya kwamba mambo haya huyawezi pekeo kuyatenda, wala kwenenda katika maagizo yake Mwenyezi Mungu na kumtumikia, usipopata neema yake. Nayo imekupasa kujifunza kumtaka neema hiyo kila wakati kwa bidii nyingi. Haya basi, nataka kuisikiza Sala ya Bwana, waweza kuisema au huwezi ?

Hujibu

B. Babaetu uliye mbinguni, jina lako litakaswe, ufalme wako na uje, mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, utuokoe maovuni; kwa kuwa ufalme, na nguvu, na utukufu, ni vyako milele. Amina.

A. Katika sala hii ni neno gani ultakalo kwake Mwenyezi Mungu?

B. Mimi katika sala hii nataka kwa Mwenyezi Mungu Bwana wangu, Babaetu wa mbinguni, ambaye ndiye mpaji wa kila wema, aniletee mimi neema yake na watu wote, ili tupate kumwabudu na kumtumikia na kumtii, kama itupasavyo. Nami naomba mumo kwa Mwenyezi Mungu, atuletee mambo yote yahitajiwayo na roho zetu na miili yetu; na kuturehemu, na kutusamehe makosa yetu; tena kwamba atapendezewa na kutuokoa na mambo yote yaliyo na hatari, na kutulinda nayo, yakiwa ni ya rohoni au mwilini: naye akubali kutuweka salama na dhambi na kila uovu, na kutuokoa na adui wetu wa rohoni, na mauti ya milele. Nami natumaini nitatendewa hayo na ye ye kwa rehema zake na wema wake, kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo. Ndipo nikasema, Amina, maana, na yawe vivile.

Huuiliza

A. Ni nyingapi Sakramenti alizoziweka Kristo katika Kanisa lake?

B. Ni mbili tu, ambazo ndizo ziwapasazo watu wote kwa wokofu: nayo ndiyo Ubatizo na Karamu ya Bwana.

A. Waonaje maana yake ni nini hilo jina la Sakramenti?

B. Mimi naona jina la Sakramenti maana yake ni alama ya nje ionekanayo, ya neema ya ndani, ya rohoni, tuliyopewa sisi: nayo alama hiyo ndiyo iliyoagizwa na Kristo mwenyewe, ipate kuwa kama njia ya kuipokelea ile neema, na kuwa buruhani ya hakika ya kuwa nayo.

A. Hii Sakramenti ina mafungu mangapi?

B. Ina mafungu mawili: nayo ni ile alama ya nje ionekanayo, na ile neema ya ndani, ya rohoni.

A. Je, huo Ubatizo, alama yake ya nje ni ipi?

B. Ni maji, ambayo yule mtu hubatizwa ndani yake, kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu.

A. Ile neema ya ndani, ya rohoni, ni ipi?

B. Ni mtu kufa kwa dhambi, akazawa upya kwa haki: kwani sisi kwa ile asili yetu tumezawa katika dhambi, nasi tu wana wa ghadhabu, lakini kwa neema hii sisi kufanywa kuwa wana wa neema.

A. Ni lipi lihitajiwalo kwao watakao kubatizwa?

B. Ni toba, ambayo katika hiyo wao huiziacha dhambi: tena imani, ambayo katika hiyo wao huyaamini sana aliyoyaahidi kwao Mwenyezi Mungu katika Sakramenti hiyo.

A. Basi huwaje kubatizwa wale watoto wachanga, nao wali hali hawawezi kwa ule utoto-uchanga wao kutenda mambo kama hayo?

B. Kwa kuwa walitoa ahadi kuyatenda yote mawili kwa midomo ya wale madhamini wao, na hiyo ahadi yao wakiisha kuwa wakubwa, inawapasa wenyewe kuitimiza.

A. Sakramenti ya Karamu ya Bwana iliagizwa kwa maana gani?

B. Ili kukumbuka daima dhabihu ya kufa* kwake Kristo, na kukumbukia zile faida tupatazo humo.

A. Ni lipi fungu la nje la Karamu ya Bwana, maana, ni ipi alama yake?

B. Ni mkate na divai, ambavyo Bwana ameagiza vipokewe.

A. Ni kama lipi lile fungu la ndani, maana, ni kama lipi lile jambo lililoonyeshwa maana yake humo?

B. Ni Mwili na Damu yake Kristo, ambazo ni kutwawa na kupokewa hakika hakika pasipo shaka na wale waa-miniu, katika Karamu ya Bwana.

A. Ni kama yapi manufaa ambayo tu wenyewe kuyashirikiana humo?

B. Ni kule kupewa nguvu na kuburudishwa roho zetu kwa Mwili na Damu yake Kristo, kama vivile miili yetu ipewavyo nguvu na ule mkate na ile divai.

A. Hao waiendeao Karamu ya Bwana imewapasa kufanyaje?

B. Waiendeao Karamu ya Bwana imewapasa kupele-leza katika nafsi zao, kuijangalia, ni waliozitubia dhambi zao zilizotangulia au hawakuzitubia, wana na azima iliyo imara ya kuishi maisha mapya na kuwa na imani iliyo hai katika rehema zake Mwenyezi Mungu awarehemuzu katika Kristo, huku wakiyakumbuka mauti yake kwa kushukuru ; kisha imewapasa kuketi na watu wote kwa mapenzi.

¶ Katika kila msikitini, yule Padre ndani yake, hijibidiisha kwa siku za Jumapili na za Idi katika Sala ya fioni katika mwisho wa Somo la pili, kuwafunza na kuwaliza vijana waziwazi mle msikitini, ambao ni wa katika mipaka ya msikitini wake yeze, kama atakavyoawona watosha hesabu yao, maneno ya fungu mojawapo katika majungu ya majibizano haya.

¶ Na mababa na kina mama, na mabwana na kina bibi kadi ya waliohuuwaacha wana wao na watumishi wao na wanafunzi wao ambao kwamba hawajifunza majibizano haya, wapate kwenda msikitini kwa saa iliyyowekoa wakamsikize yule Padre kwa kutii hata waishe kujifunza yote ambayo kwamba humu wameagizwa kujifunza.

¶ Na wale wana, mara wakiisha kupata umri wa kufaa, wakajua kuyahenya kwa maneno yao waliozawa nayo, maneno ya Imani na Sala ya Bwana na zile Amri kumi, wakajua na kuyajibu mengine yaulizwayo katika majibizano mafupi haya, hapo ndipo wapelekwe kwa Bishopu. Na kila meno na ave na mmoja katika madhamini wake kule kushuhudia kuwekewa mikono kwake.

¶ Hata yule Bishopu atakapokwisha kuwajivisha wenywewe ni wakati gani atakapoletewa vijana kwake wapate kuwekewa mikono, hapo ndipo, wakati huo Padre wa kila msikitini aandike orodha wa majina yao watu hao wote walio katika mipaka ya msikitini wake, ambao kwamba awaona ni watu wa kuletu kwa Bishopu ili kuthubutishwa, aandike na jina lake mumo, ampeleke au aende nao nafsi yake akampe : na watu hao yule Bishopu atakapowaoa wafadu huwaweka mikono kama itaka-vyoletwa baada ya haya.

TARATIBU YA KUTHUBUTISHA,

au ya kuwawekea mikono watu ambaa kwamba wamekwisha kufikilia umri wa kupata akili.

¶ Kwa siku waliokwisha kuwekewa wale watu ambaa kwamba watathubutishwa wakati huo, haja wakapangwa na kusimama mbele yake yule Bishopu, kisha yeze (au Padre mwingine ataka-vekwa na yeze kwa ajili ya neno hili) husoma mwanzo huu wa maelezo uandamao hapa.

¶ LI kwamba wasongezewe huku kuthubutisha kwa jinsi ya kuwafaa zaidi, hao watakaopewa, Kanisa limeona vyema kuagiza ya kwamba huko mbeleni asithubutishwe mtu ila ajue kuyasema maneno ya Imani yake, na Sala ya Bwana, na zile Amri kumi ; ajue na kuyajibu hayo yali-yobaki yaulizwayo katika Majibizano Mafupi : nayo ni ada moja ambayo yafaa sana kuishika ; ili kwamba wale watoto wakiisha kukua kuwa watu wenyewe akili zao, nao wakiisha kujifunza ambayo wale madhamini wao wali-yatoa ahadi kuwafanya Ubatizo wao, wewe kuyakiri hayo na kuyathubutisha waziwazi mbele ya Kanisa kwa midomo yao na miyo yao ; watoe na ahadi ya wao kwendelea mbele kwa uaminifu katika kujibidiisha kuyatunza, kwa neema yake Mwenyezi Mungu, hayo ambayo kwamba wayaungama kuwa waliyakubali kuyatenda.

Au huu,

WAPENZI katika Bwana, Kanisa kwa kutumia kuthubutisha hufuata walivyoonyesha mitume wa Kristo. Kwa kuwa katika mlango wa nane wa Vitendo vyta Mitume twasoma haya :—

Wale waliotawanyika wakazunguza-zunguka waki-lilhubiri lile neno. Filipu akateremka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri *habari njema za Kristo*. Walipomwamini Filipu akihubiri ile habari njema ya ufalme wa Mungu na lile jina la Yesu Kristo, wakabatizwa waume kwa wake. Wale mitume walio-kuwa ndani ya Yerusalem waliposikia ya kwamba

Samaria imelipokea neno la Mwenyezi Mungu, wakawapelekeea Petero na Yohana; ambao wali-pokwisha kuteremkia kwao, wakawaombea, ili kwamba wapewe Roho Mtakatifu: kwani hajamshukia mtu wao hata mmoja: isipokuwa wamebatizwa katika jina la Bwana Yesu. Ndipo wakawekea mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

Maandiko haya yatufundisha ya kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu cha kupita kawaida hutolewa kwa kuweka mikono na kuomba. Na kwa kuwa kipawa hiki hutoka kwa Mungu tu, sisi tulio hapa tumwombe Mwenyezi Mungu kwamba wao walio-fanywa watoto wake katika Ubatizo awatie nguvu kwa Roho wake Mtakatifu katika kuthubutishwa.

Basi ninyi, mtakaowekewa mikono sasa, imewapasa kusema mbele ya mkutano huu kwamba mwakusudia sana kwa msaada wa kipawa hiki, kwenenda katika imani ya Kristo, na kutii mapenzi ya Mungu na amri zake; na kukiri waziwazi ya kwamba hamna budi kutimiza mambo ya Kikristo mliofungiwa na Ubatizo wenu.

¶ Hapo ndipo yule Bishopu hunena,

JE, ninyi mliopo mbele zake Mwenyezi Mungu, na mkutano huu, mwarejeza upya ile nadhiri yenyе maana makuu, ile ahadi yenu iliyowekwa kwa majina yenu katika kubatizwa kwenu; huku mkikubali kuithubutisha ninyi wenyewe, na kuyakirii kuwa yamewalazimu kuya-mini na kuyatenda yote, madhamini wenu waliyojitewe wakati ule kwa ajili yenu?

**¶ Ndipo wao hujibu kila mmoja, kwa sauti yenyе kusikilikanaa,
Naam, ndiyo**

**¶ Ndipo yule Bishopu hunena,
Huitika,** SAADA wetu u katika jina la Yehova, Aliyeumba mbingu na nchi. Bishopu. Jina la Yehova na libarikiwe, Huitika. Tokea sasa hata milele. Bishopu. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu, Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Bishopu

Na tuombe

EWE Mwenyezi Mungu, wewe una nguvu zote, nawe maisha yako ni ya milele, wewe umeridhika hata umewapa kuzawa upya hawa watumishi wako kwa maji na Roho Mtakatifu, umewapa na msamaha wa madhambi yao, pia yote; sisi twakuomba Bwana, uwatie nguvu watu hawa, kwa yule Msada, yule Roho Mtakatifu; nawe kila siku uvikuze ndani yao vipawa vyako namna nyingi nya neema: navyo ni roho ya hekima na fahamu, roho ya shauri na nguvu za rohoni, roho ya maarifa na ya kumtii Mwenyezi Mungu kweli; nawe uwajalize roho yenyе kukucha kwa utakatifu, sasa na hata milele. *Amina.*

¶ Ndipo hapo wao huja kwa taratibu yao na kupiga magoti kila mmoja mbele ya Bishopu, naye huwavekeea mikono yake kadiri ya walioipo mmoja mmoja, akinena,

UMKINGE huyu mtoto wako, ewe Bwana, (*au, Umkinge huyu mtumishi wako, ewe Bwana*) kwa neema yako ya mbinguni, ili apate kudumu katika kuwa mtu wako milele, ili naye aongee kila siku katika Roho wako Mtakatifu, aendelee na mbele, hata aufikilie ufalme wako usio mwisho. *Amina.*

¶ Hapo ndipo yule Bishopu hunena,

BWANA na awe pamoja nanyi. *Huitika.* Na awe pamoja na roho yako.

¶ Hata wakiisha kupiga magoti yule Bishopu huongeza kunena,

Na tuombe

BABAETU ulije mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kutotosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. *Amina.*

Na sala hii,

EWE Mwenyezi Mungu, una nguvu zote, na maisha yako ni ya milele; wewe ndiwe utupaye kuyapenda na kuyatenda ambayo ni ya kufaa na kupendekeza mbele zako, ewe Mungu Mfalme wetu; sisi tu miguuni pako, twawaombea hawa watumishi wako, ambao tumewawekea mikono sasa kwa kufuata kielelezo cha mitume wako watakatifu, ili kuwapa hakika, kwa ishara hiyo, ya fadhili yako uliyo nayo kwa, na wema wako wenye neema. Nasi twakuomba sana, mkono wako wewe wa ubaba na uwe juu yao daima; Roho wako Mtakatifu naye awe pamoja nao milele, hata kwa jinsi utakavyowaongoza katika kulijua na kulitii Neno lako, iwe wao, mwisho wa yote, kuupata uzima wa milele; kwa Bwana wetu Yesu Kristo, naye ndiye aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, uli Mungu mmoja daima, milele. *Amina.*

EWE Bwana Mweza, Mungu usiye mwanzo wala mwisho, twakuomba sana utuneemeshe ya kwamba miyo yetu pamoja na miili yetu, vipate kuongozwa hivyo na kutakaswa na kutawaliwa na wewe, katika njia za sheria yako na vitendo vya mausio yako, ili, kwa vile utakavyotulinda duniani na ahera, tuhifadhike miili yetu na roho zetu; kwa Bwana wetu Mwokozi wetu Yesu Kristo. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Bishopu huwaombea baraka, kwa kusema hivi :*

BARAKA yake Mungu Mweza-wa-yote, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, iwe juu yenu na kukaa kwenu milele. *Amina.*

Au hivi,

ENENDENI ulimwenguni na amani; muwe hodari; lishikeni lililo jema; msimlipe mtu mabaya kwa mabaya; watieni moyo walio wanyonge; wategemezeni wasio na nguvu; wasaidieni walio mashakani; waheshimuni watu wote; mpe-

ndeni Bwana na kumtumikia, mkifurahi katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Na baraka ya Mwenyezi Mungu, Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, iwe mwenu ikae kwenu daima. *Amina.*

¶ *Wala mtu asikaribishwe katika Ushirika Mtakatifu hata ataka-powekewa mikono au kuwa mtu aliye tayari kwa kuwekewa mikono, naye yuataka kama hayo mwenyewe.*

TARATIBU YA NDOA

¶ *Watu wote watakaoaa na kuolewa hutangulia kuitangaza habari ya ndoa yao msikitini siku za fumapili tatu mbali mbali, wakati wa Sala ya Asubuhi, au, (ikiwa hakuna Sala ya Asubuhi,) wakati wa Sala ya Jioni : yule Padre hunena kama taratibu ya desturi,*

MIMI naitangaza habari ya ndoa kati ya Fulani, mtu pahetiye pahali fulani na Fulani mwanamke aketiye pahali fulani. Pakiwa na mtu kwenu ajua sababu au kizuizi cha haki cha kuwazuwa watu hawa wawili wasiungamanishwe katika Ndoa takatifu, imempasa kusema.

Hii ndiyo mara ya kwanza, (*au ya pili, au ya tatu*), ya kuwaauliza kama haya.

¶ *Na wakiwa wakaa katika mipaka ya misikiti mbali mbali, hutolewa maulizo ya habari yao katika misikiti yote mwili, yule Padre wa msikitii huu na asiwaaze asipopata hati ya kumpa hakika ya kuwa yamekwisha kuulizwa maulizo mara tatu, nayo hati hiyo huipata kwa Padre yule wa msikitii ule wa pili.*

¶ *Siku ilioagizwa kuwaaza wale wawili ikifika saa yake, yule atakayeo na yule atakayeolewa, huingga ndani ya msikitii pamoa na rafiki zao na jirani zao, wasimame pamoa wale wawili, yule mwanamume upande wa mkono wa kuume na yule mwanamke upande wa mkono wa kushoto : ndipo hunena yule Padre,*

ENYI mpendwao sana, tumekutana hapa mbele za Mwenyezi Mungu na mukutano huu, tupate kuwau-niganisha mwanamume huyu na mwanamke huyu katika Ndoa takatifu, nayo ni hali moja iliyowekwa na Mwenyezi Mungu zamani walipokuwa watu hawajafanya makosa, tena yatuonyesha ule umoja ulio wa siri alio nao Kristo na kanisa lake : nayo hali hiyo iliyotakatifu sana Kristo aliiheshimu na kuitia uzuri, kwa vile aliviyokwenda arusini yeze mwenyeewe, na kwa ishara yake ya kwanza aliyoitenda katika Kana ya Galilaya ; kisha yasifiwa hali hiyo na mtakatifu Paulo kuwa ni hali ya kuheshimiwa na

watu wote ; na kwa ajili ya hayo imekuwa haifai kujititia wala kuingia kwa upesi na pasipo kuifikiri wale wenyeewe, ili kutimiza tamaa na shauku zao za miili yao, wakawa mfano wa nyama wasiokuwa na akili. Basi waingiao na waingie kwa ustahivu, kwa busara na mashauri na kwa makini na kumcha Mungu, huku wayafikiri ni kwa maana gani haya yakawekwa na Mwenyezi Mungu haya mambo ya Ndoa.

Kwanza : yaliwekwa kwa maana ya kuzaa wana, wapate kulewa hao katika kicho cha Bwana na ulezi wake ; na kulivutia sifa jina lake lililo takatifu.

Pili : yaliwekwa ili yapate kuwa dawa ya dhambi, ili watu wapate kujitenga na uzinifu, na kwamba hao ambaio kwamba kile kipawa cha kujizua hawanacho wapate kuo, na kujiweka hali ya kuwa via visivyo na najisi vya mwili wa Kristo.

Tatu : yaliwekwa kwa ajili ya wenyeewe kufungamana na kusaidiana na kutunzana, kama ambavyo yampasa huyu kuvipata kwake huyu katika mambo ya maisha yao, katika kufanikiwa na katika shida : nao watu hawa wawili waliopo sasa wamekuja kuungamanishwa katika hali hiyo iliyotakatifu. Basi, akiwa mtu aweza kuonyesha sababu ya haki iwayo yote itakayowazuilia kuungamanishwa pamoa kwa halali, na aiseme sasa, au tokea sasa mielele anyamaze.

¶ *Kisha baadaye husema na wale watakaozwaa, akinena,*

MIMI nawaonya na kuwaamuru ninyi nyote wawili, kwa mtakavyohukumiwa katika siku kuu ya hukumu, ambayo ni ya kutisha sana, napo ndipo zitakapofunuliwa siri za miyo ya watu wote, ya kwamba, akiwa immoja katika ninyi wawili amejua kizuizi kitakachowazua ninyi wawili kuungamanishwa katika Ndoa kwa halali, muungame hivi sasa kizuizi hicho na kukifunua. Kwani jueni sana ya kwamba kadiri ya waungamanishwao kwa jinsi isivyoambiwa kuwa halali na Neno lake Mwenyezi Mungu, hawaungamanishwi watu hao na Mwenyezi Mungu, wala Ndoa zao si halali.

¶ Na siku ya ndoa hizo, akiwa mtu awaye yote yuashuhudia na kuonyesha kizuizi chochote, kitakachowazia kuungamanishwa katika ndoa kama ilivyoagizwa na sheria ya Mungu au ya Ufalmehu, naye mtu yule yu tayari kutoa dhamana na madhahimi wengine pamoja naye, ambaa ni wa kutosha katika hayo, kwaan watakaoana ; au aweke rahani kewa thamani iliyotimia ya gharama walizogharimishwa wale watakaoana, ili apate kuyathubutisha kuwa kweli ayashuhudiayo, ndipo hapo, yala-zimu kutaaarisha kule kuzipisha ndoa zao watu wawili wale, hata iishe kuangaliwa ile kweli.

¶ Na ikiwa hakikusemwa kizuizi kiwacho chote, ndipo hapo yule Padre humuuliza yule mtu mume,

EWE Fulani, umependa uwe naye mwanamke huyu, kuwa mkeo wa kumwoa, mwishi wewe naye kama maagizo ya Mwenyezi Mungu, katika hali takatifu ya Ndoa ? Utampenda, utamtuliza moyo wake, na kumstahi, na kumtunza, akiwa hawezi, akiwa mzima ; na wengine wote utawaepuka, ujiweke wewe kuwa na yeze muda wote mtakaokuwa hai pamoja duniani ?

¶ Yule mume hujibu,

Nakubali.

¶ Ndipo hapo yule Padre humuuliza yule mwanamke,

EWE Fulani, umependa uwe naye mtumume huyu kuwa mumeo wa kukoao, mwishi pamoja kama maagizo ya Mwenyezi Mungu katika hali takatifu ya Ndoa ? Utamtii na kumtumikia, utampenda na kumstahi na kumtunza, akiwa hawezi, akiwa mzima ; na wengine wote utawaepuka, ujiweke wewe kuwa naye muda wote mtakaokuwa hai pamoja duniani ?

¶ Yule mke hujibu,

Nakubali.

¶ Ndipo hapo yule Padre hunena,

Ni nani amtoaye mwanamke huyu ili kumwoza mume huyu ?

¶ Ndipo watakapoapiana yamini kama hivi : yule Padre humpoeke yule mwanamke mikononi mwa babaye, au rafikiye, na kumfanya yule mume, kwa mkono wake yeze wa kuume, amshike mkono wake wa kuume yule mwanamke, akimfunza kusema,

MIMI Fulani nakutwaa wewe Fulani kuwa mke wangu wa kukuo, niwe nawe nikushike toka hii siku ya leo, kwa wema kwa ubaya, kwa wingi wa mali kwa uchache wa vitu, katika ugonjwa katika afya, nikupende na kukutunza hata kufa, kama amri zake takatifu Mwenyezi Mungu. Nami kwa ajili ya neno hili nakupa yamini yangu.

¶ Ndipo hapo huachana mikono, kisha baadaye yule mwanamke kwa mkono wake wa kuume humshika yule mume mkono wake wa kuume, na kunena naye kwa kufuata yule Padre,

MIMI Fulani nakutwaa wewe Fulani kuwa mume wangu wa kunioa, niwe nawe nikushike toka hii siku ya leo, kwa wema kwa ubaya, kwa wingi wa mali kwa uchache wa vitu, katika ugonjwa katika afya, nikupende na kukutunza na kukutii hata kufa, kama amri zake takatifu Mwenyezi Mungu. Nami kwa ajili ya neno hili nakupa yamini yangu.

¶ Ndipo hapo huachana mikono mara ya pili, yule mume humpa yule mke pete, akiweke juu ya Chuo, pamoja na ada, kama walivyozeza kupewa Padre na katibu wake. Yule Padre akiisha kuitwaa ile pete humpa yule mume, yule mume apate kumvika yule mwanamke kidole cha nne cha mkono wa kushoto ; kisha yule mume huishika ile pete hapo, na kunena kwa kufunzwa na yule Padre,

MIMI kwa pete hii nakuoa, kwa mwili wangu naku-heshimu, nami nakupa vitu vyangu vyote vya duniani : kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

¶ Ndipo hapo yule mume huachaka ile pete katika kidole cha nne cha mkono wa kushoto wa yule mwanamke, kisha wakipiga magoti wote wawili, yule Padre hunena,

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho ; Muumba wa wanadamu wote ni wewe, nawe ndiwe mwenye kuwatunza ; wewe watupa kila neema ya rohoni ;

ndiwe mwenye kuanziza maisha yasiyo ukomo : uwatemshie baraka yako hawa watumishi wako, mtumume huyu na mwanamke huyu, ambao sisi twawaombea hivi kwa jina lako ; ili kwamba kama walivyoishi pamoja Isaka na Rebeka kwa uaminifu, watu hawa nao washike vivyo kuondoa na kutimiza yamini zao na maaganano walivyo-wekeana, ambayo pete hii walivopanana na kupokeana hivi ndiyo dalili yake na sahihi yake ; nao wadumu daima katika umoja wa mapenzi na amani vilivyotimia, waishi kwa kufuata sheria yako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ Ndipo hapo yule Padre huwashikamanisha mikono yao ya kuune, huyu na huyu, na kunena,

ALIOWAUNGAMANISHA Mwenyezi Mungu, bina-damu na asiwatenganishe.

¶ Ndipo hapo yule Padre husema na wale watu,

KWA maana ya kuwa *Fulani* na *Fulani* wamekubaliana katika Ndoa takatifu, nao neno hilo wamekiri mbele za Mwenyezi Mungu na mukutano huu, tena wamepanana yamini, wameapiana wenyeve kwa wenyeve, nayo wameiweka wazi na kuikiri mbele ya watu kwa kutoa na kupokea pete na kushikana mikono ; mimi nasemaha hawa ni mume na mkeve pamoja, kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. *Amina.*

¶ Yule Padre huongeza na maneno haya ya Baraka,

MUNGU Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu, na awabarikishe, awalinde na kuwaweka salama ; Bwana na awaangalie kwa rehema zake na kuwaneemesha, na kwa mtakavyojawa na baraka za rohoni na neema pia kwake yeye, muwe watu wa kukaa pamoja kwa wema katika maisha haya, wenyeve kwa wenyeve, hata katika ulimwengu ujao myapate maisha yasiyo mwisho. *Amina.*

¶ Ndipo hapo yule Padre au wale wenyewe daraja, hwenda katika Meza ya Bwana, na kunena au kuimba Zaburi hii inayofuatana hapa.

Beati Omnes. Zaburi 128

YUNA heri kila mtu amchaye Yehova : aendaye katika njia zake.

2. Taabu ya mikono yako hakika utaila : utakuwa na heri, na kwako kwema.

3. Mke wako atakuwa kama mzabibu uzaao vyumbani mwa nyumba yako : wanao kama vichipukizi nya mizeituni wakizunguka meza yako.

4. Hivyo ndivyo atakavyobarikiwa : mtu yule amchaye Yehova.

5. Yehova akubarikie toka Zayuni : upate kuyaona mema ya Yerusalem siku zote za maisha yako.

6. Naam, ukawaone wana wa wanao : amani na iwe juu ya Israeli.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

¶ Au Zaburi hii,

Deus Misereatur. Zaburi 67

MUNGU na atufanyie fadhili, atubarikie : na atufikizie nuru za uso wake kwetu :

2. Ili njia yako itamburikane juu ya nchi : wokofu wako ujulikane katika mataifa wote.

3. Watu na wakushukuru wewe, Mungu : watu wote pia na wakushukuru wewe.

4. Mataifa na wafurahi, waimbe kwa furaha : kwa kuwa wewe utawahukumu watu haki, utawaongoza mataifa walio duniani.

5. Watu na wakushukuru wewe, Mungu : watu wote pia na wakushukuru wewe.

6. Nchi na itoe mazao yake : Mungu, Mungu wetu, na atubarikie.

7. Mungu atatubarikia : ncha zote za dunia na zimche yeye.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Baada ya kwisha ile Zaburi, yule mtu na yule mke hupiga magoti mbele ya Meza ya Bwana, yule Padre husimama mbele ya Meza na kuvalakea, na kunena,

Bwana, uturehemu.

Huitika. Kristo, uturehemu.

Padre. Bwana uturehemu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribwi, Utuokoe maovuni. Amina.

Padre. Ewe Bwana, uwaokoe mtumwa wako na kijakazi chako,

Huitika. Waliokutumaini wewe.

Padre. Ewe Bwana, uwaletee msaada kutoka katika pahali patakatifu pako ;

Huitika. Uwalinde milele.

Padre. Uwe kwao ukuta wenye imara,

Huitika. Kuwakinga na uso wa adui zao.

Padre. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu ;

Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Padre. Ewe Mungu wa Iburahimu, nave u Mungu wa Isaka, tena u Mungu wa Yakobo, uwabarikie hawa watumishi wako ; nave uipande mbegu ya maisha ya milele miyoni mwao, ili watakalojifunza lolote katika Neno lako takatifu, walitimizie halisi. Nawe huko uliko mbinguni uwaangalie kwa wema uwabarikie. Nawe kama vile uliviyowateremshia baraka yako Iburahimu na Sara, kwa kuwatuliza sana, na hawa watumishi wako nao uwafadhilli kwa kuwateremshia baraka yako vivile ; hata,

kwa watakavyoyatii mapenzi yako wewe, na kukaa salama daima katika ulinzi wako, iwe wao kudumu mumo katika kupendana na wewe, hata maisha yao ya huku yaishe ; kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

I Sala hiyo ifuatanyayo huachwa awapo yule mwanamke si mtu wa kuchukua mimba tena.

EWE Bwana mwenye rehema, Babaetu wa mbinguni, ni kwa vipawa vyako vya neema binadamu waongezekavyo ; sisi twakuomba kwamba uwasaidie watu wawili hawa kwa kuwabarikia, hata iwe wao kuwa watu wa baraka katika kuzaa wana, nao wawe watu wa kukaa pamoja kwa kupendana kwa uaminifu, hata iwe wao kuwaona wana wao wenye kulewa katika imani ya Kristo na adili, kwa kukutukuza na kukuheshimu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, wewe kwa nguvu za uwezo wako ulifanya vitu vyote pasi kitu chochote ; tena, (baada ya kwisha kutengea yale mengine), ukaamuru kwa yule mtu mume Adamu (yule uliyemuumba kwa mfano wa sura zako wewe), ipatikane asili ya yule mwanamke, ikawa ndio mwanzo wake ; nave, kwa vile uliviyowauingamanisha wale wawili ukafunza kana kwamba hao uliokwisha kuwaungamanisha pamoja kwa ndoa, haitakuwa halali kuwatenganisha popote : ewe Mwenyezi Mungu, uliyetakasa hali hiyo ya ndoa ikawa ni siri tukufu sana kwa jinsi ambavyo ndani yake zimefananshwa na kufunuliwa ndoa na umoja vya rohoni, vilivyo kati yake Kristo na kanisa lake ; uwaangalie kwa rehema hawa watumishi wako, ili kwamba huyu mume ampende mkewe kwa mfano wa Neno lako (vivile kama Kristo alivyompenda mposwa wake, nalo ni kanisa, akajitoa mwenyewe kwa ajili yake, kwa kulipenda na kulilea, vivile kama mtu apendavyo mwili wake) ; tena na kwamba huyu mke naye awe mwenye kupenda na kupendeka, kwa uaminifu na usikizi, kwa mumewe, kwa kuwaandama watuwake wote wamchao Mungu, kwa utulivu na makini na imani.

Ewe Bwana, uwabarikie wao wote wawili, uwape na kuurithi ufalme wako wa milele, kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo hunena yule Padre,*

MWENYEZI Mungu, aliyewaumba hapo kwanza wazazi wetu wa asili, Adamu na Hawa, akawatakasa na kuwaungamanisha pamoja katika ndoa, na awamiminie juu yenu mali ya neema yake, awatakase na kuwabarikia, ili kwamba mpendekeze kwake, huku katika miili yenu na huku katika roho zenu, nanyi mwishi pamoja katika mapenzi matakatifu hata maisha yenu yaishe. *Amina.*

¶ *Baada ya kwisha sala hizi, ikikosekana hotuba ya kufunua yaliyowapasa mu na mkewe, yule Padre husoma haya :*

ENYI nyote mliongwa au kuolewa, au mlion na azima ya kuingia katika hali takatifu ya Ndoa, sikizeni yanenwayo na Maandiko matakatifu katika yaliyowapasa wale waume kwa wake wao, na wale wake kwa waume wao.

Mtakatifu Paulo katika Waraka wake aliovapelekea Waefeso, Mlango wa tano, yuawaagiza maagizo haya waume wote waliooa wake : Ninyi waume, wapendeni wake wenu, vivile kama Kristo naye aliviyolipenda kanisa, na kutoa nafsi yake kwa ajili yake : ili kwamba apate kulitenga, akiisha kulisafi kwa kuosha kwa maji katika neno, ili kwamba aipatie nafsi yake kanisa tukufu, lisilo na kipaku wala alama ya mkuto, wala neno lolote kama haya : lakini ya kwamba liwe takatifu pasipokuwa na aibu. Ni vivyo hivyo imewapasa watu waume nao kuwapenda wake wao kama vile *waipendawyo* miili yao wenye. Ampendaye mkewe huipenda nafsi yake : kwani hapana mtu aliyeichukia nyama ya mwili wake popote : lakini ni kuilisha na kuienga-engi, vivile kama Kristo naye *aliviyolitunza* kanisa : kwa kuwa sisi tu via vya mwili wake, vya nyama yake na vya mifupa yake. Kwa ajili ya hayo mtu atawaacha babaye na mamaye, naye ataambatana na mkewe, nao hao wawili watakuwa ni mwili mmoja. Siri hii ni *siri kuu* : ila mimi naleta habari ya Kristo na hilo kanisa. Pamoja na hayo, na

ninyi kila mtu nafsi yake na ampende mkewe mwenyeewe kama nafsi yake.

Naye yeyle mtakatifu Paulo, akiwaandikia Wakolosai anena hivi na waume wote waliooa ; Enyi waume, wapendeni wake wenu, msiwaonee machungu.

Msikizeni na aliyojanena mtakatifu Petero, mtume wake Kristo, naye ni mtu aliyeoa mke, awaambiapo waliooa : Nanyi waume, ni vivyo hivyo, ketini na *wake wenu* sawasawa ha kujua kwenu, kwa kumpa mwanamke heshima impasayo, kama chombo kilicho kinyonge zaidi ya *ninyi*, tena kama mlivyokuwa warithi pamoja wa neema ya uhai ; ili kwamba kuomba kwenu kusizuiliwe.

Haya mlipyasikia hivi ni yampasayo yule mume kwa mkewe. Basi nanyi wake kadhalika sikizeni yawapasayo kwa waume wenu, nayo yameonyeshwa wazi katika Maandiko matakatifu.

Mtakatifu Paulo katika Waraka ule ule aliovapelekea Waefeso tuliotaja huku mbele, huwafunza ninyi kama haya : Ninyi wake, *nyenyekeni* kwa waume wenu, kama vile kwa Bwana. Kwa kuwa mtu mume ni kichwa cha mwanamke, vivile kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa, mwenyeewe ni mwokozi wa mwili. Lakini kama kanisa liliviyomnyenyeka Kristo, ni vivyo hivyo na wanawake *wave* kwa waume wao katika mambo yote. Naye anena tena, Huyo mwanamke naye *na aangalie* ya kwamba amche mumewe. Naye katika Waraka wake aliovapelekea Wakolosai mtakatifu Paulo huwafunza haya yaliyo mafupi, Enyi wake, *nyenyekeni* kwa waume wenu, kama vifaavyo katika Bwana.

Mtakatifu Petero naye huwafunza vyema sana anenapo kama haya : Enyi wanawake, jiwekeni nafsi zenu chini ya waume wenu wenyeewe ; ili kwamba, ikiwa wengine wako wasiolitii hilo neno, wapatikane kwa njia ya miendo ya hao wake wao, pasipokuwa na lile neno ; wakiutunza kwa macho yao ule mwendo wenu ulio safi, ulio wa hofu. Ambao, *kujipamba kwenu* kusiwe kule *kujipamba* kwa nje kwa kusongea nywele, na kuvala vyombo vya dhahabu, au kujivika nguo ; lakini na kuwe mtu aliyejichamana wa moyoni, katika *mavao* hayo yasiyoharibika, maana, ni

TARATIBU YA NDOA

yale ya roho ya upole na utulivu, *roho ambayo mbele za Mwenyezi Mungu ina thamani kuu.* -Kwani hao wanawake watakatifu nao hapo kale, hao waliotumaini kwa Mungu, ndivyo walivyozipamba nafsi zao, na kunyenyeka kwa waume wao wenywewe : kama Sara alivyomtii Iburahimî, akimwita bwana : nanyi mu watoto wake huyo, mkifanya yaliyo mema, nanyi hamtishwi kwa hofu yoyote.

¶ Yafaa, wale walivoana upya washirikiane Ushirika Mtakatifu zamani za kuoaa, au mara watakapowahi baada ya kuoana.

¶ Kama hapana Ushirika Mtakatifu wala hotuba ya kuonyeshya yawapasayo mume na mkeve, na lisomiwe fungu la Maandiko matakatifu ; au yule Padre aseme maonyo yaliyo karika Chuo cha Sala cha tangu hapo. Ndipo yule Padre huwafumua wale watu walioikutamika, akisema,

Na tuombe.

EWE Bwana Mwenyezi Mungu, Mungu wa milele, Etwakuomba uone vyema kutuongoza, na kututakasa, na kututawala, mioyo yetu na miili yetu, katika njia za sheria zako, na katika kazi za maagizo yako ; ili kwa kulindwa na wewe kwa nguvu zote, hapa na hata mirele, tuhifadhike miili yetu na roho zetu, kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

BARAKA ya Mungu, Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, iwe mwenu, ikae kwenu daima. *Amina.*

TARATIBU YA KUWAANGALIA
WAGONJWA

¶ Mtu atakapokuwa hawezi, hupewa habari yule Padre wa mipaka ya msikitî ule ; naye aktiisha kuungia nyumbani kwa yule aliye hawezi, hunena,

A MANI na iwe juu ya nyumba hii na wote wakao humu.

¶ Aktiisha kupata kwa yule aliye hawezi, hupiga magoti na kunena,

USIKUMBUKE makosa yetu, ewe Bwana, wala makosa ya babazetu ; wala usitwae kisasi cha madhambi yetu ; utusamehe, Bwana mwema, utusamehe watu wako, uliowakomboa kwa damu yako ya thamani, wala usitukasirikie mielele.

Huitika. Utusamehe, Bwana mwema.

¶ Ndipo hapo yule Padre hunena,

Na tuombe.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, **U**sfalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kutotosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. *Amina.*

Padre. Ewe Bwana, umwokoe mtumishi wako,
Huitika. Akutumainiye.

Padre. Umletee msaada utoke pahali patakatifu pako ;

Huitika. Umlinde mirele kwa uwemo mkuu.

Padre. Yule adui na asipate nafasi kwake

Huitika. Wala asimkaribie na kumdhuru yule mtu mwovu.

Padre. Ewe Bwana, uwe kwake ukuta ulio imara ;
Huitika. Kumkinga na uso wa adui wake .
Padre. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu ;
Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Padre

EWE Bwana, utuangalie huko uliko mbinguni, nawe Umtazame huyo mtumishi wako, umwangalie kwa kumsaidia ; nawe umwonee huruma, umpe kutua moyo na kutumaini kwako wewe ; umkinge na shari la adui, nawe umweke daima katika raha na salama : kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

UTUSIKIZE, ewe Mungu, Mweza-wa-yote, Mwenye rehemza zisizo kifani, Mwokozi wetu, umsongezee wema huyu mtumishi wako kama mazoea yako, ambaye yu katika kusumbuka kwa maradhi. Nawe umtakase kwa hivi umtiavyo adabu kwa mkono wako wa ubaba, ili kwamba kwa hivyo ajionavyo kuwa hana nguvu, aongezeka nguvu katika imani yake, zaidi na toba yake aliyotubu izidi kuwa ya maana ; ili kwamba wewe upendapo kumrejeza ile hali ya afya ya siku zote, awe kuyapisha maisha yake yaliyosalia katika kukucha wewe na kuktukiza : au, umpe neema ayakubali hayo uliyompiga, ili kwamba, baada ya kwisha kukoma maisha haya ya mashaka, awe mtu wa kuishi milele pamoja nawe katika maisha yasiyo ukomo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo hapo yule Padre humwonya yule aliye hawesi, kwa kusema kama haya :*

EWE mpenzi, neno hili juu sana, ya kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Bwana wa maisha na wa kufa, na yaliyohusika nayo yote, nayo ni ujana, nguvu, afya, uzee, unyonge, ugonjwa. Basi maradhi yako yawayo yote, neno hili moja fahamu sana, ya kuwa ni amri ya Mungu. Na sababu yake iwayo yote hata ukapatikana na mateso haya ; ikiwa ni kutaka kukujaribu ulivyo na uvumiliu ili kuwaonya wenzio, na kuonekana wazi imani yako uliyo nayo, ionekane katika siku ya Bwana kuwa ni

imani ya kusifiwa na kutukuzwa na kuheshimiwa, kwa kuzidi utukufu na hali njema isiyo ukomo ; au ikiwa unaletewa kwa kukurudi na kikutua adabu kwa mambo yako yachukizayo machoni mwake Babaako wa mbinguni : lakini, juu hakika ya kwamba ukitubia kwa madhambi yako toba ya kweli, nawe ukistahimili ugonjwa wako kwa uvumiliu, kwa kutegemea kwa rehema zake Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Yesu Kristo Mwanawele mpenzi wake, na kumshukuru miguuni pake kwa hivyo alivyokurudi kwa mkono wake wa ubaba, kwa kujinyenyekenza kabisa chini ya mapenzi yake : amri hii itageuka iwe faida, nayo itakusongeza mbele katika hiyo njia njema ifikishayo kwenye uzima wa milele.

¶ *Na akiba hawesi sana yule aendewaye, yule Padre na asimsomee zaidi katika maonyo yake ; ila yule awezapo, huendelea mbele kunena,*

BASI wewe uwe radhi kwa kurudiwa kwako na Bwana, kwani ni kama vile anenavyo mtakatifu Paulo, Waraka wa Wahibirania, Mlango wa kumi na mbili ; Huyo ambaye Bwana ampenda humrudi, naye humpiga kila mwana amkubaliye. Ni kwa ajili ya kurudiwa *kwenu* mwavumilia ; Mwenyezi Mungu awatendea kama wana ; kwani ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye ? Basi kwamba hamna kurudiwa, na watu wote wameshiriki *kurudiwa*, hapo ndipo mmekuwa wana-wa-haramu, si wana-wa-halali. Na hayo yote, tulikuwa na baba zetu za mwili kururudi, nasi tuliwastahi : je, hatutajiweka afadhalii sana chini yake yeeye Baba wa roho zetu, tuwe hai ? Kwani wao kweli siku chache waliturudi kama walivyoo na vyema wenye ; ila yeeye kwa kutufaa, tuplicate kutwaa sehemu ya utakatifu wake.

Maneno haya, ewe ndugu yangu, yameandikwa katika Chuo kitakatifu kwa kutufariji roho zetu na kutufunza, ili kwamba tuvumili kwa saburi na shukrani turudiwapo na Babaetu wa mbinguni, kila apendapo kwa wema wake wenye neema kuturudi hivyo. Wala halipatikani neno la pili, la kuwafariji Wakristo miyo yao, kama hilo la kulinganishwa kwao na Kristo, watakaposubirishwa miyo yao kwa kuvumilia misiba na mashaka na maradhi. Kwani

ye ye mwenyewe hakupaa juu kwenda furahani kwake, ili alipokwisha kupatikana kwanza na maumivu na mateso ; hakuungia utukufuni mwake kabla ya kuteseka kwake msalabani. Nasi hakika yetu ni vivyo ; tutesekavyo pamoja na Kristo imekuwa ndio njia yetu ya kuingia katika furaha ya milele ; na tufavyo kufa kwa furaha pamoja na Kristo, imekuwa ndio mlango wetu wa kuingia katika maisha ya milele ; ili kwamba tuwe watu wa kufufuka kutoka kwa wafu, kwenda kuketi pamoja naye katika maisha yasiyo ukomo. Haya basi, huu ugonjwa wako ulivyo na manufaa kwako, mimi nakusihi uupokee kwa uvumilivu na upole, tena nakunasihi kwa jina lake Mwenyezi Mungu, uyakumbuke uliyoyakiri kwa Mwenyezi Mungu zamani za kubatizwa kwako. Na kwa maana ya tusiviyokuwa na budi ya kutozwa hesabu ya maisha haya na yule Mwamuzi wa haki, yule ambaye imepasa watu wote kuamuliwa mbele zake pasipo kuangaliwa uso wa mtu awaye yote ; mimi kwa ajili ya hayo naukambia hivi sasa uangalie nafsi yako na hali yako, ulivyokaa mbele za Mwenyezi Mungu na mbele ya watu ; ili kwamba kwa kujishtaki mwenyewe na kujihukumu na kujilaumu kwa makosa uliyoyakosa, upate rehema mikononi mwa Babaetu wa mbinguni kwa ajili yake Kristo, usije ukashtakiwa na kulaumiwa katika hukumu ya siku ile ya utisho. Basi mimi nitakutajia Sharti za Imani yetu, upate kujijua, wayaamini yampasayo mtu wa Kikristo, au huyaamini.

¶ Ndipo hapo yule Padre huzitaja Sharti za Imani kwa kunena ; JE, wewe waamini kwa Mwenyezi Mungu Baba, Miumba mbingu na nchi ?

Na kwa Yesu Kristo, Mwanawе Mzaliwa pekee, Bwana wetu ? Na ya kuwa alitungishwa mimba na Roho Mtakatifu, akazaliwa na Mwanamwali Mariamu ; tena kuwa aliteswa katika enzi ya Pontio Pilato ; akasalibiwa, akafa, akazikwa ; kisha alishuka akaingia kuzimu, hata kwa siku ya tatu akasimama tena, ametoka kwa wafu ; kisha alipaa akaingia na mbinguni ; tena amekaa upande wa mkonu wa kuume wa Mwenyezi Mungu Baba ; naye

kutoka huko atakuja tena, katika mwisho wa ulimwengu, apate kuwaamua walio hai haja walio kufa ?

Nawe waamini kwa Roho Mtakatifu ; Kanisa takatifu lililo ulimwenguni mote ; Ushirika wa watakatifu ; Madhambi kusamehewa ; Mwili kufufuka ; na Maisha ya milele baada ya mauti ?

**¶ Yule aliye hawezi hujibu,
Haya yote ninakubali sana kuyaamini.**

¶ Ndipo hapo yule Padre hupeleleza katika kutubia kwake kwa makosa yake, kumwangalia kwamba ametubu kweli, na kwamba yu katika mapendano na watu wote wa ulimwenguni, naye humwonya ya kuwasamehe kwa ndani ya moyo wake watu wote kadiri ya walionienda uoru. Na kwamba amemtenda mwenziwe awaye yote uoru, humwonya ya kumtaka msanaha ; na kwa kila alilomkosa mtu au kundhilimi, humwambia amrudishie kila mmoja kadiri ya awezaevo. Na kwamba kabla ya wakati huo hajausia vitu vyake vifanyweje, na aonywe kuandika hati ya kuwarithisha watakaomrithi, na kuyaweka wazi madeni aliyo mayo, aviwayo, au avivyo yeye, ili kuusaji sawasawa moyo wake mwenyewe na kuwastarehesha mawasii watakaogawanya mali yake yatakorithishwa. Nao imewopasa watu kukumbushwa mara kwa mara ya kuusia vitu vyao vya duniani kwa kutengeza urithi wake wakali na afya na uzima.

¶ Moneno hayo yaliyokwisha kutajwa, huseme ka kwanza asijasali yule Padre, kama aonavyo kupasa.

¶ Yule Padre na asiache kuwaonya sana wagonjwa hao awaonaо kuwa wawea, ili wapate kuwapa maskini kwa ukarimu.

¶ Wakati huu yule mgonjwa huonywa ya kuungama madhambi yake, kwamba ajiona amelemeva moyo wake na neno lililo zito kwake lolote, naye baada ya kule kuungama hupewa msamaha na yule Padre (akiwa yuataka kama hayo kwa kupenda na kunya-nyekeed) kwa kunena kama haya,

BWANA wetu Yesu Kristo, aliyeliachia kanisa lake Amri kuwapa msamaha wa madhambi yao wenye dhambi wote watubuo kweli, na kuamini kwake, kwa rehema zake zilizo kuu na akusamehe makosa yako. Nami kwa amri yake niliyowekewa juu yangu, nakupa msamaha wa madhambi yako yote, kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

¶ Ndipo hapo yule Padre huisoma sala hii ;

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, rehema zako ni nyingi sana, Enawe kwa wingi wa hizo rehema wawaondolea ma dhambi yao hao watubuo kweli, hata umekuwa huyakumbuki kamwe ; umwangalie kwa huruma huyu mtumishi wako, atakaye sasa msamaha na ondoleo la madhambi. Nawe Baba uliye mwangi wa kupenda, mrejezee upya yaliyoharibika ndani yake, kwa udanganyifu na uovo wa Shetani, au kwa mapenzi yake ya mwilini na ule unyonge wake alio nao ; kia hiki kilicho hakiwezi ukiponye nawe ukidumishe katika umoja wa kanisa ; umwangalie alivyopondeka moyo, umkubalie machozi yake, umpunuguze maumivu yake, kwa hivyo utakavyoona ni vya kumfaa. Nawe kwa maana ya alivyozitumainia rehema zako, hizo tu, usimhesabie makosa yake ya tangu hapo, bali umtie nguvu kwa Roho wako Mwenye-baraka ; hata utakapopenda kumwondoaa huku, uwe kumchukua hata kwenye radhi yako, kwa alivyostahili Mwanayo umpendaye sana, Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

¶ Ndipo hapo yule Padre husoma Zaburi hii :

In te, Domine, speravi. Zaburi 71

NIMEKUKIMBILIA wewe, ewe Yehova : nisiaibike milele.

2. Kwa haki yako uniponye, uniopoe : unitegee sikio lako, uniokoe.

3. Uwe kwangu mwamba wa makazi yangu nitakakkowenda siku zote ; umeamuru niokolewe ; ndiwe genge langu na ngome yangu.

4. Ewe Mungu wangu uniopoe katika mkono wa mtu asiyehaki : katika mkono wa mtu mwovu, dhalimu.

5. Kwani ndiwe taraja langu, ewe Bwana Yehova : tumaini langu tokea ujana wangu.

6. Nimekutegermea wewe tangu kuzaliwa, ndiwe uliyenitoa tumboni mwa mama yangu : nitakusifu wewe daima.

7. Nimekuwa kitu cha ajabu kwa watu wengi : na wewe ndiwe kimbilio langu la nguvu.

8. Kinywa changu kitajazwa kwa sifa zako : na kwa heshima yako mchana kuchwa.

9. Usinitupe wakati wa uzee : nguvu zangu zipungukapo usiniache.

10. Kwa maana adui zangu wananiamba : na wanaonotea nafsi yangu hufanya shauri pamoja.

11. Wakisema, Mungu amewmawacha : mfuatieni mkamateni, hakuna wa kumponya.

12. Ewe Mungu, usiwe mbali nami : ewe Mungu wangu, ufanye haraka kunisiaidia.

13. Waabitshwe, watoweshwe adui za nafsi yangu : wavikwe laumu na fedheha wanaonitakia mabaya.

14. Nami nitatumaini daima : nitazidi kuongeza sifa zako zote.

15. Kinywa changu kitasimulia haki yako : na wokofu wako mchana kuchwa, kwani sijui hesabu yake.

16. Nitakuja na mambo ya ajabu ya Bwana Yehova : nitataja haki yako wewe peke yako.

17. Ewe Mungu, umenifundisha tokea ujana wangu : nimekuwa nikitangaza miujiza yako hata hivi leo.

18. Na hata sasa nikiwa mzee mwenzye mvi, usiniache, ewe Mungu : hata njishe kuwaeleza watu wa kizazi hiki nguvu zako ; na kila atakayekuja uwezo wako.

19. Na haki yako, ewe Mungu, imefika juu sana : wewe uliyefanya mambo makuu ; ewe Mungu, ni nani aliyekama wewe ?

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

¶ Na huku aongeza maneno haya,

EWE Mwokozi wa ulimwengu, wewe ambaye kwa Msalaba wako na Damu yako ya thamani ulitukomboa, utuokoe utuletee msaada, twakuomba miguuni pako, ewe Bwana.

¶ Ndipo hapo hunena yule Padre,

BWANA, ambaye ndiye Mweza-wa-yote naye ni ngome ilio imara sana kwa wote hao wamtumainio, naye kwake vitu vyote vya mbinguni na vya duniani na vya chini ya dunia humsujudia na kumtii ; basi Bwana huyo na awe ulinzi wako wewe, hivi sasa na milele, na akupe kujua na kufahamu neno hili, ya kwamba hakuna tena jina jingine chini ya mbingu, walilopewa wanadamu, ambalo mumo wapata kupokea afya na wokofu, ila jina lake Bwana wetu, Yesu Kristo, hilo tu. Amina.

¶ Kisha baadaye hunena,

T'WAKUTIA katika rehema na ulinzi alizotufadhilli Mwenyezi Mungu : Bwana na akubarikie akulinde. Bwana na akukunjulie uso wake akuneemeshe : Bwana na akuinulie uso wake akupe na salama, sasa, na milele. Amina.

Sala ya kumwombea mtoto aliye hawez

EWE Mungu Mweza-wa-yote, Baba mwenye rehema, Ekwamba ni kuishi kwamba ni kufa pia yana wewe pekeo ; sisi tu miguuni pako twakuomba huko uliko mbinguni umwangalie kwa rehema mtoto huyu, amelala hapa kitandani ali hali ni mgonjwa : umwangalie kwa wokofu wako, Bwana ; nawe kwa majira uyaonayo yatafaa umponye na maumivu yake ya mwilini, uiokoe roho yake kwa ajili ya rehema zako : ili kwamba (utakapopenda kuzifanya nyingi siku zake za humu ulimwenguni) aishi katika kukulekea wewe, kisha awe chombo cha kuonyesha utukufu wako, kwa kukutumikia kwa uaminifu na kufanya ambayo yatautia faida zamani zake. Au, umkaribishe katika hayo maskani ya mbinguni zikaamo roho zao waliolala katika Bwana Yesu, hali ya raha na furaha za milele. Nawe utupe haya, Bwana, kwa ajili ya rehema zako, kwa ye ye Mwanayo Bwana wetu, Yesu Kristo, aishiye na kutawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele. Amina.

Sala ya kumwombea aliye hawez, amwonapo kwamba hatapoa

EWE Baba wa rehema, Mungu wa utilizi wote, Msada wetu kila wakati wa dhiki ni wewe pekeo ; tumekukimbia wewe kwa kukuomba kwa ajili ya huyu mtumishi wako, ali hali amelala hapa chini ya mkono wako na unyonge mwingi wa mwilini. Umtulizie macho yako ya rehema, ewe Bwana : na kama utakavyoharibika mwili, nawe uzidi kumpa nguvu, kwa neema yako na Roho wako Mtakatifu, katika nafsi yake ya ndani. Nawe umpe kutubia toba isiyo shaka ya makosa yote ya maisha yake yaliyopita, na imani iliyokaza katika Mwanayo Yesu ; ili kwamba dhambi zake ziondolewe kwa rehema yako, naye apigiwe muhuri wa msamaha wake mbinguni, kabla asijaondoka huku akawa kutoonekana tena kwetu. Tumejua, Bwana, ya kwamba hakuna neno kwako wewe lisilowezekana, na ya kuwa hata hivi waweza kumwinua ukamrejeza afya, ukiwa wapenda, apate kwendelea katika kukaa mwetu ; ila, pamoja na haya, kwa maana ya kuwa aonekana kuwa amekaribia kuingia katika kufariki, twataka kwako ya kumtengeza na kumweka tayari kwa saa ya kufa, hata iwe, baada ya kuondoka kwake huku na amani yako na neema, kuwa roho yake yakaribishwa katika ufalme wako usio mwisho ; kwa kustahili kwake na uombezi wake Mwanayo pekee, Bwana wetu, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

SALA ya kuiombea roho ya mtu aliye hawez, katika muda wa kufariki kwake

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, zaishi kwako wewe Eroho za wenye haki waliokamilika baada ya kwisha kufunguka hivyo vifungo vya duniani : basi sisi tulio hapa miguuni pako twaitia roho yake huyu ndugu yetu tumpendaye katika mikono yako wewe, nayo ndiyo mikono ya Muumba aliye mwaminifu, mikono ya Mwokozi aliye mwingi wa rehema ; na huku twataka kwako iwe ya thamani machoni mwako roho hii. Twakuomba uioshe katika damu ya yule Mwana-wa-kondoo asiye kosa, aliyechinjwa kwa kuondoa dhambi za ulimwengu, ili kwamba yangawaje hayo mambo ya unajisi

yaliyoipata ili humu katika ulimwengu huu dhaifu na upotofu, kwa tamaa za mwili au udanganyifu wa Shetani, lakini (kwa kutakaswa na kuondolewa hizo zote) iwe kuletwa mbele zako wewe hali ya kutakata pasipo kipaku kiwachcho chote. Na sisi tuliosalia hali tuli munu katika mambo haya ya mauti yaliyo machoni mwetu kila siku, utufunze kujijua hali yetu wenyewe tulivyo wanyonge, na tulivyo watu tusiojua siku zetu zilivyo, utufunze na kuzihesabu siku zetu sana, hata tuwe kuitia miyo yetu katika hekimahiylo takatifu ya mbinguni, siku zote tuishizo hapa; nayo hekimahiylo ndiyo itakayotusongeza hatima yake katika maisha yasiyo mwisho ; kwa fadhilli zake na kustahili kwake Mwanayo pekee, Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

*Sala ya kuwaombea hao wasumbukao katika miyo
yao au dhamiri zao*

EWE Bwana Mwenye-baraka, wewe ndiwe Baba wa Elkila rehema, nawe u Mungu wa utilizi wote ; twataka kwako umwangalie kwa huruma na rehema huyu mtumishi wako atesekaye. Wewe umemwandikia machungu, nawe u katika kumkumbusha viovu vyake vya tangu hapo : ghadhabu zako zimekaza kumlemea ; nafsi yake nayo imejaa huzuni ; lakini wewe, ewe Mungu mwenye rehema, uliyeadhika Neno lako kwa ajili ya kutusunza sisi, ili kwamba kwa vile tutakavyopata uvumilivu na utilivu mumo katika Maandiko yako matakatifu, tupate taraji na matumaini ; umpe mtu huyu fahamu za kujua nafsi yake sawasawa, tena kuufahamu sawasawa utisho wako na ahadi zako ; asije akatupa tumaini lake alilo nalo kwako, wala asiliweke pahali pengine isipokuwa kwako wewe. Umpe nguvu za kujizua na majaribu ajaribwayo yote, nawe umpoze magonjwa yake yote. Huu mwanzo uliopondeka usiuvunjue, hii katani ifukayo moshi usiizime. Wala usizue huruma zako za ndani kwa kasirani ; bali msikizishe mtu huyu ya furaha na nderemo, ili kwamba mifupa uliyovinjua ipate kufurahi. Umwokoe na utisho wa adui, umwinulie na mwanga wa uso wako, umpe raha na amani, kwa kustahili kwake na uombezi wake Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

WALIO HAWAWEZI KUWASONGEZEZA USHIRIKA

¶ *Kwa maana ya kuwamo wanadamu wote katika hatari aina nyingi, na magonjwa na maradhi mengine mengine ya ghafula, na kule kuhaa kwao kila mmojawapo hali hajui wakati wake atakao-fariki dunia ; kwa ajili ya hayo, ili kwamba kuwaacha wakaka tarayi daima, wali hali ipasayo katika kufariki, pindi Mwenyezi Mungu atakapoonaa vyema kuwaita, wale Mapadre na wafanye bidii mara kwa mara kuwaonya walio mipakanii mwa kila msikitii, kwamba warae katika kuupokea mara kwa mara Ushirika Mtakatifu wa Mwili na Damu vyake Mwokozi wetu Kristo, utakaposongezwa mbele ya watu msikitini ; ili wafanyaapo kama hayo, wakikutwa na neno la ghafula wapungue kusumbuka, uwapo Ushirika huo haapatikani. Lakini akiba yule mgonjwa hawezi kwenda msikitini, naye yuataka kuupokea Ushirika kwake nyumbani ; ndipo hapo yule mgonjwa humpa habari yule Padre na mapema, na kumjuvya hesabu ya hao ambaa watashirikiana pamoja naye, ni watu wangapi (nao hawapungu) watu watatu hesabu yao, au uchache ni wawili) ; na akipata pahali nyumbani mwake yule atiye hawezi, ambapo hu'aa kwa haja ile, pamoja na vitu vyote vitakwavyo, vimentenga sawasawa, hata apate yule Padre kuusongezwa kwa heshima ule Ushirika ; basi pahali hapo yeeye hufanya Ushirika Mtakatifu, kwa kusoma mbele Sala hii na Waraka huu na Injili hii :*

Sala

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, Mkazi wa milele, Muumba wa binadamu, ndiwe mwenye kuwarudi uwapendao, na kumtia adabu kila mtu umkubaliye ; twaomba sana umrehemu huyu mtumishi wako, uliyemrudi kwa mkono wako, umpe kustahimili huu ugonjwa wake kwa uvumilivu, arejee afya yake ya mwilini, kwamba ndiyo mapenzi yako ya neema, naye atakapokuwa mwili kutokwa na roho yake, iwe hiyo kusongezwa pasipo kosa kwako wewe : kwa Bwana wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

Waraka. Wahibirania 12. 5-6

MWANANGU, usione kuwa ni kudogo kurudiwa kwa Bwana, wala usizime moyo ukikaripiwa naye ; kwani huyo ambaye Bwana ampenda humrudi, naye humpiga kila mwana amkubaliye.

Injili. Yohana 5. 24

NI kweli, ni kweli, nawaambia ya kwaniba, mwenye kusikia neno langu, na kumwamini aliyenileta, yuna uzima wa milele, wala haingii katika hukumu, ila amekwisha kupita kutoka mautini kuingia uzimaní.

¶ *Kisha baadaye yule Kasisi huendelea kusoma kwa kuifuata kawaida iliyokwisha kuagizwa ya Ushirika Mtakatifu, naye huanza penye maneno haya, Ninyi mtubiao kwa dhambi zenu kwa kweli (w.k.).*

¶ *Hata muda wa kuugawanya ule Ushirika Mtakatifu, yule Kasisi huanza kwa kuipokea Ushirika Mtakatifu nafsi yake, kisha baadaye huwasongezea wao waliowekwa kuwa watu wa kushirikiana na aliye hawezí; hatima yake humsongezea yule mtu aliye hawezí.*

¶ *Lakini akipatikana mtu, ambaye kwa ulivyo kwenda mno ule ugonjwa wake, au kwa kukosekana neno lolote, kwamba ni kuto-mwambia mbele sawasawa yule Kasisi, kwamba ni kutopata kikao cha watu ambao watashirikiana naye, kwamba ni kizuzi cha haki kingine kiwachó chote, haupokei Ushirika wa Mwili na Damu vyake Kristo; hapo ndipo yule Kasisi humweleza ya kwamba atubia po kueli yale madhambi yake, na kukaza kuamini ya kuwa Yesu Kristo amepatikana na mauti juu ya msalaba kwa ajili yake, hata ametokwa na damu yake nayo kwa kumkombo, naye ayakumbukapo kwa bidii manusaa aliyoypata karika hayo, akawa na kumshukuru shukran za moyoni kwa ajili ya hayo; mambo haya ayafanyapo yule mgonjwa, na aje kuwa huku ndiko kula na kunyanya Mwili na Damu vyake Mwokozi wetu kwa kufaa, nako huivutia afya roho yake, na angawa haupokei ule Ushirika midomoni mwake.*

¶ *Na yule mgonjwa akiangaliwa, naye wakati uo huo akaipokea Ushirika Mtakatifu, ndipo hapo yule Kasisi, kwa ajili ya kufupiza mambo kwa kuyaendeleza kwa upesi zaidi, humaliza ile kawaida kabla asijasoma Zaburi ya Nimekukimbia wewe, ewe Yehova, na kwendelea mara kuusoma Ushirika.*

¶ *Na zamani za tauni au maradhi, au zamani nyiningine kama hizo, za wito wa maradhini au magonjwani, pasipapatikaná mióngoni mwa watu wa mipaka ya misikití mle wala jírani, watu ambao wataka kushirikanishwa na walio hawavezi nyumbani mwao, kwa ajili ya kuchelea kupatikana na wito, atakawapo yule Kasisi na yule mwenye maradhi hayo, huweza kushirikiana naye yeye pekee.*

TARATIBU YA KUZIKA MAITI

¶ *Hapa ni kuangaliwa kwamba Taratibu hii haitumiwi kwa kuzika waliokufa hawajabatizwa, wawao wote, wala waliopigwa marufku ya kanisa, wala waliojiua wenyeewe.*

¶ *Yule Padre na makatibu humwendea yule maiti na kukutana naye langoni pa uwanda wa mazishi, huntangulia, kwamba ni kuingia msikitiri, kwamba ni kwenda upande wa kaburi lake, huku wanena (au kuumba),*

YESU akamwambia, Mimi ndimi huko kufufuliwa, nami ndimi maisha. Aaminiye kwangu ajapokuwa amekufa, ataishi. Na kila mtu aishiye na kuamini kwangu, hafi milele.

Yohana 11. 25-26.

MIMI najua ya kuwa Mkombozi wangu yu hai, na mwisho atasimama juu ya nchi: hata ngovi yangu itakapokwisha kuharibika hivi, pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mwenyezi Mungu: naye nitamwona nafsi yangu, tena macho yangu yatamwangalia, wala si kana mgeni.

Ayubu 19. 25-27.

KWANI hatukuingia na kitu ndani ya ulimwengu, kwa kuwa hata kutoka na kitu hatuwezi.

i Timotheo 6. 7.

YEHOVA alitoa, na Yehova ametwaa; jina la Yehova na libarikiwe.

Ayubu 1. 21.

¶ *Hata wakiisña kuingia ndani ya misikití, husomwa Zaburi hizi mojawapo, au zote mbili.*

Dixi custodiam. Zaburi 39

NILISEMA, Nitazitunza njia zangu, nisije nikakosa kwa ulimi wangu: nitazuia kinywa changu kwa ukanda, akiwapo mbele yangu yule mbaya.

2. Nilikuwa sisemi, nilinyamaa kimya, nisitamke hata neno jema: maumivu yangu yakazidi.

3. Moyo wangu ukawa moto ndani yangu, na katika

kuwaza kwangu moto ukawaka : nilisema kwa ulimi wangu.

4. Ewe Yehova, unijulishe mwisho wangu, na kiasi cha siku zangu ni kiasi gani : njue jinsi nilivyo dhaifu.

5. Tazama, umefanya siku zangu kuwa mashubiri, maisha yangu kama si kitu mbele zako : ubatili tu ni kila mwanadamu ingawa amesitawi.

6. Binadamu huenda tu huko na huko kama kivuli, hufanya ghasia tu kwa ajili ya ubatili : huweka akiba wala hajui ni nani atakayeichukua.

7. Na sasa ninangojea nini, ewe Yehova : matumaini yangu ni kwako.

8. Uniokoe na maasi yangu yote : usinifanye laumu ya wapumbavu.

9. Nilinyamaza sikufumbua kinywa changu : kwani wewe ndiwe uliyefanya.

10. Uniondolee pigo lako : kwa uadui wa mkono wako nimeangamia.

11. Ukimrudi mtu kwa kumkemea kwa ajili ya uovu wake, watowesha uzuri wake kama nondo : ubatili tu ni kila mwanadamu.

12. Usikie maombi yangu, ewe Yehova ; utege sikio lako niliapo, usiyanyamalie machozi yangu : kwa maana mimi ni mgeni wako, msafiri kama baba zangu wote.

13. Uniachilie nipate nafuu : kabla siajondoka nisiwepo tena.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Domine refugium. Zaburi 90

EWE Bwana, wewe umekuwa makao yetu : kizazi baada ya kizazi.

2. Kabla hajazaliwa milima, kabla hujaiumba dunia : na tangu milele hata milele ndiwe Mungu.

3. Wamrudisha mtu mavumbini : ukisema, Rudini, enyi wanadamu.

4. Kwani miaka elfu machoni pako ni kama siku ya jana ikiisha kupita : na kama kesha la usiku.

5. Wawagharikisha, huwa kama usingizi : asubuhi wa kama majani yameayo.

6. Asubuhi yachipuka na kumea : jioni yakatika na kukauka.

7. Kwani tumetoweshwa kwa hasira yako : na kwa ghadhabu yako tumefadaishwa.

8. Umeyaweka maovu yetu mbele zako : siri zetu katika mwanga wa uso wako.

9. Kwani siku zetu zote zimepita katika hasira yako : tumetoweshwa miaka yetu karna hadithi.

10. Siku za miaka yetu ni miaka sabuini, na ikiwa tuna nguvu miaka themanini : kiburi chake ni taabu na ubatili, kwani chapita upesi tukatokomea mara.

11. Ni nani aujuaye uwezo wa hasira yako : na ghadhabu yako kiasi cha kicho kilicho haki yako ?

12. Basi utujulishe kuzihesabu siku zetu : tujipatie moyo wa hekima.

13. Urudi, ewe Yehova ; hata lini ? uwahurumie watumishi wako.

14. Utushibishe asubuhi kwa fadhili zako : nasi tutashangiria na kufurahi siku zetu zote.

15. Utufurahishe kwa kadiri ya siku ulizotutesa : kama miaka ile tulioona mabaya.

16. Matendo yako na yaonekane kwa watumishi wako : na adhama yako kwa watoto wao.

17. Na uzuri wa Yehova Mungu wetu uwe juu yetu : na kazi ya mikono yetu utufanyie thabiti, naam, kazi ya mikono yetu uifanye thabiti.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ Ndipo hapo hufuatana lile Somo, limetwaliwa katika Waraka wa kwanza wa mtakatifu Paulo aliowaandikia Wakorintho, Mlango wa kumi na tano.

I Wakorintho 15. 20-58

ILA sasa Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu, naye Iamekuwa ni malimbuko ya hao walilola. Kwani, kwa kuwa mauti yakaja kwa njia ya binadamu, kufufuka kwa

wafu vivyo huja kwa njia ya binadamu. Kwani vivile kama wote wafavyo katika Adamu, vivyo katika Kristo wote watafanywa kuwa hai. Ila ni kila mmoja katika pahali pake mwenyewe ; Kristo ni malimbuko ; baadaye ni hao amba ni wa Kristo katika kuja kwake. Kisha *huja* ule mwisho, hapo *Kristo* atakapompa Mwenyezi Mungu, yeze Baba, ule ufalme ; hapo atakapoyabatilisha kila mamlaka na kila amri na uwezo. Kwani yapasa kwamba atawale yeze hata atakapotwia adui zake wote chini ya nyayo zake. Adui wa mwisho wa kutoweshwa ni mauti. Kwani, Aliviweka vitu vyote viwe chini ya nyayo zake. Ila hapo asemapo ya kwamba, Vitu vyote vimewekwa viwe chini, ni dhahiri ya kwamba yeze aliyeviweka vitu vyote viwe chini yake, hamo. Na hapo vitu vyote vitakapowekwa viwe chini yake, ndipo hapo Mwana naye mwenyewe atawekwa chini ya huyo aliyeviweka vitu vyote chini yake, ili kwamba Mwenyezi Mungu awe vyote katika vyote.

Auje, watafanya nini hao wabatizwao kwa ajili ya wafu ? Kwamba wafu hawafufuki kabisa, wamebatizwa kwa ajili ya wafu kwa maana gani ? na sisi tumo katika hatari kila saa kwa maana gani ? Kila siku nafa, naam, kwa majivuno yangu kwa ajili yenu, ndugu zangu, niliyo nayo katika Kristo Yesu Bwana wetu. Kwamba kwa hali ya ki-binadamu nilipigana na nyama za mwitu huko Efeso, nina faida gani ? Kwamba wafu hawafufuki, na tule, na tunywe, kwa kuwa kesho twafa. Msidanganyike ; vikao vibaya huharibu tabia njema. Levuka kwa kutenda mema, nanyi misifanye dhambi ; kwani wengine hawana kumjua Mungu ; nanena *haya* kuwatahayarisha ninyi.

Kwenda mtu mmoja atanena, Je, wafu wafufuliwaje ? Nao huja na mwili namna gani ? Ewe mpumbavu, kile upandacho wewe hakipewi uhai, kikiwa hakijakufa ; na hicho upandacho, upandi ule mwili utakaokuwapo, lakini ni tembe tupu, huenda ikawa ni ya nganu, au nyingineyo yoyote ; ila Mwenyezi Mungu huipa mwili vivile kama alivyopenda, na kila mbegu *hupewa* mwili wake mwenyewe.

Nyama zote si nyama moja : lakini iko *nyama* ya binadamu, na nyama nyingine ni ya nyama wa miguu minne, na nyiningine ni ya nyuni, na nyiningine ni ya samaki. Tena iko miili ya mbinguni, na miili ya nchi : lakini utukufu wa ile ya mbinguni ni aina mbali, na utukufu wa ile ya nchi ni aina mbali. Kuna utukufu wa juu, na mwininge wa mwezi, na mwininge wa nyota, kwani hufadhiliana nyota na nyota kwa utukufu. Na kufufuka kwao wafu ni vivyo hivyo. Hupandwa katika kuharibika, hufufuliwa katika hali isiyo ya kuharibika : hupandwa katika unyonge ; hufufuliwa katika utukufu : hupandwa katika udhaifu ; hufufuliwa katika nguvu : hupandwa mwili wa nafsi ; hufufuliwa mwili wa roho. Kwamba kuna mwili wa nafsi na *mwili* wa roho pia uko. Ndipo yakaandikwa na haya, Mtu wa kwanza huyo Adamu akawa nafsi iliyo hai. Adamu wa mwisho *akawa* roho ihuishayo. Lakini ule uliokuwa wa roho, sio wa kwanza, lakini ni ule wa nafsi *uliokuwa wa kwanza*, baadaye ule ulio-wa roho. Mtu wa kwanza alitoka katika nchi, ni wa udongo ; mtu wa pili alitoka mbinguni, naye ni Bwana. Jinsi alivyo huyo wa udongo, na hao wa udongo ni vivyo ; na jinsi alivyo huyo wa mbinguni, na hao wa mbinguni ni vivyo. Tena, vivile kama tulivyochukua sura za huyo wa udongo, nasi vivyo tutachukua sura za huyo wa mbinguni.

Basi nanena neno hili, ndugu zangu, ya kwamba nyama na damu haviwezi kuurithi ufalme wa Mungu ; wala kiharibikacho hakiwezi kukirithi hicho kisichoharibika. Hili ndilo, nawaambia ninyi jambo lililofichamana : Sisi hatatalala sote, ila sote tutabadilika, mara, kama kupesa na *kufumbua*, *ipigwapo* parapanda ya mwisho : kwani parapanda itavuma, na wafu watafufuliwa katika hali isiyo ya kuharibika, na sisi tutabadilika. Kwani imepasa huu uharibikao uvikwe kutoharibika, na huu upatikanao na mauti uvikwe kutookufa. Ila hapo huu uharibikao utakapovikwa kutoharibika, na huu upatikanao na mauti utakapovikwa kutookufa, ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, *nalo ni hili*, Mauti yameremezwa katika kushindwa. Ku wapi, ewe mauti, kushinda kwako ? ki wapi, ewe mauti, chembe chako cha ushungu ? Ushungu

wa mauti ni dhambi ; na nguvu za dhambi ni ile sheria : ilia asante ni yake Mwenyezi Mungu atupaye kushinda kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu. Kwa ajili ya hayo, ndugu zangu, wapenzi wangu, thubutikeni, msiweze kuondolewa, mfanye kazi kwa wingi katika Bwana kila wakati, kwa kuwa mwajua ya kwamba taabu yenu si ya bure katika Bwana.

¶ *Badala ya Zaburi hizi na Somo hili, moja katika Masomo yafuatanyo laveza kusomwa.*

2 Wakorintho 4. 16-18 na 5. 1-10

Ufunuo 7. 9-17

Ufunuo 21. 1-7

¶ *Hata wakifika Kaburini, wakati wa kumtengeneza yule maiti ili kumlaza ndani ya nchi, yule Padre hunena maneno haya, au yule Padre na wale makaribu huyaimba :*

BINADAMU aliyezawa na mwanamke siku zake Batakaoishi ni haba, nazo zilizooaa taabu. Yeye hutepuza kama vile ua, kisha hukatwa : hukimbia kama kivuli kikimbiavyo, wala hasimami.

Tuwapo hai tu katika kufa ; tumwendee nani tupate msaada tusipokuwa kwako, ewe Bwana ? nawe uliye na haki kuchukiwa kwa makosa yetu.

Na haya yote, ewe Bwana Mungu uliye mtakatifu sana, ewe Mola mwangi wa uwezo, ewe Mwokozi mtakatifu, mwenye rehema zote ; usitutie katika maumivu ya uchungu ya kufa kwa milele.

Wewe, Bwana, wajua siri za miyoni mwetu ; usituzibie masikio yako ya rehema tukuombao, nawe utusamehe, ewe Bwana uliye mtakatifu kabisa, ewe Mwenyezi Mungu mwangi wa uwezo, ewe Mwokozi mtakatifu mwenye rehema, nawe ndiwe Mwamuzi mwenye haki wa milele, usituache saa yetu ya kufa kwa maumivu ya mauti yawayo yote tukatengwa nawe.

¶ *Ndipo hapo, muda ule mwili ukitupiwa mchanga juu yake na wengine waliosimama kando, yule Padre hunena,*

KWA maana ya hivyo alivyopendezewa Mwenyezi Mungu na kuitwaa roho yake huyu ndugu yetu mpenzi aliyesariki, sisi kwa ajili ya neno hili, twauweka

mwili wake katika nchi : kilicho mchanga kirejee mchanga, kilicho ivu kirejee ivu, kilicho uvumbi kirejee uvumbi, kwa tumaini lililo yakini na imara la kufufuliani kwa maisha ya milele, kwa Bwana wetu Yesu Kristo, atakayegeuzea mwili huu wa unyonge wetu uwe mfano mmoja na mwili wa utukufu wake, kwa kadiri ya kutenda kwake yeye aezavyo hata kuvitweza vitu vyote chini yake.

¶ *Kisha husomwa au huimbwa,*

NILISIKIA sauti iliyyotoka mbinguni, ikinena, Andika, Heri ni yao wafu wafao katika Bwana tokea sasa ; naam, yuanena huyo Roho, ya kwamba wapate kupumzika baada ya taabu zao za kazi.

¶ *Kisha husoma yule Padre,*

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo makte wetu wa kutotosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. Amina.

Padre

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, zi hai pamoja nawe Eroho za waondokao huku katika Bwana ; tena roho zao waaminifu waliopona katika taabu ya miili zi pamoja na wewe katika furaha na raha ; sisi twakushukuru sana kwa kuwa umependia kumponya huyu ndugu yetu, umemwokoa na mashaka ya ulimwengu huu wa madhabbi ; na huku twaomba upende kwa fadibili za wema wako kufanya haraka kuitimiliza hesabu ya wateule wako, ili kwamba sisi tulio hai huku, pamoja na hao wenzetu wote waliokwisha kufariki dunia wenyewe imani ya kweli ya jina lako .takatifu pia sote, tupate kukamilika katika utimilifu wa heri, miili yetu na roho zetu, katika utukufu wako wa milele : kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Sala

EWE Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, ndiwe Babaye Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ndiye huko kufufuliwa, tena ndiye maisha : naye aaminiye kwake, ajapokuwa amekufa, ataishi ; kisha kila mtu aishiye na kuamini kwake hafi kifo cha milele ; tena ndiye aliye-tufunza, kwa mtume wake mtakatifu yule Paulo, ya kwamba, tuisisikitike kama watu wasiokuwa na tumaini wasikitikavyo, kwa ajili ya hao waliolala ndani yake ; sisi twakunya nyenyekeea sana, twaomba kwako, ewe Baba, kwamba utufufue sisi katika hiki kifo cha dhambi, ututie katika maisha ya haki ; ili kwamba wakati tutakopofariki dunia hii, tupate kupumzika ndani yake yeze ; nasi ndivyo ambavyo twatumaini kuwa amepumzika huyu ndugu yetu naye : hata iwe, katika kule kufufuliwa kwa watu wote, katika siku ya mwisho, kuwa sisi kupata radhi machoni pako ; tupate na hiyo baraka, Mwanayo mpenzi wako umpedayse sana atakayowabarikia watu wote wakupenda na kukucha wewe, kwa kuwaambia, Njoni, enyi mliobarikiwa na Babaangu, mje muurithi usalme miliontengenezewa ninyi tokeea kupigwa msingi ulimwengu : utuneemeshe hayo, Baba mwangi wa rehema, kwa Yesu Kristo, Mwombezi wetu aliyetukomboa. *Amina.*

¶ *Sala iwezayo kutumiwa mbele ya Baraka.*

EWE Mwenyezi Mungu, Baba wa rehema zote, Mpaji wa faraja yote ; twakuomba uwahurumie wao waliao, ili kwa kukutwika wewe taabu zao zote, wajue faraja ya mapenzi yako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

NEEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, viwe pamoja nasi soté milele. *Amina.*

SHUKRANI ZA WANAWAKE BAADA YA KWISHA KUZAA

¶ *Wale wanawake, ukifika wakati wao wa kutoka kutawa kwa baada ya kujifungua, huingga msikitini hali wamevaa mavao ya lesima, huenda na kupiga magoti pahali pafaaipo, kama ilivyo ada ya msikitii ule : au kamé atakavyoamuru mwenye amri ya mambu haya :*

KWA maana ya hivyo alivyopenda Mwenyezi Mungu kuwapa kwa wema wake ya kujifungua salama, na alivyowaponya katika hiyo hatari kubwa mno ya uzazi : kwa ajili ya hayo *ninyi* mshukuruni Mwenyezi Mungu shukrani ya miyoni sana, *mseeme*,

¶ *Ndipo hapo Padre husoma,*

Dilexi quoniam. Zaburi 116

NAMPENDA Yehova kwa kuwa amesikiliza : sauti zangu na sala zangu.

2. Kwa maana amenitegea sikio lake : kwa hiyo nita-mlingana siku zangu zote.

3. Kamba za mauti zilinizinguka, shida za kuzimu zilinipata : niliona taabu na huzuni.

4. Nikalilingana jina la Yehova : ewe Yehova, nakuumba sana, uniokoe nafsi yangu.

5. Yehova ni mwenye neema na haki : naam, Mungu wetu ni mwenye rehema.

6. Yehova huwalinda wasio hila : nilidhiliaka akanikoa.

7. Urudi, ewe nafsi yangu, rahani mwako : kwa kuwa Yehova amekutendea kwa ukarimu.

8. Kwani umeniponya nafsi yangu na mauti, macho yangu na machozi : na miguu yangu na kuanguka.

9. Nitaenenda mbele za Yehova : katika nchi ya walio hai.

10. Naamini, kwani nitasema : mimi niliteswa sana.

11. Mimi nilisema katika haraka yangu : wanadamu wote ni waongo.

12. Nimirudishie Yehova nini : kwa ukarimu wake wote alionitendea?

13. Nitakipokea kikombe cha wokofu : nitalilingana jina la Yehova.

14. Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Yehova : naam, mbele ya watu wake wote.

15. Ina thamani machoni pa Yehova : mauti ya watakatifu wake.

16. Ewe Yehova, hakika *mimi ni mtumishi wako : mtumishi wako, mwana wa kijakazi chako ; umefungua vifungo vyangu.

17. Nitakutolea dhabihu ya kushukuru : nitalilingana jina la Yehova.

18. Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Yehova : naam, mbele ya watu wake wote ;

19. Katika nyua za nyumba ya Yehova : ndani yako, ewe Yerusalem. Aleluya.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Au hii, Zaburi 127

YEHOVA asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure : Yehova asipoulinda mji, ye ye aulindaye akesha bure.

2. Kazi yenu ni bure, ninyi mnaoamka mapema na kukawia kwenda kulala, mmapokula chakula cha taabu : humpa impenzi wake usingizi.

3. Wana ndio walio urithi wa Yehova : uzao wa tumbo ni thawabu.

4. Kama mishare mkononi mwa shujaa : ndivyo walivyo wana wa ujanani.

5. Yuna heri mtu yule aliyelijaza podo lake hivyo : naam, hawataona aibu wanapokuwa wakisema na adui langoni.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ Ndipo hapo yule Padre hunena,

Na tuombe.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

BABAETU ulije mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe usutamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleka katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. Amina.

Padre. Ewe Bwana, uwaokoe hawa vijakazi vyako ; Huitika. Wakutumainio wewe.

Padre. Uwe kwao ngome iliyo imara ; Huitika. Penye uso wa adui wao.

Padre. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu ; Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Padre.

Na tuombe.

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, sisi tu miguuni pako twakushukuru kwa ajili ya ulivyopenda kuwaokoa hawa vijakakazi vyako na mambo ya uzazi, ambayo maumivu yake ni mengi na hatari yake ni kubwa mno ; nasi twakunyenyekeea, ewe Baba ulije na rehema, twakuomba, uwajalie huku katika maisha haya ya sasa kuwa waaminifu wa maisha, na kuwa watu wa kwenenda katika mwendo wao kama upendavyo wewe ; na katika maisha yajayo, wawe washirika wa utukufu usio ukomo ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

¶ Wale wanawake wajao kumpa Mwenyezi Mungu shukrani na asante, hawana budi na kutoa ada ; na pakishirikanwa Ushirika, yafaa waupokee Ushirika Mtakatifu.

MAONYO,

MAANA YAKE NI KUONYA HASIRA ZAKE Mwenyezi Mungu na Hukumu Zake ; kwa kuwatisha wenyewe dhambi,

pamoja na sala kadhawakadha, zitumikazo kwa siku ya kwanza ya Saumu, na nyakati nyingine zisizokuwa huo, kama atakavyoagiza yule mwenye kuamrisha.

¶ Baada ya Sala ya Asubuhi, ikiisha kusomwa Litania, kama desturi, yule Padre ali pahali pasomwapo Litania, au Mimbarini, hunena,

ENYI ndugu zangu, zamani za Kanisa la Kale kuli-kuwa na desturi moja nzuri ya kufunza adabu katika kumcha Mungu, waliyoifanya mwanzo wa Saumu ; ya watu waliopatikana na laumu ya dhambi zilizo na aibu, kutubishwa mbele ya watu, na kuadhibiwa katika ulimwengu huu, ili kwamba nafsi zao zipate kupona kwa Siku ya Bwana, na kwamba watu wengine, walioonywa na kurudiwa kwa wale, wapewe ya kuzidi kujilinda na makosa.

Badala ya hayo, (hata wakati itakapowezekana kuyarejeza upya, nalo ndilo litamaniwalo,) tumependezewa kama wakati huu wa sasa, kuwasomea mbele yenu nyote hukumu zake Mwenyezi Mungu zipasazo watu wote za kuwalaani kwake wenyewe dhambi ambao hawajatubia, nazo zimetolewa katika Chuo cha Marejezo, au Deuteronomy, Mlango wa ishirini na saba, na mwahali kadhawakadha mwagine mwa Maandikoni ; na ya ninyi katika kila mtamko mmoja wa maneno kuniitikia, *Amina* : nayo twayafanya hivyo ili kuwapa ninyi, kwa huku kuonywa ya kasirani nyingi awaoneayo Mwenyezi Mungu wenyewe dhambi, ya kuingwa miyoni mwenu na toba iliyoye na ndani kweli ; na ya kwenenda mbele kwa mwendo wa kujitunza katika zamani hizi za hatari, kwa kuijepua na aibu namna hizo ambazo wenyewe kwa vinywa vyenu mmeyatuhutisha kuwa yastahili na laana yake Mwenyezi Mungu.

AMELAANIWA mtu afanyaye sanamu wa kuchonga au wa kusubu, ili kumwabudu.

¶ Wale watu huitika, wakinena,

Amina.

Padre. Amelaaniwa amtukanaye babaye au mamaye.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa atupaye mpaka wa jirani yake.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa apotezaye kipofu kutaka kumkosesa njia.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa aipotoshaye hukumu ya mgeni, na ya yatima, na ya mjane.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa ampigaye mwensiwe kwa siri.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa alalaye na mke wa mwensiwe.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa atwaaye ujira wa kumuua asiye makosa.

Huitika. Amina.

Padre. Amelaaniwa amtumainiye binadamu, na kurejea kwa binadamu, akamwepuka Yehova moyoni mwake.

Huitika. Amina.

Padre. Wamelaaniwa wasio wa rehema, na wazinifu, na waṭwaao wake wa watu, na wenyewe macho ya kutamanzi, na waabuduo sanamu, na wenyewe kusingizia, na walevi, na wanyang'anyi.

Huitika. Amina.

Padre

HAYA basi, kwa kwamba wao ni watu wa ¹kulaaniwa (kama ashuhudiavyo nabii Daudi) ambao wakosa katika maagizo yake Mwenyezi Mungu, wakienda kutangatanga ; sisi kwa tukumbukavyo

¹ Zaburi 119. 21.

hukumu ya utisho ilewa-lewayo juu ya vichwa vyetu, isiyokawia kutuangukia, na tumrejee Mungu wetu, kwa miyo iliypondeka na kunye-

MAONYO

² *Mathayo* 3. 10.³ *Wahibirania* 10. 31.⁴ *Zaburi* 11. 6.⁵ *Isaya* 26. 21.⁶ *Malaki* 3. 2.⁷ *Mathayo* 3. 12.⁸ ¹ *Wathesalonike* 5. 2-3.⁹ *Warumi* 2. 4-5.

nyekea kabisa ; kwa kuyaombolea na kuyaonea machungu maisha yetu yenyé madhambi ; kwa kula-lamia na kumuungamia makosa yetu ; na ²kutafuta njia ya kufanya matunda yastahiliyo toba. Kwani hivi sasa limekwisha kukaa lile shoka mashinani mwa miti, hata imekuwa kila mti usiozaa matunda mema hukatwa ukatupwa motoni. ³Ni jambo la kutisha kuangukia katika mikono ya Mungu aliye hai ; ⁴atawashushia wale wenye dhambi, mitambo na moto na kiberiti, na dharuba za upepo na tufani ; ndilo litakalokuwa ni fungu lao la kunywa. ⁵Kwani, huyo ndiye, Yehova yuatoka pahali pake, ili awaadhibishe hao wakaa duniani kwa sababu ya uovu wao. ⁶Lakini ni nani atakayeistahimili ile siku ya kuja kwake, ni nani atakayesimama atokeapo ? ⁷Na uteo wake anao mkononi mwake, atausafi uwanda wake, akusanye nafaka zake uchagani, ila yale matwa atayateketeza kwa moto usiozimika. ⁸Siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo wakati wa usiku ; hapo wasemapo, Ni amani na salama, ndipo watakapotokewa na uharibifu ghafula ; kama vile uchungu wa uvyyazi umfikiliapo mwenye mimba, nao hawatapona kabisa. Ndipo zitakapoonekana hasira zake Mwenyezi Mungu kwa siku ya kisasi chake, ⁹ambazo kwamba wenye dhambi kwa kufuata ugumu wa moyo wao

MAONYO

usio na toba wamejiwekeaa akiba ya hasira hizo, waliodharau wema na subira na uvumilivu wa Mwenyezi Mungu, akiwavutia toba.

¹⁰Hapo ndipo watakaponilingana (asema Yehova), lakini mimi sitaitika ; watanitafuta kwa bidii, lakini hawataniona ; kwa kuwa walichukia maarifa, wala hawakuchagua kumcha Yehova ; hawakukubali mashauri yangu, wakayadharau maonyo yangu yote.

¹¹Ndipo hapo watakapochelewa kubisha, mlango umekwisha kufungwa ; watachelewa walalamapo, tena hukumu yao imewafikilia.

A ! sauti yenyé kutisha ya maa-muzi ya haki hasa, ¹²watakopolaumiwa na kuambiwa, Ondokeni kwangu mimi, enyi mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, huo aliotengezewa Ibilisi na malai-ka zake. Basi, enyi ndugu zangu, na tujiangalie mapema, ¹³siku ya wokofu isijaisha ; ¹⁴kwani usiku waja, wakati asioweza mtu kutenda kazi. Afadhali tuwapo na huu mwanga, nasi twenende kama ambaa tu wana wa mwanga,

¹⁵tusije tukatupwa katika giza lililo la nje sana, kuliko na kulia na kukaza-kaza meno. Tusuhe-sabu kuwa ni mdogo wema wake Mwenyezi Mungu, naye yuatuua huku yuatuambia kurejeza upya mambo yetu, hata kwa huruma zake zisizo ukomo ametupa ahadi ya kutusamehe makosa yetu yali-yotangulia, tukiwa tu wenye kum-

¹⁰ *Mithali* 1. 28-30.¹¹ *Mathayo* 25. 10-12.¹² *Mathayo* 25. 41.¹³ ² *Wakorintho* 6. 2.¹⁴ *Yohana* 9. 4-5.¹⁵ *Mathayo* 25. 30.

MAONYO

¹⁶ Isaya 1. 18.

¹⁷ Ezekiel 18. 30-32.

¹⁸ I Yohana 2. 1-2.

¹⁹ Isaya 53. 5.

²⁰ Mathayo 11. 29-30.

rejea kwa miyo iliyokamilika ya ¹⁶kweli. Kwani ijapokuwa dhambi zetu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kabisa kama theluji ; kwamba ni nyekundu mno kama bendera, zitakuwa kama manyoya ya kondoo. ¹⁷Rejeeni ninyi, mkazingatie na kuya-acha hayo makosa yenu yote ; basi hivi uovu hautakuwa uhari-bifu wenu ; yatupilie mbali nanyi hayo makosa yenu yote, ambayo mmekosa ndani yake, nanyi jifanyeni miyo mipya, na roho mipya ; kwani mtakufa kwa maana gani, enyi wa nyumba ya Isiraeli ? Kwani sioni furaha katika kufa kwake huyo afaye, asema Yehova Mungu : basi zingatiени mrejee, mkaishi. ¹⁸Na ijapokuwa tumekosa, lakini tuna mwenye kutuombea kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye dhabihu wa dhambi zetu. ¹⁹Kwani ndiye aliyejeruhiwa kwa makosa yetu, alishetwa yeye kwa maovu yetu sisi. Basi na tumrejee yeye (naye ndiye mwenye kuwakaribisha kwa rehema wakosa wote watubuo kweli) kwa kujithubutisha miyo yetu kuwa yu radhi nasi tukimka-ribia, naye apenda sana kutusamehe, tukimwendea kwa toba iliyo na imani ; na kumfuata kwa atakalo lote, na kwenenda mbele tokeaa sasa katika njia zake ; ²⁰kwa kujitweka kongwa lake lililo jepesi, na mzigo wake ulio hafifu na kumwandama kwa unyenyekevu,

MAONYO

kwa subira, na kwa mapenzi, na kuamrishiwa mambo yetu kwa Roho wake Mtakatifu kututawala ; hali twataka atukuzwe yeze daima, na kumtumikia kwa kumshukuru kama ipasavyo hali tulioitiwa na Mwenezei Mungu. Basi, tuyafanyapo hayo, Kristo atatuokoa na laana ya sheria, tena atatuokoa na kule kuapizwa kwa nguvu, ²¹wata-kavyoapizwa hao ambao ni wa kuwekwa upande wa mkono wa hushoto ; naye atatuweka upande wa mkono wake wa kuume sisi ; atatupa na baraka ya Babaye iliyo na neema, kwa kutuambia kutakabadhi ufalme wa fahari, ambao na apendezewe ni kututia sote, kwa ajili ya rehema zake zisizo mpaka. Amina.

¶ Ndipo hapo hupiga magoti jamii ya waliopo, yule Padre na wale wenye daraja wa kanisani nao wali hali ya kupiga magoti pahali ambapo wamezoea kusoma Litania, na kusoma Zaburi hii :

Miserere mei, Deus. Zaburi 51

UNIREHEMU, ewe Mungu, kwa kadiri ya fadhili zako : kwa kadiri ya wingi wa rehema zako uyafute makosa yangu.

2. Unioshe kabisa na uovu wangu : unitakase dhambi yangu.

3. Kwani ninakiri mimi makosa yangu : na dhambi yangu i mbele yangu daima.

4. Nimekutendea dhambi wewe peke yako na maovu nimefanya mbele za macho yako : ili uhesabiwe kuwa una haki unenapo, na kuwa safi utoapo hukumu.

5. Mimi niliumbwaa katika hali ya uovu : mama yangu alinichukua mimba hatiani.

6. Bali wapendezwa na kweli iliyo moyoni : utanijulisha hekima kwa siri.

7. Unisafishe kwa husopo nami nitakuwa safi : unioshe nami nitakuwa mweupe kuliko theluji.

8. Unisikize furaha na shangwe : mifupa ulioiponda ifurahi.

9. Ufiche uso wako usitazame dhambi zangu : uzifute hatia zangu zote.

10. Ewe Mungu, uniumbie moyo safi : uifanye upya roho yangu ndani yangu.

11. Usinitenge na uso wako : wala Roho wako Mtakatifu usiniondolee.

12. Unirudishie furaha ya wokofu wako : unitegemeze kwa Roho wako bora.

13. Nitawafundisha wakosaji njia zako : na wenye dhambi watarejea kwako.

14. Uniponye na damu za watu, ewe Mungu, Mungu wa wokofu wangu : na ulimi wangu utaiimba haki yako.

15. Ewe Bwana, ufunue midomo yangu : na kinywa changu kitanena sifa zako.

16. Kwani wewe hupendezwi na dhabihu, kama sivyo ningetoia : walakini huridhii sadaka za kuteketezwa.

17. Dhabihu za Mungu ni roho iliyounjika : moyo uliyounjika na kupondeka, ewe Mungu, hutaudharau.

18. Uitendee mema Zayuni kwa radhi yako : uziengene kuta za Yerusalem.

19. Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za haki, na sadaka za kuteketezwa hata hizo zilizo nzima : ndipo watakapotoa ng'ombe juu ya madhabahu yako.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa, Utuokoe maovuni. Amina.

Padre. Ewe Bwana, uwaokoe watumishi wako ;
Huitika. Wakutumainio wewe.

Padre. Uwaletee msaada utokao juu ;

Huitika. Uwalinde kwa uwezo wako milele.

Padre. Utusaidie, ewe Mungu Mwokozi wetu ;

Huitika. Nawe kwa ajili ya utukufu wa jina lako utuokoe ; uturehemu sisi wenye dhambi, kwa ajili ya jina lako.

Padre. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu ;

Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Padre

Na tuombe.

E WE Bwana, twakuomba sana, usikize kwa rehema maombi yetu, uwaachilie hao wote wakuungamiao dhambi zao, ili kwamba wao waishtakio miyoni mwao kuwa ni wenye dhambi, kwa msamaha wa rehema zako waachiliwe ; kwa Kristo Yesu, Bwana wetu. *Amina.*

E WE Mungu, Mweza-wa-yote, Baba mwenye rehema, Euwahurumiaye wanadamu wote, nawe huchukii kitu chochote ulichokumba ; wewe hutaki mauti ya mwenye dhambi, ila afadhali wataka auache uovu wake aokolewe ; utusamehe kwa rehema zako makosa yetu ; utupokee na kututuza miyoni sisi tuliohuzunika na kuchoka na huu mzigo wa madhambi yetu. Ni lako wewe kuwa na rehema daima, ni lako wewe pekeo kusamehe madhambi. Basi utuachilie sisi, Bwana mwema, uwaachilie watu wako, uliowakomboa ; usiwatieve hukumuni watumishi wako, ambao ni udongo dhaifu, maskini wenye dhambi ; lakini utuwekee mbali na hasira zako, tuliokiri uovu wetu kwa unyenyekevu, na kutubia makosa yetu kweli kweli, tena utusaidie haraka katika ulimwengu huu, ili kwamba tupate kuishi pamoja nawe milele katika ulimwengu ujao ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ Ndipo hapo watu husoma maneno haya, baada ya Padre :

UTUGEUZE, ewe Bwana mwema, nasi tutageuka. Uwe radhi, ewe Bwana, uwe radhi na watu wako, wageukao kukulekea wewe kwa kulia na kufunga na kuomba. Kwa kuwa wewe u Mungu mwenye rehema, mwingu wa huruma, mvumilivu na mwenye sikitiko kuu.

Wewe watusamehe tustahilipo na kuadhibiwa, na katika hasira zako wakumbuka rehema. Uwasamehe watu wako, Bwana mwema, uwasamehe, nawe usiiwache milki yako wakafedheheka. Utusikize, ewe Bwana, kwa kuwa rehema zako ni kuu. Na kwa kadiri ya wingi wa rehema zako utuangalie ; kwa sababu ya kustahili kwake na kutuombea kwake Mwanayo Mwenye-baraka, Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

¶ Kisha yule Padre husoma peke yake,

BWANA na atubarikie na kutulinda, Bwana na atufizie nuru za uso wake juu yetu, na kutupa amani, sasa na milele. Amina.

ZABURI ZA DAUDI

Siku 1. Sala ya Asubuhi

ZABURI 1

YUNA heri mtu yule asiyekwendà katika shauri la wasio haki : wala hasimami katika njia ya wakosaji, wala haketi katika baraza ya wenye mizaha.

2. Bali sheria ya Yehova ndiyo impendezayo : na sheria yake huifikiri inchanana na usiku.

3. Naye atakuwa kama miti uliopandwa kando-kando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake : na jani lake halinyauki, na kila alitendalo litafanikiwa.

4. Wasio haki hawawi hivyo : hao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo.

5. Kwa hiyo wasio haki hawatasimama hukumuni : wala wakosaji katika kusanyiko la wenye haki.

6. Kwa kuwa Yehova anajua njia ya wenye haki : bali njia ya wasio haki itapotea.

ZABURI 2

MBONA mataifa wanafanya ghasia : na makabila wanafikiri ubatili ?

2. Wafalme wa dunia wanajipanga, na wakuu wanafanya shauri pamoja : juu ya Yehova na juu ya Masihi wake.

3. Na tuvipasue visfungo vyao : na tuzitupie mbali nasi kamba zao.

4. Yeye aketiye mbinguni atacheka : Bwana atawafanya dhihaka.

5. Ndipo atasema nao kwa hasira yake : na kwa ghadhabu yake atawafadhaisha.

6. Nami nimeweka mfalme wangu : juu ya Zayuni, mlima wangu mtakatifu.

7. Nitaihubiri amri : Yehova aliniambia, Ndiwe mwanangu, mimi leo nimekuzaa.

8. Uniombe nami nitakupa mataifa kuwa urithi wako : na miisho ya dunia kuwa milki yako.

9. Utawaponda kwa fimbo ya chuma : kama chombo cha mfinanzi utawavunja.

10. Na sasa, enyi wafalme, muwe na akili : mwadibiwe, enyi waamuzi wa dunia.

11. Mtumikieni Yehova kwa kicho : shangirieni kwa kutetemeka.

12. Mbusuni Mwana asije akafanya hasira, nanyi mkapotea njiani : kwa kuwa hasira yake itawaka upesi ; wana heri wote wanaokimbilia.

ZABURI 3

EWE Yehova, watesi wangu wamezidi kuwa wengi : ni wengi wanaonishambulia.

2 Ni wengi wanaoiambia nafsi yangu : hana wokofu huyu kwa Mungu.

3. Na wewe, Yehova, ndiwe ngao yangu pande zote : utukufu wangu, uniiyuaye kichwa changu.

4. Kwa sauti yangu namlingana Yehova : naye anijibu toka mlima wake mtakatifu.

5. Nilijilaza nikalala usingizi, nikaamka : kwa kuwa Yehova ananitegemeza.

6. Sitayaogopa maelfu kumi ya watu : waliojipanga juu yangu pande zote.

7. Uondoke, ewe Yehova, uniokoe, ewe Mungu wangu : kwani umewapiga taya wote wanaonichukia ; wasio haki umewavunja meno.

8. Wokofu una Yehova : baraka yako na iwe juu ya watu wako.

ZABURI 4

NILINGANAPO unijibu, ewe Mungu wa haki yangu : umenifanyizia nafasi wakati wa shida ; unifadhili, uisikie sala yangu.

2. Enyi wanadamu, hata lini utukufu wangu utafedhe-heka ? Hata lini mtapenda ubatili na kutafuta uwongo ?

3. Lakini jueni ya kuwa Yehova amejichagulia mtu aliye mtawa : Yehova atasikia nimlinganapo.

4. Muwe na hofu wala msitende dhambi : fikirini mioyoni mwenu vitandani mwenu, katulieni.

5. Toeni dhabihu za haki : kamtumainieni Yehova.

6. Wako wengi wanaosema, ni nani atakayetuonyesha mema ? Ewe Yehova, utuinulie nuru ya uso wako.

7. Umenitia furaha moyoni mwangu : kupita *furaha* yao wanapozidishiwa nafaka na divai.

8. Katika amani nitajilaza na kupata usingizi mara : kwani wewe peke yako, ewe Yehova, ndiwe unijaliaye kukaa salama.

ZABURI 5

USIKILIZE, ewe Yehova, maneno yangu : uangalie kufikiri kwangu.

2. Usikie sauti ya kilio changu, ewe Mfalme wangu na Mungu wangu : kwa maana wewe ndiwe nikuombaye.

3. Ewe Yehova, asubuhi utasikia sauti yangu : asubuhi nitakutengenezea sala yangu na kutazamia.

4. Kwani wewe huwi Mungu apendezwaye na yasiyo haki : uovu hautakaa kwako.

5. Wajivunao hawatasimama mbele za macho yako : wawachukia wote watendao ubatili.

6. Utawaharibu wasemao uwongo : mwenye kumwaga damu na mwenye hila, Yehova achukizwa naye.

7. Bali mimi, kwa wingi wa fadhili zako, nitaingia nyumbani mwako : nitasujudu kwa kukucha, nikielekea hekalu lako takatifu.

8. Ewe Yehova, uniongoze kwa haki yako, kwa sababu ya adui zangu : uisawazishe njia yako mbele ya uso wangu.

9. Kwani hamna uaminifu vinywani mwao : mitima yao ni mashimo matupu, koo zao ni makuburi wazi, ndimi zao huipendekeza.

10. Uwapatilize, ewe Mungu ; na waanguke kwa mashauri yao : uwatoe nje kwa ajili ya wingi wa makosa yao, kwa maana wamekuasi wewe.

11. Na wafurahi wote wanaokimbilia ; wapige daima kelele za furaha : kwa kuwa wewe unawahifadhi ; walipendao jina lako wakufurahie.

12. Kwa maana wewe utambarikia mwenye haki : ewe Yehova, utamzungushia radhi yako kama ngao.

Siku I. Sala ya Jioni

ZABURI 6

EWE Yehova, usinikemee kwa hasira yako : wala usinirudi kwa ghadhabu yako.

2. Unifadhilli, ewe Yehova, kwani ninanyauka : ewe Yehova, uniponye, mifupa yangu imefadhaika.

3. Na nafsi yangu imefadhaika sana : na wewe, Yehova, hata lini ?

4. Urudi, ewe Yehova, uniopoe nafsi yangu : uniokoe kwa ajili ya fadhili zako.

5. Kwa maana katika mauti hapana kumbukumbu lako : katika kuzimu ni nani atakayekushukuru ?

6. Nimechoka kwa kuugua kwangu : kila usiku nakieleza kitanda changu, kwa machozi yangu nalilowesha godoro langu.

7. Jicho langu linadhoofika kwa masumbufu : lina-chakaa kwa sababu ya adui zangu.

8. Ondokeni kwangu ninyi nyote mtendao uovu : kwa kuwa Yehova ameisikia sauti ya kilio changu.

9. Yehova ameisikia sala yangu : Yehova atakubali maombi yangu.

10. Wote wanaonichukia wataaibika na kufadhaika : watarudi nyuma, kwa ghafula wataaibika.

ZABURI 7

EWE Yehova, Mungu wangu, nimekukimbilia wewe : Uniokoe na wote wanaonifuatia, uniponye :

2. Asije akaipapura nafsi yangu kama simba : akii-vunjavunja ambapo hapana wa kuponya.

3. Ewe Yehova, Mungu wangu, ikiwa nimetenda haya : ikiwa mna uovu mikononi mwangu ;

4. Ikiwa nimemlipa mabaya yeye aliyekaa kwangu salama : (naam, nimemponya yeye aliyejkuwa adui yangu bila sababu :)

5. Basi adui na anifuatie na kuikamata nafsi yangu : naam, aukanyage uzima wangu, aulaze utukufu wangu mavumbini.

6. Ewe Yehova, uondoke kwa hasira yako, ujiinue juu ya jeuri ya adui zangu : uamke kwa ajili yangu ; umeamuru hukumu.

7. Kusanyiko la mataifa na likuzunguke : na juu yake uketi utawale.

8. Yehova anawaamua mataifa : unihukumu mimi, ewe Yehova, kwa kadiri ya haki yangu na kwa kadiri ya unyofu nilio nao.

9. Ubaya wao wasio haki na ukome ; umweke imara mwenye haki : kwa maana Mungu mwenye haki ndiye anayeijaribu mioyo na viuno.

10. Ngao yangu ina Mungu : awaokoaye wanyofu wa moyo.

11. Mungu ni mwamuzi mwenye haki : naam, Mungu aghadhabikaye kila siku.

12. Mtu asiporejea ataunoa upanga wake : ameupinda uta wake na kuuweka tayari :

13. Naye amemtengenezea silaha za mauti : akifanya mishare yake kuwa ya moto.

14. Tazama, huyu ana uchungu wa uovu : naam, amechukua mimba ya madhara, amezaa uwongo :

15. Amechimba shimo, amelichimba chini sana : akatumrukia katika handaki aliyoifanya :

16. Madhara yake yatamrejea kichwani : na dhulumu yake itamshukia utesini.

17. Nitamshukuru Yehova kwa kadiri ya haki yake : nitaimba na kulisifu jina la Yehova aliye juu.

ZABURI 8

EWE Yehova, Bwana wetu ; jina lako jinsi lilivyo na Utukufu katika dunia yote ! Wewe uliyeweka utukufu wako katika mbingi.

2. Kwa vinywa vya watoto wachanga na wanyonyao umeweka misingi ya nguvu : kwa sababu ya adui zako, umkomeshe yule adui na mwenye kujilipiza kisasi.

3. Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako : mwezi na nyota ulizozitengeneza ;
4. Mtu ni nini hata umkumbuke : na binadamu hata umwangalie ?
5. Kwani umemfanya mdogo punde kuliko Mungu : umemvika taji ya utukufu na heshima ;
6. Umemtawaza juu ya kazi ya mikono yako : umetia vitu vyote chini ya nyayo zake ;
7. Kondoo na ng'ombe zote pia : naam, na nyama za kondeni ;
8. Ndege za angani na samaki za baharini : kila kipitachoo njia za baharini.
9. Ewe Yehova, Bwana wetu : jina lako jinsi liliyvo na utukufu katika dunia yote !

Siku 2. Sala ya Asubuhi

- N**ITAMSHUKURU Yehova kwa moyo wangu wote : nitasimulia matendo yako yote ya ajabu.
2. Nitafurahi na kushangiria kwako wewe : nitaimba na kulisfu jina lako, ewe uliyie juu.
 3. Adui zangu warudipo nyuma : hujikwaa na kuangamia mbele zako.
 4. Kwa maana umenifanyia hukumu na haki : umeketi kitini pa enzi ukihukumu kwa haki.
 5. Umewakemea mataifa, umewaangamiza wasio haki : umelifuta jina lao milele na milele.
 6. Adui wamekoma na kuachwa ukiwa milele : nayo miji uliyoiharibu kumbukumbu lao nalo limepotea.
 7. Bali Yehova anakaa milele : ameweeka kiti chake tayari kwa hukumu.
 8. Naye atauhukumu ulimwengu kwa haki : atawaamua watu kwa adili.
 9. Na Yehova atakuwa ngome kwake aliyeonewa : naam, ngome kwa nyakati za shida.
 10. Nao wakujuao jina lako watakutumaini wewe : kwa kuwa wewe, ewe Yehova, hukuwaacha wakutafutao.

11. Mwimbieni na kumsifu Yehova akaaye Zayuni : tangazeni katii ya watu matendo yake.
12. Kwani atafutaye habari za damu awakumbuka : hakukisahau kilio cha wanyonge.
13. Unifadhili, ewe Yehova : tazama mateso niteswayo na wanaonichukia, wewe unayeniinua katika milango ya mauti ;
14. Ili nizisimulie sifa zako zote katika milango ya binti Zayuni : nitaufurahia wokofu wako.
15. Mataifa wamezama katika shimo walilolifanya : kwa wavya waliouficha imenaswa miguu yao.
16. Yehova amejidhihirisha na kutekeleza hukumu : amemnasa asiye haki kwa kazi ya mikono yake.
17. Wasio haki waterejea kuzimu : naam, mataifa wote wanaomsahau Mungu.
18. Kwa maana mhitaji hatasahauliwa daima : matumaini ya wanyonge hayatapotea milele.
19. Uondoke, ewe Yehova, asipate nguvu binadamu : mataifa wahukumiwe mbele zako.
20. Uwawekee utisho juu yao, ewe Yehova : mataifa na wajijue kuwa ni binadamu tu.

ZABURI 10

- E**WE Yehova, ya nini kusimama mbali : **kwa nini** kujificha nyakati za shida ?
2. Kwa kiburi chao wasio haki mnyonge anaafuatiwa kwa ukali : na wanawesi wao kwa hila zizo hiso walizoziwaza.
 3. Kwani asiye haki hujisifia tamaa ya moyo wake : na mwenye choyo humkana Yehova na kumdharaau.
 4. Asiye haki kwa kiburi cha uso wake asema, Hata-patiliza : hakuna Mungu, ndio jumla ya mawazo yake.
 5. Njia zake zi thabiti kila wakati ; hukumu zako ziko juu asizione : adui zake zote awafonya.
 6. Aserna moyoni mwake, Sitaondoshwa : kizazi baada ya kizazi sitakuwamo maoavuni.
 7. Kinywa chake kimejaa laana na hila na dhulumu : chini ya ulimi wake mna madhara na uovu.

8. Hukaa katika maoteo ya vijiji, mwahali mwa siri humuua asiye hatia : macho yake humvijja mtu asiye msaada.

9. Huotea pahali pa siri kama simba pangoni ; huotea amkamate mtu maskini : naam, humkamata mtu maskini, akimkokota wavuni mwake.

10. Hujikunyata na kuinama : wasio msaada huanguka kwa hao walio wake wenye nguvu.

11. Asema moyoni mwake, Mungu amesahau : auficha uso wake, hataona kamwe.

12. Uondoke, ewe Yehova, ewe Mungu, uinue mkono wako : usiwasahau walio maskini.

13. Kwa nini asiye haki kumdharaau Mungu : akisema moyoni mwake, Hutapatiliza ?

14. Umeona, kwani unaangalia madhara na jeuri, uytawae mkononi mwako : asiye msaada hukuachia *nafsi yake* ; umekuwa msaidizi wa yatima.

15. Uuvunje mkono wa mtu asiye haki : na yule mwovu uandarie uovu wake hata usiuone.

16. Yehova ndiye Mfalme milele na milele : mataifa wamepotea kutoka nchi yake.

17. Tamaa ya wanyonge umeisikia, ewe Yehova : uitaitengeneza miyo yao, utatega sikio lako :

18. Ili kumhukumu yatima naye aliyeonewa : binadamu aliye udongo asizidi kudhilimu.

ZABURI II

YEHOVA ndiye niliyemkimbilia : mbona mnaiambia nafsi yangu, Kimbia kama ndege uende mlimani kwako ?

2. Kwa maana, tazama, wasio haki wanaupinda uta, wanaitia mishbare yao katika uzi : ili kuwapiga gizani wanyofu wa moyo.

3. Misingi ikiharibika : mwenye haki atafanya nini ?

4. Yehova yu katika hekalu lake takatifu ; Yehova, kitii chake cha enzi kiko mbinguni : macho yake yanaangalia, kope zake zinawajaribu wanadamu.

5. Yehova humjaribu mwenye haki : bali nafsi yake humchukia mtu asiye haki na mwenye kupenda udhalimu.

6. Atawanyeshea wasio haki mitego : moto na kiberiti na upepo wa hari vitakuwa fungu la kikombe chao.

7. Kwa kuwa Yehova yu mwenye haki ; apenda mateendo ya haki : wanyofu wa moyo watamwona uso wake.

Siku 2. Sala ya Jioni

ZABURI 12

UKWANI, ewe Yehova, kwani mtawa amekoma : kwani waaminifu wametoweka katika wanadamu.

2. Husemezana yasiyofaa kila mtu na mwensiwe : wenye midomo ya kujipendeleza husemezana kwa mioyo ya unafiki.

3. Yehova atakata midomo yote ya kujipendeleza : ulimi unenao maneno ya kiburi.

4. Waliosema, Kwa ndimi zetu tutashinda ; midomo yetu ni yetu wenye : ni nani aliye bwana juu yetu ?

5. Kwa ajili ya kuonewa wanyonge, kwa ajili ya kuugua kwao wahitaji, sasa nitaondoka, asema Yehova : nita-mweka salama yeeye wanayemfyonya.

6. Maneno ya Yehova ni maneno safi : kama fedha ilijoaribiwa kalibuni juu ya nchi, iliyosafika mara saba.

7. Wewe, ewe Yehova, ndiwe utakayewahifadhi : utawalinda na kizazi hiki milele.

8. Wasio haki hutembea pande zote : ujisadi ukitukuka kati ya wanadamu.

ZABURI 13

EWE Yehova, hata lini utanisahau ; hata milele ? Hata lini utanificha uso wako ?

2. Hata lini nifanye mashauri nafsimi mwangu nikihuzunika moyoni mchana kuchwa ? Hata lini adui wangu atukuke juu yangu ?

3. Uangalie, unijibu, ewe Yehova Mungu wangu : uyatiie nuru macho yangu nisije nikalala *usingizi wa mauti*.

4. Adui wangu asije akasema, Nimemshinda : watesi wangu wasifurahi kwa kuwa nimeondoshwa.

5. Nami nimezitumainia fadhili zako : moyo wangu utafurahia wokofu wako.

6. Nitamwimbia Yehova : kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu.

ZABURI 14

MPUMBAVU amesema moyoni, Hakuna Mungu : wameharibika na kufanya machukizo, hakuna mtena mema.

2. Toka mbinguni Yehova aliwachungulia wanadamu : aone kama yuko mtu mwenye akili amtafutaye Mungu.

3. Wote wamepotoka, wameoza wote pamoja : hakuna mtena mema, la, hata mmoja.

4. Je, wote wafanyao maovu hawajui ? Walao watu wangu kama walavyo mkate, hawamlingani Yehova.

5. Hapo ndipo walipoingiwa na hofu nyngi : kwani Mungu yupo pamoja na kizazi cha mwenye haki.

6. Mnalitia aibu shauri la mtu maskini : kwani Yehova ndiye aliye kimbilio lake.

7. Ngawa wokofu wa Isiraeli hautoki katika Zayuni ! Yehova atakapowerudisha wafungwa wa watu wake, Yakobo atashangiria, Isiraeli atafurahi.

Siku 3. Sala ya Asubuhi

ZABURI 15

EWE Yehova, ni nani atakayekaa hemani mwako : ni nani atakayefanya maskani yake katika kilima chako kitakatifu ?

2. Ni mtu aendaye kwa ukamilifu na kutenda haki : asemaye kweli kwa moyo wake.

3. Asiyesingizia kwa ulimi wake, wala hamtendi mwensiwe mabaya : wala hamtolei jirani yake laumu.

4. Ambaye machoni pake mtu asiyefaa hudharauliwa, bali huwaheshimu wamchao Yehova : ingawa ameapa kwa hasara yake, habadili maneno yake.

5. Hatoi fedha yake apate faida, wala hapokei rushwa amwangamize asiyehatia : mtu atendaye mambo haya hataondoshwa milele.

ZABURI 16

UNIHIFADHI, ewe Mungu : kwani nakukimbilia wewe.

2. Nimemwambia Yehova, Ndiwe Bwana wangu : sina wema ila utokao kwako.

3. Watakatifu walipo duniani : ndio walio bora, hao ndio niliopendezwa nao.

4. Huzuni zao zitaongezeka wambadilio Mungu kwa mwininge : sitazimimina sadaka zao za damu, wala kuyataja majina yao midomoni mwangu.

5. Yehova ndiye fungu la posho langu, na la kikombe changu : wewe unaishika kura yangu.

6. Kamba zangu zimeniangukia mwahali mwema : naam, nimepata urithi mzuri.

7. Nitamhimidi Yehova aliyenipa shauri : naam, mtima wangu hunifundisha usiku.

8. Nimemweka Yehova mbele yangu daima : kwa kuwa yu katika mkono wangu wa kuume sitaondoshwa.

9. Kwa hiyo moyo wangu unafurahi, nao utukufu wangu unashangiria : naam, mwili wangu nao utakaa kwa salama.

10. Kwani hutaiachia kuzimu nafsi yangu : wala hutamtoa mpendwa wako aone uharibifu.

11. Utanijulisha njia ya uzima : mbele ya uso wako ziko furaha tele, na katika mkono wako wa kuume mna mema ya milele.

ZABURI 17

USIKIE haki, ewe Yehova, usikilize kilio changu : utege sikio lako kwa maombi yangu, yasiyotoka katika midomo yenye hila.

2. Hukumu yangu na itoke kwako : macho yako na yatazame mambo ya adili.

3. Umenijaribu moyo wangu, umenijilia usiku, umenihakikisha usione neno : nimekusudia kinywa changu kisikose.

4. Kwa habari za matendo ya wanadamu : kwa neno la midomo yako pimejiepusha na njia za wenye jeuri.

5. Nyayo zangu zimeshikamana na njia zako : hatua zangu hazikuteleza.

6. Nimekulingana kwa maana utanijibu, ewe Mungu : utege sikio lako uyasikie maneno yangu.

7. Dhihirisha fadhili zako za ajabu, wewe uwaokoaye wanaokukimbilia : kwa mkono wako wa kuume *uwaokoe* na hao wanaowaondokea.

8. Unilinde kama mboni wa jicho : unifiche chini ya uvuli wa mbawa zako,

9. Wasiniione wasio haki wanaonionea : adui za roho yangu wanaonizunguka.

10. Warnezibikana kwa kuwanda kwao : kwa vinywa vyao hutoa majivuno.

11. Sasa wametuzunguka hatua zetu : wameyakaza macho yao watuangshe chini.

12. Yeye ni kama simba atakaye kurarua : kama mwana simba aoteaye katika maoteo yake.

13. Uondoke, ewe Yehova, ukutane naye umwina-mishe : uiokoe nafsi yangu na mtu aziye haki kwa upanga wako ;

14. *Unioke* na watu, ewe Yehova, kwa mkono wako ; watu wa dunia hii ambafungu lao ni katika maisha haya ; matumbo yao wayajaza kwa hazina yako : hushiba wana, huwaachia watoto wao mabaki ya mali yao.

15. Bali mimi nitakutazama uso wako katika haki : niamkapo nitashibishwa kwa mfano wako.

Siku 3. Sala ya fioni

ZABURI 18

NAKUPENDA sana, ewe Yehova, nguvu zangu.

2. Yehova ni jabali langu na boma langu na mwokozi wangu ; Mungu wangu, mwamba wangu, nitamkimbilia : ngao yangu na pembe ya wokofu wangu na ngome yangu.

3. Nitamlingana Yehova astahiliye kusifiwa : nami hivyo nitaokoka na adui zangu.

4. Kamba za mauti zilinizinguka : mafuriko ya uovu yakanitia hofu.

5. Kamba za kuzimu zilinizinguka : mitego ya mauti ikanipata.

6. Katika shida yangu nilimlingana Yehova, na kula-lamikia Mungu wangu : akaisikia sauti yangu hekaluni mwake, kilio changu mbele zake kikaingia masikioni mwake.

7. Ndipo nchi ilipotikisika na kutetemeka : misingi ya milima ikataharuki, ikatikisika kwa sababu alikuwa na ghadhabu.

8. Kukapanda moshi kutoka puanı mwake ; moto ukatoka kinywani mwake ukala : makaa yakawashwa nao.

9. Aliziinamisha mbingu akashuka : kukawa na giza kuu chini ya miguu yake.

10. Akapanda juu ya kerubi akaruka : naam, aliruka upesi juu ya mabawa ya upepo.

11. Alifanya giza kuwa pahali pake pa kujificha, kuwa hema lake la kumzunguka : giza la maji mengi, mawingu makuu ya mbinguni.

12. Toka mwangaza uliokuwa mbele zake kukapita-mawingu yake makuu : mvua ya mawe na makaa ya moto.

13. Yehova akapiga radi mbinguni ; yeye aliye juu akatoa sauti yake : mvua ya mawe na makaa ya moto.

14. Akaipiga mishare yake akawatawanya : akatoa umeme mwingu sana, akawatapanya.

15. Ndipo ilipoonekana mikondo ya maji, misingi ya ulimwengu ikakashifiwa : kwa kukemea kwako, ewe Yehova, kwa mvumo wa pumzi ya puanı mwako.

16. Alipeleka kutoka juu akanishika : akanitoa katika maji mengi.

17. Akanikoa na adui wangu mwenye nguvu : na wale walionichukia, kwani walikuwa na nguvu kuliko mimi.

18. Walinishambulia siku ya msiba wangu : lakini Yehova alikuwa tegemeo langu.

19. Akanitoa akanipeleka pahali peupe : aliniponya kwa kuwa alipendezwa nami.

20. Yehova alinitendea kwa kadiri ya haki yangu : kwa kadiri ya utakatifu wa mikono yangu akanilipa.

21. Kwani nimezishika njia za Yehova : wala sikumwasi Mungu wangu.

22. Hukumu zake zote zilikuwa mbele yangu : wala amri zake sikujiepusha nazo.
23. Nami nilikuwa mkamilifu mbele zake : nikajilinda na uovu wangu.
24. Basi Yehova amenilipa kwa kadiri ya haki yangu : kwa kadiri ya utakatifu wa mikono yangu machoni pake.
25. Kwa mtu mwenye fadhili utakuwa mwenye fadhili : kwa mtu mkamilifu utajionyesha kuwa mkamilifu.
26. Kwa mtu aliyejitatasa utajionyesha kuwa mtakatifu : na kwa mtu mpotofu utajionyesha kuwa mkaidi.
27. Kwani wewe utawaokoa watu wanaoonewa : na macho ya kiburi utayadhilli.
28. Kwa kuwa wewe utaiwasha taa yangu : Yehova Mungu wangu ataniangazia giza langu.
29. Kwani kwa msaada wako nafuatia jeshi : kwa msaada wa Mungu wangu naruka ukuta.
30. Mungu, njia yake ni kamilifu ; neno la Yehova limehakikishwa : yeye ni ngao ya watu wote wanaomkimbilia.
31. Kwani ni nani aliye Mungu ila Yehova ? Ni nani aliye mwamba ila Mungu wetu ?
32. Mungu anifungaye mshipi wa nguvu : naye anaifanya kamilifu njia yangu.
33. Miguu yangu anaifanya kuwa kama ya kulungu : ananisitamisha mwahali mwangu mwa juu :
34. Ananifundisha mikono yangu vita : hata mikono yangu ikaupinda uta wa shaba.
35. Nawe umenipa ngao ya wokofu wako : mikono wako wa kuume umenitegemeza, na unyenyekevu wako umenikuza.
36. Umenifanyizia nafasi kwa hatua zangu : na miguu yangu haikuteleza.
37. Nitawafuatia adui zangu na kuwapata : wala sitarudi nyuma hata wakomeshe.
38. Nitawapiga-piga wasiweze kusimama : wataanguka chini ya miguu yangu.
39. Nawe umenifunga mshipi wa nguvu kwa vita : umenituishia chini yangu walioniondokea.

40. Naam, adui zangu umewafanya wanipe visogo : ili niwakatilie mbali walionichukia.
41. Walipiga yowe, lakini hakuna wa kuokoa : *walimlingana* Yehova lakini hakuwajibu.
42. Nikawaponda kama mavumbi mbele ya upepo : nikawatupilia mbali kama matope ya njiani.
43. Umeniokoa na mashindano ya watu, umenifanya kichwa cha mataifa : watu nisiowajua watanitumikia.
44. Wakisikisa habari zangu, mara watanitii : wageni watakuja kwangu wakinyenyekrea.
45. Wageni watatepetea : watatoka katika ngome zao wakitetemeka.
46. Yehova yu hai ; na ahimidiwe mwamba wangu : na afukuzwe Mungu wa wokofu wangu :
47. Yeye ambaye ni Mungu anipatiaye kisasi : huwatisha watu chini yangu.
48. Huniponya na adui zangu : naam, waniinua juu ya adui zangu, na kuniponya na mtu wa jeuri.
49. Kwa hiyo nitakushukuru kati ya mataifa, ewe Yehova : nami nitazimba sifa za jina lako.
50. Humpa mfalme wake wokofu mkuu : humfanyia fadhili Masihi wake, Daudi na mzao wake, hata milele.

Siku 4. Sala ya Asubuki

ZABURI 19

- M**BINGU zauhubiri utukufu wa Mungu : na anga yaitangaza kazi ya mikono yake.
2. Mchana husemezana na mchana : usiku hutolea usiku maarifa.
 3. Hakuna lugha wala maneno : sauti yao haisikilikani.
 4. Kanuni yao imeenea duniani mote, na maneno yao hata miisho ya ulimwengu : katika hizo ameliwkeea jua hemu.
 5. Ambalo ni kama bwana arusi atokaye chumbani mwake : lafurahi kama mtu aliye hodari kwenda mbio katika njia yake.
 6. Kutoka kwake lautoka mwisho wa mbingu, na

kuzunguka kwake hata miisho yake : wala kwa hari yake hakuna kitu kilichofichwa.

7. Sheria ya Yehova ni kamilifu, huiburudisha nafsi : usuhuda wa Yehova ni amini, humtia mjinga hekima.

8. Maagizo ya Yehova ni ya adili, huufurahisha moyo : amri ya Yehova ni safi, tuyatia macho nuru.

9. Kumcha Yehova ni kutakatifu, kunadumu milele : hukumu za Yehova ni kweli, zina haki kabisa :

10. Ni za kutamaniwa kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi : nazo ni tamu kuliko asali, naam, kuliko sega la asali.

11. Tena mtumishi wako huonywa nazo : katika kuzishika kuna thawabu nydingi.

12. Ni nani awezaye kuyatambua makosa yake : unitakase na *mambo* ya siri.

13. Umzuie mtumishi wako asitende mambo ya kiburi, yasinitawale mimi : ndipo nitakapokuwa kamili, nami nitakuwa safi, sina kosa lililo kubwa.

14. Maneno ya kinywa changu, na mawazo ya moyo wangu : yapate kibali mbele zako, ewe Yehova, mwamba wangu na mwokozi wangu.

ZABURI 20

YEHOVA akujibu siku ya dhiki : jina la Mungu wa Yakobo likuinue ;

2. Akupelekee msaada toka pahali patakatifu pake : na kukutegemeza toka Zayuni ;

3. Azikumbuke sadaka zako zote : na kuzikubali sadaka zako za kuteketezwa ;

4. Akujalie kwa kadiri ya haja ya moyo wako : na kuyatimiza mashauri yako yote.

5. Tutashangiria wokofu wako, na kwa jina la Mungu wetu tutazipepeza bendera zetu : Yehova akutimizie maombi yako yote.

6. Sasa najua ya kuwa Yehova amwokoa Masihi wake : atamjibu toka mbingu zake takatifu kwa matendo makuu ya wokofu ya mkeno wake wa kuume.

7. Hawa *wanataja* magari na hawa farasi : bali sisi tutalitaja jina la Yehova Mungu wetu.

8. Wao wameinama na kuanguka : bali sisi tumeinuka na kusimama.

9. Uokoe, ewe Yehova : mfalme na atuitike tuitapo.

ZABURI 21

MFALME atazifurahia nguvu zako, ewe Yehova : na wokofu wako ataufanya shangwe kwa jinsi gani !

2. Umempa haja ya moyo wake : wala hukumzuilia hayo aliyoyataka kwa midomo yake.

3. Kwani umemtangulizia baraka za heri : umemvika taji ya dhahabu safi kichwani mwake.

4. Alikuumba uhai ukampa : muda mrefu wa siku nydingi, hata milele na milele.

5. Utukufu wake ni mkuu kwa wokofu wako : heshima na adhama waweka juu yake.

6. Kwani unamfanya kubarikiwa sana milele : wamfurahisha kwa furaha ya uso wako.

7. Kwa kuwa mfalme humtumaini Yehova : na kwa fadhili zake aliye juu hataondoshwa.

8. Mkono wako utawapata adui zako wote : mkono wako wa kuume utawapata wanaokuchukia.

9. Utawafanya kuwa kama tanuru ya moto wakati wa ghadhabu yako : Yehova atawameza kwa ghadhabu yake, na moto utawala.

10. Matunda yao utayaharibu na kuyaondoa katika nchi : na wazao wao katika wanadamu.

11. Kwa kuwa walikusudia kukutenda mabaya : waliwaza hila wasipate kuitimiza.

12. Kwa maana utawafanya kukupa visogo : nyusoni mwao utaziweka tayari nyuzi za nyuta zako.

13. Utukuzwe, ewe Yehova, kwa nguvu zako : nasi tutaimba na kuuhimidi uwemo wako.

Siku 4. Sala ya Jioni

ZABURI 22

MUNGU wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha : mbona u mbali na wokofu wangu, na maneno ya kuugua kwangu ?

2. Ewe Mungu wangu, nalia mchana lakini hujibu : na wakati wa usiku wala sinyamai.
3. Ila wewe u mtakatifu : uketiye juu ya sifa za Isiraeli.
4. Baba zetu walikutumaini wewe : walitumaini nawe ukawaokoa.
5. Walikilia wewe wakaokoka : walikutumaini wala hawakuabika.
6. Lakini mimi ni mdudu wala si mtu : laumu ya wanadamu na mzaha wa watu.
7. Wote wanionao hunicheka sana : hunifyonya wakitisika vichwa vyao,
8. Umtegemee Yehova ; na amponye : na amwokoe sasa, kwani apendezwa naye.
9. Naam, wewe ndiwe ulienitoa tumboni : ulinitumainisha nilipokuwa maziwani mwa mama yangu.
10. Kwako nilitupwa tokea tumboni : toka tumboni mwa mama yangu ndiwe Mungu wangu.
11. Usiwe mbali nami kwani taabu i karibu : kwa maana hakuna msaidizi.
12. Mafahali wengi wamenizunguka : walio hodari wa Bashani wamenisonga.
13. Wanafumbulia vinywa vyao : kama simba apuraye na kunguruma.
14. Nimemwagika kama maji ; mifupa yangu yote imeteguka : moyo wangu umekuwa kama nta, umeyeyuka ndani ya mtima wangu.
15. Nguvu zangu zimekauka kama gae ; ulimi wangu waambatana na taya zangu : umeniweka katika mavumbi ya mauti.
16. Kwa maana mbwa wamenizunguka ; kusanyiko la waovu wamenisonga : wamenichoma mikono na miguu.
17. Naweza kuhesabu mifupa yangu yote : wao wanantazama na kunikodolea macho.
18. Wanagawanya nguo zangu : na vazi langu wanalipigia kura.
19. Nawe, Yehova, usiwe mbali : ewe nguvu zangu, fanya haraka kunisaidia.
20. Uniponye nafsi yangu na upanga : mpenzi wangu na nguvu za mbwa.

21. Kinywani mwa simba unioke : naam, toka pembe za nyati umenijibu.
22. Nitalihubiri jina lako kwa ndugu zangu : katikati ya kusanyiko nitakusifu.
23. Ninyi mnaomcha Yehova, msifuni : enyi nyote mlilo wazo wa Yakobo, mtukuzeni ; mcheni, enyi nyote mlilo wazo wa Isiraeli.
24. Kwani hakulidharau teso la mteswa, wala haku-chukizwa nalo, wala hakumficha uso wake : bali alipo-mlilia akamsikia.
25. Kwako zinatoka sifa zangu katika kusanyiko kubwa : nitaziondoa nadhiri zangu mbele yao wamichao.
26. Wapole watakula na kushiba : warntafutao Yehova watamsifu, miyo yenu na iihi milele ;
27. Walioko ncha zote za dunia watakumbuka na kum-rejea Yehova : jamaa zote za mataifa wasatusudu mbele zako.
28. Kwani ufalme una Yehova : naye ndiye awatawalaye mataifa.
29. Waliowanda wote wa dunia watakula na kusujudu ; mbele zake watainama wote washukao mavumbini : naam, ye ye asiyeweza kuihuisha nafsi yake.
30. Wazao wake watamtumikia : zitasimuliwa habari za Yehova kwa kizazi kitakachokuja.
31. Watakuja na kuwahubiria watakaozaliwa haki yake : ya kwamba ndiye aliyeyafanya haya.

ZABURI 23

- YEHובה** ni mchunga wangu : sitapungukiwa na kitu.
2. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza : kando ya maji ya utulivu huniongoza.
 3. Hunihuisha nafsi yangu na kuniongoza : katika mapito ya haki kwa ajili ya jina lake.
 4. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya : kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji.
 5. Waandaa meza mbele yangu machoni pa watesi

wangu : umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika.

6. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu : nami nitakaa nyumbani mwa Yehova muda wa siku nydingi.

Siku 5. Sala ya Asubuhi

ZABURI 24

NCHI na vyote viijazavyo ni mali ya Yehova : dunia na wote wakao ndani yake.

2. Kwani ye ye ndiye aliyeiweka misingi yake juu ya bahari : na juu ya mito ya maji aliihubutisha.

3. Ni nani atakayepanda katika mlima wa Yehova ? Ni nani atakayesimama katika pahali patakatifu pake ?

4. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe, asiyeiinua nafsi yake kwa ubatili : wala hakuapa kwa hilu.

5. Atapokea baraka kwa Yehova : na haki kwa Mungu wa wokofu wake.

6. Hiki ndicho kizazi cha wamtafutao : wakutafutao uso wako, ewe Mungu wa Yakobo.

7. Inueni vichwa vyenu, enyi malango ; inukeni, enyi malango ya milele : Mfalme wa utukufu apate kuingia.

8. Ni nani Mfalme wa utukufu ? Yehova mwénye nguvu na uhodari, Yehova hodari wa vita.

9. Inueni vichwa vyenu, enyi malango ; naam, viueni, enyi malango ya milele : Mfalme wa utukufu apate kuingia.

10. Ni nani huyu Mfalme wa utukufu ? Yehova wa majeshi, ye ye ndiye Mfalme wa utukufu.

ZABURI 25

EWE Yehova : nakuinulia nafsi yangu.

2. Ewe Mungu wangu, nimekutumaini wewe : nisiaibike, adui zangu wasifurahi kwa kunishinda.

3. Naam, wakungojeao hawataaibika hata mmoja : wataaibika watendao hiana bila sababu.

4. Unijulishe njia zako, ewe Yehova : unifundishe mapito yako.

5. Uniongoze katika kweli yako, na kunifundisha : kwani wewe ndiye Mungu wa wokofu wangu ; nakungojea wewe mchana kuchwa.

6. Ukumbuke, ewe Yehova, rehema zako na fadhili zako : kwani zimekuwako tokeza zamani.

7. Usizikumbuke dhambi za ujana wangu, wala maasi yangu : unikumbuke kwa kadiri ya fadhili zako, ewe Yehova, kwa ajili ya wema wako.

8. Yehova ni mwema, ni mwénye adili : kwa hiyo atawafundisha wenye dhambi njia.

9. Wenye upole atawaongoza katika hukumu : wenye upole atawafundisha njia yake.

10. Njia zote za Yehova ni fadhili na kweli : kwao walishikao agano lake na shuhuda zake.

11. Kwa ajili ya jina lako, ewe Yehova : unisamehe uovu wangu, kwani ni mwingu.

12. Ni nani amchaye Yehova : atamfundisha katika njia atakayoichagua.

13. Nafsi yake itakaa hali ya kufanikiwa : wazao wake wataairithi nchi.

14. Siri ya Yehova iko kwa wamchao : naye atawaijulisha agano lake.

15. Macho yangu yamlekea Yehova daima : kwani atanitoa miguu yangu katika wavu.

16. Uniangularie, unifadhili : kwani mimi ni mkiwa na mteswa.

17. Mateso ya moyo wangu yameongezeka : unitoe katika dhiki zangu.

18. Utazame teso langu na taabu yangu : unisamehe dhambi zangu zote.

19. Uwatazame adui zangu, kwani ni wengi : wanachukia kwa machukio ya ukali.

20. Unilinde nafsi yangu, uniponye : nisiaibike, kwani nakukimbilia wewe.

21. Ukamilifu na unyofu zinihifadhi : kwani nakungojea wewe.

22. Umkomboe Israeli, ewe Mungu : katika taabu zake zote.

ZABURI 26

UNIHUKUMU, ewe Yehova, kwani nimekwenda kwa ukamilifu wangu : nami nimemtumaini Yehova, sikusita.

2. Unijaribu, ewe Yehova, na kunipima : unisafishe mrima wangu na moyo wangu.

3. Kwani fadhili zako zipo mbele ya macho yangu : nami nimekwenda katika kweli yako.

4. Sikuketi pamoja na watu wa ubatili : wala sitaingia mnamo wanafiki.

5. Nalichukia kusanyiko la watenda mabaya : wala sitaketi pamoja na wasio haki.

6. Nitanawa mikono yangu kwa kutokuwa na kosa : ndivyo nitakavyozunguka madhabahu yako, ewe Yehova :

7. Ili nipaaze sauti ya kushukuru : niitangaze miujiza yako yote.

8. Ewe Yehova, napenda makao ya nyumba yako : na pahali pa maskani ya utukufu wako.

9. Usitie nafsi yangu pamoja na wenye dhambi : wala maisha yangu pamoja na watu wamwagao damu.

10. Mikononi mwao mna madhara : na mkono wao wa kuume umejaa rushwa.

11. Lakini mimi kwa ukamilifu wangu nitakwenda : unikomboe, unirehemu.

12. Mguu wangu unasimama palipo sawa : katika makusanyiko nitamkuza Yehova.

Siku 5. Sala ya Jioni

ZABURI 27

YEHOVA ni nuru yangu na wokofu wangu, nimwo-gope nani? Yehova ni ngome ya uzima wangu, nimhofu nani?

2. Watenda mabaya waliponikaribia wanile nyama yangu ; watesi wangu na adui zangu, walijikwaa wakaangukua.

3. Jeshi lijapoipanga kupigana nami, moyo wangu hautaogopa : vita ijaponiondokea, hata hapo nitatumaini.

4. Neno moja nimelitaka kwa Yehova, nalo ndilo nitakalotafuta : nikae nyumbani mwa Yehova siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Yehova, na kufikiri hekaluni mwake.

5. Kwani atanificha bandani mwake siku ya mabaya, katika starehe ya hema lake atanificha : juu ya mwamba ataniinua.

6. Na sasa kichwa changu kitainuka juu ya adui zangu wanaonizunguka : nami nitatoa dhabihu za shangwe hemani mwake ; nitaimba, naam, nitamhimidi Yehova.

7. Usikie, ewe Yehova, ninapolia kwa sauti yangu : unifadhili, unijibju.

8. *Uliponena*, Nitafuteni uso wangu : moyo wangu ulikuambia, Uso wako, ewe Yehova, nitautafuta.

9. Usinifiche uso wako ; usijiepushe na mtumishi wako kwa hasira : umekuwa msaada wangu ; usinitupe, wala usiniache, ewe Mungu wa wokofu wangu.

10. Baba yangu na mama yangu wameniacha : bali Yehova atanikaribisha kwake.

11. Unifundishe njia yako, ewe Yehova : uniongoze katika njia iliyonyoka kwa sababu ya adui zangu.

12. Usinitie katika nia ya adui zangu : kwani mashahidi wa uwongo wameniondokea, nao watoao jeuri kama pumzi.

13. Ningezima roho, kwamba sikuamini ya kuwa nitauona wema wa Yehova : katika nchi ya walio hai.

14. Umngoojee Yehova, uwe hodari : upige moyo konde ; naam, umngoojee Yehova.

ZABURI 28

NITAKULINGANA wewe, Yehova, mwamba wa-nangu ; usiwe kwangu kama kiziwi : nisije nikafanana nao washukao shimonii, ikiwa umeninyamalia.

2. Usikie sauti ya sala zangu nikuombapo : nikipainulia pahali patakatifu pako mikono yangu.

3. Usinikokote pamoja na wasio haki, wala pamoja na watenda maovu : wawaambiao jirani zao maneno ya amani, lakini miyoni mwao mna madhara.

4. Uwape kwa kadiri ya kazi yao, na kwa kadiri ya ubaya wa matendo yao : uwape kwa kadiri ya kazi ya mikono yao, uwalipe stahili zao.

5. Kwani hawazifahamu kazi za Yehova, wala matendo ya mikono yake : atawavunja wala hatawajenga.

6. Na ahimidiwe Yehova : kwani ameiskia sauti ya sala zangu.

7. Yehova ni nguvu zangu na ngao yangu ; moyo wangu umemtumaini, nami nimesaidiwa : basi moyo wangu unashangiria, na kwa wimbo wangu nitamshukuru.

8. Yehova ni nguvu zao *watu wake* : naye ni ngome ya wokofu kwa Masihi wake.

9. Uwaokoe watu wako, uubarikie urithi wako : uwachunge, uwachukue milele.

ZABURI 29

MPENI Yehova, enyi wana wa wenye uwezo : mpeni Yehova utukufu na nguvu.

2. Mpeni Yehova utukufu wa jina lake : mwabuduni Yehova kwa uzuri wa utakatifu.

3. Sauti ya Yehova i juu ya maji : Yehova, ye ye Mungu wa utukufu, hupiga radi juu ya maji mengi.

4. Sauti ya Yehova ina nguvu : sauti ya Yehova ina adhama.

5. Sauti ya Yehova yaivunja mierezi : naam, Yehova aiunja-vunja mierezi ya Lebanon.

6. Airusha-rusha kama ndama ya ng'ombe : Lebanoni na Sirioni kama mwana nyati.

7. Sauti ya Yehova : yaipasua miali ya moto.

8. Sauti ya Yehova yalitetemesha jangwa : Yehova alitetemesha jangwa la Kadeshi.

9. Sauti ya Yehova yawazalisha ayala, na kuikashifu misitu : na ndani ya hekalu lake wanasema wote, Utukufu.

10. Yehova aliketi juu ya gharika : naam, Yehova ameketi ali mfalme milele.

11. Yehova atawapa watu wake nguvu : Yehova atawabarikia watu wake kwa amani.

Siku 6. Sala ya Asubuhi

ZABURI 30

EWE Yehova nitakutukuza, kwa maana umeniinua : wala hukuwaacha adui zangu wakashangiria juu yangu.

2. Ewe Yehova, Mungu wangu : nilikulilia ukniponya.

3. Umeniinua nafsi yangu, ewe Yehova, kutoka kuzimu : umenihuisha nisishuke shimonii.

4. Mwimbieni Yehova sifa, enyi watakatifu wake : kalishukuruni jina lake takatifu.

5. Kwani ghadhabu zake ni za kitambo ; katika radhi yake mna uhai : labda kilio huja kukaa usiku, lakini asubuhi huwa furaha.

6. Nami nilipofanikiwa niliseema : sitaondoshwa milele.

7. Wewe, ewe Yehova, kwa radhi yako uliuweka imara milima wangu : uliuficha uso wako nami nikafadhaika.

8. Nilikulilia wewe, ewe Yehova : naam, kwa Yehova niliomba sala.

9. Mna faida gani katika damu yangu nishukapo shimonii ? Mavumbi yatakusifu, yataitangaza haki yako ?

10. Usikie, ewe Yehova, unirehemu : ewe Yehova, uwe msaidizi wangu.

11. Umegeuza matanga yangu kuwa machezo : umeniuva gunia, na kunivika furaha :

12. Ili utukufu wangu ukusifu, wala usinyamaze : ewe Yehova, Mungu wangu, nitakushukuru milele.

ZABURI 31

NIMEKUKIMBILIA wewe, ewe Yehova ; nisiaibike milele : kwa haki yako uniponye.

2. Unitegee sikio lako, unioke hima : uwe kwangu mwamba wa nguvu, nyumba yenyе maboma ya kuniokoa.

3. Ndiwe genje langu na ngome yangu : kwa ajili ya jina lako unionongoze, unichunge.

4. Unitoe katika wavu walionitegea kwa siri : kwani wewe ndiwe ngome yangu.
5. Mikononi mwako naiweka roho yangu : umeníkomboea, ewe Yehova, Mungu wa kweli.
6. Nawachukia wao washikao yasiyofaa yenze uwongo : bali mimi namtumaini Yehova.
7. Nitashangiria na kuzifurahia fadhili zako : kwa kuwa umeyaona mateso yangu ; umejua nafsi yangu taabuni ;
8. Wala hukuniacha nikashikwa mikononi mwa adui : miguu yangu umeisimamisha panapo nafasi.
9. Unifadhilli, ewe Yehova, kwani ni katika dhiki : jicho langu limenyauka kwa masumbufu, naam, mwili wangu na nafsi yangu.
10. Kwani maisha yangu yamekoma kwa huzuni, na miaka yangu kwa kuugua : nguvu zangu zinatetemeka kwa sababu ya uovu wangu, na mifupa yangu imekauka.
11. Kwa sababu ya watesi wangu wote nimekuwa laumu, naam, hasa kwa jirani zangu, na kitu cha kutisha kwa rafiki zangu : walioniona njiani walnikimbia.
12. Nimesahauliwa kama mfu asiye kumbukwa : nimekuwa kama chombo kilichovunjika.
13. Kwani nimesikia masingizio ya wengi ; hofu *ziko* pande zote : waliposhauriana juu yangu walifanya hila waiondoe nafsi yangu.
14. Lakini mimi nilikutumaini wewe, ewe Yehova : nilisema, Wewe ndiwe Mungu wangu.
15. Nyakati zangu zimo mikononi mwako : uniponye na mkono wa adui zangu, nao wanaonifuatia.
16. Umwangaze mtumishi wako kwa nuru ya uso wako : uniokoe kwa ajili ya fadhili zako.
17. Usinjache niaibishwe, ewe Yehova, kwani nimekulingana : waaibishwe wasio haki, wanyamaze kuzimuni.
18. Midomo ya uwongo iwe na ububu : inenayo juu ya mwenye haki maneno ya kiburi kwa majivuno na dharaau.
19. Jinsi ilivyo ajabu ya wingi wa fadhili zako ulizowawekea wakuchao : ulizowatendea wakukimbiao mbele ya wanadamu !
20. Utawaficha na fitina za watu katika starehe ya

- kuwapo kwako : utawaficha katika *hema na mashindano* ya ndimi.
21. Yehova ahimidiwe : kwa maana amenitendea fadhili za ajabu katika mji wenye boma.
 22. Nami nilisema kwa haraka yangu, Nimekatiliwa mbali ya macho yako : lakini ulisikia sauti ya sala zangu wakati nilipokulilia.
 23. Mpendeni Yehova, ninyi nyote mlio watakatifu wake : Yehova huwahifadhi waaminifu, humlipa atendaye kiburi malipo tele.
 24. Muwe hodari, mpige moyo konde : ninyi nyote mnaomtumaini Yehova.
- Siku 6. Sala ya Jioni*
- ZABURI 32
- Y**UNA heri aliyesamehewa dhambi : na kufichwa makosa yake.
2. Yuna heri Yehova asiyemhesabia upotofu : ambaye rohoni mwake hamna hila.
 3. Niliponyamaza mifupa yangu ilichakaa : kwa kuugua kwangu mchana kuchwa.
 4. Kwa maana mchana na usiku mkono wako ulinilemea : jasho langu likageuka kuwa kama hari wakati wa kaskazi.
 5. Nilikujulisha dhambi yangu, wala sikuficha upotofu wangu : nilisema, Nitakiri maasi yangu kwa Yehova ; nawe ukaniisamehe upotofu wa dhambi yangu.
 6. Kwa hiyo kila mtu mtawa akuombe wakati unapaptikan : hakika maji makuu yafurikapo hayatamfikia yeeye.
 7. Ndiwe starehe yangu, utanihifadhi na mateso : utanizungusha nyimbo za wokofu.
 8. Nitakufundisha, nitakuonyesha njia utakayoiendea : nitakushauri, jicho langu likikutazama.
 9. Msiwe kama farasi wala nyumbu walio hawana akili ambaeo wasipozuiliwa kwa matandiko ya lijamu na hatamu watakukaribia.
 10. Mtu asiye haki ana mapigo mengi : bali amtu mainiye Yehova fadhili zitamzunguka.

11. Mfurahieni Yehova, shangirieni, enyi wenyе haki : pige ni vigelelele vya furaha, ninyi nyote mlio wanyofu wa moyo.

ZABURI 33

MPIGIENI Yehova vigelelele vya furaha, enyi wenyе haki : kusifu kunawapasa wanyofu wa moyo.

2. Mshukuruni Yehova kwa kinubi : kwa kinanda chenyе nyuzi kumi mwimbieni sifa.

3. Mwimbieni wimbo mpya : pige ni kwa ustadi kwa sauti ya shangwe.

4. Kwani neno la Yehova lina adili : na kazi yake yote hutenda kwa uaminifu.

5. Hupenda haki na hukumu : nchi imejaa fadhili za Yehova.

6. Kwa neno la Yehova mbingu zilifanyika : na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake.

7. Hukusanya maji ya bahari kama chungu : huviweka vilindi katika ghala.

8. Nchi yote na imwogope Yehova : wote wakao duniani na wamche.

9. Kwani ye ye aliсema, ikawa : na ye ye aliamuru, ikasimama.

10. Yehova huyabatilisha mashauri ya mataifa : huya tangua makusudi ya watu.

11. Shauri la Yehova lasimama milele : makusudi ya moyo wake vizazi na vizazi.

12. Lina heri taifa ambalo Yehova ni Mungu wao : watu aliowachagua kuwa urithi wake.

13. Toka mbinguni Yehova huchungulia : huwatazama wanadamu wote pia ;

14. Toka pahali pake aketipo huwaangalia : wote wakao duniani ;

15. Ye ye aiumbaye mioyo yao wote : azifikiri kazi zao zote.

16. Hapana mfalme akokaye kwa wingi wa uwezo : wala shujaa haokoki kwa wingi wa nguvu.

17. Farasi hafai kitu kwa wokofu : wala hamponyi mtu kwa wingi wa nguvu zake.

18. Tazama, jicho la Yehova ni kwao wamchao : wazitumainio fadhili zake ;

19. Ili kuwaponya nafsi zao na mauti : na kuwahuisha wakati wa njaa.

20. Nafsi zetu zimemngojea Yehova : ye ye ndiye msaada wetu na ngao yetu.

21. Kwani mioyo yetu itamfurahia : kwa kuwa tumelitumainia jina lake takatifu.

22. Fadhili zako, ewe Yehova, zikae nasi : kama vile tulivyokungojea wewe.

ZABURI 34

NITAMHIMIDI Yehova kila wakati : sifa zake zitakuwa kinywani mwangu daima.

2. Katika Yehova nafsi yangu itajisifu : wanyenyekevu watasikia na kufurahi.

3. Mtukuzeni Yehova pamoja nami : na tulituke jina lake pamoja.

4. Nilimtafuta Yehova akanijibu : akaniponya na hofu zangu zote.

5. Walimwelekea macho wakatiwa nuru : wala nyuso zao hazitaona haya kamwe.

6. Maskini huyu alitoa sauti, Yehova akasikia : aka mwokoa na taabu zake zote.

7. Malaika wa Yehova huwazungushia boma hao wamchao : na kuwaokoa.

8. Onjeni mwone ya kuwa Yehova yu mwema : yuna heri mtu yule anayetumaini.

9. Mcheni Yehova, enyi watakatifu wake : kwani wamchao hawahitaji kitu.

10. Wana simba hutindikiwa, huona njaa : bali wamtafuta Yehova hawatahitaji kitu chochote kilcho chema.

11. Njoni, enyi watoto, mkanisikilize : nami nitawa fundisheni kumcha Yehova.

12. Ni nani mtu yule apendezwaye na uzima : apendaye siku nyinyi apate kuona mema ?

13. Uuzuie ulimi wako na mabaya : na midomo yako na kusema hila.

14. Uache mabaya ukatende mema : utafute amani ukaiatuatie.

15. Macho ya Yehova huwaelekea wenyе haki ; na masikio yake hukielekea kilio chao.

16. Uso wa Yehova ni juu ya watenda mabaya : aliondoe kumbukumbu lao duniani.

17. Walilia, Yehova akasikia : akawaponya na taabu zao zote.

18. Yehova yu karibu nao waliovunjika moyo : na waliopondeka roho huwaokoa.

19. Mateso ya mwenye haki ni mengi : lakini Yehova humponya nayo yote.

20. Huihifadhi mifupa yake yote : haukuvunjika hata mmoja.

21. Uovu utamuua asiyе haki : nao wamchukiao mwenye haki watahukumiwa.

22. Yehova huzikomboa nafsi za watumishi wake : na wote wamkimbiliao hawatahukumiwa.

Siku 7. Sala ya Asubuhi

ZABURI 35

EWE Yehova, utete nao wanaoteta nami : upigane nao wanaopigana nami.

2. Uishike ngao na kigao : ukasimame unisaidie.

3. Utoe na mkuki uwapinge wanaonifuatia : uiambie nafsi yangu, Mimi ni wokofu wako.

4. Waaibishwe, wafedheheshwe, wanaoitafuta nafsi yangu : warudishwe nyuma, wafadhaishwe, wanaonizulia mabaya.

5. Wawe kama makapi mbele ya upepo : malaika wa Yehova akiwaangusha chini.

6. Njia yao iwe giza na utelezi : Malaika wa Yehova akiwafuatia.

7. Kwani bila sababu wamenifichia mtego : bila sababu wameichimbia shimo nafsi yangu.

8. Uharibifu na umgate kwa ghafula, na wavu aliouficha umnase yeye mwenyewe : kwa uharibifu aanguke ndani yake.

9. Na nafsi yangu itamfurahia Yehova : itaushangiria wokofu wake.

10. Mifupa yangu yote itasema : Ewe Yehova, ni nani aliye kame wewe : umponyaye maskini na mtu aliye hodari kumshinda yeye ; naam, maskini na mhitaji na mtu amtekayea ?

11. Mashahidi wa udhalimu wanasi mama : wananiuliza nisiyoyajua.

12. Wananilipa mabaya kwa wema : hata nafsi yangu ikaingia ukiwa.

13. Bali mimi, walipougua wao, nguo yangu iliкуwa gunia : nilijitesa nafsi yangu kwa kufunga, maombi yangu yalirejea kifuani mwango.

14. Nilijifanya kana kwamba ni rafiki yangu au ndugu yangu : miliinama kama aliyeifiwa na mamaye.

15. Lakini nilipojikwaa walifurahi na kukusanyana : walinikusanyikia watu ovyo nami sikujuia ; wananiparura wala hawakomi :

16. Kama wafanyao mzaha wakikufuru karamuni : wakanisagia meno.

17. Ewe Yehova, hata lini utatazama ? Uiokoe nafsi yangu na maharabu yao : na mpenzi wangu na wana simba.

18. Nitakushukuru katika kusanyiko kubwa : nitakusifu kati ya watu wengi.

19. Usiwaache walio adui zangu bila sababu wanisi-mangize : wanaonichukia bure wasining'ong'e.

20. Kwani hawasemi ya amani : ila huwaza maneno ya hila juu ya watulivu katika nchi.

21. Naam, walinfumbulia vinywa vyao : walisema, Ewe ! ewe ! jicho letu limeona.

22. Umeona, ewe Yehova, usinyamaze : ewe Yehova, usiwe mbali nami.

23. Uamke, uwe macho ili kunipatia hukumu kwa ajili ya madai yangu : ewe Mungu wangu na Bwana wangu.

24. Unihukumu kwa haki yako, ewe Yehova, Mungu wangu : wala usiwaache wanisimangize.

25. Wasise me moyoni, Haya ! ndivyo tutakavyo : wasise me, Tumemmeza.

26. Waaibishwe, wafedheheshwe pamoja, wanaoifurahia hali yangu mbaya : wavikwe aibu na fedheha, wanaojikuza juu yangu.

27. Washangirie na kufurahi, wapendezwao na haki yangu : naam, waseme daima, Atukuzwe Yehova, apendezwaye na amani ya mtumishi wake.

28. Na ulimi wangu utanena haki yako : na sifa zako mchana kuchwa.

ZABURI 36

KUASI kwake mtu asiyé haki hunena moyoni mwanngu : hakuna hofu ya Mungu mbele ya macho yake.

2. Kwa maana hujipendekeza machoni pake : ya kwamba upotofu wake hautatambulikana na kuchukiwa.

3. Maneno ya kinywa chake ni uovu na hila : ameacha kuwa na akili na kutenda mema.

4. Huwaza maovu kitandani pake : hujiweka katika njia isiyo njema, ubaya hauchukii.

5. Fadhili zako, ewe Yehova, zafika hata mbinguni : uaminifu wako hata mawinguni.

6. Haki yako ni kama milima ya Mungu, hukumu zako ni vilindi vikuu : ewe Yehova, unawaokoa wanadamu na nyama.

7. Jinsi zilivyo na thamani hizo fadhili zako, ewe Mungu ! Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa zako.

8. Watashibishwa kwa unono wa nyumba yako : nawe utawanywesha mto wa furaha zako.

9. Kwani kwako wewe iko chemchemi ya uzima : katika nuru yako tutaona nuru.

10. Uwadumishie wakujuao fadhili zako : na wanyofu wa moyo uaminifu wako.

11. Mguu wa kiburi usinikaribie : wala mkono wa wasio haki usinifukuze.

12. Huko ndiko walikoanguka wafanyao maovu : wameangushwa chini wasiweze kusimama.

Siku 7. Sala ya Jioni

ZABURI 37

USIKASIRIKE kwa sababu ya watenda mabaya : usiwahuhsudu wafanyao ubatili.

2. Kwani kama majani watakatiwa mara : kama miche mibichi watanyaauka.

3. Umtumaini Yehova ukatende mema : ukae katika nchi, upendezwe na uaminifu.

4. Nawe ujifurahishe kwa Yehova : naye atakupa haja za moyo wako.

5. Umkabidhi Yehova njia yako : umtumaini naye atafanya.

6. Ataitokeza haki yako kama nuru : na hukumu yako kama aduhuhuri.

7. Ukae kimya mbele za Yehova, ukamngojee : wala usikasirike kwa sababu ya mtu afanikiwaye katika njia yake, kwa sababu ya mtu afanyaye hila.

8. Ukomeshe hasira, uache ghadhabu : usikasirike, mwisho wake ni kutenda mabaya.

9. Kwani watenda mabaya wataharibiwa : bali wamngongo Yehova ndio watakaoirithi nchi.

10. Kwani bado kitambo kidogo asiyé haki hatakuwapo : naam, utapaangalia pahali pake wala hatakuwapo.

11. Bali wenye upole watairithi nchi : watajifurahisha kwa wingi wa amani.

12. Asiyé haki hukusudia mabaya juu ya mwenye haki : na kumsagia meno.

13. Yehova atamcheka : kwani aona kwamba siku yake inakuja.

14. Wasio haki wameuvuta upanga, wamecupinda uta wao : wamwangushe chini maskini na mhitaji, na kuwachinja wenye mwenendo wa unyofu :

15. Upanga wao utaingia miyoni mwao wenye : na nyuta zao zitavunjika.

16. Kidogo alicho nacho mwenye haki ni bora : kuliko wingi wa mali wa wengu wasio haki.

17. Kwani mikono ya wasio haki itavunjika : bali Yehova huwategemeza wenye haki.

18. Yehova anazijua siku za wakamilifu : na urithi wao utakuwa wa milele.

19. Hawataaibika wakati wa ubaya : na siku za njaa watashiba.

20. Bali wasio haki watapotea, nao wamchukiao Yehova watatoweka : kama uzuri wa mashamba, kama moshi watatoweka.

21. Asiy e haki hukopa wala halipi : bali mwenye haki hufadhili, hokarimu.

22. Kwani waliobarikiwa na yeye watairithi nchi : nao walilaaniwa na yeye wataharibiwa.

23. Hatua za mtu zafanywa imara na Yehova : naye aipenda njia yake.

24. Ajapo jikwaa hataanguka chini : kwani Yehova humshika mkono na kumtegemeza.

25. Nilikuwa kijana nami sasa ni mzee : lakini sija-mwona mwenye haki ameachwa, wala mzao wake akiomba chakula.

26. Mchana kuchwa hufadhili na kukopesh : na mzao wake hubarikiwa.

27. Jiepue na uovu, ukatende mema : na kukaa hata milele.

28. Kwa kuwa Yehova hupenda haki, wala hawaachi watakatifu wake ; wao hulindwa milele : bali wana wa wasio haki wataharibiwa.

29. Wenye haki watairithi nchi : nao watakaa humo milele.

30. Kinywa cha mwenye haki hunena hekima : na ulimi wake husema hukumu.

31. Sheria ya Mungu wake imo moyoni mwake : hatua zake hazitelez.

32. Mtu asiy e haki humvizia mwenye haki : na kutafuta jinsi ya kumiua.

33. Yehova hatamwacha mkononi mwake : wala hata-mlaamu atakapohukumiwa.

34. Wewe umngojee Yehova, uishike njia yake ; naye atakutukuza uirithi nchi : wasio haki watakapoharibiwa utaona.

35. Nimemwona mtu asiy e haki ali na uwezo mwingu : akijieneza kama mtende katika udongo wake wa asili.

36. Akapita mtu, na kumbe ! hayuko : naam, nikamtafuta wala hakuonekana.

37. Umwangalie sana mtu mkamilifu, umtazame mtu mnyofu : kwani mwisho wake mtu huyo ni amani.

38. Wakosaji wataangamizwa pamoja : wasio haki mwisho wao wataharibiwa.

39. Na wokofu wa wenye haki una Yehova : ye ye ni ngome yao wakati wa taabu.

40. Naye Yehova huwasaidia na kuwaopoa ; huwaopoa na wasio haki na kuwaokoa : kwa kuwa wamemtumaini ye ye.

Siku 8. Sala ya Asubuhi

EWE Yehova, usinilaumu kwa ghadhabu yako : wala usiniadhibu kwa ukali wa hasira yako.

2. Kwa maana mishare yako imenichoma : na mkono wako umenipata.

3. Hamna uzima katika mwili wangu kwa sababu ya ghadhabu yako : wala hamna amani mifupani mwangu kwa sababu ya hatia zangu.

4. Kwani dhambi zangu zimenifunikiza kichwa : kama mzigo mzito zimenilemea mno.

5. Majeraha yangu yananuka, yameoza : kwa sababu ya upumbavu wangu.

6. Nimepindika na kuinama sana : mchana kuchwa nimekwenda nikihuzunika.

7. Kwani viuno vyangu vimejaa homa : wala hamna uzima katika mwili wangu.

8. Nimedhoofika na kuchubuka sana : nimeugua kwa ajili ya fadhaa ya moyo wangu.

9. Ewe Bwana, haja zangu zote ziko mbele zako : kuugua kwangu hakukufichwa kwako.

10. Moyo wangu unapwita-pwita ; nguvu zangu zimeniacha : nuru ya macho yangu nayo imeniondokea.

11. Wanipendao na rafiki zangu wanasi mama mbali ya pigo langu : karibu zangu wamesimama mbali.

12. Nao wanaoitafuta nafsi yangu hutega mitego : nao wanaotaka kunidhuru hunena mabaya, na kufikiri hila mchana kuchwa.

13. Lakini kama kiziwi sisikii : nami ni kama bubu asiyejumbua kinywa chake.

14. Naam, nimekuwa kama mtu asiyesikia : ambaye hamna hoja kinywani mwake.

15. Kwa kuwa nakutumaini wewe, ewe Yehova : utajibu wewe, ewe Yehova Mungu wangu.

16. Kwani nilisema, Wasije wakanfurahia : mguu wangu ukiteleza wajitukuzu juu yangu.

17. Kwa maana mimi ni karibu ya kusita : na maumivu yangu yako mbele yangu daima.

18. Kwa maana nitaungama uovu wangu : nitasikitikia dhambi yangu.

19. Lakini adui zangu ni wa'zima wenye nguvu : nao wanaonichukia bure wamekuwa wengi.

20. Walipao mabaya kwa mema huwa adui zangu : kwa kuwa nalifuata lililo jema.

21. Usiniache, ewe Yehova : ewe Mungu wangu, usijitenge nami.

22. Ufanye haraka kunisaidia : ewe Yehova, wokofu wangu.

ZABURI 39

NILISEMA, Nitazitunza njia zangu, nisije nikakosa kwa ulimi wangu : nitazuia kinywa changu kwa ukanda, akiwapo mbele yangu yule mbaya.

2. Nilikuwa sisemi, nilinyamaa kimya, nisitamke hata neno jema : maumivu yangu yakazidi.

3. Moyo wangu ukawa moto ndani yangu, na katika kuwaza kwangu moto ukawaka : nilisema kwa ulimi wangu ;

4. Ewe Yehova, unijulishe mwisho wangu, na kiasi cha siku zangu ni kiasi gani : njue jinsi nilivyo dhaifu.

5. Tazama, umefanya siku zangu kuwa mashubiri, maisha yangu kama si kitu mbele zako : ubatili tu ni kila mwanadamu ingawa amesitawi.

6. Binadamu huenda tu huko na huko kama kivili, hufanya ghasia tu kwa ajili ya ubatili : huweka akiba wala hajui ni nani atakayeichukua.

7. Na sasa ninangojea nini, ewe Yehova : matumaini yangu ni kwako.

8. Uniokoe na maasi yangu yote : usinifanye laumu ya wapumbau.

9. Nilinyamaza sikufumbua kinywa changu : kwani wewe ndiwe uliyecifanya.

10. Uniondolee pigo lako : kwa uadui wa mkono wako nimeangamia.

11. Ukimrudi mtu kwa kumkemea kwa ajili ya uovu wake, watowesha uzuri wake kama nondo : ubatili tu ni kila mwanadamu.

12. Usikie maombi yangu, ewe Yehova, utege sikio lako niliapo, usiyanyamalie machozi yangu : kwa maana mimi ni mgeni wako, misafiri kama baba zangu wote.

13. Uniachilie nipate nafuu : kabla sijaondoka nisiwepo tena.

ZABURI 40

NILIMNGOJEA Yehova kwa uvumilivu : akanii-namia akasikia kilio changu.

2. Akanipandisha toka shimo la uharibifu, toka udongo wa utelezi : akaisimamisha miguu yangu mwambani, akazifanya imara hatua zangu.

3. Akatia wimbo mpya kinywani mwangu, ndio sifa zake Mungu wetu : wengi wataona na kuogopa, nao wata-mtumaini Yehova.

4. Yuna heri mtu yule aliyemfanya Yehova kuwa tumaini lake : wala hakuwaelekea wenye kiburi, nao wanaogeukia uwongo.

5. Ewe Yehova Mungu wangu, umefanya kwa wingi miujiza yako na mawazo yako kwetu ; hakuna awezaye kuyapanga mbele zako : kama ningependa kutangaza na kuhubiri, ni mengi sana hayahesabiki.

6. Dhabihu na toleo hukupendezwa nazo ; masikio yangu umeyazibua : kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka.

7. Ndipo nilisema, Tazama nimekuja : katika gombo la chuo nimeandikiwa :

8. Niyafanye mapenzi yako, ewe Mungu wangu, ndiyo yanipendezayo : naam, sheria yako imo moyoni mwangu.

9. Nimehubiri habari njema za haki katika kusanyiko kubwa : naam, sitaizua midomo yangu, ewe Yehova, wewe unajua.

10. Sikuficha haki yako moyoni mwangu, nimetangaza uaminifu wako na wokofu wako : sikuficha fadhili zako na kweli yako katika kusanyiko kubwa.

11. Nawe, ewe Yehova, usiniziulie rehema zako : fadhili zako na kweli yako zinilinde daima.

12. Kwa maana mabaya yasiyohesabika yameni-zunguka mimi ; maovu yangu yamenipata hata siwezi kuinua macho : yamezidi kuliko nywele za kichwa changu, na moyo wangu umeniacha.

13. Ewe Yehova, uwe radhi kuniokoa : ewe Yehova, unisaidie hima.

14. Waaibike, wafedheheke pamoja, wanaoitufuta nafsi yangu waiangamize : warudishwe nyuma, watahayarishe, wapendezwao na shari yangu.

15. Wakae hali ya ukiwa kwa sababu ya aibu yao : wanaoniambia, Ewe ! Ewe !

16. Washangirie, wakafurahie, wote wakutafutao : waupendao wokofu wako waseme daima, Atukuzwe Yehova.

17. Nami ni maskini na mhitaji ; Bwana hunitunza : ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu ; ewe Mungu wangu usikawie.

Siku 8. Sala ya Jioni

ZABURI 41

YUNA heri amkumbukaye maskini : Yehova atamwokoa siku ya taabu.

2. Yehova atamlinda na kumhifadhi hai, naye atafanikiwa katika nchi : wala usimtie katika hali wamtakiayo adui zake.

3. Yehova atamtegemeza alipo mgonjwa kitandani : watandika matandiko yake katika ugonjwa wake.

4. Nilisema, Ewe Yehova, unifadhili : uniponye nafsi yangu kwani nimekutendea dhambi.

5. Adui zangu wanantaja kwa maneno mabaya : *wakisema*, Atakufa lini, jina lake likapotea ?

6. Na *mmoja wao* akija kunitazama asema uwongo : moyo wake hujikusanya maovu, naye atokapo nje huyanena.

7. Wote wanaonichukia waninaninong'ona : wananiwazia mabaya.

8. *Wasema*, Neno la uovu limemgandama : na iwapo amelala hatasimama tena.

9. Msiri wangu naye niliyemtumainji, aliyekula chakula changu : ameniinulia kisigino chake.

10. Lakini wewe, ewe Yehova, unifadhili : uniinue nipaye kuwalipa.

11. Kwa neno hili najua ya kuwa wapendezwa nami : kwa kuwa adui yangu hapigi kelele za furaha kwa kuni-shinda.

12. Nami katika ukamilifu wangu wanitegemeza : na kuniweka mbele ya uso wako milele.

13. Na atukuzwe Yehova, Mungu wa Isiraeli : tangu milele hata milele. Amina. Amina.

ZABURI 42

KAMA kulungu aioneavyo shauku mito ya maji : vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, ewe Mungu.

2. Nafsi yangu inamwonea kiu Mungu, Mungu aliye hai : nitakuja lini nioneokane mbele za Mungu ?

3. Machozi yangu yamekuwa chakula changu mchana na usiku : wanaponiambia mchana kuchwa, Yuko wapi Mungu wako ?

4. Nayakumbuka haya nikiweka wazi nafsi yangu ndani yangu, jinsi niliyokuwa nikienda na mkutano : na kuwaongoza nyumbani kwa Mungu, kwa sauti ya furaha na kusifu, mkutano wa siku kuu.

5. Kwa nini umeinama, nafsi yangu, na kufadhaika

ndani yangu ? Umtumainie Mungu, kwa maana nitakuja kumsifu kwa afya ya uso wake.

6. Ewe Mungu wangu, nafsi yangu imeinama ndani yangu, kwa hiyo nakukumbuka : toka nchi ya Yorodani, na Maherimoni, na toka kilima cha Mizari.

7. Kilindi chaita kilindi kwa sauti ya maboromoko ya maji yako : gharika zako zote na mawimbi yako yote yamepita juu yangu.

8. Mchana Yehova ataagiza fadhili zake, na usiku wimbo wake utakuwa nami : naam, sala kwa Mungu wa uhai wangu.

9. Nitamwambia Mungu mwamba wangu, Kwa nini umenisahau ? Kwa nini ninakwenda nikihuzunika, adui wakinionea ?

10. Watesi wangu hunitukana kama kuniponda mifupa yangu : kwa kuniambia mchana kuchwa, Yuko wapi Mungu wako ?

11. Kwa nini umeinama, roho yangu, na kufadhaika ndani yangu ? Umtumainie Mungu, kwa maana nitakuja kumsifu, aliye afya ya uso wangu na Mungu wangu.

ZABURI 43

UNIHUKUMU, ewe Mungu, unitetee kwa taifa lisilo haki : uniokoe na mtu wa hila asiyé haki.

2. Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wa nguvu zangu : kwa nini umenifukuza ? Kwa nini ninakwenda nikihuzunika, adui wakinionea ?

3. Niletée nuru yako na kweli yako, viniongoze : vinifikishe kwenye mlima wako mtakatifu na hata maskani yako.

4. Hivyo nitakwenda madhabahuni kwa Mungu, kwa Mungu aliye furaha yangu na shangwe langu : nitakusifu kwa kinubi, ewe Mungu, Mungu wangu.

5. Kwa nini umeinama, nafsi yangu, na kufadhaika ndani yangu ? Umtumainie Mungu, kwa maana nitakuja kumsifu, aliye afya ya uso wangu na Mungu wangu.

Siku 9. Sala ya Asubuhi

ZABURI 44

EWE Mungu, tumesikia kwa masikio yetu, baba zetu wametuambia : matendo uliyoyatenda siku zao, siku za kale.

2. Wewe kwa mkono wako uliwafukuza mataifa, ukawakalisha wao : uliwatesa watu wa nchi, ukawaeneza wao.

3. Kwani si kwa upanga wao walivyoiimilki nchi wala si mkono wao uliowaokoa : bali mkono wako wa kuume ; naam, mkono wako na nuru ya uso wako, kwa kuwa uliwaridhia.

4. Wewe ndiwe Mfalme wangu, ewe Mungu : uagize mambo ya wokofu kwa Yakobo.

5. Kwa nguvu zako tutawaangusha adui zetu : kwa jina lako tutawakanyaga watupingao.

6. Kwani sitautumaini uta wangu : wala upanga wangu hautaniokoa.

7. Bali wewe ndiwe uliyetuokoa na adui zetu : na watuchukiao umewaaibisha.

8. Tumejisifia Mungu mchana kuchwa : na jina lako totalishukuru milele.

9. Lakini sasa umetutupa, umetufedhehesha : wala hutoki na majeshi yetu.

10. Waturudisha nyuma tukampa adui visogo : na watuchukiao wanajipatia mateka.

11. Umetutoa kama kondoo tuwe chakula : na kutuwanya kati ya mataifa.

12. Wawaiza watu wako bila kupata mali : wala hukupata faida kwa tharmani yao.

13. Umetufanya kuwa laumu kwa jirani zetu : mzaha na dhihaka kwao wanaotuzunguka.

14. Umetufanya kuwa methali kwa mataifa : *sababu ya kutikisa kichwa kwa watu wa nchi*.

15. Mchana kuchwa fedheha yangu i mbele yangu : na haya ya uso wangu imenifunika,

16. Kwa sababu ya sauti ya mtu mwenye kulaumu na kukufuru : kwa sababu ya adui na mijilipiza kisasi.

17. Haya yote yametupata lakini hatukukusahau : wala hatukulihalifu agano lako.

18. Hatukuiacha miyo yetu irudi nyuma : wala hatua zetu hazikuiacha njia yako ;

19. Ingawa umetuponda katika kao la mbwa wa mwitu : ukatufunika kwa uvuli wa mauti.

20. Ikiwa turnelisahau jina la Mungu wetu : au kumnyoshea mungu mgeni mikono yetu ;

21. Je, Mungu hatalipeleza neno hilo ? Kwani ndiye azijuaye siri za moyo.

22. Hasha ! kwa ajili yako tunauawa mchana kuchwa : tunahesabiwa kama kondoo waendao kuchinjwa.

23. Amka, kwa nini umelala, ewe Bwana : uondoke, usitutupe kabisa.

24. Kwa nini unatuficha uso wako : na kusahau kuonewa kwetu na kudhilimiwa kwetu ?

25. Kwani nafsi zetu zimeinama mavumbini : matumbo yetu yameigandama nchi.

26. Uondoke, uwe msaada wetu : utukomboe kwa ajili ya fadhilli zako.

ZABURI 45

MOYO wangu umefurika kwa neno jema : mimi nasema niliyomfanyizia Mfalme : ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi mstadi.

2. Wewe u mzuri sana kuliko wanadamu, neema imemiminiwa midomoni mwako : kwa hiyo Mungu amekubarikia hata milele.

3. Jifungie upanga wako pajani, wewe uliye hodari : utukufu wako na fahari yako.

4. Katika fahari yako usitawi uendelee, kwa ajili ya kweli na upole na haki : na mkono wako wa kuume utakufundisha mambu ya kutisha.

5. Mishare yako ni mikali, watu huanguka chini yako : imo miyoni mwa adui za Mfalme.

6. Kiti chako cha enzi, ewe Mungu, ni cha milele : simbo ya enzi ya ufalme wako ni simbo ya adili.

7. Umeipenda haki, umeichukia dhulumu : kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekupaka mafuta, mafuta ya furaha kuliko wenzako.

8. Mavazi yako yote ni manemane na uudi na mdalasini : katika majumba ya pembe, vinubi vimekufurahisha.

9. Binti za wafalme wamo mionganii mwa kina bibi wako wenye heshima : inkono wako wa kuume amesimama malkia, amevaa dhahabu ya Ofiri.

10. Sikia, binti, utazame, utege sikio lako : uwashahau watu wako na nyumba ya baba yako ;

11. Na Mfalme atautamani uzuri wako : kwani ndiye Bwana wako nawe umsujidie.

12. Na binti Turo *ataleta* kipawa chake : nao matajiri wa watu watajipendeleza kwako.

13. Binti Mfalme yumo ndani ana fahari tupu : mavazi yake ni nyuzi za dhahabu.

14. Atapelekwa kwa Mfalme na mavazi yaliyofumwa kwa uzuri : wanawali wenzake wanaomfuata watapelekwa kwako.

15. Watapelekwa kwa furaha na shangwe : wataingia katika nyumba ya Mfalme.

16. Badala ya baba zako watakuwapo watoto wako : ambao utawafanya kuwa wakuu katika nchi zote.

17. Jina lako nitalifanya kuwa kumbukumbu katika vizazi vyote : kwa hiyo mataifa watakushukuru milele na milele.

ZABURI 46

MUNGU kwetu sisi ni kimbilio na nguvu : msaada uonekanao wakati wa mateso.

2. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi : ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari :

3. Maji yake yajapovuma na kuumka : ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.

4. Kuna mto vijito vyake vyaufurahisha mji wa Mungu : pahali patakatifu pa maskani zake aliye juu.

5. Mungu yu katikati yake hautatetemeshwa : Mungu atausaidia asubuhi na mapema.

6. Mataifa yalighadhabika, falme zikataharuki : alitoa sauti yake, nchi ikayeyuka.
7. Yehova wa majeshi yu pamoja nasi : Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.
8. Njoni mkyayatazame matendo ya Yehova : jinsi alivyofanya ukiwa katika nchi.
9. Akomesha vita hata mwisho wa dunia : auvunja uta, aukata mkuki, ayateketeza magari ya vita motoni.
10. Tulieni, kajueni ya kuwa mimi ni Mungu : nitatukuzwa katika mataifa, nitatukuzwa katika nchi.
11. Yehova wa majeshi yu pamoja nasi : Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.

Siku 9. Sala ya Jioni

ZABURI 47

ENYI watu wote, pigeni makofi : mpigieni ukelele Mungu kwa sauti ya shangwe.

2. Kwa kuwa Yehova aliye juu ni mwenye kuogofya : ndiye Mfalme mkuu juu ya dunia yote.
3. Atawatisha watu wa nchi chini yetu : na mataifa chini ya miguu yetu.
4. Atatuchagulia urithi wetu : fahari ya Yakabo ambaye alimpenda.
5. Mungu amepaa kwa kelele za shangwe : Yehova kwa sauti ya baragumu.
6. Mwimbieni Mungu, naam, imbeni : mwimbieni Mfalme wetu, naam, imbeni.
7. Kwani Mungu ndiye Mfalme wa dunia yote : imbeni kwa akili.
8. Mungu awamilki mataifa : Mungu ameketi katika kiti chake kitakatifu.
9. Wakuu wa watu wamekussanyika wawe watu wa Mungu wa Iburahimu : kwani ngao za dunia zina Mungu, ametukuka sana.

ZABURI 48

YEHOVA ndiye aliye mkuu na mwenye kusifiwa sana : katika mji wa Mungu wetu, mlima wake mtakatifu.

2. Katika kuinuka kwake ni mzuri sana, ni furaha ya

- dunia yote : mlima Zayuni, pande za kaskazini, mji wa Mfalme mkuu.
3. Mungu katika majumba yake : amejijulisha kuwa ngome.
4. Kwani ni ajabu, wafalme walikusanyika : walipita wote pamoja.
5. Waliona, mara wakashangaa : wakafadhaika na kukimbia.
6. Papo hapo tetemeko liliwashika : uchungu kama wa mwanamke azaaye.
7. Kwa upopo wa mashariki : wavunja jahazi za Tarashishi.
8. Kama tulivyosikia ndivyo tulivyoona katika mji wa Yehova wa majeshi, mji wa Mungu wetu : Mungu ataufanya imara hata milele.
9. Tumezifiki fadhili zako, ewe Mungu : katikati ya hekalu lako.
10. Kama liliyvo jina lako, ewe Mungu, ndivyo sifa yako hata miisho ya dunia : mkono wako wa kuume umejaa haki.
11. Na ufurahi mlima Zayuni, binti za Yuda na washangirie : kwa sababu ya hukumu zako.
12. Tembeeni katika Zayuni, uzungukeni mji : ihe-sabuni minara yake.
13. Tieni moyoni boma zake, yafikirini majumba yake : mpatte kuwaambia kizazi kitakachokuja.
14. Kwa maana Mungu huyu ndiye Mungu wetu milele na milele : yeye ndiye atakayetuongoza hata mauti.

ZABURI 49

SIKIENI haya, enyi mataifa yote : sikilizeni, ninyi nyote mnaokaa duniani :

2. Watu wakuu na watu wadogo wote pia : tajiri na maskini wote pamoja.
3. Kinywa changu kitanena hekima : na fikira za moyo wangu zitakuwa za ujuzi.
4. Nitatega sikio langu nisikie methali : nitafumbua fumbo langu kwa kinubi.
5. Kwa nini niogope siku za uovu : ubaya ukinizunguka miguuni pangu ?

6. Wao wanaozitumainia mali zao : na kujisifia wingi wa utajiri wao ;

7. Hakuna awezaye kumkomboa ndugu yake : wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake :

8. (Kwani fidia ya nafsi zao ina gharama nyngi : naye hana budi kuiacha hata milele :)

9. Ili aishi siku zote : asiuone uharibifu.

10. Naam, yualiona, hata wenye hekima hufa : mpu-mbau na mjinga hupotea pamoja, na kuwaachia wengine mali zao.

11. Wafikiri miyoyoni mwao nyumba zao ni za milele, maskani zao vizazi hata vizazi : wataja mashamba yao kwa majina yao wenyewe.

12. Lakini mwanadamu hadumu katika heshima : bali amefanana na nyama wapoteao.

13. Hii ni njia yao, nayo ni ujinga wao : pamoja na hayo walioko baada yao huyaridhia maneno yao.

14. Kama kondoo wamebekwa kwenda kuzimu, na mauti itawachunga : watu wanyofu watawamilki asubuhi, uzuri wao utaliwa na kaburi, usikae popote.

15. Bali Mungu atanikomboa nafsi yangu, na kunitoa mkononi mwa kuzimu : kwani atanikaribisha.

16. Usiogope mtu atakapopata utajiri : na fahari ya nyumba yake itakapozidi :

17. Kwani atakapokuka hatachukua chochote : utukufu wake hautashuka ukimfuata.

18. Ajapoijibarikia nafsi yake alipokuwa hai : na watu wakusifu ukijitendea mema,

19. Atakwenda kunako kizazi cha baba zake : hawa-taona nuru hata milele.

20. Mwanadamu mwenye heshima asiyeh na akili : amefanana na nyama wapoteao.

Siku 10. Sala ya Asubuhi

ZABURI 50

MUNGU, Mungu Yehova, amenena : ameiita nchi, toka maawio ya juu hata machweo yake.

2. Tokea Zayuni, ukamilifu wa uzuri : Mungu ame-mulika.

3. Mungu wetu atakuja wala hatanyamaza : moto utakula mbele zake, na tufani yavuma sana ikimzunguka pande zote.

4. Atazilingana mbingu zilizo juu, na nchi pia : awahukumu watu wake :

5. Nikusanyieni watakatifu wangu : waliofanya agano nami kwa dhabihu.

6. Na mbingu zitatangaza haki yake : kwa maana Mungu ndiye aliye hakimu.

7. Sikieni, enyi watu wangu, nami nitanena, nami nitakushuhudia, ewe Isiraeli : mimi ndimi niliye Mungu, Mungu wako.

8. Sitakukemea kwa ajili ya dhabihu zako : na kafara zako ziko mbele zangu daima.

9. Sitatwaa ng'ombe katika nyumba yako : wala beberu katika mazizi yako.

10. Kwani kila nyama wa mwitu ni wangu : na makundi ya nyama juu ya milima elfu elfu.

11. Nawajua ndege zote za milima : na nyama zote za mashamba ni zangu.

12. Kama ningekuwa na njaa singkuambia : kwani ulimwengu ni wangu navyo viujazavyo.

13. Je, nile nyama ya mafahali ? Au ninywe damu ya mbuzi ?

14. Mtolee Mungu dhabihu za kushukuru : mtimizie aliye juu nadhiri zako :

15. Ukanilingane siku ya mateso : nitakuokoa nawe utanitukuzu.

16. Bali mtu asiyeh haki, Mungu amwambia, Una nini wewe kuitangaza sheria yangu : na kuliweka agano langu kinywani mwako ?

17. Kwani wewe wachukia maonyo : wayatupa maneno yangu nyuma yako.

18. Ulipomwona mwivi ulikuwa radhi naye : umeshirikiana na wazinzi.

19. Umekiachia kinywa chako kinene mabaya : na ulimi wako watunga hila.

20. Unakaa na kumsengenya ndugu yako : na mwana wa mama yako unamsingizia.

21. Ndivyo ulivyofanya, nikanyamaza, ukadhani ya kuwa mimi ni kama wewe : lakini nitakukemea, nitayapanga hayo mbele ya macho yako.

22. Yafahamuni haya, ninyi mnaomsahau Mungu : nisije nikawararueni, asipatikane mwenye kuwaponya :

23. Atoaye dhabihu za kushukuru ndiye anitukuzaye : naye autengenezaye mwenendo wake nitamwonyesha wokofu wa Mungu.

ZABURI 51

UNIREHEMU, ewe Mungu, kwa kadiri ya fadhili zako : kwa kadiri ya wingi wa rehema zako uya fute makosa yangu.

2. Unioshe kabisa na uovu wangu : unitakase dhambi yangu.

3. Kwani ninakiri mimi makosa yangu : na dhambi yangu i mbele yangu daima.

4. Nimekutendea dhambi wewe peke yako na maovu nimefanya mbele za macho yako : ili uhesabiwe kuwa una haki unenapo, na kuwa safi utoapo hukumu.

5. Mimi niliumbwaa katika hali ya uovu : mama yangu alinichukua mimba hatiani.

6. Bali wapendezwa na kweli iliyio moyoni : utanijulisha hekima kwa siri.

7. Unisafishe kwa husopo nami nitakuwa safi : unioshe nami nitakuwa mweupe kuliko theluiji.

8. Unisikize furaha na shangwe : mifupa uliyoiponda ifurahi.

9. Ufiche uso wako usitazame dhambi zangu : uzifute hatia zangu zote.

10. Ewe Mungu, uniumbie moyo safi : uifanye upya roho yangu ndani yangu.

11. Usinitenge na uso wako : wala Roho wako Mtakatifu usiniondolee.

12. Unirudishie furaha ya wokofu wako : unitegemeye kwa Roho wako bora.

13. Nitawafundisha wakosaji njia zako : na wenye dhambi watarejea kwako.

14. Uniponye na damu za watu, ewe Mungu, Mungu wa wokofu wangu : na ulimi wangu utaiimba haki yako.

15. Ewe Bwana, ufunue midomo yangu : na kinywa changu kitanena sifa zako.

16. Kwani wewe hupendezwi na dhabihu, kama sivyo ningetia : walakini huridhii sadaka za kuteketezwa.

17. Dhabihu za Mungu ni roho iliyounjika : moyo uliovunjika na kupondeka, ewe Mungu, hutaudharau.

18. Uitendee mema Zayuni kwa radhi yako : uzijenge kuta za Yerusalem.

19. Ndipo utakapopendezwa na dhabihu za haki, na sadaka za kuteketezwa, hata hizo zilizo nzima : ndipo watakapotoa ng'ombe juu ya madhabahu yako.

ZABURI 52

KWA nini kujisifia uovu, ewe mtu hodari : wema wa Mungu upo siku zote.

2. Ulimi wako watunga madhara : kama wembe mkali, ukifanya hila.

3. Wapenda mabaya kuliko mema : na uwongo kuliko kusema kweli.

4. Wapenda maneno yote ya kupoteza watu : ewe ulimi wenye hila.

5. Lakini Mungu atakuharibu hata milele, atakukamata : atakupokonya hemani mwako ; atakung'oaa katika nchi ya walio hai.

6. Nao wenye haki wataona : wataingiwa na hofu na kumcheka, *wakisema*,

7. Kumbe ! huyu ndiye mtu yule asiyemfanya Mungu kuwa nguvu zake : aliutumainia wingi wa mali zake, na kujifanya hodari kwa madhara yake.

8. Bali mimi ni kama mzeituni umeao katika nyumba ya Mungu : nazitumainia fadhili za Mungu milele na milele.

9. Nitakushukuru milele kwa maana umeitenda : nitalingojea jina lako, kwa kuwa ni jema, mbele ya watakatifu wako.

Siku 10. Sala ya Jioni

ZABURI 53

MPUMBAVU amesema moyoni mwake, Hakuna Mungu : wameharibika na kufanya uovu wa kuchukiza, hakuna mtenda mema.

2. Toka mbinguni Mungu aliwachungulia wanadamu : aone kama yuko mtu mwenye akili amtafutaye Mungu.

3. Kila mtu amepotoka, wameoza wote pamoja : hakuna mtenda mema, la, hata mmoja.

4. Je, wafanyao maovu hawajui ? walao watu wangu kama walavyo mkate, hawamlingani Mungu.

5. Hapo waliingwi na hofu pasipokuwa na hofu, kwani Mungu ameitawanya mifupa yake aliypanga vita juu yako : umewatia aibu kwa sababu Mungu amewadharau.

6. Lau kwamba wokofu wa Isiraeli watoka katika Zayuni : Mungu atakapowerudisha wafungwa wa watu wake, Yakobo atashangiria, Isiraeli atafurahi.

ZABURI 54

EWE Mungu, kwa jina lako uniokoe : na kwa uwezo wako unifanyie hukumu.

2. Ewe Mungu, usikie maombi yangu : usikilize maneno ya kinywa changu.

3. Kwa maana wageni wamenishambulia, watu watishao wanantafuta nafsi yangu : hawakumweka Mungu mbele yao.

4. Tazama, Mungu ndiye anayenisaidia : Bwana ndiye anayenitegemeza nafsi yangu.

5. Atawarudishia adui zangu ubaya wao : uwaangamize kwa kweli yako.

6. Kwa ukunjufu wa moyo nitakutolea dhabihu : nitalishukuru jina lako, ewe Yehova, kwani ni jema.

7. Kwa kuwa ameniokoa na kila taabu : na jicho langu limeridhika kwa huwatazama adui zangu.

ZABURI 55

EWE Mungu, uisikilize sala yangu : wala usijifiche Enikuombapo.

2. Unisikilize na kunijibu : nimetanga-tanga nikilalama na kuugua ;

3. Kwa sababu ya sauti ya adui, kwa sababu ya dhulumu yake asiye haki : kwa maana wanantupia uovu, na kwa ghadhabu wananiudhi.

4. Moyo wangu unaumia ndani yangu : na hofu za mauti zimeniangukia.

5. Hofu na tetemeko vimenijia ; na hofu kubwa imenifunikiza.

6. Nikasema, Laiti ningekuwa na mbawa kama njiva : ningerukia mbali na kustarehe !

7. Ningekwenda zangu mbali : ningetua jangwani.

8. Ningefanya haraka kuzikimbia : dharuba na tufani.

9. Uwaangamize, Bwana, uzichafue ndimi zao : kwani nimeona dhulumu na fitina katika mji.

10. Mchana na usiku huzunguka kutani mwake : uovu na taabu zimo ndani yake.

11. Tamaa mbaya zimo ndani yake : dhulumu na hila haziondoki mitaani mwake.

12. Kwa maana aliyenitukana si adui, ningevumilia : aliyejituksa juu yangu siye anichukiaye, ningejificha asinione :

13. Bali ni wewe, mtu mwenzangu : rafiki yangu, niliyejua na we sana.

14. Tulipeana shauri tamu : tukatembea nyumbani mwa Mungu pamoja na mikutano.

15. Mauti na iwapate kwa ghafula, na washuke kuzimuwangali hai : kwani uovu u makaoni mwao na katikati yao.

16. Nami nitamlingana Mungu : na Yehova ataniokoa.

17. Jioni, asubuhi, na adhuhuri nitalalama na kuugua : naye ataaisikia sauti yangu.

18. Ameikoa nafsi yangu iwe salama, katika vita vilivyonilemea : kwani ni wengi waloteta nami.

19. Mungu ndiye ye ye akaaye tangu milele : atasikia na

kuwajibu wasioona mageuzi ya mambo, wasiomcha Mungu.

20. Amenyosha mkono wake awadhuru waliopatana naye : amelihalifu agano lake.

21. Kinywa chake kilikuwa laini kuliko siagi, bali moyo wake ni vita : maneno yake yalikuwa maororo kuliko mafuta, bali ni panga wazi.

22. Umtweke Yehova mzigo wako naye atakutegemeza : hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele.

23. Nawe, ewe Mungu, utawateremsha walifilikie shimo la uharibifu : watu wa damu na hila hawataishi nusu ya siku zao ; bali mimi nitakutumaini wewe.

Siku II. Sala ya Asubuhi

ZABURI 56

UNIREHEMU, ewe Mungu, kwani binadamu anataka kunimeza : mchana kuchwa ananionea akileta vita.

2. Adui zangu wanataka kunimeza mchana kuchwa : kwani waletao vita juu yangu kwa kiburi ni wengi.

3. Siku ya hofu yangu : nitakutumainia wewe.

4. Kwa msaada wa Mungu nitalisifu neno lake : nimemtumainia Mungu, sitaogopa ; mwenye mwili atanitenda nini ?

5. Mchana kuchwa wanapotosha maneno yangu : mawazo yao yote ni juu yangu kunitakia mabaya.

6. Hukutanika, hujificha, huziangalia hatua zangu : wakinotea nafsi yangu.

7. Je, wataokoka kwa uovu wao : kwa hasira yako uwaaangamize watu, ewe Mungu.

8. Umehesabu kutanga-tanga kwangu : uyatie machozi yangu katika chupa yako ; je, hayamo katika kitabu chako ?

9. Ndipo adui zangu watakaporudi nyuma, siku ile nilinganapo : neno hili nalijua kwa kuwa Mungu yu upande wangui.

10. Kwa msaada wa Mungu nitalisifu neno lake : kwa msaada wa Yehova nitalisifu neno lake.

11. Nimemtumainia Mungu, sitaogopa : mwanadamu atanitenda nini ?

12. Nadhiri zako, ewe Mungu, ni juu yangu : nitakutolea dhabihu za kushukuru.

13. Kwani umeniponya nafsi yangu na mauti ; je, hukuizua miguu yangu isianguke ? ili nienende mbele za Mungu katika nuru ya walio hai.

ZABURI 57

UNIREHEMU, ewe Mungu, unirehemu mimi, kwani nafsi yangu imekukimbilia wewe : nitaukimbia uvuli wa mbawa zako, hata misiba hii itakapopita.

2. Nitamlingana Mungu aliye juu : Mungu anitimiziaye mambo yangu.

3. Atapeleka toka mbinguni na kuniokoa, atukanapo yule atakaye kunimeza : Mungu atazipeleka fadhili zake na kweli yake.

4. Nafsi yangu i kati ya simba, nastarehe kati yao walio moto : wanadamu ambao meno yao ni mikuke na mishare, na ndimi zao ni upanga mkali.

5. Utukuzwe juu ya mbingu, ewe Mungu : na juu ya nchi yote utukufu wako.

6. Wameweka wawu ili kuninasa miguu, nafsi yangu imeinama : wamechimba shimo mbele yangu, wametu-mbukia ndani yake.

7. Roho yangu i thabitii, ewe Mungu, roho yangu i thabitii : nitaimba, nitaimba sifa.

8. Amka, utukufu wangu ; amka, kinanda na kinubi : mimi nitaamka alfajiri.

9. Nitakushukuru, ewe Bwana, kati ya watu : nitakuimbia sifa kati ya mataifa.

10. Kwani fadhili zako ni kubwa hata mbinguni : na uaminifu wako hata mawinguni.

11. Utukuzwe juu ya mbingu, ewe Mungu : na juu ya nchi yote utukufu wako.

ZABURI 58

JE, ni kweli? Mnanena haki, ninyi? Mnahukumu kwa adili, enyi wanadamu?

2. Sivyo! miyoni mwenu mnatenda maovu : katika nchi mnapima udhalimu wa mikono yenu.

3. Wasio haki wamejitenga tangu tumboni : tangu kuzaliwa kwao wamepotea, wakisema uwongo.

4. Sumu yao, mfano wake ni sumu ya nyoka : mfano wao ni nyoka kiziwi azibaye sikio lake;

5. Asiyeiskiliza sauti ya waganga : wajapofanya uganga kwa ustadi.

6. Ewe Mungu, uyavunje meno yao vinywani mwoo : uyavunje majego ya wana simba, ewe Yehova.

7. Na watoweke kama maji yapitayo kwa kasi : akiilekeza mishare yake, iwe kama ilivyokatika.

8. Kama konokono ayeyukaye na kutoweka : kama mimba iliyoharibika, isiyoliona juu.

9. Kabla masufuria yenu hayajapata moto wa miiba : ataipeperusha kama chanchela, iliyo mibichi na iliyo moto pamoja.

10. Mwenye haki atafurahi akionapo kisasi : ataosha miguu yake katika damu ya wasio haki.

11. Na mwanadamu atasema, Hakika iko thawabu ya mwenye haki : hakika yuko Mungu anayehukumu katika dunia.

Siku II. Sala ya jioni

ZABURI 59

UNIPONYE na adui zangu, ewe Mungu wangu : uniinue juu yao wanaoshindana nami.

2. Uniponye nao wafanyao maovu : unikoe na watu wa damu.

3. Kwa maana wanaiotea nafsi yangu, wenyewe nguvu wamenikusanyikia : si kwa kosa langu, ewe Yehova, wala si kwa hatia yangu.

4. Bila kosa langu huenda mbio, hujiweka tayari : uamke unisaidie, ukatazame.

5. Na wewe, Yehova Mungu wa majeshi, Mungu wa Isiraeli, uamke : uwapatilize mataifa wote, usiwarehemu waou wa fanyao uovu hata mmoja.

6. Wakati wa jioni hurudi, hulia kama mbwa : huzunguka-zunguka mjini.

7. Tazama kwa vinywa vyao hupiga mbweu, midomoni mwao mna panga : kwa maana *wasema*, Ni nani asikiaye?

8. Na wewe, ewe Yehova, utawacheka : utawadhihaki mataifa wote.

9. Ewe nguvu zangu, nitakungojea wewe : kwani Mungu ndiye aliye ngome yangu.

10. Mungu wa fadhili zangu atanitangulia : Mungu atanijalia kuwatazama adui zangu.

11. Usiwaue, watu wangu wasije wakasahau : uwatanwaye kwa uwezo wako, na kuwaangamiza, ewe Bwana, ngao yetu.

12. Kwa dhambi ya kinywa chao, na kwa neno la midomo yao, wanaswe kwa kiburi chao : kwa ajili ya kulaani na uwongo wanaosema.

13. Uwakomeshe kwa hasira, uwakomeshe watoweke : wajue ya kuwa Mungu atawala katika Yakobo, na hata miihio ya dunia.

14. Na wakati wa jioni na warudi, walie kama mbwa : na kuzunguka-zunguka mjini.

15. Watanga-tanga hao wakitafuta chakula : wasiposhiba watakesha usiku kucha.

16. Nami nitaziimba nguvu zako asubuhi, nitaziimba fadhili zako kwa furaha : kwa kuwa ndiwe uliyekuwa ngome yangu na makimbilio siku ya shida yangu.

17. Ewe nguvu zangu, nitakuimbia kwa furaha : kwani Mungu ni ngome yangu, Mungu wa fadhili zangu.

ZABURI 60

EWE Mungu, umetutupa na kututawanya : umekuwa na hasira, uturudishe tena.

2. Umetitetemesha nchi na kuipasua : upaponye palipobomoka kwani inatikisika.

3. Umewaonyesha watu wako mazito : umetunywesha mvinyo wa kutuyumbisha.

4. Umewapa bendera wakuogopao : ili wajitwekee kwa ajili ya kweli.

5. Ili wapenzi wako waopolewe : uokoe kwa mkono wako wa kuume, ututike.

6. Mungu amenena kwa utakatifu wake, nami nita-shangiria : nitaigawanya Shekemu, nitalipima bonde la Sukothi.

7. Gileadi ni yangu, Manase ni yangu, na Efiraimu ni nguvu ya kichwa changu : Yuda ni fimbo yangu ya kifalme.

8. Moabu ni bakuli langu la kunawia, nitamtrupia Edomu kiatu changu : Filisitia, piga ukelele kwa ajili yangu.

9. Ni nani atakayenipeleka hata mji wenye maboma ? Ni nani aliyeniongoza hata Edomu ?

10. Ewe Mungu, je, hukututupa ? Nawe, ewe Mungu, hutoki na majeshi yetu.

11. Utuletee msaada juu ya adui : kwani wokofu wa binadamu haufai.

12. Kwa msaada wa Mungu tutatenda mambo ya ushujaa : kwani yeye ndiye atakayewakanyaga adui zetu.

ZABURI 61

USIKIE kilio changu, ewe Mungu : usikilize maombi yangu.

2. Toka mwisho wa nchi nitakulilia, moyo wangu ukizimia : uniongoze niufikilie mwamba ulio juu kuliko mimi.

3. Kwa maana ulikuwa kimbilio langu : ngome yenyenuguu adui asinipate.

4. Nitakaa katika hema lako milele : nitaikimbilia starehe ya mbawa zako.

5. Kwani wewe, ewe Mungu, umezisikia nadhiri zangu : umewapa urithi wao waliohopao jina lako.

6. Utaziongeza siku za Mfalme : miaka yake itakuwa kama vizazi vingi.

7. Atakaa mbele za Mungu milele : uziagize fadhili na kweli zimhifadhi.

8. Ndivyo nitakavyolisu jina lako, nikiimba daima : ili niondoe nadhiri zangu kila siku.

Siku 12. Sala ya Asubuhi

ZABURI 62

NAFSI yangu yamngojea Mungu tu : wokofu wangu hutoka kwake.

2. Yeye peke yake ni mwamba wangu na wokofu wangu : ngome yangu, sitatikisika sana.

3. Hata lini mtamshambulia mtu mpate kumuua ninyi nyote pamoja ? kama ukuta unaoinama, kama kitalu kilicho tayarri kuanguka.

4. Wamefanya shauri moja, ni la kumwangusha katika cheo chake ; huufurahia uwongo : kwa kinywa chao hubarikia, kwa moyo wao hulaani.

5. Nafsi yangu, umngojee Mungu tu : tumaini langu hutoka kwake.

6. Yeye ndiye mwamba wangu na wokofu wangu : ngome yangu, sitatikisika.

7. Ni kwa Mungu wokofu wangu na utukufu wangu : mwamba wa nguvu zangu na kimbilio langu ni kwa Mungu.

8. Enyi watu, mtumainieni siku zote, ifunueni miyo yenu mbele zake : Mungu ndiye kimbilio letu.

9. Hakika, watu wanyonge ni ubatili, na watu wenye cheo ni uwongo : katika mizani huinuka ; wote pamoja ni hafifu kuliko ubatili.

10. Msiumainie dhulumu, wala msijivune kwa unyan'anyi : mali izidipo msiiangalie sana moyoni.

11. Mara moja amenena Mungu, mara mbili nimesikia haya : ya kuwa nguvu zina Mungu.

12. Na fadhili ziko kwako, ewe Bwana : kwani ndiwe umlipaye kila mtu kwa kadiri ya kazi yake.

ZABURI 63

EWE Mungu, wewe ndiwe Mungu wangu, nitakutafuta mapema : nafsi yangu inaona kiu kwako, mwili wangu wakuonea shauku ; katika nchi kayu na uchovu, isiyo na maji.

2. Ndivyo nilivyokutazama katika pahali patakatifu : nzione nguvu zako na utukufu wako.

3. Kwani fadhili zako ni njema kuliko uhai : midomo yangu itakusifu.

4. Ndivyo nitakavyokubarikia muda niwapo hai : kwa jina lako nitaiinua mikono yangu.

5. Nafsi yangu itashiba kama kwa mafuta na vinono : kinywa changu kitakusifu kwa midomo yenyenfuraha.

6. Ninapokukumbuka kitandani mwangu : nakufikiri wewe makesha yote ya usiku.

7. Kwani wewe umekuwa msaada wangu : na katika uvuli wa mbawa zako nitashangiria.

8. Nafsi yangu inakuandama sana : mkono wako wa kuume unanitegemeza.

9. Bali waitafutao nafsi yangu ili kuiharibu : wataingia pande za nchi zilizo chini.

10. Watatolewa wafe kwa nguvu za upanga : watakuwa riziki za makala.

11. Bali mfalme atamfurahia Mungu : kila aapaye kwa ye ye atashangiria, kwa maana kinywa chao wasemao uwongo kitafumbwa.

ZABURI 64

UISIKIE sauti yangu, ewe Mungu, katika malalamiko yangu : unilinde uhai wangu na hofu ya adui.

2. Unifiche mbali na shauri la siri la watenda mabaya : mbali ya ghasia ya watu wafanyao maovu.

3. Walionuo ulimi wao kama upanga : wameielekeza mishare yao, maneno ya uchungu.

4. Wapate kumpiga mtu mkamilifu katika pahali pa siri : kwa ghafula humpigia wala hawaogopi.

5. Walijifanya hodari katika jambo bayo : hushauriana kutega mitego kwa siri, husema, Ni nani atakayeiona ?

6. Hutunga matendo maovu, *husema*, Tumekwisha kupeleleza sana : na mawazo ya ndani ya kila mmoja wao, na moyo wake, huwa siri kabisa.

7. Kwa hiyo Mungu atawapiga shabaha : kwa mshare mara watapigwa.

8. Ndivyo watakavyokwazwa, ulimi wao wenye wewe ukishindana nao : wote wawaonao watakitisa vichwa.

9. Na watu wote wataogopa, wataitangaza kazi ya Mungu : na kuyafahamu matendo yake.

10. Mwenye haki atamfurahia Yehova na kumkimbilia : na wote wenye moyo wa adili watajisifu.

Siku 12. Sala ya Jioni

ZABURI 65

SIFA zakungojea wewe, ewe Mungu, katika Zayuni : Sna kwako wewe itaondolewa nadhiri.

2. Wewe usikiaye kuomba : wote wenye mwili watakuja.

3. Maovu mengi yananishinda : wewe utayafuta maasi yetu.

4. Yuna heri mtu yule umchaguaye na kumkaribisha akae nyuani mwako : tutashiba wema wa nyumba yako, pahali patakatifu pa hekalu lako.

5. Kwa mambo ya kutisha utatujibu katika haki, ewe Mungu wa wokofu wetu : wewe uliyetumaini la wote wakao katika miisho ya nchi na la wao walio mbali sana baharini :

6. Aiwekaye milima imara kwa nguvu zake : ambaye amejifunga uwezo kama mshipi :

7. Autulizuye uvumi wa bahari, uvumi wa mawimbi yake : na ghasia ya mataifa.

8. Wao nao wakao mbali kabisa huogopa ishara zako : milango ya asubuhi na jioni waifurahisha.

9. Wajjilia nchi na kuisitawisha, waitajirisha sana : mto wa Mungu umejaa maji ; wawaruzuku watu nafaka,ukiisha kuitengeneza nchi ;

10. Matuta yake wayajaza maji, wapasawazisha palipoinuka : wailainisha nchi kwa manyunu, waibarikia mimea yake.

11. Umeuvika mwaka taji ya wema wako : mapito yako yadondoza unono.

12. Huyadondokea malisho ya nyikani : na vilima vyajifunga furaha.

13. Na malisho yamevikwa kondoo, na mabonde yamepambwa nafaka : yanashangiria, naam, yanaimba.

ZABURI 66

MPIGIE Mungu kelele za shangwe : nchi yote.
2. Imbeni utukufu wa jina lake : tukuzeni sifa zake.

3. Mwambieni Mungu, matendo yako jinsi yalivyo na utisho ! Kwa ajili ya wingi wa nguvu zako adui zako watakuja wakijinyenyekeza mbelé zako.

4. Nchi yote itakusujudu na kukuimba : naam, italiimba jina lako.

5. Njoni kayatazameni matendo ya Mungu : hutisha kwa mambo ayatendayo kwa wanadamu.

6. Aligeuza bahari ikawa nchi kavu, katika mto walivuka kwa miguu : huko ndiko tulikomfurahia.

7. Atawala kwa uwezo wake milele : macho yake yawaangalia mataifa ; waasio wasijitukuze nafsi zao.

8. Enyi mataifa, mtukuzeni Mungu wetu : wasikizeni watu sauti yenyé sifa zake.

9. Aliyeiweka nafsi yetu katika uhai : wala hakuuacha mguu wetu usogezwe.

10. Kwa maana umetupima, ewe Mungu : umetu-jaribu kama inavyojaribiwa fedha.

11. Ulituingiza ndani ya wavu : uliweka viunoni mwetu mzigo uliotulemea.

12. Uliwakaribisha watu juu ya vichwa vyetu : tulipita motoni na majini, ukatutoa na kutuleta kunako wingi.

13. Nitaingia nyumbani mwako na sadaka za kuteke-tezwa : nitaondoa kwako nadhiri zangu,

14. Ambazo midomo yangu ilizinena : kikazisema kinywa changu nilipokuwa taabuni.

15. Sadaka za kuteketezwa za vinono nitakutolea, pamoja na fukizo la kondoo waume : nitatoa ng'ombe pamoja na mbuzi.

16. Njoni, sikieni, ninyi nyote mnaomcha Mungu : nami nitawahadithieni aliyonitendea nafsi yangu.

17. Nilimlingana kwa kinywa changu : na sifa zake kuu zilikuwa chini ya ulimi wangu.

18. Nikiwaza maovu moyoni mwangu : Bwana hata-sikia.

19. Hakika Mungu amesikia : ameisikiliza sauti ya maombi yangu.

20. Na ahimidiwe Mungu asiyeyakataa maombi yangu : wala kuniondolea fadhili zake.

ZABURI 67

MUNGU aturehemu, atubarikie : uso wake atuangazie.
2. Njia yako ijulikane duniani : wokofu wako kwa mataifa wote.

3. Watu wakusifu, ewe Mungu : watu wote wakusifu.

4. Mataifa wafurahi na kuimba kwa furaha : kwani wewe utawahukumu watu kwa haki, utawaongoza watu walioko duniani.

5. Watu wakusifu, ewe Mungu : watu wote wakusifu.

6. Nchi imesitawi : Mungu, Mungu wetu atatubarikia.

7. Mungu atatubarikia : ncha zote za duniani zita-mwogopa.

Siku 13. Sala ya Asubuhi

ZABURI 68

MUNGU na aondoke, adui zake watawanyike : nao wamchukiao waukimbie uso wake.

2. Kama moshi upeperushwayo uwapeperushe vivyo : kama nta iyeyukavyo mbele ya moto, wabaya wapotee vivyo mbele za Mungu.

3. Bali wenye haki wafurahi, washangirie mbele za Mungu : naam, wapige ukelele kwa furaha.

4. Mwimbieni Mungu, lisifuni jina lake : mtengenezeeni njia kuu apitaye majangwani kama mpanda farasi ; jina lake ni Yehova, shangirieni mbele zake.

5. Mungu katika kao lake yu mtakatifu : yu baba wa yatima na mwamuizi wa wajane.

6. Mungu huwakalisha wapweke katika nyumba, huwatoa wafungwa wakae hali ya **kufanikiwa** : bali wakaidi hukaa katika nchi kavu.

7. Ewe Mungu, ulipotoka mbele ya watu wako : ulipopita nyikani :

8. Nchi ilitetemeka, naam, mbingu zilidondoka mbele za Mungu : Sinai ile mbele za Mungu, Mungu wa Israeli.

9. Ulinyesha mvua ya neema, ewe Mungu : urithi wako ulipochoka uliutia nguvu.

10. Kabilia lako liliifanya kao lake humo : kwa wema wako, ewe Mungu, uliwakeea akiba walioonewa.

11. Bwana anatoa neno lake : wanawake wanaotangaza habari ni jeshi kubwa.

12. Wafalme wa majeshi wanakimbia, wanakimbia : na mwanaamke akaaye nyumbani anagawanya mateka.

13. Je, mtalala katika mazizi : mbawa za njiva zilizofunikwa fedha na manyoya yake dhahabu ?

14. Mwenyezi Mungu alipotawanya wafalme humo : kulikunya theluji katika Salumoni.

15. Ni mlima wa Mungu ule mlima Bashani : ni mlima mrefu ule mlima Bashani.

16. Enyi mlima mirefu, kwa nini kuchungulia ? Mlima alioutamani Mungu acae juu yake, naam, Yehova atakaa juu yake milele.

17. Magari ya Mungu ni elfu ishirini, naam, ni elfu nyingi sana : Bwana yumo kati yao, katika pahali patakatifu, Sinai.

18. Wewe umepaa juu, umeteka mateka, umepewa vipawa kwa ajili ya wanadamu : naam, hata kwa wakaidi nao, ili Yehova Mungu acae nao.

19. Na ahimidiwe Bwana, ambaye kila siku hutuchuklia mzigo wetu : naye ni Mungu wa wokofu wetu.

20. Mungu kwetu sisi ni Mungu wa kuoko : na kwake Yehova Bwana ziko njia za kutoka mautini.

21. Naam, Mungu atakipasua kichwa cha adui zake : na utosi wenye nywele nyingi wa mtu afulizaye kukosa.

22. Bwana alisema, Kutoka Bashani nitawarudisha : nitawarudisha kutoka vilindi vya bahari :

23. Upate kuchovya mguu wako katika damu : na ulimi wa mbwa zako upate schemu yake katika adui zako.

24. Wameona miendo yako, ewe Mungu : miendo ya Mungu wangu, Mfalme wangu, katika pahali patakatifu.

25. Waimbaji walitangulia, nyuma yao wapiga vinanda : katikati ya wanawali wapiga matari.

26. Katika makutano mhimidini Mungu Bwana : ninyi mlio wa chemchemi ya Israeli.

27. Yuko Benjamini mdogo, mtawala wao : wakuu wa Yuda, kundi lao : wakuu wa Zabuloni, wakuu wa Nafitali.

28. Mungu wako amekuagizia nguvu zako : uyathubitishe, ewe Mungu, uliyotutendea.

29. Kwa ajili ya hekalu lako katika Yerusalem : wafalme watakuletea hedaya.

30. Mkemee nyama wa manyasini, kundi la mafahali na nzao za watu : wakivikanyaga vipande vya fedha, amewatawanya watu wapendezwao na vita.

31. Masheki watakuja kutoka Misiri : Ethiopia itafanya haraka kumnyoshea Mungu mikono yake.

32. Mwimbieni Mungu, enyi falme za dunia : msifuni Bwana kwa nyimbo ;

33. Yeye apandaye mbingu za mbingu zilizo za kale : atoa sauti yake, sauti ya nguvu.

34. Mhesabieni Mungu nguvu : enzi yake ni juu ya Israeli, na nguvu zake mawinguni.

35. Ewe Mungu, u mwenye utisho toka mwahali mtakatifu mwako : Mungu wa Israeli, yeye huwapa watu wake nguvu na uwezo. Mungu na ahimidiwe.

UNIOKOE, ewe Mungu : kwani maji yamefika hata nafsini mwangu.

2. Ninazama katika matope mengi pasiposimamika : nimefika maji ya vilindi, maji yanaponigharikisha.

3. Nimechoka kwa kulia kwangu, koo yangu imekauka : macho yangu yamedhoofu kwa kumng'oeja Mungu wangu.

4. Wanaonichukia bure ni wengi kuliko nywele za kichwa changu : watakao kunikatilia mbali wamekuwa hodari, adui zangu kwa sababu ya uwongo : ndipo nililipa vitu nisivyovichukua.

5. Ewe Mungu, wewe unajua upumbavu wangu : wala hukufichwa dhambi zangu.

6. Wanaokungojea wewe wasiaibishwe kwa ajili yangu, ewe Bwana Yehova wa majeshi : wanaokutafuta wewe wasifedheheshwe kwa ajili yangu, ewe Mungu wa Israeli.

7. Kwani kwa ajili yako nimestahimili laumu : fedheha imenifunika uso wangu.

8. Nimekuwa mgeni kwa ndugu zangu : na mtu wa nchi nyininge kwa wana wa mama yangu.

9. Kwani wivu wa nyumba yako umenia : na laumu zao wanaokulaumu zimenipata.

10. Nilipolia *na kuiadhibu* nafsi yangu kwa kufunga : ikawa laumu juu yangu.

11. Nilipofanya gunia kuwa nguo zangu : nikawa methali kwa.

12. Waketio langoni hunisema : na wanywaji wa tembo hunimba.

13. Nami maombi yangu nakuomba wewe, ewe Yehova, wakati ukupendezao : ewe Mungu, kwa wingi wa fadhili zako, unijibu katika kweli ya wokofu wako.

14. Uniponye kwa kunitoa matopeni, wala usiniache nikazama : na niponywe nao wanaonichukia, na katika vilindi nya maji.

15. Maji ya gharika yasinishinde, wala vilindi visinimeze : wala shimo lisifumbe kinywa chake juu yangu.

16. Unijibu, ewe Yehova, kwani fadhili zako ni njema : kwa kadiri ya wingi wa reherma zako unielekee.

17. Wala usinifiche uso wako mimi mtumishi wako : kwani mimi nimo taabuni, unijibu upesi.

18. Uikaribie nafsi yangu, uikomboe : kwa sababu ya adui zangu unifidie.

19. Wewe wajua kulaumiwa kwangu na kuaibika kwangu na kufedheheka kwangu : mbele zako wewe wako watesi wangu wote.

20. Laumu imenivunja moyo nami ninaugua sana : nikangoja aje wa kunihirumia, wala hakuna mtu, na wa kunifariji, wala sikumwona mtu.

21. Wakanipa uchungu kuwa chakula changu : nami nilipokuwa na kiu wakaninywesha siki.

22. Meza yao mbele yao na iwe mtego : naam, salama yao *na iwe* kitu cha kuwanasa.

23. Macho yao yatiwe giza wasione : na viuno vyao uvitetemeshe daima.

24. Umwage ghadhabu yako juu yao : na ukali wa hasira yako uwapate.

25. Matuo yao na yawe ukiwa : pasiwe na mtu wa kukaa hemani mwao.

26. Kwani wanamuudhi mtu uliyempiga wewe : wana-simulia maumivu yao uliowatia jeraha.

27. Uwaongeze uovu juu ya uovu wao : wala wasiingie katika haki yako.

28. Na wafutwe katika chuo cha uhai : wala pamoja na wenye haki wasiandikwe.

29. Nami ni maskini na mtu wa huzuni : wokofu wako, ewe Mungu, uniinue.

30. Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo : nami nitamtukuzza kwa shukrani.

31. Nayu yatampendeza Yehova kuliko ng'ombe : au nzao mwenye pembe na kwato.

32. Walioonewa wameiona na kufurahi : ninyi mnao-mtaafuta Mungu, miyo yenu ihuishwe.

33. Kwa kuwa Yehova huwasikia wahitaji : wala hawadharau wafungwa wake.

34. Mbingu na nchi na zimsifu : bahari na vyote vitukutavyo ndani yake.

35. Kwani Mungu ataiokoa Zayuni, na kuijenga miji ya Yuda : nao wataaka ndani yake na kuimilki.

36. Wazao wa watumishi wake watairithi : na walipendaao jina lake wataaka humo.

ZABURI 70

E WE Mungu, uniookoe : ewe Yehova, unisaidie hima.
 2. Waibike, wafedheheke, wanaoitafuta nafsi yangu : warudishwe nyuma, watahayarishwe, wapendezwao na shari yangu.

3. Na warudishwe nyuma kwa sababu ya aibu yao : wanaosema, Ewe ! Ewe !

4. Washangirie, wakufurahie, wote wakutafuta : waupendao wokofu wako waseme daima, Atukuzwe Mungu.

5. Nami ni maskini na mhitaji, ewe Mungu, unijilie kwa haraka ; ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu ; ewe Yehova, usikawie.

Siku 14. Sala ya Asubuhi

ZABURI 71

NIMEKUKIMBILIA wewe, ewe Yehova : nisiaibike milele.

2. Kwa haki yako uniponye, uniopoe : unitegee sikio lako, uniookoe.

3. Uwe kwangu mwamba wa makazi yangu nitakkokwenda siku zote : umeamuru niokolewe ; ndiwe genge langu na ngome yangu.

4. Ewe Mungu wangu, uniopoe katika mkono wa mtu asive haki : katika mkono wa mtu mwovu, dhalimu.

5. Kwani ndiwe taraja langu, ewe Bwana Yehova : tumaini langu tokea ujana wangu.

6. Nimekutegemea wewe tangu kuzaliwa, ndiwe uliyenitoa tumboni mwa mama yangu : nitakusifu wewe daima.

7. Nimekuwa kitu cha ajabu kwa watu wengi : na wewe ndiwe kimbilio langu la nguvu.

8. Kinywa changu kitajazwa kwa sifa zako : na kwa heshima yako mchana kuchwa.

9. Usinitupe wakati wa uzee : nguvu zangu zipungukapo usiniache.

10. Kwa maana adui zangu wananiamba : na wanaoniatea nafsi yangu hufanya shauri pamoja,

11. Wakisema, Mungu amewwacha : mfuatieni mka-mateni, hakuna wa kumponya.

12. Ewe Mungu, usiwe mbali nami : ewe Mungu wangu, ufanye haraka kunisaida.

13. Waibishwe, watoweshwe adui za nafsi yangu : wavikwe laumu na fedheha wanaonitakia mabaya.

14. Nami nitatumaini daima : nitazidi kuongeza sifa zako zote.

15. Kinywa changu kitasimulia haki yako : na wokofu wako mchana kuchwa, kwani sijui hesabu yake.

16. Nitakuja na mambo ya ajabu ya Bwana Yehova : nitataja haki yako wewe peke yako.

17. Ewe Mungu, umenifundisha tokea ujana wangu : nimekuwa nikitangaza miujiza yako hata hivi leo.

18. Na hata sasa nikiwa mzee mwenye mvi, usiniache, ewe Mungu : hata niishe kuwaeleza watu wa kizazi hiki nguvu zako ; na kila atakayekuja uwezo wako.

19. Na haki yako, ewe Mungu, imefika juu sana : wewe uliyefanya mambo makuu ; ewe Mungu, ni nani aliye kama wewe ?

20. Wewe uliyetuonyesha mateso mengi mabaya utatuhuisha tena : utatupandisha juu tena tokea pande za chini ya nchi.

21. Uniongezee ukuu wangu : urejee tena na kunifariji moyo.

22. Nami nitakushukuru kwa kinanda, na kweli yako, ewe Mungu wangu : nitakuimbia wewe sifa kwa kinubi, ewe Mtakatifu wa Israeli.

23. Midomo yangu itafurahi sana nikuimbiapo sifa : na nafsi yangu uliyikombea.

24. Ulimi wangu nao utasimulia haki yako mchana kuchwa : kwa maana wameaibishwa, wametahayarika wanaonitakia mabaya.

ZABURI 72

E WE Mungu, umpe mfalme hukumu zako : na mwana wa mfalme haki yako.

2. Atawaamua watu wako kwa haki : na watu wako walioonewa *atawaamua* kwa hukumu.

3. Milima itawazalia watu amani : na vilima navyo kwa haki.

4. Atawahukumu walioonewa wa watu : atawaokoa wana wa wahitaji, atamseta mwénye kuonea.

5. Watakuogopa wakati wote wa kudumu juu : na wakati wa kung'aa mwezi kizazi hata kizazi.

6. Atashuka kama mvua juu ya majani yaliyokatwa : kama manyunyu yainyweshayo nchi.

7. Siku zake ye ye mwénye haki atasitawi : na wingi wa amani hata mwezi utakapokoma.

8. Atatawala toka bahari hata bahari : toka Mto hata miisho ya nchi.

9. Wakaao jangwani watainama mbele zake : adui zake wataramba mavumbi.

10. Wafalme wa Tarashishi na visiwa wataleta zawadi : wafalme wa Sheba na Seba watatoa vipawa.

11. Naam, wafalme wote watamsujidia : na mataifa wote watamtumikia.

12. Kwa maana atamwokoa mhitaji aliapo : na mtu aliyeonewa iwapo hana msaidizi.

13. Atamhurumia aliye dhaifu na maskini : na nafsi za wahitaji ataziokoa.

14. Atawakomboa nafsi zao na kuonewa na kudhili-miwa : na damu yao itakuwa na thamani machoni pake.

15. Basi wataishi, naye atapewa dhahabu ya Sheba : na watamwombea daima na kumbarikia mchana ku-chwa.

16. Utakuwa wingi wa nafaka katika nchi juu ya milima : matunda yake yatalewa-lewa kama Lebanonii ; na watu wa mjini watasitawi kama majani ya nchi.

17. Jina lake litadumu milele, wakati wote wa kung'aa juu jina lake litakuwa na wazao : watu watabarikiwa kwake ye ye ; mataifa wote watamwita mwénye heri.

18. Na ahimidiwe Yehova Mungu, Mungu wa Israeli : atendaye miujiza ye ye peke yake.

19. Jina lake tukufu na lhimidiwe milele : dunia yote na ijae utukufu wale. Amina. Amina.

Siku 14. Sala ya fioni

ZABURI 73

HAKIKA Mungu ni mwema kwa Israeli : kwa walio safi mioyo yao.

2. Nami miguu yangu ilikuwa karibu na kupotoka : hatua zangu zilikuwa karibu na kuteleza.

3. Kwani niliwaonea wivu wenye kujivuna : nilipoiona hali ya amani ya wasio haki.

4. Kwani hawana maumivu katika kufa kwao : na miili yao ina nguvu.

5. Katika taabu ya watu hawamo : wala hawapati mapigo pamoja na wanadamu.

6. Kwa hiyo kiburi kimekuwa kama mkufu shingoni mwao : jeuri huwavika kama nguo.

7. Macho yao hutokeza kwa kunenepa : waliyo nayo yamepita azima za mioyo yao.

8. Hudhihaki, katika ubaya hunena dhulumu : hunena kwa kujivuna.

9. Wameweeka kinywa chao mbinguni : na ndimi zao huenda huko na huko katika nchi.

10. Kwa hiyo watu wake hurudi : nao hunyweshewa maji tele.

11. Nao husema, Mungu ajuaje ? Yako maarifa kwake aliye juu ?

12. Fahamu, ndivyo walivyo wasio haki : na kwa kuwa wana raha siku zote warne pata mali nydingi.

13. Hakika nimejisafisha moyo wangu bure : na kunawa mikono yangu kwa kutokuwa na kosa ;

14. Kwani mchana kuchwa nimepigwa : na kuadhibiwa kila asubuhii.

15. Kama ningalisema, Nitasililia kama hayo : kumbe ! ningaliwadanganya kizazi cha wana wako.

16. Nami nilipofikiri jinsi ya kuyafahamu haya : ikawa taabu machoni pang'.

17. Hata nilipoingia katika pahali patakatifu pa Mungu : nikaufikiri mwisho wao.

18. Hakika wewe huwaweka penye utelezi : huwa-ngusha katika maharibifu.

19. Namna gani warmekuwa ukiwa mara moja ! Wame-tokomea, wame-toweshwa kwa utisho.
20. Kama ndoto wakati wa kuamka : ewe Bwana, uondokapo utaidharau sanamu yao.
21. Kwani moyo wangu uliona uchungu : viuno vyangu viliponichoma,
22. Nilikuwa kama mjinga, sijui neno : nilikuwa kama nyama tu mbele zako.
23. Walakini mimi ni pamoja nawe daima : umenishika mkono wa kuurme.
24. Utaniongoza kwa shauri lako : na baadaye utan-karibisha kwa utukufu.
25. Ni nani niliye naye mbinguni : na pamoja nawe sina nipayendezwacho nacho duniani.
26. Mwili wangu na moyo wangu hupunguka : bali Mungu ni nguvu za moyo wangu na sehemu yangu milele.
27. Kwani wajitengao nawe watapotea : umewaa-nga-miza wote waliozini kwa kukuacha.
28. Nami kumkaribia Mungu ni kwema kwangu : nimefanya kimbilio kwa Bwana Yehova, nihubiti matendo yako yote.

ZABURI 74

EWE Mungu, kwa nini umetutupa milele : kwa nini hasira yako inatoka moshi juu ya kondoo za malisho yako ?

2. Ulikumbuke kusanyiko lako ulilolinunua zamani, ulilolikomboa liwe kabilia la urithi wako : mlima Zayuni ulioufanya maskani yako.

3. Uinue miguu yako upatazame palipoharibika milele : kila ubaya alioufanya adui katika pahali patakatifu.

4. Adui zako wamenguruma kati ya kusanyiko lako : wameweka bendera zao ziwe alama.

5. Walionekana kama watu wainuo mashoka : wakate miti ya msituni.

6. Na sasa nakshi yake yote pia : wanaivunja-vunja kwa mashoka na nyundo.

7. Wamepatia moto pahali patakatifu pako : wameina-jisi maskani ya jina lako *na kuiangusha chini*.

8. Walisema miyoni mwao, Na tuwaangamize kabisa : wame-mchoma moto mwahali mwenye mikutano ya Mungu katika nchi yote.
9. Hatuzioni ishara zetu, wala sasa hakuna nabii : wala kwetu hakuna ajuaye hata lini.
10. Ewe Mungu, mtesi atalaumu hata lini ? Adui alidharau jina lako hata milele ?
11. Mbona unaurudisha mkono wako, naam, mkono wako wa kuume : uutoe kifuanu mwako, ukaangamize.
12. Lakini Mungu ni Mfalme wangu tokeea zamani : afanyaye mambo ya wokofu katikati ya nchi.
13. Wewe uliipasua bahari kwa nguvu zako : wavivunja vichwa vya nyangumi juu ya maji.
14. Wewe waviseta vichwa vya lewiathani : ulimtoa awe chakula cha watu wakao jangwani.
15. Wewe ulitokeza chemchemi na kijito : wewe uli-kausha mito mikubwa sana.
16. Mchana ni wako, usiku nao ni wako : ndiwe uliyefanya mwanga na juu.
17. Wewe umeiweka mipaka yote ya dunia : kaskazi na kusi umezitengeneza wewe.
18. Uyakumbuke hayo, adui amelaumu, ewe Yehova : na watu wapumbavu wamelitekana jina lako.
19. Usimpe nyama mkali nafsi ya hua wako : usiusahau milele uhai wa watu wako walioonewa.
20. Ulikiriki agano : kwani mwahali mwenye giza katika nchi mmejaa makao ya dhulumu.
21. Aliyeonewa asirejee ametiwa haya : mnyonge na mhitaji na walisifu jina lako.
22. Usimame, ewe Mungu, ujitetee nafsi yako : ukumbuke unavyotukanwa na mpumbavu mchana kuchwa.
23. Usiisahau sauti ya adui zako : ghasia yao wanao-kuondokea inapaa daima.

Siku 15. Sala ya Asubuhi

ZABURI 75

TWAKUSHUKURU wewe, ewe Mungu, twaku-shukuru kwa kuwa jina lako ni karibu : watu huya-simulia matendo yako ya ajabu.

2. Nitakapoufikia wakati ulioamriwa : mimi nitahukumu hukumu za haki.
3. Dunia imeyeyuka na wote wakaao ndani yake : mimi mwenyewe nimezisimamisha nguzo zake.
4. Niliwaambia waliojivuna, Msijivune : na wasio haki, Msiiinue pembe :
5. Msiiinue pembe yenu juu : wala msinene kwa shingo ya kiburi.
6. Kwani si katika mashariki wala magharibi : wala kusini itokako heshima.
7. Bali Mungu ndiye ahukumuye : humdhili huyu na kumwinua huyu.
8. Kwani mkononi mwa Yehova mna kikombe, na mvinyo yake inatoka povu, kimejaa machanganyiko, naye huyamimina : na sira zake wasio haki wa dunia watazifyonza na kuzinywa.
9. Bali mimi nitatangaza *matendo yako* milele : nita-mwimbia Mungu wa Yakobo.
10. Pembe zote za wasio haki nitazikata : na pembe za mwenye haki zitainuka.

ZABURI 76

- K**ATIKA Yuda Mungu amejulikana : katika Israeli jina lake ni kuu.
2. Kibanda chake pia kiko Salemi : na maskani yake iko Zayuni.
 3. Huko ndiko alikoivunja mishare ya uta : ngao na upanga na vita.
 4. Wewe u mwenye fahari na adhama : toka milima ya mateka.
 5. Wametekwa wenyewe moyo thabiti, wamelala usingizi : na watu wote walio hodari hawakuiona mikono yao.
 6. Kwa kukemea kwako, ewe Mungu wa Yakobo : gari na farasi wameshikwa na usingizi mzito.
 7. Wewe ndiwe utishaye, naam, wewe : na nani awezaye kusimama mbele zako ufanyapo hasira ?
 8. Toka mbinguni uliwasikiza watu hukumu : nchi iliogopa ikakaa kimya,

9. Mungu aliposimama ili kuhukumu : na kuwaokoa wapole wa dunia wote pia.
10. Hakika hasira ya binadamu itakusifu : masilio ya hasira utajifunga kama mshipi.
11. Wekeni nadhiri mkaziondoe kwa Yehova Mungu wenu : wote wanaomzunguka wamletee hedaya, yeze astahiliye kuogopwa.
12. Yeye huzikata roho za wakuu : huwatisha wafalme wa dunia.

ZABURI 77

- N**ITAMPAZIA Mungu sauti yangu : naam, *nitampazia* Mungu sauti yangu naye atanisikia.
2. Siku ya taabu yangu *nilitafuta* Bwana : mkono wangu ulinyoshwa usiku, haukulegea, nafsi yangu ilikataa kufarrijika.
 3. Namkumbuka Mungu nikifadhaika : nalalamika roho yangu ikizimia.
 4. Wazishika kope za macho yangu *zisifumbike* : naona mashaka nisiweze kunena.
 5. Nimefikiri habari za siku za kale : miaka ya zamani zilizopita.
 6. Nakumbuka wimbo wangu usiku : nawaza moyoni mwangu, roho yangu ilitafuta.
 7. Je, Bwana atatupa milele na milele ? Hataenda fadhili tena kabisa ?
 8. Rehema zake zimekoma hata milele ? Ahadi yake imekwisha hata vizizi vyote ?
 9. Mungu amesahau fadhili zake ? Amezia kwa hasira rehema zake ?
 10. Nikasema, ndio udhaifu wangu huo : lakini nitakumbuka miaka ya mkono wa kuume wa aliye juu.
 11. Nitayakumbuka *matendo* ya Yehova : naam, nitayakumbuka *matendo* yako ya kale ya ajabu.
 12. Pia nitaifikiri kazi yako yote : nitawaza habari ya *matendo* yako.
 13. Ewe Mungu, njia yako ni katika pahali patakatifu : ni nani aliye mungu mkuu kama Mungu ?

14. Wewe ndiwe Mungu ufanyaye maajabu : uliudhi-hirisha uwezo wako kati ya mataifa.
15. Kwa mkono wako umewakomboa watu wako : wana wa Yakobo na Yusufu.
16. Yale maji yalikuona, ewe Mungu, yale maji yali-kuona, yakaogopa : vilindi nya maji navyo vikatetemeka.
17. Mawingu yakamwaga maji, mbingu zikatoa sauti : mishare yako nayo ikaenda huko na huko.
18. Sauti ya radi yako ikawa katika kisulisuli ; umeme uliuangaza ulimwengu : nchi ilitetemeka na kutikisisa.
19. Njia yako ilikuwa katika bahari, na mapito yako katika maji makuu : hatua zako hazikujulikana.
20. Uliwaongoza watu wako kama kundi : kwa mkono wa Musa na Haruni.

Siku 15. Sala ya Jioni

ZABURI 78

- S**KILIZENI sheria yangu, enyi watu wangu : tegeni masikio yenu kwa maneno ya kinywa changu.
2. Nitafunua kinywa changu kwa mithali : nitatamka mafumbo ya kale :
 3. Mambo tuliyoyasikia tukayajua : na baba zetu wali-yotuambia.
 4. Hayo hatutawaficha wana wao tukiwaambia kizazi kingine : sifa za Yehova na nguvu zake, na mambo yake ya ajabu aliyofanya.
 5. Kwani alikaza usuhuhuda katika Yakobo na sheria aliweka katika Israeli : aliyoamuru baba zetu, kuwalishwa wana wao :
 6. Ili kizazi kitakachokuwa wajue, hao wana watakao-zaliwa : wasimame na kuwaambia wana wao :
 7. Wamwekee Mungu tumaini lao, wala wasiyasahau matendo ya Mungu, bali wazishike amri zake :
 8. Wala wasiwe kama baba zao, kizazi cha ukaidi na uasi : kizazi kisichojitengeneza moyo, wala roho yake haikuwa amini kwa Mungu.
 9. Wana wa Efiraimu ingawa ni wenye silaha, wapeta uta : walirudi nyuma siku ya vita.

10. Hawakulishika agano la Mungu : wakakataa kwenenda katika sheria yake ;
11. Wakayasahau matendo yake : na mambo yake ya ajabu aliyowaonyesha.
12. Mbele ya baba zao alifanya mambo ya ajabu : katika nchi ya Misiri, konde la Zoani.
13. Aliipasua bahari akawavusha : aliyasimamisha maji mfano wa chungu.
14. Akawaongoza kwa wingu mchana : na usiku kucha kwa nuru ya moto.
15. Akapasua miamba jangwani : akawanywesha maji mengi kama maji ya vilindi.
16. Akatokeza na vijito gengeni : akateremsha maji kama mito.
17. Lakini wakazidi kumtendea dhambi : wakimwasi aliye juu jangwani.
18. Wakamjaribu Mungu miyoni mwao : kwa kutaka chakula kwa tamaa zao.
19. Naam, walimnenea Mungu, wakasema : Je, Mungu awenza kuandika meza jangwani ?
20. Ndio kweli, aliupiga mwamba, maji yakabubujika, ikafurika mito : pia weaza kutupa mkate ? Atawaandalia watu wake nyama ?
21. Basi Yehova alisikia na kughadhabika : moto ukawashwa juu ya Yakobo, hasira nayo ikapanda juu ya Israeli ;
22. Kwa kuwa hawakumwamini Mungu : wala hawakutumainia wokofu wake.
23. Lakini aliyaamuru mawingu juu : akaifungua milango ya mbinguni ;
24. Akawanyeshea manna wale : akawapa nafaka ya mbinguni.
25. Mwanadamu akala chakula cha mashujaa : aliwapelekecha chakula cha kuwashibisha.
26. Alieulekeza upopo wa mashariki mbinguni : akaiongoza kusi kwa uwezo wake.
27. Akawanyeshea nyama kama mavumbi : na ndege zenye mabawa kama mchanga wa bahari :
28. Akaziangusha kati ya matuo yao : pande zote za maskani zao.

29. Wakala wakashiba sana : kwani aliwaletea walivivotamani.
30. Hawakuzuiwa katika tamaa zao : chakula chao kikali vinywani mwao ;
31. Hasira ya Mungu ikapanda ishindane nao : ikawaua walio wanono, ikawaangusha chini vijana wa Israeli.
32. Pamoja na hayo wakazidi kutenda dhambi : wala hawakuamini matendo yake ya ajabu.
33. Kwa hiyo alizikomesha siku zao kama pumzi : na miaka yao kwa hofu ya kuwashtusha.
34. Alipowaua ndipo walipomtafuta : wakarudi wakamtaka Mungu kwa bidii.
35. Walikumbuka kuwa Mungu ni mwamba wao : na Mungu aliye juu mkombozi wao.
36. Lakini waliundanganya kwa vinywa vyao : wakamwambia uwongo kwa ndimi zao.
37. Kwa maana miyo yao haikuwa thabiti kwake : wala hawakuwa waaminifu katika agano lake.
38. Lakini yeye kwa kuwa ana rehema alisamehe uovu wala hakuangamiza : naam, mara nyangi aliipishia mbali ghadhabu yake, wala hakuiwasha hasira yake yote.
39. Akakumbuka ya kuwa wao ni mwili : upepo upitao wala haurudi.
40. Walimwasi jangwani mara ngapi : na kumhuzunisha nyikani !
41. Wakarudi nyuma wakamjaribu Mungu : wakamkasirisha Mtakatifu wa Israeli.
42. Hawakukumbuka mkono wake : wala siku ile alipowakomboa na adui :
43. Alivyoweka ishara zake katika Misiri : na miujiza yake katika konde la Zoani :
44. Aligeuza damu mito yao na vijito vyao : wasipate kunywa.
45. Aliwapelekea mainzi yakawala : na vyura vikawaharibu.
46. Akawapa panzi mazao yao : na nzige akawapa kazi yao.
47. Aliharibu mizabibu yao kwa mvua ya mawe : na mikuyu yao kwa mawe ya barafu.

48. Aliacha ng'ombe zao wapigwe kwa mvua ya mawe : na makundi yao kwa umeme.
49. Aliwapelekea ukali wa hasira yake, ghadhabu na uchungu na taabu : kundi la malaika waletao mabaya.
50. Akaifanyizia hasira yake ijia, wala hakuziepusha nafsi zao na mauti : bali aliiachia tauni uhai wao ;
51. Akampiga kila mzaliwa wa kwanza wa Misiri : malimbuko ya nguvu katika mahema ya Hamu :
52. Bali alwaongoza watu wake kama kondoo : akawachungu kama kundi jangwani.
53. Akawachukua salama wala hawakuogopa : bali bahari iliwanfunikiza adui zao.
54. Akawapeleka hata mpaka wa pahali patakatifu pake : mlima huu alioununua kwa mkono wake wa kuume.
55. Akawafukuza mataifa imbele yao, akawapimia urithi kwa kamba : akawakalisha makabila ya Israeli katika mahema yao.
56. Lakini walimjaribu Mungu aliye juu wakamwasi : wala hawakuzishika shuhuda zake ;
57. Bali walirudi nyuma wakatenda udanganyifu kama baba zao : wakapinduka kama uta usiofaa.
58. Wakamkasirisha kwa mwahali mwao mwa juu : wakamtia wivu kwa sanamu zao.
59. Mungu aliposikia akaghadhabika : akamkataa Israeli kabisa :
60. Hata akaicha maskani ya Shilo : hema aliloliweka kati ya wanadamu :
61. Akazitia nguvu zake kifungoni : na fahari yake mkononi mwa adui.
62. Akawatoa watu wake wapigwe kwa upanga : akaughadhabikia urithi wake.
63. Moto ukawala vijana wao : wanawali wao hawakuimbiwa nyimbo za arusi.
64. Makuhani wao walanguka kwa upanga : wala wajane wao hawakuomboleza.
65. Ndipo Bwana akaamka kama aliyelala usingizi : kama shujaa apigaye kelele baada ya kunywa mvinyo.
66. Akawapiga adui zake akawarudisha nyuma : akawatia aibu ya milele.

67. Akalikataa hema la Yusufu : wala hakulichagua kabilia la Efiraimu :

68. Bali alilichagua kabilia la Yuda : mlima Zayuni alioupenda.

69. Akajenga pahali patakatifu pake kama vilele : kama dunia aliyoureka imara milele.

70. Akamchagua Daudi mtumishi wake : akamwondoa katika mazizi ya kondoo :

71. Nyuma ya kondoo wanyonyeshao alimwondoa : awachunge Yakobo watu wake, na Israeli urithi wake.

72. Akawalisha kwa ukamilifu wa moyo wake : aka-waongoza kwa busara ya mikono yake.

Siku 16. Sala ya Asubuhi

ZABURI 79

EWE Mungu, mataifa wameingia urithi wako : wame-Elinajisi hekalu lako takatifu, wamefanya Yerusalem chungu chungu.

2. Wameziacha maiti za watumishi wako ziwe chakula cha ndege za anga : na mili ya watakatifu wako iwe chakula cha nyama za nchi.

3. Wamemwaga damu yao kama maji pande zote za Yerusalem : wala hapakuwa na mzishi.

4. Tumekeuwa laumu kwa jirani zetu : mzaha na dhihaka kwa wanaotuzunguka.

5. Hata lini, ewe Yehova, utaona hasira milele ? Wivu wako utawaka kama moto ?

6. Ukali wako uwamwagie wasiokujua : na falme zao wasiolingana kwa jina lako.

7. Kwa maana wamemla Yakobo : na matuo yake wameyaharibu.

8. Usikumbuke juu yetu maovu ya baba zetu : rehema zako zije kututangulia hima, kwani tumedhilika sana.

9. Utusaidie, ewe Mungu wa wokofu wetu, kwa ajili ya utukufu wa jina lako : utuokoe, ufute dhambi zetu kwa ajili ya jina lako.

10. Kwa nini waseme mataifa, Yuko wapi Mungu

wao ? Kisasi cha damu ya watumishi wako iliyomwagika kijulikane kati ya mataifa machoni petu.

11. Kuugua kwake aliyefungwa na kuingie mbele zako : kwa kadiri ya uwezo wako uwalinde waliowekewa kufa ;

12. Ukwalipe jirani zetu mara saba vifuani mwao : laamu zao walizokulaumu, ewe Bwana.

13. Na sisi tulio watu wako na kondoo za malisho yako tutakushukuru milele : tutazisimulia sifa zako kizazi kwa kizazi.

ZABURI 80

WEWE uchungaye Israeli, usikie, umwongozaye Yusufu kama kundi : uketiye juu ya makerubi, utoe nuru.

2. Mbele ya Efiraimu na Benjamini na Manase : uziamshe nguvu zako, uje utuokoe.

3. Ewe Mungu, uturudishe : uangazishe uso wako nasi tutaokoka.

4. Ewe Yehova, Mungu wa majeshi : hata lini utaya-ghadhabikia maombi ya watu wako ?

5. Umewalisha mkate wa machozi : umewanywesha machozi kwa kipimo kikuu.

6. Unatufanya sababu ya ugomvi kwa jirani zetu : na adui zetu wanacheka wao kwa wao.

7. Ewe Mungu wa majeshi, uturudishe : uangazishe uso wako nasi tutaokoka.

8. Ulileta mzabibu kutoka Misiri : ukawafukuza mataifa ukaupanda.

9. Ulitengeneza nafasi mbele yake : ukatia mizizi sana ukaijaza nchi.

10. Milima ilifunikwa kwa uvuli wake : matawi yake yalikuwa kama mierezi ya Mungu.

11. Ulieneza matawi yake hata bahari : na vichipuzi yake hata mto.

12. Kwa nini umezibomoa kuta zake ? Hata wote wapitao njiani wakauchuma ?

13. Nguruwe wa msituni huuharibu : na nyama wakali za mashamba wanautafuna.

14. Ewe Mungu wa majeshi, tunakusihi urudi : utazame toka mbinguni, uone, uujiile mzabibū huu,
15. Na mche ule ulioupanda mkono wako wa kuume : na tawi lile ulilofanya imara kwa nafsi yako.
16. Umechomwa moto, umekatwa : kwa laumu ya uso wako wanapotea.
17. Mkono wako na uwe juu ya mtu wa mkono wako wa kuume : juu ya mwanadamu uliyemfanya imara kwa nafsi yako.
18. Nasi hatutakuacha kwa kurudi nyuma : utuhuishe nasi tutalingana kwa jina lako.
19. Ewe Yehova, Mungu wa majeshi, uturudishe : uangazishe uso wako nasi tutaokoka.

ZABURI 81

MWIMBIENI Mungu aliye nguvu zetu : mshangirieni kwa furaha Mungu wa Yakobo.

2. Pazeni zaburi, leteni ngoma : kinubi chenye sauti nzuri na kinanda.
3. Pigeni panda mwandamo wa mwezi : wakati wa mbalamwezi, siku kuu yetu.
4. Kwa maana ni sheria kwa Israeli : ni hukumu ya Mungu wa Yakobo.
5. Aliamuru iwe ushuhuda katika Yusufu, alipoondoka apite katika nchi ya Misiri : nilisikia lugha nisiyoijua.
6. Nililitenga bega lake na mzigo : mikono yake ikaachana na kikapu.
7. Katika shida ulinilingana nikakuokoa, nilikuitika katika starehe ya radi : nilikujaribu penye maji ya Meriba.
8. Sikieni, enyi watu wangu, nami nitakuonyeni : ewe Israeli, kama ukitaka kunisikiliza !
9. Kusiwe na mungu mgeni kwako : wala usimsujidie mungu mgeni.

10. Mimi ni Yehova Mungu wako, niliyekupandisha toka nchi ya Misiri : fumbua sana kinywa chako nami nitakijaza.

11. Lakini watu wangu hawakuisikiliza sauti yangu : na Israeli hawakunitaka.

12. Nikawaacha wakaenda kwa ukaidi wa mioyo yao : waenende katika mashauri yao.
13. Lau kwamba watu wangu wanisikiliza : na Israeli kwenenda katika njia zangu !
14. Ningewadibili adui zao kwa upesi : na juu ya watesi wao ningegeuza mkono wangu.
15. Wamchukiao Yehova wangenyenyeka mbele zake : bali wakati wao ungedumu milele.
16. Naam, angewalisha kwa unono wa nganu : ningekushibisha kwa asali itokayo mwambani.

Siku 16. Sala ya Jioni

ZABURI 82

MUNGU asimama katika kusanyiko la Mungu : katikati ya miungu huhukumu.

2. Hata lini mtahukumu kwa dhulumu : na kuzikubali nyuso za wasio haki ?
3. Mfanyieni hukumu mnyonge na yatima : mtendeeni haki aliyeonewa na maskini.
4. Mwokoeni mnyonge na mhitaji : mwopoeni mikononi mwa wasio haki.
5. Hawajui wala hawafahamu, huenda huko na huko gizani : misingi yote ya nchi imetikisika.
6. Mimi nilisema, Ndinyi miungu : na wana wa aliye juu nyote pia.
7. Lakini mtakufa kama wanadamu : mtaanguka kama mmoja wa wakuu.
8. Usimame, ewe Mungu, uihukumu nchi : kwani wewe utawarithi mataifa wote.

ZABURI 83

EWE Mungu, usinyamae : usifumbe kinywa, usitulie, Ewe Mungu.

2. Kwani adui zako wanafanya ghasia : nao wakuchukiao warcinua vichwa vyao.
3. Juu ya watu wako wanafanya shauri la hila : na kushauriana juu yao uliowaficha.

4. Wamesema, Njoni, tuwakatilie mbali wasiwe taifa : na jina la Isiraeli lisikumbukwe tena.

5. Kwani wameshauriana kwa moyo mmoja : juu yako wanafanya agano :

6. Mahema ya Edomu na Waishmaeli : Moabu na Wahagari :

7. Gebali na Amoni na Amaleki : Filisitia nao wanaokaa Turo :

8. Ashuri naye amepatana nao : wamewasaidia wana wa Loti.

9. Uwatende kama Midiani : kama Sisera, kama Yabini, penye kijito Kishoni :

10. Walioangamizwa Endori : wakawa samadi juu ya nchi.

11. Uwafanye wakuu wao kama Orebu na Zeebu : na masheki yao wote kama Zeba na Zalumuna :

12. Ambao walisema : Na tutamalaki makao ya Mungu.

13. Ewe Mungu wangu, uwafanye wawe kama mavumbi ya kisulisuli : kama wishwa mbele ya upepo :

14. Kama moto uteketezao msitu : kama miali ya moto iiwashayo milima :

15. Ndivyo utakayowafuatia kwa tufani yako : na kuwafadhaisha kwa dharuba yako.

16. Uwajaze nyuso zao fedheha : walitafute jina lako, ewe Yehova.

17. Waabitike, wafadhaike milele : naam, watahayarike na kupotea :

18. Wajue ya kuwa wewe, ambaye jina lako ni Yehova : ndiwe peke yako uliyе juu, juu ya nchi yote.

ZABURI 84

MASKANI zako zapendwa namna gani : ewe Yehova wa majeshi !

2. Nafsi yangu imezionea shauku nyua za Yehova, naam, na kuzikondea : moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu aliye hai.

3. Ndege naye ameoona nyumba, na mbayuwayu kioto

kwa nafsi yake alipoweka makinda yake : madhabahu zako, ewe Yehova wa majeshi, Mfalme wangu na Mungu wangu.

4. Wana heri wakaao nyumbani mwako : watakuhimidi daima.

5. Yuna heri ambaye nguvu zake zatoka kwako : na njia ziendazo *Zayuni* moyoni mwake.

6. Wakipita kati ya bonde la vilio hulifanya kuwa chemchemi : naam, mvua ya vuli hulivika baraka.

7. Huendelea roka nguvu hata nguvu : huonekana *Zayuni* mbele za Mungu kila mmoja wao.

8. Ewe Yehova, Mungu wa majeshi, usikie maombi yangu : usikilize, ewe Mungu wa Yakobo.

9. Ewe Ngao yetu, uangalie : umtazame uso Masihi wako.

10. Kwani ni bora siku moja katika nyua zako, kuliko siku elfu : ningependa kusimama penye kizingiti cha nyumba yako, kuliko kukaa katika mahema ya uovu.

11. Kwa kuwa Yehova Mungu ni jua na ngao ; Yehova atatoa fadhili na utukufu : hatawanyima kitu chema waeenda kwa ukamilifu.

12. Ewe Yehova wa majeshi : yuna heri mwanadamu anayekutumaini wewe.

ZABURI 85

EWE Yehova, umeiridhia nchi yako : umewarejeza wafungwa wa Yakobo.

2. Umeusamehe uovu wa watu wako : umesetiri hatia zao zote.

3. Umeondoa ghadhabu yako yote : umerudi na kuacha ukali wa hasira yako.

4. Uturudishe, ewe Mungu wa wokofu wetu : uukomeshe uchungu ulio nao juu yetu.

5. Je, utatufanya hasira hata milele ? Utadumisha ghadhabu yako kizazi hata kizazi ?

6. Je, hutatuhisha tena : watu wako wakufurahie ?

7. Ewe Yehova, utuonyeshe rehema zako : utupe wokofu wako.

8. Nitasikia atakavyosema Mungu Yehova : kwani atawaambia watu wake amani, na watakatifu wake ; bali wasiurudie upumbavu tena.

9. Hakika wokofu wake u karibu na wamchao : utukufu ukae katika nchi yetu.

10. Fadhili na kweli zimekutana : haki na amani zimebusana.

11. Kweli imechipuka katika nchi : haki imechungulia kutoka mbinguni.

12. Naam, Yehova atatoa kilicho chema : na nchi yetu itatoa mazao yake.

13. Haki itakwenda mbele zake : nayo itafanya hatua zake kuwa njia.

Siku 17. Sala ya Asubuhi

ZABURI 86

UTEGE sikio lako, ewe Yehova, unijibu : kwani mimi ni maskini na mhiti.

2. Unilinde nafsi yangu kwani mimi ni mtu mtawa : ewe Mungu wangu, umwokoe mtumishi wako anayekutumainia wewe.

3. Unifadhilli, ewe Bwana : kwani nakulilia wewe mchana kuchwa.

4. Uifurahishe nafsi ya mtumishi wako : kwani nafsi yangu nakuinulia wewe, ewe Bwana.

5. Kwa maana wewe, Bwana, u mwema, u tayari kusamehe : na mwangi wa fadhili kwa watu wote wakulunganao.

6. Usikie, ewe Yehova, maombi yangu : usikilize sauti ya sala zangu.

7. Siku ya mateso yangu nitakulingana : kwa maana utanijibu.

8. Hakuna kama wewe, ewe Bwana, mionganoni mwa miungu : wala matendo mfano wa matendo yako.

9. Mataifa wote uliowafanya watakuja : watasujudu mbele zako, ewe Bwana, watalitokuza jina lako.

10. Kwa kuwa wewe u mkuu, nawe wafanya miujiza : ndiwe Mungu peke yako.

11. Unifundishe njia yako, ewe Yehova ; nitakwenda katika kweli yako ; uniunge moyo wangu na kicho cha jina lako.

12. Nitakusifu, ewe Bwana Mungu wangu kwa moyo wangu wote : nami nitalitokuza jina lako milele.

13. Kwani fadhili zako kwangu ni nytingi sana : nawe umeniopoa nafsi yangu katika chini ya kuzimu.

14. Ewe Mungu, wenye kiburi wamenishambulia, mkutano wa wenye jeuri wamenitafuta nafsi yangu : hawakukuweka wewe mbele ya macho yao.

15. Lakini wewe, ewe Bwana, u Mungu wa rehema na neema : mvumiliyu, mwangi wa fadhili na kweli.

16. Unielekee, unifadhilli : umpe mtumishi wako nguvu zako, umwokoe mwana wa kijakazi chako.

17. Unionyeshe ishara ya wema, wanichukiao waione na kuaibishwa : kwa kuwa wewe, Yehova, umenisaidia na kunifariji.

ZABURI 87

MSINGI wake upo : juu ya milima mitakatifu.

2. Yehova aipenda milango ya Zayuni : kuliko maskani zote za Yakobo.

3. Umetajwa kwa mambo matukufu : ewe mji wa Mungu.

4. Nitataja Rahabu na Babeli mionganoni mwao wanaonjua : tazama Filisitia na Turo pamoja na Ethiopia : huyu alizaliwa humo.

5. Naam, katika habari za Zayuni itasemwa, Huyu na huyu walizaliwa humo : na yeye aliye juu ataufanya imara.

6. Yehova atahesabu awaandikapo mataifa : huyu walizaliwa humo.

7. Waimba na wacheza pia *watasema* : visima vyangu vyoite vimo mwako.

ZABURI 88

EWE Yehova, Mungu wa wokofu wangu : mchana na Eusiku nimelia mbele zako :

2. Maombi yangu yafike mbele zako : uutegee ukelele wangu sikio lako :

3. Kwani nafsi yangu imeshiba taabu : na uhai wangu umekaribia kuzimu.

4. Nimehesabiwa pamoja nao washukao shimoni : nimekuwa kama mtu asiyé na msaada :

5. Mionganoni mwao waliokufa nimetupwa kama walioawa walalao makaburini : ambao huwakumbuki tena, nao wametengwa mbali na mkono wako.

6. Umenilaza katika chini ya shimo : katika mwahali mwenye giza vilindini.

7. Ghadhabu yako imenilemea : umenitesa kwa mawimbi yako yote.

8. Wanijuao umewatenga nami : umenifanya kuwa chukizo kwao : nimefungwa wala siwezi kutoka.

9. Jicho langu limefisia kwa ajili ya mateso : nimekulangana, ewe Yehova, kila siku, nimekunyoshea wewe mikono yangu.

10. Wafu je, utawaonyesha miujiza : au waliofariki watasisima na kukuhimidi ?

11. Fadhili zako zitasimuliwa kaburini : au uaminifu wako katika uharibifu ?

12. Miujiza yako itajulikana gizani : na haki yako katika nchi ya usahafuli ?

13. Lakini mimi nimekulilia wewe, ewe Yehova : na asubuhi maombi yangu yatakuwasilia.

14. Ewe Yehova, kwa nini kuitupa nafsi yangu : na kunificha uso wako ?

15. Nateswa mimi nami ni katika hali ya kufa tangu uwana : ninapovumilia vitisho vyako nafadhaika.

16. Hasira zako kali zimepita juu yangu : maogofyo yako yameniangamiza.

17. Yamenizunguka kama maji mchana kuchwa : yamenisongea yote pamoja.

18. Mpenzi na rafiki umewatenga nami : nao wanijuao umewatia gizani.

Siku 17. Sala ya Jioni

ZABURI 89

FADHILI za Yehova nitaziimba milele : kwa kinywa changu nitavijulisha vizazi vyote uaminifu wako.

2. Kwani nimesema, Fadhili zitajengwa milele : katika mbingu utauthubutisha uaminifu wako.

3. Nimefanya agano na mteule wangu : nimemwapia Daudi mtumishi wangu ;

4. Wazao wako nitawafanya imara milele : nitakijenga kiti chako cha enzi hata milele.

5. Na mbingu zitaisifu miujiza yako, ewe Yehova : naam, uaminifu wako katika kusanyio la watakatifu wako.

6. Kwani ni nani katika mbingu awezaye kulinganishwa na Yehova ? Ni nani afananaye na Yehova mionganoni mwa wana wa Mungu ?

7. Mungu huogopwa sana katika baraza la watakatifu : huhofiwa kuliko wote wanaomzunguka.

8. Ewe Yehova, Mungu wa majeshi, ni nani aliye hodari kama wewe, ewe Yehova ? na uaminifu wako unakuzunguka.

9. Wewe watawala kiburi cha bahari : mawimbi yake yainukapo wayatuliza wewe.

10. Umemseta Rahabu akawa kama aliyeuawa : kwa mkono wa nguvu zako umewatawanya wakuchukiao.

11. Mbingu ni mali yako, nchi nayo ni mali yako : ulimwengu na vyote viujazavyo ndiwe uliyeupiga msingi wake.

12. Kaskazini na kusini ndiwe uliyeziumba : Taboro na Herimoni hulifurahia jina lako.

13. Wewe una mkono wenye uwezo : mkono wako una nguvu, mkono wako wa kuume umetukuka.

14. Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako cha enzi : fadhili na kweli zahudhuria imbele za uso wako.

15. Wana heri watu wale waijuaon sauti ya shangwe : huuenenda, ewe Yehova, katika nuru ya uso wako.

16. Kwa jina lako hufurahi mchana kuchwa : na kwa haki yako hutukuzwa.

17. Kwani fahari ya nguvu zao ni wewe : na kwa radhi yako pembe yetu itatukuka.

18. Kwani ngao yetu ina Yehova : na mfalme wetu ni wake Mtakatifu wa Israeli.

19. Ndipo ulipowaambia wapendwa wako kwa njozi : ukasema, Nimempa aliye hodari msaada, nimemtukuzu mmoja aliyechaguliwa mionganoni mwa watu.

20. Nimemwona Daudi mtumishi wangu : kwa mafuta yangu matakatifu nimempaka :

21. Ambaye mkono wangu utakuwa thabiti kwake : na mkono wangu utamitia nguvu.

22. Adui hatamwonea : wala mwana wa uovu hata-mtesa.

23. Bali nitawaponda adui zake mbele yake : nitawapiga wanaomchukia.

24. Na uaminifu wangu na fadhili zangu zitakuwa pamoa naye : na kwa jina langu pembe yake itatukuka.

25. Nitaweka mkono wake juu ya bahari : na mkono wake wa kuume juu ya mito.

26. Yeye atanilingana, Wewe u baba yangu : Mungu wangu na mwamba wa wokofu wangu.

27. Mimi nami nitamjalia kuwa mzaliwa wangu wa kwanza : kuwa juu sana kuliko wafalme wa dunia.

28. Hata milele nitamwekea fadhili zangu : na agano langu litafanyika amini kwake.

29. Wazao wake nao nitawadumisha milele : na kiti chake cha enzi kama siku za mbingu.

30. Wanawe wakiiacha sheria yangu : wasiende katika hukumu zangu ;

31. Wakizihalifu amri zangu : wasiyashike maagizo yangu ;

32. Basi nitawarudi makosa yao kwa fimbo : na uovu wao kwa mapigo.

33. Lakini fadhili zangu sitamwondolea : wala sitafanya uaminifu wangu kuwa uwongo.

34. Sitalihalifu agano langu : wala sitalibadili neno lilitotoka midomoni mwangu.

35. Mara moja nimeapa kwa utakatifu wangu : hakika sitamwambia Daudi uwongo ;

36. Wazao wake watadumu milele : na kiti chake cha enzi *kitakuwa* kama jua mbele zangu.

37. Kitathubutika milele kama mwezi : na kama shahidi mwaminifu aliye mbinguni.

38. Lakini wewe umetupa, umekataa : umemghadhabikia Masihi wako.

39. Umechukiwa na agano la mtumishi wako : umenajisi taji yake na kuitupa chini.

40. Umeboma maboma yake yote : umefanya ngome zake kuwa magofu.

41. Wote wapitao njiani wanateka mali zake : amekuwa laumu kwa jirani zake.

42. Umetutkuza mkono wa kuume wa watesi wake : umewafurahisha wote wanaomchukia.

43. Naam, umeurudisha nyuma ukali wa upanga wake : wala hukumsimamisha vitani.

44. Umeikomesha fahari yake : kiti chake cha enzi umekitupa chini.

45. Umezipunguza siku za ujana wake : umemvika abu.

46. Hata lini, ewe Yehova ; utajificha hata milele ? *Hata lini* ghadhabu yako itawaka kama moto ?

47. Ukumbuke jinsi mimi nilivyo wa kitambo : kwa ubatili wa namna gani umeiumba jamii ya wanadamu ?

48. Ni mwandanamu gani atakayeishi asione mauri : atakayejiokoa nafsi yake na nguvu za kuzimu ?

49. Zi wapi fadhili zako za kwanza, ewe Bwana : ulizomwapia Daudi kwa uaminifu wako ?

50. Ukumbuke, ewe Bwana, wanavyotukanwa, watumishi wako : jinsi ninavystahimili kifuani mwangu matukano ya watu walio wakuu :

51. Ambayo adui zako wametukana, ewe Yehova : ambayo wamezitukana hatua za Masihi wako.

52. Na ahimidiwe Yehova mile. Amina. Amina.

Siku 18. Sala ya Asubuhi

ZABURI 90

EWE Bwana, wewe umekuwa makao yetu : kizazi baada ya kizazi.

2. Kabla haijazaliwa milima, kabla hujaiumba dunia : na tangu milele hata milele ndiwe Mungu.

3. Wamrudisha mtu mavumbini : ukisema, Rudini, enyi wanadamu.

4. Kwani miaka elfu machoni pako ni kama siku ya jana ikiisha kupita : na kama kesha la usiku.

5. Wawaghari kisha, huwa kama usingizi : asubuhi wa kama majani yameayo.

6. Asubuhi yachipuka na kumea : jioni yakatika na kukauka.

7. Kwani tumetoweshwa kwa hasira yako : na kwa ghadhabu yako tumefadhaishwa.

8. Umeyaweka maovu yetu mbele zako : siri zetu katika mwanga wa uso wako.

9. Kwani siku zetu zote zimepita katika hasira yako : tumetoweshwa miaka yetu kama hadithi.

10. Siku za miaka yetu ni miaka sabuini, na ikiwa tuna nguvu miaka themanini : kiburi chake ni taabu na ubatili, kwani chapita upesi tukatokomea mara.

11. Ni nani aujuaye uwezo wa hasira yako : na ghadhabu yako kiasi cha kicho kilicho haki yako ?

12. Basi utujulishe kuzihesabu siku zetu : tujipati moyo wa hekima.

13. Urudi, ewe Yehova ; hata lini ? Uwahurumie watumishi wako.

14. Utushibishe asubuhi kwa fadhili zako : nasi tutashangiria na kufurahisi siku zetu zote.

15. Utufurahishe kwa kadiri ya siku ulizotutesa : kama miaka ile tulioona mabaya.

16. Matendo yako na yaonekane kwa watumishi wako : na adhama yako kwa watoto wao.

17. Na uzuri wa Yehova Mungu wetu uwe juu yetu : na kazi ya mikono yetu utufanyie thabiti ; naam, kazi ya mikono yetu uifanye thabiti.

ZABURI 91

AKETIYE pahali pa siri pake aliye juu : atakaa katika uvuli wake Mwenyezi.

2. Katika habari za Yehova nitasema, Yeye ndiye kimbilio langu na ngome yangu : Mungu wangu nitakayemtumainia.

3. Kwani yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji : na tauni iharibuyo.

4. Kwa manyoya yake atakufunika, chini ya mbawa zake utapata kimbilio : uaminifu wake ni ngao na kigao.

5. Hutaogopa hofu ya usiku : wala mshare urukao mchana ;

6. Wala tauni ipitayo gizani : wala uwele uharibuo aduhuri.

7. Wajapoanguka watu elfu ubavuni pako, na watu elfu kumi mkono wako wa kuume : lakini hautakukaribia wewe.

8. Kwa macho yako tu utatazama : na adhabu ya wasio haki utaiona.

9. Kwani wewe, ewe Yehova, ndiwe kimbilio langu ! Umemfanya aliye juu kuwa makao yako ;

10. Mabaya hayatakupata : wala tauni haitalikaribia hemu lako.

11. Kwani atakuagizia malaika zake : wakulinde katika njia zako zote.

12. Mikononi mwao watakuchukua : usije ukajikwaa miguu wako katika jiwe.

13. Utawakanyaga simba na nyoka : mwana simba na joka utawaseta kwa miguu.

14. Kwa kuwa amekaza kunipenda nitamwokoa : nitamweka palipo juu kwa kuwa amenijua jina langu.

15. Atanilingana nami nitamjibu : nitakuwa pamoa naye taabuni, nitamwokoa na kuumtukuza.

16. Kwa siku nyngi nitamshibisha : nami nitamwonyesa wokofu wangu.

ZABURI 92

- N**I neno jema kumshukuru Yehova : na kulisifu jina lako kwa kuimba, ewe uliyi juu ;
2. Kuzitangaza fadibili zako asubuhi : na uaminifu wako wakati wa usiku,
 3. Kwa chombo chenyenye nyuzi kumi, na kwa kinanda : na kwa mlion wa kinubi.
 4. Kwa maana umenifurahisha, ewe Yehova, kwa kazi yako : nitashangiria kwa ajili ya matendo ya mikono yako.
 5. Matendo yako, ewe Yehova, jinsi yalivyo makuu ! Mawazo yako ni siri kuu.
 6. Mtu mjinga hajui : wala mpumbavu hayatambui haya.
 7. Wasio haki walipochipuka kama majani, na wote waliotenda maovu walipositawi : ni kusudi waangamizwe milele.
 8. Bali wewe, ewe Yehova : u mtukufu milele.
 9. Kwani hao adui zako, ewe Yehova, hao adui zako watapotea : na watendao uovu watatawanyika wote pia.
 10. Bali pembe yangu umeinua mfano wa pembe ya nyati : nimepakwa mafuta mabichi.
 11. Na jicho langu limewatazama walioniotea : masikio yangu yamesikia habari za waovu walionishambulia.
 12. Mwenye haki atasitawi kama mtende : atakua kama mwerezi wa Lebanonii.
 13. Walipandwa katika nyumba ya Yehova : watasitawi katika nyua za Mungu wetu.
 14. Watazaa matunda hata wakati wa uzee : watajaa utomvu, watakuwa na ubichi :
 15. Ili kutangaza ya kuwa Yehova ni mwenye adili : ndiye mwamba wangu, ndani yake hamna udhalimu.

Siku 18. Sala ya Jioni

ZABURI 93

YEHOVA hutamalaki, amejivika adhama ; Yehova amejivika, amejifunga nguvu kama mshipi : naam, ulimwengu umethubutika usitikisike.

2. Kiti chako cha enzi kimekuwa thabiti tokea zamani : ndiwe uliyi tangu milele.
3. Ewe Yehova, mito imepaza, mito imepaza sauti zao : mito imepaza mawimbi yao.
4. Kupita sauti ya maji mengi, maji makuu, kupita mawimbi ya bahari yaumkayo : Yehova aliye juu ndiye mwenye mambo makuu.
5. Shuhuda zako ni amini sana : utakatifu ndio uifaa o nyumba yako, ewe Yehova, milele na milele.

ZABURI 94

EWE Mungu wa kisasi, ewe Yehova : ewe Mungu wa kisasi, uangaze.

2. Ujitu kuze, ewe mwenye kuihukumu nchi : uwape wenye kiburi stahili zao.
3. Ewe Yehova, hata lini wasio haki : hata lini wasio haki watashangiria ?
4. Wanatoa maneno makubwa wote watendao uovu : na kusema kwa majivuno na kufanya kiburi.
5. Wanawaseta watu wako, ewe Yehova : wanautesa urithi wako.
6. Wanamuua mijane na ingeni : wanawafisha yatima.
7. Nao husema, Yehova hataona : Mungu wa Yakobo hafikiri.
8. Fikirini, enyi wajinga mionganoni mwa watu : enyi wapumbavu, lini mtapata akili ?
9. Aliyelitia sikio pahali pake asisikie ? Aliyelifanya jicho asione ?
10. Awaadibuye mataifa asikemee : ndiye amfundishaye mwanadamu ?
11. Yehova anajua mawazo ya mwanadamu : ya kuwa ni ubatili.
12. Yuna heri mtu yule umwadibuye, ewe Yehova : umfundishaye kwa sheria yako ;
13. Upate kumstarehesha siku za mabaya : hata asiye haki atakapochimbiwa shimo.
14. Kwani Yehova hatawatupa watu wake : wala hatauacha urithi wake

15. Kwani hukumu itairejea haki : na wote walio wanyofu wa moyo wataifuata.

16. Nani atakayesimama kwa ajili yangu juu ya wabaya ?
Nani atakayenisida juu yao wafanyao maovu ?

17. Kama Yehova asingalikuwa msaada wangu : nafsi yangu kwa upesi ingalikaa penye kimya.

18. Niliposema, Mguu wangu unateleza : fadhili zako, ewe Yehova, zilinitegemeza.

19. Katika wingi wa mashaka yaliyo ndani yangu : faraja zako zaifurahisha nafsi yangu.

20. Je, kiti cha udhalimu kishirikiane nawe : kitungacho madhara kwa njia ya sheria ?

21. Huishambulia nafsi ya mwenye haki : huihukumu damu isiyo hatia.

22. Lakini Yehova amekuwa ngome kwangu : na Mungu wangu mwamba wangu wa kukimbilia.

23. Naye amewarudishia uovu wao, atawaangamiza katika ubaya wao : naam, Yehova Mungu wetu atawaangamiza.

Siku 19. Sala ya Asubuhi

ZABURI 95

NJONI, tumwimbie Yehova : tufanyie shangwe mwamba wa wokofu wetu.

2. Tuje mbele zake kwa shukrani : tumfanyie shangwe kwa zaburi.

3. Kwani Yehova ni Mungu mkuu : na Mfalme mkuu juu ya miungu yote.

4. Mkononi mwake zimo bonde za dunia : hata vilele vya milima ni vyake.

5. Bahari ni yake, ndiye aliyeifanya : na mikono yake iliumba nchi kavu.

6. Njoni, tuabudu, tusujudu : tupige magoti mbele za Yehova aliyetuumba.

7. Kwani ndiye Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake, na kondoo za mkonono wake. Ingekuwa heri leo msikie sauti yake !

8. Msifanye migumu mioyo yenu : kama vile Meriba, kama siku ya Masa jangwani ;

9. Baba zenu waliponijaribu : wakanipima, wakayaona matendo yangu.

10. Miaka arobaini nilihuzunika nacho kizazi hiki nikasema : Ni watu waliopotoka mioyo hawa, hawakuja njia zangu :

11. Ndipo nikaapa kwa hasira yangu : wasiingie rahani mwangu.

ZABURI 96

MWIMBIENI Yehova wimbo mpya : mwimbieni Yehova, nchi yote.

2. Mwimbieni Yehova, libarikieni jina lake : tangazeni habari njema za wokofu wake kila siku.

3. Wahubirini mataifa habari za utukufu wake : na watu wote habari za maajabu yake.

4. Kwani Yehova ni mkuu, mwenye kusifiwa sana : na wa kuogopwa kuliko miungu yote.

5. Kwani miungu yote ya watu ni sanamu tu : lakini Yehova ndiye aliyezifanya mbingu.

6. Heshima na adhama ziko mbele zake : nguvu na uzuri vimo katika pahali patakatifu pake.

7. Mpeni Yehova, enyi jamaa za watu : mpeni Yehova utukufu na nguvu.

8. Mpeni Yehova utukufu wa jina lake : leteni sadaka mkaizingie nyua zake.

9. Mwabuduni Yehova kwa uzuri wa utakatifu : tetemekeni mbele zake, nchi yote.

10. Semeni katika mataifa, Yehova hutamalaki : naam, ulimwengu umethubutika usitikisike, atawahukumu watu kwa adili.

11. Mbingu na zifurahi, nchi na ishangirie : bahari na ivume na vyote viijazavyo ;

12. Shamba na lipige shangwe na vyote vilivyomo : ndipo miti yote ya mwituni itaimba kwa furaha :

13. Mbele za Yehova, kwa maana anakuja, kwa maana anakuja aihukumu nchi : atauhukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa kwa uaminifu wake.

ZABURI 97

YEHOVA hutamalaki, nchi na ishangirie : visima vingi na vifurahi.

2. Mawingu na giza vyamzunguka : haki na hukumu ndio msingi wa kiti chake.

3. Moto hutangulia mbele zake : nao huwateketeza adui zake pande zote.

4. Umeme wake uliuangaza ulimwengu : nchi ikaona ikatetemeka.

5. Milima iliyeyuka kama nta mbele za Yehova : mbele za Bwana wa dunia yote.

6. Mbingu zinatangaza haki yake : na watu wote wameuona utukufu wake.

7. Na waabishwe wote waabuduo sanamu za kuchonga, wajivunao kwa sanamu : msujidieni yeye, enyi miungu yote.

8. Zayuni imesikia ikafurahi, binti za Yuda wakashangiria : kwa sababu ya hukumu zako, ewe Yehova.

9. Kwani wewe, Yehova, ndiwe uliye juu, juu sana kuliko nchi yote : umetukuka sana juu ya miungu yote.

10. Enyi mmpendao Yehova, uchukieni uovu : awalinda wapendwa wake nafsi zao ; awaokoa na mkono wa wasio haki.

11. Nuru imemzukia mwenye haki : na furaha *ime-wazukia* wanyofu wa moyo.

12. Mfurahieni Yehova, enyi wenye haki : kalishukuruni jina lake takatifu.

Siku 19. *Sala ya Jioni*

ZABURI 98

MWIMBIENI Yehova wimbo mpya, kwa maana Mametenda mambo ya ajabu : mkono wa kuume wake mwenyewe, mkono wake mtakatifu umemtendea wokofu.

2. Yehova ameujulisha wokofu wake : machoni pa mataifa amedhihirisha haki yake.

3. Amezikumbuka fadhili zake na uaminifu wake kwa

nyumba ya Israeli : miisho yote ya dunia imeuona wokofu wa Mungu wetu.

4. Mshangirieni Yehova, nchi yote : inueni sauti, imbeni kwa furaha, imbeni sifa.

5. Mwimbieni Yehova sifa kwa kinubi : kwa kinubi na sauti ya zaburi.

6. Kwa panda na sauti ya baragumu : shangirieni mbele za Mfalme, Yehova.

7. Bahari na ivume na vyote viijazavyo : ulimwengu nao wanaokaa ndani yake ;

8. Mito na ipige makofi : milima na iimbe pamoja kwa furaha ;

9. Mbele za Yehova, kwa maana anakuja aihukumu nchi : atauhukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa atawahukumu kwa adili.

ZABURI 99

YEHOVA hutamalaki, mataifa na watetemeke : naam, yeye aketiye juu ya makerubi ; nchi na itikisike.

2. Yehova katika Zayuni ni mkuu : naye ametukuka juu ya mataifa wote.

3. Na walishukuru jina lako kuu la kuhofiya : ndiye mtakatifu.

4. Nguvu za mfalme nazo zapenda hukumu : wewe wathubutisha adili ; wewe wafanya hukumu na haki katika Yakobo.

5. Mtukuzeni Yehova Mungu wetu ; kasujidieni penye daraja la kiti chake cha enzi : ndiye mtakatifu.

6. Musa na Haruni mionganini mwa makuhani wake, na Samweli mionganini mwa walilinganao jina lake : walipomlingana Yehova aliwajibu.

7. Katika nguzo ya wingo alikuwa akisema nao : walishika shuhuda zake na amri aliowapa.

8. Ewe Yehova Mungu wetu, uliwalijib : Mungu msameheji ulikuwa kwao, ingawa uliwapatiliza matendo yao.

9. Mtukuzeni Yehova Mungu wetu, kasujidieni mnikabilii mlima wake mtakatifu : kwa kuwa Yehova Mungu wetu ndiye mtakatifu.

ZABURI 100

MFANYIENI Yehova shangwe, ewe dunia yote.
2. Mtumikieni Yehova kwa furaha : njoni mbele zake kwa kuimba.

3. Jueni kwamba Yehova ndiye Mungu : ndiye aliyetuumba na sisi tu wake; watu wake na kondoo za malisho yake.

4. Ingieni milangotii mwake kwa kushukuru, nyuani mwake kwa kusifu : mshukuruni, lihimidini jina lake.

5. Kwa kuwa Yehova ndiye mwema, fadhilli zake ni za milele : na uaminifu wake vizazi na vizazi.

ZABURI 101

FADHILI na hukumu nitaziimba : kwako wewe, ewe Yehova, nitaimba sifa.

2. Nitajitunza niende kwa akili katika njia ya unyofu ; utakuja kwangu lini ? Nitakwenda kwa unyofu wa moyo ndani ya nyumba yangu.

3. Sitaweka mbele ya macho yangu neno la uovu : kazi yao waliopotoka naichukia, haitaambatana nami.

4. Moyo wa ukaidi utaondoka kwangu : lililo ovu sitalijua.

5. Amsingiziaye jirani yake kwa siri, kuyu nitamharibu : mwenye macho ya kiburi na moyo wa majivuno, huyu sitavumilia naye.

6. Macho yangu yatawaelekeea waaminifu katika nchi, hawa wakae nami : ye ye aendaye katika njia kamiliflu ndiye atakayenitumikia.

7. Hatakaa ndani ya nyumba yangu mtu atendaye hila : asemaye uwongo hatathubutika mbele ya macho yangu.

8. Asubuhi hata asubuhi nitawaharibu wabaya wote wa nchi : niwatenge wote watendao uovu na mji wa Yehova.

Siku 20. Sala ya Asubuhi

ZABURI 102

EWE Yehova, unisikize maombi yangu : na kilio changu kikufikilie uliko.

2. Usiniche uso wako siku ya shida yangu : unitegee sikio lako, siku nilinganapo unijibu upesi.

3. Kwani siku zangu zinatoweka kama moshi : na mifupa yangu inateketea kama kinga.

4. Moyo wangu umepigwa kama majani na kukauka : naam, ninasahau kula chakula changu.

5. Kwa ajili ya sauti ya kuugua kwangu : mifupa yangu imiegandamana na nyama yangu.

6. Nimekuwa kama mwari-nyuni wa jangwani : nimefanana na bundi wa mahameni.

7. Nakesha, tena nimekuwa kama ndege : aliye peke yake juu ya nyumba.

8. Adui zangu wanana ilamu mchana kuchwa : wanao-nichukia kana kwamba wana wazimu huapa kwa kunitaja mimi.

9. Kwani nimekula majivu kama mkate : kinywaji changu nimekichanganya na machozi.

10. Kwa sababu ya ghadhabu yako na hasira yako : kwani umeniinua na kunitupilia mbali.

11. Siku zangu ni kama kivuli kilichotanda : nami nimenyauka kama majani.

12. Bali wewe, ewe Yehova, utakaa milele : na kumbu-kumbu lako kizazi hata kizazi.

13. Wewe utasimama na kuirehemu Zayuni : kwa maana ndio wakati wa kuihurumia, naam, majira yali-yoamriwa yamewadia.

14. Kwani watumishi wako wameyaridhia mawe yake : na kuyaonea huruma mavumbi yake.

15. Na mataifa wataliogopa jina la Yehova : na wafalme wote wa dunia utukufu wako ;

16. Kwani Yehova ameijenga Zayuni : ameonekana katika utukufu wake ;

17. Ameyaelekeea maombi yake aliye mhitaji : wala hakuyadharau maombi yao.

18. Kizazi kitakachokuja kitaandikiwa haya : na watu watakaoumbwa watamsifu Yehova.

19. Kwani ametazama toka pahali patakatifu pake pa juu : toka mbinguni Yehova ameiangalia nchi ;

20. Ili asikie kuugua kwake aliye fungwa : na kuwafungua walioandikiwa kufa ;

21. Watu walitangaze jina la Yehova Zayuni : na sifa zake Yerusalem ;
22. Pindi mataifa wanapokusanyika pamoja : falme nazo ili kumtumikia Yehova.
23. Alizipunguza nguvu zangu njiani : alizifupisha siku zangu.
24. Nilisema, ewe Mungu wangu, usiniondoe katikati ya siku zangu : miaka yako ni tangu kizazi hata kizazi.
25. Mwanzo uliutia msingi wa nchi : na mbingu ni kazi ya mikono yako.
26. Hizi zitaharibika bali wewe utadumu : naam, hizi zitachakaa kama nguo, na kama mavazi utazibadilisha, nazo zitabadilika.
27. Lakini wewe u yeze yule : na miaka yako haitakoma.
28. Wana wa watumishi wako watakaa : na wazao wao watafanywa imara mbele zako.

ZABURI 103

- U**MHIMIDI Yehova, ewe nafsi yangu : na vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu.
2. Umhimidi Yehova, ewe nafsi yangu : wala usizisahau fadhili zake zote ;
 3. Anayekusamehe maovu yako yote : anayekuponya magonjwa yako yote ;
 4. Anayeukomboa uhai wako na uharibifu : anayekutia taji ya fadhili na rehema ;
 5. Anayekushibisha kwa mema kinywa chako : ujana wako ukarejezwiba kama tai.
 6. Yehova anayafanya mambo ya haki : na hukumu kwa wote wanaoonewa.
 7. Alimjulisha Musa njia zake : wana wa Israeli matendo yake.
 8. Yehova amejaa huruma na neema : haoni hasira upesi, ni mwungi wa fadhili.
 9. Hatateta siku zote : wala hatashika *hasira yake* milele.
 10. Hakututendea kwa kadiri ya hatia zetu : wala hakutulipa kwa kadiri ya maovu yetu.

11. Kwani kama mbingu zilivyoinuka juu ya nchi : ndivyo rehema zake zilivyokuwa kuu kwa wamchao.
 12. Kama mashariki yalivyo mbali na magharibi : kadiri ile ile ameweka dhambi zetu mbali nasi.
 13. Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake : ndivyo Yehova anavyowahurumia wamchao.
 14. Kwa maana yeze anatujuua umbo letu : anakumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi.
 15. Mwanadamu siku zake ni kama majani : kama ua la kondeni ndivyo asitawiyivo.
 16. Kwani upepo hupita juu yake, kumbe hayuko : na pahali pake hapatamjua tena.
 17. Bali fadhili za Yehova zina wamchao tangu milele hata milele : na haki yake ina wana wa wana ;
 18. Wale walishikao agano lake : na kuyakumbuka maagizo yake ili wayafanye.
 19. Yehova ameweka kiti chake cha enzi mbinguni : na ufalme wake unatawala vitu vyote.
 20. Mhimidini Yehova, enyi malaika zake : ninyi mlion hodari, ninyi mtendao neno lake, mkiisikiliza sauti ya neno lake.
 21. Mhimidini Yehova, enyi majeshi yake yote : enyi watumishi wake mfanyakao mapenzi yake.
 22. Mhimidini Yehova, enyi matendo yake yote, mwahali mote mwa milki yake : umhimidi Yehova, ewe nafsi yangu.
- Siku 20. Sala ya Jioni*
- ZABURI 104
- U**MHIMIDI Yehova, ewe nafsi yangu : ewe Yehova Mungu wangu, umejfanya mkuu sana, umejivika heshima na adhama :

 2. Unayejivika nuru kama vazi : unayezitandika mbingu kama pazia.
 3. Anayeziweka boriti za orofa zake majini : anayefanya mawingu kuwa gari lake, na kwenda juu ya mabawa ya upepo.
 4. Anayewafanya wajumbe wake kuwa pepo : na watumishi waké kuwa moto wa miali.

5. Aliyeiweka nchi juu ya misingi yake : isitikiske milele.
6. Uliifunika kwa vilindi kama kwa vazi : maji yalikuwa yakisimama juu ya milima.
7. Kwa kukemea kwako yakakimbia : kwa sauti ya radi yako yakaenda zao kwa haraka ;
8. Yakapanda milima, yakateremka mabonde : mpaka pahali ulipoyatengenezea.
9. Umeweka mpaka hayaupiti : hayarudi kuifunikiza nchi.
10. Apeleka chemchemi katika bonde : zapita kati ya milima :
11. Zamnywesha kila nyama wa kondeni : punda za mwitu huzima kiu yao.
12. Kando-kando hukaa ndege za anga ; huimba kati ya matawi.
13. Huinywesha milima toka orofa zake : nchi imeshiba kwa mazao ya kazi zako.
14. Huyameesha majani kwa hayawani : na maboga kwa matumizi ya mwanadamu, ili atoe mkate katika nchi :
15. Na diyai imfurahishayo mtu moyo wake, mafuta kung'aza uso wake : na mkate umburudishao mtu moyo wake.
16. Miti ya Yehova imeshiba : mirezi ya Lebanon aliyoipanda.
17. Ndimo ndege wafanyamo vitundu vyao : na korongo, misunobari ni nyumba yake.
18. Milima mirefu ndiko waliko mbuzi za mwitu : na magenge ni kimbilio la kwanga.
19. Aliufanya mwezi kwa ajili ya muda : jua lajua kuchwa kwake.
20. Wafanya giza kukawa usiku : ndipo atambaapo kila nyama wa mwitu.
21. Wana simba hunguruma wakitaka mawindo : wakatafuta chakula chao kwa Mungu.
22. Jua lachomoza wakaenda zao : na kujilaza mapangoni mwao.
23. Mwanadamu atoka kwenda zake kazini : na kwenye utumishi wake mpaka jioni.

24. Jinsi yalivyo mengi matendo yako, ewe Yehova : kwa hekima umevifanya vyote pia ; dunia imejaa mali zako.
25. Bahari iko kule, kubwa na upana : ndimo vilimo vinavyotukuta havina hesabu ; viumbe.hai vidogo kwa vikubwa.
26. Ndimo zipitamo merikebu : ndimo lewiathani uliyemuumbaacheze ndani yake.
27. Hawa wote wanakungojea wewe : uwape chakula chao wakati wake.
28. Hicho uwapacho wakakiokota : wakunjua mkono wako wakashiba mema.
29. Wauficha uso wako wakafadhaika : waiondoa pumzi yao wakafa, na kuyarudia mavumbi yao.
30. Wampeleka Roho wako wakaumbwa : nawe wau-fanya upya uso wa nchi.
31. Utukufu wa Yehova na udumu milele : Yehova na ayafurahie matendo yake :
32. Anayeitazama nchi ikatetemeka : aigusa milima ikatoka moshi.
33. Nitamwimbia Yehova muda ninaoishi : nitamwimbia Mungu wangu kwa kumsifu wakati wa uhai wangu.
34. Kufikiri kwangu na kuwe kutamu kwake : mimi nitamfurahia Yehova.
35. Wenye dhambi waangamizwe katika nchi ; wasio haki wasiwe huko tena : umhimidi Yehova, ewe nafsi yangu. Aleluya.

- M**SHUKURUNI Yehova, likirini jina lake : wajulisheni watu matendo yake.
2. Mwimbieni, mwimbieni kwa sifa : zungumzeni ajabu zake zote.
 3. Jisifuni kwa jina lake takatifu : na ufurahi moyo wao wamtafutao Yehova.

4. Mtakeni Yehova na nguvu zake : utafuteni uso wake siku zote.

5. Zikumbukeni ajabu zake alizozifanya : miujiza yake na hukumu za kinywa chake ;

6. Enyi wazao wa Iburahimu, mtumishi wake : enyi wana wa Yakobo, wateule wake.

7. Yeye, Yehova, ndiye Mungu wetu : duniani mote mna hukumu zake.

8. Amelikumbuka agano lake milele : neno lile aliloviamuru vizazi elfu ;

9. Alilofanya na Iburahimu : na uapo wake kwa Isaka ;

10. Alilomithubutishia Yakobo iwe amri : na Israeli liwe agano la milele ;

11. Akisema, Nitakupa wewe nchi ya Kanaani : iwe urithi wenu mliopimiwi ;

12. Walipokuwa ni watu wachache tu : naam, wachache sana, kisha wageni ndani yake ;

13. Wakatanga-tanga toka taifa hata taifa : wakitoka ufalme mmoja kwenda kwa watu wengine.

14. Hakumwacha mtu awaonee : hata wafalme ali-wakemea kwa ajili yao ;

15. Akisema, Msiwaguse wapakwa-mafuta wangu : wala msiwadhuu nabii zangu.

16. Akaita njaa ijilie nchi : akaharibu chakula chote walichokitegemea.

17. Alimpelea mtu mbele yao : Yusufu aliuzwa utumwani ;

18. Walimumuuma miguu yake kwa pingu : akatiwa katika minyororo ya chuma ;

19. Hata wakati wa kuwadia neno lake : ahadi ya Yehova ilimjariibu.

20. Mfalme alituma watu akamfungua : mkuu wa watu akamwachia.

21. Akamweka kuwa bwana wa nyumba yake : na mwenye mamlaka juu ya mali zake zote :

22. Awafunge masheki wake kama apendavyo : na kuwafundisha wazee wake hekima.

23. Israeli naye akaingia Misiri : Yakobo akakaa hali ya mgeni katika nchi ya Hamu.

24. Akawajalia watu wake wazae sana : akawafanya kuwa hodari kuliko adui zao.

25. Akawageuza moyo wawachukie watu wake : wakawatendea hila watumishi wake.

26. Akamtuma Musa mtumishi wake : na Haruni ambaye amemchagua.

27. Wakazidhihirsha ishara zake kati yao : na miujiza yake katika nchi ya Hamu.

28. Alitura giza, akalifanya giza : wala hawakuyaasi maneno yake.

29. Aligeuza maji yao yakawa damu : akawafisha samaki zao.

30. Nchi yao ilijaa vyura : vyumbani mwa wafalme wao.

31. Alisema, kukaja makundi ya mainzi : na chawa mipakanii mwao mote.

32. Badala ya mvua aliwapa mvua ya mawe : na moto wenye miali katika nchi yao.

33. Akaipiga mizabibu yao na mitini yao : akaivunja miti ya mipaka yao.

34. Alisema, kukaja nzige : na wana wa nzige wasio-hesabika,

35. Wakala miche yote ya nchi yao : wakala matunda ya ardhi yao.

36. Akawapiga wazaliwa wa kwanza katika nchi yao : malimbuko ya nguvu zao.

37. Akawatoa wenye fedha na dhahabu : na katika makabilaa yao hapakuwa na mtu mwenye kuchecchea.

38. Misiri ilifurahi walipotoka : kwani kwa ajili yao hofu imewaangukia.

39. Alitandaza wingu liwe funiko : na moto utoe nuru usiku.

40. Walitaka akaleta kware : akawashibisha kwa mkate wa mbinguni.

41. Akaufunua mwamba, kukabubujika maji : yakapita katika mwahali mkavu kama mto.

42. Kwani alilikumbuka neno lake takatifu : na Iburahimu mtumishi wake.

43. Akawatoa watu wake kwa furaha : na wateule wake kwa nyimbo za shangwe.

44. Akawapa nchi za mataifa : wakairithi kazi ya watu ;
 45. Ili wazishike amri zake : na kuzitii sheria zake. Aleluya.

Siku 21. Sala ya Jioni

ZABURI 106

A LELUYA. Mshukuruni Yehova kwa kuwa ni mwema : kwa maana fadhili zake ni za milele.

2. Ni nani awezaye kuyanena matendo makuu ya Yehova : kuzihubiri sifa zake zote ?

3. Wana heri washikao hukumu : na kutenda haki siku zote.

4. Unikumbuke, ewe Yehova, kwa kibali uliyo nayo kwa watu wako : unijilie kwa wokofu wako ;

5. Nipate kuuona wema wa wateule wako : nipate kuifurahia furaha ya taifa lako, na kujisifu pamoja na urithi wako.

6. Tumetenda dhambi pamoja na baba zetu : tume-tenda maovu, turnefanya yasiyo haki.

7. Baba zetu katika Misiri hawakufahamu matendo yako ya ajabu : hawakukumbuka wingi wa fadhili zako ; wakaasi penye bahari, Bahari Nyekundu.

8. Lakini aliwaokoa kwa ajili ya jina lake : audhihirishe uwezo wake mkuu.

9. Akaikemea Bahari Nyekundu ikakauka : akawao-ngoza vilindini kana kwamba ni uwanda.

10. Akawaokoa na mkono wa mtu aliyewachukia : na kuwakomboa na mkono wa yule adui.

11. Maji yakawafunika watesi wao : hakusalia hata mmoja wao.

12. Ndipo walipoyaamini maneno yake : waliziimba sifa zake.

13. Wakayashau matendo yake kwa haraka : hawaku-lingojea shauri lake ;

14. Bali walitamani sana jangwani : wakamjaribu Mungu nyikani.

15. Akawapa walichomtaka : akawakondesha nafsi zao.

16. Wakamhusudu Musa matuoni : na Haruni, mta-katifu wa Yehova.

17. Nchi ikapasuka ikammeza Dathani : ikaufunika mkutano wa Abiramu.

18. Moto ukawaka katika mkutano wao : miali yake ikawateketeza wabaya.

19. Walifanya nzao huko Horebu : wakaisujudia sanamu iyeyukayo.

20. Wakaubadili utukufu wao : kuwa mfano wa ng'ombe alaye majani.

21. Wakamsahau Mungu mwokozi wao : aliyetenda makuu katika Misiri ;

22. Matendo ya ajabu katika nchi ya Hamu : mambo ya kutisha penye Bahari Nyekundu.

23. Akasema ya kuwa atawaangamiza, lakini Musa mteule wake alisimama imbele zake kama palipobomolewa : ili aigeuze hasira yake asije akaharibu.

24. Naam, wakaidharau nchi ile ya kupendeza : wala hawakuliamini neno lake ;

25. Bali wakanung'unika hemani mwao : wala hawakuisikiliza sauti ya Yehova.

26. Ndipo akawainulia mkono wake : ya kuwa atawaangamiza jangwani :

27. Ya kuwa atawatawanya wazao wao kati ya mataifa : na kuwatapanya katika nchi mbali-mbali.

28. Wakajambatiza na Baali-Peori : wakala dhabihu za wafu.

29. Wakamkasirisha kwa matendo yao : tauni ikawashambulia.

30. Ndipo Finehasi akasimama akafanya hukumu : tauni ikazuiwa.

31. Akaheabiwa kuwa ana haki : kizazi baada ya kizazi hata milele.

32. Wakamghadhabisha penye maji ya Meriba : hasara ikampata Musa kwa ajili yao ;

33. Kwa sababu waliiasi roho yake : akasema yasiyofaa kwa midomo yake.

34. Hawakuwaharibu watu wa nchi : kama Yehova alivyowaambia ;

35. Bali walijichanganya na mataifa : wakajifunza matendo yao ;
36. Wakazitumikia sanamu zao : nazo zikawa mtego kwao ;
37. Naam, walitoa wana wao na binti zao : kuwa dhabihu kwa mashetani ;
38. Wakamwaga damu isiyo hatia, damu ya wana wao na binti zao : waliowatotoa kuwa dhabihu kwa sanamu za Kanaani ; nchi ikatiwa najisi kwa damu.
39. Ndivyo waliviyotiwa uchafu kwa kazi zao : wakafanya uasherati kwa matendo yao.
40. Hasira ya Yehova ikawaka juu ya watu wake : acauchukia urithi wake.
41. Akawatia mikononi mwa mataifa : na waliowachukia wakawatawala.
42. Adui zao wakawaonea : wakatiishwa chini ya mkono wao.
43. Mara nyingi aliwaponya : lakini wao walikuwa wakimwasi kwa mashauri yao, wakadhilika katika uovu wao.
44. Lakini aliyaangalia mateso yao : aliposikia kilio chao ;
45. Akawakumbukia agano lake : akawahurumia kwa wingi wa fadhili zake.
46. Akawajalia kuhurumiwa : na watu wote walio-wateka.
47. Utuokoe, ewe Yehova Mungu wetu, utukusanye kwa kututoa katika mataifa : ili tulishukuru jina lako takatifu ; tuzifanyie shangwe sifa zako.
48. Na ahimidiwe Yehova, Mungu wa Isiraeli tangu milele hata milele : watu wote na waseme, Amina. Aleluya.

Siku 22. Sala ya Asubuhi

MSHUKURUNI Yehova kwa kuwa ni mwema : kwa maana fadhili zake ni za milele.

2. Na waseme hivi waliokombolewa na Yehova : aliowakomboa na mkono wa mtesi ;

3. Akawakusanya kutoka nchi zote : toka mashariki na magharibi, toka kaskazini na kusini.
4. Walitanga-tanga jangwani katika njia ya nyika : hawakuona mji wa kukaa.
5. Waliona njaa, waliona na kiu : nafsi zao zilikuwa zikizimia ndani yao.
6. Wakamlilia Yehova katika dhiki zao : akawaponya na shida zao.
7. Akawaongoza kwa njia ya kunyoka : wapate kwenda hata mji wa kukaa.
8. Na wamshukuru Yehova kwa fadhili zake : na maajabu yake kwa wanadamu !
9. Kwani aliihibisha nafsi yenye shauku : na nafsi yenye njaa alijaza mema.
10. Waliokaa katika giza na uvuli wa mauti : wame-fungwa katika taabu na chuma ;
11. Kwa sababu waliyaasi maneno ya Mungu : wakalidharau shauri lake aliye juu ;
12. Hata akawadhilli moyo kwa taabu : wakajikwaa wala hakuna msaidizi.
13. Wakamlilia Yehova katika dhiki zao : akawaponya na shida zao.
14. Aliwatoa katika giza na uvuli wa mauti : akayavunja mafungo yao.
15. Na wamshukuru Yehova kwa fadhili zake : na maajabu yake kwa wanadamu !
16. Kwani ameivunja milango ya shaba : ameyakata mapingo ya chuma.
17. Wapumbavu kwa sababu ya ukosaji wao : na kwa sababu ya maovu yao hujitesa.
18. Nafsi zao zachukia kila namna ya chakula : nao waikaribia milango ya mauti.
19. Wamlilia Yehova katika dhiki zao : naye huwaponya na shida zao.
20. Hilituma neno lake, huwaponya : huwatoa katika maangamizo yao.
21. Na wamshukuru Yehova kwa fadhili zake : na maajabu yake kwa wanadamu !

22. Na wamtolee dhabihu za kushukuru : na kuyasimulia matendo yake kwa kuimba.
23. Washukao baharini katika merikebu : wafanyao kazi katika maji mengi ;
24. Hao wameiona kazi ya Yehova : na maajabu yake vilindini.
25. Kwani yuasema na kuondokesha upopo wa dharuba : uyainua juu mawimbi yake ;
26. Wapanda mbinguni, wateremka vilindini : nafsi zao zayeyuka kwa hali mbaya ;
27. Wayumba-yumba, wapepesuka kama mlevi : akili zao zote zawapotea.
28. Wakamlilia Yehova katika dhiki zao : naye huwatoa katika shida zao.
29. Huituliza dharuba ikawa shwari : hata mawimbi yake yakanyamaza.
30. Ndipo wafurahi kwa kuwa yametulia : naye huwleta hata bandari waliyoitamani.
31. Na wamshukuru Yehova kwa fadhili zake : na maajabu yake kwa wanadamu !
32. Na wamtukuze katika kusanyiko la watu : na wamhimidi katika baraza ya wazee.
33. Hugeuza mito ikawa jangwa : na chemchemi za maji zikawa nchi ya kiu ;
34. Nchi ya matunda mengi ikawa uwanda wa chumvi : kwa sababu ya ubaya wao walioikaa.
35. Hugeuza jangwa ikawa ziwa la maji : na nchi kavu ikawa chemchemi za maji.
36. Akawakalisha huko wenye njaa : watengeneze mji wa kukaa ;
37. Na kupanda mbegu mashambani, na kutulua mizabibu : na kujipatia matunda yake.
38. Naye huwabarikia wakaongezeka sana : wala hayapunguzi makundi yao.
39. Tena wapungua na kudhilika : kwa kuonewa na mabaya na huzuni.
40. Humwagia wakuu dharau : na kuwazungusha katika nyika isiyo njia.

41. Humweka mhitaji juu mbali na mateso : akamfanya jamaa kama kundi la kondoo.
42. Wanyofu wa moyo wataona na kufurahi : na uovu wa kila namna unajifumba kinywa.
43. Aliye na hekima atayaangalia hayo : nao watazfikiri fadhili za Yehova.

Siku 22. Sala ya Jioni

- N**AFSI yangu i thabiti, ewe Mungu nitaimbba, naam, nitaimba na kusifu, kwa huo utukufu wangu.
2. Amka, kinanda na kinubi : nitaamka mimi alfajiri.
 3. Nitakushukuru, ewe Yehova, kati ya watu : nita-kuimbia sifa kati ya mataifa.
 4. Kwani fadhili zako ni kubwa hata mbinguni : na uaminifu wako hata mawinguni.
 5. Utukuzwe juu ya mbingu, ewe Mungu : na juu ya nchi yote utukufu wako.
 6. Ili wapenzi wako waopolewe : uokoe kwa mkono wako wa kuume, utuitike.
 7. Mungu amenena kwa utakatifu wake, nami nita-shangiria : nitaigawanya Shekemu, nitalipima bonde la Sukothi.
 8. Gileadi ni yangu, na Manase ni yangu, na Efiraimu ni nguvu ya kichwa changu : Yuda ni fimbo yangu ya kifalme.
 9. Moabu ni bakuli langu la kunawia : nitamtupia Edomu kiatu changu, nitampigia Filisitia kelele za vita.
 10. Ni nani atakayenipeleka hata mji wenye maboma ? Ni nani aliyeniongoza hata Edomu ?
 11. Hukututupa, ewe Mungu ? Nawe, ewe Mungu, hutoki na majeshi yetu.
 12. Utuletee msaada juu ya adui : kwani wokofu wa binadamu haufai.
 13. Kwa msaada wa Mungu tutatenda mambo ya ushujaa : kwani ye ye atawakanyaga adui zetu.

ZABURI 109

- E**WE Mungu wa sifa zangu : usinyamaze ; :
2. Kwa maana wamenifumbulia kinywa cha mtu asiyi haki, kinywa cha hila : wamesema nami kwa ulimi wa uwongo.
 3. Naam, kwa maneno ya chuki wamenizunguka : wamepigana nami bure.
 4. Badala ya upendo wangu hunishtaki : ila mimi, naomba.
 5. Wamenilipa mabaya badala ya mema : na chuki badala ya upendo wangu.
 6. Uweke mtu asiyi haki juu yake : mshtaki asimame mkono wake wa kuume.
 7. Katika kuhukumiwa na aonekane kuwa ni mtu asiyi haki : na sala yake igeuzwe kuwa ni dhambi.
 8. Siku zake na ziwe chache : usimamizi wake na atwae mtu mwininge.
 9. Wanawe na wawe yatima : na mkewe mjane.
 10. Kutanga na watange wanawe na kuomba : watafute chakula katika mahame yao.
 11. Mdai na anase vitu vyote alivyo navyo : wageni na wateke mapato ya kazi yake.
 12. Asiwe na mtu wa kumfanya fadhili : wala mtu wa kuwahurumia yatima wake.
 13. Wazao wake waangamizwe : jina lao likafutwe katika kizazi cha pili.
 14. Uovu wa baba zake ukumbukwe mbele za Yehova : na dhambi ya mama yake isifutwe.
 15. Ziwe mbele za Yehova daima : aliondoe kumbuku-mbu lao duniani.
 16. Kwa kuwa hakukumbuka kutenda fadhili : bali alimfukaza mnyonge na mhitaji, hata kumfisha mtu aliyeunjika moyo.
 17. Naye alipenda kulaani, kukampata : hakupendezwa na kubarikia, kukawa mbali naye.
 18. Alijivika laana kana kwamba ni vazi lake : ikamwilingilia moyoni kama maji, na kama mafuta mifupani mwake.

19. Na iwe kwake kama vazi ajivikalo : na kama mshipi ajifungao daima.
 20. Hayo ndiyo malipo ya washtaki wangu, yatokayo kwa Yehova : na ya hao wanaoisingizia nafsi yangu mabaya.
 21. Nawe, ewe Yehova Bwana, unitendee kwa ajili ya jina lako : kwa kuwa fadhili zako ni njema uniokoe ;
 22. Kwa maana mimi ni mnyonge na mhitaji : na moyo wangu umjejeruhwa ndani yangu.
 23. Nimepitia kama kivuli kianzacho kutoweka : ninapeperushwa kama nzige.
 24. Magoti yangu yamedhoofu kwa kufunga : na mwili wangu umekonda kwa kukosa mafuta.
 25. Nami nimekuwa laumu kwao : wanianapo watikisa vichwa vyao.
 26. Unisaide, ewe Yehova, Mungu wangu : uniokoe kwa kadiri ya fadhili zako ;
 27. Ili wajue ya kuwa ndio mkono wako : ya kwamba wewe, Yehova, umeyafanya.
 28. Wao na walaani, bali wewe ubarikie : watakapoo-ndoka wao wataaibishwa, bali mtumishi wako atafurahi.
 29. Washtaki wangu na wavikwe fedheha : wajivike abu yao kama joho.
 30. Nitamshukuru sana Yehova kwa kinywa changu : naam, nitamsifu kati ya makutano.
 31. Kwani atasimama mkono wa kuume wa mhitaji : amwokoe nao wanaoihukumu nafsi yake.
- Siku 23. Sala ya Asubuhi**
- ZABURI 110
- Y**EHOVA alimwambia bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume : hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako.

 2. Yehova atainyosha firimo ya nguvu zako toka Zayuni : uwe na enzi kati ya adui zako.
 3. Watu wako wanajitoa kwa hiari siku ya uwezo wako : kwa uzuri wa utakatifu, tokea tumbo la asubuhi, unao umande wa ujana wako.

4. Yehova ameapa wala hataghairi : ndiwe kuhani milele kwa mfano wa daraja la Melikisedeki.
5. Bwana mkono wako wa kuume : atawaseta wafalme siku ya ghadhabu yake.
6. Atahukumu kati ya mataifa, atajaza *nchi* mizoga : ataseta kichwa katika *nchi* nyangi.
7. Atakunywa maji ya mto njiani : kwa hiyo atajinau kichwa chake.

ZABURI III

- A LELUYA.** Nitamshukuru Yehova kwa moyo wangu wote : katika baraza la wanyofu wa moyo na katika mukutano.
2. Matendo ya Yehova ni makuu : yatafutwa sana na wapendezwao nayo.
 3. Kazi yake ni heshima na adhama : na haki yake yakaa milele.
 4. Amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu : Yehova ni mwenye fadhili na rehema.
 5. Amewapa wamchao chakula : atalikumbuka agano lake milele.
 6. Amewajulisha watu wake uwezo wa matendo yake : kwa kuwapa urithi wa mataifa.
 7. Matendo ya mikono yake ni kweli na hukumu : maagizo yake yote ni amini.
 8. Yamethubutika milele na milele : yamefanywa katika kweli na adili.
 9. Amewapelekeea watu wake ukombozi, ameamuru agano lake liwe la milele : jina lake ni takatifu la kustahiwa.
 10. Kumcha Yehova ndio mwanzo wa hekima, wote wafanyao haya wana akili njema : sifa zake zakaa milele.

ZABURI III

- A LELUYA.** Yuna heri mtu yule amchaye Yehova : apendezwaye sana na maagizo yake.
2. Wazao wake watakuwa hodari duniani : kizazi cha wenyewe adili kitabarikiwa.

3. Nyumbani mwake mna utajiri na mali : na haki yake yakaa milele.
4. Nuru huwazukia wenyewe adili gizani : *ana* fadhili na huruma na haki.
5. Yuna heri atendaye fadhili na kukopesha : atategeneza mambo yake kwa haki.
6. Kwa maana hataondoshwa kamwe : mwenye haki atakumbukwa milele.
7. Hataogopa habari mbaya : moyo wake u imara ukimtumaini Yehova.
8. Moyo wake umethubutika hataogopa : hata atakapowaona adui zake.
9. Amekirimi, amewapa maskini, haki yake yakaa milele : pembe yake itatukuzwa katika utukufu.
10. Asiye haki ataona na kusikitika, atasaga meno yake na kuyeyuka : tamaa ya wasio haki itapotea.

ZABURI III

- A LELUYA.** Sifuni, enyi watumishi wa Yehova : Alisifuni jina la Yehova.
2. Jina la Yehova lihimidiwe : tangu leo na hata milele.
 3. Toka maawio ya juu hata machweo yake : jina la Yehova husifiwa.
 4. Yehova ni mkuu juu ya mataifa wote : na utukufu wake ni juu ya mbingu.
 5. Ni nani aliye mfano wa Yehova : Mungu wetu aketiye juu,
 6. Ajinyenyekaze ili atazame : ya mbinguni na ya duniani ?
 7. Humwinua mnyonge kutoka mavumbini : humpanidsha maskini kutoka jaani ;
 8. Amketishe pamoja na wakuu : pamoja na wakuu wa watu wake.
 9. Humweka nyumbani mwanamke aliye tasa : ni mama wa watoto mwenye furaha. Aleluya.

Siku 23. Sala ya Jioni

ZABURI 114

- I**SRAELI alipotoka katika Misiri : nyumba ya Yakobo
katika watu wa lugha ya kigeni ;
 2. Yuda ilikuwa pahali patakatifu pake : Israeli milki
yake.
 3. Bahari iliona ikakimbia : Yorodani ilirudishwa
nyuma.
 4. Milima iliruka kama kondoo waume : vilima kama
wana kondoo.
 5. Una nini, ewe bahari, hata ukimbie ? Nawe
Yorodani, hata ukarudi nyuma ?
 6. Enyi milima, hata mkaruka kama kondoo waume :
nanyi vilima, kama wana kondoo ?
 7. Tetemeka, ewe nchi, mbele za uso wa Bwana : mbele
za uso wa Mungu wa Yakobo ;
 8. Aliyeugeuza mwamba kuwa ziwa la maji : jiwe gumu
kuwa chemchemi ya maji.

ZABURI 115

- U**SITUTUKUZE, ewe Yehova, usitutukuze sisi, bali
ulitukuze jina lako : kwa ajili ya fadhili zako, kwa
ajili ya uaminifu wako.
 2. Mbona wasema mataifa : Yuko wapi Mungu wao ?
 3. Lakini Mungu wetu yuko mbinguni : alitakalo lote
amelitenda.
 4. Sanamu zao ni fedha na dhahabu : kazi ya mikono ya
wanadamu.
 5. Zina vinywa lakini hazisemi : zina macho lakini
hazioni ;
 6. Zina masikio lakini hazisikii : zina pua lakini hazisikii
harufu ;
 7. Zina mikono lakini hazishiki kitu, zina miguu lakini
haziendi : wala hazitoi sauti kwa koo zao.
 8. Wazifanyao watafanana nazo : kila mmoja anaye-
zitumainia.

9. Ewe Israeli, mtumainini Yehova : yeze ni msaada
wao na ngao yao.
 10. Ewe nyumba ya Haruni, mtumainini Yehova : yeze
ni msaada wao na ngao yao.
 11. Enyi mmchao Yehova, mtumainini Yehova : yeze
ni msaada wao na ngao yao.
 12. Yehova ametukumbuka, naye atatubarikia : atai-
barikia nyumba ya Israeli, ataibarikia nyumba ya
Haruni.
 13. Atawabarikia wamchao Yehova : wadogo kwa
wakubwa.
 14. Yehova na azidi kuwaongeza ninyi : ninyi na watoto
wenu.
 15. Mbarikiwe ninyi na Yehova : aliyezfanya mbingu
na nchi.
 16. Mbingu ni mbingu za Yehova : bali nchi amewapa
wanadamu.
 17. Sio wafu wamsifuo Yehova : wala wowote washukao
kwenye kimya ;
 18. Bali sisi tutamhimidi Yehova : tangu leo na hata
milele. Aleluya.

Siku 24. Sala ya Asubuki

ZABURI 116

- N**AMPENDA Yehova kwa kuwa amesikiliza : sauti
yangu na sala zangu.
 2. Kwa maana amenitegea sikio lake : kwa hiyo nitam-
lingana siku zangu zote.
 3. Kamba za mauti zilinizunguka, shida za kuzimu
zilinipata : niliona taabu na huzuni.
 4. Nikalilingana jina la Yehova : ewe Yehova, nakuo-
mba sana, unioke nafsi yangu.
 5. Yehova ni mwenye neema na haki : naam, Mungu
wetu ni mwenye rehema.
 6. Yehova huwalinda wasio hila : nilidhilika akanikoa.
 7. Urudi, ewe nafsi yangu, rahani mwako : kwa kuwa
Yehova amekutendea kwa ukarimu.

8. Kwani umeniponya nafsi yangu na mauti, macho yangu na machozi : na miguu yangu na kuanguka.

9. Nitaenenda mbele za Yehova : katika nchi ya walio hai.

10. Naamini, kwani nitasema : mimi niliteswa sana.

11. Mimi nilisema katika haraka yangu : wanadamu wote ni waongo.

12. Nimirudishie Yehova nini : kwa ukarimu wake wote alionitendea ?

13. Nitakipokea kikombe cha wokofu : nitalilingana jina la Yehova.

14. Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Yehova : naam, mbele ya watu wake wote.

15. Ina thamani machoni pa Yehova : mauti ya watakatifu wake.

16. Ewe Yehova, hakika mimi ni mtumishi wako : mtumishi wako, mwana wa kijakazi chako ; umefungua vifungo vyangu.

17. Nitakutolea dhabihu ya kushukuru : nitalilingana jina la Yehova.

18. Nitaziondoa nadhiri zangu kwa Yehova : naam, mbele ya watu wake wote ;

19. Katika nyua za nyumba ya Yehova : ndani yako, ewe Yerusalem. Aleluya.

ZABURI 117

MSIFUNI Yehova, enyi mataifa wote : mhimidini, enyi watu wote.

2. Kwani fadhili zake kwetu sisi ni kuu : na uaminifu wa Yehova ni na milele. Aleluya.

ZABURI 118

MSHUKURUNI Yehova kwa kuwa ni mwema : kwa maana fadhili zake ni za milele.

2. Isiraeli na aseme sasa : ya kwamba fadhili zake ni za milele.

3. Nyumba ya Haruni na waseme sasa : ya kwamba fadhili zake ni za milele.

4. Wamchao Yehova na waseme sasa : ya kwamba fadhili zake ni za milele.

5. Katika shida yangu nilimlingana Yehova : Yehova akanijibu akaniweka panapo nafasi.

6. Yehova yuko upande wangu, sitaogopa : mwana-damu atanitenda nini ?

7. Yehova yuko upande wangu, msaidizi wangu : kwa hiyo nitawatazama wanaonichukia.

8. Ni heri kumkimbilia Yehova : kuliko kuwatumania wanadamu.

9. Ni heri kumkimbilia Yehova : kuliko kuwatumania wakuu.

10. Mataifa wote walinizunguka : kwa jina la Yehova nitawakatilia mbali.

11. Walinizunguka, naam, walinizunguka : kwa jina la Yehova nitawakatilia mbali.

12. Walinizunguka kama nyuki, wamezimika kama moto wa miibani : kwa jina la Yehova nitawakatilia mbali.

13. Ulinisukuma sana ili nianguke : Yehova akanisidia.

14. Yehova ni nguvu zangu na wimbo wangu : naye amekuwa wokofu wangu.

15. Sauti ya furaha na wokofu imo hemani mwa wenyewe haki : mkono wa kuume wa Yehova hutenda makuu.

16. Mkono wa kuume wa Yehova umetukuzwa : mkono wa kuume wa Yehova hutenda makuu.

17. Sitakufa bali nitaishi : nami nitasimulia matendo ya Yehova.

18. Yehova ameniadhibu sana : lakini hakuniacha nife.

19. Nifungulieni milango ya haki : nitaingia, nita-mshukuru Yehova.

20. Mlango huu ni wa Yehova : wenyewe haki watauingia.

21. Nitakushukuru kwa maana umenijibu : nawe umekuwa wokofu wangu.

22. Jiwe walilolikataa waashi : limekuwa jiwe kuu la pembeni.

23. Neno hili limetoka kwa Yehova : ni ajabu machoni petu.

24. Siku hii ndiyo aliyoifanya Yehova : tutashangiria na kuifurahia.

25. Ewe Yehova, utuokoe sasa, twakusihi : twakusihi, ewe Yehova, utufanikishe.

26. Na abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Yehova : tumewabarikia ninyi toka nyumbani mwa Yehova.

27. Yehova ndiye aliye Mungu, naye ametupa nuru : ifungeni madhabuha kwa kamba pemberi mwa madhabuha.

28. Ndiwe Mungu wangu nami nitakushukuru : ewe Mungu wangu, nitakutukuza.

29. Mshukuruni Yehova kwa kuwa ni mwema : kwa maana fadhilli zake ni za milele.

Siku 24. Sala ya Jioni

ZABURI 119. 1-32

Alef

WANA heri walio kamili katika njia : waendao katika sheria ya Yehova.

2. Wana heri wazitii shuhuda zake : wamtafutao kwa moyo wote.

3. Naam, hawatendi ubatili : waenda katika njia zake.

4. Wewe umetuamuru mausio yako : ili tuyatii sana.

5. Lau kwamba njia zangu zathubutishwa : ili nizitii amri zako !

6. Ndipo sitaaibika : nikiyaangalia maagizo yote.

7. Nitakushukuru kwa unyofu wa moyo : nikiisha kujifunza hukumu za haki yako.

8. Nitazitii amri zako : usiniache kabisa.

Bethi

9. Kijana ataisafishaje njia yake ? Kwa kuitunza, akilifuata neno lako.

10. Kwa moyo wangu wote nimekutafuta : usiniache nipotee mbali na maagizo yako.

11. Moyoni mwangu nimeliweka neno lako : nisije nikakutendea dhambi.

12. Umchimidiwa, ewe Yehova : unifundishe amri zako.

13. Kwa midomo yangu nimezisimulia : hukumu zote za kinywa chako.

14. Nimeifurahia njia ya shuhuda zako : kana kwamba ni jamii ya mali.

15. Nitayafikiri mausio yako : nami nitaziangalia njia zako.

16. Nitajifurahisha sana kwa amri zako : sitalisahau neno lako.

Gimeli

17. Umtendee mtumishi wako kwa ukarimu, nipate kuishi : nami nitalitii neno lako.

18. Fumbua macho yangu niyatazame : maajabu yatokayo katika sheria yako.

19. Mimi ni mgeni katika nchi : usinifiche maagizo yako.

20. Nafsi yangu imepondeka kwa kutamani : hukumu zako kila wakati.

21. Umewakernea wenye kiburi waliolaaniwa : waendao mbali na maagizo yako.

22. Uniondoolee laumu na dharau : kwani nimezishika shuhuda zako.

23. Wakuu nao waliketi wakanineni : mtumishi wako alizifikiri amri zako.

24. Shuhuda zako nazo ndiyo furaha yangu : na washauri wangu.

Dalethi

25. Nafsi yangu imeambatana na mavumbi : unihuise sawasawa na neno lako.

26. Nilizisimulia njia zangu ukanjibu : unifundishe amri zako.

27. Unifahamishe njia ya mausio yako : nami nitaya-fikiri maajabu yako.

28. Nafsi yangu inayeyuka kwa uzito : unitie nguvu sawasawa na neno lako.

29. Uniondoolee njia ya uwongo : unineemeshe kwa sheria yako.

30. Nimeichagua njia ya uaminifu : hukumu zako nimeziweka *mbele yangu*.
31. Naambatana na shuhuda zako : ewe Yehova, usiniaibishe.
32. Nitakwenda mbio katika njia ya maagizo yako : utakaponikunjua moyo wangu.

Siku 25. Sala ya Asubuhi

ZABURI 119. 33-72

He

33. Unifundishe, ewe Yehova, njia ya amri zako : nami nitaishika hata mwisho.
34. Unifahamishe nami nitaishika sheria yako : naam, nitaitii kwa moyo wangu wote.
35. Uniendeshe katika mapito ya maagizo yako : kwa maana nimependezwa nayo.
36. Unielekeze moyo wangu na shuhuda zako : wala usielekee tamaa.
37. Unigeuze macho yangu nisitazame visivyofaa : unihuise katika njia yako.
38. Umthubutishie mtumishi wako neno lako : inayohusu kicho chako.
39. Uniondolee laumu niiogopayo : kwani hukumu zako ni njema.
40. Tazama, nimeyatamani mausio yako : unihuise kwa haki yako.

Vau

41. Fadhili zako zinifiki na mimi, ewe Yehova : wokofu wako sawasawa na neno lako.
42. Nami nitarnjibu neno anilaumuye : kwa maana nalitumainia neno lako.
43. Wala usiliondoe neno la kweli kinywani mwangu kabisa : kwani nimezingojea hukumu zako.
44. Nami nitaitii sheria yako daima : milele na milele.
45. Nami nitakwenda panapo nafasi : kwa kuwa nimejifunza mausio yako.

46. Nitazinena shuhuda zako mbele ya wafalme : wala sitaona aibu.
47. Nami nitajifurahisha sana kwa maagizo yako : niliyoyapenda.
48. Na mikono yangu nitayainulia maagizo yako niliyoyapenda ; nami nitazifikiri amri zako.

Zaini

49. Likumbuke neno ulilomwambia mtumishi wako : kwa sababu umenitumainisha.
50. Hii ndiyo faraja yangu katika taabu yangu : ya kwamba ahadi yako imenihuisha.
51. Wenyewe kiburi wamenidharau mno : sikujiepusha na sheria zako.
52. Nimezikumbuka hukumu zako za kale, ewe Yehova : nikajifariji.
53. Ghadhabu imenishika : kwa sababu ya wasio haki waiachao sheria yako.
54. Amri zako zimekuwa nyimbo zangu : katika nyumba ya ugeni wangu.
55. Wakati wa usiku nimelikumbuka jina lako, ewe Yehova : nikaitii sheria yako.
56. Hayo ndiyo niliyokuwa nayo : kwa sababu nimeyashika mausio yako.

Hetu

57. Yehova ndiye aliye fungu langu : nimesema kwamba itayattii maneno yako.
58. Nilikuomba radhi yako kwa moyo wangu wote : unifadhili sawasawa na neno lako.
59. Nilizifikiri njia zangu : na miguu yangu nilizielekezea shuhuda zako.
60. Nilifanya haraka wala sikukawia : kuyatii maagizo yako.
61. Kamba za wasio haki zimenifunga : sikuisahau sheria yako.
62. Katikati ya usiku nitaamka nikushukuru : kwa sababu ya hukumu za haki yako.

63. Mimi ni mwenzi wa wote wakuchao : na wao wayatio mausio yako.
 64. Ewe Yehova, dunia imejaa fadhili zako : unifundishe amri zako.

Tethi

65. Umemtendea mema mtumishi wako : ewe Yehova, sawasawa na neno lako.
 66. Unifundishe akili na maarifa : kwani nimeyaamini maagizo yako.
 67. Kabla sijateswa mimi nilipotea : lakini sasa nime-litii neno lako.
 68. Wewe u mwema na mtenda mema : unifundishe amri zako.
 69. Wenye kiburi wamenizulia uwongo : mimi kwa moyo wangu wote nitayashika mausio yako.
 70. Miyo yao imenenepe ~~kama~~shahamu : mimi nime-furahia sana sheria yako.
 71. Ilikuwa vyema kwangu kuwa niliteswa : nipate kujifunza amri zako.
 72. Sheria ya kinywa chako ni njema kwangu : kuliko maelfu ya dhahabu na fedha.

Siku 25. Sala ya Jioni

ZABURI 119. 73-104

Yodi

73. Mikono yako imenifanya na kunitengeneza : uni-fahamishe nijifunze maagizo yako.
 74. Wakuchao wataniona na kufurahi : kwa sababu nimelingojea neno lako.
 75. Najua ya kuwa hukumu zako zina haki, ewe Yehova : na kwa uaminifu umenitesa.
 76. Fadhili zako, nakuomba, na ziwe faraja kwangu : sawasawa na neno lako kwa mtumishi wako.
 77. Rehema zako zinijie nipate kuishi : kwani sheria yako ni furaha yangu.

78. Wenye kiburi waaibike, kwani wamenidhilimu kwa uwongo : nitayafikiri mausio yako.
 79. Wakuchao wanirudie : nao watajua shuhuda zako.
 80. Moyo wangu uwе mkamilifu katika amri zako : nisije nikaabika.

Kafu

81. Nafsi yangu imedhoofu kwa shauku ya wokofu wako : nalingojea neno lako.
 82. Macho yangu yamedhoofu kwa kulitazamia neno lako : nisemapo, Lini utakaponifariji ?
 83. Kwani nimekuwa kama kiriba katika moshi : nami sizisahau amri zako.
 84. Siku za mtumishi wako ni ngapi : ni lini utakapofanya hukumu juu yao wanaonifuatia ?
 85. Wenye kiburi wamenichimbia mashimo : ambao hawaifiati sheria yako.
 86. Maagizo yako yote ni amini : wanani fuatia bure, unisaidie.
 87. Walikuwa karibu na kunikomesha katika nchi : lakini sikuyaacha mausio yako.
 88. Unihuishe kwa fadhili zako : nami nitazishika shuhuda za kinywa chako.

Lamedi

89. Milele, ewe Yehova : neno lako lasimama imara mbinguni.
 90. Uaminifu wako huenea kizazi baada ya kizazi : umeiweka nchi nayo inakaa.
 91. Kwa hukumu zako vimesimama imara hata leo : kwani vitu vyote ni watumishi wako.
 92. Kama sheria yako isingalikuwa furaha yangu : ningalipotea hapo katika taabu zangu.
 93. Hata milele sitayasahau maagizo yako : kwani kwa hayo umenihuisha.
 94. Mimi ni wako, uniockoe : kwa maana nimetafuta sana mausio yako.
 95. Wasio haki wameniotea ili kunipoteza : nitazifikiri shuhuda zako.

96. Nimeuona mwisho wa ukamilifu wote : agizo lako ni pana mno.

Mem

97. Sheria yako naipenda mno ajabu : ndiyo kufikiri kwangu mchana kuchwa.

98. Maagizo yako hunitia hekima kuliko adui zangu : kwa maana siku zote iko kwangu.

99. Nina akili kuliko wakufunzi wangu wote : kwani shuhuda zako ndizo nizifikirizo.

100. Nina ufahamu kuliko wazee : kwa kuwa nimeyashika mausio yako.

101. Nimeiepusha miguu yangu na kila njia mbaya : ili nilitii neno lako.

102. Sikuijepusha na hukumu zako : kwani wewe mwenyewe umenifundisha.

103. Maneno yako ni matamu sana kwangu : kupita asali kinywani mwangu.

104. Kwa mausio yako najipatia ufahamu : kwa hiyo nachukia kila njia ya uwongo.

*Siku 26. Sala ya Asubuhi**ZABURI 119. 105-144**Nun*

105. Neno lako ni taa kwa miguu yangu : na mwanga wa njia yangu.

106. Nimeapa nami nimeithubutisha : ya kwamba nitazishika hukumu za haki yako.

107. Nimeteswa mno, ewe Yehova : unihuishe sawasawa na neno lako.

108. Sadaka za kinywa changu uziridhie, ewe Yehova : na kunifundisha hukumu zako.

109. Nafsi yangu imo mkononi mwangu daima : lakini sheria yako siisauhau.

110. Wasio haki wamenitegea mtego : lakini sikuikosa njia ya mausio yako.

111. Shuhuda zako nimezfanya kuwa urithi wa milele : kwani ndizo zilizo changamko la moyo wangu.

112. Nimeuelekeza moyo wangu nizitende amri zako : hata milele na milele.

Sameku

113. Watu wa kusita-sita nawachukia : lakini sheria yako naipenda.

114. Ndiwe starche yangu na ngao yangu : neno lako nalingojea.

115. Ondokeni kwangu, enyi watenda mabaya : niyashika maagizo ya Mungu wangu.

116. Unitegemeze sawasawa na neno lako, nikaishi : wala usiniache nikaabikie matumaini yangu.

117. Unitegemeze nami nitakuwa salama : nami nitaziangalia amri zako daima.

118. Umewakataa wote wazikosao amri zako : kwa maana hila zao ni uwongo.

119. Wabaya wa nchi wote pia umewaondoa kama takataka : kwa hiyo nazipenda shuhuda zako.

120. Mwili wangu unatetemeka kwa kukucha wewe : nami ninaziogopa hukumu zako.

Aini

121. Nimefanya hukumu na haki : usiniache mikononi mwao wanaonieea.

122. Uwe mdhamini wa mtumishi wako apate mema : wenye kiburi wasinione.

123. Macho yangu yamedhoofu kwa shauku ya wokofu wako : na neno la haki yako.

124. Umtendee mtumishi wako sawasawa na fadhil zako : na amri zako unifundishe.

125. Mimi ni mtumishi wako, unifahamishe : nizijue shuhuda zako.

126. Wakati umewadia Yehova atende : *kwa kuwa* wameitangua sheria yako.

127. Kwa hiyo nayaona maagizo yako : kuliko dhahabu, naam, *kuliko* dhahabu iliyo safi.

128. Kwa hiyo nayaona mausio yako yote kuwa ya adili : kila njia ya uwongo naichukia.

Pe

129. Shuhuda zako ni maajabu : kwa hiyo nafsi yangu huzishika.
130. Kufafanusha maneno yako hutia nuru : na kumfa-hamisha mijinga.
131. Nilifunua kinywa changu nikatweta : kwani niliyatamani maagizo yako.
132. Unigeukie, unirehemu : kama ulivyozoa kuwa-tendea walipenda o jina lako.
133. Uzielekeze hatua zangu kwa neno lako : uovu usije ukanimilki.
134. Unikomboe na dhulumu ya mwanadamu : nipate kuyashika mausio yako.
135. Umwangazie mtumishi wako uso wako : unifun-dishe amri zako.
136. Macho yangu yanachuruzika mito ya maji : kwa sababu hawaitii sheria yako.

Tsadi

137. Wewe u mwenye haki, ewe Yehova : na hukumu zako ni za adili.
138. Umeziagiza shuhuda zako kwa haki : na kwa uaminifu mwangi.
139. Juhudi yangu imeniangamiza : kwa sababu watesi wangu wameyasahau maneno yako.
140. Neno lako limesafika sana : kwa hiyo mtumishi wako amelipenda.
141. Mimi ni mdogo, nadharauliwa : lakini siyasahau mausio yako.
142. Haki yako ni haki ya milele : na sheria yako ni kweli.
143. Taabu na dhiki zimenipata : maagizo yako ni furaha yangu.
144. Haki ya shuhuda zako ni ya nilele : unifahamishe nami nitaishi.

*Siku 26. Sala ya Jioni**ZABURI 119. 145-176**Kofu*

145. Nimelingana kwa moyo wangu wote ; unijibu, ewe Yehova : nitazishika amri zako.
146. Nimekulingana, uniokoe ; nami nitazishika shu-huda zako.
147. Kutangulia mapambazuko niliomba msaada : ni-liyangojea maneno yako kwa tumaini.
148. Macho yangu yalitangulia makesha ya usiku : ili kulifikiri neno lako.
149. Uisikie sauti yangu sawasawa na fadhili zako : ewe Yehova, unihuishe sawasawa na hukumu zako.
150. Wanakaribia wafuatao uovu : wako mbali na sheria yako.
151. Wewe u karibu, ewe Yehova : na maagizo yako yote ni kweli.
152. Tokea zamani nimejua kwa shuhuda zako : ya kuwa umeziweka zikae milele.
- Reshi*
153. Uyaangalie mateso yangu, uniokoe : kwani sikuisahau sheria yako.
154. Unitetee na kunikomboa : unihuishe sawasawa na neno lako.
155. Wokofu u mbali na wasio haki : kwa maana hawa-zisomi amri zako.
156. Rehema zako ni nyingi, ewe Yehova : unihuishe sawasawa na hukumu zako.
157. Wanaonifuatia na watesi wangu ni wengi : *lakini* sikujiepusha na shuhuda zako.
158. Nimewaona watendao hila nikachukizwa : kwa sababu hawalitii neno lako.
159. Uangalie niyapendavyo mausio yako : ewe Yehova, unihuishe sawasawa na fadhili zako.
160. Jumla ya neno lako ni kweli : na kila hukumu ya haki yako ni ya milele.

Shin

161. Wakuu wameniudhi bure : lakini moyo wangu una hofu kwa sababu ya maneno yako.
162. Nalifurahia neno lako : kama apataye mateka mengi.
163. Nimechukia uwongo na kuuzira : sheria yako nimeipenda.
164. Mara saba kila siku nakusifu : kwa sababu ya hukumu za haki yako.
165. Wana amani nyangi waipendao sheria yako : wala hawana la kuwakwaza.
166. Nimeungojea wokofu wako, ewe Yehova : na maagizo yako nimeyatenda.
167. Nafsi yangu imezishika shuhuda zako : nami nzipenda mno.
168. Nimeyashika mausio yako na shuhuda zako : njia zangu zote ni mbele zako.

Tau

169. Kilio changu na kikukaribie, ewe Yehova : unifahamishe sawasawa na neno lako.
170. Sala yangu na ifike mbele zako : uniponye sawasawa na neno lako.
171. Midomo yangu na itoe sifa : kwa kuwa unanifundisha mausio yako.
172. Ulimi wangu na uliimbe neno lako : kwani maagizo yako yote ni haki.
173. Mkono wako na uwe tayari kunisaidia : kwani nimeyachagua mausio yako.
174. Nimeutamani wokofu wako, ewe Yehova : na sheria yako ndiyo furaha yangu.
175. Nafsi yangu na iishi, ipate kukusifu : na hukumu zako zinisaidie.
176. Nimetanga-tanga kama kondoo aliyepotea, umtufute mtumishi wako : kwani sikuyasahau maagizo yako.

*Siku 27. Sala ya Asubuhi**ZABURI 120*

- K**ATIKA shida yangu nilimlilia Yehova : naye akaniiitkia.
2. Ewe Yehova, uiponye nafsi yangu na midomo ya uwongo : na ulimi wenye hila.
 3. Utapewa nini, utazidishiwa nini : ewe ulimi wenye hila ?
 4. Mishare ya mtu hodari iliyotiwa ncha : pamoja na makaa ya mretemi.
 5. Ole wangu mimi, kwa kuwa nimekaa katika Mesheki : na kufanya maskani yangu kati ya mahema ya Kedaru !
 6. Nafsi yangu imekaa siku nyangi : pamoja naye aichukiaye amani.
 7. Mimi ni wa amani : bali ninenapo, wao huelekea vita.

ZABURI 121

- N**ITAINUA macho yangu niitazame milima : msaada wangu utatoka wapi ?
2. Msaada wangu u kwa Yehova : aliyezifanya mbingu na nchi.
 3. Hataacha mguu wako utikisike : wala hatalala akulindaye.
 4. Naam, ye ye aliye mlinzi wa Israeli : hatasinzia wala hatalala usingizi.
 5. Yehova ndiye mlinzi wako : Yehova ni uvuli mkono wako wa kuume.
 6. Jua halitakupiga mchana : wala mwezi wakati wa usiku.
 7. Yehova atakulinda na mabaya yote ; atakulinda nafsi yako.
 8. Yehova atakulinda utokapo na uingiapo : tangu sasa na hata milele.

ZABURI 122

- N**ILIFURAHIA waliponiambia : Na twende nyumbani kwa Yehova.
2. Miguu yetu inasimama ndani ya malango yako : ewe Yerusalem ;

3. Yerusalem uliojengwa : kama mji ulioshikamana :
4. Huko ndiko walikopanda makabila, makabila ya Yehova : usuhuhuda kwa Israeli, ili kulishukuru jina la Yehova.
5. Kwani huko viliwekwa viti vya hukumu : viti vya enzi vya nyumba ya Daudi.
6. Utakieni Yerusalem amani : watafanikiwa wakupendao.
7. Amani na ikae ndani ya kuta zako : na kufanikiwa ndani ya majumba yako.
8. Kwa ajili ya ndugu zangu na rafiki zangu : nitasema sasa, Amani ikae ndani yako.
9. Kwa ajili ya nyumba ya Yehova Mungu wetu : nitakutafutia mema.

ZABURI 123

- N**AKUINULIA macho yangu : wewe uketiye mbinguni.
2. Naam, kama vile macho ya watumishi kwa mkono wa bwana zao, kama macho ya kijakazi kwa mkono wa bibi yake : ndivyo macho yetu kwa Yehova Mungu wetu, hata atakapoturehemu.
 3. Uturuhemu, ewe Yehova, uturuhemu sisi : kwa maana tumeshiba dharau.
 4. Nafsi zetu zimeshiba mzaha wa wenyе raha : na dharau ya wenyе kiburi.

ZABURI 124

- K**AMA isingalikuwa Yehova aliyejkuwa pamoja nasi : Israeli na aseme sasa ;
2. Kama isingalikuwa Yehova aliyejkuwa pamoja nasi : wanadamu walipotushambulia :
 3. Papo hapo wangalitumeza hai : hasira yao ilipowaka juu yetu :
 4. Papo hapo maji yangalitushinda kabisa : mto ungalipita juu ya nafsi zetu :
 5. Papo hapo yangalipita juu ya nafsi zetu : maji yafurikayo.

6. Na ahimidiwe Yehova : asiyetutoa kuwa mawindo kwa meno yao.
7. Nafsi zetu zimeokoka kama ndege katika mtego wa wawindaji : mtego umevunjika nasi tumeokoka.
8. Msaada wetu u katika jina la Yehova : aliyezifanya mbingu na nchi.

ZABURI 125

- W**AMTUMAINIAO Yehova ni kama milima Zayuni ambao hautatikisika : wakaa milele.
2. Kama milima inavyouzunguka Yerusalem : ndivyo Yehova anavyowazunguka watu wake, tangu sasa na hata milele.
 3. Kwa maana fimbo ya udhalimu haitakaa juu ya fungu la wenyе haki : wenyе haki wasije wakainyosha mikono yao kwa upotofu.
 4. Ewe Yehova, uwatendee mema walio wema : nao walio wanyofu wa moyo.
 5. Bali wao wanaozigeukia njia zao zilizopotoka : Yehova atawaondoa pamoja na watenda maovu. Amani na iwe juu ya Israeli.

Siku 27. Sala ya Jioni

ZABURI 126

- Y**EHOVA alipowarejeza mateka wa Zayuni : tulikuwa kama waotao ndoto.
2. Ndipo vinywa vyetu vikajaa kicheko, na ndimi zetu nyimbo za furaha : ndipo waliposema katika mataifa, Yehova amewatendea mambo makuu.
 3. Yehova ametutendea mambo makuu : nasi tumefurahi.
 4. Ewe Yehova, unawarejeze mateka wetu : kama vijito vya Ku...ii.
 5. Wapandao kwa machozi : watavuna kwa furaha.
 6. Ingawa anakwenda zake akilia achukuapo mbegu za kupanda : hakika atarudi kwa furaha achukuapo miganda yake.

ZABURI 127

YEHOVA asipoijenga nyumba, waijengao wafanya kazi bure : Yehova asipoulinda mji, ye ye aulindaye akesa bure.

2. Kazi yenu ni bure, ninyi mnaoamka mapema na kukawia kwenda kulala, mnapokula chakula cha taabu humpa mpenzi wake usingizi.

3. Wana ndio walio urithi wa Yehova : uzao wa tumbo ni thawabu.

4. Kama mishare mkononi mwa shujaa : ndivyo walivyo wana wa ujanani.

5. Yuna heri mtu yule aliyelijaza podo lake hivyo : naam, hawataona aibu wanapokuwa wakisema na adui langoni.

ZABURI 128

YUNA heri kila mtu amchaye Yehova : aendaye katika njia zake.

2. Taabu ya mikono yako hakika utaila : utakuwa na heri na kwako kwema.

3. Mke wako atakuwa kama mzabibu uzao vyumbani mwa nyumba yako : wanao kama vichipukizi vya mizeituni wakizunguka meza yako.

4. Hivyo ndivyo atakavyobarikiwa : mtu yule amchaye Yehova.

5. Yehova akubarikie toka Zayuni : upate kuyaona mema ya Yerusalem siku zote za maisha yako.

6. Naam, ukawaone wana wa wanao : amani na iwe juu ya Israeli.

ZABURI 129

MARA nyingi wamenitesa tangu ujana wangu : Israeli na aseme sasa ;

2. Mara nyingi wamenitesa tangu ujana wangu : lakinii hawakuniweza.

3. Wakulima wamelima mgongoni mwangu : wamefanya mirefu mifuo yao.

4. Yehova ndiye mwenye haki : amezikata kamba zao wasio haki.

5. Na waaibishwe, warudishwe nyuma : wote wanacikua Zayuni.

6. Na wawe kama majani ya darini : yanyaukayo kabla hayajamea :

7. Ambayo mvunaji haujazi mkono wake : wala mfunga miganda kifua chake.

8. Wala hawasemi wapitao, Amani ya Yehova ikae nanyi : twababarikia kwa jina la Yehova.

ZABURI 130

TOKA vilindini nimekulilia : ewe Yehova.

2. Ewe Bwana, uisikilize sauti yangu : masikio yako na yaiangalie sauti ya sala zangu.

3. Kama ungehesabu maovu, ewe Yehova : ewe Bwana, ni nani atakayesimama ?

4. Lakini kwako kuna msamaha : ili uogopwe.

5. Namngojea Yehova, nafsi yangu inangoja : na neno lake nimelitumainia.

6. Nafsi yangu *inamongojea* Bwana zaidi ya *waingojeao* asubuhi : naam, *waingojeao* asubuhi.

7. Ewe Israeli, umtumaini Yehova : kwani kwa Yehova kuna rehemba, tena kwake kuna kukomboa kwingi.

8. Nayé atamkomboa Israeli : katika maovu yake yote.

ZABURI 131

EWE Yehova, moyo wangu hauna kiburi wala macho yangu háyainuki : wala sijishughulishi na mambo makuu, wala na mambo yashindayo nguvu zangu.

2. Hakika nimeituliza nafsi yangu na kuinyamazisha kama mtoto aliyeachishwa kifuanii mwa mama yake : kama mtoto aliyeachishwa ndivyo nafsi yangu ilivyo kwangu.

3. Ewe Israeli, umtumainie Yehova : tangu leo na hata milele.

Siku 28. Sala ya Asubuhi

ZABURI 132

EWE Yehova, umkumbukie Daudi : taabu zake zote alizotaabika ;

2. Aliviyomwapia Yehova : na kuweka nadhiri kwa Shujaa wa Yakobo :

3. Hakika yangu sitaingia hemani mwa nyumba yangu : wala kulala kitandani mwangu ;
4. Sitaacha macho yangu kuwa na usingizi : wala kope zangu kusinzia ;
5. Hata nitakapompatia Yehova pahali : na Shujaa wa Yakobo maskani.
6. Tazama, tulisikia habari zake katika Efirata : katika konde la msitu tuliiiona.
7. Tutaingia maskani yake : tutasujudu penye kiti cha kuwekea miguu yake.
8. Uondoke, ewe Yehova, uende kwenye raha yako : wewe na sanduku la nguvu zako.
9. Makuhani wako na wavikwe haki : watakatifu wako na washangirie.
10. Kwa ajili ya Daudi mtumishi wako : usiurudisha nyuma uso wa Masihi wako.
11. Yehova amemwapia Daudi katika kweli ; hatarudi nyuma akaihalifu : Katika uzao wa mwili wako nita-kuwekea juu ya kiti chako cha enzi.
12. Wana wako wakiyashika maagano yangu na shuhuda nitakazowafundisha : wana wao nao wataketi katika kiti chako cha enzi milele.
13. Kwani Yehova ameichagua Zayuni : ameitamani akae ndani yake.
14. Hapa ndipo pahali pangu pa raha milele : hapa nitakaa, kwa maana nimepatamani.
15. Riziki yake nitaibarikia sana : wahitaji wake nitawashibisha kwa mkate.
16. Na makuhani wake nitawavika wokofu : na watakatifu wake watashangiria.
17. Hapa nitamchipushia Daudi pembe : na taa nime-ntengenezea Masihi wangu.
18. Adui zake nitawavika aibu : bali juu yake taji yake itasitawi.

ZABURI 133

JINSI lilivyo jambo jema, tena la kupendenza : ndugu wakikaa pamoja, kwa umoja halisi !

2. Ni kama mafuta mazuri kichwani yashukayo

- ndevuni, ndevu za Haruni : yashukayo mpaka upindo wa mayazi yake ;
3. Kama umande wa Herimoni, ushukao milimani pa Zayuni : kwani ndiko Yehova alikoamuru baraka, naam, uzima hata milele.

ZABURI 134

- M**HIMIDINI Yehova, enyi watumishi wa Yehova wote pia : ninyi mnaosimama usiku katika nyumba ya Yehova.
2. Painulieni pahali patakatifu mikono yenu : kamhimi-dini Yehova.
 3. Yehova akubarikie toka Zayuni : aliyezifanya mbingu na nchi.

ZABURI 135

- A**LELUYA ! Lisifuni jina la Yehova : sifuni, enyi watumishi wa Yehova.
2. Ninyi msimamao nyumbani mwa Yehova : nyuani mwa nyumba ya Mungu wetu.
 3. Msifuni Yehova kwa kuwa Yehova ni mwema : liimbeni jina lake kwa maana lapendeza.
 4. Kwa sababu Yehova amejichagulia Yakobo : na Israeli, wawe watu wake hasa.
 5. Kwani najua mimi ya kuwa Yehova ni mkuu : na Yehova wetu ni juu ya miungu yote.
 6. Yehova amefanya kila lilitompendeza : katika mbingu na katika nchi, katika bahari na vilindi vyote.
 7. Huipandisha mivuke toka miisho ya nchi : huifanyia mvua umeme, hutoa upepo katika hazina zake.
 8. Aliyewapiga wazaliwa wa kwanza wa Misiri : wa wanadamu na wa nyama.
 9. Alipeleka ishara na maajabu kati yako, ewe Misiri : juu ya Farauni na watumishi wake wote.
 10. Aliyewapiga mataifa mengi : na kuwaua wafalme wenye nguvu ;
 11. Sihoni, mfalme wa Waamori, na Ogu, mfalme wa Bashani : na falme zote za Kanaani ;

12. Akatoa nchi yao iwe urithi : urithi wa Isiraeli watu wake.

13. Jina lako, ewe Yehova, ni la milele : kumbukumbu lako, ewe Yehova, *laendelea* vizazi hata vizazi.

14. Kwa kuwa Yehova atawaamua watu wake : atawa-hurumia watumishi wake.

15. Sanamu za mataifa ni fedha na dhahabu : kazi ya mikono ya wanadamu :

16. Zina vinywa lakini hazisemi : zina macho lakini hazioni :

17. Zina masikio lakini hazisikii : wala hamna pumzi vinywani mwake.

18. Wazifanyao watafanana nazo : naam, na kila mmoja anayezitumainia.

19. Ewe nyumba ya Isiraeli, mhimidini Yehova : ewe nyumba ya Haruni, mhimidini Yehova :

20. Ewe nyumba ya Lawi, mhimidini Yehova : ninyi mnaomcha Yehova, mhimidini Yehova.

21. Na ahimidiwe Yehova toka Zayuni : akaaye Yerusalem. Aleluya.

Siku 28. Sala ya Jioni

ZABURI 136

MSHUKURUNI Yehova kwa kuwa ni mwema : kwa maana fadhili zake ni za milele.

2. Mshukuruni Mungu wa miungu : kwa maana fadhili zake ni za milele.

3. Mshukuruni Bwana wa mabwana : kwa maana fadhili zake ni za milele.

4. Yeye ambaye ndiye pekee afanyaye maajabu makuu : kwa maana fadhili zake ni za milele.

5. Yeye ambaye alifanya mbingu kwa fahamu zake : kwa maana fadhili zake ni za milele.

6. Yeye ambaye alitandaza nchi juu ya maji : kwa maana fadhili zake ni za milele.

7. Yeye ambaye alifanya mianga mikubwa : kwa maana fadhili zake ni za milele.

8. Jua litawale mchana : kwa maana fadhili zake ni za milele :

9. Mwezi na nyota zitawale usiku : kwa maana fadhili zake ni za milele.

10. Yeye ambaye aliwapiga Wamisiri kwa kuwaua wazaliwa wa kwanza wao : kwa maana fadhili zake ni za milele :

11. Akawatoa Waisiraeli watoke katikati yao : kwa maana fadhili zake ni za milele :

12. Kwa mkono hodari na mkono ulionyoshwa : kwa maana fadhili zake ni za milele.

13. Yeye ambaye aliigawa Bahari Nyekundu : kwa maana fadhili zake ni za milele :

14. Akawavusha Isiraeli katikati yake : kwa maana fadhili zake ni za milele :

15. Akamwangusha Farauni na jeshi lake katika Bahari Nyekundu : kwa maana fadhili zake ni za milele.

16. Yeye ambaye aliwaongoza watu wake jangwani : kwa maana fadhili zake ni za milele.

17. Yeye ambaye aliwapiga wafalme wakuu : kwa maana fadhili zake ni za milele :

18. Akawaua wafalme mashuhuri : kwa maana fadhili zake ni za milele :

19. Sihoni, mfalme wa Waamori : kwa maana fadhili zake ni za milele :

20. Na Ogu, mfalme wa Bashani : kwa maana fadhili zake ni za milele :

21. Akaitoa nchi yao iwe urithi : kwa maana fadhili zake ni za milele :

22. Urithi wa Isiraeli watumishi wake : kwa maana fadhili zake ni za milele.

23. Ambaye alitukumbuka katika unyonge wetu : kwa maana fadhili zake ni za milele :

24. Naye ametuokoa na adui zetu : kwa maana fadhili zake ni za milele.

25. Kila mwene mwili humpa chakula chake : kwa maana fadhili zake ni za milele.

26. Mshukuruni Mungu wa mbingu : kwa maana fadhili zake ni za milele.

ZABURI 137

KANDO ya mito ya Babuloni, ndiko tulikoketi : naam, tukalia tulipoikumbuka Zayuni.
2. Katika miti iliyo katikati yake : tulivitundika vinubi yetu.

3. Kwani huko waliotuchukua mateka wālitaka tuwai-mbie : na walioituonea *walitaka furaha* ; Tuimbieni baadhi ya nyimbo za Zayuni.

4. Tuimbeje wimbo wa Yehova : katika nchi ya ugeni ?

5. Kama nikikusahau, ewe Yerusalem : mkono wangu wa kuume na usahau.

6. Ulimi wangu na ugandamane na kaakaa la kinywa changu, nisipokukumbuka : nisipoikuza Yerusalem zaidi ya furaha yangu iliyo kuu.

7. Ukumbuke, ewe Yehova, juu ya wana wa Edomu hiyo siku ya Yerusalem : waliosema, Bomoeni, bomoeni hata misingini.

8. Ewe binti Babuloni uliye tayari kuangamia : yuna heri atakayekupatiliza uliviyotupatiliza sisi.

9. Yuna heri atakayewakamata watoto wako walio wachanga : na kuwaseta juu ya mwamba.

ZABURI 138

NITAKUSHUKURU kwa moyo wangu wote : mbele ya miungu nitakuimbia sifa.

2. Nitasujudu nikikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako : kwa maana umelikuza jina lako juu ya yote.

3. Siku ile niliyokulingana ulinjibu : ukafariji nafsi kwa kunitia nguvu.

4. Wafalme wote wa dunia watakushukuru, ewe Yehova : watakaposikia maneno ya kinywa chako.

5. Naam, wataziimba njia za Yehova : kwa maana utukufu wa Yehova ni mkuu.

6. Kwani ingawa Yehova yuko juu amwona mnnyekevu : naye amjua mwenye kujivuna tokea mbali.

7. Nijapokwenda kati ya shida utanihuisha : utanyosha

mkono wako juu ya ghadhabu ya adui zangu, na mkono wako wa kuume utaniokoa.

8. Yehova atanitimilizia mambo yangu : fadhili zako, ewe Yehova, ni za milele ; usiziache kazi za mikono yako.

Siku 29. *Sala ya Asubuhi*¹

ZABURI 139

EWE Yehova : umenipeleleza na kunijua.
E 2. Wewe wajua kuketi kwangu, *wajua* na kuondoka kwangu : wafahamu wazo langu tokea mbali.

3. Waangalia mwenendo wangu na kulala *kwangu* : umeelewa na njia zangu zote.

4. Kwani hamna neno ulimini mwangu : usilolijua kabisa, ewe Yehova.

5. Umenizunguka nyuma na mbele : na kunishika kwa mkono wako.

6. Maarifa haya ni ya ajabu, yanishinda mimi : haya-dirikiki, siwezi kuyafikia.

7. Niende wapi nijiepushe na roho yako : niende wapi niukimbie uso wako ?

8. Nijapopanda mbinguni, wewe uko : nijapofanya kuzimu kitanda changu, wewe uko.

9. Nijapoziitwaa mbawa za asubuhi : na kukaa pande za mwisho za bahari ;

10. Huko nako mkono wako utaniongoza : na mkono wako wa kuume utanishika.

11. Kama nikisema, Hakika giza litanificha : na nuru inizungukayo ikawa usiku ;

12. Giza nalo halikufichi kitu, bali usiku huangaza kama michana : giza na mwanga kwako ni sawasawa.

13. Kwani wewe umemilki mtima wangu : umeniunga tumboni mwa mama yangu.

14. Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu na kutisha : matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana.

15. Mifupa yangu haikufichwa kwako nilipoumbwa kwa siri : nilipoungwa kwa ustadi pande za chini za nchi.

16. Macho yako yaliniona kabla sijakamilika : chuoni mwako viliandikwa vyote pia *viunga vyangu*, ambavyo siku baada ya siku vilumbwa kabla havijawa bado.

17. Kwangu mimi fikara zako zina thamani nyingi, ewe Mungu : wingi wa jumla yake jinsi ulivyo na ajabu !

18. Kama ningezihesabu ni nyingi kuliko mchanga : niamkapo nikali pamoja nawe.

19. Hapana budi utawaua waovu, ewe Mungu : basi ondokeni kwangu, enyi watu wa damu.

20. Kwa maana wakunena kwa ubaya : adui zako wakutaja jina lako kwa upuzi.

21. Je, siwachukii, ewe Yehova, wanaokuchukia : je, sikirihiki nao wakuasio ?

22. Nawachukia kwa ukomo wa chuki : nawahesabu kuwa ni adui kwangu.

23. Unipeleleze, ewe Mungu, ujue moyo wangu : unijaribu, ujue mawazo yangu :

24. Ukaone kama iko njia ya uovu ndani yangu : ukaniongoze katika njia ya milele.

ZABURI 140

UNIOKOE, ewe Yehova, na mtu mbaya : unihifadhi na mtu wa jeuri :

2. Waliowaza mabaya miyoni mwao : kila siku huondokesha vita.

3. Wamenoa ndimi zao kama nyoka : sumu ya fira i chini ya midomo yao.

4. Unilinde, ewe Yehova, na mikono ya mtu asiye haki : unihifadhi na mtu wa jeuri, waliowaza kupotosha hatua zangu.

5. Wenye kiburi wameficha mitego na kamba waninase : wametandika wavu kando ya njia, wameniwekea matanzi.

6. Nilimwambia Yehova, Ndiye Mungu wangu : ewe Yehova, usikie sauti ya sala zangu.

7. Ewe Yehova Bwana, nguvu za wokofu wangu : umefunka kichwa changu siku ya vita.

8. Ewe Yehova, usimpe asiye haki tamaa zake : usiifanikishe hila yake, wasije wakajiinua.

9. Tena, hao watu wanaonizunguka wainuapo vichwa vyao : madhara ya midomo yao yawafunike.

10. Makaa ya moto yawaangukie : watupwe motoni, na katika mashimo wasipate kusimama tena.

11. Msingiziaji hatawekwa imara katika nchi : mtu wa jeuri mabaya yatamwinda hata kumwangamiza.

12. Najua ya kuwa Yehova atamfanyia hukumu aliyeonewa : na wahitaji *atawafanya* haki yao.

13. Hakika wenye haki watalishukuru jina lako : wenye adili watakaa pahali ulipo wewe.

ZABURI 141

E WE Yehova, nimekulingana, unijie hima : usikie sauti yangu nikulinganapo.

2. Sala yangu ipae mbele zako kama uvumba : na kuinuka kwa mikono yangu kama dhabihu ya jioni.

3. Uweke ulinzi, ewe Yehova, kinywani pangu : uulinde mang'o wa midomo yangu.

4. Usielekeze moyo wangu kunako jambo bayo, nisizoelee matendo yasiyofaa pamoja na watu watendao maovu : wala nisile vyakula vyao vya anasa.

5. Mwenye haki na anipige, *itakuwa* fadhili ; anikemee, *itakuwa* kama mafuta kichwani ; kichwa changu kisikatae : kwani siachi kusali hata kati ya mabaya yao.

6. Makadhi wao huangushwa kando ya genge : watasikia maneno yangu, kwani ni matamu.

7. Kama mtu alimapo na kuchimbua-chimbua udongo : ndivyo ilivyo mifupa yetu kwenye mdomo wa kuzimu.

8. Kwani macho yangu yanakuelekea wewe, ewe Yehova Bwana : nimekukimbilia wewe, usiniache nafsi yangu.

9. Unilinde na mitego walionitegea : na matanzi yao watendao maovu.

10. Wasio haki na waanguke katika nyavu zao wenywewe : pindi ninapokuwa nimeokoka salama.

Siku 29. Sala ya Jioni

ZABURI 142

KWA sauti yangu namlilia Yehova : kwa sauti yangu namwomba sala kwa Yehova.

2. Nafunua mbele zake malalamiko yangu : shida yangu naitangaza mbele zake.

3. Roho yangu ilipozimia ndani yangu ulijua mapito yangu : katika njia niendayo wamenifichia mtego.

4. Utazame mkono wa kuume ukaone, kwa maana sina mtu anijuaye : makimbilio yamenipotea, hakuna wa kuitunza nafsi yangu.

5. Nilikulingana, ewe Yehova : nilisema, Ndiwe kimbilio langu, fungu langu katika nchi ya walio hai.

6. Ukitikilize kilio changu kwa maana nimedhilika sana : uniponye nao wanaonifuatia, kwa maana ni hodari kuliko mimi.

7. Utoe nafsi yangu kifungoni nipate kulishukuru jina lako : wenye haki watanizunguka kwa kuwa wewe utanikirumu.

ZABURI 143

EWE Yehova, usikie sala yangu, usikilize maombi yangu : kwa uaminifu wako unijibu, kwa haki yako.

2. Wala usimhukumu mtumishi wako : kwani mbele zako hakuna aliye hai atakayehesabiwa kuwa ni mwénye haki.

3. Kwani adui amefiuatia nafsi yangu, ameutupa chini uzima wangu : amenikalisha mwahali mwenye giza kama watu waliokufa zamani.

4. Kwa hiyo roho yangu imezimia ndani yangu : moyo wangu ndani yangu umeshtuka.

5. Nazikumbuka siku za kale, nayafikiri matendo yako yote : naziwaza kazi za mikono yako.

6. Nakunyoshea mikono yangu : roho yangu yakutamani kama nchi iliyo kavu.

7. Unijibu hima, ewe Yehova, roho yangu imelegea : usinifice uso wako, nisifanane nao washukao shimoni.

8. Unisikize fadhili zako asubuhi kwa maana nakutumaini wewe : unijulishe njia nitakayoiendea, kwa maana nakuinulia nafsi yangu.

9. Uniponye, ewe Yehova, na adui zangu : nakukimbilia wewe, unifiche.

10. Unifundishe kuyatenda mapenzi yako kwa maana ndiye Mungu wangu : Roho wako ni mwema, unionongoze katika nchi ya haki.

11. Kwa ajili ya jina lako, ewe Yehova, unihuishe : kwa haki yako unitoe nafsi yangu taabuni.

12. Kwa fadhili zako uwakatilie mbali adui zangu, na kuwaangamiza wote wanitesao : kwa maana mimi ni mtumishi wako.

Siku 30. Sala ya Asubuhi

ZABURI 144

NA ahimidiwe Yehova, mwamba wangu : anifundi-shaye mikono yangu vita, vidole vyangu kupigana :

2. Fadhili zangu na boma langu, ngome yangu na mwokozi wangu : ngao yangu, naye ndiye niliyemkimbilia, naye ndiye awatiishaye watu wangu chini yangu.

3. Ewe Yehova, mtu ni nani hata umjue ? Na bina-damu, hata umwangalie ?

4. Binadamu amefanana na ubatili : siku zake ni kama kivuli kipitacho.

5. Ewe Yehova, uziinamishe mbingu zako, ushuke : wiguse milima nayo itatoka moshi.

6. Utupe umeme, uwatawanye : uipige mishare yako, uwafadhaishé.

7. Unyoshe mikono yako toka juu : uniponye, unitoe katika maji mengi, katika mkono wa wageni ;

8. Ambao vinywa vyao vyasema visivyoofaa : na mkono wao wa kuume ni mkono wa uwongo.

9. Nitakuimbia wimbo mpya, ewe Mungu : kwa kinanda chenyé nyuzi kumi nitakuimbia.

10. Ndiye awapaye wafalme wokofu : amwokoaye Daudi mtumishi wake na upanga wa uovu.

11. Uniponye, unitoe katika mkono wa wageni : ambao vinywa vyao vyasema visivyoofaa, na mkono wao wa kuumi ni mkono wa uwongo.

12. Wana wetu watakapokuwa kama miche waliojukua ujanani : binti zetu nao kama nguzo za pembeni zili-zonakishiwa kwa kupamba hekalu ;

13. Ghala zetu zitakapojaa, zenyne akiba za jinsi zote : kondoo zetu zitakapozaa elfu na elfu kumi mashambani mwetu ;

14. Ng'ombe zetu zitakapochukua mizigo : kusipokuwa na kushambuliwa wala kuhamishwa, wala malalamiko katika njia zetu ;

15. Wana heri watu wenye hali hiyo : wana heri watu ambao Yehova ni Mungu wao.

ZABURI 145

NITAKUTUKUZA, Mungu wangu, ewe Mfalme : nitalihimidi jina lako milele na milele.

2. Kila siku nitakuhimidi : nitalisifu jina lako milele na milele.

3. Yehova ndiye mkuu, mwenye kusifiwa sana : na ukuu wake hautambulikani.

4. Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yako : na kuyatangaza matendo ya uwezo wako.

5. Nitaifiki fahari ya utukufu wa adhama yako : na matendo yako yote ya ajabu.

6. Wataitaja nguvu ya matendo yako ya kutisha : nami nitausimulia ukuu wako.

7. Watahubiri kumbukumbu la wema wako mkuu : watauiimba haki yako.

8. Yehova ana fadhili, ni mwangi wa huruma : si mwepesi wa hasira, ni mwangi wa fadhili.

9. Yehova ni mwema kwa watu wote : na rehema zake ni juu ya kazi zake zote.

10. Kazi zako zote zitakushukuru, ewe Yehova : na watakatifu wako watakuhimidi.

11. Wataunena utukufu wa usalme wako : na kuuhadithia uwezo wako ;

12. Ili kuwajulisha wanadamu matendo ya uwezo wake : na utukufu wa fahari ya usalme wake.

13. Ufalme wako ni usalme wa zamani zote : na mamlaka yako ni ya vizazi vyote.

14. Yehova huwategemeza wote waangukao : huwainua wote walioinama chini.

15. Macho ya watu wote yakuelekea wewe : nawe kuwapa chakula chao wakati wake.

16. Waufumbua mkono wako : washibisha maridhawa kila kilicho hai.

17. Yehova ni mwenye haki katika njia zake zote : na mwenye fadhili katika kazi zake zote.

18. Yehova ni karibu na wote wamlinganao : wote wamlinganao kwa uaminifu.

19. Atawafanya wamchao yale watakayo : naye atasikia kilio chao na kuwaokoa.

20. Yehova huwahifadhi wote wampendao : na wote wasio haki atawaangamiza.

21. Kinywa changu kitazinena sifa za Yehova : wote wenye mwili na walihimidi jina lake takatifu milele na milele.

ZABURI 146

ALELUYA ! Ewe nafsi yangu, umsifu Yehova.

2. Nitamsifu Yehova muda ninaoishi : nitamwambia Mungu wangu kwa kumsifu muda wa uhai wangu.

3. Msiyatumanie wakuu : wala binadamu ambaye hakuna wokofu kwake.

4. Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake : siku hiyo mawazo yake yapotea.

5. Yuna heri mwenye Mungu wa Yakobo kuwa msaada wake : ambaye tumaini lake ni kwa Yehova Mungu wake :

6. Aliyezifanya mbingu na nchi, bahari na vitu vyote iliyovomo : aishikaye kweli milele :

7. Awafanyiaye hukumu walioonewa, awapaye wenye jaa chakula : Yehova hufungua waliofungwa ;

8. Yehova huwafumbua macho waliofopuka : Yehova huwainua walioinama : Yehova huwapenda wenye haki ;

9. Yehova huwahifadhi wageni, huwategemeza yatima na mjane : bali njia ya wasio haki luipindua.
10. Yehova atatawala milele : Mungu wako, ewe Zayuni, kizazi hata kizazi. Aleluya.

Siku 30. Sala ya Jioni

A LELUYA ! Kwani ni vyema kumwimbia sifa Mungu wetu : kwani kwapendeza, kusifu ni kuzuri.

2. Yehova ndiye ajengaye Yerusalem : huwakusanya waliotawanyika wa Israeli.

3. Huwaponya waliopondeka miyo : na kuyafunga majeraha yao.

4. Huihesabu idadi ya nyota : huzipa zote majina.

5. Bwana wetu ni mkuu na mwingu wa nguvu : akili zake hazina idadi.

6. Yehova huwategemeza wenye upole : huwaangusha chini wasio haki.

7. Mwimbieni Yehova kwa kushukuru : mwimbieni Mungu wetu kwa kinubi :

8. Azifunikaye mbingu kwa mawingu, aitengenezeaye nchi mvua : ayameeshaye majani milimani.

9. Humpa nyama chakula chake : wana kunguru waliao.

10. Hapendezwi na nguvu za farasi : wala hairidhii miguu ya mtu.

11. Yehova huwaridhia wamchao : wazingojeao fadhili zake.

12. Msifuni Yehova, ewe Yerusalem : msifuni Mungu wako, ewe Zayuni!

13. Kwani ameyakaza mapingo ya malango yako : amewabarikia wanao ndani yako.

14. Hufanya amani mipakani mwako : hukushibisha kwa unono wa nganu.

15. Huipeleka amri yake juu ya nchi : neno lake lapiga mbio sana.

16. Hutoa theluji kama sufu : humuwaga kama majivu umande ulioganda.

17. Hutupa mvua ya mawe kama makombo : mbele ya baridi yake ni nani awezaye kusimama ?

18. Hulituma neno lake akavyeyusha : huuvumisha upopo wake, maji yakatiririka.

19. Humhubiri Yakobo neno lake : Israeli amri zake na hukumu zake.

20. Hakulitenda taifa lolote mambo kama hayo : na hukumu zake hawakuzijua. Aleluya.

A LELUYA ! Msifuni Yehova kutoka mbinguni : msifuni katika mwahali mlipo juu.

2. Msifuni, enyi malaika zake wote : msifuni, jeshi lake lote.

3. Msifuni, juu na mwezi : msifuni, nyota zote zenye mwanga.

4. Msifuni, enyi mbingu za mbingu : nanyi maji mlioko juu ya mbingu.

5. Na vilisifu jina la Yehova : kwa maana aliamuru vikaumbwa.

6. Naye amevithubutisha hata milele na milele : amevipa amri wala haitakoma.

7. Msifuni Yehova kutoka nchi : enyi nyangumi na vilindi vyote :

8. Moto na mvua ya mawe, theluji na mvuke : upopo wa dharuba ultendalo neno lake :

9. Milima na vilima vyote : miti yenye matunda na mieriizi yote :

10. Nyama za mwitu na nyama wafugwao : wata-mbabao na ndege zenye mbawa :

11. Wafalme wa dunia na watu wote : wakuu na makadhi wote wa dunia :

12. Vijana waume na wanawali : wazee na watoto :

13. Na walisisfu jina la Yehova, maana jina lake peke yake limetukuka : adhama yake i juu ya nchi na mbingu.

14. Naye amewainulia watu wake pembe : sifa za watakatifu wake wote, wana wa Israeli, watu walio karibu naye. Aleluya.

ZABURI 149

ALELUYA. Mwimbieni Yehova wimbo mpya : sifa zake katika kusanyiko la watakatifu.

2. Israeli na amfurahie ye ye aliye msanya : wana wa Zayuni wamshangirie Mfalme wao.

3. Na walisi jina lake kwa kucheza : kwa ngoma na kinubi wamwimbie na kumsifu.

4. Kwa kuwa Yehova awaridhia watu wake : huwapamba wenye upole kwa wokofu.

5. Watakatifu waushangirie utukufu : waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao.

6. Sifa kuu za Mungu ziwe vinywani mwao : na upanga wenye mkali kuwili mikononi mwao ;

7. Ili kufanya kisasi juu ya mataifa : na adhabu juu ya makabila ya' watu ;

8. Kuwfunga wafalme wao kwa minyororo : na wakuu wao kwa mapingu ya chuma ;

9. Kuwfanya hukumu ilioandikwa : hii ndiyo heshima ya watakatifu wake wote. Aleluya.

ZABURI 150

ALELUYA ! Msifuni Mungu katika pahali patakatifu apake : msifuni katika nafasi ya uwezo wake.

2. Msifuni kwa matendo yake makuu : msifuni kwa kadiri ya wingi wa ukuu wake.

3. Msifuni kwa mvumo wa baragumu : msifuni kwa kinanda na kinubi.

4. Msifuni kwa ngoma na kucheza : msifuni kwa zeze na filimbi.

5. Msifuni kwa matoazi : msifuni kwa matoazi yavumayo sana.

6. Kila mwenye pumzi na amsifu Yehova. Aleluya.

TARATIBU NA JINSI YA KUFANYA, NA KUAMURU, NA KUWEKWA WAWE

MABISHOPU, NA MAKASISI, NA MASHEMASI,
KATIKA KANISA LA UINGEREZA

Dibaji

*N*l dhakir i kwa watu wote wayasomao sana Maandiko matakati fu na vyuo vya watu wa kale, ya kwamba tangu zamani za mitume yamo madaraja haya ya watumikao katika kanisa la Kristo ; nayo ni ya mabishopu, na makasisi, na mashemasi. Na kazi zao ziliheshimiwa na kusifiwa siku zote, hata mtu asisubutu kulitenda mojawapo katika hayo ila aliyeitwa kwanza, na kujaribiwa, na kuulizwa, na kujulikana kuwa ni mtu mwenye hali zile zipasazo kazi hiso ; tena akakubaliwa na kupewa amri kwa njia ya sala ya kuwekwa na walio na amri. Kwa ajili ya hayo, ili kwamba madaraja hayo yadumu, na kuheshimiwa, na kusifiwa katika Kanisa la Uingereza, mtu na asihesabiwe wala kukubaliwa kuwa ni bishopu, wala kasisi, wala shemasi, wa kweli, katika kanisa la Uingereza, wala asikubaliwe kutenda hiso kazi zilizotajwa mojawapo, isipokuwa ameitwa, na kujaribiwa, na kuulizwa, na kupewa amri ya kuzitenda, kwa taratibu ifuatanyo hapa, au ni mtu ambaye aliwekwa na bishopu tangu hapo kwa kazi hiso, au kuamriwa.

Tena mtu asikubaliwe kuwa shemasi, asiye pata umri wa miaka ishirini na mitatu, asipokuwa na hati-ya-ruhusa. Na kila mtu atakayekubaliwa kuwa kasisi awe ametimiza unri wa miaka ishirini na minne. Na kila mtu atakaye am iwa au kuwekwa kuwa bishopu awe na umri wa miaka thelathini asipungue.

Na bishopu, ali hali mwenyewe ajua, au awe amepata ushuhuda utoshao, ya kuwa fulani ni mtu wa mwendo mwema, asiye kuwa mwovu ; tena akiisha kuulizwa na

kujaribiwa, akimwona amefunzwa Maandiko matakatifu kwa kutosha, amkubali kuwa shemasi kwa nyakati zilizogizwa katika kanuni, au pakiwa na sababu kubwa, na afanye katika Jumapili au Siku kuu nyingine, mbele ya kanisa, kwa jinsi na taratibu ifuatanayo hapa.

TARATIBU NA JINSI YA KUFANYA MASHEMASI

IIkifikilia ile siku iliyoagizwa na bishopu, baada ya Sala ya Asubuhi, huwa kuhutubu au kuonya, kwa kuyaweka wazi mambo yawapasayo na kazi zao hao wajao kukubaliwa kuwa mashemasi; jinsi daraja hilo likitajiwayo katika kanisa la Kristo, tena jinsi iwapasavyo watu kuwaheshimu watumikao katika hiyo kazi yao.

IKwanza huyu Archdeacon, au badili yake, humletea bishopu (hali ameketi kitini mwake karibu ya Meza takatifu) wale watakao kufanywa mashemasi (kila mtu axe amevaa vao limpasalo), na kumena maneno haya,

BABA mwenye kuheshimiwa kwa mambo ya Mungu, nimekuletea watu hawa walipo hapa wakubaliwe kuwa mashemasi.

Bishopu

ANGALIA sana watu utuleteao wawe wafao na Akustahili kwa elimu yao na kwa miendo myema, kuutenda utumishi wao kama ipasavyo, kwa heshima ya Mwenyezi Mungu, na kwa kumjengea kanisa lake.

Archdeacon

NIMEWATAFITI, na kuwaaliza, nami nimewaona ndivyo walivyo.

I Ndipo Bishopu huwaambia watu walipo :

NDUGU zangu, akiwa mmojawapo miongoni mwenu mwenye kujua kizuizi chochote, au uovu ulio dhahiri, katika watu hawa mmojawapo walioletwa hapa wapewe daraja la ushemasi, ambao humzuilia asitiwe katika daraja lile, na aje sasa kwa jina la Mungu, aonyeshe uovu huo au kizuizi hicho.

¶ Na kama uovu mkubwa ulio wote au kizuizi chatajwa, Bishopu huacha kumwamuru mtu yule, hata wakati atakapoonekana kuwa uovu huo hakutenda huyo aliyeshktawi.

Ndipo Bishopu aseme,

NATAKA ninyi mnaokutanika hapa mwaombee watu hawa ambao wameonekana kuwa wamestahili kuamriwa wawe mashemasi.

¶ Kisha Bishopu, pamoja na mapadre na watu waliopo, aimbe au kusoma Litania, kama ilivyoamriwa, katika ukurasa wa 33, isipokuwa sala ya mtakatifu Chrysostom na baraka ya mwisho ziachwe zisismwe.

¶ Kisha baada ya Litania huimbwa au husomwa taratibu ya Ushirika Mtakatifu, pamoja na Sala hii, na Waraka huu, na Injili hii ;

SALA

EWE Mwenyezi Mungu, weve kwa uangalizi wako wa Uungu, umeamuru madaraja mbali-mbali ya watumikao katika kanisa lako, tena ukawavuvilia mawazo mitume wako wamchague na kumtia katika daraja la ushemasi huyo shahidi wa kwanza Stefano mtakatifu, pamoja na wengine ; uwaangalie kwa rehema hawa watumwa wako ambao sasa wanaitwa na kutiwa katika kazi hiyo na utumishi ; uwajaze ile kweli ya elimu yako, na kuwapamba kwa maisha mema, ili kwamba wao kwa maneno yao na kielelezo chao chema wakutumikie kwa uaminifu katika kazi hiyo, ili jina lako litukuzwe, na kanisa lako lijengwe ; kwa kustahili kwake Yesu Kristo Mwokozi wetu, aishiye na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. *Amina.*

WARAKA. 1 Timotheo 3. 8-13

NI vivyo hivyo na watumishi wa kanisa na wawe wenyе utulivu, si wenyе ndimi mbili, si wenyе kutumia divai nydingi, si wenyе kutamani mapato ya uovu, wawe wenyе kuishika hiyo siri ya ile imani katika nia iliyotakata. Tena hao nao wajarikiye kwanza ; baadaye watumike wakiwa hawana matayo. Wanawake ni vivyo

na wawe wenyе utulivu, wasiwe wenyе kusingizia, ila na wawe wenyе kudhibiti nafsi, waaminifu katika mambo yote. Watumishi wa kanisa na wawe kila mtu mume wa mke mmoja, wenyе kuwasimamia watoto na nyumba zao wenyewe kwa wema. Kwani hao waliokuwa wametumika vyema wajipatia daraja zuri, na uthubutifu mwingu katika imani iliyo katika Kristo Yesu.

¶ Au maneno haya, katika mlango wa sita wa Vitendo vya Mitume ;

Vitendo vya Mitume 6. 2-7

WALE kumi na wawili wakaiita jamii ya wanafunzi waje kwao, wakiwaambia, Hailekei kuliacha neno la Mungu sisi na kuyatumikia mambo ya meza. Basi, ndugu zetu, angalieni watu saba kwenu walioshuhudiwa kuwa wema, wenyе kujawa na Roho na hekima, tupate kuwaweka kwa shughuli hii. Sisi tutadumu katika kuomba Mungu na katika matumishi ya lile Neno. Neno hilo likapendeza kwa jamii nzima : wakamchagua Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipi, na Porokoro, na Nikanora, na Timona, na Paramena, na Nikola aliyekuwa mwongofu atokaye *mji wa Antiochia* : wakawaweka hao mbele ya mitume, na wakiisha kuomba Mungu, wakawaweka mikono yao juu yao. Na neno la Mungu likakua ; na hesabu ya wanafunzi ikaongea sana ndani ya Yerusalem ; mikutano mkubwa wa makuhani wakaifuata ile imani.

¶ Na mbele ya kusoma Injili, Bishopu, hali ameketi kitini mwake humuuliza kila mmoja wao watahaoamriwa, mbele ya watu waliopo, kwa jinsi hii ifuatanyo.

JE, ninyi mwaamini ya kwamba mwaongozwa mioyoni na Roho Mtakatifu, kujitweka daraja hili na utumishi, kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa kuutukuza utukufu wake, na kuwathubutisha watu wake ?

Huitika. Naam, ndivyo niaminivyo.

Bishopu

MWAONA kwamba mwaitwa kweli kuuingia utumishi wa kanisa, kama apendavyo Bwana wetu Yesu Kristo, na kama ipasavyo katika ufalme huu?

Huitika. Naam, ndivyo nionavyo.

Bishopu

MWAAMINI pasipo shaka Maandiko yote ya kanuni ya Agano la Kale na ya Agano Jipyä?

Huitika. Naam, nayaamini.

Bishopu

MTAWASOMEA watu hayo kwa bidii watakapokutani ka katika kanisa mtakalowekwa kulitumikia?

Huitika. Naam, nitawosomea.

Bishopu

YAPASA kazi ya shemasi, katika kanisa atakalowekwa kulitumikia, kumsaidia kasisi katika ibada ya Mungu, tena ni zaidi atakaposongeza Ushirika Mtakatifu, kumsaidia katika kuwaeneza watu, na kusoma Maandiko matakatifu, na hotuba, kanisani; na kuwafunza watoto mafunzo ya Katekismo; na kasisi asipokuwapo kuwabatiza watoto wachanga, na kuhutubu akiruhusiwa na bishopu. Tena ni kazi yake, yatengezwapo mambo haya, kuwatatafuta wagonjwa, na maskini, na wanyonge, katika mipaka yake, kumpa kasisi habari ya hali zao, na majina yao, na mwahali mwao, ili kwamba wapate kusaidiwa kwa sadaka za watu wa mipaka ile, au wengine, wakiisha kuonywa na yeeye. Haya utayatenda kwa furaha na kwa ukunjufu wa moyo?

Huitika. Naam, nitayatenda, kwa msaada wa Mwenezezi Mungu.

Bishopu

MTAJITIA kwa moyo kuyatengeza maisha yenu, na maisha ya jamaa zenu, katika mafunzo ya Kristo; na kuonyesha nafsi zenu, na zao pia, kama mwezavyo, muwe vielelezvo vyenye manufaa mbele ya kundi la Kristo?

Huitika. Naam, nitayatenda, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu

JE, mtamtii kwa heshima bishopu wenu na watumishi wengine wakubwa wa kanisa, na waliopewa kuwangalia na kuwaamuru, na kuyafuata maonyo yao yaliyo sawasawa na mafunzo ya Maandiko ya Mungu kwa moyo wa furaha na mapenzi?

Huitika. Naam, nitajitahidi, kwa msaada wa Bwana.

¶ *Ndipo Bishopu huweka mikono kichwani mwake kila mmoja, hali amepiga magoti kwa unyenyekevu mbele yake, akinena,*

POKEA amri ya kuitenda kazi ya shemasi unayopewa katika kanisa la Mwenezezi Mungu; kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

¶ *Kisha Bishopu humpa kila mmoja chuo cha Agano Jipyä, akinena,*

POKEA amri ya kuisoma Injili katika kanisa la Mwenezezi Mungu, na kuihubiri hiyo, upewapo ruhusa kwa hiyo na bishopu mwenyewe.

¶ *Kisha mmoja mionganî mwao, aliyechagulitwa na Bishopu, husoma Injili*

Luka 12. 35-38

VYUNO vyenu na viwe kufungwa na taa zenu kuwaka: nanyi wenyewe iweni mfano wa watu wamongojeao bwana wao arudi kutoka arusini, ili ajapo akibisha, wamfungulie kwa upesi. Raha ni yao watumwa wale watakaoonekana kuwa wa macho na bwana wao ajapo. Ni kweli nawaambia, atajifunga atawakaribisha chakulani, awajongelee na kuwatumikia. Akija zamu ya pili, akija ya tatu, awaonapo hivi, raha ni yao watumwa wale.

¶ *Kisha Bishopu huendelea katika taratibu ya Ushirika Mtakatifu, na wote waliopewa daraja hukaa na kuipokea pamoja naye.*

¶ *Baada ya sala ya mwisho ya taratibu ya Ushirika Mtakatifu, na mbele ya kutamka kuavarikta watu, husoma sala hizi zifuatanzo hapa.*

EWE Mwenezezi Mungu, Mpaji wa mambo yote mema, wewe kwa wema wako bora umeridhika kuwakubali na kuwapokea watumwa wako hawa na kuwatia katika daraja

la ushemasi katika kanisa lako ; ewe Bwana, twakuomba, uwanjalie wawe na upole, na unyenyekevu, na bidii, katika utumishi wao, kisha wawe na miyo myepesi ya kuongozwa kwa maonyo yote ya rohoni ; ili kwamba huku wakishuhudiwa na nia zao njema siku zote, na kudumu daima kwa kukaa katika Mwanayo Kristo, waendee vyema katika daraja hili la mwanzo wapate kustahili kuitwa na kupewa kazi zilizo kuu katika kanisa lako ; kwa huyu Mwanayo Yesu Kristo Mwokozi wetu, ambaye ni vyake utukufu na heshima milele na milele. *Amina.*

UTUONGOZE, ewe Bwana, katika vitendo vyetu vyote kwa fachili ya neema yako, utupeleke mbele mumo kwa msaada wako daima ; ili kwa kazi zetu kuanzilizwa na kufulizwa na kutimilizwa ndani yako wewe, tulitukuze jina lako takatifu, na mwishowe tuyapate kwa rehema yako maisha ya milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

AMANI ya Mungu ipitayo fahamu zilizo zote, na Aiwalinde miyo yenu na nia zenu katika kumjua na kumpenda Mungu, na Bwana wetu, Yesu Kristo Mwanawewe. Na baraka ya Mungu Mweza-wa-yote, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, iwe mwenu ikae kwenu daima. *Amina.*

¶ *Wakati huo huyo shemasi na ambiwe ya kwamba adumu katika kazi ile ya ushemasi muda wa mwaka mzima (isipokuwa ni kwa sababu zifaazo bishopu apendapo ryingine) makusudi apate kuhitimu na kuyazoca sana mambo yapasayo kazi ya kanisani. Katika kutenda kazi hilo aonekanapo m' amini na kuwa na bidii, hupata kukubaliwa na bishopu wake na kuitwa katika daraja la ukasisi, kwa nyakati zilizoamriwa katika kanuni ; au pakiwa na sababu kubwa katika Jumapili au Siku kuu ryingine, mbele ya kanisa, kwa taratibu na jinsi ifuatanyo hapa.*

TARATIBU NA JINSI YA KUAMURU MAKASISI

¶ *Ikipikilia ile siku iliyogizwa na bishopu, baada ya Sala ya Asubuhi, huwa kuhutubu au kuonya, kwa kuyaweka wazi mambo yawapasayo na kazi zao hao wajao kukubaliwa kuwa makasisi ; jinsi daraja hilo lihitajiwavyo katika kanisa la Kristo, tena jinsi iwapasavyo watu kuwaheshimu katika hiyo kazi yao.*

¶ *Kwanza, Archdeacon, au badili yake, humletea bishopu (hali ameketi kitini mwake karibu ya Meza takatifu) wale watakao kufanya makasisi (kila mtu amevoaa vao limpasalo), na kunena maneno haya,*

BABA mwenye kuhashimiwa kwa mambo ya Mungu, Bnimekuletea watu hawa waliopo hapa wakubaliwe kuwa makasisi.

Bishopu

ANGALIA sana watu utuleteao wawe wafaa na kustahili kwa elimu yao na kwa miendo myema, kuutenda utumishi wao kama ipasavyo, kwa heshima ya Mwenyezi Mungu, na kwa kumjengea kanisa lake.

Archdeacon

NIMEWATAFITI, na kuwaauliza, nami nimewaona ndivyo walivyo.

¶ *Kisha Bishopu huwaambia watu waliopo :*

ENYI watu wema, hawa ndio tutakaowakubali hivi leo na kuwatia katika kazi takatifu ya ukasisi, Mungu akipenda : kwani tumekwisha kuwaauliza kama ipasavyo hatukuona neno la kinyume, ila twaona ya kwamba waitwa kwa njia ya halali, waingie katika kazi na utumishi wao ; tena ya kwamba ni watu wastahilio. Walakini akiwa immojawapo mionganoni mwenu mwenye kujua kizuizi chochote, au uovu ulio dhahiri, katika watu hawa

mmojawapo, ambao humzuilia asitiwe katika utumishi mtakatifu huu, na aje sasa kwa jina la Mungu aonyeshe uovu huo au kizuizi hicho.

¶ Na kama uovu mkubwa au kizuizi chatajwa, Bishopu huacha kumwamuru mitu yule, hata wakati atakapoonekana kuwa uovu huo hakuutenda huyo aliyeshtakiwa.

¶ Kisha Bishopu, pamoja na mapadre na watu waliopo, aimbe au kusoma Litania, kama ilivyoamriwa katika ukurasa wa 33, isipokuwa sala ya mtakatifu Chrysostom na baraka ya mwisho ziachwe zisisomwe.

¶ Kisha baada ya Litania huimbwa au husomwa taratibu ya Ushirika Mtakatifu, pamoja na Sala hii, na Waraka huu, na Injili hii ;

SALA

EWE Mwenyezi Mungu, Mpaji wa mambo yote yaliyo mema, wewe umeamuru, kwa Roho wako Mtakatifu, yawe madaraja mbali-mbali ya watumikao katika kanisa lako ; uwaangalie kwa rehema hawa watumwa wako, wanaoitwa na kutiwa katika daraja la ukasisi ; uwajaze ile kweli ya elimu yako, na kuwapamba kwa maisha mema, ili kwamba wao kwa maneno yao na kielelezo chao chema, wakutumikie kwa uaminifu katika kazi hiyo, ili jina lako litukuzwe, na kanisa lako lijengwe ; kwa kustahili kwake Yesu Kristo Mwokozi wetu, aishiyе na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. *Amina.*

WARAKA. Waefeso 4. 7-13

ILA tulipewa kila mmoja wetu ile neema, kwa kadiri ya kipimo cha kipawa cha Kristo. Kwa ajili ya hayo, asema, Alipopaa juu, aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa. (Basi neno hili, Alipaa, ni nini, isipokuwa ya kwamba alishuka pia na kuingia mwahali mwa chini mwa nchi ? Yeye aliyeshuka ndiye yeye huyo aliyepaa juu sana kuliko zile mbingu zote, ili kwamba avijaze vitu vyote.) Naye akawapa watu wengine *wawe* mitume : na wengine *wawe* manabii : na wengine *wawe* wahubiri wa ile habari njema : na wengine *wawe* wachuruga na waalimu : kwa

kukamilika kwao watakatisu, kufikilia kazi ya utumishi, kwa majengo ya mwili wa Kristo : hata tuufikilie ule umoja wa imani pia sote, na umoja wa kule kumjua Mwana wa Mwenyezi Mungu, hata *kuwa* mtu mtimilifu, hata kipimo cha umri wa kujaa kwake Kristo.

¶ Baadaye husomwa Injili fungu la mlango wa kenda wa Mathayo mtakatifu kama ifuatatanavyo

Mathayo 9. 36-38

NA alipowaona makutano ya watu, akawaonea huruma, kwa kuwa wao wa hali ya kulemewa, kisha wametawanyikana kama kondoo wasio na mchunga. Ndipo hapo akawaambia wanafunzi wake, Mavuno kweli ni mengi ; lakini watenda-kazi ni wachache. Basi mwombeni Bwana wa mavuno awapeleke watenda-kazi katika mavuno yake.

¶ Au badala yake, haya yafuutanayo, katika mlango wa kumi wa *Yohana*.

Yohana 10. 1-16

NI kweli, ni kweli nawaambia, asiyeingia kwa mlango ni katika zizi la kondoo, akweaye kwa pengine, ni mwivi huyo, tena ni mpokonyi. Na aingiaye kwa mlango ndiye mchunga wao kondoo. Yeye ndiye afunguliwaye mlango na mngeozeji, nao kondoo huisikia sauti yake, akawaita kondoo zake kila mmoja kwa jina lake, akawaongoza nje. Akisha kuwatoa nje wale kondoo wake wote, huwatangulia mbele yao ; nao kondoo humfua, kwa kuwa waijua sauti yake. Na mtu mgeni hawamfuati, wamkimbia, kwa kuwa hawazijui sauti za wageni. Simo hii aliwaambia Yesu, wala wasiyatambue ni maneno gani aliyonena nao. Basi akawaambia mara ya pili Yesu, Ni kweli, ni kweli nawaambia, mimi ndimi mlango wao kondoo. Waliokuja mbele yangu wote ni wevi, tena ni wapokonyi ; na kondoo hawakuwasikia. Mimi ndio mlango ; mtu atakapoingia kwangu mimi atakokoka, naye ataingia ndani akitoka nje, na malisha atayaona. Mwivi haji ili kwa kuiba na kuchinja na kuangamiza : mimi

nilikuja wapate kuwa na uzima, kisha wawe nao kwa wingi zaidi. Mimi ndimi mchunga mwema. **Mchunga** mwema huweka nchi uhai wake kwa ajili ya kondoo. Ila mtu mwajiriwa ambaye si mchunga, mtu yasiyokuwa mali yake wale kondoo, humwona mbwa-mwitu yuaja, akawaacha kondoo akakimbia, yule mbwa-mwitu akawakamata na kuwatawanya-tawanya ; mwajiriwa hukimbia kwa kuwa ni mwajiriwa yeye, wala hayafikiri ya kondoo. Mimi ndimi mchunga mwema ; nami hao wangu nawajua, nao wanijua walio wangu, kama Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba ; tena uhai wangu nauweka nchi kwa ajili ya kondoo. Nami nina kondoo wengine, wasiokuwa wa zizi hili ; nao hao imenipasa kuwaongoza, na sauti yangu wataisikia : kisha, watakuwa ni kundi moja, mchunga mmoja.

Kisha Bishopu, hali ameketi kitini mwake, huwaambia kama haya ;

MMESIKIA, ndugu zangu, hapo mlipoulizwa kwa faragha, na katika maonyo hayo mliyoonywa sasa, na katika masomo matakatifu yaliyotwaliwa katika Injili, na katika maandiko ya mitume, jinsi daraja hili mliolitiba lilivyo na heshima na sifa kubwa. Na sasa tena twawaonya katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo, ili mkumbuke, jinsi ilivyo kuu hiyo heshima mliyoitiwa, na jinsi ilivyo bora hiyo kazi na hayo maagizo yenu ; maana, ni kuwa wajumbe, na walinzi, na mawakili wa Bwana ; kufunza, na kuonya, kulisha na kuwatunza jamaa za Bwana ; kuwatafuta kondoo wa Kristo waliotawanyika, na kuwatafuta watoto wake walio katika dunia hii mbovu, ili kwamba waokoke kwa njia ya Kristo milele.

Basi, siku zote muwe na neno hili lenye kupigwa muhuri katika kukumbuka kwenu, maana, jinsi ilivyo kuu hiyo hazina mliyopewa. Kwa kuwa hawa ni kondoo wa Kristo, aliowanunua kwa kifo chake, na kwa ajili yao alimwaga damu yake. Hilo kanisa na huo mukutano mtakaoutumikia ni bibi-arusi wake, kisha ni mwili wake. Ikitukia, kanisa hilo, au via vyake kimojawapo, kupati-kana na maumivu au kizuizi kwa ajili ya kutoangalia

kwenu, mwajua jinsi liliyvo kuu kosa hilo, tena mwajua jinsi ilivyo na utisho adhabu hiyo itakayoandama. Kwa ajili ya hayo wazeni na kufikiri kwa nafsi zenu huo mwisho wa utumishi wenu kwa ajili ya watoto wa Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya bibi-arusi, mwili wa Kristo ; mwangalie kwamba msiache kutumika kwenu, na kutunza kwenu, na bidii zenu, hata mtende yote mwezayo, kama vile iwapasavyo, kuwaleta wote hao waliowekwa au watakaowekwa katika tunza lenu, hata wafikilie yale mapatano katika imani na kumjua Mwenyezi Mungu, na kufikilia kuhitimu na kukamilika katika Kristo, ili kwamba pasiwe na nafasi kati yenu, kwa uwongo wa dini au kwa uovu wa mwendo.

Basi kwa kuwa kazi yenu ilivyo na heshima kuu, pamoja na kuwa na uzito mwingi, mwaona jinsi iwapasavyo kujibidiisha kwa kujitunza sana na kwa kusoma sana, tena kuonyesha nafsi zenu wenye kutii na wenye shukrani kwa Bwana aliywaweka katika heshima kuu jinsi hiyo ; pamoja na haya kujitunza, ili msikunguwae wenyewe, wala msiwakunguaze wengine. Lakini, hamwezi kuwa na nia na mapenzi katika hayo kwa nafsi zenu peke yenu ; kwa kuwa mapenzi hayo na nguvu hizo hutolewa na Mwenyezi Mungu pekee : kwa ajili ya hayo inawapasa, tena mwahitajia sana, kuomba kwa bidii ili mpewe Roho wake Mtakatifu. Nanyi kwa kuwa hamwezi kwa njia nyininge iwayo yote kufanya kazi iliyo na uzito jinsi hii, ipasayo wokofu wa binadamu, isipokuwa kwa mafunzo na maonyo yapatikanayo katika Maandiko matakatifu, na kwa mwendo wa maisha ufananao nayo ; wazeni jinsi iwapasavyo kuwa na bidii sana katika kuyasoma na kuifunza hayo Maandiko, na katika kuyalinganisha mambo ya maisha yenu wenyewe, na maisha ya hao walio karibu nanyi, sawasawa na kanuni ya Maandiko hayo : tena kwa ajili iyo hiyo jinsi iwapasavyo kujitenga nayo na kuweka kando (kama mwezavyo) mambo yote na shughuli zote za dunia.

Twatumaini sana ya kwamba mmekwisha kuyapima na kuyafikiri mambo hayo kwa nafsi zenu tangu hapo ; tena ya kwamba mmekusudia sana, kwa kuneemeshwa na

Mwenyezi Mungu, kujitia kabisa katika kazi hii, ambayo Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nayo kuwaitia : hata iwe, kama mwezavyo, kuweka nafsi zenu kwa jambo hili kabisa, na kuyalekeza mambo yenu yote na kusoma kwenu kote katika njia hii ; tena kwamba mtamwomba Mwenyezi Mungu Baba, daima, kwa njia ya kuombea kwake Mwokozi wetu aliye pwekee Yesu Kristo, ili mpate msaada wa mbinguni, maana, wa Roho Mtakatifu ; ili kwamba, kwa kusoma Maandiko kila siku na kuyafikiri, mpate kwendelea kuhitimu na kupata nguvu katika utumishi wenu ; tena ya kwamba mfanye bidii, nyakati zote, kutakasa maisha yenu na maisha ya watu wenu na kuyalinganisha na kanuni na mafunzo ya Kristo, ili kwamba muwe vielelezo na namna yenyе manufaa na yenye uchaji-wa-Mungu, yatakayofuatwa na watu.

Basi sasa, ili kwamba mukutano huu wa Kristo uliopo hapa, upate kujuua nia zenu na mapenzi yenu katika mambo hayo, tena kwamba ahadi yenu hii iwahimize zaidi kufanya yawapasayo, mtayajibu wazi-wazi maneno haya, ambayo sisi, katika jina la Mwenyezi Mungu, na katika jina la kanisa lake, tutakayowauliza kuliko kazi hii.

JE, mwaona ndani ya mioyo yenu ya kwamba mmeitwa kweli kama apendavyo Bwana wetu Yesu Kristo, kwa taratibu ya Kanisa la Uingereza, mwingie katika daraja na utumishi wa ukasisi ?

Huitika. Naam, ndivyo nionavyo.

Bishopu

MWAONA hakika-hakika ya kwamba hayo Maandiko matakatifu yana utoshelevu wa mafunzo yote yahitajiwayo kwa kuupata wokofu wa milele kwa njia ya imani iliyo kwa Yesu Kristo ? Tena mwakusudia kuwafunza watu waliowekwa katika tunza lenu, katika Maandiko hayo, wala msifunze neno lolote, kusema kwamba lahitajiwa kuupata wokofu wa milele, lisilokuwa ni hilo mlilohakikishwa ya kwamba lapatikana na kuthubutishwa na hayo Maandiko ?

Huitika. Naam, ndivyo nilivyohakikishwa, nami nakusudia kufanya hivyo, kwa kuneemeshwa na Mwenyezi Mungu.

Bishopu

JE, mtafanya bidii kwa uaminifu kutumia mafunzo na sakramenti pamoja na amri-za-kurudiwa, kama Bwana Kristo alivyozi amuru, na kama kanisa hili na ufalme huu ulivyozi pokea, sawasawa na maagizo ya Mwenyezi Mungu ; ili kwamba mwafunze watu hao mliopewa ninyi kuwaturunza na kuwachunga, wayashike na kuyaandama hayo kwa bidii yote ?

Huitika. Naam, ndivyo nitakavyofanya, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu

JE, mtakuwa tayari, kwa bidii ya uaminifu, kuyaacha na kuyakataza mafunzo yote yaliyo ya uwongo na uzusi, yapingamanayo na Neno la Mwenyezi Mungu ; tena mtatumia maonyo na kuhimiza, yaliyo dhahiri na yaliyo ya siri, yaliyo kwa wagonjwa na yaliyo kwa wazima, katika mipaka yenu, kama ihitajiwayo, na kama mtakavyopewa nafasi ?

Huitika. Naam, nitafanya, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu

JE, mtakuwa na bidii na kuomba, na kusoma Maandiko matakatifu, tena katika kusoma kwingine kwenye kutia msaada katika ujuzi wa hayo, huku mkiweka kando utume wa dunia na wa mwili ?

Huitika. Naam, nitafanya bidii kufanya vivyo, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu

JE, mtakuwa na bidii kutengeza nafsi zenu wenywewe, na za jamaa zenu, kuzilinganisha na mafunzo ya Kristo ; na kufanya nafsi zenu na zao, kama mwezavyo, ziwe vielelezo na namna mbele ya kundi la Kristo ?

Huitika. Naam, nitajibidiisha kwa hayo, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu

JE, mtathubutisha, na kuhimiza, kama mwezavyo, utulivu, na amani, na mapenzi katika Wakristo wote, lakini sana ni katika hao waliowekwa au watakaowekwa katika tunza lenu ?

Huitika. Naam, nitafanya vivyo, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu

JE, mtamtii kwa heshima bishopu wenu, pamoja na watumishi wengine wakubwa wa kanisa, waliopewa kuwaangalia na kuwaamuru : na kuyafuata siku zote kwa moyo wa furaha na mapenzi maonyo yao na mashauri yao yaliyo sawasawa na Maandiko ya Mwenyezi Mungu ?

Huitika. Naam, nitafanya vivyo, kwa msaada wa Bwana.

¶ *Kisha Bishopu husimama na kusema,*

MWENYEZI Mungu, aliywapa ninyi nia hii kufanya mambo hayo yote ; na awape nguvu na uwezo wa kuyatimiza ; ili kwamba aikamilishe kazi yake aliyoanziliza ndani yenu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, Amina.

¶ *Kisha mukutano hutakwa, katika kuomba kwa kwa siri, wamnyenyeknee Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mambo hayo yote : na kwa ajili ya maombi hayo huwa kimya muda mdogo.*

¶ *Kisha huimbwa au husomwa na Bishopu (na wakati huo hao watakaotiwa katika daraja la ukasisi wa hali ya kupiga magoti), wimbo huu, Veni, Creator Spiritus ; Bishopu mwenyewe huanza, na makasisi na wengine waliopo huitika mstari kwa mstari.*

Roho Muumba, vuvia,
Washe moto kwetu pia ;
Ndiwe Mpaka-mafuta,
Saba-saba tukipata.

Neema itokayo juu
Mna uhai na nafuu ;
Tutie nuru daima,
Macho na yawe mazima.

Twoshe, nyusoni tupake ;
Usafi, Bwana, tivikwe ;
Waepushe na adui ;
Ulipo hawasumbui ;

Tujuvye Baba na Mwana
Na wewe kuungamana ;
Kwamba kwa zamani zote
Kukwimbia tusiache.

Baba, Mwana, twakusifu,
Nawe Roho Mtakatifu. Amina.

(Huu ni wimbo wa 214 katika Chuo cha Nyimbo.)

¶ *Ndipo Bishopu huomba hivi ;*

Na tuombe

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, Baba uliye mbinguni, wewe, katika mapenzi yako yasiyo ukomo, na mema yako yatufikiliayo sisi, umetupa sisi Mwanayo wa pekee, mwenye kupendwa sana, Yesu Kristo, awe Mwokozi wetu, na mwenye kuanziliza uzima wa milele ; ambaye, akiisha kukamilisha ukombozi wetu kwa mauti yake mwenyewe, na kupaa juu na kuingia mbinguni, akawatuma mitume wake, na manabii wake, na wahubiri-wa-habari-njema, na waalimu, na wachunga, waende katika ulimwengu ; ambao kwa njia ya kazi zao na utumishi wao alikutanisha pamoja kundi kuu pande zote za ulimwengu, waweke wazi sifa za milele za jina lako takatifu ; kwa ajili ya hizi fadhili kuu za wema wako wa milele, na kwa kuwa wewe umekuwa radhi kuwaita watumishi wako hawa waliopo hapa waingie katika kazi iyo hiyo ya utumishi huu ulioamuru kwa wokofu wa binadamu, twakushukuru sana ndani ya mriyo yetu, twakusifu, na kukusujudia ; nasi twakuomba kwa kunyenyeka, kwa yeze huyo Mwanayo Mwenye-baraka, utupe sote ambao, hapa au penginepo twalingana jina lako takatifu, kwamba tudumu na kuonyesha nafsi zetu wenye shukrani kwako kwa ajili ya fadhili zote hizi na nyingine zote ; ili kwamba tuongee kila

siku na kwendelea mbele katika kukujua na kukuamini wewe na Mwanayo, kwa Roho Mtakatifu. Na iwe hivyo ili kwamba jina lako litukuzwe siku zote na hawa watumishi wako, na wale ambao watu hawa watakaowekwa wawe watumishi wako juu yao, tena ufalme wako ulio na baraka utangae ; kwa yeze huyo Mwanayo Yesu Kristo, Bwana wetu, ambaye yuaishi na kutawala pamoja na wewe katika umoja wa yeze Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. *Amina.*

¶ *Ndipo husaliwa sala hiyo ; Bishopu pamoja na makasisi walio po wakieka mikono yao juu ya kichwa cha kila mmoja apewaye daraja la ukasisi ; hao wapewao daraja wawe hali ya kupiga magoti kwa unyenyekevu, na Bishopu hunena,*

POKEA Roho Mtakatifu kwa daraja na kazi ya kasisi katika kanisa la Mwenyezi Mungu, upewayo sasa kwa kukuwekea mikono yetu. Kadiri ya watu uwasameheo madhambi yamesamehewa : kadiri ya watu uwazuliao madhambi, yamezuliiwa. Nawe uwe wakili mwaminifu wa Neno la Mwenyezi Mungu, na wa sakramenti zake takatifu ; kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. *Amina.*

¶ *Kisha Bishopu huwapa watu hao kila mmoja, hali amepiga magoti, Biblia mkononi mwake, na kumwambia,*

TWAA amri wewe kuhubiru Neno la Mwenyezi Mungu, na kuwapa watu sakramenti takatifu katika mkuano, hapo utakapowekwa kwa amri.

¶ *Ndipo huimbwa au kusomwa Imani ya Nikea.*

¶ *Baadaye Bishopu huendelea katika taratibu ya Ushirika Mtakatifu, ambao wote hawa walipokea daraja hushiriki pamoja, na kukaa pahali hapo ambapo waliwekewa mikono, hata wakiisha kuupokea.*

¶ *Ukiisha Ushirika Mtakatifu, baada ya sala ya mwisho, na mbele ya kuwabarikia watu, kusomwa sala hizi zifuatanzo hapa.*

EWE Baba, mwingi wa rehema, twakuomba sana ulete baraka yako ya mbinguni juu ya watumishi wako hawa ; ili kwamba wavikwe haki, tena kwamba Neno lako

litamkwalo kwa vinywa vyao lifae, lisinenwe bure majira yoyote. Utupe nasi, kwamba tuneemeshwe kusikia na kukubali lolote watakalotuambia litokalo katika Neno lako lililo takatifu sana, au lilingamanalo nalo, kuwa ni njia ya wokofu wetu ; kwamba katika maneno yetu yote na vitendo vyetu vyote tutukuze utukufu wako, na maongeo ya ufalme wako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

UTUONGOZE, ewe Bwana, katika vitendo vyetu vyote kwa fadhilli ya neema yako, utupeleke mbele mumo kwa msaada wako daima ; ili kwa kazi zetu kuanzilizwa na kufulizwa na kutimilizwa ndani yako wewe, tulitukuze jina lako takatifu, na mwishowe tuyapate kwa rehema yako maisha ya milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

AMANI ya Mungu ipitayo fahamu zilizo zote, na iwalinde miyo yenu na nia zenu katika kumjua na kumpenda Mungu, na Bwana wetu Yesu Kristo Mwanawee. Na baraka ya Mungu Mweza-wa-yote, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, iwe mwenu ikae kwenu daima. *Amina.*

¶ *Ikiwa kwa siku ile ile moja wengine hupewa daraja la ushemasi, na wengine hupewa daraja la ukasisi ; hao mashemasi huletwi kwanza, baadaye huletwi hao makasisi ; tena hutosheleza hiyo Litania kusomwa mara moja kwa ajili ya wote. Hizo sala hutumwa zote mbili ; kwanza ile sala kwa ajili ya mashemasi, baadaye ile kwa ajili ya makasisi. Waraka huwa Waefeso 4. 7-13, kama ilivyotangulia katika taratibu hii. Mara baadaye wale watakapewa daraja la ushemasi huulizwa na kuwekewa mikono, kama ilivyaoambwa nyuma.*

Kisha watu hao mnojawapo akiisha kusoma Injili (nayo hutwaliwa katika Mathayo 9. 36-38, kama ilivyowekwa hapo nyuma katika taratibu hii, au ya Luka 12. 35-38, kama ilivyo hapo nyuma katika taratibu ya kuweka mashemasi,) hao watakapewa daraja la ukasisi huulizwa na kuwekewa mikono, kama ilivyaoamriwa hapo nyuma katika taratibu hii.

TARATIBU YA KUAMURU AU KUWEKA
KWA KAZI TAKATIFU BISHOPU MKUU
AU BISHOPU

(TARATIBU HII HAITUMIWI ISIPOKUWA NI KATIKA
SIKU YA JUMAPILI AU SIKU NYINGINE ILIYO TAKATIFU.)

Vitru vyote vikiisha kuwekwa tayari msikitini kama ipasavyo, na kutengenzwa, baada ya Sala ya Asubuhi, bishopu mkuu (au bishopu mwingine aliyeagizwa), huanza taratibu ya Ushirika Mtakatifu; na sala yake ni hii :

SALA

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, wewe kwa Mwanayo Yesu Kristo uliwapa mitume wako watakatifu vipawa vingi vilivyo bora, kisha ukawaagiza kulilisha kundi lako : twakuomba sana, uwaneemeshe mabishopu wote, wachunga wa kanisa lako, ili kwamba wahubiri neno lako kwa bidii sana, kisha watumie amri-za-kurudiwa kama utakavyowaongoza : uwape watu waliandarne hilo kwa kutii, ili kwamba wote wapate taji ya utukufu wa milele : kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Kisha bishopu mwingine husoma Waraka

1 Timotheo 3. 1-7

NI la kuaminiwa lile neno, Mtu awaye yote akitaka sana kazi ya mwangalizi, atamani kazi nzuri. Basi inampasa huyo mwangalizi awe hana matayo, awe mume wa mke mmoja, mwenye kudhibiti nafsi, mwenye akili kamili, mwenye adabu, mwenye kukaribisha wageni, mwenye uwezo wa kufunza ; asiwe mwenye kupenda ulevi, asiwe mwenye kuwapiga watu, asiwe mwenye kutamani mapato ya uovu ; lakini awe mwenye upole, asiwe mwenye kuteta na watu, asiwe mwenye kutamani-tamani ; awe ni mtu asimamiaye nyumba yake mwenyewe kwa wema, mwenye watoto wenye kunyenyeka kwa kila

utulivu : (ila ikiwa mtu hajui kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje kanisa la Mungu ?) asiwe mpya wa *iman*, ili isiwe akifura kichwa bure, akaanguka na kuingia hukumu ya Shetani. Zaidi ya hayo inampasa ashuhudiwe kuwa mwema na hao walio nje ; ili isiwe akaanguka katika laumu na katika tanzi la Shetani.

Au huu :

BADALA YA WARAKA. *Vitendo vya Mitume 20. 17-35*

PAULO akatuma watu kutoka Mileto kwenda Efeso, akawaita wazee wa kanisa waje kwake. Basi wali-pomfikilia, akaawaambia, Ninyi wenyewe mwajua, tangu siku ile nilipoanza kukanyaga nchi hii ya Asia, ni kwa jinsi gani nilivyoketi nanyi majira hayo yote ; niki-mtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote wa moyo, na machozi mengi, na taabu zile zilizonipata kwa kunivizia kwao Mayahudi : jinsi nisivyosita katika kuwhabiri neno lolote lenye kuwafaa, nikiwafunza mbele ya watu, tena nyumba baada ya nyumba, nikiwaonya Mayahudi, na Mayunani pia, kutubia kwa Mwenyezi Mungu, na kuamini kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Na sasa angalieni, mimi naenda zangu Yerusalem, ni hali ya kufungwa roho yangu, nisiyajue mambo yale yatakayonipata huko : asipokuwa ye ye Roho Mtakatifu hunishuhudia katika kila mji, akaniambia ya kwamba vifungo na taabu vyaningoeja. Lakini katika hayo yote hapana linistushalo lolote, wala sitii hesabu ya uhai wangu kuwa ni kitu kwangu mimi, ili nipate kutimiliza maisha yangu kwa furaha, na utumishi huo niliopokea kwa Bwana Yesu, nipate kushuhudia ile habari njema ya neema ya Mwenyezi Mungu. Na sasa angalieni, najua ya kwamba ninyi nyote ambao nimezunguka-zunguka kati yenu, na kuhubiri ufalme wa Mwenyezi Mungu, hamtaniona tena uso wangu. Ndipo kuwashuhudia ninyi hivi leo, ya kwamba mimi ni safi katika damu za watu wote. Kwani sikusita katika kuwhabiri ninyi mapenzi yote ya Mwenyezi Mungu. Kwa ajili ya hayo zilindeni nafsi zenu, *mkalilinde* na kundi lote, ambalo Roho Mtakatifu amewafanya ninyi

kuwa waangalizi ndani yake, mpage kulilisha kanisa la Mwenyezi Mungu, ambalo ameinunulia nafsi yake, liwe lake, kwa damu yake mwenyewe. Kwani mimi najua neno hili, ya kwamba baada ya kuondoka kwangu mimi mbwa-mwititu wakali wataingia ndani yenu, wasiolihurumia lile kundi ; na watu wengine watainuka kutoka katika ninyi wenyewe, na kunena yaliyopotoka, wapatekuwavuta wanafunzi wawaandamie wao. Kwa ajili ya hayo basi kesheni, na kukumbuka ya kwamba kwa muda wa miaka mitatu, usiku na mchana, sikuacha kumwonya kila mtu mmoja na *kumwaga machozi*. Na sasa, ndugu zangu, nawatia kwa Mwenyezi Mungu, na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kufanisha, na kuwapa urithi katika wale wote waliotakaswa. Sikutamani fedha ya mtu awaye yote, wala dhahabu, wala mavao. Naam, ninyi wenyewe mwajua ya kwamba mikono yangu hii ilitumika kwa ajili ya haja zangu mwenyewe na za wale waliokuwa nami. Katika yote niliwapa ninyi kielelezo, ya kwamba mkitaabika kwa kazi jinsi hiyo, imewapasa kuwasaidia walio wanyonge, na kukumbuka yale maneno ya Bwana Yesu, jinsi yeze mwenyewe alivyo sema, Ina heri kuwapa *watu* zaidi ya kupokea.

Kisha bishopu mwingine husoma Injili

Yohana 21. 15-17

YESU akamuuliza Simoni Petero, Je, Simoni wa Yona, wanipenda zaidi ya hawa? Akamwambia, Ndiyo, Bwana : wewe umenijua kuwa nakupenda. Akamwambia, Walishe wana-wa-kondoo wangu. Akamuuliza tena mara ya pili, Ewe Simoni wa Yona, wanipenda? Akamwambia, Ndiyo, Bwana ; wewe umenijua kuwa nakupenda. Akamwambia, Wachunge kondoo zangu. Akamuuliza mara ya tatu, Ewe Simoni wa Yona, wanipenda? Akaingiwa na huzuni Petero kwa vile aliyomuuliza mara ya tatu, Wanipenda? Akamwambia, Ewe Bwana, wewe mambo yote umeyajua : watambua mwenyewe kwamba nakupenda. Yesu akamwambia, Walishe kondoo zangu.

Au hii :

Yohana 20. 19-23

BASI siku ile ile, nayo ni ya sabatu-mosi, kulipokuchwa, ile milango imekwisha kufungwa pale walipokuwapo wanafunzi, maana kwa hofu waliyo nayo ya Mayahudi, akaenda Yesu akasimama katikati ; akawaambia, Amani iwe kwenu! Aliposema hayo, akawaonyesha mikono yake na ubavu wake. Ndipo wakafurahi wanafunzi kwa kumwona Bwana. Basi Yesu akawaambia tena, Amani iwe kwenu! Kama vile alivyonituma Baba, nami nawapeleka vivyo. Akisema haya akawavuvia, akawaambia, Twaeni Roho Mtakatifu. Kadiri ya watu mwameheo madhambi, yamesamehewa kwao : kadiri ya watu mwazui-liao madhambi, yamezuiliwa kwao.

Au hii :

Mathayo 28. 18-20

YESU akaenda akasema nao, akawaambia, Nimepewa amri yote katika mbingu na nchi. Basi endeni mifikanye mataifa wote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu : huku mkiwafunza kuyashika niliyowaagiza yote : mimi nami ni pamoja nanyi zamani zote, hata ukamilifu wa dahari. Amina.

I Baada ya Injili, na Imani ya Nikea, na kuhubiri kukiisha, huyo bishopu aliyezaguliwa (huwa hali amevaa Rochet) hulewa na mabishopu watili mbele ya bishopu mkuu wa nchi ile (au mbele ya bishopu mwingine aliyeagizwa kwa halali), bishopu mkuu hali aneketi kitini mwake karibu ya Meza takatifu, na hawa mabishopu wanaomleta hunena,

BABA mkuu mwenye kuheshimiwa kwa mambo ya Mungu, twakuletea mtu huyu, mchaji-wa-Mungu, mwenye elimu, aamriwe na kuwekwa kwa kazi takatifu ya ubishopu.

¶ Hapo huyo Bishopu mkuu hutaka hati ya amri ya Mfalte kwa kumweka kwa kazi takatifu, ataamrisha isomwe. Kisha huapishwa kumtii bishopu mkuu kama vipasavyo, kwa maneno yafuananayo,

Hiki ni kiapo cha kumtii bishopu mkuu kama vipasavyo

KWA jina la Mwenyezi Mungu. Amina. Mimi (*fulani*) niliyechaguliwa kuwa bishopu wa kanisa na ubishopu wa (*nchi fulani*) nakubali na kuahidi heshima yote ipasayo na kumtii kama vipasavyo bishopu mkuu na kanisa kuu la (*nchi fulani*) na kwa hao watakoakuja baada yake : Mwenyezi Mungu na anisaidie kwa hayo, katika Yesu Kristo.

¶ Kiapo hiki hakitakuwa aewekwapo bishopu mkuu kwa kazi takatifu.

¶ Kisha Bishopu mkuu huutaka mkutano uliopo kuomba, akawaambia maneno haya ;

NDUGU zangu, yameandikwa katika Injili ya mtakatifu Luka, ya kwamba Mwokozi wetu Kristo alikesha usiku kucha kuomba Mungu, ndipo akawachagua na kuwatuma mitume wake kumi na wawili. Tena yameandikwa katika chuo cha Vitendo vya Mitume, kwamba hao wanafunzi waliokuwa mji wa Antiokia wakafunga na kuomba Mungu, ndipo wakawekea mikono Paulo na Baranaba, na kuwatuma. Sisi nasi basi, kwa kufuata kielelezo cha Mwokozi wetu Kristo, na mitume wake, kwanza tujitie katika kuomba Mungu, mbele ya kumwamuru na kumtuma mtu huyu tulieletewa, aende katika kazi ambayo twatumaini Roho Mtakatifu amemwitia.

¶ Kisha husomeva Litania kama ilivyoamriwa katika ukurasa wa 33, isipokuwa, hapo palipo maneno haya, Uwe radhi, hao mabishopu wote, w.k., sala ile huachwa, na maneno haya yatiwe pahali pake,

UWE radhi kumbarikia ndugu yetu aliyechaguliwa, umpe neema yako, ili kwamba apate kufanya kazi hiyo aliyoitiwa, kwa kujenga kanisa lako, na kwa heshima na sifa na utukufu wa jina lako :

Twakuomba utusikize, Bwana mwema.

¶ Kisha husomeva sala hii ifuatanyo,

EWE Mungu, Mweza-wa-yote, Mpaji wa vitu vyote vyema, wewe kwa Roho wako Mtakatifu umeamuru madaraja mbali-mbali ya watumikao katika kanisa lako : umwangalie kwa rehema huyu mtumwa wako aitwaye sasa kwa kazi na utumishi wa bishopu ; umjaze ile kweli ya elimu yako, na kumpamba kwa maisha mema, ili kwamba, kwa maneno yake na kwa vitendo vyake, akutumikie kwa uaminifu katika kazi hii, kwa utukufu wa jina lako, na kwa kulijenga kanisa lako ; kwa kustahili kwake Mwokozi wetu Yesu Kristo, ambaye yuaishi na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, sasa na hata milele. Amina.

¶ Kisha Bishopu mkuu, hali ameketi kitini mwake, humwambia huyo atakayewekwa kwa kazi takatifu, maneno haya,

NDUGU yangu, kwa kuwa Maandiko matakatifu na kanuni za zamani zimetuamuru, kwamba tusiwe na haraka katika kumwekeea mtu mikono wala kumkubali mtu awaye yote katika kutawala ndani ya kanisa la Kristo, alilolinunua kwa thamani kuu ya kumwaga damu yake mwenyewe ; kabla sijakutia katika utumishi huu, nitakuulla maneno kadhawakadha, ili kwamba huu mkutano uliopo ukujaribu, na kushuhudia jinsi unuiliavyo kuishi maisha yako katika kanisa la Mungu.

JE, wewe waona hakika-hakika ya kwamba umeitwa kweli katika utumishi huu, kama apendavyo Bwana wetu Yesu Kristo, na kama ipasavyo katika ufalme huu ? *Huitika.* Naam, ndivyo nionavyo.

Bishopu mkuu

JE, wewe waona hakika-hakika ya kwamba Maandiko matakatifu yana utoshelevu wa mafunzo yote yahitajiwayo kwa kuupata wokofu wa milele kwa njia ya imani iliyo kwa Yesu Kristo ? Tena wewe wakusudia kuwafunza watu waliowekwa katika tunza lako katika Maandiko hayo,

wala usifanye neno lolote kusema kwamba lahitajiwa kuupata wokofu wa mielele lisilokuwa ni hilo ulilohakikishwa ya kwamba lapatikana na kuthubutishwa na hayo Maandiko ?

Huitika. Naam, ndivyo nilivyohakikishwa, nami naku-sudia kufanya hayo, kwa kuneemeshwa na Mwenyezi Mungu.

Bishopu mkuu

JE, utajizoeza kwa uaminifu katika hayo Maandiko matakatifu, na kumlingana Mwenyezi Mungu kwa maombi, upate kuelewa na hayo ; ili kwamba upate kwa hayo kufunza na kuhimiza kwa mafunzo yenye manufaa, na kuwazuia na kuwashinda hao washikao kinyume ?

Huitika. Naam, ndivyo nitakavyofanya, kwa msaada wa Mungu.

Bishopu mkuu

JE, u tayari, kwa bidii na uaminifu, kuyaacha na kuya-kataza mafunzo yote yaliyo ya uwongo na uzusi yapi-ngamanayo na Neno la Mwenyezi Mungu ; tena kwa faragha na kwa dhahiri utawataka na kuwashimiza wengine wafanye vivyo ?

Huitika. Naam, ni tayari, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu mkuu

JE, utajiepu na uovu wote na shauku za dunia, nawe Jutaishi kwa kudhibiti nafsi, na kwa utakatifu, na uchajiji-wa-Mungu, katika dunia hii ya sasa : ili kwamba upate kuonyesha nafsi yako katika mambo yote kuwa u kielelezoo cha vitendo vyema mbele ya wengine, ili kwamba huyo adui atahayari, maana, hana neno la kusema juu yako ?

Huitika. Naam, nitafanya, kwa msaada wa Bwana.

Bishopu mkuu

JE, utathubutisha, na kuhimiza, kama uwezavyo, utulivu, na mapenzi, na amani katika watu wote : na kuwatia na kuwatia adabu hao walio watesi na wasiotii na wakosaji

katika ubishopu wako, kwa kadiri ya amri uliyopata katika Neno la Mwenyezi Mungu, na kama utakavyopewa na amri ya ufalme huu ?

Huitika. Naam, nitafanya, kwa msaada wa Mungu.

Bishopu mkuu

JE, utakuwa mwaminifu katika kuamuru, kutuma, na kuwekeea mikono wengine ?

Huitika. Naam, ndivyo nitakavyokuwa, kwa msaada wa Mungu.

Bishopu mkuu

JE, utaonyesha nafsi yako kuwa mpole, na mwenye kurehemu kwa ajili ya Kristo, hao maskini na wahitaji, na wageni wote wasio na msaada ?

Huitika. Naam, nitaonyesha nafsi yangu hivyo, kwa msaada wa Mungu.

¶ Hapo Bishopu mkuu husimama na kusema,

MWENYEZI Mungu, Babaetu aliye mbinguni, ye ye Maliyekupa wewe nia njema ya kuyafanya haya yote, na akupe tena nguvu na uwezo kuyatimiza hayo ; ili kwa ye ye kutimiliza ndani yako hizo kazi njema alizoanziliza, upatikane wewe kuwa mtimilifu pasipokuwa na laumu kwa siku ya mwisho ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Hapo ndipo huyo bishopu aliyechaguliwa atavaa mavao mengine ya bishopu kwa utimilifu wake ; naye aktisha kupiga magoti, Veni Creator Spiritus, huimbwa au husomwa juu yake, bishopu mkuu mwenyewe huanza na wale mabishopu wengine, pamoa na wale watu wengine waliopo, huitika, mstari kwa mstari, kama visuatatanavyo (ni wimbo wa 214 katika Chuo cha Nyimbo) ;*

Roho Muumba, vuvia,
Washe moto kwetu pia ;
Ndiwe Mpaka-mafuta,
Saba-saba tukipata.

Neema itokayo juu
Mna uhai na nafuu ;
Tutie nuru daima,
Macho na yaree mazima.

KUAMURU BISHOPU

Twoshe, nyusoni tupake
Usafi, Bwana, twikwe ;
 Waepushe na adui ;
Ulipo hawasumbui ;

Tujuvye Baba na Mwana
Na wewe kuingamana ;
 Kwamba kwa zamani zote
Kukwimbia tusiache.

Baba, Mwana, twakusifu,
 Nawe Roho Mtakatifu. Amina.

Ndipo Bishopu mkuu hunena,

Ewe Bwana, utusikize maombi yetu ;
Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Na tuombe

EWE Mwenyezi Mungu, Baba mwangi wa rehema, Ewewe kwa wema wako usio ukomo ultupa Mwanayo wa pekee, Mpenzi wako sana, Yesu Kristo, awe Mkombozи wetu, awe mwenye kutuanzilizia uzima wa milele ; ye ye ambaye baada ya kuukamilisha wokofu wetu kwa njia ya mauti yake, na kupaa na kuingia mbinguni, aliwamininia vipawa vyake juu ya wanadamu kwa wingi, akawafanya wengine wawe mitume, na wengine wawe manabii, na wengine wawe wahubiri-wa-habari-njema, na wengine wawe wachunga na waalimu, kwa kulijenga kanisa lake na kulikamilisha ; twakuomba sana umpe huyo mtumishi wako neema hiyo ili kwamba awe tayari siku zote kuitangaza Injili yako, habari njema ya upatanisho, watu watakavyopatana na wewe ; tena atumie hii amri apewayo, si kwa uvunjifu, lakini kwa wokofu ; si kwa kuumiza, lakini kwa kusaidia ; na kama mtumishi mwenye akili, mwaminifu, awapaye jamaa zako chakula kiwapasacho wakati wake, awe mwisho mtu wa kukubaliwa katika furaha za milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, ambaye pamoja na wewe na Roho Mtakatifu ni mwenye kuishi na kutawala, Mungu mmoja milele. Amina.

KUAMURU BISHOPU

I Hapo ndipo huyo bishopu mkuu na mabishopu walipo wataweka mikono yao juu ya kichwa cha huyo bishopu aliyechaguliwa, hali amepiga magoti mbele yao, na bishopu mkuu hunena,

POKEA Roho Mtakatifu, kwa daraja na kazi ya bishopu katika kanisa la Mwenyezi Mungu, upewayo kwa kukuwekea mikono yetu ; kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina. Nawe kumbuka uchochee hiyo neema ya Mungu uliyopewa hivi kwa kuwekewa mikono yetu ; kwa kuwa Mwenyezi Mungu hakutupa roho ya hofu, ila ametupa roho ya uwezo, na mapenzi, na akili kamili.

I Hapo huyo Bishopu mkuu humpa Biblia mkononi
mtwake, akinena,

JITAHIDI sana kwa kusoma na kuonya, na kufunza ; ukifikiri sana mambo haya yaliyomo ndani ya chuo hiki. Uwe na bidii sana katika mambo haya, ili kwamba maongeo yako yapatikanayo kwa bidii yako katika mambo haya, yapate kuonekana na watu wote. Itunze sana nafsi yako, na hayo mafunzo pia yatunze sana, uwe na bidii kwa kuyatenda, kwa kuwa ukifanya hivi uteakoa nafsi yako na hao wakusikiao pia utawaokoa. Uwe mchunga wa kundi la Kristo, usiwe mbwa-mwitu ; uwalishe, usiware. Washikilie wanyonge, wapoze wagonjwa, funga-funga kilichovunjika, warejeze hao waliotupwa nje, watafute walipotea. Uwe na rehema kwa kiasi usiachilie mno ; uwe mwenye kurudi kwa kiasi usisahau rehema ; ili Mchunga mkuu atakapotokea upate kupokea taji ya utukufu isiyonyauka milele, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

I Yakiisha kufanywa hayo, Bishopu mkuu huendelea katika taratibu ya Ushirika Mtakatifu, na huyo bishopu aliyezewekwa kwa kazi takatifu siku hiyo (pamoja na wengine) hushiriki pamoja naye.

I Na badala ya sala ya mwisho, mbele ya kuwabarikia watu, husomwa sala hizi zifuatanzo hapa ;

EWE Baba, mwangi wa rehema, twakuomba sana, Eumletee mtumwa wako huyu baraka yako ya mbinguni ; umtie Roho wako Mtakatifu, hata awapo kuhu-

biri Neno lako, awe na bidii kukemea, na kusihi-sihi, na kukanya, kwa subira yote na mafunzo yote ; na pamoja na hayo awe kielelezo chenye manufaa kwa hao waaminio, katika neno, katika mazungumzo, katika mapenzi, katika imani, katika kujizua, na katika usafi ; ili kwamba, huku akitimiza maisha yake kwa uaminifu, siku ya mwisho apate kupokea taji ya haki aliywewekewa na Bwana, Mwamu ni mwenye haki, ambaye yuaishi na kutawala Mungu mmoja pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, milele. *Amina.*

UTUONGOZE, ewe Bwana, katika vitendo vyetu vyote kwa fadhili ya neema yako, utupeleke mbele mumo kwa msaada wako daima ; ili kwa kazi zetu kuanzilizwa na kufulizwa na kutimilizwa ndani yako wewe, tulitukuze jina lako takatifu, na mwishowe tuyapate kwa rehema yako maisha ya milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

AMANI ya Mungu ipitayo *fahamu* zilizo zote, na iwalinde mioyo yenu na nia zenu katika kumjua na kumpenda Mungu, na Bwana wetu Yesu Kristo Mwanawe. Na baraka ya Mungu, Mweza-wa-yote, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, iwe mwenu ikae kwenu daima. *Amina.*

SHARTI THELATHINI NA KENDA ZA DINI

1. Ya imani iliyo katika Utatu Mtakatifu

MUNGU wa kweli aliye hai ni yeye mmoja tu, hana mwanzo hana mwisho, hana mwili, wala viungo, wala nia ya kubadili ; yuna uwemo na hekima na wema vilivyopita mpaka ; Ni Muumba wa vyote, ni Mlinzi wa vyote, vionekanavyo na visivyoonekana pia. Tena katika umoja wa hiyo asili ya Uungu mna Nafsi tatu ; nazo ziliyyokaa katika hali yake ya kuwa na kuweza na kuwako milele ni vivile : ni Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.

2. Ya Neno, naye ni Mwana wa Mungu, aliyefanywa Mtu kamili

MWANA, naye ndiye Neno la Baba, amezaliwa na Baba tokea milele, ni Mungu wa kweli, hana mwanzo hana mwisho, tabia yake ya asili na hiyo ya Baba ni ya namna moja : yeye alijivika asili ya mtu katika tumbo la mwanamwali aliyebarikiwa, katika tabia yake ; ikawa kuungamana asili mbili, ya Uungu na ya Utu, katika umoja wa nafsi, zisigawanyikane tena : na katika hiso mna Kristo mmoja ; ni Mungu wa kweli, tena ni Mtu wa kweli : naye aliteswa kweli, akasalibiwa, akafa, akazikwa ; ili apate kurutudishia Babaye, na kuwa dhabihu, wala si kwa kuondoa dhambi ya asili tu, ila kwa makosa yote ya watu ya katika vitendo.

3. Ya alivyoshuka Kristo kwenda ahera

MFANO wa vile alivyokufa Kristo kwa ajili yetu na kuzikwa, vivyo na iaminiwe kuwa alishuka kwenda ahera.

4. Ya alivyofufuka Kristo

KRISTO alifufuka kwa kweli katika ufu, akautwaa tena mwili wake, una nyama na misupa na vipasavyo ukamilifu wa asili ya mtu, vyote ; akapaa navyo mbinguni ;

yuko sasa amekaa hata atakaporudi aamue watu wote siku ya mwisho.

5. Ya Raho Mtakatifu

ROHO Mtakatifu, atokaye katika Baba na Mwana, Ryuna asili na enzi na utukufu vimoja na Baba na Mwana : naye ni Mungu wa kweli hana mwanzo hana mwisho.

6. Ya Maandiko matakatifu, ya kuwa yatosha kumwokoa mitu

KATIKA Maandiko matakatifu kila neno lipasalo wokofu li mumo : basi kwa ajili hii haifai kumkaza mtu aamini yawayo yote kama ni kiungo cha imani mambo yasiyosomeka humo, au yasiyoweza kuhakikishwa kwayo ; wala kwamba yadhaniwe kupasa katika wokofu. Vyuo tusemayyo vi katika hesabu ya Maandiko matakatifu ni hivyo vya Agano la Kale na Agano Jipya vilivyo katika mizani, visiviyoshindaniwa tangu hapo siku zote hukumu yake katika kanisa.

Vyuo vya Maandiko matakatifu ya mizani vilivyo katika Agano la Kale :—

Genesis, au Mwanzo.
Exodus, au Kutoka.
Leviticus, au Ya Walawi.
Numbers, au Hesabu.
Deuteronomy, au Marcjezo.

Yoshua.
Waamuzi.
Ruthu.

Chuo cha kwanza cha Samweli.
Chuo cha pili cha Samweli.
Chuo cha kwanza cha Wafalme.
Chuo cha pili cha Wafalme.
Chuo cha kwanza cha Mambo ya Nyakati, au cha Tarehe.
Chuo cha pili cha Mambo ya Nyakati, au cha Tarehe.
Chuo cha Ezra, au Chuo cha kwanza cha Ezdrasi.

Chuo cha Nehemia, au Chuo cha pili cha Ezdrasi.
Chuo cha Esteri.
Chuo cha Ayubu.
Zaburi.

Mifano ya Maneno, au Mithali.
Kohelethu, au Mhubiri mkuu.
Wimbo wa nyimbo, au Wimbo wa Suleimani.
Manabii wanne wakuu.
Manabii kumi na wawili wadogo.

Na vyuo vilivybaki, kama asemavyo Hieronumo, husoma kanisa vipate kuwa mfano wa maisha, kwa kufunza adabu, wala halivileti katika kuhakikisha mambo ya imani ; navyo ni hivi :—

Chuo cha kwanza (au cha tatu) cha Ezdrasi.
Chuo cha pili (au cha nne) cha Ezdrasi.
Chuo cha Tobiti.
Chuo cha Yudithi.
Usalizi wa chuo cha Esteri.
Chuo cha Hekima ya Suleimani.
Chuo cha Yesu wa Siraki, au Ecclesiasticus.
Nabii Baruki.
Wimbo wa Watoto watakatifu watatu.
Hadithi ya Susanna.
Habari ya Beli na Joka.
Sala ya Manase.
Chuo cha kwanza cha Wamakabi.
Chuo cha pili cha Wamakabi.

Vyuo vyote vya Agano Jipya, tumevikubali kama vilivykubaliwa na watu, twavihesabu ni vya mizani.

7. Ya Agano la Kale

AGANO la Kale halipingi Agano Jipya, kwani humo katika Agano la Kale vivile kama katika Agano Jipya wanadamu huonywa maisha ya milele kwa Kristo, ambaye ni mpatanishi pekee kati ya Mungu na watu ; ambaye ni Mungu, tena ni Mtu. Kwa ajili hii hawana haki hao wapuzi wasemao kwamba ahadi walizokuwa wakitumaini watu wa kale hazina maisha. Ijapokuwa sheria waliyo-

pewa na Mungu kwa Musa haifungi watu Wakristo katika mambo ya ada na ibada, wala maagizo yaliyomo ya katika mambo ya serikali haikupasa kushika watu wa serikali yoyote kama ambayo hayana budi : pamoja na haya, ni kweli, hapana mmoja Mkristo, awaye yote, aliyeachwa asizishike amri ziitwazo za adabu.

8. *Kukiri kutatu*

MAKUBALIO matatu, ya Nikea, na ya Athanasio, na hayo yaitwayo ya mitume, imepasa kuyashika kabisa na kuyaamini ; kwani yaweza kuonywa kuwa ni kweli kwa ushuhuda mwingu ulio imara sana katika Maandiko matakatifu.

9. *Ya dhambi ya asili, au dhambi mtu azaliwayo nayo*

DHAMBI ya asili haikukaa katika kumwigiza Adamu (kama wapuzavyo wafuasi wa Pelagio) ; ni kilema na uharibifu vya tabia ya kila mtu azaliwaye katika kizazi cha Adamu ; ndipo ikawa kwa ajili ya haya yeye kuwa mbali sana na hali ya kwanza ya haki, akawa mwenye kupendelea uovu kwa tabia yake, ikawa hivi mwili siku zote kupingamana na roho ; nayo ndiyo sababu ya kustahili hasira ya Mungu wazaliwao duniani kila mmojawapo. Na uharibifu huu wa tabia ukalimo hata katika waliozaliwa upya, ikawa hazifati sheria ya Mungu tamaa za mwili, (au Kiyunani, *phronema sarkos*, itafsiriwayo na wengine kuwa "hekima ya mwili," na wengine, "kusikia katika mwili," na wengine, "kupatikana na mambo" ndani yake, na wengine, "kuutunza"). Tena, ijapokuwa hao walioamini na kuzaliwa mara ya pili hawamo tena hao kwa ajili ya Kristo katika hali ipasayo hukumu, pamoja na haya, mitume yuaungama kuwa asili ya dhambi mnayo katika kule kutamani.

10. *Ya mapenzi ya mtu, au nia aliyo nayo katika mambo*

JINSI ilivyokaa hali ya mtu baada ya kuanguka kwa Adamu, hawesi mtu kujirejeza wala kujitengeza kwa zile nguvu zake alizo nazoz za asili, na vitendo vya wema,

akamwamini Mungu na kumlingana. Kwa ajili ya hayo hatuna sisi nguvu zozote za kufanya kazi za haki zitaka-zompendeza Mungu na kukubaliwa kwake, ila tujaliwe kwanza msaada wa neema ya Mungu iliyo katika Kristo, tupate kupenda kuzifanya, ikatufanya kazi ile neema pamoja nasi, tukiisha kupata kule kupenda.

11. *Ya mtu apewavyo haki*

SISI huhesabiwa kuwa na haki mbele za Mungu kwa Swema uliokubaliwa wa Bwana wetu Mwokozi wetu Yesu Kristo tu, tukimwamini ; wala si kwa sababu ya vitendo vyetu au wema wetu : kwa ajili hii, sisi kuhesabiwa kuwa na haki kwa imani tu, ni mafunzo ya afya sana hayo, yamtaza mtu moyo, kama ielezavyo kwa urefu zaidi Hotuba ya Mtu Apewavyo Haki.

12. *Ya vitendo vyema*

VITENDO vyema ni matunda ya imani, hufuata nyuma, watu wakiisha kupewa haki ; navyo ijapo-kuwa haviwezi kuondoaa dhambi zetu, wala kuuhimili ukali wa maamuzi ya Mungu ; pamoja na haya vyapendekeza kwa Mungu na kukubaliwa kwake katika Kristo, navyo vyatokana na imani ya kweli iliyo hai kama havina budi. Na jinsi ilivyokaa imani ya kweli yajulikana kwa vitendo vyake vivile kama mfano wa mti ujulikanavyo kwa matunda yake.

13. *Ya hayo aliyyoyatenda mtu kabla hajapewa haki*

VITENDO vifanywavyo na mtu asijapewa neema ya Kristo na kuvuviwa na Roho wake, kwa kuwa havikutoka katika kumwamini Yesu Kristo, havipendekezi kwa Mungu kamwe, wala havikustahili na neema kwa kuwa hali ya kupasa, kama wasemavyo wengine ; lakini afadhalii vi katika hesabu ya madhambi, hatuna shaka ; kwa kuwa havikutendwa kama Mungu aliviyotaka akaagiza kwamba vifanywe.

**14. Ya vitendo vya zaidi, au vitakavyomzidisha
mtu wema zaidi ya huo aliopaswa**

VITENDO hivyo waviitavyo ni vya zaidi havifunziki pasipo kujikinai na kumtukana Mungu, kwani kwa vitendo hivyo watu hujifanya kuwa wamrudishiao Mungu hayo yaliyowapasa ; wala si hayo tu, wamekuwa wamfanyao kwa ajili yake zaidi ya aliyowahitaja ; ingawa ase-mayo Kristo ni haya, ya wazi : " Mtakapokwisha kufanya mliyogizwa yote, semeni, Tu watumwa sisi tusiofaa."

15. Hapana asiye dhambi isipokuwa Kristo pekee

KRISTO alifafanishwa nasi kweli-kweli katika asili yetu kwa mambo yote, isipokuwa dhambi tu, nayo ndiyo aliyokosa kabisa, huko katika mwili wake, na huko katika roho yake. Alikuja awe mfano wa kondoo asiye kipaku, ili ayaondoe makosa ya ulimwengu, kwa vile alivyofanywa sadaka mara moja tu ; wala dhambi haikuwa ndani yake, kama alivyosema mtakatifu Yohana. Lakini sisi wengine, ingawa tumebatizwa na kuzaliwa mara ya pili katika Kristo, twachukiza sote kwa mambo mengi. Na tutakaposema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenye, wala hamna kweli ndani yetu.

16. Ya dhambi baada ya kubatizwa

KILA dhambi ipasayo kufa afanyayo mtu kwa kupenda kwake baada ya kubatizwa siyo dhambi juu ya Roho Mtakatifu isiyosameheka. Kwa ajili hii, basi, na wasikanywe pahali pa kutubu hao walioteleza katika dhambi baada ya kubatizwa. Baada ya kumpokea Roho Mtakatifu twaweza kugeuka katika neerna tuliyopewa na kupatikana na dhambi, kisha huenda tukainuka tena kwa neema ya Mungu, tukarejea hali nzuri. Basi kwa sababu hii na wasikubaliwe wasemao kwamba wao hawawezи kufanya dhambi tena waishipo duniani, wala wawanyimao pahali pa kutubu waliorejea kwa kweli.

**17. Ya walivyoazimiwa mwanzo watu hali yao na
Mwenyezi Mungu, na kuchaguliwa naye**

KUAZIMIWA mwanzo maisha ni vile Mungu alivyo-wakusudia watu hali zao milele, alipoamuru daima tokea usijatiwa msingi ulimwengu, kwa shauri lake tulilogichwa, ya kwamba atawaoko na laana na uangamivu hao aliowichugua ndani ya Kristo katika kizazi cha wanadamu, kisha kwa Kristo awafikilize katika wokofu wa milele, kama mitungi iliyofinangwa iwe kwa utumishi wa heshima. Na haya yaonya watu hao waliokirimiwa na Mungu kipawa kitukufu hicho, kuwa wameitwa na yeze kama vile alivyo-kusudia, kwa Roho wake ndani yao kwa wakati uliochaguliwa ; tena watu hao huufuata mwito wao kwa neema wapewayo, wakapewa haki bure, tena wamechaguliwa na Mungu kuwa wanawe, wamefanywa mfano wa Yesu Kristo vivile, Mwana pekee wa Mungu, nao kuwa na mwendo wao mtakatifu katika vitendo vyema, kisha, kwa rehema za Mungu hufikilia katika raha isiyokoma.

Kuazimiwa mwanzo na kuchaguliwa katika Kristo, mambo haya wayawazapo kwa kumnyenyekaa Mungu hao wamchao, hujaa utulivu uwatuzao watu moyo na kuwafurahisha kwa namna isiyosemeka hao wamsikiao Roho wa Kristo atendavyo kazi zake ndani yao, akua vitendo vya mwili, ambao ni via vyao ambavyo vikaliko juu ya nchi, akiwavuta nia zao akizipeleka katika mambo ya juu mbinguni. Na sababu ya kufanya hivi, si hii tu ya kuwa yatuthibitisha sana sana na kutuweka imara katika kujiamini kwamba tu watu wa kupata wokofu wa milele kwa Kristo, ila zaidi ni hii, ya kuwa yatuwashia mapenzi ndani yetu tukampenda Mungu. Ni kama hivyo kwa wenze fadhaa na tamaa za mwili wasiokuwa na Roho Mtakatifu ndani yao, waonywapo daima watu hao mbele ya macho yao hukumu ya kuazimiwa mwanzo na Mwenyezi Mungu, imekuwa ni maboromoko katili sana, huku Shetani akiwasukumia chini katika kutotumaini, au katika kujipurukusha kwa mwendo wa taka sana, utakao kuwaangamiza vile vile.

Tena zaidi yatupasa kuzikubali ahadi za Mungu kama

vile zilivyowekwa wazi kwetu katika Maandiko matakatifu huku na huku ; na maagizo ya Mungu tuonayo kuwa yamefunuka sana katika Neno la Mungu ndiyo ya kufuatwa katika vitendo vyetu.

18. Ya kupatikana wokofu wa milele kewa jina la Kristo tu

HAO ni watu wa kulaaniwa waliosubutu kusema kwamba kila mtu aweza kuijokoa kwa sheria au madhihabi ayafuatayo, kwamba atakwendelea kuketi nayo akiyashika kwa bidii, akifuata na mwanga wa asili yake. Kwa kuwa Maandiko matakatifu yamefunua kuwa ni kwa jina la Yesu Kristo tu, watakavyookoka watu.

19. Ya kanisa au mkutano

KANISA la Kristo lionekanalo ni kusanyiko la waamini ifu lihubiriwalo Neno safi la Mungu na kusongezewa vyema ndani yake zile sakramenti mfano wa vile alivyoziweka kwanza ye ye Kristo katika mambo yote yahitajiwayo.

Kama yaliyyokengeuka makanisa ya Yerusalemu na Alekisanderia na Antiochia, kanisa la Rumi nalo limekengeuka, vivyo hivyo ; wala si katika vitendo vyao tu na ada zao za ibada, ni katika mambo yapasayo imani nayo.

20. Ya amri liliyo nayo kanisa

KANISA lina haki ya kuweka ada na ibada ; tena lina Amri yatakaposhindaniwa mambo ya imani. Pamoja na haya haliwezi kuagiza neno lolote likalipinga Neno la Mungu, la Maandikoni, wala kutafsiri habari moja katika Maandiko kwa jinsi itakavyoshindana na habari ya pili. Basi kwa sababu hii, kanisa lijapokuwa ni shahidi la vyuo vya Mungu na ulinzi wake, pamoja na haya, kama vile isivyopasa kuusia neno lolote juu ya vyuo hivi, ni kama hivyo haifai kukazwa watu wakaamini neno lolote kama lipasalo wokofu, isipokuwa ni la humu vyuoni.

21. Ya amri ya makutano makuu, au mashaurizano ya jamii ya kanisa

MAKUTANO ya kushaurizana katika kanisa zima hayakutaniki pasipo agizo la maseyidi na kutaka kwao. Nayo wakati yakiisha kukusanyika yaweza kwenda kombo, tena pengine yamekwisha kwenda kombo, hata katika mambo ya Mungu : kwa kuwa makutano haya ni ya watu waisotawaliwa wote na Roho wa Mungu na Neno lake. Basi kwa sababu hii, imekuwa mambo yaliyoagizwa na watu hawa kama yapasayo wokofu, hayana nguvu wala amri, isipokuwa yawezekana kuonywa kuwa yamepatikana katika Maandiko matakatifu.

22. Ya matakasoni

MAFUNDISHO ya Warumi ya matakasoni, na misamaha, na sanamu na visalizi vya wafu kuabudiwa na kuombwa : na waliokufa kale watakatifu kulinganwa ; ni mambo ya upuzi yaliyozuliva bure, yasiyotegemea ushahidi wa Maandikoni wowote, afadhali yapingana na Neno la Mungu.

23. Ya waitwavyo katika utumishi watumikao katika mkutano

SI halali mtu kujitweka kazi ya kuhubiri mbele ya watu sau ya kuwasongezea sakramenti katika mkutano, ikiwa hajaitwa na kutumwa kama vilivyoagizwa kwa kuyafanya haya. Tena hao ndio iliotupasa kuwadhania wameitwa na kutumwa kama iagizavyo sheria, hao wenye kuchaguliwa na kuitwa na watu waliopewa uwezo mbele ya mkutano wa kuwaita watumikao na kuwatuma katika shamba la Bwana.

24. Ya ibada ya msikitini ipasavyo kuwa katika lugha ijulikanayo

KUIENDELEZA ibada ya mkutanoni, au kuzisongeza sakramenti katika maneno yasiyojulikana na watu, yapingana kabisa mambo haya na Neno la Mungu na desturi ya kanisa la asili.

25. Ya sakramenti, au ibada ziitwazo siri

SAKRAMENTI zilizowekwa na Kristo haziwi kama Salama tu za kuwa watu ni Wakristo dini yao, afadhalii huwa ushuhuda wa hakika, tena huwa dalili za neema ya Mwenyezi Mungu zenye kuileta, tena za alivyotuwia radhi ; na kwa hizo mwenyewe hutufanyia kazi yake isiyookeekana, na kututia imani tupate kumwamini akaiweka imara tena.

Siri zilizowekwa na Kristo Bwana wetu katika Injili ni mbili : ni Ubatizo na Karamu ya Bwana.

Zile tano nazo ziitwazo siri, maana, Kutiwa mikono (au Confirmation) ; na Dhambi kumuungamia kasisi akakupa msamaha (au Penance) ; na Apewapo mtu daraja katika utumishi wa kanisa kama la ushemasi au la ukasisi au la ubishopu (au Orders) ; na Nd^{ba} (au Matrimony) ; na Kupakwa mafuta katika saa ya kuwa (au Extreme Unction) ; na zisidhaniwe zile kuwa ni siri za katika Injili, kwa kuwa nyingine zilitokana na kule kutoandama sawasawa mafunzo ya mitume ; na nyinginé ni hali za maisha, zimetajwa kwa wema (ni kweli) katika Maandiko matakatifu, lakini hazina maana ya siri yale yale ya zile za Ubatizo na Karamu ya Bwana, kwa kuwa dalili lionekekano au ada iliyowekwa na Mungu hukosekana katika siri hizo.

Siri hazikuwekwa na Kristo, ili watu wapate kuzikodolea macho na kupita nazo huku na huku ; lakini kwamba tuzitumie mfano wa maana yake. Wala hazina manufaa ya afya, isipokuwa kwa hao wazipokeao kama ilivopasa : na wasiozipokea kama ilivopasa hupatikana wao na hukumu ya nafsi zao, kama asemavyo mtakatifu Paulo.

26. Ya nguvu zilizo katika mambo yaliyowekwa na Kristo, kwa haziondoki kwa ubaya wa wayasongezao

INGAWA katika kanisa lionekekalo wabaya siku zote wamechanganyikana na wema, na pengine utumishi wa Neno la Mungu na mambo yake matakatifu waimeyatawala wale wabaya, pamoja na haya kwa kuwa hawayafanyi mambo hayo kwa jina lao wenyeewe, ni kwa jina la Kristo ;

tena kwa kuwa wafanyakavyo utumishi wao ni kwa agizo lake na amri yake ; twaweza kutumia utumishi wao, ikiwa kwa kusikiza Neno la Mungu, au kwa kupokea sakramenti zake. Tena manufaa ya mambo yaliyowekwa na Kristo hayaondoki kwa ubaya wao, wala neema itokanayo na vipawa nya Mungu, haiwapungukii waliosongezewa sakramenti hizo, wakizipokea kwa imani na maana ; na nguvu zinazo, kwa ajili ya vile zilivyowekwa na Kristo na zile ahadi alizotoa, ijapokuwa zimesongezwa na wabaya.

Na haya yote, yapasa taratibu ya kanisa kwamba yapeleleze mambo ya madhalimu wenyewe daraja, washtakiwe watu hao na waujuao ule udhalimu wao, na mwisho wake, wakiisha kufunuliwa kuwa ni wakosaji, wauzuliwe kwa hukumu ya haki.

27. Ya ubatizo

UBATIZO si dalili tu ya kuwa watu ni Wakristo dini yao, wala si alama ya kutengwa tu, waliyotengewa Wakristo na wasiokuwa Wakristo ; afadhalii ni dalili ya kuzaliwa mara ya pili, wakitiwa kwa hiyo katika kanisa hao walioipokea kama ipasavyo : ahadi za kusamehewa dhambi na kukubaliwa tuwe wana wa Mungu kwa Roho Mtakatifu zapigwa muhuri, kwa wazi ; imani yakazwa na neema yaongezwa kwa nguvu za kumwomba Mungu.

Kubatizwa watoto wachanga ni ada moja iliyopasa sana kushikwa ndani ya kanisa, kwa kuwa ni ada iliyopatana sana na maweko yake Kristo.

28. Ya karamu ya Bwana

KARAMU ya Bwana si dalili tu ya kupasa Wakristo kupendana wao kwa wao lakini afadhalii ni sakramenti ya kukombolewa kwetu kwa mauti ya Kristo ; ni kama hivyo, kwa hao waupokeao kama ipasavyo kwa maana na imani, imekuwa mkate tuvunja ni kupewa fungu la mwili wa Kristo, na kikombe cha kubarikia vivyo hivyo ni kupewa fungu la damu ya Kristo.

Ya kuwa vimegeuka mkate na divai hali ya tabia yake katika karamu ya Bwana haiwezekani kuthibitishwa kamwe

katika Maandiko matakati ; ni vingine, haikupatana na maneno ya Maandikoni ya wazi-wazi, yapindua yale maana ya sakramenti, tena yazuia ibada nyingi zisizofaa.

Mwili wa Kristo hupewa na kupokewa na kutafunwa katika karamu hii kwa maana ya mbinguni ya rohoni tu. Na watu waupokeavyo na kuutafuna mwili wa Kristo katika karamu hii, ni kwa njia ya imani walio nayo.

Na hiyo sakramenti ya karamu ya Bwana haikuagizwa na Kristo kwamba iwekwe pahali, wala chukuchuliwa huko na huko, wala kuinuliwa, wala kuabudiwa.

29. Ya utafumwavyo mwili wa Kristo na wasivyowezwa madhalimu kuutafuna

MADHALIMU, na wasiokuwa na imani ilio hai, Mingawa washindikiza katika sakramenti ya mwili na damu vya Kristo kwa meno yao, kama alivyo sema Augustino, hawapati hivi kuwa na fungu katika Kristo. Lakini afadhalii, ni kwa hukumu yao watafunavyo na kunywa katika siri ya neno kuu kama hilo.

30. Ya aina zote mbili

KIKOMBE cha Bwana na wasikanywe wasio daraja katika kanisa, kwani imepasa kusongezewa Wakristo wote vipande vyote viwili vya sakramenti ya Bwana, hiki na hiki, mfano wa vile Kristo alivyoianziliza siri hii na kuusia.

31. Ya matoleo ya pekee ya Kristo yaliyotimizwa na yeeye juu ya msalaba

KWA vile alivytotlewa Kristo mara moja hupatikana Mwenyezi Mungu, na kutimiziwa wahitajiavyo, huku wakiondolewa makosa yao yote, yakiwa ya asili yakiwa ya katika vitendo ; wala dhambi haziondoki kwa matoleo mengine yoyote, isipokuwa kwa haya tu. Basi kwa ajili hii imekuwa ni hadithi zenye kumtukana Mungu, ni madanganyifu yenye hatari, hizo sadaka zao za katika

Mass, ziambiwazo na wengi kwamba kasisi humsongeza Kristo humo, ikawa sadaka kwa kuachiwa walio hai na waliokufa, ikiwa dhambi zao ikiwa adhabu zao.

32. Ya makasisi kwamba waweza kuoa

MABISHOPU wala makasisi wala mashemasi hawa-kuusiwa na amri yoyote ya Mungu, kuweka nadhiri kwamba hawataaoa, wala kujiepua na ndoa. Kwa ajili hii, waweza watu hao kuoa vile vile kama Wakristo wenziwao wote kwa nia yao, waonapo kwamba itazidi kufaa katika uchajii-wa-Mungu.

33. Ya ipasavyo kuwaepuka waliotengwa

MTU aliyetengwa kwa haki katika umoja wa kanisa, kwa mambo yake kuonywa na kanisa wenyewe mbele ya watu kuwa ni dhaifu, akatupwa nje ; na adhan-iwe mtu huyo na jamii ya waaminifu kuwa ni Pagano (au Kafiri), hata aishe kupatanishwa na kanisa mbele ya watu kwa kutenda toba, kwa amri ya mwamuzi afaaye humo.

34. Ya mausio ya kanisani yaliyopokewa kale

MAUSIO ya kanisani yaliyopokewa kale, na ada, havina haja ya kuwa vimoja wala ya kufanana kabisa mwahali mote, kwani siku zote vilikuwa mbali-mbali : vyaweza kugeuzwa, mfano wa tofauti za nchi na zamani na desturi, ikiwa haliwekwi jambo juu ya Neno la Mungu.

Atakayevunja mausio na ada vya kanisani kwa kufuata akili zake mwenyewe, kwa kujua na kukusudia, yakiwa ni katika maneno yasiyopingana na Neno la Mungu, yame-wekwa na kukubaliwa kwa amri ya watu wote : amekuwa huyu ni mtu wa kurudiwa mbele ya watu, ili wengine wapate kuogopa, wasije wao wakafanya kama yale, kwani ni mtu aliyekosa juu ya taratibu ya kanisa, na kuidhoofisha amri ya aliyetawazwa, tena amewaumiza nia zao ndugu wanyonge.

Kila kanisa lililo mbali na mengine au lililo katika kabilalau watu, lina uwezo wa kuweka na kugeuza na kutangua mausio au ada za kanisani, zilizowekwa kwa amri ya watu, yawapo kuteendeke yote kwa kufaa.

35. Ya hotuba

JUZU ya pili ya hotuba tuliyoweka dibaji za mafungu yake kila moja mwisho wa sharti hii, ina mafundisho ya uchaji-wa-Mungu yenyeye afya, yaliyohitajiwa sana zamani hizi, mfano vilevile wa ile juzu ya kwanza ya hotuba iliyo tangazwa zamani za Edward wa sita; ndipo nasi twaamuru zisomwe hotuba hizi katika misikiti na watumikao, kwa bidii na sauti iliyopazwa, wapate kuelewa watu na maana yake.

Ya majina ya hotuba

1. Ya kuutumia msikiti kama ilivyopasa.
2. Ionyayo hatari ya kuabudu sanamu.
3. Ya misikiti, ipasavyo kuifanyiza upya na kuiweka safi.
4. Ya vitendo vyema : hasa ya kufunga.
5. Ikatazayo ulafi na ulevi.
6. Ikanyayo umaridadi mwinci wa mavao.
7. Ya kuomba.
8. Ya pahali paombwapo, na majira yapasayo kuomba.
9. Ya kwamba yahitajia kutumia maneno ya siku zote, yajulikanayo na watu, katika kushukuru misikitini na kusongeza sakramenti.
10. Ya ipasavyo kusomwa Neno la Mungu kwa kulihehimu.
11. Ya kuwapa maskini sadaka.
12. Ya kuzaliwa kwake Kristo.
13. Ya kuumizwa kwake Kristo.
14. Ya kufufuka kwake Kristo.
15. Ya ipasavyo watu kupokea sakramenti ya mwili na damu vya Kristo.
16. Ya vipawa vya Raho Mtakatifu.
17. Ya katika siku za kuuliza.
18. Ya hali ya ndoa.
19. Ya toba.
20. Ikanyayo uvivu.
21. Ikanyayo ukaidi na fitina.

36. Ya kuwarveka kwa Mungu mabishopu na watumikao

CHUO cha wawekwavyo mabishopu wakuu na mabishopu, na wapewavyo madaraja yao makasisi na mashemasi, kilichotangazwa juzi-juzi zamani za Edward wa sita, kikawekwa imara kwa hukumu ya Baraza kuu ya shauri, (Parliament) zamani zizo hizo, kina mambo yote ndani yake chuo hicho yaliyopasa wawekwavyo watu hao na kupewa madaraja : wala hamna neno kabisa ambalo kwa nafsi yake ni la upuzi katika dini, au la kumwasi Mungu. Basi kwa ajili hii, watu waliowekwa kwa Mungu au kutiwa daraja kwa mfano wa ada zilizo katika chuo hicho, tangu mwaka wa pili wa yule mathukuri Edward wa sita hata zamani hizi, au watakaowekwa kwa Mungu na kutiwa daraja zamani za mbeleni mfano wa ada hizo, twaamuru watu hao kuwa wamebekwa kwa Mungu na kutiwa daraja kila mmoja kwa haki, na taratibu, na sheria, wawao wote.

37. Ya waliotawazwa mambo ya serkali

M FALME wetu aliyetukuka yuna uwezo ulio bora katika huu ufalme wa Uingereza, na katika nchi zake nyiningine alizozitawala, naye ndiye aliye na amri ya kukata juu ya madaraja yote ya watu katika ufalme huu, yakiwa ya kanisani, au ya serkalini, katika mambo yote ; na hiyo amri yake hai chini ya amri yoyote ya ugenini, wala haikupasa kuwa chini yake.

Nasi tujapoisifu enzi ya Mfalme kuwa ni amri iliyo kuu, nayo ni heshima tufahamuyo kuwa imewachukiza nia zao wengine wenye fitina ; pamoja na haya hatuwapi maseyidi wetu kazi ya utumishi wa Neno la Mungu wala ya siri zilizowekwa na Kristo ; nalo ni jambo lililosuhudiwa wazi-wazi sana hilo na maonyo yaliyotangazwa juzi-juzi na Mfalme wetu Elizabethi : tuwapayo ni hiyo haki yao tu, tuiionayo kuwa maseyidi wote waandamao uchaji-wa-Mungu wamepewa siku zote na Mungu katika Maandiko yake matakatifu, ya kuwa wao ndio wenye kutawala madaraja yote na tofauti za watu walizoamaniwa na Mwenyezi

Mungu, ikiwa za kanisani ikiwa za serkalini, na kuzua wakaidi na wafanyakaji-wa-uvu kwa upanga wa serkali.

Bishopu wa Rumi hana amri kamwe katika ufalme huu wa Uingereza.

Sheria ya ufalme yaweza kuwaadhibu Wakristo kwa mauti kwa makosa mazito yapasayo kuuawa.

Wakristo waamriwapo na aliyetawazwa waweza kuchukua silaha na kwenda vitani.

38. Ya mali za Wakristo, kuwa haziwi shirika kwa watu wote

MALI za Wakristo ni vitu vyao, wala isikubaliwe watu wote kuwa na haki navyo wawe wenye navyo (navyo ndivyo wapuzavyo watu kadhwakadha kwa kinai na uwongo katika hao Wabatizao watu mara ya pili, maana, *Anabaptists*). Pamoja na haya, imempasa kila mtu kuwapa maskini sadaka mfano wa uwezo wake.

39. Ya kiapo cha Mkristo

KAMA vile tuungamavyo kwamba kuapa kwa uwongo na upuzi wamekatazwa Wakristo na Bwana wetu Yesu Kristo, na mtume wake Yakobo, twaamua vilevile kwamba dini ya Ukristo haimkatazi mtu kwamba asiape atakapotakwa na aliyetawazwa, katika habari ya imani na mapenzi, ikiwa yatendwa mambo haya kama tulivyo-fundishwa na nabii, kwa haki, na hukumu, na kweli.

TARATIBU YA KUONYESHA UZAZI,

AMBAO KATIKA MAANDIKO MATAKATIFU NA SHERIA ZA NCHI WAMEKATAZWA WASIOANE

<i>Mtu mume hana ruhusa ya kumwoa</i>	<i>Mwanamke hana ruhusa ya kuolewa na</i>
1. Nyanyaye.	1. Babuye.
2. Mke wa babuye.	2. Mume wa nyanyaye.
3. Nyanyaye mkewe.	3. Babu wa mumewe.
4. Shangaziye.	4. Ndugu wa babaye.
5. Nduguye mamaye.	5. Nduguye mamaye.
6. Mke wa ndugu wa babaye.	6. Mume wa shangaziye.
7. Mke wa ndugu wa mamaye.	7. Mume wa ndugu wa mamaye.
8. Ndugu wa baba wa mkewe.	8. Ndugu wa baba wa mumewe.
9. Ndugu wa mama wa mkewe.	9. Ndugu wa mama wa mumewe.
10. Mamaye.	10. Babaye.
11. Mama wa kambo.	11. Baba wa kambo.
12. Mama wa mkewe.	12. Baba wa mumewe.
13. Binti wake.	13. Mwanawewe.
14. Binti wa mkewe.	14. Mwana wa mumewe.
15. Mke wa mwanawewe.	15. Mume wa binti wake.
16. Nduguye mke.	16. Nduguye mume.
17. Nduguye mkewe.	17. Nduguye mumewe.
18. Mke wa nduguye.	18. Mume wa nduguye.
19. Binti wa mwanawewe.	19. Mwana wa mwanawewe.
20. Binti wa binti wake.	20. Mwana wa binti wake.
21. Mkewe mwana wa mwanawewe.	21. Mumewe binti wa mwanawewe.
22. Mkewe mwana wa binti wake.	22. Mumewe binti wa binti wake.
23. Binti wa mwana wa mkewe.	23. Mwanawewe mwana wa mumewe.
24. Binti wa binti wa mkewe.	24. Mwanawewe binti wa mumewe.

- | | |
|---|---|
| <i>Mtu mume hana ruhusa
ya kumwoa</i> | <i>Mwanamke hana ruhusa
ya kuolewa na</i> |
| 25. Binti wa nduguye. | 25. Mwana wa nduguye. |
| 26. Binti wa nduguye mke. | 26. Mwana wa nduguye
mume. |
| 27. Mkewe mwana wa
nduguye. | 27. Mumewe binti wa
nduguye. |
| 28. Mkewe mwana wa
nduguye mke. | 28. Mumewe binti wa
nduguye mume. |
| 29. Binti wa ndugu mume
wa mkewe. | 29. Mwana wa ndugu wa
mumewe. |
| 30. Binti wa ndugu mke wa
mkewe. | 30. Mwanawe ndugu mke wa
mumewe. |

SUPPLEMENT

TARATIBU IWEZAYO KUTUMIWA KWA KUZIKA MTOTO

¶ Padre na waimbaji humwenda yule maiti na kukutana naye langoni pa uwanda wa mazishi, humtangulia, kwamba ni kuingia msikitini, kwamba ni kwenda upande wa kaburi lake, nuku wanena (au kuimba) :

YESU akamwambia, Mimi ndimi huko kufufuliwa, nami ndimi maisha. Aaminiye kwangu ajapokuwa amekufa, ataishi. Na kila mtu aishiye na kuamini kwangu, hafi milele. *Yohana 11. 25-26.*

MIMI najua ya kuwa Mkombozi wangu yu hai, na mwisho atasimama juu ya nchi : hata ngovi yangu itakapokwisha kuharibika hivi, pasipokuwa na mwili wangu nitamwona Mwenyezi Mungu : naye nitamwona nafsi yangu, tena macho yangu yatamwangalia, wala si kana mgeni. *Ayubu 19. 25-27.*

KWANI hatukuingia na kitu ndani ya ulimwengu, kwa kuwa hata kutoka na kitu hatuwezi. *I Timotheo 6. 7.*

YEHOVA alitoa, na Yehova ametwaa ; jina la Yehova na libarikiwe. *Ayubu 1. 21.*

ATALILISHA kundi lake kama mchunga alishavyo, awana-wa-kondoo atawaambata mikononi mwake, naye atawachukua kifuani mwake. *Isaya 40. 11.*

ZABURI 23

YEHOVA ni mchunga wangu : sitapungukiwa na kitu.

2. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza : kando ya maji ya utulivu huniongoza.
3. Hunihuisa nafsi yangu na kuniongoza : katika mapito ya haki kwa ajili ya jina lake.

4. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya : kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyaniifariji.

5. Waandaa meza mbele yangu machoni pa watesi wangu : umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe changu kinafurika.

6. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu : nami nitakaa nyumbani mwa Yehova muda wa siku nyingi.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ *Ndipo hufuata somo hili :*

Mariko 10. 13-16

IKAWA watu kumpelekea watoto apate kuwagusa ; Iwale wanafunzi wakiwakemea waliowaleta. Yesu akiona yale yakamchukiza, akawaambia, Waacheni watoto wani-jilie, siwakanyeni : kwani usfalme wa Mwenyezi Mungu ni wa kama hawa. Ni kweli nawaambia, asiyeupokea usfalme wa Mwenyezi Mungu kama vile mtoto, haingii ndani yake kamwe, awaye yote. Kisha akawachukua mikononi mwake, ikawa kuwabarikia, huku akiwawekeea mikono.

¶ *Hata wakifika kaburini, wakati wa kumtengeneza yule maiti ili kumlaza ndani ya nchi, yule Padre hunena maneno haya, au yule Padre na wale waimbaji huyaimba :*

BINADAMU aliyezawa na mwanamke siku zake atakazoishi ni haba, nazo zilizooja taabu. Yeye hutepuza kama vile ua, kisha hukatwa : hukimbia kama kivuli kikimbiavyo, wala hasimami.

¶ *Ndipo hapo muda ule mwili ukitupiwa mchanga juu yake na wengine waliosimama kando, yule Padre hunena,*

KWA maana ya hivyo alivyopendezewa Mwenyezi Mungu na kuitwaa roho yake huyu mtoto mpenzi aliyefariki, sisi kwa ajili ya neno hili, twauweka mwili

wake katika nchi : kilicho mchanga kirejee mchanga, kilicho ivu kirejee ivu, kilicho uvumbi kirejee uvumbi, kwa tumaini lililo yakini na imara la kufufuliwani kwa maisha ya milele, kwa Bwana wetu Yesu Kristo, ataka-yeugeuza mwili huu wa unyonge wetu uwe mfano mmoja na mwili wa utukufu wake, kwa kadiri ya kutenda kwake yeje awezavyo hata kuvitweza vitu vyote chini yake.

¶ *Kisha husomwa au huimbwa,*

HAWATAONA njaa baadaye, wala hawatakuwa na kiu baadaye ; halitawafikilia jua, wala hari'iliyo yote : kwa kuwa huyo Mwana-wa-kondoo, yeje aliye katikati ya hicho kiticha-enzi, atakuwa mchunga wao, naye atawaongoza hata wafikilie penye macho-ya-maji ya uhai : na Mwenyezi Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.

¶ *Ndipo Padre aseme haya :*

KWA Mfalme ambaye ni wa milele, asiyetoweka, wala Kasiyeonekana, ni Mungu mwenye hekima pwekee, ni vyake heshima na utukufu milele na milele. *Amina.*

¶ *Ndipo Padre aseme,*

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje, Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliyoywasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribwi ; Utuokoe maovuni. *Amina.*

Na tuombe.

EWE Bwana Yesu Kristo, uliyechukua watoto wadogo mikononi mwako na kuwabarikia : twakuomba ufunue macho yetu, ili tuone kwamba ni kwa wema wako

uliviyomchukua mtoto wako huyu katika mikono ya milele ya mapenzi yako yasiyokoma ; uishiye na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja, milele na milele. *Amina.*

EWE Mungu, njia zako hufichwa, kazi zako ni za ajabu sana, huumbi kitu bure, kisha wapenda vyote ulivyoumba : uwafariji watumishi wako, ambao mioyo yao ina uchungu sana na kulemewa ; uwajalie kwa jinsi watakyokupenda na kukutumikia katika maisha haya, wao pamoja na mtoto wako huyu wapate utimilifu wa ahadi zako katika ulimwengu ujao ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

Ndipo yasemwe haya,

z Wakorintho 13. 14

NEEMA ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi ya Mwenyezi Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, viwe pamoja nasi sote milele. *Amina.*

TARATIBU YA KUWATIA WASIKIZI KATIKI KUNDI LA WATAFITI

¶ *Yapasa taratibu hii itumiwe kwa ajili ya watu waliosundishwa hata twaweza kufahamu sana maana ya haya wafanyayo, isitumiwe kwa wengine.*

Yafaa taratibu hii itumiwe pamoja na Sala ya Asubuhi au Sala ya Jioni, au peke yake. Nyimbo ziimbwe kama Padre aonavyo vyema.

¶ *Watu wa mkutano wakiisha kuketi, hao watakaokubaliwa wasimame, naye Padre asimame mbele yao, na kunena maneno haya :—*

ENYI ndugu wapenzi, tumekutanika hapa mbele za Mwenyezi Mungu na mkutano huu, tuwakubali mwingle katika kundi la watafiti. Twamshukuru Mwenyezi Mungu ya kwamba amewapa mioyo kumtafuta, nasi, ili tuwakuze mioyo katika haya mfanyakayo, twawaambia kwa nguvu za Neno la Mungu ya kwamba wote wamtatuo kwa bidii na uaminifu hapana budi watamwona.

Katika Injili ya Yohana, mlango wa sita, kifungu cha thelathini na saba, tuna maneno ya Bwana Yesu Kristo mwenyeewe : asema, Ajaye kwangu simtu pi nje kamwe. Nasi tuna ahadi yake katika Injili ya Luka, mlango wa kumi na mmoja, vifungu vya kenda na kumi ; Ombeni, mtapewa ; tafuteni, mtaona ; bisheni, mtafunguliwa. Kwani kila aombaye hupewa, na atafutaye huona, na abishaye hufunguliwa.

Sisi, tuliokwisha kumtafuta, kwa necma yake tume-mwona, nasi twaweza kushuhudia ya kwamba ye ye ni Mungu wa mapenzi na huruma, hataki mwenye dhambi afe, ataka auache uovu wake awe hai.

Basi, wote wapendao kuingia kundi la watafiti yapasa waseme mbele ya watu ya kwamba wataka kufundishwa habari njema za Yesu Kristo na kufanya apendayo ye ye, na kujitenga na yote yapingamanayo na mafundisho yake ; tena yawapasa kuahidi mbele za Mungu kufanya

bidi kwenda nyumbani mwa Mungu siku zote ili kumwabudu yeye, tena kwenda kilasi ya watafiti, awafundishwe hayo yawapasayo kujua wapate kuwa wafiasi wake wa kweli. Tena yawapasa sana kukusudia kumwomba kila siku.

Basi kwa ajili ya hayo nakuuliza :—

1. Wewe wataka kufundishwa habari njema za Bwana wetu Yesu Kristo, Mwokozi wa wanadamu, na kufanya apendayo yeye?

Hujibu. Nataka.

2. Utafanya bidii kwenda nyumbani mwa Mungu kila siku, na kilasi ya kujifunza kusoma?

Hujibu. Nitafanya bidii, kwa msaada wa Mungu.

3. Utafanya bidii kujitenga na kila neno lipingamanalo na mafundisho ya Bwana Yesu Kristo, hasa . . . ?

(Hapa zitajwe dhambi kadhwakadha na desturi za nchi ambazo watafiti hujaribiva sana nazo.)

Hujibu. Nitafanya bidii, kwa msaada wa Mungu.

4. Utafanya bidii kumwomba Mwenyezi Mungu kila siku akupe Roho wake Mtakatifu kukusaidia na kufundisha?

Hujibu. Nitafanya bidii, kwa msaada wa Mungu.

¶ *Ndipo Padre amshike mnono kila mmoja atakayekubaliwa, na kunkubali, akitumia maneno haya :*

Fulani, nakukubali uwe mtafiti.

¶ *Ndipo Padre awahubiri hao waliokubaliwa wawe watafiti maneno haya :*

WAPENZI, mmeekwisha kufanya hatua ya kwanza katika njia ipelekayo kwa kanisa la Kristo. Sisi, tulio watumishi wake, twawakaribisha kwa furaha, nasi twataka kuwafundisha zaidi na zaidi ya mapenzi yake na wema wake. Nanyi ni juu yenu kufanya bidii mpare faida ya nafasi hii mliyo rayo.

Kwa ajili ya hayo, nawasihi mfanye bidii sana katika kwenda hizo kilasi mlizotengenezewa mpare kufundishwa mambo makubwa aliyowafanya Mungu, tena mfu-

ndishwe vile Mungu awatakiavyo katika hali yenu. Kumbukeni ya kuwa ameahidi kuwapa nguvu zote mlizo na haja nazo, basi kwa ajili ya hayo tunzeni sana, kama mlivyoahidi, kumwomba yeze kila siku, mkijua ya kwamba hapana budi atawasikiza na kuwabarikia.

Wala msisahau ya kuwa kama yeye alivyowaongoza kutamani kujifunza habari zake, vivyo ataka ya kwamba rafiki zenu na jirani zenu wajifunze habari zake yeye. Basi awataka katika kujifunza kwenu mlele wengine pamoja nanyi mpare nyote kuwa watumishi wake watakatifu.

Basi na tumtukuze sote kwa ajili ya wema wake wa tangu hapo, na kumwomba atimize mwenu kazi aliyoanza kufanya.

Na tuombe.

EWE Baba mwenye rehema, wewe jinsi ulivyoupenda ulimwengu ulimtuma Mwana wako Bwana wetu Yesu Kristo awe Mwokozi wa wote wamwaminio, twakushukuru kwa vile ulivyowaongoza watu hawa kutaka kujifunza habari zako njema. Uwajalie wawe waaminifu katika kutaka kumfuata yeye, na kuacha mambo yamchukizayo. Ewe Baba wa mbinguni, uwakirimu kwamba Roho wako Mtakatifu awaongoze katika njia yako, wapate kuwa wana wako wa kweli, kisha wawe watu waaminifu wa kanisa lako takatifu; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

BWANA na awabarikie na kuwalinda, Bwana na awainulie nuru ya uso wake, na kuwapa armani, sasa na hata milele. *Amina.*

TARATIBU YA KUWAKUBALI WATAFITI WAWE WASOMAJI

¶ Taratibu hii hutumiwa wakati wa Sala ya Asubuhi au Sala ya Jioni, au peke yake. Nyimbo ziimbwe kama Padre atakavyoona vyema.

¶ Hao watakaokubaliwa wakiisha kuwekwa vyema mbele ya watu, watu wa mkutano husimama, nao husoma au kuimba Zaburi hii :—

ZABURI 115

USITUTUKUZE, ewe Yehova, usitutukuze sisi, bali ultukuze jina lako : kwa ajili ya fadhili zako, kwa ajili ya uaminifu wako.

2. Mbona wasema mataifa : Yuko wapi Mungu wao ?
3. Lakini Mungu wetu yuko mbinguni : alitakalo lote amelitenda.

4. Sanamu zaô ni fedha na dhahabu : kazi ya mikono ya wanadamu.

5. Zina vinywa lakini hazisemi : zina macho lakini hazioni ;

6. Zina masikio lakini hazisikii : zina pua lakini hazisikii harufu ;

7. Zina mikono lakini hazishiki kitu, zina miguu lakini haziendi : wala hazitoi sauti kwa koo zao.

8. Wazifanyao watafanana nazo : kila mmoja anayezitumainia.

9. Ewe Israeli, mtumainini Yehova : yeye ni msaada wao na ngao yao.

10. Ewe nyumba ya Haruni, mtumainini Yehova : yeye ni msaada wao na ngao yao.

11. Enyi mmchao Yehova, mtumainini Yehova : yeye ni msaada wao na ngao yao.

12. Yehova ametukumbuka, naye atatubarikia : atabarikia nyumba ya Israeli, ataibarikia nyumba ya Haruni.

13. Atawabarikia wamchao Yehova : wadogo kwa wakubwa.

14. Yehova na azidi kuwaongeza ninyi : ninyi na watoto wenu.

15. Mbarikiwe ninyi na Yehova : aliyezifanya mbingu na nchi.

16. Mbingu ni mbingu za Yehova : bali nchi amewapa wanadamu.

17. Sio wafu wamsifuo Yehova : wala wowote washukao kwenye kimya ;

18. Bali sisi tutahimidi Yehova : tangu leo na hata milele. Aleluya.

Utukufu uwê kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

¶ Kisha watu wa mkutano huketi, na huyo Padre husoma fungu moja au zaidi katika mafungu haya ya Maandiko matakatifu :

i Wafalme 8. 41-43

Isaya 56. 6-9

Mika 4. 2

Vitendo vya Mitume 10. 34-35

Yohana 10. 1-16

¶ Ndipo, watu wote wa mkutano wakiketi vivyo, hao warakao-kubaliwa husimama, naye Padre akisimama mbele yao, husema :

NDUGU zangu wapenzi, sisi tumekutanika hapa mbele za Mwenyezi Mungu na mkutano huu, tuwakubali ninyi muwe wasomaji katika kanisa la Kristo.

Ninyi hapo mbele mlakirii mbele ya watu ya kwamba militaka kufundishwa habari njema ya Bwana wetu Yesu Kristo, aliye Mwokozi wa wanadamu, na kujaribu kufanya ayatakayo yeye. Tena wakati huo mliahidi ya kwamba mtafanya bidii kujitenga na yote yasiyopatana na mafundisho yake, tena mliahidi ya kuwa mtakuja nyumbani uiwa Mungu siku zote zipasazo : tena mliahidi ya kuwa

mtafanya bidii katika kumwomba Mungu kila siku awape Roho wake Mtakatifu, awasaidie na kuwafundisha.

Twatumaini ya kwamba mmekeuwa na bidii katika kutimiza kwa uaminifu ahadi hizo mlizofanya siku hiyo. Na sasa kwa mliviyotaka kukubaliwa kuwa wasomaji, nanyi mmepeata kujuu maana yake dini ya Yesu Kristo zaidi ya mlivyojua siku hiyo, yawapasa zaidi sana kuwa na mwendo unaopatana na ahadi hizo mlizoahidi. Basi sasa nitawataka mseme mbele ya mukutano huu, ya kwamba mtajitahidi kwendelea mbele kwa siku zijazo vilevile kama mlivyoahidi siku hiyo.

Tena twatumaini ya kwamba mmefundishwa na kuelwa sana maana ya maneno haya mtakayosema : yapasa kusema wazi-wazi mbele ya watu, ya kuwa mmeyatubia madhambi yenu, tena ya kwamba mwaamini kwake Bwana Yesu Kristo kuwa ndiye Mwokozi wenu, Mfalme wenu, tena ya kwamba mwakusudia kweli-kweli kumtii yeye kila siku ya maisha yenu.

Tena msisahau ya kwamba yeye Bwana Yesu Kristo anasimama kati yetu hivi leo, kama aliyotuhidia, yuasikiza maneno yenu, yuaelewa yeye na makusudi na mawazo ya miyo yenu, tena yuataka sana kuwapa baraka zake na nguvu zake.

Basi kwa sababu hii nakuuliza :

1. Kwa ulivyoolewa zaidi sasa maana yake hizo ahadi ulizofanya ulipokubaliwa kuwa mtafiti, je, hata sasa wataka kuzitimiza ahadi hizo ?

Hujibu. Ndivyo nitakavyo, kwa msaada wa Mungu.

2. Yeye Bwana Yesu Kristo alikuwa juu ya msalaba kwa ajili yako wewe mwenye dhambi : je, wayatubia madhambi yako kweli ?

Hujibu. Nayatubia kweli.

3. Waamini kwake Bwana Yesu Kristo kuwa ndiye Mwokozi wako, tena kuwa ndiye Mfalme wako ?

Hujibu. Ndiyo, naamini kwake.

4. Wataka kweli kumtii Bwana Yesu Kristo kila siku ya maisha yako sawasawa na Neno lake na maagizo yake ?

Hujibu. Ndivyo nitakavyo, kwa msaada wa Mungu.

¶ *Ndipo Padre hushika nkono wa kuume wa kila mtu atakaye-kubaliwa, na kumkubali kuwa msomaji kwa kunwambia maneno haya :*

Fulani, nakukubali wewe kuwa msomaji katika kanisa la Kristo.

¶ *Ndipo Padre huwafundisha na kuwahimiza hao walokubaliwa kwa kuwaambia maneno haya :*

WAPENZI wangu, sasa mmekebaliwa kuwa wasomaji wa kanisa la Kristo, nanyi hivi mwaweza kuanza kufundishwa mpate baadaye kuingia katika kanisa lake takatifu kwa njia ya ubatizo.

Yakaliko mafundisho mengi yawapasayo kujifunza, basi nawahimiza mfanye bidii zaidi sana katika kusoma kwenu, tena yawapasa kufanya bidii katika kutenda ayatakayo Kristo, kama mtakavoyelewa. Lakini mmekwisha kuelewa na mafundisho yasiyo haba, nami nawataka sana mkumbuke ya kwamba kwa mwendo wenu mtakuwa kuwavuta watu sana, zaidi hao ambao hawajapata kufika mnafokika ninyi.

Kila siku yawapasa kumwomba Mungu ; kila siku fanyeni bidii kusoma Neno lake takatifu, mkamwombe awafundishe mumo kwa Roho wake Mtakatifu ; tena katika siku yake takatifu fanyeni bidii zaidi kumkumbuka yeye, na kuingia nyumbani kwake kwa ibada yake takatifu pasipo kuzuwa.

Tena nawaambia sana kwamba muwe na bidii katika kuwasaidia watu wa nyumba zenu, na jamaa zenu, na watoto wenu, na rafiki zenu, ili wao nao wamfuate Bwana Yesu Kristo, kama ninyi mlivyoahidi kufanya. Tena, kama aliyowaaagiza yeye mwenyewe, jaribuni kutangaza habari zake njema, hasa kwa hao walio katika giza.

Katika mambo haya yote mna haja sana kuwa na msaada wa Mungu na neema yake, maana, mkikosa kuwa na haya hamtakuwa na uwezo wa kumtumikia kabisa. Basi sasa na tupige magoti sote, na kumpa Mungu shukrani zetu na maombi yetu.

Na tuombe.

EWE Mungu wa milele, Mweza-wa-yote, Babaetu wa Embinguni ; sisi tu miguuni pako, twakushukuru kwa ulivyopenda kuwaita hawa watumishi wako waijue neema yako, na kukuamini wewe ; uongeze ujuzi huo, na kuikaza mioyoni mwao imani hiyo milele, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu uliye mbinguni, wewe hutaki mwenye dhambi afe, wataka auache uovu wake awe hai. Uwajalie watumishi wako hawa kutubia kweli dhambi zao siku zote, na kutiwa nguvu na Roho wako Mtakatifu wapate kukutumikia kwa uaminifu, kwa Yesu Kristo, Mwokozi wetu. *Amina.*

EWE Mwokozi Kristo, wewe uliye Mchunga mwema Uliyetao uzima wako kwa ajili ya kondoo : twakuomba, uwaongoze kwa mkono wako kondoo hawa waliokuwa wamepotea, na kutanga-tanga barani, ila sasa wataka kukubaliwa katika zizi lako. Uwalishe, ewe Bwana, chakula kiwafaacho, uwanyeshe maji yaliyo hai, kisha wakati utakapofika uwajalie kubatizwa na kutiwa kwako wewe, na kurithi usfalme wako ulio wa milele. *Amina.*

EWE Roho Mtakatifu, uwapaye uzima mpya wao waliokuwa wamekuwa katika makosa na dhambi, nawe umeanza kazi yako njema katika mioyo ya watu hawa ; sisi twakuomba sana kwamba utimize kazi hii ndani yao, uwaweke tayari kupokea ubatizo wako mtakatifu kwa kutubu kweli na kuwa na imani iliyohai, tena uwamiminie katika mioyo yao iliyohai na kiu neema yako iletayo uzima. Uwafundishe, uwaongoze, uwatakase, wawe waaminifu hata kufa, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

MUNGU Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu, awabarikie, awalinde, na kuwaweka salama. Bwana awaangalie kwa rehema zake na kuwatia nguvu kwa neema yake, ili mpate kumtumikia kwa uaminifu katika maisha haya, na katika ulimwengu ujao mpate uzima wa milele. *Amina.*

TARATIBU YA NDOA

YA WATU AMBAO MMOJAWAPO HAJABATIZWA

¶ *Watu wote watakaoaa na kuolewa hutangulia kuitangaza habari ya ndoa yao msikitini siku ya Jumapili tatu mbali-imbali, wakati wa Sala ya Asubuhi, au, (ikiwa hakuna Sala ya Asubuhi), wakati wa Sala ya Jioni : yule Padre hunena kama taratibu ya desturi,*

MIMI naitangaza habari ya ndoa kati ya Fulani, mtu maketiye pahali fulani, na Fulani, mwanamke aketiye pahali fulani. Pakiwa na mtu kwenu ajua sababu au kizuizi cha haki cha kuwazuia watu hawa wawili wasiunganishwe katika ndoa takatifu, imempasa kusema.

Hii ndiyo mara ya kwanza, (*au ya pili, au ya tatu*), ya kuwaauliza kama haya.

¶ *Na wakiwa wakaa katika mipaka ya misikiti mbali-imbali, hutolewa maulizo ya habari yao katika misikiti yote miwili, yule Padre wa msikiti huu na asiwaoze asipopato hati ya kumpa hakika ya kuwa yamekwisha kuulizwa maulizo mara tatu, nayo hati hiyo huipata kwa Padre yule wa msikiti ile wa pili.*

¶ *Siku iliyagizwa kuwaaza wale wawili ikifika saa yake, yule atakayeoa na yule atakayeolewa, huangia ndani ya msikiti pamoja na rafiki zao na jirani zao, wasiname pamoja wale wawili, yule mwananume upande wa mkono wa kuume na yule mwanamke upande wa mkono wa kushoto : ndipo hunena yule Padre,*

NDUGU zangu, mmekuja hapa leo kuungamanishwa katika ndoa takatifu. Ingawa hamjabatizwa bado nyote wawili, mwatumaini ya kuwa baadaye nyote mtakuwa watu wa kanisa la Kristo kwa ubatizo, nanyi mwataksa kwamba arusi yenu leo iwe sawasawa na mapenzi yake. Basi nataka kwanza kuwaauliza mambo kadhwakadhada mbele ya hawa watakaowashuhudia, mpate kufahamu vizuri maana ya jambo hili kubwa.

Je, nyote mwasema kwa kufikiri sana kwamba mwakusidia kuwa watu waaminifu wa kanisa la Kristo na kutii mapenzi yake ?

Hujibu. Ndivyo nitakavyo.

Mmeelewa nyote kuwa Kristo alitufundisha kwamba ndoa ya Wakristo iliyo kweli ni mume mmoga na mke mmoga kuungamanishwa na kuepukana na wengine wote, siku zote watakazoishi wote wawili ?

Hujibu. Naelewa.

Mwataka kweli mioyoni mwenu kwamba ndoa yenu hivi leo iwe alivyofundisha Kristo, kisha siku zote mtakazoishi nyote wawili hamtashikana na mtu mwengine ?

Hujibu. Ndivyo nitakavyo.

Mwasema kweli ya kwamba hamjui kizuio cha kuwa-zuilia msiungamanishwe katika ndoa ? Kwani kumbukeni kwamba wao waungamanishwao kwa jinsi isiyoomriwa kwa neno la Mungu, hawaungamanishwi na Mungu, kisha ndoa yao si halali.

Hujibu. Nasema kweli.

¶ *Kuuliza mkuutano.*

NDUGU zangu, ikiwa kuna mtu kwenu ajuaye sababu ya haki ya kuwazuilia watu hawa wawili wasiungamanishwe katika ndoa takatifu, na aseme sasa, au tokea sasa hata milele anyamaze.

Na tuombe.

(Wote wasimame vilevile.)

BABAETU wa mbinguni, uliyetuumba na kutuhifadhi, nawe ulimtuma Yesu Kristo, Mwanayo, awe Mwo-kozi wetu, uwabarikie watumishi wako hawa ambaa wamekuja hapa kuungamanishwa, wawe mtu na mkewe. Uwasaidie kufahamu sawasawa ahadi watakazotoa sasa, Uwape neema yako wawe waaminifu kila mtu kwa mwenzive siku zote watakazoishi wote wawili, kisha wawe waaminifu kwako wewe, kwa jinsi apendavyo yeeye ambaye twaomba kwa jina lake, Yesu Kristo, Mwokozi wetu. *Amina.*

¶ *Na ikiwa hakikusemwa kizuizi kiwachcho chote, ndipo hapo yule Padre humuuliza yule mtu mume,*

FULANI, umependa uwe naye mwanamke huyu, kuwa mkeo wa kumwoa, mwishi wewe naye kama maagizo ya Mwenyezi Mungu, katika hali takatifu ya ndoa ? Utampenda, utamtuliza moyo wake, na kumstahi, na kumtunza, akiwa hawezo, akiwa mzima ; na wengine wote utawaepuka, ujiweke wewe kuwa na yeeye muda wote mtakaokuwa hai pamoja duniani ?

¶ *Yule mume hujibu,*

Nakubali.

¶ *Ndipo hapo yule Padre humuuliza yule mwanamke,*

FULANI, umependa uwe naye mtumume huyu kuwa mumeo wa kukoao, mwishi pamoja kama maagizo ya Mwenyezi Mungu katika hali takatifu ya ndoa ? Utamtii na kumtumikia, utampenda na kumstahi na kumtunza, akiwa hawezo, akiwa mzima ; na wengine wote utawaepuka, ujiweke wewe kuwa naye muda wote mtakaokuwa hai pamoja duniani ?

¶ *Yule mke hujibu,*

Nakubali.

¶ *Ndipo hapo yule Padre hunena,*

Ni nani amtoaye mwanamke huyu ili kumwoza mume huyu ?

¶ *Ndipo watakapoapiana yamini kama hivi : yule Padre humpokea yule mwanamke mikononi mwa babaye, au rafikiye, na kumfanya yule mume, kwa mkono wake yeeye wa kuume, amshike mkono wake wa kuume yule mwanamke, akimfunza kusema,*

MIMI Fulani nakutwaa wewe Fulani kuwa mke wangu wa kukoao, niwe nawe nikushike toka hii siku ya leo, kwa wema kwa ubaya, kwa wingi wa mali kwa uchache wa vitu, katika ugonjwa katika afya, nikupende na

kukutunza hata kufa, kama amri zake takatifu Mwenyezi Mungu. Nami kwa ajili ya neno hili nakupa yamini yangu.

¶ *Ndipo hapo huachana mikono, kisha baadaye yule mwanamke kwa mkono wake wa kuume humshika yule mume mkono wake wa kuume, na kunena naye kwa kumfuata yule Padre,*

MIMI Fulani nakutwaa wewe Fulani kuwa mume wangu wa kunioa, niwe nawe nikushike toka hii siku ya leo, kwa wema kwa ubaya, kwa wingi wa mali kwa uchache wa vitu, katika ugonjwa katika afya, nikupendele na kukutunza na kukutii hata kufa, kama amri zake takatifu Mwenyezi Mungu. Nami kwa ajili ya neno hili nakupa yamini yangu.

¶ *Ndipo hapo huachana mikono mara ya pili, yule mume humpa yule mke pete, akiitweka juu ya Chuo, pamoja na ada, kama walivyozeoa kupewa Padre na katibu wake. Yule Padre akiisha kuitwaa ile pete humpa yule mume, yule mume apate kuhivika yule mwanamke kidole cha mne cha mkono wa kushoto ; kisha yule mume huishika ile pete hapo, na kunena kwa kufunzwa na yule Padre,*

MIMI kwa pete hii nakuoa, kwa mwili wangu naku-heshimu, nami nakupa vitu vyangu vyote vya duniani : kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

¶ *Ndipo hapo yule mume huiacha ile pete katika kidole cha mne cha mkono wa kushoto wa yule mwanamke, kisha, wakipiga magoti wote wawili, yule Padre hutena,*

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, huna mwanzo huna mwisho ; Muumba wa wanadamu wote ni wewe, nawe ndiwe mwenye kuwatunza ; wewe watupa kila neema ya rohoni ; ndiwe mwenye kuanziza maisha yasiyo ukomo : uwatere-mshie baraka yako hawa watumishi wako, mtumume huyu na mwanamke huyu, ambao sisi twawaombea hivi kwa jina lako ; ili kwamba kama walivyoishi pamoja Isaka na Rebeka kwa uaminifu, watu hawa nao washike vivyo kuondoa na kutimiza yamini zao na maagano waliyo-

wekeana, ambayo pete hii waliyopanana na kupokeana hivi ndiyo dalili yake na sahihi yake ; nao wadumu daima katika umoja wa mapenzi na amani viliviyotimia, waishi kwa kufuata sheria yako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

¶ *Ndipo hapo yule Padre huashikamanisha mikono yao ya kuume, huyu na huyu, na kunena,*

ALIOWAUNGAMANISHA Mwenyezi Mungu, bina-damu na asiwatenganiche.

¶ *Ndipo hapo yule Padre husema na wale watu,*

KWA maana ya kuwa Fulani na Fulani wamekubaliana katika ndoa takatifu, nao neno hilo wamekiri mbele za Mwenyezi Mungu na mkutano huu, tena wamepanana yamini, wameapiana wenyeve kwa wenyeve, nayo wameiweka wazi na kuikiri mbele ya watu kwa kutoa na kupokea pete na kushikana mikono ; mimi nasema hawa ni mume na mkewe pamoja, kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

¶ *TUNZA. Katika ndoa ya watu ambao mmojawapo hajabatizwa bado, wasisonge mbele mume na mke mpaka Meza ya Bwana, ila ibada tendingee vivyo paali hapo ilipoanzwa.*

Baraka.

MUNGU Baba, Mungu Mwana, Mungu Roho Mtakatifu, na awabarikishe, awalinde na kuwaweka salama ; Bwana na awaangalie kwa rehema zake na kuwaneemesha, na kwa mtakavyojawa na baraka za rohoni na neema pia kwake yeye, muwe watu wa kukaa pamoja kwa wema katika maisha haya, wenyeve kwa wenyeve, hata katika ulimwengu ujao myapate maisha yasiyo mwisho. Amina.

¶ *Watu wote wa mkutano wapige magoti.*

Na tuombe.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekayyo mbinguni. Utupe leo

mkate wetu wa kututoshia. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tulivyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwia ; Utuokoe maovuni : Kwa kuwa ufalme, na nguvu, na utukufu, ni vyako milele. *Amina.*

Padre. Ewe Bwana, uwaokoe mtumwa wako na kijakazi chako.

Huitika. Waliokutumainia wewe.

Padre. Ewe Bwana, uwaletee msaada kutoka katika pahali patakatifu pako ;

Huitika. Uwalinde milele.

Padre. Uwe kwao ukuta wenye imara,

Huitika. Kuwakinga na uso wa adui zao.

Padre. Ewe Bwana, utusikize maombi yetu ;

Huitika. Kilio chetu kikufikilie uliko.

Padre. Ewe Mungu wa baba zetu, uwabarikie hawa watumishi wako, upande mbegu za uzima wa milele mioyoni mwao ; ili yote watakayojifunza katika Neno lako takatifu wayatimiza kwa matendo yao. Uwajalie kuwa waaminifu katika kujifunza zaidi mapenzi yako, uwasaide wawe na bidii kufuliza mbele hata wakati ukifika wote wawili waingie kabisa katika kanisa lako, na kwa kukutii wali hali wamelindwa na wewe siku zote, wakae katika mapenzi yako hata mwisho wa maisha yao, na kumfuata kwa uaminifu Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Sala hiyo ifuatanyayo huachwa awapo yule mwanamke si
mtu wa kuchukua mimba tena.*

EWE Bwana mwenye rehema, Babaetu wa mbinguni, ni kwa vipawa vyako vya neema binadamu wao-ngezekavyo ; sisi twakuomba kwamba uwasaide watu wawili hawa kwa huwabarikia, hata iwe wao kuwa watu wa baraka katika kuzaa wana, nao wawe watu wa kukaa pamoja kwa kupendana kwa uaminifu, hata iwe wao kuwaona wana wao wenye kulewa katika imani ya Kristo na adili, kwa kukutukuza na kukuheshimu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

MWENYEZI Mungu Babaetu awamiminie ninyi mali za neema yake, awatakase na kuwabarikia, ili mwendelee kujua mapenzi yake, mmpendeze katika mwili na roho, na kukaa pamoja katika mapenzi matakatifu, hata mwisho wa maisha yenu. *Amina.*

(¶ *Ndipo itaweza kuletwa hotuba.*)

BWANA na awabarikie na kuwalinda, Bwana na awainulie nuru ya uso wake, na kuwapa amani, sasa na hata milele. *Amina.*

TUNZA. Kabla ya siku ya kuweka wakf, msikiti utiwe nyombo vitakwavyo na mwenye amri sawasawa na desturi ya Kanisa la Uingereza. Archdeacon, au mitu mwingine ataka-yagizwa, auangalie msikiti, na kuleta habari kama maagizo hayo yametimizwa.

Bishopu, pamoja na kasisi aliye msaada wake, akaribishive mlangoni mwa msikiti na Padre wa msikiti na mapadre wengine (nao wawe wamevaa mavazi ya madaraja yao), na wazee wa msikiti.

Padre wa msikiti amwambie Bishopu,

ABA mwenye kuheshimiwa kwa mambo ya Mungu, twakutaka uweke wakf msikiti huu.

Bishopu aitike,

NI tayari kufanya hivyo.

Mlango wa msikiti uwe umefungwa, ndipo Bishopu aupige mara tatu kwa bakora yake ya ubishopu.

Ndipo mlango ufunguliwe wazi, naye Bishopu aingie, na kusema,

Amani itokayo kwa Babaetu wa mbinguni na iwe juu ya nyumba hii.

Amani itokayo kwa Mwanawe, aliye amani yetu, na iwe juu ya nyumba hii.

Amani itokayo kwa Roho Mtakatifu Msafiri na iwe juu ya nyumba hii.

Bishopu na mapadre na wazee wa msikiti na wengine waende penye Meza takatifu, inaposemwa au kuimbwa zaburi hii :

ZABURI 122

NILIFURAH waliponiambia : Na twende nyumbani kwa Yehova.

2. Miguu yetu inasimama ndani ya malango yako : ewe Yerusalem :

3. Yerusalemu uliojengwa : kamá mji ulioshikamana :

4. Huko ndiko walikopanda makabila, makabila ya Yehova : ushuhuda kwa Israeli, ili kulishukuru jina la Yehova.

5. Kwani huko viliwekwa viti vy a hukumu : viti vy enzi vy nyumba ya Daudi.

6. Utakieni Yerusalem amani : watafanikiwa wakupendao.

7. Amani na ikae ndani ya kuta zako : na kufanikiwa ndani ya majumba yako.

8. Kwa ajili ya ndugu zangu na rafiki zangu : nitasema sasa, Amani ikae ndani yako.

9. Kwa ajili ya nyumba ya Yehova Mungu wetu : nitakutafutia mema.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Bishopu asimame mbele ya Meza takatifu, awaelekee watu, aseme,

WAPENZI wangu katika Bwana, tangu hapo, wakati wa Torati, na wakati wa Injilli, watu watakatifu, kwa kuyutwa na Roho Mtakatifu, walijenga nyumba za kutumiwa kwa ibada ya Mwenyezi Mungu, ili watu wazidi kuuheshimu utukufu wake, na kumtumukia kwa bidii na unyenyekevu ; nazo kazi zao njema Babaetu wa mbinguni alizipenda na kuzikubali. Basi tusiwe na tashwishi, tujue ya kwamba atapenda shauri letu hili jema la kuweka wakf nyumba hii kwa ajili ya taratibu za ibada yake ; nasi kwa kuamini na kunyenyeka tumwombe aibarikie kazi yetu hii.

Ndipo watu wapige magoti, Bishopu aseme,

EWE Mwenyezi Mungu wa milele, utukufu wako hautambúlikani, mbingu za mbingu hazitoshi kuwa makao yako, licha misikiti ijengwayo kwa mikono ya watu, walakini wewe kwa neema yako umeahidi ya

kwamba wawili au watatu wakikutanika kwa jina lako, utakuwapo pamoja nao : uone vyema, ewe Bwana, kuwa pamoja nasi tunaokutanika hapa kupaweka wakf kwa heshima ya jina lako kuu ; twakuomba ukubali nyumba hii mikononi mwetu kwa ajili ya kuongeza utukufu wako, na kwa utumishi wa Neno lako na sakramenti zako, na kwa wokofu wa watu wako ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, Mwokozi wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo Bishopu na mapadre waende mbele ya fonti, watu wote wasimame vivyo.*

Bishopu asome,

Tito, 3. 5-7

SI kwa njia ya kazi zilizo katika haki tulizofanya sisi, slakini alituokoa kwa njia ya rehema yake, kwa kuosha kwa kuzaliwa-upya na kwa kufanywa-upya kwa Roho Mtakatifu, aliyetumwagia juu yetu kwa wingi kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu ; ili kwamba tukihesabiwa kuwa na haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi, sawasawa na matumaini ya uhai wa milele.

Padre. Waliopandwa katika nyumba ya Yehova.

Huitika. Watasitawi katika nyua za Mungu wetu.

Padre. Bwana na awaongeze ninyi,

Huitika. Ninyi na watoto wenu.

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu wa milele, Baba wa mianga yote, asili ya wema wote, usikie maombi ya watumishi wako, na kuibarikia fonti hii, tunayoweka wakf sasa kwa utumishi wako, iwe birika ya uzazi mpya kwa wote watakaobatizwa mumo : uwajalie kwamba kwa vile watakavyooshwa na kutakaswa kwa Roho Mtakatifu, waifie dhambi, na kufufukia haki pamoja na Kristo, na kudumu siku zote katika jumla ya watoto wako waaminifu, wateule ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo Bishopu aende pamoja na mapadre pasomwapo masomo, asome,*

2 Timotheo 3. 16-17

KILA meno la maandiko lililovuviiliwa na Mungu lina manufaa nalo kwa mafunzo, na kwa kuonya makosa, na kwa kurejeza upya, na kwa kuadibisha katika njia za haki : ili kwamba huyo mtu wa Mwenyezi Mungu apate kuwa mtimilifu : mwenye kuijandalia kwa kila kazi njema.

Padre. Neno lako ni taa kwa miguu yangu,

Huitika. Na mwanga wa njia yangu.

Na tuombe.

EWE Bwana, uwajalie wao watakaosoma Maandiko matakatifu waiamini sana Injili yako, na kwa jinsi watakavyosoma, wote waifahamu ; tena uwajalie wote watakaosikia walipokee lile Neno kwa mioyo myeupe, na kuzaa matunda kwa uvumilivu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo Bishopu aende penye mimbari pamoja na mapadre, asome haya,*

2 Timotheo 4. 2

HUBIRI lile neno, simama *kwa hilo* wakati wa kufaa na wakati usiofaa ; karipia, kanya, himiza, kwa uvumilivu wote na mafunzo.

Padre. Kufafanusha maneno yako kwtia nuru,

Huitika. Na kumfahamisha mijinga.

Na tuombe.

EWE Bwana, uwajalie wote watakaolihubiri Neno lako pahali hapa wajazwe Roho wako Mtakatifu, ili kwa hekima yao na bidii yao kuu mioyo ya wenye dhambi igeuzwe, na imani ya watoto wako ikaze kuwa imara ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ Ndipo Bishopu aende pamoja na mapadre pale zisomwapo sala, asome,

I Petero 4. 10

VVIVILE kama kila mtu alivyopata kipawa ; mkikitumia kati yenu kama mawakili wema wa neema za Mungu zilizo za aina nyingi.

Padre. Makuhani wako na wavikwe haki,
Huitika. Watakatifu wako na washangirie.

Na tuombe.

EWE Bwana, uwajalie mapadre na waimbaji wa msikitihuu wakumbuke siku zote heshima ya kazi wanayoitiwa, sala zao na sifa zao ziwaongoze watu wako hata kiti cha neema, zichangamane na maombezi ya Kuhani wetu mkuu, Msaada wetu, Yesu Kristo, Bwana wetu. Amina.

¶ Ndipo Bishopu aende penye Meza takatifu, asome haya,

I Wakorintho 10. 16

KIKOMBE cha baraka ambacho twakibarikia, je, si Kushirika wa damu ya Kristo ? Huo mkate tuuvnjao, je, si ushirika wa mwili wa Kristo ?

Padre. Huu ndio mkate ushukao kutoka mbinguni,
Huitika. Wa mtu kuula wala asife.

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, Babaetu wa mbinguni, Elyietupa Mwanayo, Mwokozi wetu, Yesu Kristo, si kwamba afe kwa ajili yetu tu, ila awe pia chakula chetu cha rohoni, riziki zetu katika sakramenti takatifu ya mwili wake na damu yake ; ujalie kwamba ukumbusho wa kufa kwake ufanywe hapa kwa heshima na uchaji, nayo sadaka ya sifa na shukranii itolewe kwa utakatifu na furaha, kwa heshima ya jina lako tukufu, na faida ya kanisa lako zima, na faraja ya roho zilishazo kwake ; kwa yeYe Yesu

Kristo, Bwanà wetu, naye apewe heshima yote na utukufu wote pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, milele na milele. Amina.

UPENDE, ewe Bwana Mungu wetu, kuibarikia na kuitakasa na kuiweka Meza hii takatifu kwa heshima yako, na kwa ukumbusho wa siku zote wa sadaka ile moja iliyotolewa mara moja tu msalabani ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala, pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja hata milele. Amina.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalmehako na uje. Mapenzi yako yatendekie juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kutotosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa ; Utuokoe maovuni : Kwa kuwa ufalmehako, na nguvu, na utukufu, ni vyako milele. Amina.

¶ Ndipo watu wote wapige magoti na kuumba wimbo huu.
(Ni wimbo wa 214 katika Chuo cha Nyimbo.)

Roho Muumba, vuvia,

Washe moto kwetu pia ;

Ndiwe Mpaka-mafuta,

Saba-saba tukipata. 1

Neema itokayo juu

Mna uhai na nafuu ;

Tutie nuru daima,

Macho na yawe mazima.

Twoshe, nyusoni tupake ;

Usafi, Bwana, tukikwe ;

Waepushe na adui ;

Ulipo hawasumbui ;

Tujuyye Baba na Mwana

Na wewe kuungamana ;

Kwamba kwa zamani zote

Kukwimbia tusiache.

Baba, Mwana, twakusifu,

Nawe Roho Mtakatifu. Amina.

¶ *Ndipo Bishopu asimane na kusema haya, (watu wakipiga magoti vivyo),*

KATIKA imani ya Yesu Kristo twauweka wakf msikiti huu kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. *Amina.*

EWE Bwana, wote watakaopokea hapa sakramenti Iiliyobarikiwa ya mwili wake na damu yake Kristo, wajie siri hii takatifu kwa toba na imani, kwa shukrani na mapenzi ; nao huku wakijawa neema yako na baraka yako ya mbinguni, wapate msamaha wa dhambi zao, na faida nyingine zote za kuteswa kwake. *Amina.*

UWAJALIE wao watakaokuja hapa kwa Ushirika Mtakatifu wajitoe wenyewe, roho zao na miili yao, kuwa kwako sadaka iliyo na maana, na uhai. *Amina.*

UWAJALIE kwamba sala zao zipande juu mbele zako, kama uvumba ; na kuinuka kwa mikono yao kuwe kama dhabihu ya kila siku. Isafishe mioyo yao, na kuzitakasa roho zao, na kutirmiza haja zao, ili yote watakyoomba kwa imani wayapate kwa kweli, na kukushukuru siku zote. *Amina.*

UWAJALIE kwamba matoleo yao na sadaka zao vifike kama ukumbusho mbele zako ; nao waone na kujua ya kwamba umependezwa na sadaka hizo. *Amina.*

UMJALIE mwahali humu mote tunamokuwekea wakf kwa kazi yetu na utumishi wetu, mtakaswe na Roho wako Mtakatifu, kwa rehema zako, ewe Bwana Mungu Mwenye-baraka, uishiye na kuyatawala mambo yote, milele na milele. *Amina.*

KWA Mfalme ambaye ni wa milele, asiyetoweka, wala Kasiyeonekana, ni Mungu mwenye hekima pwekee, Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na viwe kwake heshima na utukufu, milele na milele.

¶ *Ndipo huimbwa wimbo.*

¶ *Ndipo huletwta hotuba.*

¶ *Baada ya hotuba wimbo mtwingine huimbwa. Unapoimbwa wimbo huu, sadaka za watu hupokewa na kutolewa.*

Na tuombe.

EWE Bwana Yesu Kristo, kwa jina lako lenye baraka, Nyumba hii ya sala imejengwa na kuwekwa wakf ; twakuomba ujalie ya kwamba kama tulivyopatengeneza pahali hapa kuonyesha mapenzi yako, sisi nasi vivyo tujengwe kuwa nyumba ya roho kwa ajili ya kukutolea utumishi utakaokufaa wewe, uishiye na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja hata milele. *Amina.*

EWE Bwana Mwenyezi Mungu wa milele, ulindaye Eroho zote ziwe hai ; twakuomba uliletii kanisa lako lililo katika mbingu na dunia pia nuru za kung'aa kwako na raha yako ya mbinguni ; 'ukatujalie sisi kwamba tukifuata mfano mzuri wa wao walioikutumikia huku, ambao hata sasa wa katika kustarehe, rupate mwisho kuingia pamoja nao katika furaha yako ya milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

TWAWAWEKA ninyi katika rehema na ulinzi wa Mwenyezi Mungu. Bwana na awabarikie na kuwallinda. Bwana na awaangazie uso wake, na kuwapa neema. Bwana na awainulie nuru ya uso wake na kuwapa amani, sasa na hata milele. *Amina.*

¶ *Wakati wa kuleta mara ya kwanza Ushirika Mtakatifu, itumiwe Sala na Waraka na Injili vifuatanganayo :*

Sala. Siku ya watakatifu Simoni na Yuda.

Waraka. Ufunuo 21. 1-7.

Injili. Mathayo 21. 12-16.

TARATIBU YA KUWEKA JIWE LA MSINGI WA MSIKITI

¶ Bishopu, au mtu navingine atakayeagizwa na yeze, aendapo hitakapowekwa jive la msingi, pamoja na mapadre na waimbaji, yamkini uimbwe wimbo.

¶ Vyote vikiisha kutengenezwa tayari kwa kazi ya kuweka lile jiwe, huyu Bishopu husema,

WAPENZI, na tuliweke jiwe hili kwa jina la Bwana. Kwanza tulisifu jina takatifu la Mwenyezi Mungu kwa alivyoifanikisha kazi yetu hata sasa, kwa rehema zake na wema wake ; tena tumwombe kwamba kwa uangalizi wake awabarikie wote watakaosaidia kuitimiza kwa njia yoyote, na kuwalinda wao watakaokuwa katika kazi ya kujenga ; na kulibarikia shauri letu hili.

Na tuombe.

TWASHUKURU sana, ewe Baba wa rehema zote, kwa vile ulivyoibarikia na kuihimiza kazi ya mikono yetu hata sasa ; upokee sifa tukuleteazo kwa miyo myeupe ilio na shukrani, ili tunapofurahiwa kwa wema wako tukubaliwe na wewe, na pahali hapa patakatifu pajazwe roho ya shukrani na ibada ya mapenzi, kwa heshima yako na utukufu wako, uishiye na kutawala, Mwenyezi Mungu, milele na milele. *Amina.*

¶ Ndipo isenwe au kuimbwa Zaburi 84

MASKANI zako zapendwa namna gani : ewe Yehova wa majeshi !

2. Nafsi yangu imezionea shauku nyua za Yehova, naam, na kuzikondea : moyo wangu na mwili wangu vinamililia Mungu aliye hai.

3. Ndege naye ameona nyumba, na mbayuwanyu kioto kwa nafsi yake alipoweka makinda yake : madhabahu zako, ewe Yehova wa majeshi, Mfalme wangu na Mungu wangu.

4. Wana heri wakao nyumbani mwako : watakuhimidi daima.

5. Yuna heri ambaye nguvu zake zatoka kwako : na njia ziendazo *Zayuni* moyoni mwake.

6. Wakinipa kati ya bonde la vilio hulifanya kuwa chemchemi : naam, mvua ya vuli hulivika baraka.

7. Huendelea toka nguvu hata nguvu : huonekana *Zayuni* mbele za Mungu kila mmoja wao.

8. Ewe Yehova, Mungu wa majeshi, usikie maombi yangu : usikilize, ewe Mungu wa Yakobo.

9. Ewe Ngao yetu, uangalie : umtazame uso Masihi wako.

10. Kwani ni bora siku moja katika nyua zako, kuliko siku elfu : ningependa kusimama penye kizingiti cha nyumba yako, kuliko kukaa katika mahema ya uovu.

11. Kwa kuwa Yehova Mungu ni jua na ngao ; Yehova atatoa fadhili na utukufu : hatawanyima kitu chema waendao kwa ukamilifi.

12. Ewe Yehova wa majeshi : yuna heri mwanadamu anayekutumainia wewe.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

¶ Ndipo yasemwe au kuimbwa maneno haya,

MSHUKURUNI Bwana kwa kuwa ni mwema ; rehema zake ni za milele.

Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema ; rehema zake ni za milele.

Mshukuruni Mungu wa miungu yote.

Kwa kuwa rehema zake ni za milele.

Utukufu uwe kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. *Amina.*

Bwana, uturehemu.

Kristo, uturehemu.

Bwana, uturehemu.

BABAETU uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke juu ya nchi, Kama yatendekavyo mbinguni. Utupe leo mkate wetu wa kututosha. Nawe utusamehe makosa yetu, Kama nasi tuliviyowasamehe watukosao. Nawe usitupeleke katika kujaribiwa ; Utuokoe maovuni : Kwa kuwa usalme, na nguvu, na utukufu, ni vyako milele. Amina.

TAZAMA, naweka katika Zayuni jiwe kuu la pemberi, lenye thamani.

Na kila amvaminiye hatatahayari.

Jiwe walilokataa waashi,

Limekuuza jiwe kuu la pemberi.

Neno hili latoka kwa Bwana,

Nalo ni la ajabu machoni mwetu.

Kwani hapana mtu awezaye kupiga msingi mwingine, zaidi ya ule uliokwisha kupigwa :

Nao ndio Yesu Kristo.

¶ Ndipo Bishopu husema,

Bwana na awe pamoja nanyi.

Na awe pamoja na roho yako.

Na tuombe.

EWE Bwana Mwenyezi Mungu, ijapokuwa mbingu za mbingu hazitoshi kuwa makao yako, ila umekubali kukaa pamoja na kanisa lako juu ya nchi ; twakuomba ya kwamba upabarikie kwa fadhili zako pahali hapa tunapopiga msingi wa nyumba itakayojengwa kwa sifa na heshima ya jina lako takatifu. Isitiwe unajisi au kutumiwa kwa njia isiyofaa ; kisha ulivyotimiza upendò wa Daudi katika kazi ya mwanawewe, utujalie sisi vivyo kwamba mapenzi yetu yatendeke, ili watumishi wako waone matendo yako, na utukufu wako uonekane kwa watoto wao ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala pamoja na wewe na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja hata milele. Amina.

¶ Ndipo huyu Bishopu huveka mkono wake juu ya jieve, akisema,

EWE Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai, Endiwe mwanga wa utukufu wake Baba msano kabisa wa nafsi yake, Msingi wa pekee, Jiwe kuu la pemberi, utubariki sisi tunapoweka jiwe hili kwa jina lako, nasi twakuomba uwe mwanzo na mfulizo na utimilivu wa kazi yetu hii, inayotendeka kwa ajili ya utukufu wa jina lako, uishiye na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja hata milele. Amina.

¶ Vyote vikitengenezwa tayari, ndipo jiwe liwekwe na mtu aliyeagizwa, kwa kutumia maneno haya,

KATIKA imani ya Yesu Kristo twaliweka jiwe hili, kwa jina la Mungu Baba, na Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. Amina.

¶ Ndipo huyu Bishopu husema,

IMANI ya kweli na ikae hapa siku zote, na uchaji-wa Mungu, na mapenzi ya ndugu pia ; napo pahali hapa panapotengwa sasa kwa sala, na kwa kuomba na kusifu jina lililo takatifu sana, pawe siku zote hekalu la Mwenyezi Mungu aliye juu ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu, aishiye na kutawala pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, Mungu mmoja hata milele. Amina.

¶ Ndipo maneno haya huimbwa,

UTUKUFU uwe kwa Baba, na kwa Mwana : na kwa Roho Mtakatifu ;

Kama vile mwanzo, na sasa : hata milele ni vivyo. Amina.

Na tuombe.

EWE Mwenyezi Mungu, kwa Mwanayo mzaliwa wa Epekee, aliye kichwa cha kanisa, umetuagiza sisi tulio viungo vyake tuwafanye mataifa wote kuwa wanafunzi ; utujalie sisi na wote watakaokuabudu baadaye katika

pahali hapa, tukumbuke siku zote tunavyodiriki na tunavyobarikiwa. Utuwezeshe kwa Roho wako Mtakatifu hata mwanga uangaze mbele ya watu, ili wao wakao kwetu ambao hawajakuja wewe, wapate kuwa pamoja nasi viungo vilivyo hai vya mwili wake yeye, aliye Mkuu wa wokofu wetu, Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu wa milele, Roho wako hutawala na kutakasa jamii yote ya kanisa ; utusikie tukiwaombea watu wa kila daraja katika kanisa lako takatifu, hasa wao walioota mali zao kwa ajili ya kazi hii njema ; ili watu hao wakutumikie kwa kweli na haki, kila mmoja kwa fungu lake la kazi na utumishi wake ; kwa Bwana wetu, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. *Amina.*

EWE Mungu uliye ngao ya watu wako, nawe ndiwe unayewakinga, twakuomba uwe karibu kuwalinda na kuwasaidia wajenzi wa nyumba hii ; uwatunze wakijenga, wasifanye dhambi, wasinene maneno mabaya ; uwakinge wasipatwe na hasara, hata kazi hii ambayo kwa rehema zako imeanzwa, kwa kutenda kwao itimizwe kwa furaha, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

¶ *Ndipo huletwa hotuba ya maneno machache ; kisha huimbwa wimbo mmoja ; baadye zisomwe sala hizi zifuatanzo :*

UTUONGOZE, ewe Bwana, katika vitendo vyetu vyote kwa fadhili ya neema yako, utupeleke mbele kwa msaada wako daima ; ili kwa kazi zetu kuanzwa, na kufulizwa, na kutimizwa kwako wewe, tulitukuze jina lako takatifu, hata mwisho wake kwa rehema zako tupate uzima wa milele ; kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

EWE Mwenyezi Mungu, ulijejenga kanisa lako juu ya Msingi wa wale mitume na manabii, na jiwe lake kuu la pembedi ni Yesu Kristo mwenyewe ; utujalie sisi kuungamanishwa katika umoja wa roho kwa mafundisho yao, ili tuwe hekalu takatifu la kukufaa wewe, kwa Yesu Kristo, Bwana wetu. *Amina.*

BWANA na awabarikie na kuwalinda ; Bwana na awaangazie uso wake na kuwapa neema ; Bwana na awainulie nuru ya uso wake na kuwapa amani, sasa na hata milele. *Amina.*